JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI

**TUME YA TAIFA YA MIPANGO**



# MPANGO WA NNE WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2026/27 – 2030/31

## Mageuzi kwa Ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji wa Ajira

Juni 2026

DIRA 2050

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI
**TUME YA TAIFA YA MIPANGO**

# MPANGO WA NNE WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2026/27 - 2030/31

## Mageuzi kwa Ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji wa Ajira

Juni 2026

© 2026 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu yoyote ya chapisho hili inayoweza kunakiliwa kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya awali kutoka Tume ya Taifa ya Mipango, isipokuwa nukuu fupi kwa matumizi ya kitaaluma, utafiti au matumizi yasiyo ya kibiashara kwa kutaja chanzo.

**Nukuu Sahihi**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2026). *Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31*. Dodoma: Tume ya Taifa ya Mipango.

**Kwa Mawasiliano**

Tume ya Taifa ya Mipango,
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 9,
Mtaa wa Kambarage, S.L.P. 1324,
41104 Tambukareli
Dodoma, Tanzania

Simu: +255 26 2961722
Baruapepe: es@planning.go.tz
Tovuti: www.planning.go.tz

**Shukrani**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika maandalizi ya Mpango huu.

# DIBAJI



Kwa nia na dhamira ya dhati ninawasilisha kwenu Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (Mpango IV), 2026/27–2030/31. Mpango huu unaashiria kuanza kwa utekelezaji wa Dira 2050, ambayo ni ajenda yetu ya muda mrefu ya kuleta mageuzi endelevu ya uchumi na ustawi wa jamii nchini. Mpango huu ni mwendelezo wa mipango ya awali.

Aidha, ni nyenzo ya kimkakati inayoendana na azma yetu ya kujenga msingi wa taifa lenye ustawi, jumuishi, haki na kujitegemea. Shabaha yetu kuu ni kufikia uchumi wa dola za Marekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050. Mpango huu ni wito kwa taifa kuchukua hatua za kukuza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi, kuongeza fursa, kuweka mazingira wezeshi kwa kila mmoja, kukuza pato la taifa na kuhakikisha manufaa yake yanawafikia wote. Hivyo, umoja wa kitaifa, mshikamano wa kijamii na dhima ya pamoja ni nguzo kuu za ustawi wetu sote.

Mpango IV unaweka msisitizo mkubwa katika mageuzi yanayolenga kuimarisha uchumi shirikishi, kukuza ajira zenye staha, na kujenga taifa lenye ushindani. Kwa muktadha huu, Mpango unaweka msisitizo katika kujenga taasisi za kisasa, kuimarisha utawala bora, kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji, pamoja na kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uwazi katika uendeshaji wa sekta zote. Aidha, Mpango unalenga kukuza uwezo wa Watanzania katika uzalishaji wenye tija kwa kuharakisha maendeleo ya viwanda, kuendeleza miundombinu muhimu, kukuza rasilimali watu, kuchochea ubunifu, pamoja na kuimarisha biashara na ujasiriamali. Lengo ni kujenga uchumi thabiti, stahimilivu na mseto, unaoweza kuzalisha ajira zenye staha, hasa kwa vijana, wanawake na nguvu kazi inayozidi kuongezeka.

Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango huu yanahitaji dhamira ya pamoja, uwajibikaji wa pamoja, na hatua zilizoratibiwa. Kila Mtanzania ana wajibu wa kuchangia kupitia ujasiriamali, ubunifu, uwekezaji, utumishi wa umma au shughuli za kijamii. Taasisi za umma, sekta binafsi, asasi za kiraia na washirika wa maendeleo, vikundi vya kijamii na wananchi wanapaswa kushirikiana katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii nchini. Sekta binafsi, kipekee, imepewa jukumu la kuongoza mageuzi haya kwa kuchangia katika kukuza uchumi, kuchochea uwekezaji, tija, ubunifu na ajira. Mafanikio ya Taifa letu yatategemea kwa kiasi kikubwa uwezo wa sekta binafsi kukua, kushindana na kutumia fursa zilizopo. Kwa kuzingatia hilo, Serikali itaendelea kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara, uwekezaji na ushiriki mpana katika shughuli za kiuchumi zenye tija.

Ninazihimiza Wizara zote, Idara, Taasisi, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchukua hatua za haraka katika utekelezaji wa Mpango huu. Hatutaruhusu kuendelea kufanya kazi kwa mazoea. Kama taifa, sharti tujenge utamaduni wa utendaji unaozingatia matokeo, ubunifu, uwajibikaji na uadilifu, nidhamu na ufanisi. Watumishi wa umma wanapaswa kutekeleza wajibu wao kwa weledi, na kwa wakati, huku wakiboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Utekelezaji wa Mpango huu unadhihirisha kaulimbiu ya "Kazi na Utu" inayomaanisha maendeleo yatapatikana kupitia bidii ya kazi inayozingatia utu, maadili, uzalendo na heshima. Mpango huu unatambua haja ya kuendeleza ajenda ya maendeleo ya taifa, hususan kwa kuongeza viwanda vitakavyoongeza upatikanaji

wa ajira zenye staha, kuwezesha vijana, na kuimarisha uwezo wa ndani wa uzalishaji. Kama nilivyobainisha wakati wa uzinduzi wa Bunge la 13, kipimo chetu cha mafanikio hakitakuwa mifumo, miundombinu na miradi tunayotekeleza pekee, bali pia thamani ya utu, tumaini na tabasamu tutakaloliacha katika nyuso za wananchi tunaowatumikia.

Serikali ina azma thabiti ya kutekeleza mageuzi na vipaumbele vya kimkakati vilivyoainishwa katika Mpango huu, ili kufikia malengo ya Dira 2050 na kujenga ustawi kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



## TAARIFA YA WAZIRI

## WITO WA KUCHUKUA HATUA



Kwa heshima kubwa, ninapokea na kuthibitisha dhamira ya kuendeleza maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na wito wa kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ili kufikia malengo ya Dira 2050.

Safari hii ya kihistoria ni ya miaka ishirini na mitano, inayoanza kwa utekelezaji wa Mpango IV, ambao ni wa kwanza, ukitafsiri kimkakati maono ya Dira 2050 na shabaha za Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2050 (Mpango Elekezi 2050) kwa vitendo na uhalisia. Mpango huu ni hatua muhimu katika kuyageuza matarajio yetu ya muda mrefu kuwa vipaumbele na hatua zinazotekelezeka kwa kipindi cha mwaka 2026/27–2030/31. Aidha, unaweka mfumo wa kimkakati wa kuendeleza na kuimarisha mafanikio yaliyopatikana kupitia mipango ya awali ya maendeleo ya taifa, ili kuweka msingi imara wa ujenzi wa uchumi imara, shindani, jumuishi, na taifa lenye ustawi.

Kwa niaba ya Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, nathibitisha dhamira yetu isiyotetereka ya kutekeleza Mpango huu kwa kasi, nidhamu, ufanisi, uwajibikaji, uwazi na uratibu thabiti katika ngazi zote za Serikali. Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango IV yanahitaji ushirikiano wa pamoja wa taasisi za umma, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, asasi za kiraia, taasisi za taaluma na Watanzania wote. Kwa msingi huo, taasisi zote za umma zinapaswa kuoanisha mipango, bajeti, programu na uwekezaji wao kwa kuakisi kikamilifu vipaumbele vya Mpango IV. Aidha, msisitizo mkubwa unapaswa kuwekwa katika utekelezaji unaolenga matokeo, uratibu wa kitaasisi, na utoaji huduma wenye ufanisi kuanzia ngazi ya Taifa hadi Serikali za Mitaa.

Mpango IV ni zao la mchakato jumuishi, shirikishi na unaozingatia ushahidi wa kisayansi. Umehusisha mashauriano ya kina ya kitaifa yaliyoshirikisha wadau mbalimbali, wakiwemo taasisi za serikali, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, asasi za kiraia na taaluma na wadau binafsi. Hivyo, Watanzania kwa pamoja wameunganishwa katika kubainisha vipaumbele na kujenga dhamira ya pamoja ya maendeleo na mwelekeo wake wa baadaye.

Tume ya Taifa ya Mipango itakuwa na jukumu kuu la kuratibu utekelezaji wa Mpango IV, kusimamia mipango na usimamizi wa uchumi, pamoja na kufuatilia maendeleo katika kufikia malengo ya Mpango na matarajio mapana ya Dira 2050. Tume itajikita zaidi katika mipango ya kimkakati ya Taifa, wakati majukumu ya mipango katika ngazi za chini yataendelea kuratibiwa kupitia Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, Tume ya Mipango itaratibu na kusimamia usanifu na utekelezaji wa programu na miradi ya kitaifa ili kuhakikisha ulinganifu wake na mwelekeo wa Dira 2050 pamoja na shabaha za Mpango Elekezi 2050. Vilevile, Tume itakuwa kitovu cha Taifa cha fikra kwa ajili ya utafiti, uchambuzi wa kisera, pamoja na ubunifu na malengo ya kimkakati yatakayosaidia kufanya maamuzi yanayozingatia ushahidi pamoja na kuongoza

maendeleo ya muda mfupi, wa kati na mrefu. Tume ya Mipango itatekeleza Mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini, Uwajibikaji na Kujifunza unaozingatia Matokeo. Chini ya mfumo huu, Tume itahusika na kuchapisha taarifa za utekelezaji mara kwa mara ili kuimarisha usimamizi wa utekelezaji, uwajibikaji wa taasisi na usimamizi wa utendaji. Hii itahakikisha uwazi, ujifunzaji endelevu, msisitizo wa utendaji unazingatia matokeo katika kipindi chote cha Mpango IV.

Mafanikio katika utekelezaji wa Mpango IV yanahitaji uzalendo, kufanya kazi kwa bidii, kuthamini ubunifu, kusimamia uadilifu na wajibu na uwajibikaji wa pamoja. Kwa pamoja, tuyatafsiri maono ya taifa kuwa maendeleo yanayogusa maisha ya Watanzania na kujenga mustakabali wenye ustawi kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**Prof. Kitila Alexander Mkumbo**
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| 3u | Uwekezaji, Uasili na Ubunifu |
| 4Rs | Mageuzi, Maridhiano, Uhimilivu na Kujenga Upya |
| MKUMBI | Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara |
| NF-MEDeP | Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo |
| SEZ | Maeneo Maalum ya Uwekezaji |
| STEM | Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TASAF | Mfuko wa Maendeleo wa Jamii |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |

# YALIYOMO

**DIBAJI** ...... **iii**

**TAARIFA YA WAZIRI: WITO WA KUCHUKUA HATUA** ...... **v**

ORODHA YA VIFUPISHO ...... vii

ORODHA YA MAJEDWALI ...... xi

ORODHA YA VIELELEZO ...... xiii

**MPANGO IV – KWA MUHTASARI** ...... **xiv**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ...... **1**

1.1 Muhtasari ...... 2
1.2 Chimbuko la Mpango ...... 2
1.3 Mpango wa Kwanza Katika Utekelezaji wa Dira 2050 ...... 3
1.3.1 Uhusiano wa Mpango IV na Dira 2050 ...... 3
1.3.2 Mpango Unaoakisi Muundo wa Dira 2050 ...... 4
1.4 Mbinu na Mchakato wa Ushirikishaji Wadau ...... 5
1.5 Mpangilio wa Kitabu ...... 5

**SURA YA PILI: MASUALA YALIYOZINGATIWA NA UHUSIANO NA DIRA 2050** ...... **9**

2.1 Muhtasari ...... 10
2.2 Masuala Muhimu ya Maendeleo ...... 11
2.3 Dhima: Tamko la Mwelekeo wa Kimkakati ...... 11
2.4 Mwelekeo wa Kimkakati ...... 12
2.5 Muundo wa Mpango ...... 13
2.5.1 Nguzo ...... 13
2.5.2 Vichocheo vya Mageuzi ...... 15
2.5.3 Misingi ya Kufikia Matokeo ...... 15
2.6 Falsafa ya Maendeleo ...... 16
2.7 Nadharia ya Mageuzi na Uasilishaji wa Kimkakati ...... 16
2.8 Malengo Mkakati ya Mpango ...... 20
2.9 Uainishaji wa Vipaumbele ...... 20
2.10 Maadili na Kanuni Msingi ...... 22
2.11 Matokeo Tarajiwa ...... 23

**SURA YA TATU: MWELEKEO NA MBINU MKAKATI** ...... **29**

3.1 Muhtasari ...... 30
3.2 Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani ...... 30
3.2.1 Utulivu na Utabirifu wa Uchumi Jumla ...... 31
3.2.2 Kuimarisha Uwezo wa Kifedha wa Serikali ...... 32
3.2.3 Uhimilivu na Usetushaji wa Sekta ya Nje ...... 34
3.3 Mageuzi katika Sekta za Kimkakati ...... 35
3.3.1 Sekta ya Kilimo ...... 35
3.3.2 Sekta ya Viwanda ...... 38
3.3.3 Sekta ya Ujenzi ...... 39

3.3.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji ........ 40
3.3.5 Sekta ya Mafuta na Gesi ........ 41
3.3.6 Sekta ya Utalii ........ 42
3.3.7 Sekta ya Fedha ........ 44
3.3.8 Sekta ya Michezo, Sanaa na Ubunifu ........ 45
3.3.9 Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo ........ 46
3.3.10 Mageuzi ya Biashara na Shughuli za Kibiashara ........ 48
3.3.11 Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi ........ 49
3.3.12 Mikakati ya Ushirikiano kati ya Nchi, Kikanda na Kimataifa ........ 50
3.3.13 Urasimishaji wa Uchumi na Usimamizi Wake ........ 52
3.4 Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu na Maendeleo ya Jamii ........ 53
3.4.1 Jamii Iliyoelimika, Yenye Ujuzi na Inayojifunza ........ 53
3.4.2 Nguvukazi Yenye Uwezo na Ari ........ 56
3.4.3 Demografia na Idadi ya Watu ........ 57
3.4.4 Soko na Taratibu za Ajira ........ 58
3.4.5 Jamii Yenye Hifadhi na Muundo Jumuishi ........ 59
3.4.6 Huduma Bora za Afya kwa Wote ........ 61
3.4.7 Usalama wa Chakula na Lishe Ulioimarishwa ........ 62
3.4.8 Upatikanaji na Uunganishaji wa Maji na Usafi wa Mazingira ........ 64
3.4.9 Jamii yenye Mshikamano, Inayowajibika na Kushirikiana ........ 65
3.4.10 Maendeleo Jumuishi Vijijini ........ 66
3.4.11 Mageuzi ya Vyama vya Ushirika ........ 67
3.4.12 Kupanua Tabaka la Kipato cha Kati ........ 68
3.5 Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ........ 69
3.5.1 Uhifadhi wa Mazingira ........ 70
3.5.2 Ukuaji Endelevu wa Miji Iliyopangika na Kusimamiwa Vizuri ........ 71
3.5.3 Mageuzi kwa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ........ 72
3.5.4 Ustahimilivu kwa Mabadiliko ya Tabianchi ........ 73
3.5.5 Uwezo wa Taasisi na Mifumo ya Utoaji wa Tahadhari ........ 75
3.5.6 Kuimarisha Ushiriki katika Biashara ya Kaboni ........ 76
3.5.7 Kuchagiza Manufaa ya Uchumi wa Buluu ........ 77
3.6 Kutumia Kikamilifu Vichocheo vya Maendeleo ........ 78
3.6.1 Nishati ........ 79
3.6.2 Mifumo ya Usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi ........ 80
3.6.3 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ........ 81
3.6.4 Utafiti na Maendeleo ........ 82
3.6.5 Matumizi ya Takwimu ........ 83
3.6.6 Mapinduzi ya Kidijitali ........ 84
3.6.7 Miundombinu na Huduma za TEHAMA ........ 85
3.6.8 Huduma za Mawasiliano na Posta ........ 87
3.6.9 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji ........ 88
3.7 Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa ........ 89
3.7.1 Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu ........ 89
3.7.2 Serikali za Mitaa Thabiti na Zenye Ufanisi ........ 90
3.7.3 Matumizi Sahihi ya Takwimu ........ 91
3.7.4 Mabadiliko ya Mitazamo na Fikra ........ 92

**SURA YA NNE: PROGRAMU ZA KIELELEZO ........ 97**

4.1 Muhtasari ........ 98
4.2 Vigezo Vilivyotumika katika Uteuzi wa Programu za Kielelezo ........ 98
4.3 Kufungamanisha Minyororo ya Thamani katika Programu za Kielelezo ........ 99
4.4 Programu za Kielelezo ........ 102
4.5 Mfumo wa Utekelezaji wa Programu za Kielelezo ........ 109

**SURA YA TANO: MAHITAJI NA MFUMO WA KUGHARAMIA UTEKELEZAJI ....... 113**

5.1 Muhtasari ....... 114
5.2 Mahitaji ya Rasilimali Fedha ....... 114
5.3 Muundo wa Ugharamiaji ....... 115
5.4 Vyanzo vya Rasilimali Fedha na Mikakati ya Serikali ....... 116
5.4.1 Vyanzo vya Kawaida vya Mapato ....... 116
5.4.2 Udhibiti wa Matumizi na Mgawanyo wa Kimkakati ....... 117
5.4.3 Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Fedha ....... 118
5.5 Vyanzo na Mikakati ya Kuvutia Uwekezaji wa Sekta Binafsi ....... 120
5.6 Vyanzo na Mikakati ya Kutumia Rasilimali za Mashirika ya Umma ....... 124
5.7 Mgawanyo wa Kina wa Rasilimali Fedha Kutoka Vyanzo Vikuu ....... 125
5.8 Ugharamiaji Kisekta ....... 127
5.9 Uratibu na Usimamizi wa Mkakati wa Kugharamia Mpango ....... 129
5.10 Hatua za Kimkakati na Viashiria Vikuu vya Utekelezaji ....... 129

**SURA YA SITA: USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA UWAJIBIKAJI ....... 135**

6.1 Muhtasari ....... 136
6.2 Mfumo na Mikakati ya Utekelezaji ....... 137
6.3 Utaratibu wa Kufungamanisha Mipango ....... 137
6.4 Mpangilio wa Majukumu ya Taasisi na Usimamizi wa Utekelezaji ....... 138
6.4.1 Tume ya Taifa ya Mipango ....... 138
6.4.2 Washirika wa Kimkakati na Taasisi Saidizi ....... 139
6.4.3 Taasisi za Usimamizi na Uwajibishaji ....... 141
6.5 Mfumo wa Usimamizi Kufikia Matokeo ....... 141
6.5.1 Usimamizi wa Kufikia Matokeo ....... 142
6.5.2 Utaratibu wa Kutoa Taarifa ....... 144
6.5.3 Mfumo wa Mapitio ya Mpango ....... 144
6.6 Mapitio ya Mwaka na Usimamizi Kuendana na Mabadiliko ....... 145
6.7 Mkakati wa Mawasiliano wa Mpango ....... 146
6.7.1 Lengo na Uratibu wa Mawasiliano ....... 146
6.7.2 Kanuni za Mawasiliano ....... 146
6.7.3 Hadhira na Mbinu za Kufikisha Ujumbe ....... 146
6.7.4 Mawasiliano na Mrejesho wakati wa Dharura ....... 147
6.7.5 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mawasiliano ....... 147

**SURA YA SABA: TATHMINI YA VIHATARISHI NA MBINU ZA KUVIKABILI ....... 151**

7.1 Muhtasari ....... 152
7.2 Maeneo ya Vihatarishi na Mikakati ya Kuvikabili ....... 152

KIAMBATISHO I: Uchambuzi wa Kina wa Mbinu na Afua Kufikia Ustawi ....... 162

KIAMBATISHO II: Viashiria vya Mwenendo/Utendaji na Matokeo kwa Kina ....... 304

# ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 2.1: Shabaha Kuu za Dira 2050 kwa Mpango IV ........ 23
Jedwali 3.1: Viashiria vya Mwenendo wa Utulivu wa Uchumi Jumla na Utabirifu.. 32
Jedwali 3.2: Viashiria vya Mwenendo wa Kuimarisha Uhimilivu wa Kifedha na Utabirifu ........ 33
Jedwali 3.3: Viashiria vya Mwenendo wa Ustahimilivu wa Sekta ya Nje na Uchumi Mseto ........ 35
Jedwali 3.4: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Kilimo ........ 38
Jedwali 3.5: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Viwanda na Uzalishaji Viwandani ........ 39
Jedwali 3.6: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Ujenzi ........ 40
Jedwali 3.7: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Madini na Uchimbaji wa Madini ........ 41
Jedwali 3.8: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia ........ 42
Jedwali 3.9: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Utalii ........ 43
Jedwali 3.10: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Fedha ........ 45
Jedwali 3.11: Viashiria vya Mwenendo wa Maendeleo ya Sekta ya Michezo, Sanaa na Ubunifu ........ 46
Jedwali 3.12: Viashiria vya Mwenendo wa Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo ........ 47
Jedwali 3.13: Viashiria vya Mwenendo wa Biashara ........ 49
Jedwali 3.14: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta Binafsi Imara ........ 50
Jedwali 3.15: Viashiria vya Mwenendo wa Ushirikiano wa Kimkakati Kati ya Nchi, Kikanda na Kimataifa ........ 52
Jedwali 3.16: Viashiria vya Mwenendo wa Urasimashaji wa Uchumi na Uendeshaji Wake ........ 53
Jedwali 3.22: Viashiria vya Huduma za Afya kwa Wote ........ 62
Jedwali 3.29: Viashiria vya Utendaji katika Uhifadhi wa Mazingira ........ 71
Jedwali 3.30: Viashiria vya Utendaji katika Ukuaji wa Miji Endelevu, Iliyopangwa na Kusimamiwa Vizuri ........ 72
Jedwali 3.31: Viashiria Muhimu katika Mageuzi ya Usimamizi Endelevu wa Ardhi ........ 73
Jedwali 3.32: Viashiria vya Utendaji katika Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ........ 74
Jedwali 3.33: Viashiria vya Mifumo ya Tahadhari ya Mapema na Uwezo wa Kitaasisi ........ 76
Jedwali 3.34: Viashiria vya Utendaji katika Kuimarisha Biashara ya Kaboni ........ 77
Jedwali 3.35: Viashiria Muhimu katika Utendaji wa Uchumi wa Buluu ........ 78
Jedwali 3.36: Viashiria vya Utendaji vya Nishati ........ 80
Jedwali 3.37: Viashiria vya Utendaji vya Mifumo Jumuishi ya Usafirishaji ........ 81
Jedwali 3.38: Viashiria Muhimu vya Utendaji wa Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ........ 82
Jedwali 3.39: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Mfumo Ikolojia wa Utafiti na Maendeleo wenye Ubora ........ 83
Jedwali 3.40: Viashiria vya Utendaji vya Ufuatiliaji wa Mfumo Endelevu wa Takwimu ........ 84
Jedwali 3.41: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Sekta ya Mageuzi ya Kidijitali ........ 85
Jedwali 3.42: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Miundombinu na Huduma za TEHAMA ........ 86
Jedwali 3.43: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Huduma Imara na za Kuaminika za Mawasiliano na Usafirishaji Vifurushi ........ 87

Jedwali 3.44: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uhamasishaji wa Uwekezaji ........ 89
Jedwali 3.45: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu ........ 90
Jedwali 3.46: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Kujenga Utawala wa Serikali za Mitaa Imara na Ufanisi ........ 91
Jedwali 3.47: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Kuimarisha Utawala wa Kidijitali na Usimamizi Mahiri wa Takwimu ........ 92
Jedwali 3.48: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Kukuza Mabadiliko ya Mtazamo ili Kuweka Mizizi ya Mageuzi ........ 93
Jedwali 4.1: Maeneo Muhimu ya Programu za Kielelezo na Matokeo ya Kila Mnyororo wa Thamani ........ 99
Jedwali 5.1: Mahitaji ya Fedha kwa kila Sekta ya Kipaumbele ........ 115
Jedwali 5.2: Muundo wa Ugharamiaji wa Mpango IV ........ 116
Jedwali 5.3: Makadirio na Uwiano wa Mchango wa Vyanzo Bunifu na Mbadala vya Fedha ........ 119
Jedwali 5.4: Mikakati ya Kupata Fedha kutoka Sekta Binafsi ........ 121
Jedwali 5.5: Mikakati ya Kutumia Rasilimali za Mashirika ya Umma ........ 125
Jedwali 5.6: Rasilimali Fedha Zinazohitajika Kufadhili Mpango IV: Vyanzo Vikuu...126
Jedwali 5.7: Ugharamiaji wa Mpango IV Kisekta (%) – Msisitizo Ukiwa katika Uwekezaji katika Utaratibu wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ........ 127
Jedwali 5.8: Ugharamiaji wa Mpango IV Kisekta (Shilingi bilioni) – Msisitizo Ukiwa katika Uwekezaji katika Utaratibu wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ........ 128
Jedwali 5.9: Muhtasari wa Hatua Muhimu za Kimkakati, Matokeo Tarajiwa, na Muda wa Utekelezaji ........ 130
Jedwali 7.1: Maeneo na Hatua za Udhibiti wa Vihatarishi (2026/27–2030/31) ........ 153

# ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 2.1: Mpango Elekezi 2050 - Dhana ya Mabadiliko ....19
Kielelezo 2.2: Vipaumbele na hatua za Utekelezaji wa Mpango Elekezi 2050 ....20
Kielelezo 6.1: Muundo wa Uratibu na Utekelezaji ....139

# MPANGO IV - KWA MUHTASARI



## Utangulizi

Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31 ni mpango wa kwanza katika awamu za utekelezaji wa Dira 2050 pamoja na malengo na shabaha zilizobainishwa katika Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2050 (Mpango Elekezi 2050). Mpango huu unaashiria mwanzo wa mwelekeo mpya wa maendeleo ya Tanzania, ukiwa umeandaliwa mahsusi kuanzisha mageuzi ya muda mrefu yaliyokusudiwa katika Dira 2050. Kwa msingi huo, dhima yake ni kuondokana na hatua za maboresho ya uendeshaji wa mfumo wa soko na kujikita katika kujenga msingi wa uchumi ushindani, jumuishi na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Aidha, unatafsiri matarajio ya Dira 2050 ya kufikia ustawi wa pamoja, haki na kujitegemea kwa kuweka kipaumbele katika afua za mageuzi na uwekezaji unaoongeza ufanisi wa masoko na kuimarisha taasisi na mifumo ya uzalishaji. Ukiongozwa na kaulimbiu ya "Mageuzi kwa Ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji wa Ajira", Mpango IV unasisitiza kuwa mageuzi thabiti ya kimuundo ndiyo msingi wa kuongeza fursa, kuboresha usimamizi wa uchumi, kuimarisha uwezo wa viwanda na kuzalisha ajira endelevu kwa Watanzania.

Mpango huu, kwa upande mmoja, unaunganisha, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Kwanza hadi wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano chini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Na kwa upande wa pili, unasukumwa na maono ya Dira 2050, ukilenga kuiweka Tanzania katika njia thabiti ya kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu ifikapo mwaka 2050. Shabaha kuu za Mpango IV ifikapo mwaka 2030/31 ni: pato la Taifa kufikia takriban dola za Marekani bilioni 118.052; kuongeza mchango wa sekta ya viwanda hadi asilimia 30 ya pato la Taifa, kwa bei za mwaka husika; kuzalisha zaidi ya MW 8,000 za umeme; kupanua upatikanaji wa huduma za intaneti kufikia wananchi wote; kuzalisha ajira mpya zenye staha milioni 8.5; na kupunguza umaskini uliokithiri kitaifa kuwa chini ya asilimia 5. Kwa ujumla, shabaha hizi zinaonesha dhamira ya makusudi ya Mpango IV katika kuongeza tija na ujumuishi, kuimarisha ushindani na kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo.

## Mawanda ya Mageuzi

Mpango IV umejengwa juu ya agenda pana ya mageuzi yenye lengo la kusasisha uendeshaji wa taasisi za umma, kuendeleza mageuzi ya utawala na kuimarisha uwezo wa Taifa kwa kutumia fursa zilizopo na zinazoibukia katika kukabiliana na changamoto mpya za kimaendeleo. Mageuzi ya utawala bora yanalenga maboresho ya kikatiba na kuimarisha utawala wa sheria, uwajibikaji, ufanisi na ushiriki wa wananchi. Mageuzi, vilevile yanalenga kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, kusasisha mfumo wa kodi, kuboresha usimamizi wa matumizi ya umma, kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuimarisha uhimilivu wa deni la taifa.

Mpango IV pia unaweka kipaumbele katika kujenga mageuzi ya msingi, hususan kwa kubadili usimamizi na utawala kuwa wa kidijitali zaidi. Katika eneo hili, Mpango unasisitiza kupanua upatikanaji wa huduma za serikali mtandaoni ili kupunguza urasimu usio wa lazima, kusasisha mifumo ya usajili wa biashara na utoaji wa leseni, na kuimarisha makusanyo ya mapato kwa njia za kidijitali. Hatua hizi zitaongeza tija, kupunguza gharama za uendeshaji biashara na kuimarisha uwazi.

Mpango pia unaweka kipaumbele katika mageuzi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na kuimarisha sekta binafsi. Katika eneo hili, Mpango unalenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kusasisha uendeshaji wa Maeneo Maalumu ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, kupanua fursa za ubia kati ya sekta za umma na binafsi, kukuza ushindani wa biashara ndogo na za kati, na kuvutia uwekezaji bora wa ndani na nje. Aidha, mageuzi ya ujuzi na rasilimali watu yanalenga kuwianisha uwezo na mahitaji ya soko ya nguvukazi na ujuzi unaohitajika katika ujenzi wa uchumi wa kisasa unaotegemea zaidi maarifa, kwa kuboresha mafunzo ya ufundi, ujuzi wa kidijitali na ubunifu. Mpango huu pia unalenga kukuza ushiriki wa Tanzania katika uchumi wa kikanda kwa kuimarisha zaidi ushindani wa biashara katika masoko ya ndani,kikanda na kimataifa. Vilevile, Mpango IV unaweka kipaumbele katika kufanyia mageuzi usimamizi wa miji, ardhi na mazingira. Katika eneo hili, Mpango unalenga kusimamia kasi ya ukuaji wa miji kwa ufanisi, kuboresha usimamizi wa ardhi, kuendeleza biashara ya ardhi, nyumba na majengo, na usimamizi wa mazingira. Hatua hizi zinalenga kuhakikisha kuwa mabadiliko ya kidemografia na matumizi ya ardhi yanaendelea kuwa endelevu.

## Wajibu wa Wadau wasio wa Kiserikali

### Sekta Binafsi: Injini ya Mageuzi

Moja ya mabadiliko makubwa katika Mpango IV ni kutambua kuwa sekta binafsi ndiyo injini kuu ya mageuzi ya kiuchumi. Katika muktadha huu, Mpango unaipa sekta binafsi nafasi ya kuongoza uzalishaji, uwekezaji, kukuza ubunifu, kuzalisha ajira, na kuhaulisha teknolojia. Aidha, Mpango unalenga kufungua zaidi fursa kwa sekta binafsi kuwekeza katika shughuli ambazo awali zilikuwa zikitekelezwa na sekta ya umma pekee. Ili kufanikisha hili, Mpango umeazimia kuboresha vivutio vya uwekezaji, kuboresha na kusasisha mifumo ya udhibiti na urekebu, uratibu, uwekezaji na uendeshaji wa shughuli katika maeneo ya uzalishaji kwa mauzo ya nje na kanda za uzalishaji, sanjari na kuweka mifumo wazi na inayotabirika ya usimamizi na uendeshaji wa uwekezaji kwa ubia kati ya sekta za umma na binafsi. Mabadiliko haya yanalenga kuchochea ujasiriamali, kuimarisha uwezo wa viwanda, kupanua minyororo ya thamani ya ndani, na kuvutia wawekezaji wa hadhi za kimataifa. Serikali, kwa upande wake, wajibu wake utakuwa zaidi katika kuwepo kwa mazingira wazi, fanisi, tabirifu na shindanishi ya kisheria na kiurekebu , sanjari na kuboresha upatikanaji wa huduma kwa umma.

### Taasisi Zisizo za Serikali, Asasi za Kiraia na Taasisi za Kijamii

Taasisi zisizo za Serikali, asasi za kiraia na taasisi za kijamii zimetambuliwa kuwa zina mchango mkubwa na hivyo zinatarajiwa kuendelea kuchangia katika kujenga uwezo wa jamii, tafiti na mapitio ya kisera, na kutoa huduma muhimu kama afya, elimu, ujuzi kwa vitendo, pamoja na uhawilishaji wa teknolojia na upatikanaji wa huduma za maji, mafunzo ya kilimo, utetezi na kuchangia maendeleo ya jamii. Katika muktadha huu, Mpango unalenga kuimarisha ushirikiano, kuratibu na kukuza ushirikiano kati ya Serikali, taasisi zisizo za serikali, asasi za kiraia na taasisi za kijamii kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa rasilimali, kuimarisha ufanisi wa utekelezaji, uwazi na kuhakikisha matumizi ya rasilimali yenye tija.

### Mbinu za Kufikia Mageuzi

Mpango unatumia dhana ya "U Tatu au kwa kifupi 3U, kumaanisha muunganiko wa hatua za Uwekezaji, Uhawilishaji na Ubunifu. Dhana hii inaweka mfumo wa kimkakati wa kuharakisha mageuzi ya kimuundo katika sekta za kipaumbele; kilimo, viwanda, madini, nishati, ujenzi, uchumi wa buluu, utalii, huduma za kifedha na sekta za ubunifu. Aidha, Mpango unatekeleza afua mtambuka kama kuendeleza matumizi ya teknolojia za kidijitali, kuimarisha diplomasia ya kiuchumi, na kurasimisha sekta isiyo rasmi ili kuongeza uwezo wake wa kuleta mageuzi ya kina.

## Programu za Kielelezo

Mpango huu unaanzisha mwelekeo mpya wa upangaji na utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Katika mwelekeo huu imeainisha shughuli msingi zinazoshabihiana na kuwezeshana na kuzijumuisha katika programu za kielelezo, zikiunganisha miundombinu, mabadiliko katika matumizi ya majaliwa na maliasili za nchi kwa lengo la kujenga minyororo ya thamani na kuimarisha ujumuishaji wa biashara za nchi katika masoko ya kikanda na kimataifa. Programu hizi zinatarajiwa kuwa majukwaa vichocheo katika mageuzi ya kiuchumi na kijamii nchini. Programu kuu za kielelezo zilizoainishwa kwa Mpango huu, ni:

i. Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi– kitovu cha viwanda, usafirishaji, ugavi na utalii kinachotegemea bandari ya maji ya kina kirefu, mifumo ya kisasa ya SEZ, na miundombinu ya usafiri wa aina mbalimbali.

ii. Kitovu Changamani cha Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga– utaongeza uzalishaji wa chuma nchini, kuchochea uzalishaji wa nishati, na kupunguza utegemezi wa bidhaa za chuma kutoka nje.

iii. Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia ya Kimiminika Lindi – utaifanya Tanzania kuwa kinara wa kikanda katika uongezaji thamani wa gesi, usalama wa nishati, na upatikanaji wa nishati kwa ajili ya uzalishaji viwandani.

iv. Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu Dodoma – mfumo wa teknolojia ya juu wa kuongeza thamani madini, teknolojia za betri na uzalishaji wa kisasa wa viwandani.

v. Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Uchakataji wa Mazao ya Kilimo -– inalenga kusasaisha kilimo kwa kupanua umwagiliaji, usindikaji wa mazao na minyororo ya thamani inayostahimili mabadiliko ya tabianchi.

vi. Kitovu cha Kisasa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Maziwa Makuu – kitovu cha kikanda cha uchakataji wa madini, viwanda vya kilimo na dawa, uchumi wa buluu na uwezeshaji wa biashara za mipakani.

vii. Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji Nchini– utaibadilisha miji ya Tanzania kuwa mifumo ya mijini inayozingatia mabadiliko ya tabianchi, usimamizi wa kidijitali, na uzalishaji wa kiuchumi.

Utekelezaji wa programu hizi za kielelezo, kwa kiasi kikubwa, zinategemea ufanisi wa uwekezaji unaoendelea katika nishati, maji, bandari, barabara, reli ya kisasa, na miundombinu ya TEHAMA. Aidha, mpangilio wake umetumia dhana ya usawa wa maendeleo kijiografia. Lengo ni kuhakikisha kuwa mageuzi ya kiuchumi yanajengwa juu ya msingi endelevu na yanaratibiwa kuchagiza kasi ya maendeleo kwa maeneo mbalimbali kijiografia. Vilevile, programu hizi zinaunganisha minyororo ya thamani kwa kuzingatia fursa zilizopo kimaeneo na hivyo kuvutia mitaji ya sekta binafsi ikisaidiwa na mfumo maalum wa ugharamiaji unaopendekezwa kwa ajili ya:

i. Kuandaa miradi inayokubalika kifedha katika kila programu ya kielelezo kwa kuendeleza minyororo ya thamani ya hatua za awali, kati na mwisho.

ii. Kuvutia wawekezaji wakuu watakaowavutia wazabuni na biashara ndogo, ndogo na za kati, kuimarisha mifumo ya uzalishaji na kuibua vyanzo vya mapato vinavyotabirika.

iii. Kuanzisha mifumo maalum ya kifedha kwa ajili ya kusaidia usindikaji wa mazao, uchakataji wa madini, uchumi wa buluu na minyororo ya thamani ya teknolojia.

iv. Kuruhusu mikataba ya minyororo ya thamani, kama vile mikataba ya manunuzi au usambazaji, kutumika kama dhamana ili kupunguza vikwazo vya upatikanaji wa fedha.

v. Kuunganisha minyororo ya thamani na masoko ya kikanda na kimataifa ili kuimarisha imani ya wawekezaji kwa Taifa letu na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

vi. Kutumia fursa chini ya utaratibu wa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania kupunguza gharama za uendeshaji biashara na kuweka mazingira ya uwekezaji yanayotabirika.

## Gharama na Mfumo wa Kugharamia Utekelezaji

Mpango umezingatia ubunifu na ustahimilivu katika mipango ya kugharamia shughuli za maendeleo. Katika kipindi cha miaka mitano, Mpango unalenga kuvutia rasilimali, takribani dola za Marekani bilioni 183 (Shilingi trilioni 477.7), huku sekta binafsi ikipangiwa kuchangia asilimia 70. Mpango, katika kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi, utatumia mbinu mseto unaochanganya vyanzo mbalimbali, vikiwa ni pamoja na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, ubia kati ya sekta za umma na binafsi, masoko ya mitaji ya ndani na ya kikanda, mifumo ya fedha za tabianchi na kijani, uhuishaji wa mali, mitaji ya ubia na hisa, uwekaji dhamana wa mali pamoja na uwekezaji wa kibiashara wa mashirika ya umma.

Kwa upande wa ugharamiaji wa umma, Mpango unalenga kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani, kutafuta mikopo ya masharti na gharama nafuu, kuoimarisha ufanisi wa matumizi ya fedha za umma, na kutumia fursa za ufadhili wa washirika wa maendeleo. Aidha, Mpango unalenga kufanyia mageuzi uendeshaji wa mashirika ya umma, yenye mali zinazozidi Shilingi trilioni 92.3, kwa kuimarisha ufanisi wa kibiashara, kuboresha usimamizi wa uendeshaji, na kuvutia uwekezaji mseto katika mashirika ya umma kupitia masoko ya mitaji na ubia kati ya sekta za umma na binafsi.

## Maadili ya Msingi Kuwezesha Utekelezaji

Mpango unajengwa juu ya maadili msingi ya taifa, ambayo ni uadilifu, uwajibikaji, uendelevu, ujumuishi, ubunifu, na nidhamu katika utendaji kazi. Aidha, Mpango unalenga kubadili mtazamo na fikra hususan kwa kuimarisha utamaduni wa utumishi wa umma, kujenga dhamira ya umiliki na ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa Mpango, na kuongeza tija ya taifa.

## Hitimisho

Mpango IV unaweka msingi utakoiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi ya kipato kati ngazi ya -juu ifikapo mwaka 2050. Hili litafikiwa kwa kuimarisha uwezo wa ushindani katika masoko, ustahimilivu wa uchumi katika misukosuko, na uendeshaji wa uchumi unaozingatia ubunifu. Kuhusiana na hili, Mpango unalenga kufanyia mageuzi makubwa uendeshaji wa biashara za uchukuzi na uzalishaji viwandani ukitambua kuwa sekta hizi ni vichocheo vikuu katika kuongeza tija, kuimarisha minyororo ya thamani, kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara, sanjari na kuchochea ukuaji wa uchumi na ajira kwa kiwango kikubwa.

Kwa msingi huo, Mpango unalenga kufanyia mageuzi muhimu mfumo wa utumishi wa umma, na ufanisi wa bandari, usafirishaji na shoroba za kibiashara. Aidha, unalenga kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa nishati, na kupanua uwezo wa viwanda vya ndani.

Mageuzi haya yataenda sambamba na kuimarisha ufanisi wa uwekezaji wa umma, huku sekta binafsi ikiongoza juhudi za ukuzaji wa maendeleo ya teknolojia, kuongeza uzalishaji viwandani, kuimarisha ushiriki katika masoko ya kikanda na kimataifa na kuchochea mageuzi ya muundo wa uchumi. Kupitia ushirikiano huu jumuishi, Mpango unaweka wazi njia na malengo makubwa kuwezesha ukuaji endelevu wa uchumi, mageuzi ya viwanda, na maendeleo ya kijamii kwa wote, ukiiweka Tanzania katika mwelekeo wa kufikia azma yake ya kuwa nchi ya hadhi ya kipato cha kati ngazi ya juu ifikapo mwaka 2050.

**Dkt. Tausi Mbaga Kida**
**Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais, Mipango na**
**Katibu Mtendaji - Tume ya Taifa ya Mipango**



# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI



# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Muhtasari

Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31 (Mpango IV) utakaotekelezwa kwa kipindi cha 2026/27–2030/31, unaanzisha awamu mpya ya utekelezaji wa maono ya Dira 2050 kwa kipindi cha muda miaka 25 ijayo. Mpango huu unaanzisha mabadiliko makubwa katika mfumo wa upangaji wa maendeleo nchini ikilinganishwa na mipango iliyotangulia. Muundo na maudhui ya mipango mitatu iliyotangulia chini ya Dira 2025 uliweka mkazo zaidi katika maboresho ya uendeshaji wa uchumi katika mfumo wa soko, hususan, ujenzi wa miundombinu msingi, uchumi wa viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali. Mpango IV umejikita katika kuimarisha zaidi misingi hiyo na kuchukua jukumu pana zaidi la kuanzisha safari ya mageuzi ya uchumi ya muda mrefu kama ilivyoainishwa katika Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050. Mpango huu pia unalenga kukuza uwezo wa ushiriki na ushindani wa uchumi katika masoko, kuongeza tija ya uzalishaji, na kujenga uchumi jumuishi na stahimilivu. Hivyo, Mpango huu unatafsiri azma kuu ya Dira 2050 ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu na ustawi jumuishi, haki na inayojitegemea. Tafsiri hiyo inaonekana kwenye afua za, programu na matokeo yanayopimika yanayolengwa kufikiwa kwa kipindi cha Mpango huu, yaani 2026/27–2030/31. Sura hii inaelezea chimbuko la Mpango, madhumuni, mbinu na mchakato wa uandaaji. Aidha, inatoa muhtasari wa maudhui yaliyomo katika andiko la Mpango na hivyo kuweka msingi kwa sura zinazofuata.

## 1.2 Chimbuko la Mpango

Maandalizi ya mipango ya maendeleo nchini, kwa zaidi ya miongo miwili, yameongozwa na azma ya muda mrefu ya kujenga taifa lenye ustawi jumuishi, haki, kujitegemea na linaloweza kushindana kimataifa. Katika kipindi cha Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Tanzania ilitekeleza mipango mitatu ya maendeleo ya miaka mitano (Mpango I–III), ambayo, licha ya tofauti za kimsisitizo, kwa pamoja, ililenga kujenga misingi ya ukuaji wa uchumi, kuimarisha mifumo-taasisi na kuboresha maendeleo ya jamii. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mipango hiyo ni kuimarika kwa utulivu wa uchumi na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi, utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu, pamoja na mafanikio katika sekta muhimu za kijamii. Hata hivyo, tathmini ya hali halisi inaonesha kuwepo kwa changamoto kadhaa, zikiwa ni pamoja na kasi ndogo ya mageuzi ya muundo wa uchumi, tija ndogo ya uzalishaji, ukuaji wa uchumi unaotegemea sekta chache, uwezo mdogo kifedha, pamoja na changamoto za uratibu na utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Kukamilika kwa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, mnamo Juni 2026, kunatoa fursa ya kipekee kwa Tanzania kutafakari na kupambanua maono mapya kwa maendeleo ya muda mrefu. Nchi sasa inaingia katika hatua mpya ya upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo inayoongozwa na Dira 2050, ambayo inaweka maono ya maendeleo kwa kipindi cha miaka 25 ijayo. Dira hii inalenga kuleta mageuzi ya kiuchumi na ustawi wa jamii, na kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi yenye kipato cha kati ngazi ya juu, yenye uchumi unaokadiriwa kufikia Pato la Taifa la takriban dola za Marekani trilioni moja, na wastani wa kipato cha mtu mmoja cha takriban dola za Marekani 7,000 ifikapo mwaka 2050.

Ili kufanikisha matarajio haya, Dira 2050 inasisitiza mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii yafanyike, yakichochewa na ongezeko la tija ya uzalishaji na ubunifu wa uendeshaji. Mageuzi haya yanajikita katika njia kuu tatu zinazohusiana na : kuongeza tija katika shughuli za kiuchumi zinazoendelea; kufanya mabadiliko ya mkakati wa

kuboresha muundo wa shughuli za uchumi zinazoendelea; na kuvutia uwekezaji katika sekta mpya zenye uwezo wa kubadili muundo wa uzalishaji, hususan kwa kukuza uwezo na matumizi ya teknolojia, kuimarisha utendaji wa kitaasisi na kuunganisha uchumi katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Dira 2050 imeandaliwa kwa kutambua kwamba, Tanzania, baada ya zaidi ya miaka 65 ya uhuru, haiwezi tena kutegemea kasi ndogo ya ukuaji wa maendeleo. Hivyo, Dira inazingatia kuwa Taifa linahitaji mageuzi makubwa, ya haraka na ya kimkakati yanayotegemea matokeo, tija na ubunifu. Mageuzi haya yanapaswa kutumia kikamilifu nafasi ya majaliwa mkakati ya Tanzania kijiografia, utajiri wa rasilimali asilia, idadi na uwezo wa rasilimali watu, pamoja na historia yake ya utulivu wa kisiasa, kuharakisha mageuzi ya uchumi na ustawi wa jamii. Masuala haya sanjari na nia ya kulinda na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mipango iliyopita, ndiyo yanayounda msingi wa Mpango IV.

Miongoni mwa mafanikio yaliyotokana na utekelezaji wa mipango iliyotangulia na hivyo kuzingatiwa katika Mpango huu ni pamoja na: uthabiti wa uchumi jumla, mafanikio katika maendeleo ya jamii na uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu msingi. Mafanikio haya, hata hivyo, bado yana changamoto kadhaa, mintaarafu: uwezo mdogo katika kukimu bajeti kufuatia ongezeko la haraka la mahitaji ya maendeleo, makusanyo madogo ya mapato ya ndani, ukuaji wa uchumi unaotegemea sekta chache, na ongezeko dogo la thamani. Aidha, kuna changamoto ya kasi ndogo ya usetushaji wa mauzo ya nje, sehemu kubwa ya uchumi kuwa katika shughuli zisizo rasmi, na vikwazo vya kimuundo na utekelezaji ndani ya taasisi za umma. Haya ni maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mpango IV.

## 1.3 Mpango wa Kwanza Katika Utekelezaji wa *Dira 2050*

### 1.3.1 Uhusiano wa Mpango IV na *Dira 2050*

Mpango IV ni wa kwanza katika mfululizo wa mipango mitano ya muda wa kati itakayoandaliwa kutekeleza Mpango Elekezi 2050. Hivyo, Mpango huu unaanzisha utekelezaji wa Dira 2050 na safari ya mageuzi ya miaka 25. Ukiwa ni wa kwanza katika hatua za utekelezaji wa Dhana ya Mabadiliko ya Mpango Elekezi 2050, Mpango IV unaanzisha mageuzi ya msingi ya uwekezaji wa kimkakati na uimarishaji wa taasisi zinazohitajika kuwezesha ongezeko la tija na ushindani wa kibiashara. Huu ni wakati wa kujifunza kutoka katika uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mipango iliyopita na kuuelekeza nguvu katika kujenga mwelekeo wa maendeleo ya baadaye.

Kwa mantiki hiyo, Mpango huu unaashiria mwelekeo mpya wa kimkakati kufuatia kukamilika kwa Dira 2025 na kuanza kwa utekelezaji wa Dira 2050. Mpango unaweka msisitizo wa kuondoka katika hatua za ujenzi wa misingi ya kukuza uchumi na hivyo kuingia katika hatua zitakazoharakisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii yanayozingatia ubunifu na tija. Mpango IV unaakisi mtazamo mpya wa maendeleo ambapo sekta binafsi imepewa nafasi ya kuongoza uwekezaji, uzalishaji, ubunifu wa teknolojia, uzalishaji wa ajira na uwezo wa kusetusha uchumi. Kadhalika, sekta ya umma itaongoza katika kuweka mazingira wezeshi ya biashara, kuongeza ufanisi na kuhakikisha uwepo wa utawala unaotabirika na wenye uwazi ili kujenga sekta binafsi imara.

Mpango huu pia unaweka mkazo katika kuondokana na utaratibu wa kufanya kazi kwa mazoea kwa kuzingatia falsafa ya Taifa ya maendeleo yenye vipaumbele vinne: Mageuzi, Maridhiano, Kujenga Upya na Ustahimilivu. Mwelekeo huu unaambatana na mabadiliko ya fikra pamoja na kuimarishwa kwa nidhamu katika utoaji wa huduma za umma. Kwa kufanya hivyo, Mpango huu unaweka msingi thabiti katika safari ya Tanzania kuelekea mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii yanayotarajiwa ifikapo mwaka 2050.

### 1.3.2 Mpango Unaoakisi Muundo wa *Dira 2050*

*Dira 2050* inaanzisha muundo mpya wa upangaji wa mipango ya maendeleo unaotofautiana na ule uliokuwa ukitumika katika kipindi cha utekelezaji wa Dira 2025. Katika kipindi hicho, michakato ya kuandaa mipango ya maendeleo ya taifa, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa mara nyingi ilikumbwa na changamoto za uratibu usioshirikishi. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba mipango ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa iliandaliwa aghalabu ikizingatia kikamilifu vipaumbele na mikakati ya taifa. Kutokana na hali hiyo, kulikuwa na baadhi ya shughuli za maendeleo za kitaasisi zilizokuwa zinajirudia, vipaumbele kushindwa kuwiana, muda wa utekelezaji usio wianifu, pamoja na mgawanyo wa rasilimali usio toshelevu. Hali hii ilipelekea kupungua kwa kasi na ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika ngazi na maeneo mbalimbali na kudunisha uwajibikaji katika utekelezaji wa mipango.

Mfumo wa uandaaji wa mipango ya maendeleo wa Dira 2050 kwa hiyo umesanifiwa kuhakikisha uwiano wa juhudi za maendeleo kitaifa, kimikoa na serikali za mitaa, kwa upande mmoja na maono ya muda mrefu pamoja na mageuzi ya uchumi na ustawi wa jamii yaliyolengwa, kwa upande mwingine. Katika kipindi hiki, Tume ya Mipango itajikita zaidi katika kuongoza na kuratibu uandaaji wa mipango ya kitaifa. Kadhalika, Tume itaongoza usimamizi wa mipango ya uendeshaji wa uchumi na utekelezaji wa programu kubwa za kitaifa, ikiwa ni pamoja na programu za kielelezo na utayarishaji na usimamizi wa mikakati ya maendeleo ya muda mrefu. Hivyo, jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya mikoa na serikali za mitaa litakasimiwa kwa Ofisi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu–Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), itakuwa na jukumu la kuwezesha, kuratibu na kujenga uwezo wa ofisi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa bila kuhodhi madaraka. Lengo ni kuhakikisha kuwa mipango ya mikoa na serikali za mitaa inaendana na usanifu na muundo wa utekelezaji unawiana na vipaumbele vya Taifa.

Muundo huu mpya unaakisi dhamira ya Dira 2050 ya kuendeleza na kuimarisha ugatuzi wa madaraka kama chachu ya mageuzi ya uchumi na ustawi wa jamii, badala ya kubaki katika muktadha wa kiutawala pekee. Aidha, tawala za mikoa na serikali za mitaa katika muundo huu zimetambulika kuwa wamiliki na wahusika wakuu katika kuibua mipango na afua za maendeleo zinazozingatia mahitaji halisi ya maeneo kuendana na malengo na shabaha za maendeleo kitaifa. Utekelezaji wa jukumu hili utaongozwa na uchambuzi wa hali ya uchumi kwa maeneo husika na kujielekeza katika kukuza minyororo ya thamani, kuimarisha na kusasisha mifumo ya uzalishaji, ukuzaji wa ajira zenye staha na kusimamia maendeleo endelevu ya miji. Kwa kugatua uandaaji wa mipango ya maendeleo, bajeti na uratibu wa utekelezaji karibu na jamii, taasisi na mashirika, muundo huu utaboresha uwezo wa kutatua changamoto, kuongeza kasi ya utekelezaji na kuinua uwajibikaji.

Mabadiliko haya ya kimfumo yanaakisi dhamira ya Dira 2050 katika mageuzi, maendeleo ya kimaeneo na kuchochea ukuaji wa uchumi wenye wigo mpana kisekta. Kwa kuwezesha mamlaka za serikali za mitaa na kuratibu upangaji kikanda, vipaumbele vya maeneo vinaunganishwa kikamilifu katika minyororo ya thamani ya kitaifa, shoroba za kiuchumi na kongani za uzalishaji. Mfumo huu unaboresha uratibu, unapunguza migongano na urasimu unaochelewesha maendeleo. Mfumo huu pia unaimarisha utekelezaji kwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu katika ngazi husika. Kadhalika, unajenga uwezo wa taasisi katika ngazi za mikoa na serikali za mitaa na kuchochea ubunifu, uwekezaji wa ndani na mipango ya maendeleo inayozingatia uhalisia wa mahitaji kimaeneo.

Dira 2050 inaimarisha muundo rasmi wa ugatuzi wa madaraka unaozingatia mahitaji ya maendeleo ya eneo husika. Kupitia Mpango IV, muundo huu utawezesha mageuzi ya uchumi yaliyofungamanishi na jumuishi, pamoja na kuboresha ustawi wa jamii kulingana na uhalisia wa maeneo husika. Kwa kufanya hivyo, Mpango huu unaweka

msingi wa Tanzania yenye maendeleo yuwianifu kijiografia na hivyo kufikia malengo ya mageuzi makubwa ya kiuchumi jumuishi ifikapo mwaka 2050.

## 1.4 Mbinu na Mchakato wa Ushirikishaji Wadau

Uandaaji wa Mpango IV umehusisha mchakato mpana na jumuishi, unaozingatia uzoefu na ushahidi wa kitaalam uliotokana na uchambuzi wa kina uliofanyika wakati wa maandalizi ya Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050. Katika mchakato huu, Serikali iliendesha uchambuzi wa kitaalamu, majadiliano ya kitaifa na mashauriano ya kina kuhusu mada mahususi ili kuhakikisha ujumuishi wa wadau na kuzingatia uhalisia wa masuala ya maendeleo yanayohitaji kushughulikiwa. Makundi ya wadau mbalimbali yalihusika, ikiwemo wizara, idara na mashirika; tawala za mikoa na serikali za mitaa; sekta binafsi; taasisi za kiraia; taasisi za vyuo vya elimu ya juu; taasisi za kitaaluma; na washirika wa maendeleo. Ushirikishwaji huu ulitoa mawanda mapana ya ufahamu wa changamoto za kisekta, fursa zinazoibukia pamoja na vipaumbele mtambuka. Vipaumbele hivi ni pamoja na usawa wa kijinsia, uimarishaji wa utawala bora, ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, athari za mageuzi ya kidijitali na mwenendo wa soko la ajira nchini.

Wakati huo huo, uchambuzi wa kina wa masuala muhimu ya kuzingatiwa katika Mpango ulifanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali za kitaalamu, ikiwemo uchambuzi wa takwimu, tathmini ya matukio na hali mfanano ya kimazingira, mchanganuo wa mienendo ya viashiria muhimu vya uchumi jumla, mabadiliko ya idadi ya watu, muundo wa kidemografia na hali na mazingira kimaeneo. Aidha, kwa kila jambo lililoonekana ni muhimu kuzingatiwa katika Mpango IV, ulinganisho wa kimataifa ulifanyika na nchi ambazo hivi karibuni, zimeweza kufikia hadhi ya uchumi wa kipato cha kati juu. Utafiti pia ulifanyika kutathmini muundo na mwelekeo wa sekta kama viwanda, pamoja na viashiria vya ustawi wa jamii, mikakati ya ukuaji wa uchumi na shughuli pamoja na namna nchi hizo zilivyoweza kufikia uwiano wa uchumi wa kijani.

Aidha, mchakato ulihusisha kuandaa majukwaa kwa ajili ya kujadili masuala hayo kwa kina. Pia, mchakato huo ulifaidika na matokeo na mafunzo yaliyotokana na kazi za uchambuzi zinazofanywa na Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji; tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) I na II; mapitio na uandaaji wa sera na mkakati wa uwekezaji nchini; tathmini maalumu ya sekta zilizosaidia kuandaa vipaumbele vya Mpango IV. Rasimu kadhaa za Mpango zilipitishwa katika mchakato wa mapitio na tathmini hatua kwa hatua ili kujiridhisha kuwa zinazingatia uhalisia na maoni yaliyotolewa katika warsha za wadau, mtiririko mzuri, kujiridhisha kuwa zinakidhi mahitaji katika mazingira ya sasa na yajayo, na kujenga uelewa na muafaka wa pamoja wa Taifa.

Wakati Tanzania inaingia katika awamu ya kwanza ya mageuzi ya uchumi na ustawi wa jamii yaliyoanishwa katika Dira 2050, ni muhimu kubaini changamoto na fursa muhimu za maendeleo katika kipindi cha muda wa kati. Sura inayofuata inachanganua masuala muhimu na utaratibu unaopaswa kuzingatiwa ili kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio imara, jumuishi na unaostahimili mabadiliko ya tabianchi. Sura hiyo inaainisha falsafa msingi, uchambuzi na mpangilio wa nguzo za Dira 2050, Nadharia ya Mabadiliko, inayoongoza mchakato wa mageuzi. Pia, Sura imeonesha vigezo vya uchaguzi wa vipaumbele vya Mpango na mpangilio wa utekelezaji wake. Vipengele hivi vinaunda muundo-dhana wa Mpango, ambamo maudhui na misingi ya mikakati ya Mpango huu yamejengwa na kuainishwa.

## 1.5 Mpangilio wa Kitabu

Mpango IV umeandaliwa kwa lengo la kubainisha mwelekeo utakaoongoza mageuzi ya uchumi na ustawi wa jamii nchini katika kipindi cha miaka mitano.

Sura ya Kwanza inaainisha muktadha, mapito ya historia kutoka Dira 2025 hadi Dira 2050, na kubainisha mbinu zilizotumika katika kuandaa Mpango huu.

Sura ya Pili inaeleza masuala muhimu ya maendeleo ambayo Tanzania inapaswa kuyazingatia na kuyashughulikia ili kufikia malengo ya maendeleo yaliyoainishwa katika Dira 2050. Aidha, sura hii inaeleza falsafa ya maendeleo ya taifa katika kipindi cha sasa, kufafanua nguzo na vichocheo vya mageuzi ya kiuchumi na kijamii yanayokusudiwa, kuwasilisha Nadharia ya Mabadiliko itakayoongoza mageuzi hayo, pamoja na kueleza mantiki ya vipaumbele na msingi wa mpangilio wa hatua za utekelezaji wake.

Sura ya Tatu inaainisha mikakati na mbinu ambazo Tanzania itatumia ili kuweza kuharakisha mageuzi ya kiuchumi, kujenga uwezo wa rasilimali watu, kuboresha mifumo ya utawala na kuweka usimamizi thabiti na endelevu wa mazingira. Pia inaainisha sekta na afua za kimageuzi, ambazo utekelezaji wake utachangia kwa kiasi kikubwa kasi ya mabadiliko ya muundo na thamani ya uchumi.

Sura ya Nne inajikita katika vipaumbele vya Mpango kwa kubainisha programu chache za kielelezo zitakazotekelezwa kwa msukumo wa kipekee katika kipindi cha Mpango. Programu hizi zitaweka msingi wa mageuzi katika vipindi vijavyo, ikiwemo mageuzi katika maeneo mahsusi ya kijiografia, kuendeleza uchumi wa viwanda, kuimarisha rasilimali watu na kukuza maendeleo ya teknolojia.

Sura ya Tano inajikita katika mbinu za kupata rasilimali fedha zinazohitajika ili utekelezaji malengo na shabaha za matokeo tarajiwa ya Mpango. Sura hii inasisitiza juu ya upatikanaji wa mitaji ya uwekezaji kutoka sekta binafsi, ubunifu wa vyanzo vipya vya mitaji na mfumo mpya wa uwekezaji, pamoja na matumizi ya mbinu mseto za uwekezaji.

Sura ya Sita inaeleza mpangilio wa utekelezaji, mifumo-taasisi ya uratibu, usimamizi wa utendaji na kujifunza kutokana na uzoefu unaopatikana katika utekelezaji, pamoja na msukumo wa kufikia matokeo unaotokana na nidhamu na uwajibikaji.

Sura ya Saba inahitimisha kwa kufanya tathmini ya vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji na kubainisha mikakati ya kuvikabili.



# MUHTASARI – SURA YA KWANZA

TANZANIA · MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA

## MPANGO IV

### Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

2026/27 — 2030/31

Mpango wa kwanza wa muda wa kati ulioandaliwa kutekeleza **Dira 2050**, ukiashiria mabadiliko ya msingi kutoka uimarishaji kwenda mageuzi, tija na ushindani wa muda mrefu.

**1** MPANGO WA KWANZA CHINI YA DIRA 2050

**5** MIAKA YA UTEKELEZAJI

**7** MUUNDO WA SURA

**3** NJIA ZA MAGEUZI

MPANGO IV · Sura ya 1 — *Utangulizi · 2026/27–2030/31*

SAFARI YA MAENDELEO YA TANZANIA

## Kutoka Dira 2025 hadi Dira 2050

Mipango minane mfululizo ya miaka mitano inajumuisha safari ya maendeleo ya muda mrefu ya Tanzania. Mpango IV ni kilele kinachozindua dira mpya ya miaka 25.

★ ULIOPO

| MPANGO I | MPANGO II | MPANGO III | MPANGO IV | MPANGO V | MPANGO VI | MPANGO VII | MPANGO VIII |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2011/12–15/16 | 2016/17–20/21 | 2021/22–25/26 | 2026/27–30/31 ★ Kuzindua Dira 2050 | 2031/32 | 2036/37 | 2041/42 | 2046/47 · Dira 2050 |

**$1T**
**UCHUMI IFIKAPO 2050**
Tanzania kuwa na uchumi wa dola za Marekani trilioni moja, taifa lenye ushindani wa kimataifa.

**>$7K**
**PATO LA TAIFA KWA MTU**
Kuongeza pato la mtu mmoja kwa mwaka kufikia dola za Marekani 7,000, ongezeko kubwa la ustawi.

**UMIC**
**HADHI YA KIPATO**
Kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu. Tanzania yenye ustawi, jumuishi na kujitegemea.

MPANGO IV · Sura ya 1 — *Safari ya Maendeleo · Shabaha za Dira 2050*

MKAKATI MKUU WA MPANGO IV

## Njia Tatu za Mageuzi Zinazotegemeana

Zinazoegemea Uongozi wa Sekta Binafsi na Uwezeshaji wa Sekta ya Umma, zikiungwa mkono na Falsafa ya Vipaumbele Vinne, Mageuzi, Maridhiano, Kujenga Upya na Ustahimilivu.

NJIA YA 01

**Kutegemea Njia Iliyopo, Kuimarisha Kinachofanya Kazi**

Kujenga juu ya misingi iliyopo ambapo kuna mifumo imara. Kutumia mazingira tulivu ya uchumi jumla, mafanikio mapana ya kijamii, na uwekezaji mkubwa katika miundombinu.

NJIA YA 02

**Kuachana na Njia ya Zamani, Kubadili Kinachopaswa Kubadilika**

Kufanya mageuzi ya kimuundo ya makusudi ili kuachana na mienendo isiyokidhi tena malengo ya maendeleo, ukusanyaji mdogo wa mapato, mapungufu ya mauzo nje, sekta isiyo rasmi na uratibu dhaifu.

NJIA YA 03

**Njia ya Mageuzi, Kubadili Muundo wa Uchumi**

Kubadili muundo wa uzalishaji wa Tanzania, kuimarisha uwezo wa kiteknolojia, kuongeza mtangamano wa kimataifa, na kubadili utamaduni wa kitaasisi na kibiashara.

**Uongozi wa Sekta Binafsi · Uwezeshaji wa Sekta ya Umma**

Falsafa ya Vipaumbele Vinne, Mageuzi, Maridhiano, Kujenga Upya na Ustahimilivu, inachochea mabadiliko ya fikra katika taasisi, utamaduni wa kibiashara na ushiriki wa wananchi.



MABADILIKO YA KIMKAKATI

## Mtazamo Mpya wa Maendeleo

Mpango IV unaihamisha Tanzania kutoka ukuaji wa kimsingi kwenda mageuzi ya kasi, yanayoongozwa na ubunifu na tija — yanayoratibiwa kupitia andiko lenye muundo wa sura saba.

### Kipindi cha Dira 2025

Ukuaji wa kimsingi · ulioongozwa na serikali, uratibu uliogawanyika · maendeleo ya hatua kwa hatua yenye mapungufu · mipango iliyoratibiwa kati · michakato sambamba ya mikoa na halmashauri.

### Kipindi cha Mpango IV / Dira 2050

Mageuzi ya kasi yanayoongozwa na ubunifu · sekta binafsi kitovu · mageuzi thabiti ya kimuundo · mipango iliyogatuliwa inayoongozwa na halmashauri · mfumo madhubuti kutoka taifa hadi mtaa.

MUUNDO WA ANDIKO — SURA SABA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 Utangulizi | 02 Masuala | 03 Mwelekeo | 04 Programu | 05 Ugharamiaji | 06 Utekelezaji | 07 Vihatarishi |









# SURA YA PILI: MASUALA YALIYOZINGATIWA NA UHUSIANO NA DIRA 2050








# SURA YA PILI

# MASUALA YALIYOZINGATIWA NA UHUSIANO NA DIRA 2050

## 2.1 Muhtasari

Sura hii inajengwa juu ya msingi uliowekwa katika Sura ya Kwanza. Inabainisha mfumo wa kimkakati unaoongoza muundo wa Mpango IV, ambao ni mpango wa kwanza katika utekelezaji wa Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050. Katika juhudi za kutekeleza Dira 2050, Tanzania ina fursa nyingi muhimu, zikiwemo ongezeko la idadi ya watu na nguvu kazi, utajiri wa rasilimali asilia, nafasi ya kimkakati kijiografia pamoja na utawala bora. Hata hivyo, Tanzania inakabiliwa na changamoto za kimuundo ambazo ni lazima zishughulikiwe ili kufikia shabaha ya kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu ifikapo mwaka 2050 ikiwa na uchumi jumuishi, shindani na stahimilivu kwa mabadiliko ya tabianchi.

Kukamilika kwa Dira 2025 na kuanza kutekeleza Dira 2050 kunahitaji mabadiliko makubwa ya namna Tanzania inavyopaswa kujiandaa kukidhi mahitaji ya maendeleo ya kipindi kijacho. Wakati Dira 2025 ilijikita zaidi katika kujenga miundombinu ya msingi na kuimarisha uthabiti wa misingi ya uchumi jumla, Dira 2050 inahitaji kuongeza tija, kujenga uchumi wa viwanda, kuimarisha miundombinu ya biashara na usafirishaji, kuongeza ushindani wa kibiashara, kuimarisha ustahimilivu wa bajeti na kuboresha ufanisi wa taasisi. Kwa mantiki hiyo, Mpango IV utatekelezwa katika mazingira ya mabadiliko, ambapo matakwa na uwezo wa kufikia malengo ya maendeleo tarajiwa lazima viwianishwe kupitia hatua thabiti na za makusudi za mageuzi, kukuza uwekezaji na uongozi wenye ubunifu.

Sura hii inaeleza mfumo huo wa kimkakati. Inaanza kwa kubainisha mwelekeo wa Mpango IV, ambao unaongozwa na kaulimbiu isemayo "Mageuzi kwa Ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji wa Ajira". Kaulimbiu hii inaonesha umuhimu wa kufanya mageuzi ya miundo ya kitaasisi, kujenga uchumi wa viwanda na kukuza ajira zenye tija na staha. Aidha, sura hii inaeleza usanifu wa Mpango IV ambao umejengwa juu ya nguzo kuu tatu: uchumi imara, jumuishi na shindani; uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; na hifadhi ya mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Nguzo hizi zinashikamanishwa na vichocheo wezeshi kadhaa, kama vile upatikanaji wa nishati, uchukuzi, sayansi, teknolojia na ubunifu, utawala unaowezeshwa na teknolojia za kidijitali na mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji. Vichocheo hivyo vinajengwa juu ya misingi muhimu ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na utawala bora, ugatuzi wa madaraka, usalama wa taifa na mtazamo na fikra chanya za kimaendeleo.

Vilevile, sura hii pia inaelezea falsafa inayoongoza mwelekeo wa maendeleo ya Tanzania kwa wakati huu na Nadharia ya Mabadiliko iliyobainishwa katika Mpango Elekezi 2050. Kwa pamoja, vipengele hivi vinafafanua jinsi mageuzi yanayotarajiwa kutokea kwa kuendeleza shughuli na mifumo iliyopo, kuboresha na kuongeza tija na matumizi ya ubunifu katika muundo wa uzalishaji uliopo, na kufanyia mabadiliko makubwa ya muundo wa uchumi na biashara. Vile vile, Sura hii inaainisha masuala muhimu yanayohitaji kushughulikiwa ili kufanikisha malengo ya Mpango; inaelezea maadili na kanuni zinazoongoza mageuzi na kuainisha sababu za uchaguzi na mpangilio wa hatua za utekelezaji wa afua zilizopendekezwa. Mwisho, inaonesha matokeo yanayotarajiwa kwa muda wa kati na mrefu kuendana na mwelekeo wa kimkakati wa Mpango IV. Kwa ujumla, vipengele hivi vinafafanua maudhui ya uchambuzi na msingi wa kimkakati wa Mpango IV.

## 2.2 Masuala Muhimu ya Maendeleo

Miongoni mwa masuala muhimu ya maendeleo yaliyozingatiwa katika Mpango IV ni mageuzi ya muundo wa uchumi, yatakayochochewa na ujenzi wa uchumi wa viwanda, ongezeko la tija, maendeleo ya sekta binafsi, mazingira wezeshi ya uwekezaji, na uimarishaji wa miundombinu. Ili kutimiza azma ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha viwanda, usafirishaji na biashara, Tanzania inahitaji kushughulikia changamoto zinazoathiri ufanisi wa kisekta, kuongeza thamani ya bidhaa na huduma, na matumizi ya teknolojia. Hivyo, ili kuwezesha ukuaji endelevu wa uchumi kuna haja ya kuimarisha mifumo ya uzalishaji, urasimishaji wa shughuli za sekta isiyo rasmi na kukuza ujasiriamali. Aidha, Tanzania inapaswa kuongeza utayari wa uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara, pamoja na kuimarisha utawala bora na kutoa huduma bora za umma kwa kuboresha miundo ya kitaasisi. Hatua hizi zitasaidia kuimarisha uthabiti wa sera, kuboresha mifumo ya udhibiti na kusimamia rasilimali kwa ufanisi. Kwa kufanya hivyo, sekta binafsi itakua zaidi, ubunifu utaongezeka, ushindani utaimarika na maisha ya wananchi yataboreka. Kadhalika, mbinu hizi za kimkakati zitasaidia kupunguza athari za mabadiliko ya mazingira ya uchumi na siasa duniani yanayoweza kuathiri biashara, uwekezaji na uthabiti wa uchumi wa taifa.

Upatikanaji wa umeme wa uhakika na gharama nafuu kwa wote ni miongoni mwa masuala ya msingi katika kuchochea maendeleo nchini. Umeme unawezesha kuendeleza viwanda, kuongeza tija katika shughuli za kiuchumi na kuboresha kutoa huduma za kijamii. Bila kuwa na umeme wa uhakika na wa gharama nafuu, jitihada za kuvutia uwekezaji, kupanua biashara na kuendeleza miundombinu hazitafanikiwa ipasavyo. Hali hii itapunguza kasi ya uchumi kukua na kuathiri ustawi wa wananchi.

Kadhalika, Mpango IV unasisitiza kukuza uwezo wa rasilimali watu, kuhamasisha ushiriki wa jamii, kuimarisha ustahimilivu wa mazingira na kuleta mabadiliko chanya ya kimitazamo na kifikra. Hivyo, Mpango IV unatambua kuwa kuleta mageuzi ya uchumi kunapaswa kwenda sanjari na kutoa elimu bora, kukuza ujuzi, kuboresha huduma za afya, kuimarisha mifumo ya kinga ya jamii na maendeleo jumuishi ili kufaidika kikamilifu na faida za kidemografia. Aidha, ni muhimu kuimarisha uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usimamizi endelevu wa rasilimali. Haya, yanahitaji hatua thabiti za usimamizi wa matumizi ya ardhi, upangaji sahihi wa miji na makazi, udhibiti wa majanga na matumizi ya teknolojia zenye uzalishaji mdogo wa kaboni na taka. Vilevile, kukuza ubunifu, nidhamu na kuimarisha uwajibikaji miongoni mwa wananchi na watumishi wa umma. Aidha, Mpango unasisitiza juu ya kufanya mageuzi ili kuinua ufanisi, kuimarisha utendaji wa sekta ya umma, kuchochea uwekezaji, kuboresha mazingira ya biashara na kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa jumuishi, endelevu kimazingira na unaboresha hali ya maisha ya Wataznania wote. Pia, maendeleo yatajumuisha ustahimilivu dhidi ya athari za mivutano ya kijiopolitiki katika ngazi ya kimataifa.

Kwa ujumla, masuala haya ya maendeleo yanaonesha umuhimu wa kuelekeza jitihada za kitaifa katika kujenga uchumi wenye tija, kukuza ushindani na kuweka muunganiko imara wa sekta mbalimbali, ambao unaunda msingi wa mwelekeo wa kimkakati wa Mpango IV.

## 2.3 Dhima: Tamko la Mwelekeo wa Kimkakati

Kaulimbiu ya Mpango IV, "Mageuzi kwa Ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji wa Ajira" inaakisi msisitizo wa Mpango wa kufanya mageuzi makubwa na ya dhati ya kimaendeleo. Lengo ni kuongeza tija katika uzalishaji, kukuza ushindani wa kibiashara na kuimarisha uhusiano kati ya sekta. Mwelekeo huu ni muhimu katika kuiwezesha Tanzania kufikia azma ya Dira 2050 ya kuwa kitovu cha viwanda, usafirishaji na biashara. Kwa muktadha huu, kitovu cha viwanda kunamaanisha kujenga uwezo wa kuzalisha na

kuongeza thamani ya bidhaa, ambapo uzalishaji utafanyika kwa ufanisi na ubora ili kukidhi mahitaji ya ndani na kuongeza mauzo nje. Aidha, kuwa kitovu cha usafirishaji na uchukuzi kunamaanisha kuijengea Tanzania uwezo wa kimkakati wa kusafirisha, kuhifadhi na kusambaza bidhaa kwa ufanisi, na hivyo kuiunganisha na masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Vilevile, kuwa kitovu cha biashara kunamaanisha kujenga mazingira wezeshi ya biashara ili kuvutia uwekezaji, kukuza ujasiriamali, kutoa huduma bora na kuchochea ubunifu, ushindani pamoja na kupanua shughuli za kiuchumi zenye tija. Kwa kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha viwanda, usafirishaji na biashara, Mpango unalenga kuboresha maisha ya wananchi kwa kuongeza fursa za ajira, mapato, upatikanaji wa bidhaa na huduma, na kuboresha ustawi wa kiuchumi na kijamii. Kwa muktadha huu, Mpango unalenga kuifanya Tanzania kuwa kinara wa maendeleo endelevu na jumuishi kikanda.

## 2.4 Mwelekeo wa Kimkakati

Mpango una mwelekeo wa kimkakati unaolenga kuchochea maendeleo ya taifa yaliyo jumuishi, endelevu na himilivu. Utekelezaji wa mkakati huu utahusisha kuongeza fursa za kiuchumi na ajira, na kuimarisha minyororo ya thamani katika sekta zenye matokeo makubwa. Vilevile, Mpango umeweka kipaumbele katika kuongeza ajira kwa vijana, kukuza sekta binafsi, kutumia rasilimali kwa njia endelevu na yenye tija, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuendeleza miundombinu msingi. Aidha, Mpango utahusisha kujenga ujuzi wa rasilimali watu, kuimarisha mifumo ya kinga ya jamii, kudumisha mshikamano wa kitaifa, kupanua upatikanaji wa huduma za mtandao, kukuza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kulinda mazingira, kuimarisha diplomasia ya uchumi na kuhakikisha ustawi na mafanikio yanayowanufaisha Watanzania wote kwa usawa.

(i) **Kuongeza Ajira kwa Vijana:** Kwa vile zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania ni vijana, Mpango umeweka kipaumbele katika kutekeleza sera na programu zinazoongeza fursa za kiuchumi, kuzalisha ajira, kupanua wigo wa kinga ya jamii na kujenga mustakabali bora kwa vijana. Vilevile, Mpango utaimarisha biashara ndogo na za kati ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa katika kuzalisha ajira, hususan kwa vijana.

(ii) **Kuimarisha Utulivu na Ukuaji wa Uchumi:** Kuchochea ukuaji wa uchumi ni jukumu kuu la Taifa. Katika kipindi hiki, sekta binafsi itaendelea kuwa nguzo muhimu ya ukuaji wa uchumi. Mpango utachukua hatua za kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na kutoa motisha kwa viwanda vya ndani ili kuzalisha kwa gharama nafuu na kusambaza bidhaa katika masoko ya ndani na kimataifa. Aidha, Mpango utaimarisha hatua za kifedha na zisizo za kifedha ili kuchochea uzalishaji na kuongeza ushindani wa bidhaa za ndani, sambamba na kudhibiti mfumuko wa bei ili kupunguza gharama za maisha.

(iii) **Kuimarisha Uwezo wa Kukusanya Mapato ya Ndani:** Mpango utapanua wigo wa kukusanya kodi, kurahisisha mifumo ya kodi na isiyo ya kodi, na kutumia teknolojia katika kusimamia kodi. Kadhalika, kuzingatia ushirikiano wa sekta binafsi na umma pamoja na vyanzo vya fedha bunifu kama vile hati fungani za kijani pamoja na kuimarisha uwezo wa taasisi na ulipaji wa kodi. Masoko ya mitaji yataimarishwa kupitia ukuzaji wa akiba, uwekezaji wa ndani na matumizi ya rasilimali za taifa, kama vile madini, ili kudhamini mikopo ya uwekezaji bila kuwa na ongezeko kubwa la deni la taifa. Jitihada hizi pia zitasaidia kuendeleza miundombinu, kuimarisha sera za biashara na mifumo ya uwekezaji inayowezesha kujenga na kukuza minyororo ya thamani yenye matokeo makubwa kiuchumi, na hivyo kuongeza rasilimali za ndani.

(iv) **Kuimarisha Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Kijamii:** Kuongeza ubora wa mafunzo ya ujuzi na elimu, ikiwemo stadi za sayansi, teknolojia, uhandisi na hesabu, kutengeneza mfumo wa soko la ajira wenye ushindani, sambamba na uimarishaji wa huduma za afya zinazohusisha tiba za kinga na matibabu ya magonjwa.

(v) **Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirisaji Kitaifa, Kikanda na Kimataifa:** Uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi utakaohakikisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi, hususan walioko katika maeneo yasiyounganishwa na usafiri wa bahari. Pia, kutengeneza mfumo wa usafirishaji uliofungamanishwa na bandari, viwanja vya ndege na reli na hivyo kuwezesha usafirishaji rahisi wa abiria na mizigo kwa ufanisi.

(vi) **Kuimarishwa kwa Umoja na Mshikamano wa Kitaifa:** Kuhamasisha umoja, mshikamano, ulinzi wa amani, na utulivu wa kisiasa. Maendeleo ya taifa lolote yanaakisi utamaduni na ustaarabu wake. Katika ulimwengu wa leo, utamaduni ni bidhaa na rasilimali ya kiuchumi; kwa hivyo, Kiswahili, lugha yetu ya taifa itapandishwa hadhi kuwa rasilimali ya utamaduni na kiuchumi.

(vii) **Kuimarisha Uwezo wa TEHAMA:** Katika utekelezaji wa Mpango, Serikali ikishirikiana na wadau wake, itahamasisha mifumo yote ya TEHAMA kusomana kwa ufanisi, ikiwemo mifumo mipya itakayoundwa. Aidha, Serikali itapanua matumizi ya teknolojia za kisasa, ikiwemo Akili Unde, ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma.

(viii) **Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi:** Suala la mazingira limeendelea kuwa kipaumbele cha maendeleo endelevu. Usimamizi wa biashara ya kaboni utaimarishwa ili kunufaisha wananchi.

(ix) **Kuimarisha Diplomasia ya Kiuchumi:** Jitihada zitazingatia kuongeza ushirikiano na fursa za kiuchumi kwa Taifa na Watanzania wote kwa kuzikizingatia heshima kwa pande zote na kuhakikisha manufaa kwa wote.

## 2.5 Muundo wa Mpango

Muundo wa Mpango IV unazingatia maono ya kimaendeleo ya Dira 2050 ambayo yanakusudia kuharakisha uchumi unakua kwa njia jumuishi na endelevu, sambamba na kujenga ustahimilivu na kukuza ushindani wa taifa kibiashara. Muundo huu unabainisha maeneo makuu matatu yanayohusiana: nguzo, vichocheo na misingi, ambayo kwa pamoja yanafafanua mwelekeo wa mkakati wa maendeleo ya Tanzania. Nguzo zinahusisha sekta zinazotarajiwa kutoa matokeo ya kimkakati na muhimu kwa mageuzi ya muundo wa uchumi na maendeleo ya rasilimali watu. Vichocheo ni sekta muhimu za mageuzi zinazochochea ukuaji, ubunifu na tija. Misingi inahusu masuala ya utawala, taasisi na miundombinu, yanayochochea maendeleo endelevu na kuhakikisha manufaa yake yanawafikia wananchi wote kwa usawa. Kwa pamoja, maeneo haya yanaunda mwongozo wa usanifu wa mipango ya maendeleo katika kipindi cha utekelezaji wa Dira 2050 na kama itavyofafanuliwa katika Sura zitazozofuata..

### 2.5.1 Nguzo

#### Nguzo ya Kwanza: Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

Tanzania inaweka kipaumbele katika kudumisha utulivu na uthabiti wa viashiria vikuu vya uchumi jumla. Vilevile, inazingatia uendelevu wa masuala ya kifedha, na kuimarisha ustahimilivu na kupanua wigo wa vyanzo vya biashara nje. Ajenda ya Taifa ya mageuzi ya muundo wa uchumi inaweka msisitizo katika maendeleo ya sekta za kimageuzi.

Kipaumbele kikuu ni  kuongeza uzalishaji na tija katika sekta hizo, kukuza ungezeko la thamani na kuanzisha minyororo mipya ya thamani kupitia sekta hizo. Haya yatakwenda sambamba na juhudi za kupanua na kuendeleza biashara ya huduma. Mkazo pia umewekwa katika kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuendeleza ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kurasimisha sekta za uchumi zisizo rasmi ili kudumisha ukuaji endelevu na ushindani wa kibiashara. Kwa kufanya hivi, Mpango unalenga kukuza uzalishaji na ufanisi wa uchumi, kuinua tija na kuimarisha usimamizi wa uchumi.

**Ukuaji wa Uchumi:** Tanzania inalenga kuharakisha ukuaji wa uchumi kupitia sekta mbalimbali kwa kuongeza tija ya uzalishaji, kupanua wigo wa mauzo nje na kuimarisha matumizi ya rasilimali zake katika kuzalisha bidhaa za viwandani. Uwekezaji wa kimkakati katika kuimarisha upatikanaji wa miundombinu ya kidijitali, nishati, usafirishaji na uchukuzi ni kichocheo muhimu cha kuongeza uzalishaji, tija  na kupanua shughuli za viwanda na huduma. Zaidi ya hayo, msukumo uliowekwa katika kupanua matumizi ya fursa za uchumi wa buluu na biashara ya kaboni ndani na nje ya nchi unadhihirisha jitihada za Tanzania za kujitokeza na kunufaika na fursa za kiuchumi zinazoibuka

**Kuongeza Tija:** Tanzania imeweka mkazo katika kuongeza tija ya uzalishaji katika sekta zote, hususan, kilimo, viwanda na huduma. Hii inatokana na kutambua kuwa tija ni msingi wa kuongeza mapato na ushindani wa uchumi. Lengo hili litafanikiwa kwa kuwa na ongezeko la matumizi ya teknolojia, zana na mitambo ya kisasa, uendelezaji ujuzi katika nyanja mbalimbali, na uimarishaji wa minyororo ya thamani. Mageuzi katika sekta za uzalishaji yataenda sambamba na maendeleo ya sekta za huduma na urasimishaji wa shughuli za uchumi zisizo rasmi, Hatua hizi zitasaidia kuongeza ufanisi na kukuza ushiriki wa jamii katika mfumo wa soko.

**Usimamizi wa Uchumi kwa Ajili ya Kuleta Mageuzi:** Usimamizi wa uchumi ulio thabiti ni msingi muhimu wa mageuzi ya muundo wa uchumi. Hii inawezesha uwiano na uthabiti wa sera, ubora wa taratibu na kanuni, pamoja na uwajibikaji wa taasisi. Kuimarisha mifumo ya utawala katika ngazi za taifa na serikali za mitaa kusaidia kujenga mazingira wezeshi ya biashara, kukuza sekta binafsi, kuvutia biashara na uwekezaji, na kuimarisha ushindani na ubunifu. Aidha, Mpango utapanua matumizi ya teknolojia za kidijitali na kuimarisha maamuzi yanayozingatia uchambuzi wa kina wa takwimu ili kuboresha ufuatiliaji wa maendeleo, kuimarisha kutoa huduma na kujenga utawala wa umma unaojibu changamoto za wananchi. Kwa ujumla, hatua hizi zinahakikisha ukuaji wa uchumi unakuwa endelevu na shirikishi na unajengwa juu ya ongezeko la tija na mifumo thabiti ya utawala inayopunguza vihatarishi na kuimarisha ustahimilivu.

### Nguzo ya Pili: Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu na Maendeleo ya Jamii

Katika Mpango huu, kitovu cha maendeleo ya taifa ni uwezo wa rasilimali watu. Hivyo, Mpango utaelekeza juhudi katika kuendeleza rasilimali watu kwa lengo la kujenga jamii iliyoelimika, yenye ujuzi na inayoweza kuhimili mabadiliko ya mahitaji ya jamii, uchumi na mazingira.  Kipaumbele cha nchi kimewekwa  katika kutumia fursa ya mgawanyo wa idadi ya watu kwa kuimarisha upatikanaji wa elimu bora na ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira. Aidha, Mpango unasisitiza kinga kwa jamii ili kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya, makazi, usalama wa chakula na lishe.

Vilevile, Mpango unalenga kuongeza upatikanaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira ili kuhakikisha maendeleo jumuishi.  Kadhalika, afua zinazojielekeza kuchochea  maendeleo jumuishi, kama vile maendeleo vijijini, mageuzi ya vyama vya ushirika na ongezeko la idadi ya watu wenye kipato cha kati, ni muhimu katika kuimarisha mshikamano wa jamii na ustawi uendelevu kwa wote.

**Nguzo ya Tatu: Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi**
Utunzaji wa mazingira na ujenzi wa ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni nguzo muhimu katika safari ya maendeleo ya Tanzania. Mtazamo wa kimkakati katika eneo hili unahusisha kuendeleza ukuaji wa miji iliyopangwa kwa ubora, na kuimarisha mipango endelevu ya matumizi ya bahari na ardhi. Kadhalika, kutekeleza mageuzi na kuimarisha uwezo wa mifumo na taasisi za usimamizi wa majanga na utoaji tahadhari za mapema ili kujenga uwezo wa kukabiliana na vihatarishi. Utekelezaji wa miradi ya kuhuisha ardhi na rasilimali za bahari, misitu na mabonde ya maji yaliyoathirika umezingatiwa. Vilevile, Mpango unasisitiza kuhusu kuimarisha afua za uchumi wa kijani kuelekea uzalishaji wa kiwango kidogo cha kaboni, kukuza ufanisi wa matumizi ya rasilimali na kubuni hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Mpango unazingatia kuchukua hatua za kulinda rasilimali asili na mifumo ya ikolojia, kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha matumizi ya mbinu endelevu katika shughuli za uzalishaji ili kudumisha utulivu wa uchumi na ustawi endelevu wa jamii.

### 2.5.2 Vichocheo vya Mageuzi
Mageuzi ya Muuundo wa Uchumi: Mageuzi ya muundo wa uchumi wa Tanzania yatachangiwa na vichocheo muhimu vya maendeleo ambavyo vitawezesha ukuaji jumuishi:

i. **Nishati:** Kuongeza upatikanaji wa nishati nafuu, ya kuaminika na endelevu ni jambo muhimu katika kuendesha viwanda na mageuzi ya kiuchumi;
ii. **Usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi:** Uwekezaji katika miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi utawezesha kufungamanishwa kwa uzalishaji ndani na minyororo ya thamani ya biashara ya kimataifa ili kuboresha ushindani katika biashara;
iii. **Sayansi, Teknolojia na Ubunifu:** Uhamasishaji wa utafiti, ubunifu na matumizi ya teknolojia mpya unakuza tija, kuongeza ufanisi na wigo wa shughuli za kisekta;
iv. **Mageuzi ya Kidijitali:** Uendelezaji wa miundombinu ya TEHAMA, huduma za umma za kidijitali na mifumo ya takwimu huimarisha misingi ya utawala bora, uwazi na maendeleo ya uchumi wa kisasa; na

v. **Mazingira ya Biashara na Uwekezaji:** Mpango utaweka mfumo wa udhibiti unaowezesha biashara na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuvutia uwekezaji na kuchochea ujasiriamali, hususan miongoni mwa vijana na wanawake.

### 2.5.3 Misingi ya Kufikia Matokeo
Ili kufanikiwa katika utekelezaji wa Mpango huu, Tanzania itaendelea kuimarisha misingi itakayowezesha mabadiliko endelevu ya kiuchumi na kijamii, hususan:

i. **Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu:** Taasisi imara, uongozi wa kidemokrasia, pamoja na utulivu wa nchi ni misingi muhimu inayohitajika katika kujenga imani ya wananchi, kuimarisha utawala wa sheria, na kuwezesha maendeleo endelevu;
ii. **Uthabiti wa Utawala katika Ngazi za Serikali za Mitaa:** Ugatuaji wa madaraka kwa wananchi, sambamba na kuimarisha uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa ni muhimu katika kutafsiri Mpango kwa usahihi, kusimamia utekelezaji wake kwa ufanisi, kuboresha utoaji wa huduma za umma na kukuza ushiriki wa wananchi;
iii. **Matumizi ya Teknolojia ya Kidijitali na Takwimu Sahihi:** Kutengeneza na kuimarisha matumizi ya mifumo inayotumia teknolojia za kidijitali, sambamba na kukuza uwezo wa taasisi kutumia takwimu kutasaidia kuandaa mikakati inayozingatia uhalisia, kuongeza uwajibikaji na kuboresha utendaji wa Serikali;

iv. **Mabadiliko ya Mtazamo, Fikra na Mageuzi katika Sekta ya Umma:** Ili kufikia mageuzi ya muundo wa uchumi na malengo ya maendeleo ya Taifa ni muhimu kuwa na mabadiliko ya kimtazamo na fikra, kukuza ubunifu, nidhamu, uwajibikaji pamoja na kujenga mwelekeo mpya wa jamii na watumishi wa umma kuhusu utoaji wa huduma.

Mpango huu jumuishi unaielekeza Tanzania katika njia yenye matarajio makubwa ya kuwa Taifa lenye ustawi, uhimilivu na jumuishi ifikapo mwaka 2050. Msisitizo wa kimkakati umewekwa katika kufanya mageuzi ya kiuchumi, kukuza uwezo wa rasilimali watu, pamoja na kusimamia mazingira endelevu na utawala bora. Aidha, Tanzania inalenga kutumia kikamilifu fursa ya ongezeko la watu wenye umri wa kufanya kazi, rasilimali asilia, nafasi ya kimkakati kijiografia, pamoja na kutumia fursa zinazotoka na teknolojia mpya ili kuchochea ukuaji wa uchumi shirikishi na endelevu.

## 2.6 Falsafa ya Maendeleo

Mpango IV umejikita katika maono ya *Dira 2050* na Mpango Elekezi 2050 na unazingatia falsafa ya maendeleo inayomtanguliza mwananchi kama kipaumbele kikuu cha maendeleo. Lengo ni kujenga taifa lenye ustawi, jumuishi, lenye haki na linalojitegemea. Aidha, unalenga kujenga uchumi shindani na jamii inayotoa fursa sawa kwa wote. Kwa muktadha huo, Mpango unawianisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Pia unalenga kuimarisha usawa wa kijamii na kulinda mazingira kwa njia endelevu. Hatua hizi zinaongozwa na misingi ya utawala bora, uwajibikaji na ubunifu. Aidha, Mpango unaweka msisitizo wa kimkakati katika kuongeza thamani kwenye bidhaa na huduma zinazozalishwa na kuimarisha mifumo ya taasisi. Aidha, Mpango unalenga kuboresha kutoa huduma za umma kwa ustawi wa jamii, kuendeleza mageuzi ya kidijitali, kukuza uchumi wa kijani na kuimarisha sekta binafsi ili iwe imara na shindani. Kwa kuunganisha vipaumbele hivi, Mpango unaweka msingi wa uchumi kukua kwa njia jumuishi, endelevu na himilivu. Hatua hizi pia zinalenga kukuza ustawi wa pamoja kwa wananchi wote. Hivyo, Mpango unatoa mwelekeo thabiti wa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuhakikisha malengo ya maendeleo ya muda wa kati yanafikiwa.

## 2.7 Nadharia ya Mageuzi na Uasilishaji wa Kimkakati

Nadharia ya Mageuzi ya Mpango Elekezi 2050, kama ilivyoainishwa katika Kielelezo 2.1, inafafanua mwongozo wa kimkakati wa utekelezaji wa mageuzi ya uchumi kwa kipindi cha miaka 25 ijayo. Madhumuni ya mageuzi hayo ni kuiwezesha Tanzania kuwa Taifa lenye ustawi, jumuishi, haki, linalojitegemea na lenye uchumi wa hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu. Aidha, yataiwezesha Tanzania kuwa na uwezo wa kushindana katika biashara za kimataifa na kufikia pato la Taifa la dola za Marekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050. Nadharia hii inaonesha kuwa Tanzania inaweza kufikia malengo hayo iwapo itaelekeza juhudi zake katika kushughulikia kikamilifu changamoto kuu za maendeleo. Changamoto hizi ni tija ndogo, ukuaji hafifu wa viwanda, minyororo dhaifu ya thamani, vikwazo vya miundombinu, shinikizo la uharibifu wa mazingira, sehemu kubwa ya uchumi kuwa katika sekta isiyo rasmi na upungufu wa nguvukazi watu yenye ujuzi. Ili kuondokana na hali ya uchumi wenye tija ndogo na kufikia uchumi wenye vyanzo mseto vya ukuaji, ustahimilivu na ubunifu wa hali ya juu, ni muhimu kubainisha kwa ufasaha hatua na vipaumbele vya utekelezaji vitakavyochochea mageuzi hayo.

Nadharia hii imejengwa katika utatu wa Uwekezaji, Uasilishaji na Ubunifu (3U). Uwekezaji unahusisha upanuzi wa miundombinu, maendeleo ya Uchumi wa viwanda, na kuimarisha nguvukazi yenye ujuzi. Uasilishaji unahusu kupokea na kutumia teknolojia, maarifa na ujuzi na mitaji ya ndani na nje katika mfumo wa uzalishaji wa ndani ili kujenga minyororo mipya ya thamani, kuongeza tija na ushindani katika masoko. Ubunifu unalenga kuharakisha ukuzaji wa teknolojia, uongezaji thamani na uzalishaji wa maarifa mapya ndani ya nchi. Haya yanaimarishwa na mapitio na maboresho ya misingi na kanuni za

utawala bora, ufanisi wa huduma za umma, uboreshaji wa utendaji wa utumishi wa umma, ukuaji wa sekta binafsi, usimamizi endelevu wa mazingira, pamoja na mabadiliko ya kidijitali na uchumi wa kijani. Kwa muda mrefu, mabadiliko haya yanatarajiwa kuongeza uwezo wa uzalishaji, kuzalisha ajira, kuongeza mauzo ya nje yaliyoongezwa thamani, kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kuboresha maisha, usawa na ustahimilivu wa kijamii.

**Mwelekeo wa Mageuzi ya Mpango IV:** Kwa kuzingatia Mpango Elekezi 2050, na Nadharia ya Mageuzi ya kufikia mabadiliko endelevu, Mpango IV unaainisha na kutekeleza mageuzi katika kipindi cha miaka mitano ya mwanzo ili kujenga msingi wa mageuzi ya muda mrefu nchini. Wakati Mpango Elekezi 2050 unalenga mageuzi makubwa ya muundo wa uchumi, Mpango IV unaweka mkazo katika mageuzi msingi na anzilishi na afua za kichocheo zitakazoondoa vikwazo vya sasa na kuweka mazingira yatakayowezesha uchumi kukua kwa kasi inayohitajika. Hivyo, katika kipindi cha Mpango IV, 2026/27–2030/31, mkazo umewekwa katika maeneo yafuatayo:

i. **Vipaumbele vya Kwanza kwa utekelezaji wa Mpango wa Nne**

Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni hatua ya kwanza ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Mafanikio yake yatategemea kushughulikia, tangu mwanzo, vikwazo vya msingi vinavyopunguza ufanisi wa uchumi na uwezo wake wa kuvutia, kupokea na kutumia uwekezaji kwa tija. Uzoefu wa kimataifa pamoja na tathmini za ndani zinaonesha kuwa mabadiliko ya kiuchumi hayategemei tu wingi wa rasilimali, bali kwa kiwango kikubwa yanategemea ubora wa mifumo ya utawala, uwezo na utendaji wa taasisi za umma, pamoja na upatikanaji wa miundombinu wezeshi iliyo imara na ya kuaminika.

Katika muktadha huu, changamoto kuu zilizobainishwa chini ya Mpango IV zimeunganishwa moja kwa moja na afua husika na kupangwa kwa mfuatano wa kimkakati unaoakisi hitaji la kushughulikia kwanza vikwazo vinavyozuia maendeleo kwa kiwango kikubwa zaidi. Mfuatano huu unaongozwa na kanuni ya kuanza na yale yanayofungua mengine. Hivyo basi, unaweka kipaumbele katika mageuzi ya utawala, udhibiti, utendaji wa sekta ya umma na utoaji wa huduma, kwani haya ndiyo yanayoweka msingi wa uwekezaji, ongezeko la tija na mabadiliko mapana ya kijamii na kiuchumi. Baada ya kuimarisha misingi hii, msisitizo mkubwa utawekwa katika kupanua uwekezaji, kuboresha miundombinu, kuongeza tija katika sekta za uzalishaji, kukuza urasimishaji na ujumuishaji, pamoja na kuimarisha rasilimali watu na ushirikiano kwa maendeleo.

Hivyo basi, Mpango IV utaweka kipaumbele katika hatua zifuatazo za kimkakati ili kuweka msingi imara wa utekelezaji wa Dira 2050, huku ukijenga mazingira wezeshi ya biashara, kuimarisha ushindani wa uchumi, na kusaidia ukuaji jumuishi na endelevu:

(a) Kuimarisha utawala, udhibiti na mageuzi ya mazingira ya biashara kwa kufanya mapitio na maboresho ya mifumo ya kisheria, udhibiti na utoaji maamuzi ili kuongeza uwazi, uhakika na ufanisi;
(b) Kuendeleza mageuzi ya utumishi wa umma na utoaji wa huduma kwa kubadili mitazamo na mifumo ya utendaji ili kuongeza kasi, ubora na uwajibikaji wa huduma kwa wananchi na wawekezaji;
(c) Kuimarisha utendaji wa taasisi na mashirika ya umma ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na matokeo katika sekta ya umma;
(d) Kuboresha miundombinu wezeshi ya uchumi kupitia ongezeko la uwekezaji na ufanisi katika nishati, usafirishaji, uchukuzi, pamoja na mifumo ya kidijitali;

(e) Kuimarisha utayari wa uchumi kupokea uwekezaji kwa kuimarisha uratibu wa taasisi, mifumo ya uwekezaji na uwezo wa kutekeleza miradi ya kimkakati;
(f) Kupanua ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na utoaji wa huduma za maendeleo;
(g) Kukuza ufanisi na tija katika sekta za uzalishaji kwa kuimarisha kilimo, viwanda, madini na utalii ili kuongeza thamani, ajira na ushindani;
(h) Kukuza urasimishaji na ujumuishaji wa shughuli za kiuchumi kwa kuweka mazingira rafiki zaidi kwa biashara ndogo, ndogo na za kati kushiriki kikamilifu katika uchumi rasmi; na
(i) Kukuza ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira kupitia mageuzi ya mifumo ya elimu na mafunzo ili kujenga rasilimali watu yenye ujuzi unaohitajika na uchumi unaobadilika.

ii. **Matokeo Msingi Yanayotarajiwa:** Vikwazo vikuu vya kufikia matokeo vinajumuisha: mapungufu katika mifumo ya udhibiti na urekebu, utoaji wa huduma za serikali kwa umma, vikwazo vya miundombinu hususan, nishati, usafirishaji, uchukuzi na mifumo ya kidijitali. Vilevile, kiwango cha chini cha urasimishaji, kutokuwa na uwiano kati ya ujuzi na mahitaji ya soko, utendaji dhaifu wa sekta za uzalishaji na utayari duni wa kushughulikia uwekezaji.

*Kielelezo 2.1: Mpango Elekezi 2050- Dhana ya Mabadiliko*



## 2.8 Malengo Mkakati ya Mpango

Mpango unalenga kuweka msingi wa mifumo ya taasisi, miundombinu na rasilimali watu itakayoiwezesha Tanzania kuondokana na uchumi wenye tija ndogo na kufikia mageuzi ya muundo wa uchumi endelevu. Mpango umeelekeza juhudi katika kuboresha mazingira ya biashara, kuongeza upatikanaji wa nishati ya uhakika na kuimarisha mifumo ya usafirishaji na uchukuzi, kukuza ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali pamoja na kukuza ujuzi wa watumishi wa umma , maadili na uwajibikaji. Lengo ni kuiwezesha Tanzania kusonga mbele kwa uthabiti na kufikia malengo yake ya ustawi wa pamoja na pato la Taifa la dola za Marekani bilioni 118.052, ukuaji halisi wa pato la Taifa wa asilimia 10.5 na wastani wa kipato cha mtu cha dola za Marekani 1,638 ifikapo mwaka 2031. Kwa kuzingatia hayo, Mpango umeainisha malengo manne mahsus:

**Lengo 1:** Kuimarisha uthabiti wa uchumi jumla na kuendeleza mageuzi ya kimuundo, yakiwemo mapitio na maboresho ya sera na mifumo, ili kuchochea ukuaji shirikishi unaoongozwa na sekta binafsi.

**Lengo 2:** Kuboresha mifumo ya usafirishaji, miundombinu na mifumo wezeshi ya biashara itakayoiwezesha Tanzania kuwa kitovu shindani cha usafirishaji, uchukuzi na biashara.

**Lengo 3:** Kujenga uwezo wa rasilimali watu; kuboresha upatikanaji wa huduma na ulinzi wa jamii; kuimarisha mazingira uendelevu na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, kuimarisha utawala bora na wa kisheria ili kuwezesha upatikanaji wa ajira jumuishi na ustawi endelevu.

**Lengo 4:** Kuharakisha mageuzi katika sekta za uzalishaji kwa lengo la kuzalisha ajira za staha, kuongeza uzalishaji wa bidhaa zenye thamani na kuimarisha ushindani wa biashara ya nje.

## 2.9 Uainishaji wa Vipaumbele

Mpango umezingatia Kielelezo 2.2 cha Mpango Elekezi 2050, ambacho kinasisitiza mpangilio unaozingati kanuni ya "Anza Kutekeleza Yanayowezesha Mengine." Kwa muktadha huo, Mpango unaweka mkazo katika upangaji wa kimkakati unaotanguliza afua zinazojenga msingi wa mageuzi na sekta zenye uwezo wa kuleta mabadiliko mapana na endelevu na kuharakisha safari ya Tanzania ya kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu. Hivyo, katika miaka mitano ya kwanza, Mpango umeweka kipaumbele katika afua za kimageuzi, hususan mapitio na maboresho ya mifumo ya utawala, udhibiti na urekebu; uimarishaji wa miundombinu ya nishati, usafirishaji na uchukuzi; maendeleo ya nguvukazi yenye ujuzi ; pamoja na masuala mengine ya kijamii yanayoboresha maisha.

Vilevile, Mpango umeweka mkazo katika kuendeleza maendeleo ya miundombinu fungamanishi ya barabara, reli, bandari na mitandao ya kidijitali. Muunganiko wa miundombinu hii utaiwezesha Tanzania kufikia masoko ya kikanda, na kukuza ustawi wa jamii, mambo ambayo ni muhimu katika kuimarisha ukuaji wa uchumi, kurahisisha biashara na kuhakikisha upatikanaji wa huduma jumuishi.

Kwa kuzingatia mwelekeo huo, Mpango unatafsiri maono ya Dira 2050 kwa kutumia mwongozo wa kimkakati wa awamu wenye hatua mahsusi na zinazotekelezeka. Mwongozo huu umejengwa katika maeneo manne ya maendeleo ya muda wa kati: mageuzi ya mifumo ya utawala na taasisi; miundombinu ya nishati, usafirishaji na miundombinu ya kidijitali; mageuzi ya viwanda na kuongeza tija; pamoja na maendeleo ya rasilimali watu na ustawi wa jamii. Mpangilio huu wa maeneo ya kipaumbele unazingatia umuhimu wa kujenga msingi utakaowezesha mageuzi endelevu ya muundo wa uchumi wa Tanzania. Kila eneo limewekewa kipaumbele kwa kuzingatia nafasi yake katika kufungua hatua zinazofuata za maendeleo. Kielelezo Namba 2.2 kinaonesha maeneo yaliyopewa kipaumbele kama ifuatavyo:

i. **Mageuzi ya Mfumo wa Utawala, Udhibiti na Urekebu**
Kuimarisha mfumo wa sheria, uwajibikaji wa taasisi na mifumo ya udhibiti na urekebu kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara, kuongeza imani kwa wawekezaji na kukuza ushindani wa sekta binafsi. Mkazo zaidi utawekwa katika maeneo manne yafuatayo:

- ✓ **Mageuzi:** Kufanya mapitio na maboresho ya sera na sheria, kulinda haki miliki, kuimarisha uwajibikaji na kuweka mazingira thabiti kwa ukuaji wa sekta binafsi, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ili kufikia maendeleo endelevu.
- ✓ **Utoaji wa huduma za Jamii:** Kuweka kipaumbele katika mageuzi yatakayoongeza ufanisi na tija katika taasisi za umma, kuhakikisha utekelezaji wa sera, kusaidia ustawi wa jamii, kuendeleza ukuaji wa miji unaopangwa kwa ufanisi, na kuweka mazingira wezeshi ya biashara ikiwemo biashara ndogondogo, za kati na sekta binafsi kwa ujumla.
- ✓ **Ugatuaji wa Madaraka:** Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafanya kazi kwa uhuru, ufanisi na tija katika kutoa huduma katika maeneo yao.
- ✓ **Mabadiliko ya Mtazamo, Fikra na Tabia:** Kuharakisha mageuzi ya mifumo ya taasisi na mitazamo katika utendaji kwa lengo la kukuza uwajibikaji, ubunifu na fikra za kijasiriamali, kuboresha mazingira ya biashara na kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa hatua za Mpango.

ii. **Miundombinu ya Nishati, Usafirishaji na Uchukuzi**
Kuweka mkazo katika kuendeleza uwekezaji kwenye miundombinu ya nishati, usafirishaji na uchukuzi kwa lengo la kuunganisha masoko ya ndani na kikanda. Msisitizo umewekwa pia katika kuboresha mifumo na taasisi za udhibiti na urekebu ili kutekelezaji miradi kwa ufanisi, kuboresha utoaji wa huduma na kuvutia ushiriki wa sekta binafsi ndani na nje ya nchi.

iii. **Ujuzi na Maendeleo ya Rasilimali Watu**
Kuweka mkazo katika mageuzi ya mfumo wa elimu na maendeleo ya ujuzi ili kuziba pengo la upungufu wa nguvukazi watu yenye ujuzi; kukuza matumizi ya teknolojia, kuchochea ubunifu na kuongeza tija. Kadhalika, kuimarisha nguvukazi ya ndani ili kuvutia zaidi kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

iv. **Uchumi wa Viwanda na Sekta za Uzalishaji**
Kuharakisha mageuzi na uwekezaji unaolenga uchumi wa viwanda, kilimo na sekta nyingine za uzalishaji. Lengo ni kuboresha muundo wa uzalishaji, kuimarisha minyororo ya thamani ya ndani, kuiunganisha Tanzania na masoko ya kikanda na kimataifa na kuongeza ushindani wa kibiashara. Hatua Hizi zitaambatana na kuimarisha mifumo ya uwezeshaji biashara mbalimbali ikiwemo, biashara changa na ubunifu. Aidha jitihada zitaelekezwa katika kukuza ujasiriamali, kuanzisha programu za kulea na kukuza biashara pamoja na teknolojia zenye uwezo mkubwa. Vilevile, kuchochea upatikanaji wa mitaji, ushauri elekezi wa kitaalamu na kufanya mageuzi ya mifumo ya kuendeleza ubunifu ili kuzalisha biashara mpya na ukuaji wa uchumi mseto. Hatua za kipaumbele za kisekta zimebainishwa katika Sura ya Tatu; na programu mahsusi za kielelezo zimefafanuliwa katika Sura ya Nne. Kadhalika, Utekelezaji wa hatua hizi utawezeshwa kupitia mifumo ya ugharamiaji na mipangilio ya ushirikishwaji iliyoainishwa katika Sura ya Tano.




*Kielelezo 2.2: Vipaumbele na hatua za Utekelezaji wa Mpango Elekezi 2050*

## 2.10 Maadili na Kanuni Msingi

Kufikiwa kwa malengo ya maendeleo ya Tanzania kunategemea kwa kiasi kikubwa uwepo wa maadili yanayolitambulisha Taifa, yanayojenga imani ya wananchi na yanayoweka dira ya mageuzi endelevu. Maadili ya msingi yanaakisi misingi ya mwenendo, mitazamo na tabia zinazopaswa kuongoza jamii na taasisi kuelekea kujenga jamii inayozingatia uadilifu, uwajibikaji, ujumuishi na ubunifu. Kanuni elekezi kama zilizoainishwa katika Dira 2050, zinaweka misingi ya demokrasia, utu, ujenzi wa amani na umoja, utunzaji wa utamaduni na usimamizi endelevu wa rasilimali asilia. Kwa misingi hiyo, maendeleolazima kuwaweka wananchi kuwa shabaha kuu, yakizingatia haki na usawa, na kujielekeza katika kutimiza maono ya Tanzania.. Maadili na kanuni hizo msingi ni:

(i) **Utu:** Kutambua thamani ya asili ya kila mtu na kuzingatia heshima, usawa na haki ya kijamii katika nyanja zote za maisha.
(ii) **Amani na Umoja:** Kukuza mshikamano wa Taifa, maelewano na utulivu wa kijamii, pamoja na kuhamasisha majadiliano ya kujenga miongoni mwa jamii.
(iii) **Utamaduni na Maadili ya Taifa:** Kuthamini na kuendeleza urithi wa utamaduni wa Tanzania, mila na desturi za pamoja, na utambulisho wa Taifa kama msingi wa fahari na mshikamano wetu.
(iv) **Uwezo wa Kubadilika, Ujifunzaji Endelevu na Ushindani:** kujenga uwezo wa kuendana na mabadiliko, kuhimiza ujifunzaji endelevu, kukuza ujuzi na kukuza ari ya kufanya vizuri na kuendeleza ushindani kimataifa. Aidha, ni muhimu kuhakikisha kuwa sera zinakuwa madhubuti, maamuzi yanayoongozwa na ushahidi, matokeo yanayopimika na utekelezaji unazingatia uwajibikaji.
(v) **Ujumuishi, Usawa na Tofauti:** Kuthamini utofauti, kukuza fursa sawa, na kuhakikisha kuwa wananchi wote, bila kujali asili yao, wanashiriki kikamilifu katika ujenzi wa jamii, uchumi na siasa.
(vi) **Uadilifu katika Usimamizi wa Utajiri na Rasilimali Asilia za Taifa:** Kutambua kuwa utajiri na rasilimali asilia ni amana ya Taifa. Hivyo, kusimamia kwa mamlaka na uwajibikaji ili kuhakikisha kuwa utajiri na rasilimali asilia hizi zinatumika kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.
(vii) **Wajibu wa Kufanya Kazi:** Ni wajibu kwa kila mtu mwenye uwezo, kufanya kazi. Hivyo, hakuna mtu anayestahili kuishi kwa kutegemea jasho la mwingine. Kwa muktadha huo, Mpango unahimiza wajibu wa kila mtu kufanya kazi kwa bidii.

## 2.11 Matokeo Tarajiwa

Jedwali Namba 2.1 linaonesha matokeo makuu ya kimaendeleo yaliyopewa kipaumbele na Mpango huu. Hii imezingatia shabaha kuu za Dira 2050 zinazotumika kama viashiria vya kupima maendeleo ya Tanzania kuelekea kuwa Taifa lenye ustawi, jumuishi, haki, linalojitegemea na lenye uchumi wa hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu. Matokeo haya yanaakisi maeneo ya kimkakati yanayozingatiwa katika kipindi cha awamu ya kwanza cha utekelezaji wa Dira 2050. Maeneo hayo ni pamoja na ukuaji wa uchumi endelevu na imara, kupungua kwa umaskini na uwezekano wa kurejea tena katika umaskini, kuimarisha uwezo wa rasilimali watu, na kuboresha ustawi wa jamii. Aidha, Mpango unatoa kipaumbele katika kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa usawa na huduma bora za afya, kupanua wigo wa kinga ya jamii, kuongeza upatikanaji wa huduma za maji safi na salama pamoja na nishati. Vilevile, kuhakikisha usafi wa mazingira kwa wote na kuendeleza wa usawa wa kijinsia. Malengo na shabaha hizi kwa pamoja, zinatoa mwelekeo wa kimkakati wa kuhakikisha kuwa afua za Mpango zinaendana na ajenda ya muda mrefu ya mageuzi iliyoainishwa katika Dira 2050.

*Jedwali 2.1: Shabaha Kuu za Dira 2050 kwa Mpango IV*

| Shabaha Kuu za Dira 2050 | Kiashiria | Kiwango Halisi | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|
| **Uchumi Imara na Thabiti** | | | |
| Nchi iliyoendelea kwa viwanda, inayotegemea maarifa, yenye kipato cha kati ngazi ya juu, uchumi wa dola za Marekani trilioni 1 na wastani wa kipato cha mtu mmoja angalau dola 7,000. | Pato la Taifa kwa bei za sasa (Bilioni $) | 81.537 (2024) | 118.052 |
| | Pato la Taifa kwa mtu mmoja ($) | 1,343.91 (2024) | 1,638 |
| | Ukuaji Halisi wa pato la Taifa – Bei za Soko (%) | 5.5 (2024) | 10.5 |
| Kupungua kwa umaskini uliokithiri kwa kuzingatia wanawake na watu wenye ulemavu | Kiwango cha umaskini uliokithiri Kitaifa (%) | 8 (2017/18) | 5 |
| | Kiwango cha Umaskini wa Kawaida Kitaifa (%) | 26.4 (2017/18) | 22 |
| | Kiashiria cha usawa wa kipato | 0.38 | 0.34 |
| Tanzania kuwa kitovu cha chakula barani Afrika na miongoni mwa nchi 10 duniani | Kiwango cha Kujitosheleza kwa Chakula (%) | 128 | 130 |
| | Nafasi miongoni mwa nchi za Afrika kwa Utoshelevu wa Chakula | 5 | 3 |
| **Maisha Bora na Ustawi kwa Wote** | | | |
| Kutokomeza vifo vya akina mama, watoto wachanga na watoto wenye umri chini ya miaka mitano | Idadi ya vifo vya watoto wachanga (kwa kila vizazi hai 1,000) | 33 (2022) | 27 |
| | Idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano (kwa kila vizazi hai 1,000) | 43 (2022) | 34 |
| | Idadi ya vifo vya akina mama (kwa kila vizazi hai 100,000) | 104 (2022) | 85 |
| Watanzania wenye afya, furaha kwa wastani wa kuishi miaka 75 | Wastani wa kuishi tangu kuzaliwa (miaka) | 68.3 (2025) | 70.4 |
| Mfumo bora na jumuishi wa elimu na mafunzo katika ngazi zote | Kiwango cha nguvukazi watu inayoweza kufanyakazi (%) | 73.2 (2024) | 74.6 |
| | Kiwango cha ajira kwa idadi ya watu (%) | 68.7 (2024) | 71.3 |
| | Kiwango cha ukosefu wa ajira kwa wenye umri wa zaidi ya miaka 15 (%) | 6.2 (2024) | 4.4 |

| Shabaha Kuu za Dira 2050 | Kiashiria | Kiwango Halisi | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|
| Watoto wote wa kike na wa kiume wanapata fursa sawa ya elimu bora ya awali na kabla ya elimumsingi kama msingi endelevu wa ujifunzaji na ustawi wa jamii | Kiwango cha Udahili (%) | 89.5 (2024) | 100.0 |
| | Kiwango halisi cha watoto wa miaka 5 waliodahiliwa kwa Elimu ya Awali(%) | 51.2 (2024) | 100.0 |
| | Uwiano wa wanafunzi kwa walimu wenye ujuzi | 105:1 (2024) | 40:1 |
| Watanzania wote wana fursa ya kupata elimumsingi bora na kati yao angalau asilimia 25 wanafikia ngazi ya elimu ya juu na ujuzi unakidhi mahitaji | Kiwango cha Jumla cha Udahili kwa Elimu ya Msingi (%) | 98.2 (2023) | 100.0 |
| | Kiwango cha Jumla cha Uandikishaji kwa ngazi ya Elimu ya Sekondari (%) | 51.7 (2024) | 79.1 |
| | Kiwango cha Wanaomaliza Elimumsingi na Kudahiliwa ngazi ya Elimu ya Juu (%) | 5.8 (2023/24) | 7.0 |
| Watoto wote wakike na wakiume wanapata malezi na makuzi bora na kati yao angalau asilimia 90 wanafikia ukomavu stahiki umri wa miaka mitano | Kiwango cha Udumavu kwa watoto wenye umri wa miezi 0–59 (%) | 30.0 | 22.6 |
| | Kiwango cha Upungufu wa uzito kwa watoto wenye umri wa miezi 0–59 (%) | 3.0 | 2.0 |
| | Kiwango cha watoto wanaozaliwa Wakiwa na uzito mpungufu (%) | 2.9 | 2.0 |
| **Upatikanaji wa Huduma za Hifadhi ya Jamii** | | | |
| Upatikanaji wa Huduma za afya kwa wote | Kiwango cha Upatikanaji wa bima za afya (%) | 67.8 (2023/24) | 100 |
| Uhakika wa upatikanaji wa ulinzi wa jamii kwa wote | Ongezeko la Upatikanaji wa Huduma za Kinga ya jamii (%) | 28.4 (2023/24) | 42.60 |
| | Upatinaji wa bima ya afya (%) | 67.8 (2023/24) | 100 |
| | Upatikanaji wa Huduma za hifadhi ya jamii (%) | 10.1 (2023/24) | 18.1 |
| Upatikanaji wa maji safi na salama na usafi wa mazingira, nishati safi na nafuu ya kupikia, na makazi bora kwa wote | Kaya za vijijini zenye vyoo bora (%) | 72.0 | 100.0 |
| | Upatikanaji wa Huduma ya maji safi vijijini (%) | 79.6 | 87.9 |
| | Upatikanaji wa Huduma ya maji safi mijini (%) | 90.0 | 97.2 |
| Angalau asilimia 50 ya Watanzania wana ajira zenye staha katika sekta rasmi | Kiasi cha ajira za sekta isiyo rasmi katika jumla ya ajira (%) | 94.2 (2024) | 81.0 |
| Kiwango cha Matumizi ya umeme cha wastani wa angalau 3,000kWh kwa mtu | Uwezo uliopo wa kuzalisha umeme (MW) | 4504.5 (2025) | 8,000 |
| | Kiwango cha wastani wa matumizi ya umeme kwa mtu (kWh) | 170 (2025) | 600 |
| Tanzania inaongoza Barani Afrika na ni miongoni mwa nchi 10 duniani zilizopunguza pengo la tofauti kijinsia kwa angalau asilimia 85 | Fahirisi ya Pengo la Kijinsia Duniani | 0.734 (2024) | 0.77 |
| | Nafasi kimataifa katika Fahirisi ya Kupunguza Pengo la Kijinsia . | 55 (2024) | 40 |
| **Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi** | | | |
| Kuimarika kwa vigezo vya uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi, na Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 10 bora Afrika | Nafasi ya Tanzania kwa nchi za Afrika katika fahirisi ya uhifadhi wa Mazingira (1 ni bora zaidi) | 19 (2022) | 15 |
| | Nafasi ya Tanzania Barani Afrika katika Fahirisi ya Uwezo wa Kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi (1 ndiyo bora zaidi) | 18 (2022) | 15 |
| | Kiwango cha mchango katika Pato la Taifa kinachotokana na matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari | 4.3 (2023/24) | 7.53 |

| Shabaha Kuu za Dira 2050 | Kiashiria | Kiwango Halisi | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|---|
| **Jamii yenye Uwezo wa Kidijitali** | | | |
| Angalau asilimia 70 ya wananchi wana ujuzi unaowawezesha kushiriki kikamilifu kidijitali katika shughuli za kiuchumi na kijamii | Kiasi cha watu wanaoweza kutumia mtandao wa intaneti yenye kasi (%) | 40 (2025) | >70 |
| | Kiwango cha ujuzi wa kidijitali kitaifa (%) | 30 (2024) | >60 |
| | Kiwango cha upatikanaji wa Mtandao (%) | 79.3 (2025) | 98 |
| | Kiasi cha jamii za vijijini zinazotumia mtandao (%) | <25 (2024) | > 65 |
| Zaidi ya asilimia 80 ya huduma za Serikali zinapatikana kupitia majukwaa salama, jumuishi na rahisi kutumia ya kidijitali | Kiasi cha huduma kuu za Serikali zinazopatikana mtandaoni (%) | 45 (2025) | 95 |
| | Kiasi cha idadi ya watu wenye kitambulisho cha kidijitali kinachofanya kazi kilichounganishwa na huduma za umma mtandaoni, katika maeneo ya vijijini (%) | 25 (2025) | 75 |
| | Kiasi cha idadi ya watu wenye kitambulisho cha kidijitali kinachofanya kazi kilichounganishwa na huduma za umma mtandaoni, katika maeneo ya mijini (%)i | 40 (2025) | 90 |
| | Kiasi cha idadi ya taasisi za kisekta zinazotumia mifumo ya data inayosomana (%) | 20 (2025) | 90 |
| | Kiasi cha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zenye mifumo ya TEHAMA inayowasiliana na kusomana (%) | 20 (2024) | 40 |

Sura ya Kwanza na ya Pili zimeweka msingi wa Mpango kwa kuelezea historia ya mabadiliko ya Tanzania kutoka Dira ya Maendeleo 2025 kwenda Dira 2050. Sura hizi pia zimeainisha maboresho kwenye mfumo wa upangaji na utekelezaji wa mipango, pamoja na mchakato shirikishi unaozingatia ushahidi wa kitakwimu uliotumika kuandaa Mpango huu.

Aidha, zimeainisha masuala muhimu ya maendeleo ya Taifa, falsafa ya Maendeleo ya Taifa na Nadharia ya Mabadiliko. Kadhalika, zimefafanua msingi wa uwekaji vipaumbele na mpangilio wa hatua kwa mfuatano utakaoongoza mageuzi, yakiwemo mapitio, maboresho na uwekezaji wa muda wa kati. Kwa ujumla, sura hizi zinauweka Mpango huu kama hatua ya mwanzo ya utekelezaji wa ajenda ya muda mrefu ya mageuzi ya Taifa. Ajenda hii imejikita katika kuimarisha mifumo ya utawala, kuboresha mifumo ya usafirishaji na uchukuzi wa mizigo, kukuza uwezo wa rasilimali watu, kuongeza tija, na kuharakisha maendeleo ya viwanda.

Kwa mwelekeo huu, Sura ya Tatu inajikita katika kubainisha mambo yanayopaswa kubadilika kwenda katika kueleza namna mabadiliko hayo yatakavyotekelezwa. Sura hii inaainisha njia za kimkakati ambazo Tanzania itazitumia kuimarisha utendaji wa taasisi, kuendesha mageuzi ya kiuchumi, kuchochea ukuaji na ubunifu wa sekta binafsi, kupanua uwezo wa uzalishaji na kuimarisha ustahimilivu wa mazingira.

Kwa hivyo, Sura ya Tatu inaweka bayana vipaumbele vya Mpango, hatua za kichocheo na mwelekeo wa utekelezaji utakaoiwezesha Tanzania kusonga mbele kwa kasi ikiyatafsiri maono kwa vitendo.

# MUHTASARI – SURA YA PILI

MPANGO IV · SURA YA 2

## Masuala Yaliyozingatiwa

### & Uhusiano na Dira 2050

Kubainisha changamoto za kimuundo ambazo Tanzania inapaswa kuzishinda — na mfumo wa nguzo, vichocheo, malengo na mielekeo ya kimkakati unaogeuza azma kuwa ajenda madhubuti ya mageuzi.

**3** NGUZO MSINGI

**5** VICHOCHEO VIKUU

**4** MALENGO MKAKATI

**9** MIELEKEO YA KIMKAKATI

MPANGO IV · Sura ya 2 — *Masuala Yaliyozingatiwa & Uhusiano na Dira 2050*

MASUALA MUHIMU YA MAENDELEO

## Changamoto Kuu Mbili za Maendeleo

Tanzania inakabiliwa na changamoto pacha zinazohusiana — mageuzi ya uchumi hayawezi kufanikiwa bila uwekezaji sambamba katika rasilimali watu na ustahimilivu wa mazingira.

CHANGAMOTO 01

### Mageuzi ya Kimuundo ya Uchumi

Yanayochochewa na ujenzi wa viwanda, tija, maendeleo ya sekta binafsi na uimarishaji wa miundombinu. Tanzania lazima isasishe uzalishaji na kuwa kitovu cha viwanda, usafirishaji na biashara.

Viwanda · Tija · Usafirishaji

CHANGAMOTO 02

### Rasilimali Watu, Ujumuishi na Mazingira

Mageuzi ya uchumi lazima yaambatane na elimu bora, ujuzi, huduma za afya na kinga ya jamii. Ustahimilivu wa tabianchi unahitaji hatua katika matumizi ya ardhi na maendeleo ya kaboni ya chini.

Elimu na Ujuzi · Afya · Tabianchi

NGUZO TATU MSINGI ZA MAGEUZI

NGUZO YA 1

**Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani**

NGUZO YA 2

**Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii**

NGUZO YA 3

**Hifadhi ya Mazingira na Ustahimilivu wa Tabianchi**

MPANGO IV · Sura ya 2 — *Changamoto za Maendeleo · Nguzo Tatu*

NADHARIA YA MABADILIKO

## Dhana ya U Tatu (3U) — Uwekezaji · Uasilishaji · Ubunifu

Nadharia ya mabadiliko iliyopangwa inayogeuza uwekezaji kuwa matokeo ya uzalishaji kupitia uunganishaji wa minyororo ya thamani na uimarishaji wa teknolojia.

U YA KWANZA

### Uwekezaji

Unapanua miundombinu, viwanda na ujuzi — ukiweka misingi ya mtaji wa kimwili na rasilimali watu inayohitajika kwa mageuzi ya kimuundo katika sekta zote.

U YA PILI

### Uasilishaji

Unaunganisha rasilimali katika minyororo ya thamani ya ndani ili kuongeza ushindani — ukiunganisha uwekezaji na shughuli halisi za kiuchumi zinazozalisha ajira na kipato.

U YA TATU

### Ubunifu

Unaharakisha uimarishaji wa teknolojia, uongezaji thamani na uzalishaji wa maarifa — ukiiwezesha Tanzania kupanda katika mnyororo wa thamani wa kimataifa na kukuza mauzo nje.

**Kanuni Elekezi — “Anza na Yale Yanayofungua Mengine”**

Mageuzi ya utawala → Miundombinu → Tija → Ujumuishi na Urasimishaji



MWELEKEO NA SHABAHA ZA KIMKAKATI

## Malengo Manne — Pato $118B na Ukuaji 10.5% ifikapo 2031

Matokeo ya juu (Jedwali 2.1) yanayoonesha kiwango cha msingi 2024/25 → shabaha 2030/31 katika viashiria vikuu vinavyoegemeza kila mwelekeo wa kimkakati.

01 **Utulivu wa Uchumi Jumla**

02 **Uchukuzi na Biashara**

03 **Rasilimali Watu na Ustahimilivu wa Kijani**

04 **Mageuzi ya Sekta za Uzalishaji**

SHABAHA KUU — MSINGI → 2030/31

| Kiashiria | Msingi | 2030/31 |
|---|---|---|
| Pato la Taifa (USD bn) | 81.5 | 118 |
| Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa | 5.5% | 10.5% |
| Pato la Mtu (USD) | 1,344 | 1,638 |
| Umaskini Uliokithiri | 8% | 5% |
| Matarajio ya Kuishi (miaka) | 68.3 | 70.4 |
| Ukosefu wa Ajira 15+ | 6.2% | 4.4% |
| Umeme (MW) | 4,505 | 8,000 |
| Upatikanaji wa Intaneti | 79% | 98% |










# SURA YA TATU: MWELEKEO NA MBINU MKAKATI







# SURA TA TATU
# MWELEKEO WA MBINU MKAKATI

## 3.1 Muhtasari

Sura hii inatafsiri masuala muhimu ya maendeleo yaliyoainishwa katika Sura ya Pili, ikiyaweka katika afua za kimkakati zitakazoongoza utekelezaji wa Mpango IV. Ikiziangazia changamoto na fursa kuu zinazoielekeza Tanzania katika safari yake ya mabadiliko ya muda mrefu, hususan, tija ndogo ya uzalishaji, uchumi usiokuwa mseto kuwezesha ushiriki na ushindani wa kina katika mauzo nje, na mapungufu katika uwezo wa rasilimali watu. Changamoto nyingine ni udhaifu katika mifumo ya utawala na ufanisi wa taasisi, tofauti za maendeleo kati ya maeneo, pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa muktadha huu, Sura hii inaainisha vipaumbele vya mageuzi, vichocheo vya uwekezaji, na hatua zinazohitajika ili kupata mwelekeo unaoendana na matarajio ya muda mrefu ya Dira 2050.

Afua za kipaumbele zilizobainishwa katika sura hii zimejengwa juu ya malengo yaliyobainishwa katika Sura ya Pili. Kila kundi la afua limeundwa ili kuchochea kufikia azma ya kuwa taifa lenye ustawi jumuishi, haki, na linalojitegemea. Aidha, afaua hizi zinashughulikia vikwazo vya kimfumo vinavyozuia Tanzania kufikia hadhi ya kuwa na uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ushindani katika masoko, na ustahimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, sura hii inaeleza njia za kimkakati ambazo zitatumika kuharakisha ukuaji wa uchumi na mabadiliko ya muundo wa uchumi, kuimarisha uwezo wa kitaasisi, na kuboresha maendeleo ya watu. Afua zilizopewa kipaumbele zinajenga msingi wa viashiria vikuu vya utendaji na shabaha za kupimia utekelezaji wa malengo yaliyobainishwa katika Kiambatisho cha Pili. Kiambatisho hiki kinafafanua namna ambavyo maendeleo yatapimwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango. Kwa hiyo, Sura ya Tatu inatafsiri vipaumbele vya maendeleo kuwa afua za kisera zinazotekelezeka na zinazopimika katika vipengele vifuatavyo: (i) masuala muhimu yaliyoainishwa katika Sura ya Pili, (ii) afua za kimkakati zilizoainishwa katika Sura ya Tatu na (iii) viashiria vikuu vya utendaji pamoja na malengo yaliyobainishwa katika Kiambatisho cha Pili; vyote kwa Pamoja vikiunda mnyororo jumuishi wa matokeo unaoongoza utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango IV.

## 3.2 Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

Mageuzi endelevu yanahitaji kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani unaokua kwa kasi, sambamba na kuendeleza uchumi wa viwanda utakaoiwezesha nchi kuwa kitovu cha kikanda cha usafirishaji, uchukuzi na biashara. Kwa msingi huo, Mpango unaweka kipaumbele katika kutekeleza mageuzi yatakayoimarisha msingi thabiti wa uchumi jumla, kuongeza ustahimilivu wa serikali kifedha, kuimarisha sekta ya nje, na kuharakisha mabadiliko katika sekta za uzalishaji. Mageuzi haya yanalenga kukuza shughuli za uongezaji thamani, kupunguza gharama za uendeshaji biashara, kuinua uwezo wa kushindana katika masoko ya nje, na kuunganisha bidhaa na makampuni ya ndani katika masoko ya kikanda na kimataifa. Usasishaji wa sera za fedha na utekelezaji wa mageuzi tarajiwa, utaimarisha uthabiti wa kifedha na kuwezesha kujengwa kwa mfumo wa kubadilishana fedha unaozingatia viwango vya riba, usimamizi madhubuti wa ukwasi na utekelezaji bora wa sera. Afua nyingine ni kupanua soko la mitaji la ndani, matumizi ya hati fungani katika kugharamia miradi ya mazingira, uchumi wa buluu na miundombinu. Hii pia itasaidia kuimarisha uwazi katika usimamizi wa madeni, uthabiti wa sekta ya nje, biashara mseto na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji kodi ya kidijitali ili kuongeza mapato. Mageuzi haya yatahakikisha uwepo wa uwezo wa kifedha wa kutosha wa Serikali kuwezesha maendeleo ya viwanda, mifumo ya usafirishaji na uchukuzi, na uvumbuzi wa bidhaa na huduma mpya.

### 3.2.1 Utulivu na Utabirifu wa Uchumi Jumla

**Hali ilivyo:** Tanzania inaingia katika utekelezaji wa Mpango IV ikiwa na msingi imara na utulivu wa uchumi jumla uliojengwa katika kipindi cha muongo uliopita. Utulivu huu unadhihirishwa kufuatia kuwepo kwa kasi ndogo ya mfumuko wa bei, ukuaji thabiti wa uchumi, na uhimilivu wa sekta ya fedha. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.1 uliendelea kubaki ndani ya kiwango cha kati ya asilimia 3–5 sawa na kiasi kilicholengwa kwa mwaka 2024 na 2025. Hii inatokana na kuwepo kwa sera thabiti za fedha na kuimarika kwa uhakika wa upatikanaji wa chakula nchini. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ndani ya kiwango kinachokubalika cha miezi 4.4 ya gharama za uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, thamani ya shilingi iliendelea kuwa imara licha ya shinikizo la ongezeko la bei katika masoko ya kimataifa. Pato la taifa lilikua kwa asilimia 5.5 mwaka 2024, likichagizwa, kwa kiasi kikubwa, na uwekezaji endelevu katika miundombinu, kuongezeka kwa mapato ya sekta ya utalii na kuimarika kwa shughuli za sekta ya huduma. Mapato ya ndani yalifikia asilimia 14.9 ya pato la Taifa, wakati uwiano wa mapato ya kodi kwa pato la Taifa ulifikia asilimia 13.1. Hata hivyo, kiwango hiki kilibaki chini ya wastani kwa nchi linganifu zenye kipato cha kati cha chini, ikidhihirisha hitaji la kuendelea kuboresha mifumo ya usimamizi wa kodi na kurasimisha shughuli za uchumi zisizo rasmi.

**Changamoto:** Pamoja na kuwepo kwa msingi imara, uchumi bado una vihatarishi vinavyosababishwa na mazingira ya nje, hususan, utegemezi mkubwa wa mapato yanayotokana na mauzo ya bidhaa ghafi na kuendelea kununua zaidi bidhaa za kati na za uzalishaji kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa. Vilevile, uwekezaji mdogo katika uchumi hali inayochangiwa na kiwango kidogo cha mikopo inayotolewa kwa sekta binafsi, takribani asilimia 16 tu ya pato la Taifa kwa mwaka 2025, pamoja na ufinyu wa upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu inayowezesha upanuzi wa viwanda na ubunifu. Masoko ya mitaji yameendelea kuwa dhaifu, na hivyo kuzuia upatikanaji wa mitaji katika soko la ndani. Shinikizo la kibajeti linalotokana na kuongezeka kwa matumizi ya kawaida ya serikali pamoja na kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu inayofikia asilimia 3.2 kwa mwaka, linaendelea kupunguza uwezo wa kifedha wa serikali kwa ajili ya kugharamia uwekezaji wa kimkakati. Vilevile, tija ndogo katika sekta muhimu, sambamba na mabadiliko ya bei yasiyotabirika katika masoko ya kimataifa, vinaendelea kudhoofisha ustahimilivu wa sekta ya nje na utulivu wa viwango vya ubadilishaji fedha. Kwa ujumla, vikwazo hivi vyote,vilichangia kutofikiwa kwa shabaha ya Mpango III (2021/22 – 2025/26) ya ukuaji wa uchumi kwa asilimia 8, na badala yake kuishia asilimia 5.5 tu mwaka 2024.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Ili kujenga msingi imara wa uchumi jumla katika utekelezaji wa Dira 2050, kwa kipindi cha miaka mitano ya Mpango IV (2026/27–2030/31), yanahitajika mabadiliko ya msingi. Mabadiliko haya yanahusisha kutoka kukazania kudumisha utulivu pekee na kuongeza kasi itakayo harakisha mageuzi na ukuaji wa uchumi. Hili litahitaji hatua za makusudi za kuimarisha usimamizi ili kuendeleza utulivu wa uchumi jumla, kujenga mazingira wezeshi na tabirifu ya uwekezaji yatakayofungua fursa za viwanda vinavyozalisha bidhaa za viwanda kwa ajili ya masoko ya nje, matumizi ya nishati safi na mageuzi ya kiteknolojia. Afua muhimu zitakazochukuliwa zinajumuisha kuhakikisha uthabiti sera za bajeti, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, kuongeza uwezo wa ufuatiliaji na kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za mitikisiko ya nje na kutekeleza mageuzi ya kimfumo yatakayolenga kuboresha na kupanua minyororo ya ugavi wa ndani ili kuendana na mahitaji ya soko, kudhibiti upandaji holela wa bei za chakula na kupanua matumizi ya mifumo ya kidijitali katika malipo na hivyo kupunguza gharama za miamala na kuongeza ushiriki wa jamii katika masuala ya fedha. Kiambatisho I (3.2.1) kinaonesha maelezo ya kina ya afua na mpangilio wa utekelezaji na kiambatisho II (3.2.1) kinaainisha mfumo wa viashiria vya matokeo vya uchumi jumla.

*Jedwali 3.1: Viashiria vya Mwenendo wa Utulivu wa Uchumi Jumla na Utabirifu*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Pato la taifa, kwa bei za sasa (dola za Marekani bilioni) | 81.537 (2024) | 118.052 |
| Ukuaji wa pato la taifa (bei za soko) (%) | 5.5.0 (2024) | 10.5 |
| Pato la mtu kwa mwaka (dola za Marekani ) | 1,343.91 (2024) | 1,638 |
| Uwiano wa deni la taifa kwa pato la taifa (ikipimwa dhidi ya viwango vya tathmini vya uhimilivu wa deni) (%) | 48.9 (2025) | <55 |
| Mfumuko wa bei (wastani kwa mwaka) (%) | 3.1 (2024) | 3–5 |
| Ukuaji wa mwaka wa mikopo kwa sekta binafsi (ukuaji kwa mwaka) (%) | 15.9 (2024) | 22.4 |
| Mikopo ya ndani kwa sekta binafsi (uwiano kwa pato la taifa) (%) | 16.3 (2025) | 25 |
| Mfumuko wa bei (%) (kiwango cha mwisho wa mwaka) | 3.1 (2024) | 3–5 |
| Kiwango cha mfumuko wa bei za msingi (%) | 3.4 (2024) | 3–5 |
| Mikopo chechefu (%) (uwiano na jumla ya madeni yote) | 3.3 (2024) | <5 |
| Ushirikishwaji katika sekta ya fedha (%) (watu wazima) | 72 (2023) | 90 |
| Watu wazima wenye akaunti za miamala (%) | 72 (2023) | 85 |
| Watu wazima wanaofanya Malipo kwa mifumo ya kidijitali (%) | 13 (2023) | 40 |

### 3.2.2 Kuimarisha Uwezo wa Kifedha wa Serikali

**Hali Ilivyo:** Tanzania inaanza utekelezaji wa Mpango IV ikiwa imeimarisha nidhamu ya usimamizi wa fedha za umma, hatua iliyowezesha kudumisha ustahilivu wa uchumi jumla licha ya mitikisiko ya uchumi wa dunia na ongezeko la mahitaji ya rasilimali za kifedha. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu, nakisi ya bajeti ilidhibitiwa katika wigo wa asilimia 3 ya pato la Taifa mwaka 2025/26 na hivyo kuendana na vigezo vilivyokubalika kwa utengamano katika Jumuiya za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Kadhalika, Serikali ilitekeleza mpango wa uwekezaji katika miradi ya umma yenye thamani ya Shilingi  trilioni 27 hadi29, sawa na dola za marekani bilioni 10.7–11.3, katika sekta za kilimo, miundombinu na huduma za jamii. Makusanyo ya mapato ya kila mwezi yalifikia Shilingi  trilioni 2.1 mwezi Aprili 2025, huku deni la Taifa likibaki kuwa himilivu katika kiwango cha asilimia 46.3 ya pato la Taifa. Kiwango hicho kilibaki chini ya ukomo wa asilimia 60 uliowekwa na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na pia chini ya kiwango cha asilimia 55 kilichotumika kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni. Kwa ujumla, matokeo haya yanaakisi nidhamu ya fedha, usimamizi madhubuti wa deni la umma, na mwelekeo sahihi wa uwekezaji wa umma unaoelekezwa katika miradi yenye tija na manufaa makubwa kwa Taifa.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio yaliyopatikana, uwezo wa kifedha wa Serikali uliendelea kuwa mdogo, ukichangiwa na wigo mdogo wa kodi, kuenea kwa shughuli zisizo rasmi, na ukuaji hafifu wa mapato ukilinganishwa na kasi ya ukuaji wa uchumi. Wakati huo huo, ongezeko la matumizi ya kawaida ya Serikali lilifikia asilimia 69 ya bajeti, likichochewa na gharama za mishahara, manunuzi ya bidhaa na huduma, pamoja

na utekelezaji wa majukumu ya kijamii. Mwenendo huu umepunguza upatikanaji wa rasilimali za maendeleo na kusababisha utekelezaji wa bajeti kuishia kwenye asilimia 67 kwa kipindi chote cha miaka mitano, na hivyo kupunguza mchango wa uwekezaji wa umma.

Gharama za kulipa deni ziliendelea kuwa kubwa katika mazingira ambayo ukuaji wa mapato uliendelea kuwa chini ya kiwango. Aidha, mapato ya ndani yalifikia asilimia 14.9 ya pato la Taifa ambayo ni chini ya lengo la asilimia 16.9 na mapato ya kodi yalifikia asilimia 13.1 chini ya shabaha ya asilimia 14.4. ya pato la Taifa. Hali hii ilichangiwa na ugumu wa kukusanya mapato ya shughuli zisizo rasmi na ufinyu wa wigo wa kodi. Kukosa ufanisi katika mashirika ya umma na taasisi zilizoundwa kisheria kulipunguza gawio kwa Serikali na kuongeza vihatarishi vya kifedha, wakati upungufu katika utayarishaji wa miradi na uwezo mdogo wa usimamizi wa utekelezaji, viliathiri ufanisi wa uwekezaji kwa baadhi ya miradi ya umma. Wakati huo huo, mifumo ya mapato ya Serikali za Mitaa haikuwa linganifu pamoja na ongezeko la misamaha ya kodi kuzidi ukomo uliowekwa wa asilimia 1 ya pato la Taifa. Vilevile, mitikisiko ya kimataifa, ikiwemo mabadiliko ya bei za bidhaa ghafi na masharti magumu ya upatikanaji wa fedha katika masoko ya kimataifa, inaongeza vihatarishi katika gharama za ukopaji wa nje na uhimilivu wa deni.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ina nafasi kubwa ya kufanya mageuzi katika usimamizi wa fedha za umma kwa kuanzisha mfumo wa kisasa, wenye wigo mpana na endelevu wa mapato unaotumia teknolojia na nyenzo za kidijitali. Aidha, urasimishaji wa shughuli za kiuchumi utaongeza vyanzo endelevu vya mapato ya ndani na kupanua wigo wa mapato. Sambamba na hilo, ni usawazishaji wa matumizi ya umma unatoa nafasi ya kuelekeza rasilimali zaidi kutoka katika matumizi ya kawaida kwenda kwenye uwekezaji wenye matokeo makubwa. Vilevile, afua nyingine ni kuhakikisha kuwa miradi inayogharamiwa kwa fedha za mikopo ina tija, kuimarisha usimamizi wa vihatarishi vya kifedha, kuongeza uhimilivu wa kiuchumi, kufungua vyanzo vipya vya mapato yasiyo ya kodi, na kuboresha matumizi ya rasilimali za umma. Kiambatisho I (3.2.2) kinaonesha afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.2.2) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa uhimilivu wa kifedha.

*Jedwali 3.2: Viashiria vya Mwenendo wa Kuimarisha Uhimilivu wa Kifedha na Utabilifu*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Uwiano wa mapato ya ndani kwa pato la Taifa (%) | 14.9 (2024/25) | 20.0 |
| Uwiano wa mapato ya kodi kwa pato la Taifa (%) | 13.3 (2024/25) | 18.0 |
| Uwiano wa mapato yasiyo ya kodi kwa pato la Taifa (%) | 2.7 (2024/25) | 5.0 |
| Kiasi cha deni la Taifa kwa pato la Taifa (%) (ikilinganishwa na shabaha ya uhimilivu wa kifedha) | 47.0 (2024/25) | <50.0 |
| Thamani ya sasa ya deni la Taifa kwa pato la Taifa (%) | 40.3 (2024/25) | 19.6 |
| Thamani ya sasa ya ulipaji wa deni kwa mapato ya ndani (%) | 44.3 (2023/24) | 15 |
| Thamani ya sasa ya deni la nje kwa thamani ya mauzo nje (%) | 123.8 (2024/25) | 100.3 |
| Nakisi ya Bajeti (% ya pato la Taifa) | -3.1 (2024) | -2.8 |
| Matumizi ya maendeleo (% ya jumla ya bajeti yote) | 31 (2024/25) | 35–40 |

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Uwiano wa malipo ya riba kwa mapato yote (%) (kwa mwaka) | 11 (2023) | ≤8 |
| Jumla ya mahitaji yote ya fedha (% ya pato la Taifa) | 35 (2024) | 35 |
| Muda wa wastani wa deni kuiva (miaka) | Miaka 9 (2023) | Miaka 12 |
| Gawio Halisi la mashirika ya umma (% ya pato la Taifa) | <0.2 (2023) | 0.5–1 |
| Hisa za dhamana (% ya pato la Taifa) | 2.8 (2023) | ≤3 |

### 3.2.3 Uhimilivu na Usetushaji wa Sekta ya Nje

**Hali Ilivyo:** Sekta ya Nje imeimarika katika kipindi cha muongo uliopita, ikichochewa na ongezeko la mauzo ya nje, maboresho ya huduma za bandari na kuongezeka kwa biashara ya kikanda. Mauzo ya dhahabu nje yalifikia dola za Marekani bilioni 3.84 huku bidhaa za viwandani, kilimo cha bustani na biashara ya huduma ikiendelea kukua. Utalii umekuwa kwa kasi kubwa na hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni. Katika kipindi cha muongo uliopita, nakisi katika urari wa malipo ya bidhaa na huduma ilipungua kutoka asilimia 10 ya pato la Taifa, mwaka 2014 hadi asilimia 3.0 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na ukuaji mkubwa wa mauzo ya nje hadi kufikia asilimia 19 kwa mwaka na utulivu wa uagizaji wa bidhaa toka nje. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa katika kiwango himilivu ikifikia kiwango cha kukidhi gharama za kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 4.4, na hivyo kuimarisha utulivu wa thamani ya shilingi. Matumizi ya mfumo wa forodha wa kidijitali, maboresho ya bandari, na kuimarishwa kwa uratibu mipakani kumeboresha uwezeshaji na kuongeza ushindani wa biashara ya usafirishaji na uchukuzi wa mizigo ya nchi jirani. Haya kwa pamoja, yameifanya sekta ya nje kuwa injini muhimu ya ukuaji wa uchumi, kuimarisha utulivu wa kifedha na ongeza mapato ya fedha za kigeni.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, mfumo wa biashara umeendelea kuwa finyu na usioweza kuhimili mitikisiko. Mauzo nje yanategemea zaidi bidhaa ghafi, ikiashiria umuhimu wa kuwekeza katika afua za kuongeza thamani na kukuza kasi ya mageuzi ya muundo wa uchumi ili kuongeza mseto wa mauzo ya nje. Ziada katika malipo ya kawaida imeendelea kudhoofishwa na utegemezi mkubwa wa ununuzi wa bidhaa kutoka nje, hususan bidhaa za petroli zinazochangia asilimia 25.9, na huduma kwa asilimia 27 ya ankara ya uagizaji. Aidha, gharama kubwa za usafirishaji na uchukuzi, mauzo ya nje ya bidhaa ghafi, changamoto za mifumo ya uwezeshaji biashara pamoja na vikwazo vya kikanda visivyokuwa vya ushuru vinaendelea kudhoofisha ushindani na kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi mseto. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuhama kutoka katika uchumi unaotegemea bidhaa ghafi kuelekea uchumi unaojikita katika viwanda, huduma na mauzo ya nje yanayotokana na matumizi ya teknolojia za kisasa.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ina fursa ya kufanya mageuzi ya msingi katika muundo wa uchumi wake kwa kupunguza utegemezi wa bidhaa ghafi na kujenga uchumi mseto wa uzalishaji na mauzo ya nje yaliyoongezwa thamani. Mikakati ya uzalishaji viwandani na uchakataji wa bidhaa za kilimo utaongeza thamani na kuzalisha bidhaa muhimu zinazoagizwa kwa wingi kutoka nje. Aidha, Taifa litaweza kuongeza ushiriki wake katika minyororo ya thamani ya biashara ya kimataifa. Mabadiliko haya yatakayoimarishwa na uwekezaji katika mifumo ya uwezeshaji wa biashara na miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi, yataiweka Tanzania katika nafasi nzuri ya kuwa kitovu shindani cha biashara ya kikanda kwa kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza ufanisi. Vilevile, kukuza mauzo ya nje ya huduma zenye mchango mkubwa,

husussan utalii na huduma za kifedha, sambamba na kuimarisha mtangamano katika biashara ya kikanda vitaongeza vyanzo vya mapato ya fedha za kigeni na kujenga mfumo imara. Kwa ujumla, juhudi hizi zitaimarisha sekta ya nje, kupunguza athari za misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa, na hivyo kuwezesha ukuaji wa uchumi endelevu na shirikishi. Kiambatisho I (3.2.3) kinaonesha afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.2.3) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta ya nje.

Jedwali 3.3: Viashiria vya Mwenendo wa Ustahimilivu wa Sekta ya Nje na Uchumi Mseto

| Kiashiria cha Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Urari wa malipo ya kawaida (% ya pato la Taifa) | -2.6 (2024) | -2.1 |
| Akiba ya fedha za nje (miezi ya uigizaji bidhaa kutoka nje) | 4.5 (2024) | 5 |
| Thamani ya uwekezaji wa moja kwa moja toka nje – dola za Marekani milioni | 1,717.6 (2024) | 8,366.28 |
| Mchango wa mauzo nje ya bidhaa asilia kwenye jumla ya mauzo yote ya nje (%) | 16.2 (2024) | 11.05 |
| Mchango wa mauzo nje ya bidhaa zisizo za asili kwenye jumla ya mauzo yote ya nje (%) | 79.2 (2024) | 84.15 |
| Mchango wa mauzo nje ya bidhaa za viwanda kwenye jumla ya mauzo yote nje ya bidhaa zisizo asilia (%) | 18.6 (2024) | 29.59 |

## 3.3 Mageuzi katika Sekta za Kimkakati

Mageuzi ya uchumi yataelekezwa katika sekta za kimkakati ambazo kwa pamoja zitaongeza tija, thamani na ukuaji jumuishi. Sekta hizo ni pamoja na kilimo, ambacho ni msingi wa usalama wa chakula na chanzo cha malighafi kwa viwanda; ujenzi, ardhi na uendelezaji wa majengo na makazi, kama vichocheo vya ustawi na uendelezaji wa miji; pamoja na madini na uchimbaji, mafuta na gesi, kama sekta muhimu za kuimarisha usalama na upatikanaji wa nishati na kuchochea uchakataji wa ndani. Kadhalika, sekta za utalii, michezo, sanaa na ubunifu zitachangia kuongeza mauzo ya huduma na kuitangaza nchi kimataifa.  Sekta ya fedha, biashara, ujasiriamali na ushiriki wa kikanda huimarisha ushirikiano na mtangamano wa masoko, uwekezaji na ushindani. Sekta hizi ni uti wa mgongo wa mabadiliko, zitaiwezesha nchi kuwa na  uchumi imara, ushindani, unaochochewa na mauzo nje, kama ifuatavyo:

### 3.3.1 Sekta ya Kilimo

Sekta ya kilimo inayojumuisha mazao, mifugo, uvuvi na ufugaji wa viumbe wa majini, misitu na mazao ya misitu, inaendelea kuwa nguzo muhimu ya uchumi wa Taifa. Kwa mwaka 2024 ilichangia asilimia 26.3 ya pato la Taifa na kuajiri asilimia 54.2 ya nguvukazi watu. Sekta hii ndiyo msingi wa usalama wa chakula, chanzo cha malighafi za viwandani, nguzo ya mapato ya mauzo nje na tegemeo kubwa la ustawi wa maisha ya wananchi vijijini. Katika utekelezaji wa Mpango III mafanikio kadhaa yalipatikana, ikiwemo upanuzi wa skimu za umwagiliaji, kuimarika kwa mifumo ya usambazaji wa mbegu na ufugaji, kuboresha huduma za mifugo na maeneo ya kutua samaki, kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi mazao na bidhaa zinazoharibika haraka, pamoja na ukuaji wa misitu ya biashara.

Hata hivyo, kasi ya mabadiliko imebaki chini ya matarajio kutokana na matumizi madogo ya mitambo, tija duni, ukosefu wa fedha na athari za mabadiliko ya tabianchi, pamoja na muunganiko dhaifu wa mnyororo wa thamani. Hivyo, Mpango unaelekeza mabadiliko kutoka kwenye kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo cha kibiashara kitakachotumia teknolojia ya kisasa. Mkazo zaidi utawekwa kwenye mauzo nje kwa

kuzingatia uwekezaji wa kimkakati, matumizi ya mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, maendeleo ya viwanda vinavyotengemea kilimo na kuimarisha uhusiano kati ya uzalishaji na masoko.

**Hali Ilivyo**

**Mazao:** Kilimo cha mazao kimeendelea kuwa mchangiaji mkubwa katika sekta ya kilimo kikichangia asilimia 16.1 ya pato la Taifa. Umuhimu wa kilimo hiki unadhihirika katika kuhakikisha upatikanaji na usalama wa chakula nchini na malighafi muhimu katika uzalishaji wa viwanda vya ndani. Pamoja na kuongezeka kwa tija katika baadhi ya maeneeo ya uzalishaji, bado kilimo cha mazao kinakabiliwa na uzalishaji usiotabirika. Hali hii inatokana na utegemezi mkubwa wa mvua na muundo wa masoko usioendana na mahitaji ya wakati.

**Mifugo**: Sekta ya mifugo inachangia asilimia 6.2 ya pato la Taifa, ikidhihirisha umuhimu wake katika uchumi wa Taifa. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika ukuzaji wa mifugo, mifumo ya ufugaji na utoaji wa huduma za kitabibu kwa wanyama, sekta hii inakabiliwa na maendeleo hafifu ya minyororo ya thamani na uwezo mdogo wa usindikaji wa mazao ya mifugo.

**Uvuvi na Viumbe:** Sekta ya uvuvi na viumbe vya majini inachangia asilimia 1.6 kwenye pato la Taifa. Licha ya maboresho yaliyofanyika katika miundombinu na ugavi, ukuaji wa sekta hii bado unakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uvuvi haramu na udhibiti usioridhisha wa vitendo visivyozingatia taratibu, matumizi ya vyombo na zana asili zilizo duni za uvuvi pamoja na mifumo na taratibu zisizoendelezwa vya kutosha za ufugaji, uvuaji na uvunaji wa viumbe wa majini.

**Misitu:** Sekta ya misitu inajumuisha misitu na ufugaji wa nyuki na inachangia asilimia 2.4 ya pato la Taifa na hivyo kuwa moja ya vichocheo muhimu katika kujenga uchumi wa viwanda. Sekta hii ina mchango mkubwa katika upatikanaji wa nishati na maendeleo ya viwanda vinavyotumia mazao ya misitu kwa kuongeza thamani ya mazao, hususan viwanda vya mbao na utengenezaji wa samani. Hata hivyo, uharibifu wa mazingira na matumizi madogo ya teknolojia za kisasa vinaendelea kudhoofisha maendeleo ya sekta hii.

**Changamoto**

**Mazao:** Ingawa kilimo cha mazao ndicho chenye mchango mkubwa zaidi katika pato la kilimo, bado kinakabiliwa na vikwazo vya muda mrefu vinavyopunguza tija. Matumizi hafifu ya mitambo na vifaa vya kisasa, usimamizi usioridhisha wa rutuba ya udongo na matumizi madogo ya kilimo cha umwagiliaji, vinadhoofisha uzalishaji. Aidha, upotevu mkubwa wa mazao baada ya kuvuna unaotokana na uhaba wa miundombinu ya kuhifadhi na kuchakata mazao, unaochangiwa na huduma za kifedha zisizotosheleza mahitaji pamoja na mitikisiko ya mara kwa mara inayotokana na mabadiliko ya tabianchi, vimeendelea kukwamisha ukuaji na wa sekta hii.

**Mifugo:** Licha ya nchi kuwa na idadi kubwa ya mifugo, sekta hii imeendelea kuwa tija ndogo huku minyororo ya thamani ya nyama, maziwa, ngozi na kuku ikiwa bado haijaendelezwa vya kutosha. Uwezo wa kuchakata mazao ya mifugo pamoja na mifumo ya baridi kwa ajili ya uhifadhi na usafirishaji hautoshelezi, hali inayosababisha ongezeko dogo la thamani. Aidha, matumizi hafifu ya mbari za mifugo zilizoboreshwa na upatikanaji duni wa huduma za tiba na afya ya mifugo vinaendela kudhoofisha uzalishaji. Ukosefu wa mifumo ya ufuatiliaji wa magonjwa, machinjio ya kisasa, vifaa vya kusafirishia na kuhifadhia maziwa pamoja na malisho ya kutosha, vinakwamisha

uzalishaji, tija na ukuaji wa biashara ya sekta ya mifugo. Aidha, utayari wa sekta kuingia na kushindana katika masoko ya nje bado unakwamishwa na kutozingatia viwango, pamoja na taratibu.

**Uvuvi na Viumbe vya Majini:** Ukuaji wa sekta ya uvuvi na viumbe vya majini unakwamishwa na uvuvi haramu, taarifa zisizo sahihi na uvuvi usiodhibitiwa ipasavyo, sanjari na uchakavu wa miundombinu ya bahari na zana duni zinazokwamisha uvuvi katika bahari ya  kina kirefu. Aidha, ukosefu wa pembejeo kwa ajili ya uzalishaji wa viumbe vya majini pamoja na kushindwa kukidhi viwango vya kimataifa na ithibati vya usalama wa chakula vinakwamisha ushindani na fursa ya ukuzaji wa biashara ya nje.

**Misitu:** Uendelevu wa misitu na ukuaji wa viwanda vya kuongeza thamani unakwamishwa na kasi ya ongezeko la ukataji miti kila mwaka, uchomaji wa misitu wa mara kwa mara, na utegemezi mkubwa wa matumizi ya mkaa. Vilevile, matumizi ya teknolojia duni za uchakataji zilizopitwa na wakati, mapungufu ya ujuzi, upatikanaji  mdogo wa fedha za kijani na utegemezi wa samani zilizosanifiwa kutoka nje vinaongeza nakisi ya biashara na kudhoofisha kasi ya mageuzi katika sekta. Ingawa sekta ya ufugaji nyuki haioneshwi bayana katika takwimu za pato la taifa, sekta hii ina fursa kubwa ya kuchangia ukuaji wa uchumi na kuongeza kipato cha kaya za vijijini. Hata hivyo, uhaba wa mizinga ya kisasa, huduma dhaifu za ugani na mifumo hafifu ya masoko vinazuia uendelezaji wa kibiashara wa sekta hiyo na kupunguza mchango wake katika uchumi wa vijijini.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Sekta ya kilimo ina fursa ya kuleta mageuzi ikiwa itabadilishwa kwenye uzalishaji wa malighafi kwenda kwenye kilimo cha biashara kilichoongezwa thamani, shindani na kuzalisha bidhaa bora na ajira zenye staha. Kwa kuwekeza katika miundombinu msingi na ya kisasa ya uchakataji, kujenga kongani za viwanda na kuendeleza ujuzi, hasa katika sekta zenye fursa kubwa kwa nchi yetu, kama vile nguo, mavazi na uchakataji wa mazao ya kilimo. Taifa linaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa upotevu wa mazao yanayoharibika baada ya kuvunwa, kuongeza mapato ya mauzo nje na kuzalisha ajira zenye staha.

Mabadiliko haya yakichochewa na maboresho ya mifumo ya uendeshaji wa sekta ya fedha, ikiwemo matumizi ya nyenzo za kupunguza vihatarishi kwa kutumia mbinu mbalimbali na ugharamiaji, ili kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa wakulima na wawekezaji wadogo, na kati na wawekezaji wengine katika sekta hiyo.

Hatua hizo zitafanya sekta ya kilimo kuwa ya kibiashara zaidi na kuboresha maisha ya watu vijijini. Aidha, kwa kuimarisha mifumo ya udhibiti, kuasili matumizi ya teknolojia za kidijitali ili kuimarisha shughuli za ufuatiliaji wa vyanzo vya mazao na huduma za ugani,  pamoja na kuhimiza matumizi ya  mbinu za kilimo-himilivu. Tanzania inaweza kuongeza tija, kukidhi viwango vya ubora na usalama wa chakula katika biashara ya kimataifa na kujenga ustahimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Mbinu hizi jumuishi zitahakikisha usalama wa chakula na pia zitaiwezesha Tanzania kuwa muuzaji wa kuaminika wa bidhaa mbalimbali za kilimo zenye thamani kubwa katika masoko ya kimataifa, na hivyo kuchochea ukuaji endelevu na jumuishi kiuchumi. Kiambatisho I (3.3.1) kinaonesha kwa kina, afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.1) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta ya kilimo.

*Jedwali 3.4: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Kilimo*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mchango wa sekta ya kilimo (%) kwenye pato la Taifa kwa bei ya miaka husika | 26.3 (2024) | 25.6 |
| Ukuaji halisi wa sekta ya kilimo (%) | 4.1% (2024) | 10% |
| Uwiano wa kujitosholeza kwa chakula | 128 (2024) | 130 |
| Mauzo ya nje ya sekta ya kilimo (Bilioni) | 3.54 | 5 |
| Mchango wa sekta ya kilimo katika mauzo ya nje ya bidhaa | 24 (2023/24) | 30 |
| Upotevu wa mazao baada ya mavuno (%) | 35 | 10 |
| Mikopo ya kilimo (% ya jumla ya mikopo yote) | 14.9 (2023) | 20 |
| Mchango wa sekta ya kilimo kwenye ajira (%) | 54.2 (2024) | 50 |

### 3.3.2 Sekta ya Viwanda

**Hali Ilivyo:** Sekta ya viwanda na uzalishaji viwandani imeendelea kukua kwa kasi, ikichangia kwa kiasi kikubwa katika mageuzi ya kiuchumi, kupanua fursa za ajira na mseto wa mauzo nje. Kufikia mwaka 2024, sekta ya viwanda, ambayo hujumuisha uzalishaji viwandani, ujenzi, madini na nishati ilikua kwa asilimia 5.5 na kuchangia asilimia 30.4 katika pato la Taifa. Kiwango hiki kilikaribia shabaha ya Mpango III ya asilimia 31.1. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na sekta za ujenzi (12.8%) na madini (10.1%), wakati uzalishaji viwandani ulichangia asilimia 7.3. Mwelekeo huu unaonesha umuhimu wa kujenga uchumi wa viwanda, kuongeza ushindani, na kupanua uzalishaji wa viwandani wenye thamani ya juu kama inavyoelezwa kwenye Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, vikwazo vya kimuundo na kitaasisi viliendelea kukwamisha kasi ya ukuaji wa sekta ya viwanda. Miundombinu isiyokidhi mahitaji, gharama kubwa za usafirishaji na uchukuzi, na ukosefu wa nishati ya uhakika viliathiri ukuaji wenye tija. Aidha, viwanda viliendelea kukabiliwa na ukosefu wa mikopo ya muda mrefu na nafuu, uwezo mdogo wa kuasili na kutumia teknolojia pamoja na uwekezaji mdogo katika shughuli za utafiti na maendeleo. Kadhalika, uhusiano dhaifu kati ya sekta za kilimo, viwanda na huduma unakwamisha maendeleo ya minyororo ya thamani, na kuendekeza utegemezi wa malighafi na vifaa vya uzalishaji kutoka nje, hivyo kudhoofisha ushindani katika masoko. Vilevile, pengo la ujuzi linaendelea kuongezeka katika nyanja za uhandisi, uzalishaji na ubunifu wa bidhaa za kidijitali. Maendeleo duni ya maeneo na kongani za viwanda, ushiriki mdogo katika minyororo ya thamani ya biashara ya kikanda na kimataifa, na utaratibu usiothabiti wa usimamizi, udhibiti na urekebu umeendelea kuzuia uwezo wa sekta kukua na muundo wake kupanuka zaidi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Sekta ya viwanda nchini ina nafasi kubwa ya kufanyiwa mageuzi ili iondoke kwenye utegemezi wa shughuli zenye thamani ndogo na kuwa kitovu shindani cha utengenezaji wa bidhaa za thamani kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu. Kwa kuazimia kuendeleza kongani za viwanda maalum, kukuza ubunifu kupitia maeneo mahsus ya ukuzaji wa teknolojia, na kuhimiza matumizi ya mbinu za kisasa za uzalishaji viwandani, nchi inaweza kujenga ikolojia ya mfumo imara wa viwanda unaojiendesha kwa ufanisi zaidi. Mfumo huo utategemea ushirikiano wa karibu kati ya sekta ya kilimo na viwanda. Aidha, biashara ndogo, za kati na kubwa, zinawezeshwa na kuunganishwa katika minyororo ya biashara ya ugavi ya kimataifa, huku wazalishaji wa ndani wakiungwa mkono kupitia taratibu mahsusi za manunuzi na upatikanaji wa mitaji. Msisitizo katika kuongeza thamani, sambamba na uzingatiaji thabiti wa viwango vya

kimataifa vya ubora na mazingira, utasaidia kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje. Vilevile, utaiwezesha Tanzania kuwa kinara wa mauzo ya bidhaa zenye thamani kubwa katika soko la kimataifa, ikiwemo vifaa vya kielektroniki na dawa. Kwa jumla, mkakati huu wa kukuza uchumi jumuishi wa viwanda utachochea fursa endelevu na kuzalisha ajira zenye staha, kukuza uchumi jumuishi na kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu kikuu cha viwanda kikanda. Kiambatisho I (3.3.2) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.2) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta.

*Jedwali 3.5: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Viwanda na Uzalishaji Viwandani*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mchango wa sekta ya viwanda (%) kwenye pato la Taifa–kwa bei za miaka inayohusika | 30.4 (2024) | 36.5 |
| Ukuaji halisi wa pato la sekta ya viwanda (%) | 5.5 (2024) | 8.0 |
| Mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani (%) kwenye pato la Taifa | 7.3 (2024) | 8 |
| Ukuaji halisi (%) wa sekta ya uzalishaji viwandani | 4.8 (2024) | 9.9 |
| Mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani katika mauzo ya nje ya bidhaa (%) | 22 | 30 |
| Mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani kwenye ya mauzo nje (%) | 9 | 15 |
| Mchango wa sekta ya viwanda kwenye ajira (%) | 9 (2024) | 15 |
| Mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani kwenye ajira (%) | 6 (2024) | 10 |

### 3.3.3 Sekta ya Ujenzi

**Hali Ilivyo:** Sekta ya ujenzi ni miongoni mwa nguzo kuu za mageuzi ya uchumi nchini. Mchango wake katika pato la Taifa ulifikia asilimia 12.8 mwaka 2024, ukichangiwa na uwekezaji mkubwa katika shoroba za usafirishaji, miundombinu ya nishati, viwanda na maendeleo ya miji. Pamoja na mchango wake wa moja kwa moja, sekta hii inaongeza mahitaji ya saruji, chuma, kioo, kauri na huduma za usafirishaji, na hivyo kuimarisha uhusiano kati ya shughuli za viwandani na huduma. Aidha, sekta ya ujenzi ina nafasi muhimu katika kuchochea mabadiliko ya maeneo, kuboresha na kuendeleza makazi na maeneo ya viwanda pamoja na miji mipya, hatua zinazochochea ukuaji jumuishi.

**Changamoto:** Licha ya sekta ya ujenzi kukua na kuimarika, uwezo wake wa kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi bado haujatumika ipasavyo. Hali hii inatokana na ushiriki mdogo wa makampuni ya ndani ya ujenzi katika miradi mikubwa, ukosefu wa mikopo ya muda mrefu ya kutosha, na kasi ndogo ya kuasili matumizi ya teknolojia za kisasa za ujenzi. Wakandarasi wa nje wameendelea kuhodhi ushiriki katika mikataba ya miradi yenye thamani kubwa, hali inayopunguza thamani halisi ya ujenzi inayobaki nchini na kasi ya uhawilishaji teknolojia.

Kwa kiasi kikubwa, sekta pia inategemea kuagiza mitambo na vifaa vya ujenzi kutoka nje. Wakati huohuo, changamoto za uendelevu zinaongezeka kutokana na kasi ya ukuaji wa miji kuliko uwezo wa kupima na kusimamia, teknolojia zenye matumizi makubwa ya nishati na kuongezeka kwa taka za ujenzi na hewa ya ukaa. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuimarisha matumizi ya teknolojia za ujenzi wa kijani na mbinu zinazozingatia uhifadhi wa mazingira.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kuna nafasi kubwa za kuibadili sekta ya ujenzi ili iwe ya kisasa zaidi, endelevu na inayoshirikisha kwa upana wakandarasi wa ndani. Kwa kuchukua hatua za makusudi kuweza kujenga mfumo wa ikolojia shirikishi, ikiwemo kuanzisha programu mahsusi za ufadhili wa kifedha, matumizi ya sheria za ubia kati ya sekta za umma na binafsi na kuweka masharti mahsusi ya ushiriki wa ndani, Taifa litawezesha wakandarasi na makampuni ya ndani ya ujenzi kushindana na kuongeza ushiriki katika miradi mikubwa ya ujenzi. Hatua hiyo itasaidia kubakiza sehemu kubwa zaidi ya mapato na thamani ya miradi ndani ya nchi. Mageuzi haya yakichochewa na matumizi ya mifumo ya kuasili na kuhamisha teknolojia za ujenzi wa kisasa, sanjari na hatua za kuendeleza ujuzi wa wafanyakazi wa ndani, kuweka utaratibu maalum wa kubadilishana ujuzi kati ya wanazuoni na makampuni ya ujenzi na uendeshaji wa mafunzo ya uanagenzi, kuongeza tija, ubora na kuinua ufanisi katika sekta ya ujenzi. Aidha, kwa kuendeleza mbinu za ujenzi wa kijani kupitia viwango, kanuni na motisha stahiki, Tanzania ina fursa ya kuwa kinara wa kikanda katika ujenzi wa miundombinu endelevu. Mwelekeo huu utasaidia kupunguza athari za uharibifu wa mazingira na kuimarisha ustahimilivu wa sekta, kuongeza ushiriki wa ndani, na kuifanya sekta ya ujenzi kuwa kichocheo muhimu cha uchumi wa viwanda na ukuzaji wa ajira zenye staha. Kiambatisho I (3.3.3) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.3) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta.

*Jedwali 3.6: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Ujenzi*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mchango wa sekta ya ujenzi (%) kwenye pato la Taifa | 12.8 (2024) | 15.5 |
| Ukuaji halisi wa sekta ya ujenzi (%) | 4.1 (2024) | 8.5 |
| Mchango (%) wa makampuni ya ndani katika soko la ndani | 40 (2023) | 50 |
| Mchango (%) wa sekta ya ujenzi kwenye ajira yote | 4 (2023) | 6 |

### 3.3.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji

**Hali Ilivyo:** Sekta ya madini na uchimbaji imeendelea kuwa kichocheo muhimu cha mageuzi ya uchumi nchini, ikichangia asilimia 10.1 ya pato la Taifa. Ukuaji halisi wa sekta ulifikia asilimia 8.3 mwaka 2024, na hivyo kuvuka lengo la Mpango III la asilimia 7.7 . Kwa miaka ya karibuni ikichangia karibu nusu ya mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Uwepo wa rasilimali nyingi za dhahabu, vito, gesi asilia na madini mkakati kama graffiti, lithiumu, kobalti, nikeli na madini adimu unaipa Tanzania nafasi nzuri ya kunufaika na mabadiliko ya dunia kuelekea katika matumizi ya nishati safi na teknolojia za betri. Maboresho yaliyofanyika chini ya Mpango III, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa vituo vya kuuzia madini kuimarishwa kwa mifumo ya kodi na kurasimisha wachimbaji wadogo, yamesaidia kukuza sekta ya madini nchini. Hatua hizi zimewezesha kudhibiti magendo, kuboresha ufuatiliaji na kuongeza kiasi cha mapato ya sekta yanayobaki nchini na hivyo kuimarisha kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na mseto wa mauzo ya nje.

**Changamoto:** Ingawa sekta ya madini ina mchango mkubwa katika uchumi, uwezo wake wa kuchochea ukuaji na mageuzi bado haujatumiwa kikamilifu. Mpaka sasa, ni asilimia 16 tu ya eneo la nchi lililofanyiwa utafiti wa kina wa ikolojia, hali inayozuia uvumbuzi wa rasilimali mpya na uwekezaji zaidi katika sekta. Kwa kiasi kikubwa, mauzo ya nje yanategemea madini ghafi, huku uwezo wa kuchakata, kusindika, na kuongeza thamani ya madini nchini ukiwa bado mdogo. Aidha, uhusiano wa sekta hii na sekta nyingine za uchumi bado ni dhaifu. Shughuli za wachimbaji wadogo zinakabiliwa na

upungufu wa mitaji, fedha za uendeshaji na teknolojia, huku uratibu miongoni mwa taasisi ukiendelea kuwa dhaifu. Vilevile, usimamizi wa uzingativu wa viwango vya mazingira na usalama bado si thabiti. Hali hii, pamoja na kuwa chini kwa faharisi ya mesto wa mauzo (-1.09), kunathibitisha umuhimu wa kubadilisha muundo wa sekta kutoka kutegemea uchimbaji wa madini ghafi kwenda kwenye kuongeza thamani na kuzalisha bidhaa za viwandani zitokanazo na madini.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Sekta ya madini ina fursa kubwa ya kuendelezwa zaidi ili isitumike kuzalisha malighafi pekee, bali pia kuwa chanzo cha uongezaji thamani na uzalishaji wa bidhaa za viwandani zitokanazo na madini. Kwa kutumia ipasavyo utajiri wa dhahabu, vito, na madini ya kimkakati, pamoja na fursa zitokanazo na ongezeko la matumizi ya nishati safi duniani, Tanzania inaweza kuvutia uwekezaji mkubwa katika uchenjuaji, usafishaji, uchakataji na utumiaji wa madini kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za viwandani zenye thamani kubwa. Hatua za msingi zinapaswa kuelekezwa katika kukamilisha utafiti wa kijiolojia, kuimarisha usimamizi wa uendeshaji wa sekta ya madini na kuziwezesha taasisi za umma ikiwemo Shirika la Madini la Taifa kujenga mazingira bora na yenye uwazi ya uwekezaji, kufufua miradi iliyokwama na kuvutia uwekezaji mpya kwa kupitia ubia kati ya sekta za umma na binafsi. Mageuzi hayo, sanjari na juhudi za kurasimisha na kusaidia wachimbaji wadogo zitawezesha wanawake, na vijana, na hivyo kufanya ukuaji wa sekta hii kuwa jumuishi na unaozalisha fursa nyingi na ajira zenye staha.

Aidha, kwa kuanzisha vituo maalum vya uendelezaji teknolojia ya madini, kuasisi "Kituo cha Vito cha Afrika" kinachotambulika kimataifa na kuongeza thamani kwenye madini, nchi itaweza kuondokana na kuuza malighafi na kuongeza kuzalisha bidhaa zinazotokana na madini, zikiwemo betri na vito. Hatua hizi zitawezesha nchi kunufaika kwa kiasi kikubwa na thamani inayopatikana katika madini, kusetusha uchumi na kuweka misingi imara na endelevu. Kiambatisho I (3.3.4) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.4) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta.

*Jedwali 3.7: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Madini na Uchimbaji wa Madini*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mchango wa sekta ya madini (%) kwenye pato la Taifa | 10.1 (2024) | 12.5 |
| Ukuaji halisi wa sekta ya madini (%) | 8.3 (2024) | 9 |
| Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Mauzo yote nje ya Nchi. | 46 (2024) | 55 |
| Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Mauzo ya Bidhaa zisizo za asili nje ya Nchi (Non-traditional goods). | 55 (2024) | 60 |

### 3.3.5 Sekta ya Mafuta na Gesi

**Hali Ilivyo:** Tanzania, ikiwa na akiba ya takribani futi za ujazo trilioni 57 za gesi asilia iliyothibitishwa, imeendelea kuwa nyenzo muhimu na ya kimkakati katika kujenga uchumi wa viwanda, kudumisha usalama wa nishati na kuhakikisha ustahimilivu wa kifedha. Kwa zaidi ya miongo miwili, uzalishaji wa gesi kutoka mashapo ya Mnazi Bay, Songo Songo na Kiliwani umeongeza matumizi ya gesi katika uzalishaji wa umeme, shughuli za viwandani na matumizi ya majumbani, na matumizi ya kibiashara. Maendeleo haya yamesaidia kupunguza utegemezi wa bidhaa za mafuta ya petroli kutoka nje, kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa umeme na kuchochea matumizi ya nishati safi, nafuu na inayotokana na vyanzo vya ndani.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio yaliyopatikana, uwezo wa sekta hii kuchochea mageuzi ya uchumi bado haujatumiwa kikamilifu. Mazungumzo ya kuendeleza miradi mikubwa ya kimkakati, hasa kituo cha kuchakata gesi asilia kuwa kimiminika cha Lindi, yamechukua muda mrefu, ingawa sasa yamefikia hatua za mwisho. Uwezo wa ndani wa kusafisha na kuchakata gesi bado ni mdogo, huku miundombinu ya usambazaji wa gesi ikishindwa kukidhi mahitaji ya viwanda, uchukuzi na kaya yanayoongezeka kwa kasi. Ushiriki wa ndani katika minyororo ya thamani ni wa kiwango cha chini, na kwa kiasi kikubwa unakwamishwa na ufinyu wa mitaji, uwezo mdogo wa kiufundi, na uhaba wa nguvukazi watu yenye ujuzi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Sekta ya mafuta na gesi ina nafasi kubwa ya kuendelezwa zaidi ili isiishie kuhudumia soko la ndani tu, bali iwe msingi wa usalama wa nishati nchini, kitovu cha biashara ya nishati katika ukanda huu, na chanzo cha mapato ya mauzo ya nje. Hatua za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ikiwemo kurahisisha kanuni na taratibu za urekebu na kisheria, pamoja na kuimarisha huduma za kuwezesha uwekezaji katika kituo kimoja, zitaharakisha utekelezaji wa miradi na programu za kielelezo kama kituo cha kuchakata gesi asilia kuwa kimiminika cha Lindi na kuvutia mitaji mikubwa inayohitajika. Mwelekeo huu wa kukuza matumizi ya gesi asilia, ukichagizwa na mikakati ya kujenga uchumi wa viwanda vya ndani, utachochea maendeleo ya maeneo na kongani za viwanda, kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje, na kukuza viwanda vinavyotegemea nishati hiyo vilivyopo nchini. Vilevile, kwa kuendeleza miundombinu ya gesi kuelekea mipakani na kuhakikisha uwiano wa sera za kibiashara za kikanda, Tanzania inaweza kuwa kitovu kikuu cha biashara ya gesi katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, na hivyo kupanua vyanzo vya mapato endelevu. Mageuzi haya yanapaswa kwenda sanjari na kujenga uwezo wa Taifa. Hivyo, ni muhimu kuimarisha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuwa shirika la mafuta na gesi la kiwango cha kimataifa na kuanzisha kituo cha umahiri cha kuendeleza ujuzi unaohitajika katika sekta. Hatua hizi zitasaidia kujenga nguvukazi watu yenye ujuzi na kuhakikisha kuwa utajiri wa maliasili za Taifa unachangia katika ustawi wa uchumi jumuishi na endelevu, pamoja na kuimarisha usalama wa nishati nchini. Kiambatisho I (3.3.5) linaonesha kwa kina, afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.5) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta.

*Jedwali 3.8: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Uzalishaji wa gesi asilia (milioni za futi za ujazo) | 69,538.30 (2024) | 90,000 |
| Mtandao wa usambazaji wa gesi asilia (KM) | 177.82 (2024) | 267.00 |
| Mchango (%) wa sekta ya gesi asilia kwenye nishati ya umeme | 63 (2024) | 45 |

### 3.3.6 Sekta ya Utalii

**Hali Ilivyo:** Utalii umeendelea kuwa moja ya nguzo muhimu za uchumi wa Tanzania, ukichangia asilimia 17 ya pato la Taifa na karibu robo ya jumla ya mapato ya mauzo nje, sambamba na kutoa ajira na kipato kwa mamilioni ya wananchi. Kwa mujibu wa Ripoti ya Utafiti wa Watalii wa Kimataifa ya 2024, Tanzania ilipokea wageni milioni 1.8 mwaka 2024, huku mapato ya utalii yakifikia dola za Marekani bilioni 3.7, ikiashiria kuendelea kuimarika kwa sekta hiyo na kuvutia zaidi soko la kimataifa. Tathmini ya kipindi cha kati cha Mpango wa Tatu inaonesha kuwa zaidi ya nusu ya viashiria vya ustawi wa sekta vimevuka asilimia 50 ya shabaha ya mwisho ya Mpango, ikichangiwa na kasi ya

ukuaji halisi iliyofikia asilimia 8.7 na ajira milioni 3.6, ambapo zimezidi shabaha kwa kiasi kikubwa. Mafanikio haya kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na kuongezeka kwa juhudi za kuitangaza Tanzania, kuimarika kwa usimamizi wa maeneo ya hifadhi, matumizi ya mifumo ya kidijitali, na kuongezeka kwa utangazaji wa vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, mathalan filamu ya Royal Tour. Ushindani linganishi wa utalii wa Tanzania unatokana na uwepo wa hifadhi za bayonuai za kipekee, ambapo eneo lililohifadhiwa ni zaidi ya asilimia 32 ya nchi. Kadhalika, utajiri wa utamaduni na historia unaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa maeneo yenye utalii wa hali ya juu.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio haya, uwezo wa sekta ya utalii bado haujatumika kikamilifu. Hali hii inatokana na kutegemea zaidi utalii wa mbuga na wanyamapori, hasa katika ukanda wa Kaskazini, jambo linalopunguza mapato katika uchumi na manufaa yanayowafikia wananchi. Vivutio vingine vya utalii, kama vile bahari na fukwe, utamaduni na malikale, utalii wa meli na hoteli za majini, mikutano na matukio, michezo, pamoja na utalii wa kilimo, bado havijaendelezwa vya kutosha. Aidha, usafiri wa anga usiokidhi mahitaji, ikiwemo uhaba wa viwanja vidogo vya ndege katika maeneo ya hifadhi, unapunguza ufanisi wa sekta. Vilevile, kuna upungufu wa wataalamu na watu wenye ujuzi katika maeneo muhimu ya sekta, kama vile waongoza watalii, wahudumu wa hoteli, na huduma za chakula na malazi. Hadi mwaka 2023, hoteli 315 pekee ndizo zilizokuwa zimepangwa katika makundi ya nyota za ubora. Pia, masharti na taratibu za kupata leseni za biashara zimeonekana kuwa kikwazo kwa ushiriki wa wawekezaji na wafanyabiashara wadogo na wa kati, hali inayochangia sekta hii kutegemea zaidi uagizaji kutoka nje ili kukidhi mahitaji yake.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Sekta ya utalii ina nafasi kubwa ya kupanua wigo wake na kuondoka katika utegemezi wa utalii wa mbuga na wanyamapori pekee, na kuwa na mseto wa maeneo mbalimbali ya utalii wa thamani duniani. Kwa kuendeleza utalii wa kimataifa wa fukwe, utamaduni, matukio na mikutano, pamoja na maeneo mengine ya kuvutia, Tanzania inaweza kujijengea nafasi imara zaidi katika soko la utalii la kimataifa. Mwelekeo huu utahitaji kuimarishwa kwa kuboresha miundombinu, kama vile viwanja vya ndege na maeneo maalum ya kiuchumi, pamoja na kuongeza msukumo katika uwekaji wa mifumo ya kidijitali kupitia majukwaa ya utalii mamboleo ili kuongeza ufanisi na uzoefu binafsi. Kwa umuhimu wa kipekee, ni muhimu kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati wa ndani kwa kurahisisha taratibu za udhibiti na kutoa ufadhili maalum pamoja na kuboresha upatikanaji wa mitaji, ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa sekta unakuwa jumuishi na kwamba sehemu kubwa ya thamani inabaki nchini. Kwa ujumla, mkakati huu wa kupanua mseto wa utalii, kuimarisha ubunifu wa kisasa na kuzingatia uendelevu, unalenga kufikia watalii milioni tano kwa mwaka na kuongeza kwa kiasi kikubwa mapato ya utalii. Lengo ni kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kivutio imara na stahimilivu cha utalii kimataifa. Kiambatisho I (3.3.6) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.6) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta.

*Jedwali 3.9:Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Utalii*

| Viashiria vya Matokeo | Halisia (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Nafasi kimataifa katika maendeleo ya usafiri na utalii | 81/119 (2021) | 60/119 |
| Mchango wa malazi kwenye pato la taifa (%) | 1.1 (2024) | 1.4 |
| Ukuaji halisi wa pato la sekta ya malazi (%) | 6 (2024) | 8.7 |
| Mapato ya mauzo nje ya utalii (dola za marekani bilioni) | 3.7 (2024) | 4.81 |
| Mchango wa mapato ya mauzo nje ya utalii (%) kwa mapato yote ya mauzo nje | 27 | 35 |

### 3.3.7 Sekta ya Fedha

**Hali Ilivyo:** Sekta ya huduma za fedha imeendelea kuwa mhimili muhimu wa mabadiliko ya uchumi wa Tanzania, ikichangia ukuaji wa uchumi wa viwanda, upatikanaji wa mitaji kwa shughuli za uzalishaji, ubunifu na ujumuishi wa wananchi katika uchumi. Kwa mwaka 2024, sekta ya benki imekua kwa kasi, ambapo jumla ya mali ilifikia shilingi trilioni 63.5 na faida halisi ya shilingi trilioni 2.15, ikiashiria ukuaji imara wa sekta. Ubora wa rasilimali uliimarika, ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulishuka hadi asilimia 3.2, kiwango ambacho ni cha chini zaidi katika miaka ya hivi karibuni, ukichangiwa na uboreshaji wa usimamizi wa vihatarishi na uwekaji wa akiba ya kutosha kwa ajili ya kufidia mikopo chechefu.

Benki za biashara zimeendelea kuwa vinara katika sekta ya benki, zikihodhi karibu nusu ya jumla ya mali na mikopo. Ujumuishi wa kifedha uliendelea kupanuka, ukichochewa na teknolojia ya ubadilishanaji fedha, huduma za benki kupitia simu za mkononi na mawakala, sambamba na maboresho katika mfumo wa udhibiti na urekebu, yaliosaidia kuimarisha utulivu na kurejesha imani yaliyosaidia wawekezaji.

**Changamoto:** Pamoja na maendeleo hayo, sekta ya fedha bado inakabiliwa na upungufu wa mitaji ya muda mrefu kwa ajili ya kuendeleza uwekezaji wenye tija. Upatikanaji wa mikopo kwa biashara ndogo na za kati, kilimo na kaya za maeneo ya vijijini bado ni mdogo kutokana na masharti magumu ya dhamana, mifumo dhaifu ya upatikanaji wa taarifa za mikopo, na matumizi hafifu ya tathmini mbadala kwa dhamana za mikopo. Upungufu wa masoko ya mitaji, ambayo kwa kiasi kikubwa yamejikita katika biashara ya dhamana za serikali, jambo linalozuia uwekezaji wa sekta binafsi. Mikopo kwa sekta binafsi ni kati ya asilimia 15 hadi 17 tu ya pato la Taifa, ikilinganishwa na zaidi ya asilimia 32 katika baadhi ya nchi jirani. Matumizi hafifu ya bima na pensheni kwa jamii, pamoja na ufinyu wa elimu ya kifedha, hasa miongoni mwa wanawake, vijana na wakazi wa vijijini, hali inayopunguza matumizi stahiki ya huduma za kifedha.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Mageuzi ya sekta ya fedha ni muhimu kwa ustawi wa Taifa, kwani yataiwezesha sekta hiyo kuondoka katika mtazamo wa kihafidhina na masharti kupita kiasi, na kuwa injini ya mabadiliko iliyojikita zaidi katika kuchochea ukuaji jumuishi wa kiuchumi. Kwa kutumia teknolojia ya kidijitali, kama vile akili unde na kanzidata kubwa katika kutathmini uwezo wa wakopaji, pamoja na usimamizi thabiti wa vihatarishi, nchi inaweza kupanua kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma za kifedha kwa biashara ndogo na za kati, sekta ya kilimo na wakazi wa vijijini.

Mageuzi haya ya kidijitali, yakienda sambamba na kuimarishwa kimkakati kwa taasisi za fedha za maendeleo na kukuza ikolojia ya upatikanaji wa mitaji ya ubia, yatasaidia kuelekeza uwekezaji wa muda mrefu katika ujenzi wa mahitaji ya msingi ya ukuaji wa uchumi na ujenzi wa uchumi wa viwanda. Kadhalika, kuimarisha masoko ya mitaji, kupanua wigo wa huduma za bima, sanjari na kuendesha programu za elimu ya fedha kitaifa, kutajenga uwanda wa huduma za kifedha ulio stahimilivu, jumuishi na wa kisasa zaidi.

Mageuzi haya ya kina hayatasaidia tu kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji wenye tija, bali pia yatahakikisha kuwa matokeo ya ukuaji wa uchumi yanawafikia watu wengi zaidi katika jamii, na hivyo kuimarisha msingi wa mapato ya Taifa katika kufikia azma ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu. Kiambatisho I (3.3.7) kinaonesha kwa kina, afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.7) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta.

*Jedwali 3.10: Viashiria vya Mwenendo wa Sekta ya Fedha*

| Viashiria vya Matokeo | Halisia (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Kiwango cha kutosheleza mtaji (%) | 19.3 (2024) | ≥16.5 |
| Kiasi cha amana kwa pato la Taifa (%) | 27.3 (2024) | ≥40 |
| Kiwango cha mikopo chechefu (%) | 3.3 (2024) | ≤5 |
| Uwiano wa amana za kidijitali kwa pato la Taifa (%) | 27.2 (2024) | ≥50 |
| Kiwango cha watu wazima wanaopata huduma za kifedha (%) | 50 (2024) | ≥68 |
| Msingi wa mtaji wa taasisi za kifedha (% ya pato la Taifa) | 0.4 (2024) | ≥1.25 |
| Kiwango cha mikopo chechefu ya taasisi za fedha (%) | 11.4 (2025) | ≤6.6 |
| Uwiano wa mikopo ya taasisi za fedha kwa pato la Taifa (%) | 22.5 (2024) | ≥35 |
| Kuenea kwa bima (% ya pato la Taifa) | 2.08 (2023) | ≥2.6 |
| Matumizi ya huduma za kidijiti katika taasisi za kifedha (%) | 55 (2024) | ≥36 |
| Idadi ya watu (%) wanaoishi vijijini wanaopata huduma katika taasisi ndogo za kifedha | 19 (2023) | ≥80 |
| Biashara ndogondogo na za wastani zenye mikopo hai kutoka wakopeshaji rasmi (%) | 19 (2023) | ≥40 |
| Ushirikishwaji wa kifedha (% watu wazima) | 72 (2023) | 85.26 |

### 3.3.8 Sekta ya Michezo, Sanaa na Ubunifu

**Hali Ilivyo:** Sekta ya michezo, sanaa na ubunifu ni miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi zaidi kiuchumi nchini Tanzania. Sekta hizi zina nafasi muhimu katika kuleta mageuzi yatakayowawezesha vijana kiuchumi, kukuza ubunifu na kujenga taswira chanya ya Taifa ulimwenguni. Katika mwaka 2024, sekta ilikua kwa asilimia 17.7, kiwango kilichozidi sekta nyingi za huduma. Ukuaji huu ulichangiwa na mafanikio ya muziki wa Tanzania katika soko la kimataifa, kukua kwa kasi kwa tasnia za filamu na mitindo, pamoja na mafanikio katika michezo kama soka, netiboli na masumbwi. Kutokana na ukweli kwamba asilimia 37 ya Watanzania ni vijana, sekta hizi zina fursa kubwa ya kuzalisha ajira, kulea vipaji, na kupanua ushiriki katika masoko ya ndani na nje.

**Changamoto:** Licha ya fursa kubwa zilizopo, ukuaji wa sekta hii bado unakabiliwa na vikwazo vya miundombinu isiyotosha na iliyopitwa na wakati, upatikanaji mdogo wa fedha, uratibu dhaifu wa kitaasisi, uwezo mdogo wa ushindani katika masoko, na usimamizi dhaifu wa haki miliki. Kuendelea kwa changamoto kama wizi wa kazi za sanaa, kutorasimishwa kwa baadhi ya kazi za sanaa na ubunifu, na matumizi hafifu ya mifumo ya kidijitali katika biashara ya kazi hizo kunaendelea kuathiri wasanii na watayarishaji. Aidha, udhaifu wa usimamizi na uzoefu mdogo wa ushiriki katika masoko ya kimataifa vinakwamisha maendeleo ya sekta, hususan mashirikisho ya michezo na taasisi za ubunifu.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Mpango huu unatambua sekta za michezo, sanaa na ubunifu kuwa vichocheo muhimu vya kukuza mseto wa uchumi, kuongeza fursa za ajira, na kuimarisha utambulisho wa Taifa, ikiwa msukumo utawekwa katika kukuza biashara, weledi na upatikanaji wa mapato kutokana na kazi za ubunifu. Kwa msingi huu, Mpango umebainisha afua kadhaa za kipaumbele ambazo kwa pamoja zinalenga kujenga minyororo jumuishi ya thamani kupitia uwekezaji katika miundombinu, maendeleo ya

vipaji, mifumo ya fedha na biashara ya kazi za ubunifu. Lengo la afua hizi ni kuanzishwa kwa jukwaa la kitaifa la kukuza vipaji vya michezo na ubunifu, likijumuisha uwanja wa michezo wa kisasa na miundombinu mingine itakayokuwa msingi wa mradi huo. Aidha, jukwaa hilo litajumuisha uwanja wa michezo wa kiwango cha kimataifa, kituo cha sayansi ya michezo, vyuo bora na vya kisasa vya kuwajengea uwezo walimu wa michezo na waamuzi, pamoja na maeneo ya kibiashara yatakayosaidia kukuza utalii wa michezo, uandaaji na uendeshaji wa utalii wa matukio, na kujenga taswira ya kitaifa. Kukamilika kwa uwekezaji huu mkubwa kutaenda sambamba na ujenzi wa vyuo vya kikanda vya vijana vya kukuza vipaji na kituo cha kitaifa cha michezo ya ubora wa juu na ubunifu. Miradi hii ya kimkakati itasaidia kukusanya vijana kutoka kanda zote, kutoa mafunzo na ushauri, na kufikia angalau wanamichezo na wabunifu 100,000 ifikapo mwaka 2031. Hivyo, utawekwa msingi wa mtandao wa kitaifa wa vipaji ulio imara na shirikishi.

Hatua hizi zinapaswa kuambatana na uboreshaji wa mfumo wa usajili wa waandaaji maudhui ya kidijitali, ulinzi wa hakimiliki, na ukuzaji wa ushirikiano na majukwaa ya kimataifa ya kidijitali. Hatua hizi zitawezesha wabunifu kuongeza mapato yanayotokana na kazi zao, kukabiliana na wizi wa kazi za sanaa na ubunifu, na kuwafikia watazamaji na wasikilizaji wa kimataifa. Kwa kuweka mazingira rafiki yatakayovutia uwekezaji wa sekta binafsi na kulea ujasiriamali kupitia viatamizi na vichapuzi vya biashara, fursa nyingi zaidi za biashara zitafunguka. Mwelekeo huu hautachochea tu ajira na ukuaji wa pato la taifa, bali pia utaimarisha utambulisho wa tamaduni za Tanzania na kukuza hadhi yake kama kitovu cha michezo na ubunifu. Kiambatisho I (3.3.8) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.8) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta.

*Jedwali 3.11: Viashiria vya Mwenendo wa Maendeleo ya Sekta ya Michezo, Sanaa na Ubunifu*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Ukuaji halisi wa sekta (%) | 17.7 (2024) | ≥20 |
| Idadi ya wanamuziki Watanzania wanaopata tuzo za kimataifa | 10 (2023/24) | ≥15 |
| Idadi ya wadau wa filamu wanaopata tuzo za kimataifa | 86 (2024) | 133 |
| Idadi ya miradi ya filamu iliyopata mikopo | 152 (2024) | 228 |
| Sehemu ya maudhui yanayopatikana kupitia majukwaa ya kidijitali ya kimataifa (%) | <20 (2024 makadirio) | ≥10 |
| Sehemu ya taasisi za michezo, burudani na ubunifu zinazopata mrabaha (%) | Wastani wa chini, <20 (2024 Makadirio.) | ≥20 |

### 3.3.9 Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo

**Hali Ilivyo:** Tanzania imepiga hatua muhimu katika sekta ya nyumba, makazi, ardhi na majengo. Mafanikio hayo yamechochewa na kasi ya ukuaji wa miji, ongezeko la uwekezaji katika miundombinu, kuimarika kwa usimamizi wa ardhi, na kupanuka kwa afua za ujenzi. Sekta hii imeendelea kuwa kichocheo muhimu cha ujenzi wa viwanda, maendeleo ya miji na uzalishaji wa ajira. Mwaka 2024, mchango wa sekta hii katika pato la taifa ulifikia asilimia 2.7. Mafanikio yaliyopatikana yalijumuisha kuboreshwa kwa utoaji wa leseni za makazi katika maeneo yasiyopangwa, kuanzishwa na kuimarishwa kwa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya, pamoja na kuongezeka kwa maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi. Aidha, kumekuwa na maendeleo katika upimaji

na uchoraji wa ramani, ugawaji wa viwanja, na upatikanaji wa huduma za jamii na miundombinu katika maeneo yaliyopimwa. Kadhalika, juhudi za taasisi kama vile Shirika la Nyumba la Taifa, Wakala wa Majengo Tanzania, vyama vya ushirika vya nyumba na Kampuni ya Kufadhili Rehani Tanzania zimechangia kupanua upatikanaji wa nyumba nafuu, kuendeleza soko la mikopo ya nyumba, na kuweka msingi wa upatikanaji wa makazi yaliyopangwa, yanayofaa kuishi na yanayostahimili mabadiliko ya tabianchi.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio yaliyopatikana, changamoto za kimuundo bado zinaendelea kudhoofisha ufanisi wa sekta hii. Hii inajumuisha upungufu wa takribani nyumba milioni 3.8, pamoja na ukuaji wa haraka wa miji unaozidi kasi ya upangaji wa matumizi ya ardhi, upatikanaji wa viwanja vilivyopimwa na kupatiwa huduma na miundombinu ya msingi. Vilevile, ukosefu wa mikopo ya muda mrefu na nafuu, gharama kubwa za ujenzi, pamoja na matumizi hafifu ya mifuko ya uwekezaji wa majengo, mifumo isiyoratibiwa ya usajili wa ardhi, na mlolongo mrefu wa taratibu za umilikishwaji yameendelea kukwamisha uwekezaji na upatikanaji wa majengo. Makazi holela na umiliki wa ardhi usio rasmi bado ni changamoto kubwa zinazodhoofisha ukuaji wa miji iliyopangwa, uhakika wa milki na uendelevu wa kimazingira. Kadhalika, mwingiliano wa majukumu ya taasisi zinazoshughulikia masuala ya ardhi, nyumba na fedha unaendelea kudhoofisha uratibu wa sekta. Vilevile, usimamizi dhaifu wa kanuni za ujenzi, matumizi madogo ya teknolojia endelevu za ujenzi, pamoja na uwepo wa vihatarishi kama vile mafuriko, mmomonyoko wa ardhi na ukame vinaendelea kuathiri upatikanaji wa makazi yaliyopangwa na yanayostahimili majanga pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inapaswa kutekeleza mageuzi jumuishi ya sekta ya nyumba, makazi ya watu na milki kwa kuimarisha usimamizi wa ardhi, kupanua upatikanaji wa fedha za ujenzi wa nyumba, na kuharakisha maendeleo ya miji iliyopangwa. Kipaumbele kiwekwe katika kulinda haki miliki za ardhi, kuratibu mifumo ya umiliki, kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali katika umilikishaji wa ardhi na miamala, pamoja na kuongeza upatikanaji wa ardhi iliyopimwa, iliyohudumiwa na iliyopangwa vizuri. Nchi inapaswa pia kuimarisha taasisi za fedha za nyumba, kupunguza gharama za mikopo ya nyumba, kuongeza matumizi ya masoko ya mitaji kupitia dhamana za uwekezaji katika majengo, na kuhamasisha matumizi ya teknolojia nafuu za ujenzi pamoja na upatikanaji wa vifaa vya ujenzi vinavyozalishwa nchini ili kuharakisha upatikanaji wa nyumba nafuu. Sambamba na hilo, maendeleo ya miji ya kisasa yatakayoimarisha upatikanaji wa usafiri wa umma, maeneo ya biashara na vituo vya ugavi yaharakishwe ili kuelekeza ukuaji wa miji iliyopangwa, inayostahimili mabadiliko ya tabianchi na yenye ufanisi, na hivyo kuondokana na makazi na miji holela. Kiambatisho I (3.3.9) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.9) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta.

*Jedwali 3.12: Viashiria vya Mwenendo wa Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mchango (%) wa sekta ya upangishaji majengo kwa pato la taifa | 2.6 (2024) | 3.4 |
| Idadi ya nyumba | 13,907,951 (2022) | 17,659,090 |
| Uwiano wa mikopo ya nyumba kwa pato la taifa (%) | 0.5 (2025) | 2 |
| Uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi, miji ya kisasa, kongani za biashara na vitovu vya usafirishaji (USD Bilioni) | 1 (2025) | 3 |

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Thamani ya mali chini ya dhamana ya uwekezaji katika majengo na mfuko wa nyumba nafuu (USD Bilioni) | USD Bilioni 1 (2025) | USD 1.5 |
| Mchango wa matumizi ya majukwaa ya kidijiali katika miamala ya upangishaji majengo (%) | 10 (2025) | 50 |
| Eneo la ardhi iliyopimwa (%) | 36 (2025) | 53.3 |
| Idadi ya nyumba zilizorasimishwa katika makazi yasiyopangwa | 3,347,275 (2025) | 5,584,224 |
| Idadi ya leseni za makazi zilizotolewa kwa wenye nyumba katika makazi yasiyopangwa | 25,748 (2025) | 296,295 |
| Eneo la ardhi lenye makazi yasiyorasimishwa (%) | 59 (2025) | 21.0 |
| Eneo la ardhi (Ekari) liliyotengwa na kulindwa kwa ajili ya matumizi ya umma | 988,790 (2023/24) | 1,672,519 |
| Idadi ya mahakama za wilaya za ardhi na nyumba zinazofanya kazi | 117 (2025) | 139 |
| Mikoa yenye mipango kabambe ya matumizi ya ardhi (%) | 81 (2025) | 100 |
| Idadi ya mikoa yenye ramani za msingi | 23 (2023/24) | 26 |
| Idadi ya viwanja vilivyogawiwa | 3,951,890 (2023/24) | 10,318,857 |
| Idadi ya miji yenye mipango ya matumizi bora ya ardhi iliyosasishwa | 26 (2023/24) | 59 |

### 3.3.10 Mageuzi ya Biashara na Shughuli za Kibiashara

**Hali Ilivyo:** Sekta ya biashara na shughuli zinazohusiana nayo ni mhimili muhimu wa mabadiliko ya muundo wa uchumi wa Tanzania, ikichochea ukuaji wa uchumi wa viwanda, uzalishaji wa ajira, na kuimarisha utangamano wa kikanda. Katika muongo mmoja uliopita, sekta hii imepata kasi kutokana na kuimarika kwa mfumo wa soko huria, utekelezaji wa mikataba ya biashara ya kikanda, na uwekezaji katika miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi. Mwelekeo huu umechagiza kuongezeka kwa biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, na hivyo kupanua fursa za masoko kwa bidhaa na huduma za ndani. Kufuatia utekelezaji wa Mpango wa Tatu, mafanikio yaliyopatikana yanajumuisha ongezeko la mauzo ya nje, kuboreshwa kwa mseto wa bidhaa zisizo za asili, na kuimarika kwa ushiriki katika masoko ya kikanda. Mafanikio haya yameimarisha uhusiano wa kisekta, kuchochea uzalishaji wa ajira, na kuthibitisha nafasi ya kimkakati ya sekta ya biashara katika kufanikisha ukuaji jumuishi na shindani wa uchumi.

**Changamoto:** Licha ya hatua zilizopigwa, vikwazo kadhaa vya kimuundo na kitaasisi bado vinaendelea kujitokeza. Mauzo ya nje yameendelea kutegemea bidhaa chache ghafi, ambapo dhahabu ilichangia takribani asilimia 40 ya jumla ya mapato ya mauzo ya nje katika mwaka 2023/24. Aidha, mchango wa mauzo ya bidhaa za viwandani umebaki chini ya asilimia 20, hali inayoashiria ufinyu wa shughuli za kuongeza thamani na mseto wa bidhaa na huduma zinazouzwa nje. Vilevile, miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi isiyotosheleza, gharama kubwa za miamala ya mauzo, pamoja na taratibu zisizo na ufanisi za forodha vinaendelea kudhoofisha ushindani katika masoko. Wakati huohuo, ukubwa wa uchumi usio rasmi na upatikanaji hafifu wa mitaji yenye riba

nafuu vinakwamisha ukuaji wa biashara ndogo na za kati. Aidha, ushiriki mdogo katika minyororo ya thamani ya kimataifa, unaotokana na changamoto ya miundombinu ya biashara ya kidijitali, pamoja na mwingiliano wa kanuni na taratibu za udhibiti na urekebu una athiri zaidi tija ya uzalishaji, hususan kwa wanawake na vijana wajasiriamali.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Sekta ya biashara ina nafasi kubwa ya mageuzi ili kuondokana na utegemezi wa mauzo ya bidhaa ghafi na kuelekea katika mfumo shindani unaotumia teknolojia ya kidijitali na kushiriki kikamilifu katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa. Kwa kutumia kikamilifu fursa za usindikaji wa mazao ya kilimo, matumizi ya madini yanayohitajika katika uzalishaji wa bidhaa muhimu za viwandani, pamoja na uwekezaji adilifu katika utafiti na maendeleo, Taifa litaweza kubadilisha muundo wa biashara ya nje na kupunguza utegemezi wa mauzo ya malighafi. Hivyo, nchi itaongeza kwa kiasi kikubwa thamani ya bidhaa na kuzalisha ajira nyingi zaidi zenye staha. Mabadiliko hayo yanapaswa kuambatana na usasishaji wa sekta ya usafirishaji na uchukuzi, pamoja na matumizi ya akili unde na mifumo ya kidijitali katika biashara na usimamizi wa miamala. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya kisasa utapunguza gharama, kurahisisha taratibu za forodha, na kuiwezesha nchi kufikia viwango vya kimataifa vya utendaji katika usafirishaji na uchukuzi. Kadhalika, ujenzi wa majukwaa ya kisasa ya biashara mtandao na mifumo ya malipo ya kidijitali utaimarisha nafasi ya Tanzania katika biashara ya kikanda na kimataifa. Mwelekeo huu wa kutumia teknolojia utaimarisha ustahimilivu wa sekta na ushirikiano wa kimataifa, na kuhakikisha ukuaji jumuishi kwa kuwezesha ushiriki wa wafanyabiashara ndogo na za kati, wanawake na vijana katika minyororo ya thamani ya kikanda na kimataifa. Kiambatisho I (3.3.11) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.11) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa biashara.

*Jedwali 3.13: Viashiria vya Mwenendo wa Biashara*

| Viashiria vy a Matokeo | Mwanzo (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Thamani ya mauzo nje kwa pato la taifa (%) | 17 (2023) | 25 |
| Mchango wa Tanzania kwenye biashara baina ya nchi wanachama (%) | 13 (2023) | 25 |
| Biashara ndogondogo na za kati zinazotumia majukwa ya kibiashara ya kielektroniki (%) | 15 (2023) | 60 |

### 3.3.11 Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi

**Hali Ilivyo:** Sekta binafsi ya Tanzania imeendelea kuwa nguzo ya mageuzi ya kiuchumi, ukuzaji wa fursa za ajira na uongezaji wa kipato kwa wananchi, na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda na kuongeza ushindani katika masoko. Katika kipindi cha muongo uliopita, mageuzi katika biashara, uwekezaji na ujasiriamali yameongeza mchango wa sekta binafsi katika uchumi. Kati ya mwaka 2015 na 2025, sekta hii ilichangia wastani wa asilimia 75 ya pato la Taifa na asilimia 70 ya mitaji mipya. Aidha, biashara ndogo na za kati zimeendelea kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi na uzalishaji wa ajira. Mafanikio haya, sambamba na mageuzi katika mfumo wa taasisi za udhibiti na urekebu, yamepanua wigo wa ushiriki katika biashara na kuimarisha mazingira ya maendeleo ya sekta binafsi.

**Changamoto:** Licha ya maendeleo yaliyofikiwa, sekta binafsi bado inakabiliwa na vikwazo vya kimfumo vinavyodhoofisha ushindani katika soko. Kwa kiasi kikubwa, ukuaji wa biashara na shughuli zinazohusiana bado unategemea zaidi matumizi ya mitaji iliyopo kuliko ubunifu na ongezeko la tija ya uzalishaji. Gharama za kutimiza matakwa ya kisheria

bado ni kubwa. Aidha, bado kuna changamoto katika kuimarisha mfumo wa udhibiti na urekebu pamoja na mfumo wa kisheria, ikiwemo uratibu wa majukumu ya taasisi na usimamizi wa sera na sheria, hali inayosababisha ucheleweshaji wa urasimishaji wa biashara. Biashara ndogo na za kati zinakabiliwa na uwezo mdogo wa usimamizi, matumizi hafifu ya teknolojia, na ushiriki mdogo katika minyororo ya thamani. Hali hii inachangiwa na ugumu wa upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na vyanzo bunifu vya fedha, hususan kwa wanawake na vijana wajasiriamali. Vilevile, matumizi madogo ya mifumo ya kidijitali, miundombinu hafifu ya usafirishaji na uchukuzi, pamoja na taratibu za usajili zenye mlolongo mrefu na mifumo isiyoridhisha ya utatuzi wa migogoro ya kibiashara vinaendelea kudhoofisha mazingira ya biashara. Aidha, kupungua kwa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje tangu kipindi cha UVIKO-19 kumeendelea kupunguza uwezo wa biashara kujipanua katika masoko mapya.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ina nafasi kubwa ya kufanya mageuzi ya kimkakati katika sekta binafsi ili kuondokana na utegemezi wa matumizi ya kawaida na kuelekeza rasilimali katika ubunifu, ufanisi na ushiriki mpana zaidi katika biashara ya kimataifa. Kwa kufanya mapitio ya kina ya mfumo wa taasisi, udhibiti na urekebu, Taifa litaweza kupunguza gharama za kutimiza masharti, kurahisisha taratibu za kisheria, kutoa motisha kwa wafanyabiashara, na kujenga mazingira ya biashara yanayokidhi viwango vya kimataifa. Hatua hizi pia zitasaidia kurejesha mwelekeo chanya wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Mazingira haya yaliyoboreshwa, yakiambatana na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu na teknolojia za kidijitali, yatafungua uwezo wa biashara ndogo na za kati, kuziwezesha kujiunga na minyororo ya thamani ya kimataifa, na kuchochea ukuaji wa kampuni changa za teknolojia. Vilevile, Taifa linapaswa kuweka kipaumbele katika viwanda vinavyotumia nguvu kazi kwa wingi, hususan katika mikoa iliyo nyuma kiuchumi. Sambamba na hilo, ni muhimu kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji wa kigeni kupitia mifumo ya kisheria na kiutendaji. Hivyo, mageuzi haya yatazalisha ajira kwa wingi, kupunguza tofauti za maendeleo ya kimaeneo, na kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani. Kiambatisho I (3.3.12) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.12) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo wa sekta binafsi.

*Jedwali 3.14:Viashiria vya Mwenendo wa Sekta Binafsi Imara*

| Viashiria vya Matokeo | Halisia (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mikopo kwa sekta bianafsi (TZS Bilioni) | 32,057.6 (2023) | 51,348.03 |
| Mchango wa uwekezaji wa sekta binafsi kwenye pato la taifa – kwa bei za miaka inayohusika (%) | 75 (2024) | 81.3 |
| Mchango wa uwekezaji wa sekta binafsi kwenye rasilimali za kudumu (%) | 70 (2024) | 87.5% |
| Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa mwaka (%) | 15.9 (2024) | 22.4 |
| Idadi ya mashirika ya umma ya kibiashara yanayojiendesha kwa faida (%) | 65 (2023) | 80 |

### 3.3.12 Mikakati ya Ushirikiano kati ya Nchi, Kikanda na Kimataifa katika Dunia Inayobadilika

**Hali Ilivyo:** Katika muongo uliopita, Tanzania imeimarisha ushirikiano wake na nchi mbalimbali, kanda za kiuchumi na jumuiya za kimataifa, na hivyo kuongeza ushiriki wake katika michakato ya utangamano wa kikanda na kimataifa. Ushiriki katika Jumuiya

ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika, Eneo Huru la Biashara la Afrika, pamoja na Mkutano wa Kimataifa wa Kanda ya Nchi za Maziwa Makuu, Jumuiya ya Nchi Zinazopakana na Bahari ya Hindi na Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote, umechangia kukuza biashara, kuimarisha mshikamano, kuvutia uwekezaji na kuratibu sera. Ushiriki huu pia umeimarisha amani, utulivu na upatikanaji wa masoko.

Mwendelezo wa ushirikiano wa Tanzania katika ngazi za kikanda na kimataifa umeimarisha ushindani Tanzania katika medani za kimataifa na kuchochea maendeleo ya kiuchumi. Aidha, utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kama vile Mji wa Ikolojia ya Bandari na Usafirishaji wa Bagamoyo pamoja na Mfumo wa Usafirishaji Changamani na Kituo Kikuu cha Viwanda vya Kisasa na Uchumi wa Buluu wa Maziwa Makuu, utaendelea kuinua hadhi ya Tanzania kama kitovu kinachochipukia cha usafirishaji, biashara na uchumi wa buluu. Kwa pamoja, jitihada hizi zitaongeza ushawishi wa kidiplomasia wa Tanzania, kuimarisha biashara, na kuinua nafasi yake kikanda katika dunia ya leo inayobadilika kwa kasi.

**Changamoto:** Licha ya maendeleo yaliyopatikana, bado kuna changamoto katika kuondoa vikwazo vya biashara visivyo vya ushuru. Vilevile, juhudi za kuwianisha sera za biashara kati ya ngazi ya kitaifa na kikanda bado zinaendelea kuhitaji kuimarishwa ili kufikia kiwango kinachotarajiwa. Ushiriki wa sekta binafsi ya ndani katika biashara zinazovuka mipaka unabaki kuwa mdogo.

Aidha, bado kuna fursa ya kuimarisha matumizi ya diplomasia ya uchumi katika kukuza uwekezaji, huku mapungufu katika uendelezaji wa miundombinu yakiendelea kuathiri ushindani katika masoko. Tanzania pia inakabiliwa na ushindani unaoongezeka kutoka kwa nchi rika, unaochangiwa na changamoto za miundombinu unganishi, kasi ndogo ya matumizi ya mifumo ya kidijitali katika shughuli za bandari, na uratibu unaohitaji kuboreshwa katika taratibu za usafirishaji na uchukuzi. Kwa upande mwingine, kuyumba kwa uchumi wa dunia, mfumuko wa bei na gharama kubwa za mikopo katika masoko ya kimataifa vimepunguza nafasi ya kifedha ya serikali na kuongeza mzigo wa kuhudumia deni. Aidha, utegemezi unaoendelea wa mauzo ya bidhaa ghafi, uhitaji wa kuongeza ubunifu katika kupanua mseto wa mauzo nje, pamoja na kasi ndogo ya matumizi ya teknolojia za kijani na kidijitali, vinaendelea kuathiri uwezo wa nchi kushiriki kikamilifu katika mfumo mpya wa biashara ya kimataifa unaozingatia uzalishaji wenye viwango vya chini vya kaboni.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ina nafasi kubwa ya kuimarisha hadhi yake kidiplomasia na kiuchumi katika jukwaa la kimataifa kwa kutumia vyema rasilimali zake za kijiografia na kiutamaduni, sambamba na kujenga uchumi imara na stahimilivu. Hii inahitaji kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, kutumia kikamilifu ofisi na shughuli za kidiplomasia katika kutangaza biashara na uwekezaji, pamoja na kuendesha kampeni za kuitangaza Tanzania kimataifa.

Aidha, ni muhimu kuchukua hatua mahsusi za kusasisha miundombinu ya biashara, usafirishaji na uchukuzi. Kwa kuwekeza katika bandari za kisasa, matumizi ya akili unde, mifumo ya kidijitali ya biashara na usimamizi wa kanzidata, pamoja na nyenzo za kisasa za kidiplomasia, Tanzania itaongeza ushindani na ushiriki wake katika minyororo ya thamani ya kimataifa.

Vilevile, hatua hizi zitasaidia kuimarisha ushawishi wa Tanzania katika medani za kimataifa. Kiambatisho I (3.3.13) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.13) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo katika ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

*Jedwali 3.15: Viashiria vya Mwenendo wa Ushirikiano wa Kimkakati Kati ya Nchi, Kikanda na Kimataifa*

| Viashiria vya Matokeo | Halisia (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Hisa za uwekezaji binafsi wa nje (USD Milioni) | 23,042.5 (2023) | 38,588.00 |
| Hisa za uwekezaji binafsi wa nje wa moja kwa moja (USD Milioni) | 19,139.6 (2023) | 28,752.53 |
| Hisa za uwekezaji wa nje (USD Milioni) | 204.3 (2023) | 659.00 |

### 3.3.13 Urasimishaji wa Uchumi na Usimamizi Wake

**Hali Ilivyo:** Uchumi usio rasmi ni mpana na una mchango mkubwa katika maisha ya watu wengi nchini. Hata hivyo, hali hii inaendelea kuathiri ongezeko la tija, kupunguza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, na kudhoofisha ukuaji jumuishi wa uchumi. Sekta zisizo rasmi zimejikita zaidi katika kilimo, biashara, ujenzi na uzalishaji wa viwanda vidogo, na kwa ujumla huchangia kati ya asilimia 72 hadi 80 ya ajira zote. Kwa mujibu wa Utafiti wa Nguvukazi watu wa mwaka 2020/21, sekta isiyo rasmi inachangia asilimia 28.7 ya ajira kwa Tanzania Bara na asilimia 41.7 kwa Zanzibar. Wanawake na vijana ni sehemu kubwa ya kundi hili. Ingawa sekta hii inachangia kipato cha kaya nyingi, bado inaendelea kuathiri juhudi za ukusanyaji wa kodi, ujumuishi wa kifedha na upanuzi wa kinga ya jamii. Miongoni mwa sababu kuu za kuendelea kwa shughuli za sekta isiyo rasmi ni taratibu tata za usajili, ugumu wa kufikia masoko, na udhaifu wa uratibu wa mfumo wa taasisi.

**Changamoto:** Kuendelea kuwepo kwa sekta isiyo rasmi kunachangiwa na ugumu wa taratibu za usajili na upatikanaji wa leseni za biashara, changamoto katika usimamizi wa kanuni na taratibu, uelewa mdogo wa masuala ya kifedha, na fursa finyu za upatikanaji wa mikopo. Mara nyingi, biashara zisizo rasmi hukosa uwezo wa kukidhi matakwa ya kisheria, hivyo hushindwa kufikia mifumo rasmi ya kibenki na kuendeshwa bila kinga ya bima. Gharama kubwa za kutimiza masharti ya kisheria, pamoja na mwingiliano wa majukumu ya taasisi, hupunguza hamasa ya usajili wa biashara. Vilevile, ukosefu wa vivutio vya kurasimisha shughuli unapunguza utayari wa kufanya hivyo kwa hiari. Kadhalika, mtawanyiko wa taarifa katika taasisi za serikali unakwamisha uratibu wa sera na ufuatiliaji. Matokeo yake, shughuli zisizo rasmi zinaendelea kudhoofisha tija ya nguvukazi watu, kupunguza usawa wa mgawanyo wa mapato, na kuathiri usimamizi wa fedha za umma. Hali hii inapunguza uwezo wa serikali kupanua wigo wa mapato na kuharakisha mabadiliko ya muundo wa uchumi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kwa kuzingatia changamoto zilizobainishwa, Tanzania ina nafasi kubwa ya kubadilisha sekta isiyo rasmi kutoka shughuli za kujikimu na kuifanya kuwa chanzo rasmi cha ukuaji na ongezeko la tija. Kwa kupunguza vikwazo vya kiutawala na kifedha vinavyokwamisha biashara, Taifa linaweza kuunganisha biashara mbalimbali katika mkondo wa uchumi rasmi. Hatua hii itapanua kwa kiasi kikubwa wigo wa mapato na kuimarisha uwezo wa mifumo ya kinga ya jamii. Mabadiliko haya yanahitaji kuanzishwa kwa mifumo ya kidijitali ya usajili chini ya taasisi moja, utoaji wa motisha zinazolenga biashara mahsusi, pamoja na utekelezaji wa programu za kuinua ujuzi. Hivyo, yatawezesha kuwepo kwa mazingira bora, yenye usawa na ufanisi zaidi wa biashara.

Aidha, biashara zisizo rasmi zinapopata fursa ya kuingia katika minyororo rasmi ya ugavi, kupata mikopo na ulinzi wa kisheria, zitakua na kupanuka. Maendeleo haya yatazalisha ajira zenye ubora na staha na kuongeza mchango wake katika azma ya

Tanzania ya kujenga uchumi wa viwanda, kukuza uchumi jumuishi na usetushaji wa uchumi, pamoja na uendelevu. Kiambatisho I (3.3.14) kinaonesha kwa kina afua na mpangilio wa utekelezaji, wakati Kiambatisho II (3.3.14) kinaonesha mfumo wa viashiria vya mwenendo  wa urasimishaji wa uchumi na uendeshaji wake.

*Jedwali 3.16:Viashiria vya Mwenendo  wa Urasimashaji wa Uchumi na Uendeshaji Wake*

| Viashiria vya Matokeo | Mwanzo (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mchango wa sekta isiyo rasmi kwenye pato la taifa (%) | 55 (2023) | 29 |
| Kiwango cha ajira katika sekta isiyo rasmi (%) | 94.6 (2024) | 81.00 |

### 3.4 Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu na Maendeleo ya Jamii

Mpango umeweka kipaumbele katika kukuza uwezo wa rasilimali watu na kuimarisha maendeleo ya jamii kama misingi ya kufikia Taifa lenye ustawi, jumuishi na la haki. Unalenga katika kuandaa nguvukazi iliyoelimika, yenye ari na ujuzi wa kufanya kazi, inayotumia kikamilifu fursa za kidemografia na kushughulikia mapungufu ili kuendana na mahitaji ya soko na hivyo kuongeza fursa za ajira. Vilevile, Mpango unalenga kuimarisha mifumo ya kinga ya jamii, huduma za afya, nyumba na makazi, maji safi na salama pamoja na usafi wa mazingira ili kuboresha maisha. Aidha, unatilia mkazo mshikamano, uwajibikaji na ushiriki wa jamii kupitia maendeleo jumuishi vijijini na mageuzi ya ushirika. Lengo kuu ni kuongeza tabaka la kipato cha kati, ambalo ni muhimu katika kuhakikisha utulivu wa uchumi, kuinua ustawi wa jamii na kujenga Taifa endelevu.

#### 3.4.1 Jamii Iliyoelimika, Yenye Ujuzi na Inayojifunza

**Hali ilivyo:** Elimu na maendeleo ya ujuzi ni mhimili wa mageuzi ya uchumi. Maendeleo katika sekta hii yatachochea ujenzi wa uchumi shindani, unaosukumwa na matumizi ya maarifa na hivyo kuchochea uzalishaji nchini. Katika Muongo uliopita, Taifa limepata mafanikio makubwa katika kuandikisha wanafunzi katika ngazi zote za elimu, kuboresha uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi, kuongeza fursa za kujiunga na elimu ya juu na kuimarisha upatikanaji wa elimu ya awali na huduma za makuzi na malezi kwa watoto. Mafanikio zaidi yalifikiwa katika nyanja za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kupitia ufadhili mahsusi, ruzuku na hatua za kupanua uwezo wa taasisi husika. Licha ya mafanikio haya, bado kuna utofauti katika viwango vya ubora wa elimu inayotolewa, hususan kwa maeneo ya vijijini. Aidha, ukosefu wa miundombinu ya kutosha, mgawanyo wa walimu na uwianifu wa matokeo ya mafanikio ya upatikanaji wa elimu na mahitaji ya soko la ajira.

**Changamoto:** Changamoto kadhaa za kimuundo na kimfumo zinaendelea kuathiri azma ya Taifa ya kujenga nguvukazi iliyoelimika na yenye ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira. Kukosekana kwa usawa wa huduma za malezi na makuzi katika elimu ya awali kunakoathiri utayari wa ujifunzaji wa watoto na mgawanyo usio sawa kati ya walimu wenye sifa na wanafunzi. Vilevile, miundombinu duni, matumizi hafifu ya teknolojia ya kidijitali na ukosefu wa huduma ya mtandao ya uhakika vinakwamisha ufundishaji na ujifunzaji.

Aidha, uwiano kati ya ujuzi na mahitaji ya soko la ajira unaendelea kuathiri muunganiko kati ya mkondo wa elimu na shughuli za uzalishaji, pamoja na msisitizo mdogo wa mafunzo kwa vitendo. Vilevile, kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika ngazi za elimu ya sekondari na elimu ya juu na uwekezaji mdogo katika utafiti na ubunifu vinadhoofisha kasi ya uzalishaji na matumizi ya maarifa. Mgawanyo usio sawa wa walimu, hasa katika

masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati na matumizi finyu ya teknolojia za kisasa katika ufundishaji na usimamizi wa elimu vinachangia kwa kiasi kikubwa tofauti baina ya maeneo katika matokeo ya elimu ya jumla.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Ili kufikia shabaha ya uchumi unaoongozwa na maarifa, mfumo wa elimu nchini unapaswa kuendana na mahitaji ya maendeleo ya Taifa katika muktadha wa uchumi wa kisasa na uchumi wa viwanda. Ili kufikia azma hii kuna haja ya kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za malezi na makuzi ya watoto na elimu bora ya awali kwa wote ili kuimarisha maandalizi yao ya kielimu na maisha. Kupitia uwekezaji wa kimkakati katika maendeleo ya walimu, hususan katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati, pamoja na kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa kutumia zana za kidijitali na miundombinu ya kisasa, taifa linaweza kuandaa nguvukazi yenye ujuzi wa hali ya juu, inayokidhi mahitaji ya teknolojia, uzalishaji na soko la ajira.

Aidha, kwa kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi ya elimu na viwanda; kukuza utamaduni wa kufanya tafiti; pamoja na kuchochea ubunifu na maendeleo ya teknolojia, nchi itapunguza pengo la ujuzi, kuwawezesha vijana na kujiimarisha kama kitovu cha kikanda cha maarifa na teknolojia, hivyo kuchochea ustawi jumuishi na endelevu. Kiambatisho I (3.4.1) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.1) kinaonesha mfumo wa viashiria muhimu vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.17: Viashiria vya Utendaji vya Jamii Iliyoelimika, Yenye Ujuzi na Inayojifunza*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| **Elimu ya Awali** | | |
| Uandikishaji wa jumla (%) | 89.5 (2024) | 100.0 |
| Uwiano halisi wa uandikishaji (asilimia ya watoto wenye umri wa miaka 5 waliopata elimu ya awali) | 51.2 (2024) | 100.0 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa | 105:1 (2024) | 40:1 |
| **Elimu ya msingi** | | |
| Uandikishaji wa jumla (%) | 98.2 (2023) | 100.0 |
| Uwiano halisi wa uandikishaji (asilimia ya wanaostahili) | 81.7 (2022) | 100.0 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu | 61:1 (2024) | 53:1 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa kitabu | 3:1 (2024) | 1:1 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa darasa | 63:1 (2024) | 50:1 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa choo (wavulana) | 42:1 (2023/24) | 25:1 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa choo (wasichana) | 39:1 (2023/24) | 20:1 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa dawati | 4:1 (2023/24) | 2:1 |
| Asilimia ya shule zenye maji safi (%) | 54 (2023/24) | 66.0 |
| Asilimia ya shule zenye umeme (%) | 48 (2023/24) | 66.0 |
| Kiwango cha kumaliza masomo (%) | 80 (2024) | 95.0 |
| Kiwango cha kuacha shule (%) | 6.2 (2024) | 1.3 |
| Kiwango cha mpito kutoka Darasa la VII kwenda Kidato cha I (%) | 73.3 (2024) | 100.0 |
| Watoto wenye ulemavu wanaosoma shule ya msingi (%) | 78.6 (2022) | 98.0 |
| **Elimu ya Sekondari Kidato I–IV** | | |
| Uwiano wa uandikishaji wa jumla | 51.7% (2024) | 79.1% |
| Uwiano halisi wa uandikishaji | 43.2% (2022) | 50.0% |

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu (kwa somo) | 26:1 (2024) | 23:1 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa darasa | 63:1 (2024) | 40:1 |
| Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu Mtihani wa Kidato cha IV | 92.37% (2024) | 100.0% |
| Kiwango cha mpito kutoka Kidato cha IV kwenda Kidato cha V | 24.4% (2024) | 29.0% |
| Uwiano wa wanafunzi kwa choo | 28:1 (2023/24) | 20:1 |
| Asilimia ya shule zenye maji safi | 85% (2023/24) | 100.0% |
| Asilimia ya shule zenye umeme | 69% (2023/24) | 100.0% |
| Ongezeko la ufaulu wa Hisabati | 25.4% (2024) | 32.0% |
| Ongezeko la ufaulu wa Sayansi | 79.37% (2024) | 85.0% |
| **Elimu ya Sekondari Kidato V–VI** | | |
| Uwiano wa uandikishaji wa jumla | 9.1% (2024) | 13.0% |
| Uwiano halisi wa uandikishaji | 7.7% (2022) | 18.0% |
| Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu Mtihani wa Kidato cha VI | 7.2% (2022) | 100.0% |
| **Elimu ya Juu** | | |
| Kiwango cha uandikishaji katika elimu ya juu | 5.8% (2023/24) | 7.0% |
| Upatikanaji wa elimu ya juu | 91.7% (2024) | 92.7% |
| Asilimia ya wahitimu wa Sayansi na Hisabati | 19.6% (2024) | 21.0% |
| Idadi ya wanafunzi wenye ulemavu katika taasisi za elimu ya juu | 1,498 (2023) | 6,108 |
| Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo na ufadhili wa masomo ya Sayansi | 229,652 (2024) | 312,235 |
| Asilimia ya mikopo kwa masomo ya Sayansi | 64% (2021) | 70.0% |
| Idadi ya wanataaluma | 6,009 (2023) | 11,854 |
| Asilimia ya wanataaluma wa kike | 30% (2024) | 50.0% |
| Idadi ya wahitimu | 56,520 | 64,998 |
| Idadi ya wahitimu wa kiume | 27,574 | 31,710 |
| Idadi ya wahitimu wa kike | 28,946 | 48,961 |
| **Elimu ya Ufundi** | | |
| Idadi ya wanafunzi katika taasisi za elimu ya ufundi | 217,204 (2024) | 289,605 |
| Asilimia ya wanafunzi wa kike | 49 (2024) | 50.0 |
| Asilimia ya wanafunzi wenye ulemavu | 0.04 (2023/24) | 0.1 |
| Kiwango cha uandikishaji wa jumla (%) | 5.8 (2023/24) | 7.0 |
| Idadi ya wahitimu kwa mwaka | 89,967 (2023/24) | 192,786 |
| Asilimia ya wahitimu wa Sayansi na Uhandisi | 17.2 (2023/24) | 28.0 |
| Asilimia ya wahitimu wa kike | 35.7 (2023/24) | 40.0 |
| Asilimia ya wanafunzi wanaopata mikopo | 1.3 (2024) | 2.0 |
| Idadi ya wakufunzi | 10,948 (2023) | 15,559 |

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya wakufunzi wa kike | 39.5 (2023/24) | 50.0 |
| **Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi** | | |
| Wastani wa wanafunzi wanaojiunga kila mwaka | 415,131 (2023/24) | 1,296,705 |
| Asilimia ya wanafunzi wa kike | 56.80 (2023/24) | 60.0 |
| Asilimia ya wanafunzi wenye ulemavu | 0.2 (2023/24) | 0.33 |
| Idadi ya wakufunzi | 2,723 (2023) | 3,318 |
| Asilimia ya wakufunzi wa kike | 34.0 (2023/24) | 44.0 |
| Uwezo wa kuajirika | | |
| Idadi ya watu waliopata mafunzo kazini (internship) | 30,000 (2021) | 150,000 |
| Idadi ya watu waliopitia programu za uanagenzi | 46,200 (2021) | 231,000 |
| Kiwango cha usomaji kwa vijana % (miaka 15–35) | 87.5 (2022) | 100 |

### 3.4.2 Nguvukazi Yenye Uwezo na Ari

**Hali ilivyo:** Nguvukazi ndiyo mhimili mkuu wa mageuzi ya kiuchumi nchini kwa kuchochea uzalishaji na ukuaji jumuishi. Katika kipindi cha muongo uliopita, kulikuwa na mafanikio katika kuimarisha soko la ajira, kupanua fursa za elimu ya ufundi na mafunzo stadi, pamoja na kukuza uwezo wa wahitimu kuajirika. Ukosefu wa ajira ulipungua kutoka asilimia 11.6 mwaka 2006 hadi asilimia 8.9 mwaka 2020/21. Aidha, ajira kwa watu wenye ulemavu iliongezeka kutoka asilimia 59.1 hadi 63.2. Ingawa fursa za mafunzo zimeongezeka, upungufu wa nguvukazi yenye ujuzi unaohitajika katika maeneo mengi, uhaba wa fursa za kujiendeleza na kukosekana kwa usawa katika upatikanaji wa ajira zenye staha, unaathiri ukuajii wa uchumi. Kadhalika, fursa za ajira bado ni ndogo ikilinganishwa na kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Vilevile, uwepo wa ajira nyingi katika sekta iliyo rasmi na shughuli zenye tija ndogo kama kilimo umeendelea kukwamisha ujenzi wa nguvukazi yenye ujuzi.

**Changamoto:** Kwa ujumla, upatikanaji wa nguvukazi nchini bado unakabiliwa na changamoto za kimuundo na kitaasisi ambazo zinaendelea kudunisha kasi ya ukuaji wenye tija na upatikanaji wa ajira zenye staha. Pengo kati ya ujuzi unaozalishwa na mfumo wa elimu na mahitaji halisi ya soko la ajira hasa katika shughuli za uzalishaji viwandani limeendelea kudhihirika. Upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi yenye ubora kwa gharama nafuu, mifumo hafifu ya uanagenzi na ukosefu wa huduma za ushauri wa fursa za kujiendeleza kitaaluma, vinaathiri utendaji na kuwakosesha vijana sifa ya kuajirika. Ajira katika sekta isiyo rasmi, pamoja na mishahara midogo na ukosefu wa kinga ya jamii vinaongezeka, hasa kwa wanawake na vijana. Mifumo hafifu ya taarifa kuhusu soko la ajira na uratibu duni kati ya watoa mafunzo na waajiri hupunguza ufanisi wa sera na mipango ya maendeleo. Sekta ya umma ina changamoto ya kushindwa kuwabakiza wafanyakazi wenye ujuzi. Kadhalika, sekta binafsi inakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi wenye umahiri wa kiufundi, hali inayodhoofisha ubunifu, ushindani na ukuaji wa uchumi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kujenga nguvukazi yenye ujuzi wa hali ya juu na inayokidhi mahitaji ya ajira kwa siku zijazo. Hili linajumuisha uwiano wa mifumo ya elimu na mafunzo ili kuendana na mahitaji ya sasa ya uchumi wa viwanda. Mabadiliko haya yanahitaji mageuzi ya kimkakati ya muundo na mitaala ya mafunzo ya ufundi na stadi za kazi, kwa kuwianisha na viwango vya kimataifa. Vilevile, ni muhimu mageuzi haya kuhusianishwa na stadi za kidijitali katika ngazi zote za mafunzo ili

kuendana na mahitaji na kuinua ushindani. Kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za elimu na sekta ya uzalishaji kwa kuweka msisitizo wa mafunzo kwa vitendo kwa ubia kati ya sekta za umma na binafsi ni muhimu. Hii itaboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia na hatimaye kuziba pengo la ujuzi katika maeneo muhimu ikiwemo teknolojia na uhandisi. Mbinu hii jumuishi, inazingatia pia ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na kupanua fursa za mafunzo kwa maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo. Mabadiliko haya yatajenga nguvukazi watu yenye uwezo wa kutumia fursa za kiuchumi, kuongeza tija ya uzalishaji, kuchochea ubunifu na kuimarisha ushindani endelevu wa uchumi nchini. Kiambatisho I (3.4.2) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.2) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.18: Viashiria vya Utendaji vya Nguvukazi Yenye Uwezo na Ari ya Kufanya Kazi*

| Viashiria vya Matokeo | Kiwango cha Msingi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya nguvukazi yenye ujuzi wa juu | 3.0(2011) | 12.0 |
| Asilimia ya nguvukazi yenye ujuzi wa kati | 13.0 (2011) | 33.0 |
| Asilimia ya nguvukazi yenye ujuzi wa chini | 84.0 (2011) | 55.0 |

### 3.4.3 Demografia na Idadi ya Watu

**Hali ilivyo:** Mienendo ya demografia nchini Tanzania inaibua fursa ya kihistoria ya kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kutokana na idadi ya watu, ukubwa wa rika la vijana na kasi ya ongezeko la watu wenye elimu na ujuzi. Idadi ya watu inatarajiwa kuongezeka kutoka takribani milioni 61.7 mwaka 2023 hadi takribani milioni 118.1 ifikapo 2050. Uwiano wa watu wa rika la kufanya kazi utaongezeka sanjari na kuanza kupungua kwa kiwango cha uzazi. Mabadiliko haya ya muundo wa kidemografia yanatoa fursa ya kuchochea ukuaji wa uchumi utakaochochea ongezeko la tija. Hii inapaswa kwenda sambamba na uwekezaji wa kimkakati katika elimu, huduma za afya na upanuzi wa fursa za ajira. Viwango vya ujuzi miongoni mwa vijana, ukuaji wa miji na ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi vinaonesha mafanikio chanya. Hata hivyo, fursa hizi hazijatumiwa kikamilifu kutokana na kukosa uwiano kati ya maendeleo ya rasilimali watu, ajira na upatikanaji wa fursa za kiuchumi zenye tija.

**Changamoto:** Ingawa muundo wa kidemografia wa Tanzania unaonesha fursa kubwa, bado kuna vikwazo vya kimuundo vinavyozuia nchi kunufaika kikamilifu na rasilimali watu iliyopo. Idadi kubwa ya vizazi, ukosefu wa ajira kwa vijana na uhaba wa huduma bora za afya ya uzazi vinaongeza utegemezi katika jamii. Pengo kati ya ujuzi unaozalishwa na mfumo wa elimu na mahitaji ya soko la ajira bado ni changamoto. Tofauti za kikanda zinazojitokeza katika ongezeko la watu na ukuaji wa miji zinazidisha shinikizo katika upatikanaji wa miundombinu na huduma za kijamii. Aidha, ukosefu wa usawa wa kijinsia, ndoa za utotoni na ushiriki mdogo wa wanawake katika ajira zenye tija vinapunguza manufaa ya muundo wa kidemografia. Udhaifu wa mifumo ya taasisi inayoshughulikia upangaji wa idadi ya watu; ukosefu wa kinga ya jamii kwa wazee; pamoja na matumizi yasiyoridhisha ya takwimu za kidemografia katika kuongoza sera na mipango ya maendeleo, vinakwamisha jitihada za kutumia demografia na idadi ya watu kuleta manufaa endelevu ya kiuchumi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kubadili changamoto ya wingi wa vijana kuwa mtaji na nyenzo yenye manufaa makubwa kiuchumi. Kwa kuwianisha kwa makusudi, mifumo ya elimu na mafunzo ya ufundi na stadi za kazi na mahitaji halisi ya ujuzi kwa uchumi wa kisasa, taifa linaweza kuandaa kizazi chenye ujuzi, ubunifu na uwezo

wa kuajirika. Mageuzi haya, yakiambatana na kujengwa kwa utamaduni wa ujasiriamali kwa vijana na uunganishaji wa fursa za uchumi wa kidijitali na ajira mtandaoni, yanaweza kuzalisha mamilioni ya ajira zenye staha. Ni muhimu pia kuimarisha usawa wa kijinsia, kuwawezesha wanawake na vijana na kukuza ushiriki wenye tija wa Watanzania waishio ughaibuni ili kuhakikisha mabadiliko ya kidemografia yanawanufaisha wote na kutumia kikamilifu vipaji vya Taifa.

Mkakati huo, ukiambatana na upatikanaji wa huduma bora za afya ya uzazi na mifumo imara ya kinga ya jamii kwa wazee, utaweka msingi wa ukuaji endelevu, jumuishi na ustawi wa pamoja kwa vizazi vijavyo. Kiambatisho I (3.4.3) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.3) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.19: Viashiria vya Kimkakati vya Usimamizi na Manufaa ya Mgawanyo wa Idadi ya Watu*

| Viashiria vya Matokeo | Kiwango cha Msingi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Kiwango cha Utegemezi wa Umri (%) | 87.4 (2025) | 79.4 |
| Kiwango cha Utegemezi kwa Watoto % (miaka 0–14) | 80.5 (2025) | 73.0 |
| Kiwango cha Utegemezi wa Wazee % (miaka 65+) | 6.8 (2025) | 6.4 |

### 3.4.4 Soko na Taratibu za Ajira

**Hali ilivyo:** Soko la ajira nchini Tanzania linaendelea kubadilika kimuundo kutokana na mabadiliko ya muundo wa kidemografia, mseto wa shughuli za kiuchumi na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia za kidijitali. Kwa kuwa zaidi ya asilimia 77 ya wananchi ni vijana wenye umri ulio chini ya miaka 35, Taifa lina fursa ya kunufaika na mwenendo wa muundo wa kidemografia. Hata hivyo, kiasi kikubwa cha ajira, takribani asilimia 94.6 siyo rasmi, hususan kilimo cha kujikimu, biashara na huduma zenye tija ndogo. Ingawa kiwango cha ukosefu wa ajira katika muongo uliopita kilipungua, upatikanaji na ubora wa ajira bado ni changamoto kubwa. Ukubwa wa sekta isiyo rasmi katika uchumi, upatikanaji finyu wa mafunzo ya ufundi na stadi za kazi, na kasi ndogo ya ukuaji wa sekta rasmi, kwa pamoja vinazuia kukua kwa uchumi jumuishi na endelevu.

**Changamoto:** Licha ya kuwa na ukuaji endelevu wa uchumi, soko la ajira nchini linaendelea kukabiliwa na vikwazo vya kimuundo vinavyopunguza ajira zenye staha. Vijana na wanawake wanaathirika zaidi na ajira duni na ajira zisizo rasmi, huku uratibu usiokidhi wa taasisi ukiathiri upangaji na ufuatiliaji wa soko la ajira. Pengo la ulinganifu kati ya elimu na mafunzo dhidi ya mahitaji halisi ya viwanda inasababisha ukosefu wa ajira, hususan katika sekta ya viwanda, TEHAMA, usafirishaji na uchukuzi na utalii. Uwezo mdogo wa mifumo ya kinga ya jamii na usimamizi wa haki za wafanyakazi unapunguza tija. Kadhalika, tofauti za maendeleo kikanda na ukosefu wa usawa wa kijinsia vinapunguza fursa za ajira kwa watanzania. Aidha, udhaifu katika mifumo ya taarifa za masoko ya ajira unadhoofisha maamuzi yanayotegemea ushahidi. Tofauti za kimaeneo katika fursa za ajira na vikwazo vya kijinsia katika ushiriki wa nguvukazi vinaendelea kuzuia mabadiliko ya kiuchumi jumuishi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kufanya mageuzi makubwa katika soko la ajira kwa kupunguza utegemezi wa ajira katika shughuli zisizo rasmi na zenye tija ndogo na kujielekeza kwenye ajira zenye staha na tija kubwa. Hivyo, ni muhimu kuweka mazingira wezeshi ya kukuza biashara changa, ndogo na za kati zinazotumia teknolojia za kisasa. Aidha, ni muhimu kuvutia uwekezaji mkubwa unaotoa ajira nyingi kwa wakati

mmoja kupitia uanzishwaji wa maeneo maalum ya kiuchumi na uteuzi wa sekta mahsusi za kimkakati. Kwa kuwianisha moja kwa moja uendelezaji wa ujuzi na mahitaji halisi ya sekta zenye kasi kubwa ya ukuaji pamoja na kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji wa ubia kati ya sekta za umma na binafsi, taifa litaandaa nguvukazi yenye umahiri na ujuzi unaokidhi mahitaji ya uchumi wa sasa na baadaye. Mkakati huu wa kukuza ujasiriamali wa ndani na kuvutia uwekezaji wa kimkakati kutoka nje, ukiambatana na motisha za kuhamasisha urasimishaji wa biashara, utaongeza ajira, kuboresha muundo wa uchumi na kukuza ushindani wa Tanzania katika masoko ya nje. Kiambatisho I (3.4.4) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.4) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.20: Viashiria vya Soko la Ajira*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Kiwango cha ushiriki wa nguvukazi (%) | 73.2 (2024) | 74.6 |
| Kiwango cha ajira kwa idadi ya watu % | 68.7 (2024) | 71.3 |
| Kiwango cha ukosefu wa ajira % (miaka 15 na zaidi) | 6.2 (2024) | 4.4 |
| Kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana % (miaka 15–35) | 8.3 (2024) | 6.0 |
| Asilimia ya watu wenye ulemavu walioajiriwa | 32.5 (2024) | 40.0 |

### 3.4.5 Jamii Yenye Hifadhi na Muundo Jumuishi

**Hali ilivyo:** Azma ya Tanzania ya kufikia maendeleo jumuishi na endelevu imejikita katika dhana ya kujenga hifadhi ya jamii madhubuti, yenye usawa na mshikamano. Kila mwananchi, hususan walio maskini, makundi yaliyo katika mazingira hatarishi na yaliyoachwa nyuma kimaendeleo, watawezeshwa kunufaika na matunda ya maendeleo ya taifa. Utekelezaji wa Mpango III uliweza kupanua wigo wa hifadhi ya jamii kupitia programu kama Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania, juhudi za kuanzisha bima ya afya kwa wote pamoja na uimarishaji wa mifuko ya pensheni na fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali na ulemavu wakiwa kazini. Ustawi wa jamii na ujumuishaji uliimarishwa kupitia utoaji wa ruzuku za kifedha, usajili wa vituo vya kulelea watoto na utoaji wa huduma za afya bila malipo kwa wazee na wasiojiweza. Mafanikio pia yalionekana katika ongezeko la udahili wa wanafunzi na mahudhurio shuleni, ongezeko la watoto wenye afya bora na kupungua kwa ajira za watoto. Kwa ujumla, mafanikio haya yanaakisi maendeleo yanayotokana na hatua thabiti zilizopigwa katika kuimarisha ustawi, kukuza ustahimilivu wa kijamii na mshikamano wa kitaifa.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio hayo, bado kuna changamoto kubwa zingalipo. Umaskini na kushindwa kukabiliana na vihatarishi kumeendelea kuathiri kaya nyingi, hasa katika maeneo ya vijijini na miongoni mwa wananchi wanaotegemea shughuli zisizo rasmi na zenye tija ndogo. Upatikanaji wa kinga ya jamii na fursa za kiuchumi bado si sawa kwa wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi. Ukatili wa kijinsia, umaskini wa mijini na kuongezeka kwa pengo la kipato vinaathiri mshikamano wa kijamii. Uratibu usioridhisha wa programu za kinga ya jamii, mifumo isiyo imara ya takwimu na rasilimali fedha zisizotosheleza vinapunguza ufanisi na uwezo wa kufikia watu wengi zaidi. Aidha, kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, milipuko ya magonjwa na misukosuko ya kiuchumi kunahatarisha mafanikio yaliyopatikana. Kushughulikia changamoto hizi kutahitaji hatua za moja kwa moja za kuwafikia walengwa, uhakika wa upatikanaji wa fedha, kuimarisha uwezo wa kitaasisi na kuoanisha mifumo kwa kuzingatia matokeo yaliyopatikana katika mifumo ya hifadhi ya jamii, upatikanaji wa ajira, huduma za afya na elimu.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ina nafasi muhimu ya kujenga jamii yenye mshikamano na mfumo thabiti wa hifadhi ya jamii usiomwacha mwananchi yeyote nyuma, kwa kuubadili mfumo huo kutoka programu zilizotawanyika kuwa mfumo jumuishi wa uwezeshaji. Kupitia utekelezaji wa sheria madhubuti za kupinga ubaguzi, kuhakikisha upatikanaji wa ardhi kwa usawa na kuunganisha sekta isiyo rasmi katika mifumo ya kinga ya jamii kwa kutumia teknolojia za kidijitali, Taifa linaweza kuondoa vikwazo vya muda mrefu vinavyozuia ujumuishi wa kijamii na kiuchumi. Mabadiliko kwenda kwenye mifumo ya kisasa ya kinga ya jamii kwa kushirikisha sekta binafsi, msukumo wa kuongeza kipato na shughuli za kujikimu, utaifanya mifumo hiyo isiwe tu kinga dhidi ya maafa, bali pia kuwa nyenzo ya kupunguza umaskini na kukuza uwezeshaji wa kiuchumi kwa njia endelevu. Vilevile, kwa kujumuisha huduma muhimu kama afya ya akili katika mifumo ya elimu na maisha, Tanzania itajenga jamii yenye uthabiti, mshikamano, na uwezo wa kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa kwa hadhi na usawa. Kiambatisho I (3.4.5) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.5) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.21: Viashiria Muhimu vya Kinga ya Jamii na Ujumuishi*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| **Kinga ya Jamii** | | |
| Ongezeko la wigo wa wanufaika wa hifadhi ya jamii % | 28.4 (2023/24) | 42.60 |
| Kiwango cha walio katika mfumo wa bima ya afya (%) | 67.8 (2023/24) | 100 |
| Kiwango cha waliojiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii (%) | 10.1 (2023/24) | 18.1 |
| Asilimia ya vijana wenye ajira hatarishi | 42.4 (2023/24) | 28.8 |
| Kiwango cha watoto wenye ulemavu wanaohudhuria shule ya msingi (%) | 95 (2023/24) | 100 |
| Asilimia ya watoto wenye umri wa miaka 5–17 wanaojihusisha na ajira za watoto | 22 (2023/24) | 0.0 |
| Idadi ya mashauri ya matunzo ya watoto yaliyopatanishwa | 39,560 (2023/24) | 163,905 |
| Idadi ya vituo vya kulelea watoto vilivyosajiliwa | 6,900 (2023/24) | 33,539 |
| Idadi ya wazee wasiojiweza wenye kadi za bima ya afya kwa huduma za matibabu bure ('000) | 268 (2023/24) | 803 |
| **Kinga ya Jamii (viashiria vingine)** | | |
| Asilimia ya ongezeko la wigo wa kinga ya jamii (%) | 28.0 (2023/24) | 43.0 |
| Wigo wa bima ya afya (%) | 15.3 (2023) | 58.0 |
| Wigo wa kinga ya jamii (%) | 10.1 (2023/24) | 18.12 |
| Asilimia ya vijana katika ajira hatarishi | 42.4 (2023/24) | 28.84 |
| Ushirikishwaji wa Kiuchumi | | |
| Asilimia ya kaya wanufaika zinazoshiriki katika vikundi vya akiba vinavyofanya kazi | 42 (2023/24) | 52.5 |
| Idadi ya wanufaika waliopata taarifa kuhusu huduma za uboreshaji maisha | 1,500,000 (2023/24) | 2,674,230 |
| Idadi ya kaya wanufaika wanaostahili waliopata msaada wa kuboresha maisha, ikiwemo mafunzo ya msingi na stadi za kazi, ujuzi na ufadhili wa kujikimu | 155,400 (2023/24) | 414,400 |

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya shughuli za uzalishaji mapato zenye mipango ya biashara iliyoidhinishwa na kuanzishwa ndani ya miezi sita baada ya kupokea ufadhili wa kujikimu | 82.0 (2023/24) | 100.0 |
| Asilimia ya wanachama waliopata mafunzo na kuripoti kuimarika kwa ujuzi kutokana na mafunzo ya yaliyotolewa kupitia Mpango wa Hifadhi ya Jamii wenye Tija | 68.0 (2023/24) | 79.0 |
| **Kazi ya Umma** | | |
| Idadi ya kaya wanufaika wanazopokea malipo kupitia kazi za umma | 988,000 (2023/24) | 4,828,930 |
| Idadi ya miradi midogo ya kazi za umma na rasilimali za jamii zilizoundwa kupitia Mpango wa Hifadhi ya Jamii wenye Tija (jumla ya mkusanyiko) | 21,200 (2023/24) | 35,780 |
| Asilimia ya miradi midogo ya kazi za umma yenye mpango wa matengenezo na hatua za kuhakikisha uendelevu | 65.0 (2023/24) | 75.8 |
| **Uhawilishaji wa Fedha Taslimu** | | |
| Idadi ya kaya wanufaika wanaopokea uhawilishaji wa fedha taslimu (wa masharti na usio na masharti) | 1,203,000 (2023/24) | 1,256,650 |
| Asilimia ya watoto wa kaya wanufaika wenye umri wa miezi 0–24 wanaohudhuria vituo vya afya mara kwa mara | 95.0 (2023/24) | 96.0 |
| Asilimia ya watoto wa kaya wanufaika wenye umri wa miaka 6–18 walioandikishwa katika shule za msingi na kuhudhuria zaidi ya 80% ya masomo kwa mwezi | 95.0 (2023/24) | 96.0 |
| Asilimia ya watoto wa kaya za wanufaika wanaostahili kujiunga na shule za sekondari | 7.0 (2023/24) | 8.0 |
| Asilimia ya kaya wanufaika wanaopokea ufadhili kutokana na ulemavu | 5.0 (2023/24) | 7.5 |

### 3.4.6 Huduma Bora za Afya kwa Wote

**Hali ilivyo:** Dhamira ya muda mrefu ya Tanzania ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wote imezaa matokeo chanya katika kipindi cha miaka ishirini na mitano iliyopita. Umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 66 mwaka 2019/20 hadi kufikia wastani wa miaka 68.3 mwaka 2025. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kwa kiasi kikubwa kutoka 112 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1,000. Vifo vya akina mama wakati wa kujifungua vimeshuka hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000, huku udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ukipungua kutoka asilimia 48 mwaka 1999 hadi asilimia 30 mwaka 2022. Idadi ya wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya afya imeongezeka hadi asilimia 81 na jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya imefikia 8,881 nchi nzima. Mafanikio haya yametokana na kuimarishwa kwa huduma za afya ya msingi, upanuzi wa programu za chanjo na lishe, kuboreshwa kwa mafunzo ya watumishi wa afya, pamoja na ongezeko la uwekezaji katika sekta ya afya uliofikia kati ya asilimia 10 hadi 11.6 ya matumizi ya umma. Kwa ujumla, hatua hizi zinaonyesha maendeleo makubwa kuelekea huduma za afya zilizo sawa, zinazofikika kwa wote na zinazozingatia mahitaji ya jamii.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna vikwazo vinavyozuia kufikiwa kwa huduma za afya kwa wote. Tofauti za kijiografia zinaendelea kujitokeza, ambapo maeneo ya vijijini na yaliyo mbali na miji yanakumbwa na uhaba wa wataalamu wa afya, upatikanaji mdogo wa dawa muhimu na uwezo hafifu wa uchunguzi wa kitabibu. Mapungufu ya miundombinu ya afya, mifumo dhaifu ya rufaa na gharama kubwa zinazolipwa moja kwa moja na wagonjwa hupunguza ubora na upatikanaji wa huduma. Wigo wa bima ya afya bado ni mdogo, ukifikia asilimia 15.3 tu mwaka 2022, hali inayoziacha kaya nyingi katika hatari ya misukosuko ya kifedha wanapougua. Kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, milipuko ya magonjwa mara kwa mara na athari za mabadiliko ya tabianchi vinaongeza shinikizo katika mfumo. Aidha, uwekezaji mdogo katika huduma za kibingwa, mgawanyo usio sawia wa wataalamu na matumizi haba ya TEHAMA vinaendelea kudhoofisha ufanisi na usawa katika utoaji wa huduma.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kufanikiwa kuimarisha afya ya jamii kwa kiwango kikubwa kwa kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa kama malaria na kuwekeza katika mifumo ya afya ya kinga, ubunifu wa kidijitali na uzalishaji wa bidhaa za afya nchini. Kwa kuimarisha miundombinu, kuwekeza katika wataalamu wa afya, na kupanua huduma za bima ya afya, taifa linaweza kujenga mfumo wa afya imara, jumuishi na unaostahimili mitikisiko. Hii itaboresha ubora wa maisha, kuboresha rasilimali watu na kuifanya sekta ya afya kuwa kichocheo cha maendeleo ya taifa. Kiambatisho I (3.4.6) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.6) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.22: Viashiria vya Huduma za Afya kwa Wote*

| Kiashiria | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Kiwango cha vifo vya watoto wachanga (kwa kila vizazi hai 1,000) | 33 (2022) | 27 |
| Kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka mitano (kwa kila vizazi hai 1,000) | 43 (2022) | 34 |
| Kiwango cha jumla cha uzazi (wastani wa idadi ya watoto kwa mwanamke wa umri wa kuzaa) | 4.8 (2022) | 4.11 |
| Asilimia ya wazazi wanaohudumiwa na wataalamu wa afya | 84 (2023/24) | 89.3 |
| Idadi ya vifo vya akina mama (kwa kila vizazi hai 100,000) | 104 (2022) | 85 |
| Matarajio ya kuishi wakati wa kuzaliwa (miaka) | 68.3 (2025) | 70.4 |
| Matumizi katika sekta ya afya (asilimia ya matumizi ya Serikali) | 11.6 (2023/24) | 14.2 |

### 3.4.7 Usalama wa Chakula na Lishe Ulioimarishwa

**Hali ilivyo:** Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha usalama wa chakula na hali ya lishe, hatua zilizochochewa na utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Mpango III). Kiwango cha kujitosheleza kwa chakula kimeongezeka kutoka asilimia 118 mwaka 2019/20 hadi asilimia 128 mwaka 2023/24. Mafanikio haya yanaashiria uwepo wa ziada kubwa ya chakula nchini. Udumavu wa watoto chini ya miaka mitano umepungua kutoka asilimia 31.8 hadi 26.5 sambamba na kupungua kwa kiwango cha utapiamlo mkali. Aidha, upatikanaji wa chakula chenye madini joto kwa wanawake umeongezeka. Vilevile, kumekuwa na ongezeko la unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee na utoaji wa virutubisho vya vitamini A, kupungua kwa watoto

wanaozaliwa na uzito mdogo na kushuka kwa upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa. Aidha, serikali na wadau mbalimbali wameendelea kutambua umuhimu na kuwekeza katika malezi bora na maendeleo ya awali ya mtoto kama msingi wa maendeleo. Hii inakwenda sambamba na kuongezeka kwa mafunzo kwa wahudumu wa afya, kampeni za chanjo na upatikanaji wa huduma za lishe.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio hayo, bado kuna mapengo katika usalama wa chakula na lishe. Utapiamlo bado ni tatizo, huku magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanayohusiana na lishe yakiendelea kuongezeka kutokana na mabadiliko ya mtindo wa maisha na kasi ya ukuaji wa miji. Upungufu wa damu, uhaba wa madini ya chuma na virutubisho vya vitamini A bado ni changamoto kwa wanawake, watoto na wajawazito. Ingawa nchi inazalisha chakula cha ziada, bado inaagiza bidhaa kama ngano, mafuta ya kula na sukari zenye thamani ya dola za Marekani milioni 400–500 kila mwaka. Hali hii inaashiria upungufu wa tija katika uzalishaji na changamoto ya ushindani katika sekta ya viwanda vya kilimo. Utegemezi mkubwa wa kilimo cha mvua, upotevu wa mazao baada ya mavuno, udhaifu wa mnyororo wa thamani, pamoja na uhaba wa miundombinu ya uhifadhi na uchakataji vinadhoofisha usalama wa chakula. Aidha, mabadiliko ya tabianchi, ukame unajitokeza wa mara kwa mara, mafuriko na wadudu waharibifu wanaendelea kuhatarisha upatikanaji wa chakula na lishe bora, hususan kwa kaya za vijijini na zilizo katika mazingira hatarishi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kuimarisha mfumo wa chakula kwa kufanya mabadiliko katika uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya lishe bora, kuongeza upatikanaji wa vyakula vyenye virutubisho muhimu na kuhakikisha usalama wa chakula. Kwa kuwekeza katika kilimo kinachostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi, kupunguza upotevu baada ya mavuno na kuimarisha minyororo ya thamani, taifa linaweza kujenga mfumo wa chakula salama, endelevu na wenye ushindani. Hatua hizi zitaboresha afya na hali ya lishe ya wananchi, huku zikikupunguza utegemezi mkubwa wa uagizaji wa bidhaa za chakula kutoka nje ya nchi. Kiambatisho I (3.4.7) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.7) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.23: Viashiria vya Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe Bora*

| Kiashiria | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Kiwango cha udumavu kwa watoto wenye umri wa miezi 0–59 % | 26.5 (2023/24) | 20.0 |
| Kiwango cha utapiamlo mkali kwa watoto wa miezi 0–59 % | 2.6 (2023/24) | 2.6 |
| Kiwango cha watoto wanaozaliwa na uzito mdogo | 3.1 (2023/24) | 2.0 |
| Asilimia ya wanawake wenye umri wa miaka 15–49 wenye upungufu wa damu | 23 (2023/24) | 12.0 |
| Kiwango cha utapiamlo mkali wa dharura kwa watoto wa miezi 0–59 % | 2.7 (2023/24) | 2.0 |
| Wastani wa kiwango cha madini ya iodini kwa wanawake wa miaka 15–49 | 100–299 (2023/24) | 100–299 |
| Kiwango cha uzito kupita kiasi kwa watoto wa miezi 0–59 % | 2.34 (2023/24) | 2.0 |
| Kiwango cha uzito kupita kiasi kwa watu wazima wa miaka 15–49 % | 22 (2023/24) | 16.0 |

| Kiashiria | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya kaya zinazotumia chumvi yenye iodini ya kutosha | 78 (2023/24) | 100 |
| Kiwango cha unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee | 62% (2023/24) | 100% |
| Kiwango cha upungufu wa vitamini A kwa watoto wenye umri wa miezi 6–59 (kiwango cha retinoli seramu < 20 μg/dl) | 18 μg/dl (2023/24) | 10 μg/dl |
| Kiwango cha Kujitosheleza kwa Chakula % | 128 (2023/24) | 128 |

### 3.4.8 Upatikanaji na Uunganishaji wa Maji na Usafi wa Mazingira

**Hali ilivyo:** Maji ni rasilimali muhimu kwa uhai, afya, ustawi wa mazingira na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Katika utekelezaji wa Mpango III, upatikanaji wa maji safi na salama na huduma za usafi wa mazingira umeongezeka. Maeneo ya vijijini yamenufaika na miradi ya maji ya bomba na uchimbaji wa visima. Aidha, mijini hasa katika makao makuu ya mikoa kumekuwa na ongezeko la kaya zilizounganishwa na mifumo ya maji ya bomba na majitaka. Vilevile, makao makuu ya wilaya na miji midogo nayo yamenufaika na maboresho ya mifumo ya usambazaji maji. Juhudi za uhifadhi zimeimarishwa kupitia upimaji na utambuzi rasmi wa vyanzo vya maji, kuimarisha Bodi tisa za Maji za Mabonde pamoja na kupanua maabara za kikanda za uchunguzi wa ubora wa maji. Hatua hizi zimechangia kufikisha maji salama kwa takribani asilimia 88 ya kaya za mijini na asilimia 77 ya kaya za vijijini huku hali ya usafi na matumizi ya vyoo bora vijijini nayo ikiboreshwa.

**Changamoto:** Idadi ya watu ilifikia takriban watu milioni 60 mwaka 2022 kutoka watu milioni 33.6 mwaka 2002, sanjari na ukuaji wa miji na shughuli za kiuchumi, hali iliyosababisha mahitaji ya maji kuongezeka kwa kiasi kikubwa. Changamoto hii imepunguza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa kila mtu kutoka wastani wa lita za ujazo 3,678 kwa mwaka hadi 2,105. Huduma za usafi wa mazingira bado ni duni ikilinganishwa na nchi nyingine za uchumi wa kipato cha kati-juu/chini. Huduma za usafi wa mazingira bado ni duni zikiwafikia asilimia 26 tu ya watu, huku wengi, hususan waishio vijijini na kwenye makazi yasiyo rasmi mijini, wakiendelea kukosa huduma za usafi wa mazingirai. Miundombinu chakavu ya maji, upotevu wa maji yasiyoingiza mapato, uwekezaji usiotosheleza, na athari za mabadiliko ya tabianchi, vinaendelea kudhoofisha huduma za maji safi na salama pamoja na usafi wa mazingira.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kuimarisha upatikanaji wa maji salama kwa kubadili mwelekeo kutoka kuongeza huduma za usambazaji pekee na kuwekeza katika usimamizi jumuishi, wenye ufanisi na unaostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Hii inahusisha kuboresha miundombinu, kupanua upatikanaji wa huduma, na kutumia teknolojia za kidijitali kama mita za kisasa na vihisishi ili kupunguza upotevu wa maji na kuongeza ufanisi wa usambazaji. Aidha, kwa kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu, hususan katika mifumo ya maji inayotumia umeme wa jua na kuhakikisha huduma bora za usafi wa mazingira kwa wote, taifa litajenga mfumo wenye usawa, unaozingatia uhifadhi wa mazingira, na utakaoimarisha afya ya jamii. Mkakati huu jumuishi unaolenga kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata maji safi na salama ya uhakika utapunguza magonjwa yanayotokana na utumiaji wa maji yasiyo salama. Kadhalika, utaweka msingi wa jamii yenye afya bora, kuimarisha shughuli endelevu za kiuchumi na ulinzi wa mifumo ya asili ya maji nchini kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Kiambatisho I (3.4.8) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.8) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.24: Viashiria vya Kukuza Upatikanaji wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira*

| Kiashiria | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya kaya zinazotumia vyanzo vilivyoboreshwa vya maji ya kunywa | 69.5 (2022) | 100 |
| Upatikanaji wa maji safi katika maeneo ya vijijini (% ya jumla) | 79.6 (2023/24) | 87.9 |
| Upatikanaji wa maji safi katika maeneo ya mijini (% ya jumla) | 90.0 (2023/24) | 97.2 |
| Asilimia ya wakazi wa vijijini wanaotumia maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 78.0 (2023/24) | 94.7 |
| Asilimia ya wakazi wa makao makuu ya mikoa wanaotumia maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 92.0 (2023/24) | 100.0 |
| Asilimia ya kaya zilizounganishwa na mfumo rasmi wa majitaka katika makao makuu ya mikoa | 26.0 (2023/24) | 60.0 |
| Asilimia ya kaya za vijijini zenye huduma bora za usafi wa mazingira | 72.0 (2023/24) | 100.0 |
| Asilimia ya maji yasiyoingiza mapato katika makao makuu ya mikoa | 14.0 (2023/24) | 9.3 |
| Asilimia ya wakazi wa makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaotumia maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 81.0 (2023/24) | 98.4 |
| Asilimia ya wakazi wa Dar es Salaam wanaotumia maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 90.0 (2023/24) | 100 |
| Asilimia ya kaya zilizounganishwa na mfumo rasmi wa majitaka katika Dar es Salaam | 22.0 (2023/24) | 50.8 |
| Asilimia ya maji yasiyoingiza mapato katika Dar es Salaam | 28.0 (2023/24) | 16.0 |
| Idadi ya vyanzo vya maji vilivyotambuliwa, kupimwa mipaka na kutangazwa rasmi kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi | 180 (2023/24) | 2,000 |

### 3.4.9 Jamii yenye Mshikamano, Inayowajibika na Kushirikiana

**Hali ilivyo:** Mafanikio ya Tanzania katika kufikia maendeleo lengwa yanategemea uwepo wa jamii yenye mshikamano, uwajibikaji na ujumuishi, inayozingatia umoja wa kitaifa, maadili na wajibu wa kila mwananchi. Katika muongo uliopita, kumekuwa na mafanikio yaliyochochewa na matumizi ya Kiswahili kama nyenzo ya kuimarisha umoja, elimu ya uraia, ushiriki wa vijana katika shughuli za taifa na za kujitolea, pamoja na juhudi za kukuza usawa wa kijinsia. Kadhalika, mageuzi katika sekta ya habari, utekelezaji wa ugatuazi wa madaraka na kuongezeka kwa ushiriki wa asasi za kiraia yameimarisha uwazi na utawala shirikishi.

Mageuzi haya yameongozwa na Falsafa ya Mabadiliko yenye misingi minne: Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga ili kuimarisha umoja wa kitaifa, uwajibikaji na utulivu wa kijamii.

**Changamoto:** Pamoja na hatua hizi, mapungufu kadhaa bado yapo katika ufahamu na uelewa kuhusu masuala ya uraia, uzingatiaji wa maadili na ushiriki katika shughuli za kijamii, hususan katika maeneo ya vijijini. Ukosefu wa usawa wa kijinsia na tofauti za kiuchumi zinaendelea, kiasi kwamba wanawake na makundi yaliyo pembezoni mwa mkondo rasmi wa uchumi yanaendelea kutengwa katika upatikanaji wa nafasi za uongozi. Aidha, ukosefu wa ajira kwa vijana, kasi kubwa ya ukuaji wa miji na mabadiliko ya desturi na tamaduni vinaendelea kudhoofisha mifumo asili ya ulinzi na mshikamano wa jamii. Kuongezeka kwa taarifa potofu, mgawanyiko wa kijamii na uelewa mdogo wa matumizi sahihi ya vyombo vya habari vinaathiri umoja wa kitaifa. Tofauti za kijamii na changamoto za jamii kushiriki katika masuala ya kiraia vinadhoofisha ushirikiano na mshikamano.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ina fursa kubwa ya kujenga mshikamano wa kijamii ulio imara na wenye ustahimilivu zaidi kwa kukuza utambulisho wa pamoja na kufungua uwezo kamili wa jamii nzima. Hili linaweza kufikiwa kwa kukuza usawa wa kijinsia kupitia mageuzi ya kisheria na programu za kimkakati za uongozi kwa wanawake katika sekta zote ili kuhakikisha wanashiriki ipasavyo katika ngazi za juu za maamuzi serikalini, katika sekta binafsi na taasisi za elimu. Aidha, kuna haja ya kuweka mkazo katika maadili kupitia mfumo wa elimu na kuhamasisha majadiliano ya kijamii kupitia sanaa na utamaduni. Hii itawezesha taifa kujikinga dhidi ya mgawanyiko wa kijamii na dhana potofu zinazoathiri umoja wa kitaifa. Mbinu hii jumuishi itachochea ukuaji wa jamii inayoshiriki kikamilifu katika maendeleo, inayowajibika na yenye amani. Hii itachangiwa na hali ya kila mwananchi kujihisi kuwa ni sehemu ya taifa na hivyo anawajibika kuchangia mustakabali wa pamoja wa maendeleo. Kiambatisho I (3.4.9) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.9) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.25: Viashiria vya Utendaji kwa Jamii Yenye Mshikamano, Uwajibikaji na Ushiriki*

| Kiashiria | Kiwango cha Msingi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Alama ya wastani ya fahirisi ya uhalifu | 53.2 (2025) | 47.8 |
| Kiwango cha kupungua kwa ajali za barabarani (%) | 35.0 (2023/24) | 40.0 |
| Kiwango cha ukatili wa kijinsia% | 38.9 (2022) | ≤20 |
| Ukatili dhidi ya watoto %( Wasichana): Kingono | 11 (2024) | ≤5.50 |
| Ukatili dhidi ya watoto (%Wasichana): Kimwili | 24 (2024) | ≤14.00 |
| Ukatili dhidi ya watoto (%Wasichana): Kisaikolojia | 22 (2024) | ≤13.20 |
| Ukatili dhidi ya watoto (%Wavulana): Kingono | 5 (2024) | ≤2.69 |
| Ukatili dhidi ya watoto (% Wavulana): Kimwili | 21 (2024) | ≤12.00 |
| Ukatili dhidi ya watoto (% Wavulana): Kisaikolojia | 16 (2024) | ≤8.00 |

### 3.4.10 Maendeleo Jumuishi Vijijini

**Hali ilivyo:** Vijiji vinabaki kuwa mhimili muhimu nchini Tanzania katika kufanikisha mageuzi ya kiuchumi yanayokusudiwa, ambapo shughuli za vijijini, kama vile kilimo, ufugaji na viwanda vidogo, ni nguzo muhimu za ustawi na maisha ya wananchi walio wengi. Hatua za hivi karibuni za utekelezaji wa Mpango III zimesaidia sana uboreshaji

upatikanaji na ubora wa miundombinu vijijini, kupanua skimu za maji, usambazaji wa nishati ya umeme, barabara unganishi za vijijini na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za kifedha, huduma za ugani na upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Huduma jumuishi za kifedha kwa njia za kidijitali zimeimarika kupitia huduma za fedha kwa simu na mtandao wa taasisi ndogo za fedha, huku mipango ya matumizi bora ya ardhi na mifumo ya usajili ikiimarisha usalama wa miliki za ardhi katika ngazi ya jamii. Hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa tija na ushiriki mpana zaidi wa wakazi wa vijijini katika masoko. Hata hivyo, tofauti za upatikanaji kati ya maeneo na jamii za vijijini, pamoja na changamoto za kimuundo, bado zinakwamisha maendeleo jumuishi na mageuzi halisi ya kiuchumi.

**Changamoto:** Maeneo ya vijijini kwa ujumla yanakabiliwa na muingiliano mdogo na masoko, ushiriki hafifu katika minyororo ya thamani, upatikanaji hafifu wa huduma za kifedha, na usalama mdogo wa miliki za ardhi pamoja na matumizi duni ya teknolojia. Upotevu wa mavuno baada ya kuvunwa, miundombinu duni ya umwagiliaji, upatikanaji duni wa huduma za ugani na ucheleweshaji wa upatikanaji wa pembejeo za kisasa, kwa pamoja zinadunisha ushindani. Uhamaji wa vijana kuelekea mijini unaendelea kuchangiwa na ufinyu wa fursa za ajira na mapato katika maeneo ya vijijini, wakati ukosefu wa usawa wa kijinsia unakwamisha ushiriki wa wanawake katika shughuli za uzalishaji na uhakika wa umiliki wa ardhi. Aidha, athari za mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa rutuba ya ardhi na migogoro ya matumizi ya rasilimali vinaendelea kudhoofisha ustawi wa maisha vijijini. Udhaifu wa uwezo wa mifumo ya kitaasisi katika uratibu wa shughuli za maendeleo vijijini, uwekezaji mdogo na kasi ndogo ya kupokea teknolojia za kidijitali pamoja na udhaifu wa kuzingatia kanuni za uhifadhi wa mazingira, vinaendelea kudhoofisha ustawi wa maeneo hayo.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kupitia Mpango huu, Tanzania itafanya mageuzi ya maeneo ya vijijini kutoka uchumi wa kujikimu na kuwa kitovu cha shughuli za kiuchumi jumuishi, zenye tija na zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi. Hili litafanikiwa kwa kuimarisha usalama wa umiliki wa ardhi, kuwekeza katika miundombinu ya kilimo inayostahamili mabadiliko ya tabianchi, kuboresha barabara vijijini na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno kupitia uhifadhi bora na usindikaji wa bidhaa. Kuongeza upatikanaji wa huduma na elimu za kifedha kwa wanawake na vijana ili kuchochea ujasiriamali wa ndani na kupunguza msukumo wa kuhamia mijini. Mkakati huu utaimarisha usalama wa chakula, kuongeza tija na kufanya vijiji kuwa injini ya maendeleo ya taifa. Kiambatisho I (3.4.10) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.10) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.26: Viashiria vya Muhimu vya Maendeleo Jumuishi Vijijini*

| Kiashiria | Kiwango cha Msingi | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Fahirisi ya Mageuzi Vijijini (RTI) | 0.35 | 0.42 |

### 3.4.11 Mageuzi ya Vyama vya Ushirika

**Hali ilivyo:** Vyama vya ushirika vimeendelea kuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini, hususan kwa maeneo ya vijijini, ambapo huwawezesha wanachama kupata mitaji, masoko, pembejeo na huduma za msingi. Kupitia utekelezaji wa Mpango III, hatua zimepigwa katika kuhuisha na kuimarisha vyama vya ushirika, kupanua vyama vya kuweka na kukopa, vyama vya ushirika wa masoko ya mazao, pamoja na kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika Tanzania kwa kuhusisha ubia na vikundi vya kifedha vya kijamii. Hatua hizi zimeongeza upatikanaji wa huduma za kifedha, kuboresha uhusiano wa masoko na kuchochea matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa vyama vya ushirika. Ushirika umeendelea kuwa jukwaa muhimu la

kuwawezesha wanawake, vijana na wajasiriamali wa vijijini kuongeza kipato na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

**Changamoto:** Licha ya umuhimu wake, vyama vingi vya ushirika vinakabiliwa na changamoto za kiuongozi na usimamizi, uwezo mdogo wa kiutendaji na mifumo ya kisheria isiyoendana na mahitaji, uwajibikaji usioridhisha na matumizi finyu ya mifumo ya kidijitali vinaathiri ufanisi. Upatikanaji mdogo wa mitaji ya gharama nafuu na ukosefu wa utaalamu wa kibiashara unapunguza uwezo wa kuongeza thamani na kushindana. Vyama vingi bado vinaegemea katika shughuli za kilimo cha msingi zenye tija ndogo, huku ufuatiliaji na ukaguzi usioridhisha ukiathiri maendeleo endelevu.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ina fursa ya kuchochea ustawi wa jamii kwa kuifanya sekta ya ushirika iwe ya kitaaluma, yenye umahiri wa kibiashara na iliyojengwa katika misingi ya uaminifu. Mageuzi haya yatalenga kuibadilisha sekta hii kutoka mifumo isiyo na muundo thabiti na uwajibikaji wa kutosha na kuifanya iwe hai, shindani na yenye uwazi. Kwa kufanya hivyo, wakulima wadogo, mafundi na wajasiriamali watawezeshwa kushiriki na kushindana katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Upatikanaji wa mitaji kwa gharama nafuu kwa ajili ya uwekezaji katika mitambo na usindikaji na kuongeza thamani utawezesha vyama kupanua zaidi shughuli za kilimo cha msingi chenye thamani ndogo na kuingia katika sekta zenye tija na ushindani mkubwa. Hatua hizi zitaimarisha vyama vya ushirika vitakavyoendeshwa kwa weledi na mwelekeo wa kibiashara na kuwa kichocheo muhimu cha ujenzi wa uchumi wa viwanda na ukuaji jumuishi wa taifa. Kiambatisho I (3.4.11) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.11) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.27: Viashiria vya Utendaji vya Mageuzi ya Vyama vya Ushirika*

| Kiashiria | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika | 328 (2023/24) | 530 |
| Idadi ya vyama vya ushirika vinavyotumia mfumo rasmi wa masoko | 4,279 (2023/24) | 5,759 |
| Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika | 8,358,000 (2023/24) | 20,540,850 |

### 3.4.12 Kupanua Tabaka la Kipato cha Kati

**Hali ilivyo:** Dhamira ya Tanzania kufikia hadhi ya nchi ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, jumuishi na himilivu imejikita katika dhana ya kujenga tabaka pana na imara la watu wa kipato cha kati. Kwa sasa, takribani asilimia 12 tu ya wananchi wanakadiriwa kuwa katika tabaka hili, kiwango ambacho ni chini kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na wastani wa Afrika wa asilimia 34. Hali hii inaakisi athari za muda mrefu za uchumi unaotawaliwa na sekta isiyo rasmi, vyanzo vya mapato visivyo na uhakika na fursa chache za kujenga mitaji ya uhakika, hususan katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji. Ingawa uchumi na uwekezaji umeongezeka katika kipindi cha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025, Mpango Elekezi 2025 na mipango ya maendeleo iliyopita umeimarisha ustawi wa wananchi, kaya nyingi bado ziko katika hatari ya kuyumba. Hii ni kutokana na kukosa kipato, gharama kubwa za maisha, ukosefu wa bima ya afya na pensheni zisizokidhi mahitaji na tofauti katika upatikanaji wa huduma zenye ubora zinazozuia kipato hasa kwa vijana, wanawake na waajiriwa walio katika shughuli zisizo rasmi.

**Changamoto:** Kupanuka kwa tabaka la kipato cha kati nchini kunakwamishwa na vikwazo vya muundo wa kiuchumi na kitaasisi. Sehemu kubwa ya ajira ziko katika shughuli zisizo rasmi, ambazo mara nyingi zina tija ndogo, vipato visivyo vya uhakika na ufikiaji mdogo wa kinga ya jamii. Aidha, tofauti za upatikanaji wa fursa za ajira zenye staha, miundombinu na huduma zisizotesheleza huzuia ukuaji wa tabaka la kipato cha kati. Ujumuishi hafifu wa kifedha unaotokana na upatikanaji mdogo wa mikopo ya muda mrefu, pamoja na mifumo hafifu ya kujenga mitaji kama vile umiliki wa nyumba, ardhi na pensheni isiyowafikia watu wengi kwa kiwango cha kutosha, unazifanya familia nyingi zenye fursa ya kuingia katika tabaka la kipato cha kati kuwa katika hatari ya kushuka kiuchumi ikiwemo kupatwa na majanga ya kiafya ya mara kwa mara. Vilevile, kukosekana kwa mifumo kujumuishi ya shughuli zisizo rasmi katika mikondo rasmi ya uchumi sanjari na ujuzi usiokidhi mahitaji ya soko hasa katika sekta na shughuli zenye fursa kubwa pamoja na kasi ndogo ya mapokeo na matumizi ya fursa za uchumi wa kidijitali na kijani, hupunguza fursa za kukua kiuchumi na kimapato kutoka kizazi kimoja kwenda kingine.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ina fursa kubwa ya kujenga tabaka la kipato cha kati thabiti na lenye nguvu kama msingi imara wa ukuaji wa uchumi unaochochewa na uwezo wa soko la ndani. Hii itawezekana kwa kutumia njia mseto na jumuishi za kuinua kipato cha jamii ikiwemo kuongeza matumizi ya teknolojia za kidijitali katika kuboresha maisha na kukuza biashara za mtandaoni. Hii ni pamoja na hatua mahsusi zinazochukuliwa na serikali ili kuwawezesha wananchi kumiliki ardhi na mali zisizohamishika na kufanya baishara ya ukodishaji kama nyenzo ya uzalishaji wa kipato. Kwa kuwashirikisha Watanzania waishio ughaibuni katika uwekezaji na utaalamu, na kuendeleza sekta za uchumi wa kijani na buluu, taifa linaweza kuzalisha ajira zenye kipato kikubwa na kuimarisha usawa wa kikanda. Mikakati hii jumuishi inaongeza fursa kwa idadi kubwa ya wananchi kuweza kupenya kuingia katika tabaka la kipato cha kati na kujenga uchumi thabiti, jumuishi na endelevu. Kiambatisho I (3.4.12) kinaonesha hatua za utekelezaji na mpangilio wa nyakati, na Kiambatisho II (3.4.12) kinaonesha viashiria vya utendaji.

*Jedwali Na. 3.28: Kiashiria cha Ongezeko la Watu wenye Kipato cha Daraja la Kati*

| Kiashiria | Kiwango cha Msingi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya idadi ya watu walioko katika tabaka la kipato cha kati (%) | 12 (2025) | 18 |

## 3.5 Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ni masuala muhimu katika kuhakikisha mageuzi endelevu yanayowezesha ukuaji wa uchumi wa viwanda, maendeleo ya miji, uhai na ustahimilivu wa ikolojia na bayoanuwai. Utekelezaji wa Mpango wa Tatu umeleta mafanikio katika maeneo mbalimbali, hususan kurejesha uoto asili na misitu, kuhifadhi bioanuwai, kutumia nishati jadidifu na kuboresha upatikanaji wa taarifa za tahadhari ya mapema. Hata hivyo, shinikizo la uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi vinaendelea kuongezeka. Mpango IV unaweka kipaumbele katika afua mseto za kuimarisha uhifadhi wa mazingira, mifumo endelevu ya matumizi ya ardhi na maendeleo ya miji, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na uzalishaji wa gesijoto, pamoja na uboreshaji wa mifumo ya utoaji wa taarifa za tahadhari ya mapema kupitia uwekezaji wa kimkakati. Vilevile, Mpango unalenga kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi unaotumia mifumo ya kidijitali pamoja na kukuza biashara ya kaboni. Hatua hizi zinalenga kuimarisha ulinzi wa maliasili na ustahimilivu ili kufikia mageuzi tarajiwa na kujenga msingi thabiti kuelekea uchumi wa kijani uliobainishwa katika Dira 2050.

### 3.5.1 Uhifadhi wa Mazingira

**Hali ilivyo:** Uhifadhi wa mazingira ni suala muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Tanzania, hususan katika kukuza uchumi wa viwanda, kuboresha uhai wa ikolojia na kuimarisha ustahimilivu wake. Utekelezaji wa Mpango wa Tatu umeleta mafanikio makubwa, ikiwemo kuongezeka kwa hifadhi ya misitu ya jamii kutoka hekta 120,000 hadi 190,000, mashamba ya misitu ya biashara kufikia hekta 510,000, na zaidi ya asilimia 128 ya miradi mikubwa iliyotekelezwa kukidhi matakwa ya Tathmini za Athari za Mazingira na kanuni za ukaguzi. Uhifadhi wa bioanuwai uliimarishwa zaidi kupitia Benki ya Taifa ya Hifadhi za Rasilimali za Kijenetiki, njia za asili za kuhifadhi viini mbegu na mbegu bora za mifugo zinazozingatia mikataba ya kimataifa inayohusu hifadhi ya bioanuwai, upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki na matumizi yake, pamoja na rasilimali za mimea kwa chakula na kilimo. Usimamizi shirikishi wa maliasili ulipunguza matumizi haramu ya misitu, kuwezesha utekelezaji wa mikakati ya nishati jadidifu na matumizi ya teknolojia safi za kupikia, na hivyo kupunguza uharibifu wa misitu. Matumizi ya teknolojia za kidijitali katika usimamizi na ufuatiliaji wa mazingira yaliboresha ufanisi wa ufuatiliaji na kuimarisha uwezo wa taifa kuelekea uchumi wa kijani.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio hayo, uharibifu wa mazingira unaotokana na ongezeko la shughuli za binadamu na mabadiliko ya tabianchi bado ni changamoto kubwa. Tanzania hupoteza takriban hekta 469,000 za misitu kila mwaka kutokana na kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Aidha, udhaifu wa usimamizi na utekelezaji wa taratibu za uhifadhi wa mazingira, ukuaji holela wa miji na matumizi ya ardhi yasiyo endelevu huleta athari katika uhifadhi. Hali hii imechochea upotevu wa viumbe hai, ukataji na uchomaji wa misitu, uharibifu wa ardhi na uchafuzi wa mazingira unaodhoofisha ikolojia. Ingawa asilimia 32 ya ardhi nchini imehifadhiwa kisheria, taifa bado linakabiliwa na ufinyu wa rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya udhibiti. Kadhalika, rasilimali nyingine kama vyanzo vya maji, bahari na vyanzo vya nishati mbadala bado hazitumiki ipasavyo, hali inayopelekea nchi kupoteza fursa za ajira na mapato yanayotokana na mifumo ya ikolojia. Kwa ujumla, upungufu wa mifumo-taasisi, bajeti ndogo isiyozingatia mahitaji, mifumo ya tahadhari isiyotosheleza, na kutozingatiwa kwa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya maendeleo hupunguza ustahimilivu na kuzuia uwiano kati ya ustawi wa uchumi na uhifadhi wa mazingira.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kwa kuzingatia mwelekeo wa dunia na mazingira ya ndani ya nchi, Tanzania inaweza kuasisi mkondo mpya wa maendeleo unaoweka uhifadhi wa mazingira katika msingi wa utambulisho wa taifa na ushindani wa uchumi wake. Hili litafanikiwa kwa kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mazingira ili kutambua changamoto mapema, kutumia takwimu katika kufanya maamuzi na kuhakikisha masuala ya mazingira yanazingatiwa katika mipango ya sekta zote. Matumizi ya teknolojia za satelaiti na droni yataimarisha ulinzi na ufuatiliaji wa mazingira. Aidha, biashara ya kaboni inaweza kuwa chanzo cha fedha za kugharamia miradi mikubwa ya uhifadhi wa mazingira. Vilevile, kwa kuzingatia vigezo vya mazingira, utawala bora katika uwekezaji na ugharamiaji wa miradi utasaidia kuelekeza rasilimali kwenye shughuli endelevu. Aidha, jamii itawezeshwa kulinda rasilimali katika maeneo yao na kuchochea ukuaji wa uchumi unaotokana na uhifadhi wa mazingira. Hatua hizi zitaifanya jamii kuwa walinzi wa rasilimali zinazopatikana katika maeneo yao, kuchochea ukuaji wa uchumi unaotokana na uhifadhi wa mazingira, kulinda utajiri wa ikolojia na maliasili, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pia zitaibua vyanzo vipya vya ajira, miundombinu endelevu na kuijengea Tanzania hadhi ya kimataifa kama taifa lenye uwajibikaji na maono ya muda mrefu. Kiambatisho I (3.5.1) kinawasilisha lengo, shabaha na mpangilio, huku Kiambatisho II (3.5.1) kinatoa mfumo wa upimaji matokeo.

*Jedwali 3.29: Viashiria vya Utendaji katika Uhifadhi wa Mazingira*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Thamani ya matumizi endelevu ya rasilimali za misitu, maji na rasilimali bahari kwa pato la taifa % | 4.3 (2023/24) | 7.53 |
| Kiwango cha uharibifu wa misitu (Ha/Mwaka). | 469,420 (2023/24) | 234,710.00 |
| Eneo la misitu chini ya usimamizi wa wananchi (Ha). | 190,000 (2023/24) | 253,333.33 |
| Asilimia ya makampuni makubwa yanayokidhi tathmini ya athari za mazingira na sheria za ukaguzi | 128 (2023/24) | 170.67 |
| Kiwango cha kupungua kwa kasi ya upotevu wa bioanuwai kwa mwaka (%) | 30 (2023/24) | 20.00 |
| Asilimia ya mifumo ikolojia ya kitaifa (ardhi, bahari, maji baridi) chini ya uhifadhi na usimamizi madhubuti (%) | 45 (2022) | ≥60 |
| Fahirisi ya utendaji katika uhifadhi wa mazingira (nafasi ya Tanzania katika nchi za Afrika ) | Nafasi ya 19 (2022) | 15 bora |
| Fahirisi katika kukabiliana na athari za mazingira (nafasi ya Tanzania katika Nchi za Afrika) | Nafasi ya 18 (2022) | 15 bora |
| Asilimia ya ardhi chini ya mipango rasmi ya matumizi ya ardhi % | 15 (2022) | 30 |
| Asilimia ya ardhioevu chini ya mifumo ya uhifadhi | 25 (makisio ya 2023) | 40 |
| Asilimia ya rasilimali za kijenetiki za kipaumbele za mimea/wanyama/msitu zilizohifadhiwa ipasavyo | 30 (2022) | 50 |

### 3.5.2 Ukuaji Endelevu wa Miji Iliyopangika na Kusimamiwa Vizuri

**Hali ilivyo:** Ukuaji wa miji nchini unaendelea kwa kasi. Kwa sasa, asilimia 35.76 ya Watanzania wanaishi mijini. Kiwango hiki kinakadiriwa kufikia asilimia 36.93 mwaka 2031 na asilimia 40 ifikapo 2050. Miji inaendelea kuwa injini ya ukuaji wa uchumi, kitovu cha ubunifu na huduma bora, na kuchochea maendeleo ya viwanda pamoja na kuongeza fursa za ajira. Utekelezaji wa Mpango wa Tatu umeleta mafanikio makubwa katika usimamizi wa miji, ambapo eneo la makazi yasiyo rasmi lilipungua na kufikia asilimia 18 ya eneo la ardhi ya makazi. Viwanja zaidi ya milioni 4.1 vilipimwa na kugawiwa; Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya 139 yaliundwa na kuanza kufanya kazi; na usalama wa umiliki pamoja na utatuzi wa migogoro uliimarishwa. Hii ilisaidia upatikanaji wa leseni za makazi na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kiwango cha wananchi waliopatiwa hati za umiliki wa makazi kiliongezeka, na hivyo kuongeza idadi ya wananchi wanaoridhika na huduma za usimamizi wa ardhi. Mafanikio haya yanaweka msingi imara kwa mwelekeo wa Mpango wa kuboresha na kusasisha mifumo ya usimamizi wa miji iliyopangwa vizuri, jumuishi na inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, kwa kuendana na Dira 2050.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio hayo, kasi ya ukuaji wa miji inazidi uwezo wa upangaji wa miji. Nakisi ya nyumba, inayokadiriwa kuwa zaidi ya nyumba milioni tatu, ni kubwa. Ardhi iliyopimwa na kuandaliwa kwa ujenzi wa makazi ni sehemu ndogo tu ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa mahitaji ya makazi na umilikishaji. Utekelezaji dhaifu wa kanuni za

upangaji wa matumizi ya ardhi, upungufu wa miundombinu, usimamizi usioridhisha wa ukusanyaji na uzoaji wa taka, na mifumo hafifu ya usafiri vimeendelea kupunguza tija na ufanisi wa miji. Hatari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, hususan mafuriko, zinakadiriwa kuongezeka na kuathiri zaidi jamii za kipato cha chini. Uratibu wa kitaasisi kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na vyombo vya upangaji bado hauridhishi, mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa ardhi haitumiki kikamilifu, na upungufu wa fedha unaathiri utekelezaji katika halmashauri. Hivyo, ili kuimarisha mipango miji, utekelezaji wa kanuni na hatua za ustahimilivu wa mazingira ni muhimu ili kudhibiti misongamano, kuzuia kuongezeka kwa makazi yasiyo rasmi na kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na kasi ya ukuaji wa miji.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kwa kuzingatia mwelekeo wa maendeleo uliobainishwa, Tanzania inaweza kuhimili kasi ya ukuaji wa miji kwa kuchukua hatua za haraka zinazozingatia mbinu za kisasa za usimamizi wa ujenzi wa miji itakayokuwa injini ya ukuaji wa uchumi na kielelezo cha maisha endelevu. Mwelekeo huu unapaswa kuzingatia dhana mpya ya mipango miji inayoongozwa na matumizi ya mifumo ya kidijitali, miundombinu inayostahimili mabadiliko ya tabianchi na mbinu bunifu za vyanzo vya fedha, kama hatifungani za kijani za manispaa. Kwa kutumia mifumo ya kisasa, mathalan mifumo ya usafiri wa umma ya kisasa ikiwemo inayotumia umeme, taifa litajenga miji bora ya kisasa inayofaa zaidi kuishi na yenye kuimarisha afya za wananchi. Aidha, Serikali kwa kutumia mfumo wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi itapunguza nakisi ya nyumba za makazi na kuendeleza maeneo ya viwanda yaliyounganishwa, ili kujenga miji ambayo itaimarisha uzalishaji na kuboresha mazingira. Miji hii itawezesha usawa, kufikia kiwango cha maisha bora, na kupanua fursa za wakazi wake. Kiambatisho I (3.5.2) kinawasilisha lengo, shabaha na mpangilio, wakati Kiambatisho II (3.5.2) kinatoa vigezo vitakavyotumika kupimia matokeo tarajiwa.

*Jedwali 3.30:Viashiria vya Utendaji katika Ukuaji wa Miji Endelevu, Iliyopangwa na kusimamiwa Vizuri*

| Viashiria vya Matokeo | Msingi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya ardhi iliyopimwa | 36 | 48 |
| Idadi ya nyumba za kisasa katika makazi ambayo hayajapangwa | 3,347,275 | 4,347,275 |
| Idadi ya leseni za makazi zinazotolewa kwa wamiliki wa nyumba katika makazi yasiyopangwa | 25,748 | 44,010 |
| Asilimia ya ardhi yenye makazi yasiyo rasmi | 59 | 25 |
| Mikoa yenye Mipango Kabambe na Mipango Miji % | 81 | 100 |

### 3.5.3 Mageuzi kwa Usimamizi Endelevu wa Ardhi

**Hali Ilivyo:** Usimamizi endelevu wa ardhi ni nguzo muhimu ya ajenda ya mageuzi tarajiwa nchini. Utawezesha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa katika kilimo, maendeleo ya miji, ujenzi wa uchumi wa viwanda na uhifadhi wa mazingira. Katika eneo hili, mafanikio makubwa yalipatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu. Hii inajumuisha upimaji na ugawaji wa viwanja takriban milioni 4.1, sawa na asilimia 97 ya lengo la mwaka 2026. Upanuzi wa mabaraza ya ardhi na nyumba katika wilaya 139 umechangia utatuzi wa migogoro ya ardhi na kuimarisha usalama wa umiliki. Aidha, urasimishaji na utoaji wa leseni za makazi katika maeneo ambayo hayajapangwa uliendelea, huku matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika usajili wa ardhi yakiboresha uwazi na uwajibikaji. Tafiti za maoni ya wananchi zilionesha kuongezeka kwa kiwango cha kuridhika na mipango ya matumizi ya ardhi na ulinzi wake, hususan mijini. Mafanikio haya yanaendana na azma

ya Dira 2050 ya kuwa na mfumo wa usimamizi wa ardhi wenye usawa, usalama na ufanisi kwa maendeleo jumuishi.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio haya, bado kuna vikwazo vingi vya kimuundo vilivyojitokeza. Takribani asilimia 20 tu ya ardhi imepimwa, jambo linaloacha kaya nyingi bila nyaraka za umiliki na hivyo kuongeza hatari ya kutokea migogoro na uvamizi, pamoja na kufanya sehemu kubwa ya makazi kuwa katika maeneo yasiyopangwa. Usimamizi usioridhisha wa matumizi ya ardhi na utumiaji hafifu wa mifumo ya kidijitali unapelekea kukosekana kwa ufanisi. Kadhalika, mwingiliano wa kitaasisi, ufinyu wa bajeti na uratibu usioridhisha vinakwamisha kasi ya mageuzi yanayohitajika. Matumizi mabaya ya ardhi, kupungua kwa vyanzo vya maji na athari za mabadiliko ya hali ya hewa, kama mafuriko, ukame na mmomonyoko wa ardhi, vinaharibu mazingira na kupunguza uzalishaji. Vilevile, ukosefu wa usawa wa kijinsia katika umiliki wa ardhi bado ni kikwazo cha maendeleo jumuishi. Wakati huohuo, nakisi ya nyumba inayozidi milioni tatu inaongeza shinikizo katika upangaji na maendeleo ya miji. Kukabiliana na changamoto hizi kunahitaji mageuzi ya kina yanayolingana na Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kwa kuzingatia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, Tanzania inaweza kujenga mkondo mpya wa maendeleo unaokuza ustahimilivu wa jamii na ustawi wa taifa. Hili litafikiwa kwa kujumuisha masuala ya tabianchi katika mipango yote ya maendeleo na kuhamasisha mbinu bunifu za fedha, kama hatifungani za kijani, ili kugharamia afua za maendeleo. Ili kuharakisha mageuzi katika sekta ya ardhi, kunahitajika maboresho ya kina ya sheria yatakayowezesha upatikanaji wa ardhi kwa usawa, hususan kwa wanawake, sambamba na kuziwezesha jamii kupitia mipango ya matumizi ya ardhi na usajili katika ngazi ya kijiji. Uanzishaji wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa ardhi utaleta mabadiliko makubwa kwa kupunguza migogoro, kuongeza uwazi na kuvutia uwekezaji. Aidha, kwa kuanzisha benki ya kitaifa ya ardhi na kuandaa mipango maalumu ya matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya viwanda, Tanzania itahakikisha kuwa rasilimali hii muhimu inatumika kama kichocheo cha ukuaji wa viwanda na ustawi endelevu kwa wananchi wote. Kiambatisho I (3.5.3) kinawasilisha malengo, shabaha na mpangilio, wakati Kiambatisho II (3.5.3) kinatoa vigezo vitakavyotumika kupima matokeo.

*Jedwali 3.31: Viashiria Muhimu katika Mageuzi ya Usimamizi Endelevu wa Ardhi*

| Viashiria vya Matokeo | Msingi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya ardhi iliyosajiliwa na kupatiwa hati miliki | 30 (2023) | ≥50 |
| Asilimia ya ardhi iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya viwanda | 5 (2023) | ≥7 |

### 3.5.4 Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

**Hali ilivyo:** Ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi umeendelea kuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya Tanzania. Hii inatokana na utegemezi mkubwa wa uchumi katika sekta zinazoathiriwa moja kwa moja na mabadiliko ya tabianchi, hususan kilimo, maji, nishati, uvuvi na miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi. Katika muongo uliopita, Tanzania ilikabiliwa na athari za mazingira, ikiwemo ukame wa mara kwa mara, mafuriko, mvua zisizotabirika na ongezeko la joto, hali iliyoathiri maisha ya wananchi, usalama wa chakula na miundombinu. Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulileta mafanikio katika maeneo mbalimbali, ikiwemo majaribio ya matumizi ya nishati jadidifu, programu za hifadhi ya misitu na upandaji miti, uboreshaji wa mifumo ya taarifa za tahadhari ya mapema, utekelezaji wa kilimo kinachozingatia uhifadhi wa

mazingira, na miradi ya kuijengea jamii uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Ushiriki wa Tanzania katika makubaliano ya kikanda na kimataifa, ikiwemo Mkataba wa Paris na Sendai, umeimarisha mshikamano wa taifa katika kukabiliana na changamoto hizi. Mafanikio hayo yanajenga msingi wa Mpango huu, unaolenga kuongeza ubora wa mifumo ili kuendana na malengo na shabaha za Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado kuna changamoto kubwa zinazoathiri shabaha tarajiwa. Athari za mabadiliko ya tabianchi zinaendelea kuongezeka na kukwamisha uzalishaji; hali hii inaziathiri zaidi kaya za kipato cha chini na za vijijini. Matumizi ya teknolojia zinazosaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi bado ni madogo. Aidha, ukosefu wa fedha za kutosha na uwepo wa mifumo ya uratibu isiyo na uwezo vinaathiri kasi na ufanisi wa utekelezaji wa miradi na programu za kuimarisha ustahimilivu wa mazingira. Vilevile, vihatarishi vya mazingira na mabadiliko ya tabianchi bado havijajumuishwa ipasavyo katika mifumo ya kupanga na kuandaa miradi. Udhaifu wa mifumo ya tahadhari ya mapema, umaskini na upungufu wa ujuzi pia vimeendelea kuathiri ustahimilivu. Hivyo, athari hizi zinaweza kupunguza pato la taifa kwa takribani asilimia 4.0 ifikapo mwaka 2050 endapo hazitadhibitiwa ipasavyo. Kukabiliana na changamoto hizi kutahitaji kuongeza matumizi ya nishati jadidifu, kuimarisha mifumo ya taasisi, kupanua uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, na kuweka utaratibu thabiti na endelevu wa kugharamia programu za kujenga ustahimilivu.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kwa kuzingatia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Tanzania inaweza kujenga mfumo unaoweka ustahimilivu wa kimazingira na wa mabadiliko ya tabianchi kuwa msingi wa kuimarisha ustawi wa Taifa. Lengo hili litafikiwa kwa kufungamanisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya kitaifa. Kadhalika, kuna umuhimu wa kuhamasisha rasilimali kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwemo hatifungani za kijani. Vilevile, kuna haja ya kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu na teknolojia zinazozingatia athari za mabadiliko ya tabianchi katika kilimo, uchukuzi na viwanda ili kupunguza athari za vihatarishi vya tabianchi na kukuza uchumi wa kijani. Aidha, kwa kuweka mifumo imara ya taifa ya kukabiliana na athari za mazingira, pamoja na kupanua bima dhidi ya vihatarishi vya kimazingira, Tanzania inaweza kulinda jamii zilizo katika mazingira hatarishi dhidi ya mitikisiko isiyozuilika. Mkakati huu utailinda nchi dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi na kuiwezesha Tanzania kuwa kinara wa ukuaji endelevu barani Afrika na sehemu salama kwa uwekezaji. Kiambatisho I (3.5.4) kinawasilisha malengo, shabaha na mpangilio, wakati Kiambatisho II (3.5.4) kinatoa vigezo vitakavyotumika kupima matokeo.

*Jedwali 3.32: Viashiria vya Utendaji katika Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi*

| Viashiria vya Matokeo | Msingi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya ardhi iliyopimwa | 36 | 48 |
| Idadi ya nyumba za kisasa katika makazi ambayo hayajapangwa | 3,347,275 | 4,347,275 |
| Idadi ya leseni za makazi zinazotolewa kwa wamiliki wa nyumba katika makazi yasiyopangwa | 25,748 | 44,010 |
| Asilimia ya ardhi yenye makazi yasiyo rasmi | 59 | 25 |
| Idadi ya Mabaraza ya Ardhi yanayofanya kazi | 117 | 139 |
| Mikoa yenye Mipango Kabambe na Mipango miji | 81 | 100 |
| Kiwango cha kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa (upunguzaji wa uzalishaji wa kaboni) (%) | 209 $MtCO_2e$ (2023) | 30–35 |

| Viashiria vya Matokeo | Msingi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Kiwango cha nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme (%) | 61.8 (2025) | 75 |
| Kiwango cha upungufu wa gharama zitokanazo na athari za mabadiliko ya tabianchi (%) | 1.0 (2023/24) | 0.90 |
| Kiwango cha kupungua kwa uharibifu wa ardhi (%) | 16 (2023/24) | 14.00 |
| Kiwango cha kuongezeka kwa matumizi ya nishati jadidifu ya mkaa mijini (tani) | 500 (2023/24) | 500,000 |
| Familia zinazotumia nishati safi ya kupikia (%) | 15 (2022/23) | 50 |
| Upatikanaji wa nishati safi ya kupikia (%) | 6.9 (2024) | 75 |
| Upatikanaji wa nishati safi ya kupikia (%) | 6.9 (2024) | 75 |

### 3.5.5 Uwezo wa Taasisi na Mifumo ya Utoaji wa Tahadhari

**Hali ilivyo:** Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema. Maendeleo yametokana na kuboreshwa kwa huduma za utabiri wa hali ya hewa, maandalizi ya mapema kwa ngazi za jamii na matumizi ya teknolojia za kidijitali. Kupitishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa ya mwaka 2019 na Sheria ya Kudhibiti Maafa ya mwaka 2022 kumeimarisha uratibu kati ya taasisi. Aidha, ushirikiano kupitia majukwaa kama Umoja wa Taasisi Zinazojihusisha na Uimarishaji wa Uhimilivu wa Majanga na Uhamasishaji wa Kukabiliana na Vihatarishi Kupitia Uwajibikaji wa Pamoja umeboresha mawasiliano kati ya mifumo ya kitaifa na jamii za maeneo husika. Mpango wa Tatu umeongeza uwezo wa nchi kukabiliana na vihatarishi vya mazingira, afya na usalama wa chakula. Maendeleo haya yanaweka msingi muhimu kwa Mpango IV, unaolenga kuboresha na kusasisha mfumo wa tahadhari ya mapema nchi kote. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati, zinazoaminika na zinazoweza kutumika kwa vitendo katika kulinda maisha, miundombinu na mifumo ya kiuchumi.

**Changamoto:** Pamoja na hatua zilizofikiwa, mifumo ya tahadhari bado haijafikia kiwango kinachohitajika katika ufikaji wa huduma na ufanisi. Takribani theluthi moja tu ya wilaya zilizo katika mazingira hatarishi zina huduma zinazotosheleza, hali hii ni sawa na asilimia mbili tu ya wanakaya walio katika mazingira hatarishi wanaopokea taarifa kwa wakati na uhakika. Hivyo, uchambuzi wa viashiria vya tahadhari hautoshelezi. Matumizi ya teknolojia za kisasa, kama vile akili unde, ufuatiliaji kwa njia ya setilaiti na mifumo jumuishi ya kidijitali, bado yako katika kiwango cha chini. Aidha, watu wanaoishi katika mazingira hatarishi vijijini na kwenye makazi yasiyo rasmi mijini bado hukumbana na vikwazo vya kupata taarifa muhimu, hali inayozidishwa na imani ndogo kwa njia rasmi za mawasiliano. Mapungufu haya yanaongeza hatari ya jamii kuathiriwa na misukosuko ya mabadiliko ya tabianchi na kudhoofisha ustahimilivu wa mazingira, hivyo kuonesha umuhimu wa kufanya maboresho ya kina katika mfumo.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Katika kipindi cha kutekeleza Mpango IV, msisitizo utawekwa katika kujenga mwelekeo mpya kwa kuugeuza mfumo wa tahadhari ya mapema kutoka mtandao uliotawanyika na unaotoa mwitikio baada ya madhara kutokea, na kuwa mfumo jumuishi unaoelekeza hatua za mapema kwa wananchi. Mabadiliko haya yatawezeshwa na matumizi ya teknolojia za kisasa, kama akili unde na ufuatiliaji kwa satelaiti, ili kuboresha utambuzi wa vihatarishi, uratibu wa taarifa na tathmini za kina zenye uhakika. Aidha, mfumo huu unapaswa kuondokana na mazoea ya kutoa tahadhari pekee na kuelekea kwenye utoaji wa ushauri wa kinga unaoweza kutekelezwa kwa vitendo. Ili kufanikisha mwelekeo huu, ni muhimu kushirikiana na

wadau mbalimbali, ikiwemo sekta binafsi, ambao watachangia katika kuchochea mageuzi katika eneo hili kupitia uwekezaji wa fedha na teknolojia mpya. Kiambatisho I (3.5.5) kinawasilisha malengo, shabaha na mpangilio, wakati Kiambatisho II (3.5.5) ni mfumo wa upimaji wa matokeo.

*Jedwali 3.33: Viashiria vya Mifumo ya Tahadhari ya Mapema na Uwezo wa Kitaasisi*

| Matokeo | Msingi | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya pato la taifa linalotengwa kila mwaka kwa ajili ya kupunguza vihatarishi vinavyotokana na majanga na mifumo ya tahadhari ya mapema | <0.05–0.1% | ≥0.2% |
| Idadi ya majiji yenye mifumo ya Uhamasishaji wa Kukabiliana na Vihatarishi Kupitia Uwajibikaji wa Pamoja inayofanya kazi pamoja na majukwaa ya kijamii ya tahadhari ya mapema | 2 (2023) | ≥10 |
| Asilimia ya watu wanaopata taarifa za tahadhari ya mapema kwa wakati sahihi | 2% (2023) | ≥30% |

### 3.5.6 Kuimarisha Ushiriki katika Biashara ya Kaboni

**Hali ilivyo:** Biashara ya kaboni, ikisimamiwa kwa ufanisi, inaipa Tanzania fursa adhimu ya kuchochea mageuzi, ukuaji endelevu, uhifadhi wa mazingira na kuongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, sambamba na kufungua vyanzo vipya vya mapato. Utajiri mkubwa wa rasilimali zake za asili, hususan misitu, ardhioevu, maeneo ya bahari na fukwe, pamoja na ardhi ya kilimo, unaipa nchi uwezo mkubwa wa kukidhi masharti ya masoko ya biashara ya kaboni. Hatua zilizochukuliwa ili kupunguza uzalishaji wa hewa ya kaboni ni pamoja na kuundwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, na juhudi za kupunguza uzalishaji unaotokana na ukataji miti na uharibifu wa misitu. Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu, kanuni za usimamizi wa biashara ya kaboni za mwaka 2022/23 zilitungwa na kufanyiwa marekebisho mwaka 2024 ili kuimarisha uendeshaji, usimamizi, uratibu, na kukifanya Kituo cha Kitaifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni kuwa mamlaka ya kitaifa. Miradi mahsusi ya kaboni katika ngazi ya jamii katika Bonde la Yaeda na Milima ya Ntakata imeonesha mafanikio katika kuthibitisha namna biashara ya kaboni inavyoweza kusaidia jamii na kuijengea uwezo wa kujikimu kimaisha. Aidha, uwezo wa kitaalamu umeendelea kuimarika kwa kutumia teknolojia za kisasa, ikiwemo ufuatiliaji kwa njia ya satelaiti na kanzidata ya kidijitali inayohifadhi taarifa mbalimbali, zikiwemo ramani za maeneo yanayonyonya kaboni. Kadhalika, ushirikiano wa kimataifa umeendelea kuimarishwa, ikiwemo kupitia Mfumo wa Pamoja na Serikali ya Japan katika usimamizi wa biashara ya kaboni.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio yaliyopatikana, ushiriki wa Tanzania katika masoko ya kimataifa ya kaboni bado ni mdogo. Tanzania inakadiriwa kupata takribani dola za Marekani bilioni 1 kila mwaka, ikilinganishwa na thamani ya soko la kaboni duniani inayotarajiwa kufikia dola za Marekani trilioni 20 kwa mwaka ifikapo 2035. Aidha, mgawanyo usio sawa wa manufaa katika mnyororo wa biashara ya kaboni hupunguza uaminifu na ari ya kushiriki katika biashara hiyo. Ushiriki wa vijana, wanawake na wawekezaji wa Kitanzania bado ni mdogo, hali inayochangiwa na udhibiti wa soko kwa wachache na uelewa mdogo wa biashara hiyo. Uwezo mdogo wa kitaasisi na kiteknolojia unaathiri utambuzi wa kina kuhusu uwezo wa nchi kunyonya hewa ya kaboni. Uratibu uliogawanyika, sera zinazoingiliana za matumizi ya ardhi, utumiaji mdogo wa nishati jadidifu na ukataji miti unaoendelea vinachangia kudhoofisha uendelevu wa soko la kaboni nchini.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kutumia urithi mkubwa wa maliasili zake kwa kugeuza misitu, ardhioevu na bahari, pamoja na mbinu endelevu za hifadhi za kijamii, kuwa rasilimali za kiuchumi zinazoweza kuthaminishwa na kuaminika katika jukwaa la kimataifa. Hii ni pamoja na kujenga mfumo wa kidijitali wa kiwango cha kimataifa wa Ufuatiliaji, Upimaji, Utoaji Taarifa na Uthibitishaji. Vilevile, kuna haja ya kuanzisha mfumo wazi wa uhifadhi wa kumbukumbu za kitaifa unaothibitisha uadilifu na kuvutia mitaji ya kimataifa ya programu na biashara za kaboni. Kadhalika, kwa kutengeneza kanzidata ya miradi inayokidhi masharti ya biashara ya kaboni katika sekta za misitu, uchumi wa buluu na mbinu endelevu za uendeshaji wa kilimo, Tanzania inaweza kuzalisha chanzo endelevu cha mapato kitakachosaidia moja kwa moja maendeleo ya jamii na kuchangia bajeti ya Serikali. Vilevile, kuweka mifumo ya wazi ya kuwezesha ushiriki wa jamii, vyama vya ushirika vya maeneo husika na mgawanyo wa manufaa kutasaidia kuhakikisha kuwa biashara hii inakuwa jumuishi, kwa kuwawezesha wananchi kuwa walinzi wa mazingira na wanufaika wakuu wa ustawi unaojengwa kwa msingi wa ustahimilivu wa tabianchi. Kiambatisho I (3.5.6) kinawasilisha afua za kina na mpangilio wa utekelezaji, huku Kiambatisho II (3.5.6) kikionesha mfumo wa viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.34: Viashiria vya Utendaji katika Kuimarisha Biashara ya Kaboni*

| Viashiria vya Matokeo | Msingi | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Ushiriki wa jamii na wawekezaji wa ndani katika miradi rasmi ya kaboni (%) | <5% (2025) | ≥10–15% |
| Uwezo wa nchi kunyonya hewa ya kaboni kwa mwaka | 120 $MtCO_2$ | 160 $MtCO_2$ |
| Mauzo katika biashara ya kaboni (USD kwa mwaka) | USD 1 bil. (2025) | USD 3 bil. |

### 3.5.7 Kuchagiza Manufaa ya Uchumi wa Buluu

**Hali ilivyo:** Maliasili za Tanzania zinazoujenga uchumi wa buluu, za bahari na maji baridi, zinatoa fursa kubwa ya kuchochea kasi ya mageuzi ya muundo wa uchumi, sanjari na kujenga ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Sekta hii inajumuisha uvuvi, kilimo na ufugaji wa viumbe vya majini, usafirishaji majini na bandari, utalii wa fukwe, uzalishaji wa nishati, na uendelezaji wa teknolojia za majini. Ikiwa na eneo la kilomita za mraba 61,500 za maji safi, kilomita za mraba 64,000 za maji ya bahari, kilomita za mraba 223,000 za Eneo la Kiuchumi Pekee, na kilomita 1,424 za ukanda wa pwani, Tanzania ni miongoni mwa mataifa machache barani Afrika yenye hazina kubwa ya rasilimali za majini. Hatua za karibuni katika kuboresha fukwe, bandari, ufugaji wa viumbe maji na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa rasilimali za bahari na maziwa zimejenga msingi wa kuimarisha sekta hii. Hata hivyo, mchango wa uchumi wa buluu katika uchumi wa taifa bado ni mdogo ikilinganishwa na uwezo wake halisi na nchi rika za kikanda.

**Changamoto:** Kwa ujumla, ukuaji wa uchumi wa buluu nchini unaathiriwa na miundombinu ya baharini isiyotosheleza, uwezo mdogo wa kusimamia rasilimali, uvuvi katika kina kirefu cha bahari kuu, na usindikaji usiokidhi vigezo, pamoja na mifumo duni ya utafiti na ubunifu. Aidha, uvuvi unaozidi uwezo, ukichangiwa na uvuvi haramu na kukosekana kwa udhibiti imara, pamoja na uchafuzi wa mazingira ya bahari, unahatarisha ustahimilivu wa bayoanuwai na ustawi wa uchumi wa buluu kwa ujumla. Vilevile, mwingiliano wa taasisi, udhaifu wa uratibu, uhaba wa fedha na mitaji, na uwezo mdogo wa kiteknolojia vinachangia kupunguza kasi ya uwekezaji katika eneo hili. Athari za mabadiliko ya tabianchi, kupungua kwa ustahimilivu na ushiriki mdogo wa jamii

katika uwekezaji kwenye minyororo yenye thamani katika uchumi wa buluu ni vikwazo kwa maendeleo jumuishi na endelevu.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania ipo katika nafasi nzuri ya kutumia kikamilifu utajiri mkubwa wa rasilimali zake za bahari, maziwa na mito ili kujenga muundo mpya wa uchumi kupitia uendelezaji wa uchumi wa buluu. Utekelezaji wa programu za kielelezo, kama vile Mji wa Ekolojia ya Bahari wa Bagamoyo na Uendelezaji wa Mfumo Fungamanishi wa Usafirishaji, bandari ya uvuvi ya Kilwa, na Kituo Kikubwa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu cha Maziwa Makuu kinachotumia teknolojia ya kisasa, zinaiweka Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazoibukia kikanda katika uchumi wa buluu. Mafanikio ya lengo hili yatahitaji, uwekezaji mkubwa na uboreshaji wa miundombinu ya bahari, maziwa na mito ili iwe katika kiwango cha kimataifa. Vilevile, kuna haja ya kuimarisha usafirishaji wa majini kwa kutumia teknolojia za kisasa za bandari, kuendeleza uzalishaji wa nishati kutokana na mawimbi ya bahari, na kutumia akili unde katika tafiti za kisayansi. Kwa kusisitiza na kusimamia uvuvi wa kisayansi sambamba na kupanua maeneo yaliyodhibitiwa, Tanzania itaweza kulinda ikolojia yake yenye thamani kwa matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo na kujihakikishia upatikanaji endelevu wa viumbe maji. Aidha, kwa kujitoa kuwa kinara wa maendeleo ya bayoteknolojia na biashara ya kaboni, nchi itaweza kupanua wigo wa kuzalisha ajira zenye staha, kuvutia uwekezaji wa kimkakati, na kujihakikishia kuwa matunda yatokanayo na utajiri wa rasilimali asili yanazifikia na kuzinufaisha jamii zinazozitunza na Taifa kwa ujumla. Kiambatisho I (3.5.7) kinawasilisha malengo, shabaha na mpangilio, wakati Kiambatisho II (3.5.7) ni mfumo wa upimaji wa matokeo.

*Jedwali 3.35: Viashiria Muhimu katika Utendaji wa Uchumi wa Buluu*

| Matokeo | Msingi | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mchango wa uvuvi na ufugaji samaki katika pato la taifa (%) | 1.7 (2023) | 3.5 |
| Shehena ya bidhaa zinazoingia na kutoka kupitia njia ya bahari (milioni tani kwa mwaka) | 21 milioni tani (2023) | 35 milioni tani |
| Mapato ya utalii wa baharini (TZS bilioni kwa mwaka) | 800 | 2,000 |
| Uwezo wa kuzalisha nishati jadidifu | 0 (2025) | ≥300 MW |

### 3.6 Kutumia Kikamilifu Vichocheo vya Maendeleo

Mabadiliko ya Tanzania kuelekea kuwa kitovu cha viwanda, usafirishaji na uchukuzi, na biashara yatategemea uwezo wake wa kutumia vichocheo vya maendeleo kuiwezesha kuinua tija ya uzalishaji, ushindani wa kibiashara na ukuaji jumuishi. Kwa msingi huo, Mpango unaweka kipaumbele katika kuendeleza vichocheo vya kimageuzi, ikiwemo nishati, usafirishaji na uchukuzi fungamanishi, sayansi na teknolojia, utafiti na ubunifu, pamoja na mifumo ya ikolojia ya kitakwimu. Vilevile, vichocheo vingine ni mageuzi ya kidijitali, matumizi mapana ya TEHAMA na mazingira ya biashara yatakayowezesha mageuzi ya muundo wa uchumi kuendana na matakwa ya taifa ya kimaendeleo yaliyobainishwa katika Dira 2050.

Uimarishaji wa vichocheo hivi ni muhimu katika kuwezesha maendeleo ya uchumi wa viwanda, miundombinu ya kisasa, kupanua uwezo wa kuuza nje, kuimarisha uwezo wa kuasili teknolojia, kuboresha utoaji wa huduma na kuvutia mitaji ya viwango vya juu. Vichocheo hivi ni muhimu katika ujenzi wa uchumi wa kisasa, fungamanishi bunifu, na endelevu utakaojenga ustahimilivu na ustawi kwa wote.

### 3.6.1 Nishati

**Hali Ilivyo:** Nishati inaendelea kuwa nguzo muhimu ya mageuzi ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania. Inawezesha ujenzi wa uchumi wa viwanda, maendeleo ya miji, matumizi ya teknolojia za kidijitali na ukuaji jumuishi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango III, uwezo wa uzalishaji wa umeme uliongezeka kufikia megawati 4,504.9 mwaka 2025. Aidha, kaya zilizounganishiwa umeme zilifikia asilimia 52.1 na vijiji vyote viliunganishiwa umeme. Mafanikio haya yalichochea ongezeko la shughuli zinazotumia nishati kwa wingi, hususan uchakataji wa mazao, utengenezaji wa saruji, mavazi, dawa, shughuli za utalii na uchenjuaji wa madini. Tanzania ina vyanzo vingi vya uzalishaji wa nishati: umeme wa maji ikiwemo Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere, Ruhuji, Rumakali, Mtera na Kidatu. Kadhalika, gesi asilia, nishati ya jua, upepo, jotoardhi, makaa ya mawe, urani na madini adimu yanachangia katika mapinduzi ya viwanda vinavyotumia nishati safi na kuibua minyororo mipya ya thamani kama vile uzalishaji wa betri, vifaa vya kielektroniki na gesi za haidrojeni. Katika safari ya Tanzania ya kuelekea kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, mahitaji ya umeme yanatarajiwa kuzidi megawati 70,000 ifikapo mwaka 2050, hali itakayohitaji uwekezaji mkubwa katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio yaliyopatikana, Tanzania bado inakabiliwa na mapungufu ya kimuundo na kiuendeshaji. Uunganishaji wa umeme kwa maeneo ya vijijini bado ni takriban asilimia 36 tu; uhakika wa upatikanaji wa umeme ni mdogo; wakati kuna viwango vikubwa vya upotevu katika njia za usafirishaji na usambazaji wa umeme. Uzalishaji wa umeme kwa kiasi kikubwa unategemea vyanzo vya gesi asilia na maji, huku kiwango cha matumizi ya nishati jadidifu kikiwa chini ya asilimia mbili. Matumizi madogo ya nishati safi ni kikwazo kwa uwekezaji wa sekta binafsi, maandalizi hafifu ya miradi, na mifumo dhaifu ya udhibiti na urekebu yanapunguza kasi ya maendeleo ya sekta. Aidha, Shirika la Umeme Tanzania linakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo upungufu wa fedha, matumizi ya mifumo iliyopitwa na wakati, na muundo wa uendeshaji uliounganishwa kwa ngazi zote unapunguza ufanisi na kudhoofisha ushiriki wa sekta binafsi. Kadhalika, upungufu wa wataalamu wenye ujuzi, matumizi hafifu ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa gridi sanjari na athari za mabadiliko ya tabianchi zinahatarisha uthabiti na ustahimilivu endelevu wa sekta. Vilevile, upanuzi wa biashara ya umeme kikanda unakwamishwa na kukosekana kwa muunganiko wa gridi za umeme za mataifa jirani sambamba na kutokuwiana kwa kanuni za uendeshaji baina yao. Hivyo, ili kukidhi mahitaji ya baadaye ni muhimu kuharakisha kasi ya mageuzi ya kisekta, kukusanya rasilimali fedha kutoka vyanzo vya kijani, na kuongeza matumizi ya teknolojia katika minyororo ya thamani ya nishati.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kufikia mageuzi ya kina katika sekta ya nishati kwa kufanya maboresho ya msingi katika mifumo ya kitaasisi na kifedha. Hii itawezesha kuweka msingi wa awamu mpya ya ukuaji wa viwanda jumuishi. Mageuzi haya yatalenga kubadili mfumo wa uendeshaji wa Shirika la Umeme Tanzania na kulifanya kuwa la kibiashara. Kadhalika, kutenganisha shughuli za kampuni katika makundi huru matatu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ifikapo Juni, 2031. Hatua hii itasaidia kujenga soko la nishati lenye ushindani, ufanisi na uwazi zaidi. Hii itavutia uwekezaji wa sekta binafsi katika uzalishaji na usambazaji wa umeme. Vilevile, Tanzania inahitaji kuboresha miundombinu ya sekta nzima, kuanzia miunganiko ya gridi za kikanda, mifumo ya kisasa ya usimamizi wa gridi pamoja na njia za usambazaji hadi kufikisha umeme kwa kaya zote. Wakati huohuo, ni muhimu kufanya mabadiliko ya kimkakati kuelekea matumizi mseto ya vyanzo vya uzalishaji, hususan nishati jadidifu. Mbinu hizi zitawezesha upatikanaji wa nishati ya uhakika, yenye ustahimilivu na endelevu kwa wananchi wote. Mkakati huu wa mageuzi ya kimuundo na upanuzi wa nishati jadidifu utafungua fursa ya Tanzania kujenga uchumi wa viwanda, na kuiwezesha kuwa kinara wa

maendeleo endelevu yenye uchafuzi mdogo wa mazingira Barani Afrika. Kiambatisho Na. I (3.6.1) kinaainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho Na. II (3.6.1) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.36: Viashiria vya Utendaji vya Nishati*

| Viashiria vya Utendaji | Halisi (Mwaka) | Lengo (2030/31) |
|---|---|---|
| Uwezo wa mitambo wa uzalishaji wa umeme | MW 4,504.9 (2025) | MW 8,000 |
| Kiwango cha matumizi ya umeme kwa kila mtu (kWh) | kWh 170 (2025) | kWh 600 |
| Kiwango cha upotevu wa umeme (%) | 14.2 (2025) | 12.4 |
| Asilimia ya vijiji vyenye umeme na kiwango cha uunganishaji umeme kwa kaya | 49 na 36 (2025) | 55.2 na 42.8 |
| Kaya zenye upatikanaji wa umeme kwa uhakika % | <50–60 | ≥80 |
| Kaya zinazotumia nishati safi ya kupikia % | 30 (2022) | 66 |

### 3.6.2 Mifumo ya Usafirishaji na Uchukuzi Fungamanishi

**Hali Ilivyo:** Usafirishaji fungamanishi na uchukuzi ni kichocheo muhimu cha kuiwezesha Tanzania kufikia azma yake ya kuwa kitovu shindani cha biashara kikanda na kimataifa. Utekelezaji wa Mpango III ulileta mafanikio makubwa katika sekta ya usafirishaji. Kwa upande wa barabara, utekelezaji ulifikia zaidi ya asilimia 95, ikihusisha uboreshaji wa barabara kuu, ujenzi wa madaraja yanayostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi, na barabara za michepuko za kimkakati. Aidha, ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR, uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, pamoja na uimarishaji wa Shirika la Ndege la Tanzania, viliimarisha muunganiko wa usafiri na kupunguza gharama za usafirishaji. Kadhalika, uwekezaji katika bandari na usafiri wa majini, hususan katika ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa, ulisaidia kuimarisha uhusiano wa kiuchumi na kibiashara wa kikanda. Maboresho haya yameweka msingi thabiti wa kuendeleza mfumo fungamanishi wa usafirishaji na uchukuzi kwa njia mbalimbali. Hii ni muhimu katika kuchochea maendeleo ya uchumi wa viwanda, kusetusha muundo wa mauzo nje, na kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika masoko ya kikanda ikiwemo, Eneo Huru la Biashara la Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna mapungufu ya kiutendaji katika ikolojia ya usafirishaji na uchukuzi. Muunganiko hafifu wa mifumo ya usafiri unapunguza ufanisi katika usafiri wa reli na majini, huku muda wa mizigo kukaa bandarini ukiongezeka kutokana na vikwazo vya kiutendaji na kutowiana kwa michakato ya utoaji wa mizigo. Uwezo wa maghala, miundombinu ya minyororo baridi ya hifadhi na vituo vya kimkakati vya usafirishaji bado ni mdogo ikilinganishwa na mahitaji yanayoongezeka ya mauzo nje ya mazao ya kilimo, bidhaa za viwandani na madini. Gharama kubwa za usafirishaji, uratibu hafifu wa majukumu miongoni mwa taasisi za umma na matumizi duni ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa mnyororo wa ugavi vinapunguza ushindani. Kadhalika, tofauti katika mifumo ya urekebu na udhibiti na kasi ndogo ya utekelezaji wa afua za majukwaa ya kisasa ya forodha vinakwamisha ufanisi wa biashara. Ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa miundombinu ya ugavi bado ni mdogo, huku upungufu wa wataalamu wenye ujuzi katika usimamizi wa mizigo, usafirishaji kwa njia za kidijitali na uchambuzi wa mnyororo wa ugavi vikiendelea kuathiri mageuzi ya sekta. Vilevile, mabadiliko ya hali ya hewa mara kwa mara yanaathiri miundombinu ya usafiri na kuongeza gharama za ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kutokana na nafasi yake ya kimkakati katika biashara ya kikanda na kimataifa, Tanzania inaweza kujenga awamu mpya ya mageuzi ya kiuchumi. Mikakati hii itahusisha jitihada za kujiimarisha kiuchumi ili kuweka lango la usafirishaji na uchukuzi fungamanishi wenye ufanisi mkubwa utakaowezesha kuyafikia masoko ya kikanda na kimataifa. Mabadiliko haya yataongozwa na mageuzi ya kina ya mifumo ya kisasa ya biashara na uchukuzi, uanzishaji wa mifumo ya kisasa ya forodha hadi ulipiaji wa nauli na mizigo, ili kupunguza gharama na muda wa ucheleweshaji. Kwa kukamilisha afua za uendelezaji wa usafirishaji katika shoroba za usafirishaji, kama vile reli na bandari za kisasa na kuziunganisha na mtandao wa bandari kavu na mabadilishano ya aina mbalimbali za usafiri, Taifa linaweza kuweka mfumo fungamanishi wa mseto wa usafirishaji na uchukuzi. Mabadiliko haya hayataimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu kikuu cha biashara pekee, bali pia yatafungua fursa nyingi na kubwa, pamoja na kuchochea ukuaji endelevu na jumuishi kiuchumi. Kiambatisho cha I (3.6.2) kinainisha hatua za kimkakati katika kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.6.2) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.37: Viashiria vya Utendaji vya Mifumo Jumuishi ya Usafirishaji*

| Viashiria vya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Mchango wa sekta ya uchukuzi katika pato la taifa kwa bei za sasa (%) | 7.5 | 7.7 |
| Ukuaji halisi wa pato la taifa katika sekta ya uchukuzi (%) | 4.2 | 8.6 |

### 3.6.3 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

**Hali halisi:** Sayansi, teknolojia, na ubunifu ni masuala ambayo, kwa kiasi kikubwa, yametambuliwa kama injini ya kufikia mabadiliko ya Tanzania ya uchumi wa viwanda unaoongozwa na maarifa. Mageuzi yaliyofanyika wakati wa utekelezaji wa Mpango III yalipanua na kuboresha elimu ya ufundi, yakaimarisha vituo vya ubunifu, na kuongeza ushirikiano kati ya taasisi za kitaaluma, serikali, na shughuli za viwanda. Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na kukua kwa matumizi ya mbinu za usimamizi za KAIZEN, kumeimarisha tija, huku vituo vya kukuza teknolojia na Mpango wa Tanzania wa Usimamizi wa Ubunifu na Uboreshaji (TIUMP) ukiboresha uendeshaji biashara. Ongezeko la uwekezaji katika huduma za kidijitali na kuanza kwa matumizi ya Akili Unde kumeweka misingi ya mageuzi ya kiteknolojia. Hata hivyo, uwezo wa ubunifu bado ni mdogo, matumizi ya fedha katika tafiti yakiwa chini ya viwango vya kimataifa na kiwango kidogo cha ubiasharishaji wa matokeo ya ubunifu. Aidha, kasi ya matumizi ya teknolojia zinazochipukia bado ni ndogo, hususan katika sekta za kawaida.

**Changamoto:** Vikwazo vikuu ni pamoja na kiwango kidogo cha ugharamiaji wa shughuli za utafiti na maendeleo mahusiano dhaifu kati ya taasisi za utafiti na shughuli za viwanda, ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika kugharamia shughuli za ubunifu, uwezo duni katika masuala ya STEM, na kiwango kidogo cha ubiasharishaji wa matokeo ya ubunifu. Aidha, mifumo ya kisheria na kikanuni kutoendana kikamilifu na teknolojia zinazoibukia kama vile Akili Unde), roboti, teknolojia ya kibaiolojia, teknolojia ya nanu (nanotechnology), na nyenzo za kisasa, jambo linalochelewesha upatikanaji na uasilishaji wa teknolojia na ukuaji wa kampuni changa (start-ups).

Juhudi nyingi za ubunifu zimetapakaa katika taasisi mbalimbali huku zikikosa ufadhili wa kutosha, na wakati huo huo kukiwa na pengo dhahiri la tofauti za kijinsia katika fani za STEM. Upatikanaji duni wa miundombinu ya kidijitali kwa maeneo ya vijijini na mifumo hafifu ya takwimu inakwamisha mageuzi ya kidijitali. Aidha, ulinzi wa miliki za ubunifu na ugharamiaji duni wa ubunifu ni hali inayopunguza motisha kwa watafiti

na wabunifu. Mapengo haya, kwa ujumla, yanazuia uwezo wa nchi kutumia kikamilifu Sayansi, Teknolojia, na Ubunifu kwa maendeleo ya viwanda na kukuza ushindani katika masoko ya kimataifa.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kwa kuzingatia manufaa ya sayansi na teknolojia, Tanzania inaweza kujenga injini imara ya mageuzi ya kiuchumi kwa kuanzisha mfumo jumuishi na mahiri, ambapo uvumbuzi wa kisayansi na ubunifu wa kiteknolojia vitatafsiriwa kwa urahisi kuwa mafanikio ya kibiashara. Hili litafanikiwa kupitia uanzishaji wa mifumo maalum ya ugharamiaji, kuimarisha ulinzi wa miliki za ubunifu, na kujenga mfumo madhubuti wa uwekezaji kwa njia ya ubia kati ya sekta za umma na binafsi. Hatua hizi zitapunguza pengo lililopo kati ya taasisi za kitaaluma na shughuli za viwanda. Kwa kuharakisha marekebisho ya sheria na kanuni za matumizi ya teknolojia za kisasa, kama vile, Akili Unde teknolojia ya baiolojia, na nyenzo za kisasa, Taifa linaweza kuzalisha kazi zenye staha, fursa nyingi zaidi za ajira, na kuvutia uwekezaji wenye thamani. Mkakati huu wa kimapinduzi, unaowawezesha wabunifu wote, hautachochea ustawi wa shughuli za viwanda pekee bali pia utaifanya Tanzania kuwa kinara kikanda katika shughuli za viwanda zinazotumia maarifa, huku ikijenga uchumi unaojitegemea kikamilifu na ulio tayari kukidhi mahitaji kwa mustakabali wa baadaye. Kiambatisho cha I (3.6.3) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.6.3) kinawasilisha viashiria vya utendaji kwa kina.

*Jedwali 3.38: Viashiria Muhimu vya Utendaji wa Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Nafasi ya Tanzania katika Fahirisi ya Ubunifu Duniani (GII) | 120/133 (2024) | 50th |
| Matumizi Ghafi Utafiti na Maendeleo (GERD) kama asilimia ya Pato la Taifa (GDP) | 0.58(2023) | 0.8 |

### 3.6.4 Utafiti na Maendeleo

**Hali Halisi:** Utafiti na Maendeleo ni kichocheo muhimu cha kuwezesha mabadiliko ya Tanzania kufikia uchumi unaosukumwa na maarifa na ubunifu. Kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita, Serikali na wadau wengine wamechukua hatua za kuimarisha uwezo wa taasisi za utafiti, kupanua vituo vya ubunifu na viatamizi, na kuboresha mifumo ya kisera inayoongoza shughuli za utafiti na ubunifu. Chini ya Mpango III, kulishuhudiwa ongezeko la bajeti za kugharamia shughuli za utafiti, uhawilishaji wa teknolojia, na kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za kitaaluma na viwanda, wakati sekta ya umma ikisaidia uandaaji wa sera kisayansi na kuimarisha viwanda vinavyoibukia. Agenda za utafiti kitaifa, programu za utafiti kisekta, na mashindano ya ubunifu yameanza kusaidia kujenga misingi ya kisayansi katika sekta za kipaumbele kitaifa, hususan kilimo, afya, viwanda na rasilimali asili. Jitihada hizi, zikifungamanishwa na Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050, tayari zinaweka msingi katika kujenga mfumo madhubuti wa kitaifa wa utafiti na ubunifu utakaosaidia kuongeza tija, kugeuza muundo wa uchumi na kuimarisha ushindani wa Tanzania katika masoko ya kikanda na kimataifa.

**Changamoto:** Kwa ujumla, ikolojia ya utafiti na maendeleo nchini inaendelea kukabiliwa na vikwazo vya kimuundo vinavyozuia tija yake kwa taifa. Matumizi katika shughuli za utafiti na maendeleo yamesalia kuwa chini ya asilimia 0.56 ya Pato la Taifa, kiwango ambacho ni kidogo kikilinganishwa na asilimia 1 hadi 2 ya kiwango cha kimataifa kinachotakiwa kufikiwa ili kukuza uchumi endelevu unaoongozwa na maarifa na ubunifu. Taasisi za utafiti zinakabiliwa na upungufu wa fedha, miundombinu, na matumizi

hafifu ya mifumo ya kidijitali ya utafiti . Aidha, uratibu hafifu miongoni mwa taasisi unakwamisha ubadilishanaji wa maarifa, huku ubiasharishaji wa matokeo ya tafiti ukiwa bado ni wa kiwango cha chini kutokana na ugharamiaji mdogo wa ubunifu na usimamizi dhaifu wa sheria za miliki bunifu. Mahusiano kati ya shughuli za viwanda na taasisi za kitaaluma hayajaimarika, jambo linalozuia kasi ya uhawilishaji wa teknolojia. Matumizi ya teknolojia zinazoibukia, kama vile Akili Unde roboti, teknolojia ya baiolojia, na nyenzo za kisasa ni wa  kiwango cha chini, huku idadi ya watafiti ikiwa haitoshelezi matarajio ya kitaifa. Tofauti za kijinsia, ugharamiaji usiokuwa na mahusiano ya kitaasisi, kanuni na taratibu zilizopitwa na wakati, na ushiriki mdogo wa sekta binafsi,  vinadhoofisha uwezo wa Tanzania katika ubunifu na kupunguza uwezekano wa kupanua matumizi ya matokeo ya utafiti.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli za utafiti na maendeleo, Tanzania inaweza kuziba pengo lililopo kati ya taasisi zake za utafiti na mahitaji ya soko, kwa kuhakikisha kuwa mawazo ya kiuvumbuzi yanabadilishwa kuwa thamani halisi ya kiuchumi. Jambo hili litafanikiwa kwa kuanzisha mfumo wa kitaifa unaounganisha moja kwa moja uvumbuzi wa kisayansi na matumizi ya kibiashara. Kwa kubuni mifumo thabiti ya ufadhili na kuimarisha haki miliki bunifu, Taifa litachochea utamaduni hai wa ubunifu ambapo watafiti na wajasiriamali wanawezeshwa kuthubutu. Aidha, kwa kuanzisha ushirikiano madhubuti kati ya sekta za umma na binafsi pamoja na vituo maalum vya ubunifu, Tanzania itajenga misingi ya kimuundo inayohitajika kutafsiri uvumbuzi wa kimaabara kuwa bidhaa na huduma zilizo tayari kwa soko. Jitihada hizi za makusudi, zinazoharakisha utumiaji wa teknolojia zinazoibuka kama vile Akili Una teknolojia ya  baiolojia, hazitachochea tu utofauti wa kiviwanda, bali pia zitaifanya nchi kuwa kiongozi wa kikanda katika utafiti, ubunifu, na viwanda vinavyoongozwa na maarifa, huku ikijenga uchumi unaojitegemea kikamilifu na ulio tayari kwa mustakabali wa baadaye. Kiambatisho cha I (3.6.4) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji cha II (3.6.4) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.39:Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Mfumo Ikolojia wa Utafiti na Maendeleo wenye Ubora*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Malengo (2030/31) |
|---|---|---|
| Matumizi ya kitaifa katika Utafiti na Maendeleo (U&M) kama asilimia (%) ya Pato la Taifa (GDP) | 0.58 (2023) | 0.8 |
| Asilimia ya sera za serikali zinazozingatia matokeo ya utafiti wa ndani | <30 (2024) | 100 |

### 3.6.5 Matumizi ya Takwimu

**Hali Halisi:** Kuwepo kwa ikolojia endelevu ya takwimu ni muhimu katika kuimarisha utawala wa kidijitali, utayarishaji wa mipango inayozingatia ushahidi, pamoja na kuinua ushindani wa taifa. Katika utekelezaji wa Mpango III, Tanzania imepata maendeleo makubwa kupitia kuanzishwa kwa mifumo ya kidijitali ya serikali, ikiwemo mifumo ya usimamizi wa ofisi, malipo ya serikali, usimamizi wa rasilimali watu, huduma za jamii, barua pepe za serikali, ubadilishanaji wa taarifa za kielektroniki, na huduma za serikali kwa njia ya simu. Vilevile, kulianzishwa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data za Serikali, mtandao wa mawasiliano wa serikali, pamoja na matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika sensa ili kuimarisha Mfumo wa Taifa wa Takwimu.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio yaliyopatikana, bado kuna mapungufu makubwa. Mifumo ya mawasiliano ya kidijitali baina ya taasisi bado haijaunganishwa ipasavyo, hali inayozuia ujumuishaji wa takwimu za kiutawala, kijiografia, na takwimu za jumla.

Vilevile, mifumo ya usimamizi wa takwimu bado haishabihiani katika kubadilishana taarifa kwa ufanisi, huku uratibu miongoni mwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa bado haujaunganishwa kikamilifu. Uwezo wa kiufundi katika sayansi ya takwimu, usalama wa mtandao, Akili Unde, na uhandisi wa mifumo bado hautoshelezi, hali inayokwamisha utumiaji wa mbinu za kisasa za kidijitali. Ubora wa takwimu, upatikanaji wake na usanifishaji vinatofautiana sana baina ya sekta, jambo linalodhoofisha uchambuzi wa takwimu kwa wakati. Udhaifu wa usimamizi wa takwimu za faragha na uhakika wa usalama wa mitandao unaathiri imani na kasi ya mabadiliko ya kidijitali. Ushiriki mdogo wa sekta binafsi, uwekezaji hafifu katika kujenga miundombinu ya kidijitali kwa ajili ya utafiti, na kutounganishwa ipasavyo kwa mifumo ya takwimu vinakwamisha ujenzi wa ikolojia ya takwimu ya kitaifa inayofanya kazi kwa ufanisi.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kukabiliana na changamoto zake za takwimu kwa kuanzisha mfumo fungamanishi unaoaminika na wenye mamlaka ya kutoa taarifa sahihi kwa ajili ya mipango ya kitaifa na maamuzi ya kisera. Kwa kuanzisha mfumo unganifu wa takwimu unaoweza kutumiwa na taasisi zote, taifa linaweza kuondokana na mifumo ya taarifa isiyofungamana na kuwa na mfumo mmoja unaochochea ufanisi na ubunifu. Muundo huu mpya, unaotumia teknolojia ya Akili Unde na wenye uwezo wa kuchambua takwimu kwa wakati halisi, hautaboresha tu utawala na utoaji wa huduma, bali pia utaifanya Tanzania kuwa imara zaidi katika zama za kidijitali. Aidha, kwa kuimarisha ushirikiano wa kimkakati kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, sambamba na kujenga uwezo wa rasilimali watu katika maeneo mahususi, nchi inaweza kukuza jamii bora ya wataalamu wa sayansi ya takwimu na wabunifu, na hivyo kuhakikisha kuwa rasilimali hii ya kitaifa inatumika kuchochea ukuaji endelevu unaozingatia ushahidi wa takwimu kwa miaka ijayo. Kiambatisho cha I (3.6.5) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.6.5) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.40: Viashiria vya Utendaji vya Ufuatiliaji wa Mfumo Endelevu wa Takwimu*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Malengo (2030/31) |
|---|---|---|
| Kiashiria cha Utendaji wa Kitakwimu | 103/186 (2023/24) | 50 |
| Fahirisi ya Dunia ya Takwimu Huria | 96/198 (2024/25) | 42 |

### 3.6.6 Mapinduzi ya Kidijitali

**Hali Halisi:** Mageuzi ya kidijitali ni nguzo muhimu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini Tanzania, yanachochea ongezeko la tija, kukuza ubunifu, kuboresha utoaji wa huduma, na kukuza ushindani wa kimataifa. Katika utekelezaji wa Mpango III, mafanikio kadhaa yalipatikana, ikiwemo upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, kuongezeka kwa upatikanaji wa mitandao ya 3G/4G/5G, na kuanzishwa kwa mifumo ya kidijitali ya serikali kama vile mifumo ya malipo ya serikali kwa njia ya kielektroniki, usimamizi wa ofisi za serikali kidijitali, ubadilishanaji wa taarifa za huduma za jamii, dirisha la huduma za jamii, ubadilishanaji wa taarifa kati ya mifumo ya serikali, usimamizi wa rasilimali watu na mishahara, pamoja na huduma za serikali kupitia vifaa vya simu. Kufikia Juni 2025, upatikanaji wa huduma ya intaneti yenye kasi kwa wananchi ulifikia asilimia 92, idadi ya watumiaji wa intaneti ilikuwa zaidi ya milioni 54, na usajili wa laini za simu ulifikia milioni 92.7. Vilevile, kupanuka kwa fursa za kujifunza kwa njia ya mtandao, kuanzishwa kwa vituo vya teknolojia, na programu za kusaidia kampuni changa kumeimarisha uwezo wa vijana katika matumizi ya Akili Unde, ushiriki katika mnyororo wa thamani wa biashara kidijitali, mtandao wa vifaa mahiri, na uundaji wa programu za kompyuta.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio haya, bado kuna vikwazo vinavyoendelea kukwamisha mageuzi ya kidijitali. Maeneo ya vijijini bado yanakabiliwa na upatikanaji mdogo wa mawasiliano na gharama kubwa za intaneti na vifaa, jambo linalopunguza ujumuishi wa kidijitali. Upenyo wa matumizi ya simu janja bado ni asilimia 39. Aidha, upinzani wa kitaasisi dhidi ya mabadiliko ya kidijitali unaendelea, huku mfumo wa usimamizi wa takwimu uliogawanyika ukizuia mifumo kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa ufanisi. Utayari katika masuala ya usalama wa mtandao bado hautoshelezi, hali inayoongeza hatari ya mashambulizi ya kimtandao. Ujuzi wa kidijitali bado unatofautiana kwa kiwango kikubwa na kasi ya uwekaji wa mifumo ya kidijitali katika sekta binafsi bado ni ndogo. Uwekezaji mdogo katika utafiti wa kidijitali, matumizi hafifu ya teknolojia zinazochipukia, na upungufu wa ujuzi katika nyanja za Akili Unde, huduma za kompyuta kwa njia ya mtandao, usalama wa mtandao, na uchambuzi wa hali ya juu wa takwimu vinakwamisha mageuzi. Vilevile, uimara wa miundombinu ya kidijitali bado haujitoshelezi ili kusaidia utoaji wa huduma za kidijitali kwa umma nchini nzima.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kuibua thamani kubwa iliyojificha ndani ya uchumi wake kwa kuweka kipaumbele katika mkakati mpana wa mageuzi ya kidijitali. Hii inajumuisha uboreshaji wa mifumo msingi ya utawala na biashara kupitia kipindi cha mpito kuelekea majukwaa ya kidijitali yaliyo salama, na uundaji wa mfumo madhubuti wa takwimu unaowezesha mifumo kuwasiliana na kubadilishana habari. Kwa kupanua upatikanaji wa huduma za intaneti ya kasi nchi nzima pamoja na kukuza sekta ya ndani ya ubunifu, taifa linaweza kuchochea kufikiwa kwa viwango vya ufanisi ambavyo havijawahi kushuhudiwa, kuvutia uwekezaji mpya, na kuimarisha utoaji wa huduma za umma. Mabadiliko haya ya kimkakati yataimarisha ushindani wa kiuchumi na kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijitali ulio imara na jumuishi. Kiambatisho cha I (3.6.6) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.6.6) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.41:Viashiria Muhimu vya Utendaji (KPIs) kwa Sekta ya Mageuzi ya Kidijitali*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Malengo (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya idadi ya watu wanaotumia intaneti ya kasi | 40 (2025) | >70 |
| Asilimia ya mchango wa TEHAMA katika pato la taifa | 14.3 (2023) | 10 |
| Upenyo wa matumizi ya simu janja (% ya idadi ya watu) | 37 (2025) | >70 |
| Asilimia ya sekta muhimu zinazotumia teknolojia zinazochipukia (Akili Unde, Mtandao wa Vitu, mifumo ya kidijitali ya biashara za hifadhi ya data utunzaji wa miamala, TEHAMA rafiki kwa mazingira) | <15 | >25 |
| Matukio ya mashambulizi makubwa ya kimtandao | 1,200 | <250 |
| Nafasi nchi katika Fahirisi ya Ubunifu Duniani | 120/133 (2024) | 60 |
| Serikali Mtandao (Asilimia) | TBD | TBD |

### 3.6.7 Miundombinu na Huduma za TEHAMA

**Hali Halisi:** Miundombinu na huduma za TEHAMA zimeendelea kuwa msingi muhimu wa kupanua ujumuishi wa kidijitali na kuwezesha shughuli za uchumi wa kisasa nchini. Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha mawasiliano ya kidijitali kupitia upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, utekelezaji wa miradi ya mawasiliano vijijini, na uboreshaji wa huduma za kidijitali za umma. Kufikia mwaka 2025, upanuzi wa mkongo huo ulikuwa umefikia zaidi ya kilomita 14,000 na kuunganisha wilaya 113 nchini. Aidha, upatikanaji wa huduma za 3G/4G/5G ulifikia asilimia 92, na asilimia 26

ya watu walikuwa wameunganishwa. Umiliki wa simu za mkononi katika ngazi ya kaya ulifikia asilimia 85.3, huku usajili wa huduma za fedha kupitia simu ukiongezeka hadi kufikia watumiaji milioni 68. Maendeleo haya yamechochea ukuaji wa biashara ya kidijitali na kuimarisha ujumuishi wa kifedha. Sambamba na hilo, mazingira ya kampuni changa katika sekta ya fedha, teknolojia ya kilimo, na maudhui ya ubunifu ya kidijitali yameongezeka kwa kiasi kikubwa.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado yapo mapungufu yanayohitaji kushughulikiwa. Maeneo ya vijijini na yale ya pembezoni yanaendelea kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa mawasiliano ya kidijitali. Aidha, matumizi ya simu janja bado ni madogo, yakiwa ni asilimia 38 pekee, huku gharama za intaneti zikiwa juu ikilinganishwa na viwango vya kikanda. Uimara wa miundombinu ya kidijitali bado hautoshelezi, huku hatari za usalama wa mtandao zikiendelea kuongezeka. Vilevile, kiwango cha ujuzi wa kidijitali miongoni mwa vijana, walimu, na jamii za vijijini bado ni cha chini, hali inayozuia ushiriki jumuishi katika uchumi wa kidijitali. Katika baadhi ya maeneo, miradi ya miundombinu inakosa uratibu wa kutosha, jambo linalosababisha mwingiliano wa kazi na matumizi yasiyo na tija ya rasilimali. Aidha, teknolojia zinazochipukia kama Akili Unde, Mtandao wa Vitu, na mifumo ya kidijitali ya biashara za hifadhi ya data na utunzaji wa miamala bado hazijatumika ipasavyo kutokana na uwezo mdogo wa kitaasisi, mapungufu ya kifedha, na mahusiano dhaifu ndani ya mfumo wa ikolojia ya ubunifu.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Ili kukabiliana na changamoto hizi, juhudi za kimkakati zinahitajika ili kuruhusu muundo mpya wa ustawi jumuishi, kuziba pengo la kidijitali, na kujenga uchumi himilivu unaoongozwa na maarifa. Hii itatekelezwa kwa kupanua upatikanaji wa miundombinu na vifaa vya kidijitali vilivyo salama, vyenye kasi, na gharama nafuu, pamoja na kuimarisha mawasiliano katika kila pembe ya nchi, ili kuhakikisha kuwa hakuna mwananchi anayebaki nyuma katika zama za kidijitali. Sambamba na hilo, kukuza nguvukazi yenye ujuzi na uelewa wa kidijitali kupitia taasisi maalum za mafunzo, mitaala ya kisasa, na programu endelevu za kujenga uwezo kutaiwezesha nchi kunufaika kikamilifu na rasilimali zake. Aidha, kwa kuimarisha mfumo thabiti wa ikolojia ya ubunifu kupitia ufadhili wa kimkakati, kuanzisha vituo vya teknolojia, na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, Tanzania itajiweka kwenye nafasi nzuri ya kuwa kinara wa kikanda katika matumizi ya teknolojia, ujasiriamali wa kidijitali, na ubunifu wenye thamani kubwa. Hatua hizi zitaiwezesha nchi kuimarisha ushindani wake katika uchumi wa dunia. Kiambatisho cha I (3.6.7) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.6.7) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.42:Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Miundombinu na Huduma za TEHAMA*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Malengo (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya idadi ya watu wanaotumia intaneti ya kasi (broadband) | 40 (2025) | >70 |
| Kiwango cha kitaifa cha ujuzi wa kidijitali (%) | 30 (2024) | >60 |
| Nafasi katika fahirisi ya usalama wa mtandao barani Afrika | ya 5 | 3 |
| Kiwango cha upenyu wa intaneti % | 79.3 (2025) | 98 |
| Idadi ya watu vijijini wenye uwezo wa kupata intaneti % | <25 (2024) | ≥65 |
| Wastani wa gharama ya GB 1 ya data ya simu kama asilimia ya kipato cha mwezi | 3.5 (2024) | ≥1 |

### 3.6.8 Huduma za Mawasiliano na Posta

**Hali Halisi:** Huduma za mawasiliano na posta zilizo imara, zinazoaminika na zenye ufanisi ni nyenzo muhimu katika kuharakisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii nchini. Huduma hizi huchochea biashara, huimarisha upatikanaji wa huduma, huendeleza ujumuishi wa kifedha, na kusaidia ubunifu wa kidijitali. Katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, sekta ndogo zinazojumuisha mawasiliano ya simu, posta, usafirishaji wa vifurushi, intaneti, na utangazaji zimekua kwa kasi kubwa. Utekelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, kipindi cha mpito kutoka utangazaji wa analojia kwenda kidijitali, pamoja na kuimarika kwa ushindani katika soko la mawasiliano vimeongeza upatikanaji na ubora wa mawasiliano nchini. Taasisi kama Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Shirika la Posta Tanzania, na kampuni binafsi za usafirishaji wa vifurushi zimeimarisha usimamizi wa sekta, ushindani wa soko, na ulinzi wa walaji. Kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kidijitali, mawasiliano ya simu, na huduma za fedha kwa njia ya simu kumechochea ukuaji wa biashara mtandaoni na kuboresha mifumo ya kisasa ya usafirishaji.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio yaliyopatikana, bado kuna vikwazo mbalimbali. Maeneo ya vijijini na yale ya pembezoni yanaendelea kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa mawasiliano kutokana na gharama kubwa za uwekezaji na miundombinu duni ya nishati. Uwezo wa kumudu gharama za vifaa na intaneti bado hauko katika kiwango kinachohitajika, na upenyo wa matumizi ya simu janja uko chini ya viwango vinavyotakiwa kwa ajili ya ushiriki mpana wa kidijitali. Uunganishaji hafifu kati ya mifumo ya posta, usafirishaji wa vifurushi, na mifumo ya kidijitali umekuwa changamoto kwa biashara mtandaoni na ufikishaji wa huduma na bidhaa katika hatua za mwisho. Miundombinu ya posta imepitwa na wakati, uwezo wa mifumo kuwasiliana na kubadilishana taarifa miongoni mwa watoa huduma za usafirishaji wa vifurushi ni mdogo, na watoa huduma wasio rasmi wanatawala soko la ufikishaji huduma hatua za mwisho, hivyo kupunguza uaminifu wa jamii. Upungufu wa ujuzi katika usimamizi wa shughuli za usafirishaji, uhandisi wa mawasiliano, na uendeshaji wa huduma za kidijitali unadhoofisha ushindani wa sekta hii. Aidha, mgawanyiko wa kitaasisi, mapungufu ya kikanuni, na matumizi madogo ya teknolojia zinazochipukia hupunguza ufanisi wa huduma na kuchelewesha ufungamanishi wa mitandao ya mawasiliano ya kikanda na kimataifa.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kuleta mageuzi makubwa katika sekta za mawasiliano na usafirishaji kwa kuunda mtiririko jumuishi na wenye ufanisi mkubwa wa bidhaa, habari, na huduma. Kwa kuunganisha mifumo ya posta, usafirishaji wa vifurushi, na biashara mtandaoni, taifa litaweza kutumia mtandao mmoja unaowezeshwa na Akili Unde ili kupunguza kwa kiasi kikubwa muda wa ufikishaji wa huduma na bidhaa. Uboreshaji huu wa kisasa, ukijumuishwa na mifumo thabiti ya usalama wa mtandao pamoja na nguvukazi yenye ujuzi wa kidijitali, hautaboresha tu ubora wa huduma bali pia utaifanya Tanzania kuwa kitovu kikuu cha usafirishaji wa kikanda. Kiambatisho cha I (3.6.8) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.6.8) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.43: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Huduma Imara na za Kuaminika za Mawasiliano na Usafirishaji Vifurushi*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya idadi ya watu wenye uwezo wa kupata huduma za posta ndani ya kilomita 5 | 75 (2023) | ≤95 |
| Thamani ya miamala ya biashara mtandaoni (e-commerce) kama asilimia (%) ya Pato la Taifa (GDP) | 1.5 (2022) | ≤5 |

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya idadi ya watu waliofikiwa na intaneti ya kasi ya mkononi (4G) | 90 (2024) | 98 |
| Asilimia ya idadi ya watu waliofikiwa na intaneti ya kasi ya mkononi (5G) | 26 (2024) | 70 |
| Alama ya Fahirisi ya Taifa ya Ushindani wa Kidijitali (kipimo cha 0-100) | 32 (2023) | ≤50 |

### 3.6.9 Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji

**Hali Halisi:** Mazingira wezeshi ya biashara na mfumo thabiti wa kuwezesha uwekezaji ni nguzo muhimu katika kuharakisha mchakato wa kujenga uchumi wa viwanda nchini Tanzania, kuongeza uwezo wa mauzo ya nje, na kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, mageuzi yamefanyika kuboresha ufanisi wa mifumo ya udhibiti na urekebu, kuimarisha usimamizi wa kodi, na kupanua utoaji wa huduma za kidijitali kupitia taasisi, hususan Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Uwekezaji. Jitihada mahsusi, zikiwa ni pamoja na Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI I) na mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, zimeongeza uwazi, kurahisisha ufikiaji wa maamuzi, na kukuza imani kwa wawekezaji. Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Uwekezaji na Uzalishaji wa Mauzo ya Nje Tanzania na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania kumeimarisha taratibu za uwekezaji na uendeshaji wa biashara. Hii imesaidia kuinua mchango wa sekta binafsi, ambapo kwa sasa inachangia takribani asilimia 80 katika pato la taifa, wakati wastani wa uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja ukifikia dola za Marekani bilioni 2 kwa mwaka.

**Changamoto:** Licha ya mageuzi haya, vikwazo kadhaa bado vinaathiri mazingira ya biashara na uwekezaji. Kukosekana kwa uwiano wa kanuni na taratibu za urekebu na udhibiti, ucheleweshaji na uwepo wa taratibu ngumu za kiutawala, na mabadiliko ya kisera yasiyotabirika hupunguza imani ya wawekezaji. Aidha, miundombinu isiyotosheleza, usimamizi dhaifu wa mikataba, na ulinzi usiotosheleza wa haki miliki vinakwamisha kasi ya uwekezaji wa sekta binafsi. Isitoshe, kasi ya urasimishaji wa biashara ndogo na za kati bado hairidhishi, huku wanawake wajasiriamali wakikumbana na changamoto za upatikanaji wa mitaji, masoko, na namna ya kukidhi masharti ya kuwekeza katika sekta zenye tija na faida kubwa. Aidha, mifumo ya kidijitali isiyowasiliana miongoni mwa taasisi inapunguza ufanisi katika usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na upatikanaji wa huduma wezeshi kwa wawekezaji. Gharama kubwa za uendeshaji, upatikanaji mdogo wa mikopo ya muda mrefu, na ucheleweshaji wa usuluhishi wa migogoro ya kibiashara vinaendelea kuathiri ushindani.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania italazimika kufanya mageuzi ya msingi ili kubadili muundo wa uendeshaji wa uchumi wake kwa kuondokana na vikwazo vya kikanuni na kuelekea katika mfumo rahisi unaowezesha kutumia fursa kwa ufanisi. Kwa kuimarisha uhusiano kati ya uthabiti wa usimamizi na mageuzi ya matumizi ya mifumo ya teknolojia ya kidijitali, nchi inaweza kujenga mazingira ya biashara yanayowezesha ushindani wa kimataifa na ujumuishi mpana. Mfumo huu, pamoja na mengine, utasaidia kuwajengea uwezo wajasiriamali wa ndani na kuvutia uwekezaji wa nje katika maeneo ya kimkakati, kuharakisha urasimishaji wa shughuli za kiuchumi, na kuchagiza kasi ya kufikiwa kwa malengo ya Dira 2050 ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uchumi na biashara ya kikanda. Kiambatisho cha I (3.6.9) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.6.9) kinawasilisha viashiria vya utendaji kwa kina.

*Jedwali 3.44: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uhamasishaji wa Uwekezaji*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Fahirisi ya ubora wa udhibiti (pointi): (Kiwango cha +2.5 hadi -2.5 yaani Imara hadi Dhaifu) | -0.59 (2023) | 1.0 |

### 3.7 Kuimarisha Misingi ya Uendelevu wa Taifa

Mafanikio ya Mpango huu yatategemea kuwepo kwa misingi imara ya uendelevu wa taifa inayozingatia utawala bora, demokrasia, umoja wa kitaifa, usalama, na mabadiliko chanya ya fikra yanayoendana na mageuzi yanayohitajika. Misingi hii itasaidia kuimarisha uwazi, uwajibikaji, usimamizi makini wa rasilimali za umma, na kujenga mazingira tulivu yanayowezesha ukuaji himilivu wa uchumi na jumuishi. Kwa muktadha huu, mageuzi ya mifumo ya taasisi ni muhimu kufanyika kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa utendaji, kuboresha mifumo ya kikanuni, na kuchochea ubunifu, tija, na mgawanyo wa rasilimali kwa usawa.

Aidha, Katiba ni nguzo muhimu katika kuhakikisha uthabiti wa sera, ufanisi, uwajibikaji wa taasisi, na ushiriki mpana wa wananchi. Vilevile, kuwepo kwa mifumo madhubuti ya usawa, uwajibikaji, na uthabiti wa sheria pamoja na mamlaka kamili ya serikali za mitaa zenye ufanisi huongeza ujumuishaji wa jamii. Hivyo, Mpango umeainisha vipaumbele vinne vya kimkakati: kuimarisha mifumo ya taasisi ya utawala wa kidemokrasia; kuboresha uendeshaji wa serikali za mitaa; kuendeleza utawala na usimamizi wa kisasa wa takwimu; na kuchochea mabadiliko ya kifikra yanayoendana na mageuzi ya kiuchumi ili kudumisha uendelevu wa taifa.

#### 3.7.1 Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu

**Hali Halisi:** Tanzania ni miongoni mwa nchi barani Afrika zenye amani na utulivu. Hii inatokana na kuwa na mfumo imara wa taasisi unaozingatia demokrasia na kuheshimu misingi ya utawala wa sheria. Katika utekelezaji wa Mpango III, Tanzania ilifanya mageuzi yaliyosaidia kuimarisha uwajibikaji, uwazi, na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Aidha, kuanzishwa kwa mifumo ya kidijitali kama mfumo wa malipo ya serikali kwa njia ya kielektroniki, mfumo unganishi wa taarifa za usimamizi wa fedha, na mfumo wa ununuzi wa kielektroniki kuliongeza nidhamu ya kifedha na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya rasilimali. Vyombo vya usimamizi, vikiwemo Bunge, Mahakama, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, viliimarisha usimamizi wa sheria, kuhakikisha uadilifu, na kuimarisha imani ya wananchi kwa taasisi za umma.

**Changamoto:** Hata hivyo, changamoto bado zinaathiri ufanisi wa utawala nchini. Fahirisi ya Mwenendo wa Rushwa kwa mwaka 2024 ilifikia alama 41 kati ya 100, ikiashiria kuwepo kwa vitendo vya rushwa. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kutegemea mgao wa ruzuku kutoka serikali kuu, hali inayopunguza uwezo wake wa kutatua kwa haraka changamoto zinazowakabili wananchi.

Hii inachangia tofauti za maendeleo kimaeneo. Aidha, uratibu usioridhisha, ushiriki mdogo wa wananchi, na ucheleweshaji wa maamuzi hupunguza ufanisi wa utekelezaji wa sera. Vilevile, kuwepo kwa vihatarishi vipya, kama vile uhalifu wa mtandaoni, kunatishia ustahimilivu wa mifumo ya taasisi na mshikamano wa kitaifa.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inakusudia kuimarisha mifumo ya utawala thabiti, wa uwazi, na unaomweka mwananchi kuwa kitovu cha mabadiliko ya mifumo ya kisheria na kitaasisi. Mageuzi haya yatatekelezwa katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango IV ikiwa ni pamoja na kuhuisha mchakato wa kuboresha Katiba, kuimarisha uwajibikaji na kuendelea kuimarisha utawala bora. Vilevile, serikali itapanga upya muundo wa sekta ya umma kwa kuzingatia mahitaji halisi na kuweka mfumo imara wa kudhibiti uhalifu wa mtandaoni. Kwa kuziimarisha mamlaka za serikali za mitaa kupitia ugatuaji wa vyanzo vya mapato na kuainisha ushiriki wa wananchi kikatiba, taifa litaweza kufikia maendeleo yanayoendana na mahitaji halisi ya kimaeneo na kwa usawa. Maboresho haya yatasaidia kuongeza uadilifu na uwazi kwa kutumia mifumo ya kidijitali. Hivyo, yataongeza imani ya wananchi kwa serikali, kuinua ufanisi, kuongeza ustahimilivu, na kuhakikisha serikali jumuishi kwa wananchi wake wote. Kiambatisho cha I (3.7.1) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.7.1) kinawasilisha viashiria vya utendaj.

*Jedwali 3.45: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Fahirisi ya utulivu wa kisiasa, kutokuwepo kwa ghasia na ugaidi | -0.05 (2023) | 0.10 |
| Fahirisi ya ufanisi wa serikali | -0.46 (2023) | -0.30 |
| Nafasi ya Tanzania katika Fahirisi ya Mtazamo wa Rushwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki | Nchi ya 2 kwa kuwa na rushwa ndogo (2024/25) | 1 |
| Nafasi katika Fahirisi ya Utawala wa Sheria miongoni mwa nchi zenye kipato cha chini na kati | 15/37 (2024) | 10 |

### 3.7.2 Serikali za Mitaa Thabiti na Zenye Ufanisi

**Hali Halisi:** Serikali za Mitaa zinaendelea kuwa nguzo muhimu katika kufikia mabadiliko jumuishi na kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa usawa. Katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, Tanzania imepiga hatua katika ugatuaji wa madaraka kupitia sera ya ugatuaji wa madaraka na mpango wa mageuzi ya serikali za mitaa, pamoja na ruzuku za kifedha zilizotolewa katika utekelezaji wa Mpango III. Mageuzi haya yameongeza upatikanaji wa huduma za elimu, afya na maji katika ngazi ya jamii. Kamati za Maendeleo za Kata na mikutano mikuu ya vijiji vimeimarisha uwajibikaji katika ngazi za msingi. Aidha, kuanzishwa kwa mifumo ya kidijitali ya ukusanyaji wa mapato kumeimarisha uwazi wa kifedha na ukusanyaji wa mapato katika ngazi ya halmashauri.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio hayo, ugatuaji wa madaraka bado haujakamilika kikamilifu. Zaidi ya asilimia 85 ya bajeti za mamlaka za serikali za mitaa bado inategemea ruzuku kutoka Serikali Kuu, jambo linalozuia mamlaka kamili na uwezo wa kutoa majibu ya haraka kwa mahitaji ya wananchi. Uratibu hafifu wa taasisi, mwingiliano wa majukumu, upungufu wa watumishi, na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha vinakwamisha upangaji wa mipango na utekelezaji wake. Katika maeneo ya vijijini, uwezo mdogo wa kidijitali, ushiriki hafifu wa wananchi, na usimamizi usiofaa vinaendelea kuathiri utoaji wa huduma, hali inayochochea tofauti za maendeleo kati ya mikoa, ambapo umaskini wa kipato unazidi asilimia 40 katika baadhi ya wilaya.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kufanya mabadiliko ya kimsingi katika mfumo wa utawala kuanzia ngazi za msingi kwa kuziwezesha serikali za mitaa

na jamii kama wadau wakuu na injini za maendeleo. Mabadiliko haya yataondokana na utaratibu usiopokea mabadiliko wa udhibiti wa serikali kuu kwa kuziwezesha serikali za mitaa kupitia ugatuaji wa fedha. Aidha, kujenga mifumo madhubuti ya wananchi kutoa mrejesho wa maoni kutasaidia kuhakikisha kuwa maendeleo yanatokana na mahitaji halisi ya maeneo na yanasambazwa kwa usawa. Sambamba na kujengea uwezo ngazi za serikali za mitaa, maboresho haya yatahakikisha utoaji wa huduma kwa ufanisi, uwazi, na utoaji wa majibu stahiki kwa watu wanaohudumiwa. Uwezeshaji huu wa kuanzia ngazi ya chini, utakaochochewa na uratibu na usimamizi thabiti wa kitaifa, utajenga ushiriki na umiliki wa jamii ulio na usawa zaidi, himilivu, na ulioimarishwa. Kiambatisho cha I (3.7.2) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.7.2) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.46: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Kujenga Utawala wa Serikali za Mitaa Imara na Ufanisi*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia (%) ya huduma zilizowekwa katika mifumo ya kidijitali katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) | 25 (2024) | ≤80 |
| Fahirisi ya kuridhika kwa wananchi (kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa - LGAs) | 40 (2024) | ≤70 |
| Kiwango cha bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) katika % Bajeti ya Taifa | (TBD) | TBD |
| Kiasi cha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) katika % mapato yote | (TBD) | TBD |
| Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) zenye hati safi za ukaguzi (zilizokidhi vigezo) | <40 (2024) | ≤80 |

### 3.7.3 Matumizi Sahihi ya Takwimu

**Hali Halisi:** Usimamizi mahiri wa matumizi ya teknolojia za kidijitali na takwimu ni nguzo muhimu katika kuwezesha Tanzania kufikia kuwa taifa lenye uwajibikaji, ufanisi, na uwazi, linalotoa huduma kwa usawa na kwa kumlenga mwananchi moja kwa moja. Hatua hizi zimeweka msingi imara wa matumizi ya teknolojia katika kuandaa mipango kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi. Vilevile, yataimarisha utawala wa uwazi na kuchochea ubunifu unaohitajika ili kufikia malengo ya Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050. Katika kipindi cha muongo uliopita, serikali imepata mafanikio kupitia matumizi ya mifumo ya kidijitali kama Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mfumo Unganishi wa Forodha, sanjari na upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Hatua hizi zimeimarisha mawasiliano, kuongeza uwazi wa kifedha, na kupanua upatikanaji wa taarifa za serikali, hali iliyoongeza ufanisi na uwajibikaji katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali, na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Changamoto:** Licha ya mafanikio hayo, mifumo ya kidijitali bado haijaunganishwa kikamilifu na inatofautiana kiuwezo. Hali hii inapunguza ufanisi wake katika kuchochea kikamilifu mageuzi yanayohitajika. Taasisi nyingi bado zinafanya kazi bila kuwasiliana na nyingine, na mifumo ya uratibu na usimamizi ikiwa dhaifu. Aidha, taasisi hizi zinawekeza kwa kiwango kidogo katika kujenga uwezo wa uchambuzi wa takwimu, usimamizi wa usalama wa mtandao, na maendeleo ya ujuzi wa kidijitali, hali inayozidi kuathiri ufanisi wa kitaasisi. Matumizi ya teknolojia za kisasa kama Akili Unde, mifumo ya kidijitali ya kuhifadhi kumbukumbu za miamala ya kibiashara, na huduma za kompyuta kwa njia ya mtandao bado ni madogo. Changamoto ya ujumuishi wa kidijitali inaendelea kuwepo,

hususan kwa wanawake, vijana, na wakazi wa maeneo ya vijijini. Sekta muhimu kama afya, elimu, na kilimo bado zinatumia mifumo ya takwimu isiyounganishwa, jambo linalokwamisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati halisi na ubadilishanaji wa taarifa. Hii inahitaji agenda ya mageuzi yenye uratibu madhubuti, inayojikita katika falsafa ya Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi, na Kujenga Upya ili kuziba pengo la kidijitali, kuoanisha mifumo, na kujenga upya imani ya wananchi kupitia majukwaa salama, jumuishi, na himilivu.

**Maeneo na Afua za Kimkakati:** Juhudi madhubuti zimeelekezwa katika kuanzisha kipindi kipya cha utawala kwa kufanya mabadiliko ya kimsingi kutoka mfumo wa usimamizi unaojikita katika mamlaka kuu kuelekea mfumo wa ugatuaji wa madaraka unaomweka mbele mwananchi. Mageuzi haya makubwa yatafikiwa kwa kuweka takwa la kisheria litakalohakikisha uhuru wa kifedha wa serikali za mitaa, kurasimisha mifumo madhubuti ya maoni ya wananchi, na kufungamanisha zana za kidijitali ili kuhakikisha kila sauti inasikika na kila uamuzi unazingatia takwimu. Muundo huu mpya hautaboresha tu utoaji wa huduma na uwajibikaji, bali pia utajenga utamaduni uliokita katika demokrasia shirikishi na kuimarisha dola iliyo himilivu na jumuishi kuanzia ngazi ya msingi. Kiambatisho cha I (3.7.3) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.7.3) kinawasilisha viashiria vya utendaji.

*Jedwali 3.47: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Kuimarisha Utawala wa Kidijitali na Usimamizi Mahiri wa Takwimu*

| Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo | Halisi (Mwaka) | Shabaha (2030/31) |
|---|---|---|
| Asilimia ya huduma za msingi za serikali zinazopatikana mtandaoni | 45 (2025) | 95 |
| Asilimia ya idadi ya watu wenye Vitambulisho vya Kidijitali vilivyounganishwa na huduma-pepe za umma, kwa mchanganuo wa vijijini | 25 (2025) | 75 |
| Asilimia ya idadi ya watu wenye Vitambulisho vya Kidijitali vilivyounganishwa na huduma-pepe za umma, kwa mchanganuo wa mijini | 40 (2025) | 90 |
| Asilimia ya sekta zinazotumia mifumo ya takwimu yenye uwezo wa kuwasiliana na kubadilishana habari | 20 (2025) | 90 |
| Sehemu ya Wizara, Idara, Wakala za Serikali (MDAs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) zenye mifumo ya TEHAMA inayoweza kuwasiliana % | 20 (2024) | 40 |

### 3.7.4 Mabadiliko ya Mitazamo na Fikra

**Hali Halisi:** Kuchochea mabadiliko ya kifikra ni msingi wa kimkakati katika mageuzi ya Tanzania ili kuhakikisha kuwa maboresho ya sera na taasisi yanatafsiriwa kuwa matokeo halisi na yanayopimika. Katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, mageuzi ya ugatuaji wa madaraka, matumizi ya mifumo ya kidijitali, na uimarishaji wa utawala bora yameongeza uwazi, uwajibikaji, na ubora wa utoaji wa huduma.

Aidha, mabadiliko haya yamejenga utamaduni wa utumishi wa umma unaozingatia matokeo. Mafanikio haya yanaonyesha kukua kwa uwezo wa nchi katika kutekeleza mageuzi yanayomlenga mwananchi. Falsafa ya vichocheo vinne: Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi, na Kujenga Upya ina maanisha mfumo jumuishi wa kuoanisha maadili, ubunifu, na wajibu wa pamoja kati ya serikali, sekta binafsi, na jamii ili kudumisha mageuzi ya kitaifa.

**Changamoto:** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado zipo changamoto za kitaasisi zinazochelewesha upokeaji na utekelezaji wa mageuzi. Maadili ya kazi yasiyoridhisha, mwitikio hafifu katika utekelezaji wa sera, na upungufu wa uwajibikaji vinakwamisha ubunifu na ufanisi. Mtazamo wa kuwa serikali pekee ndiyo injini ya maendeleo unapunguza uwajibikaji wa wananchi na mchango wa sekta binafsi. Aidha, ushiriki mdogo wa wananchi, kanuni wezeshi zisizotosheleza, na mifumo ya motisha isiyolingana na malengo ya utendaji ni miongoni mwa changamoto zinazoathiri utendaji na ufanisi. Hali hii inaonyesha wazi kuwa mageuzi hayawezi kuzaa matokeo endelevu bila kubadilisha fikra, mitazamo, na utamaduni wa kufanya kazi katika ngazi zote.

**Maeneo ya Hatua za Kimkakati:** Tanzania inaweza kufanya mabadiliko ya kina ya kitamaduni na kitaasisi kwa kuingiza falsafa ya mabadiliko katika mifumo ya utawala na utumishi wa umma. Mwelekeo huu unalenga kuhamisha mfumo kutoka katika utamaduni wa kufuata taratibu pekee kuelekea katika utamaduni wa uwajibikaji, ubunifu, na uwezeshaji wa wananchi. Juhudi hizi zitaimarishwa kwa kuanzisha kitengo cha mageuzi cha ngazi ya juu kitakachosimamia uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji. Chombo hiki kitakuza utamaduni wa uadilifu na ubunifu na kuhakikisha kuwa mageuzi yanamilikiwa na jamii kwa upana, badala ya kuonekana kama maelekezo ya kutoka juu kwenda chini. Mageuzi haya yanayozingatia maadili na manufaa ya wote, yatakuwa msingi wa kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu nchini. Kiambatisho cha I (3.7.4) kinainisha hatua za kimkakati na kipindi cha utekelezaji, wakati Kiambatisho cha II (3.7.4) kinawasilisha viashiria vya utendaji kwa kina.

*Jedwali 3.48: Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa Kukuza Mabadiliko ya Mtazamo ili Kuweka Mizizi ya Mageuzi*

| **Kiashiria cha Ngazi ya Matokeo** | **Halisi (Mwaka)** | **Shabaha (2030/31)** |
|---|---|---|
| Fahirisi ya Maendeleo ya Jamii (Alama) | 57.74 | 65+ |

# MUHTASARI – SURA YA TATU

MPANGO IV · SURA YA 3

## Mwelekeo na Mbinu Mkakati

### Kugeuza vipaumbele kuwa afua za kichocheo

Mkusanyiko madhubuti wa afua za kichocheo, mageuzi na uwekezaji unaogeuza vipaumbele vya maendeleo vya Tanzania kuwa hatua zinazopimika na zilizopangwa — kila kundi linajengwa juu ya jingine kuegemeza Mpango IV kwenye Dira 2050.

| | |
|---|---|
| **6** MAENEO YA KIPAUMBELE | **48** VIPENGELE |
| **200+** VIASHIRIA | **$118B** PATO LENGWA IFIKAPO 2031 |

MPANGO IV · Sura ya 3 — *Mwelekeo na Mbinu Mkakati · 2026/27–2030/31*

MUUNDO WA MWELEKEO

## Makundi Sita ya Afua Yanayohusiana

Kutoka masuala muhimu (Sura 2) → afua za kimkakati (Sura 3) → viashiria na shabaha (Kiambatisho II). Kila kundi linajengwa juu ya jingine kuegemeza Mpango IV kwenye mwelekeo wa Dira 2050.

3.2 · VIPENGELE 3
**Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani**
Utulivu wa uchumi jumla · uhimilivu wa kifedha · ustahimilivu wa sekta ya nje.

3.3 · VIPENGELE 13
**Mageuzi ya Sekta Muhimu**
Kilimo · viwanda · madini · utalii · fedha · biashara · nyumba.

3.4 · VIPENGELE 12
**Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu**
Elimu · nguvukazi · afya · kinga ya jamii · tabaka la kati.

3.5 · VIPENGELE 7
**Hifadhi ya Mazingira na Tabianchi**
Uhifadhi · ukuaji wa miji · tabianchi · biashara ya kaboni · uchumi wa buluu.

3.6 · VIPENGELE 9
**Kutumia Vichocheo vya Maendeleo**
Nishati · usafirishaji · sayansi na teknolojia · utafiti · kidijitali · TEHAMA.

3.7 · VIPENGELE 4
**Misingi ya Uendelevu wa Taifa**
Utawala · serikali za mitaa · utawala wa kidijitali · mabadiliko ya fikra.

MPANGO IV · Sura ya 3 — *Makundi Sita ya Kimkakati*

DASHIBODI YA VIASHIRIA VIKUU

## Kiwango cha Msingi 2024/25 → Shabaha 2030/31

Viashiria vikuu vilivyochaguliwa katika makundi matatu ya kimaudhui — Uchumi, Watu, na Kijani na Vichocheo — vinavyoegemeza ufuatiliaji wa matokeo katika makundi yote sita.

### UCHUMI

| Kiashiria | Kiwango cha Msingi | Shabaha |
|---|---|---|
| Pato la Taifa (USD bn) | 81.5 | 118 |
| Ukuaji Halisi wa Pato | 5.5% | 10.5% |
| Uwekezaji kutoka Nje (USD M) | 1,718 | 8,366 |
| Mauzo ya Bidhaa za Viwandani | 18.6% | 29.6% |

### WATU

| Kiashiria | Kiwango cha Msingi | Shabaha |
|---|---|---|
| Ukosefu wa Ajira 15+ | 6.2% | 4.4% |
| Bima ya Afya | 67.8% | 100% |
| Matarajio ya Kuishi | 68.3 | 70.4 |
| Tabaka la Kipato cha Kati | 12% | 18% |

### KIJANI NA VICHOCHEO

| Kiashiria | Kiwango cha Msingi | Shabaha |
|---|---|---|
| Umeme wa Nishati Mbadala | 61.8% | 75% |
| Nishati Safi ya Kupikia | 6.9% | 75% |
| Umeme (MW) | 4,505 | 8,000 |
| Upatikanaji wa Intaneti | 79% | 98% |

MPANGO IV · Sura ya 3 *Dashibodi ya Viashiria · Shabaha Kuu*

MANTIKI YA MAGEUZI FUNGAMANISHI

## Njia Zimepangwa na Zinaimarishana

Kila kundi linafungua jingine — likiegemea Dira 2050. Misingi inawezesha sekta, ambazo zinawawezesha watu, ambao kwa upande wao wanalinda mustakabali.

**1**
**Misingi Kwanza**
Utulivu wa uchumi jumla, nidhamu ya kifedha na ustahimilivu wa sekta ya nje vinatengeneza mazingira tabirifu na wezeshi kwa uwekezaji.

**2**
**Kufungua Sekta**
Sekta za uzalishaji na huduma zinaongeza uongezaji thamani na mauzo nje — kilimo, viwanda, madini, mafuta na gesi.

**3**
**Kuwezesha Watu**
Elimu, ujuzi, afya, kinga ya jamii na maendeleo jumuishi vijijini vinajenga nguvukazi inayochochea mageuzi.

**4**
**Kulinda Mustakabali**
Hifadhi ya mazingira, ustahimilivu wa tabianchi na misingi ya uendelevu vinalinda maendeleo endelevu.

| USTAWI | UJUMUISHI | HAKI | KUJITEGEMEA |
|---|---|---|---|
| Pato $81.5B → $118B | Tabaka la kati 12% → 18% | Bima ya afya 100% | Uzalishaji wa ndani · ujuzi |

MPANGO IV · Sura ya 3 *Muhtasari · Mantiki ya Mageuzi Fungamanishi*











# SURA YA NNE: PROGRAMU ZA KIELELEZO







# SURA YA NNE
# PROGRAMU ZA KIELELEZO

## 4.1 Muhtasari

Sura hii inaeleeza namna Mpango IV unavyotafsiri afua na mwelekeo wa kimkakati ulioainishwa katika Sura ya Tatu kwa kuainisha programu chache zenye matokeo makubwa. Wakati Sura ya Tatu ina wigo mpana wa afua zote za kipindi chote cha Mpango, sura hii inatumia Kanuni ya Ufanisi ya Pareto ya uwiano wa 20:80 kubainisha asilimia 20 ya afua za kimkakati zenye uwezo wa kuchangia takriban asilimia 80 au zaidi ya matokeo tarajiwa ya Mpango. Matokeo hayo yanajumuisha kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi, kuimarisha ushindani, kuharakisha mageuzi makubwa ya muundo wa uchumi, kuongeza tija na kupanua upatikanaji wa fursa za ajira zenye staha.

Kwa kuzingatia kanuni ya ufanisi ya Pareto, Sura hii imechagua afua na miradi michache ya kimkakati yenye uwezo mkubwa wa kuchochea matokeo, na kuifungamanisha katika programu za kielelezo. Utekelezaji wake unatarajiwa kuharakisha ukuaji wa uchumi, kuongeza tija katika uzalishaji, na kuimarisha uchumi wa viwanda.

Vilevile, utekelezaji wake utachochea maendeleo ya teknolojia, kuimarisha mifumo ya utawala, na kuweka msingi imara wa mageuzi endelevu ya uchumi na ustawi wa jamii nchini. Aidha, programu hizi zinaunganisha matumizi ya rasilimali zinazopatikana ndani ya eneo la programu ili kujenga minyororo ya thamani husika. Kwa ujumla, programu za kielelezo zimechaguliwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kuongeza thamani, kudhibiti mtawanyo wa rasilimali usiokuwa na tija, kuwianisha majukumu, kuondoa mwingiliano wa kitaasisi, na kuongeza kasi pamoja na ufanisi katika utekelezaji wa Mpango.

## 4.2 Vigezo Vilivyotumika katika Uteuzi wa Programu za Kielelezo

Kila programu ya kielelezo imepitiwa na kutathminiwa kwa kutumia vigezo vinavyoendana na mwelekeo wa kimkakati wa Mpango IV. Vigezo hivyo ni:

i. Uwianifu wa Afua za Programu na Malengo ya Dira 2050, Mpango Elekezi 2050 na Mpango IV;
ii. Uwezo wa programu kuleta matokeo makubwa ya kijamii na kiuchumi, hususan katika kuzalisha ajira, kuongeza thamani, ujumuishi na kuongeza tija;
iii. Mchango wa programu katika kuleta maendeleo endelevu na ustahimilivu, hususan, mbinu za maendeleo zinazoendana na mabadiliko ya tabianchi, uzalishaji mdogo wa kaboni na zenye uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi;
iv. Utayari wa utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kukamilika au hatua za mwisho za kukamilisha upembuzi yakinifu wa miradi, kuwa na vibali vyote muhimu, kuanza kwa kazi za awali, na upatikanaji wa fedha za utekelezaji;
v. Kiasi cha uhusiano na mfungamano wa kisekta, hususani mfungamani wa programu na mifumo ya kitaifa ya miundombinu, usafirishaji na uchukuzi, TEHAMA na nishati.
vi. Uwezo wa programu kuvutia mitaji ya sekta binafsi, hususan uwekezaji wa ndani, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje na mitaji ya Watanzania waishio ughaibuni;
vii. Uwezo wa kuimarisha ushiriki na ushindani wa Taifa katika biashara ya Kimataifa kwa kukuza wigo wa mauzo ya nje, kukuza teknolojia na ubunifu wa uzalishaji na bidhaa za viwandani;
viii. Kuweka uwiano wa maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi na kuleta manufaa kwa jamii, ili kuhakikisha maendeleo ya taifa yanakuwa yenye usawa na ustawi wa pamoja.

### 4.3 Kufungamanisha Minyororo ya Thamani katika Programu za Kielelezo

Ili kuhakikisha kuwa programu za kielelezo zinakuwa na manufaa mapana zaidi kwa biashara, uchumi na kaya za maeneo husika, Mpango umebaini na kuipa kipaumbele minyororo ya thamani ya kimkakati. Minyororo inakuwa ni sehemu ya mifumo ya mwendelezo kuwezesha manufaa yanayotoka na miundombinu msingi, shoroba za usafirishaji na uchukuzi, pamoja na maeneo mahsusi ya viwanda yaliyoanzishwa kupitia programu za kielelezo, kusambaa katika uchumi. Manufaa hayo ni pamoja na ushiriki wa biashara ndogo, za kati na kubwa, ongezeko la tija, uzalishaji wa ajira, na kupanuka kwa vyanzo mseto vya mapato. Minyororo hii ya thamani imeainishwa kwa kuzingatia:

i. Ulinganifu na sifa za kijiografia za eneo husika;
ii. Mahitaji ya mnyororo wa thamani yanavyoendana na miundombinu iliyopo;
iii. Uwezo wa kuongeza thamini bidhaa na kuongeza mauzo ya nje;
iv. Kiwango cha mahitaji ya nishati na huduma za usafirishaji na uchukuzi;
v. Uwezo wa kujenga na kuimarisha kongani za viwanda.

Kufungamanisha minyororo ya thamani katika programu za kielelezo kunaharakisha mageuzi ya kiuchumi nchini kwa kujenga mifumo jumuishi ya kiuchumi inayohusiana kwa karibu na kila mradi kichocheo. Lengo ni kuhakikisha kuwa miundombinu, viwanda, usafirishaji na uchukuzi, biashara ndogo, za kati na kubwa, maendeleo ya ujuzi pamoja na uasilishaji wa teknolojia vinafanya kazi kwa uwiano, badala ya kutekelezwa kama miradi inayotengana. Aidha, utaratibu huu unapunguza changamoto za uratibu, unachochea mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika maeneo husika, inaongeza mvuto wa uwekezaji wa sekta binafsi, na kuimarisha muunganiko kati ya Sura za Tatu na Sura ya Nne na viashiria vya upimaji wa matokeo vilivyoainishwa katika Kiambatisho II.

Kuunganisha programu za kielelezo na minyororo ya thamani kunalenga kuongeza tija ya uzalishaji, kukuza ushindani wa kibiashara, kupanua wigo wa mapato yatokanayo na mauzo ya nje, na kuongeza ajira kwa kiwango kikubwa. Jedwali 4.1 linaonesha maeneo muhimu ya kila programu ya kielelezo pamoja na matokeo yanayotarajiwa katika kila mnyororo wa thamani.

*Jedwali 4.1: Maeneo Muhimu ya Programu za Kielelezo na Matokeo ya Kila Mnyororo wa Thamani*

| Programu ya Kielelezo | Maeneo Muhimu | Minyororo ya Thamani ya Inayohusika |
|---|---|---|
| Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi | Bandari ya kina kirefu; eneo maalumu la kiuchumi; kituo cha uchumi wa buluu; bandari, usafirishaji na uchukuzi, na mifumo ya uchukuzi fungamanishi. | Bahari, usafirishaji na uchukuzi, uvuvi, ufugaji wa viumbe maji, usindikaji na uzalishaji wa bidhaa za bahari, mauzo ya nje ya mazao ya bustani, huduma na ukarabati wa meli. |
| Kitovu Changamani cha Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga | Mgodi na kiwanda cha kuchenjua chuma; kiwanda cha kuzalisha bidhaa za chuma; eneo mahsusi la viwanda; kituo cha utafiti; mgodi wa makaa ya mawe; kituo cha kufua umeme. | Uzalishaji wa bidhaa na vifaa chuma na mitambo; biashara ndogo na za kati za bidhaa za chuma na uhandisi; usafirishaji na uchukuzi |

| Programu ya Kielelezo | Maeneo Muhimu | Minyororo ya Thamani ya Inayohusika |
|---|---|---|
| Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia ya Kimiminika Lindi | Kuanza kwa uwekezaji kutoka nje ;<br>uzalishaji wa gesi asilia ya kimiminika;<br>uzalishaji wa nishati unaochochea viwanda;<br>kongani la viwanda maeno ya pwani | Mbolea, bidhaa za kemikali zinazotokana na gesi asilia ya kimiminika, huduma za gesi, plastiki, amonia, uzalishaji wa polima. |
| Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu Dodoma | Kituo cha ubunifu na teknolojia; kiwanda cha uzalishaji wa betri; eneo maalumu la viatamizi vya ubunifu wa teknolojia;<br>kituo cha usafirishaji na uchukuzi. | Kiwanda cha betri, kituo cha teknolojia ya umeme wa jua, viwanda vya kuunganisha vifaa vya kielektroniki, Viwanda vya kuongeza thamani ya madini na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na madini. |
| Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Uchakataji wa Mazao ya Kilimo | Upanuzi wa miundombinu ya umwagiliaji;<br>maeneo ya usindikaji wa bidhaa za kilimo;<br>mtandao wa usafirishaji na usambazaji wa vifaa vya kuhifadhi mazao;<br>mifumo ya kilimo cha umwagiliaji kidijitali; mifumo ya kidijitali ya kilimo. | Minyororo ya thamani ya mazao ya chakula, usindikaji wa mafuta ya kupikia, chakula cha mifugo, ufugaji, mauzo ya mazao ya bustani nje ya nchi, maziwa na viungo. |
| Kitovu cha Kisasa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Maziwa Makuu | Upanuzi wa bandari kavu;<br>kituo cha uzalishaji wa dawa;<br>eneo maalumu la uchumi wa buluu;<br>mfumo wa uzalishaji wa biashara ya kidijitali;<br>kuimarishwa kwa shirika la ndege la taifa. | Bidhaa za kilimo na dawa, viwanda vya kusindika samaki, huduma za usafirishaji wa madini kikanda; uchakataji wa bidhaa unaoendana na shughuli za utalii |
| Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji Nchini | Kutumika kwa mifumo ya miji ya kisasa;<br>kuimarika kwa kituo cha vifaa vya ujenzi;<br>kufungamanishwa kwa mfumo wa chakula mijini;<br>kuanzishwa kwa maeneo ya ubunifu. | Vifaa vya ujenzi, usafirishaji na uchukuzi mijini, teknolojia za fedha, sekta ya ubunifu, huduma za TEHAMA |

Kujumuisha minyororo ya thamani katika programu za kielelezo ni hatua muhimu katika kuhamasisha mtaji wa sekta binafsi. Hatua zinazopaswa kuchukuliwa ni pamoja na:

(i) Kuandaa maandiko ya miradi inayoweza kupata fedha za wawekezaji katika mkondo wa juu, kati, na wa chini kwa kila mnyororo wa thamani;
(ii) Kuvutia wawekezaji wakubwa watakaoweza kushawishi na kushirikiana na wawekezaji wadogo na wa kati, kuimarisha mifumo ya uzalishaji, kuimarisha mifumo ya uchumi na kubuni vyanzo vya mapato vinavyotabirika.

(iii) Kuanzisha mifumo maalum ya uwezeshaji wa kifedha kwa minyororo ya thamani katika usindikaji wa bidhaa za kilimo, uongezaji thamani madini, uchumi wa bluu na teknolojia.
(iv) Kuruhusu mikataba ya manunuzi na usambazaji ndani ya mnyororo wa thamani kutumika kama dhamana ili kupunguza vikwazo vya upatikanaji fedha.
(v) Kuunganisha minyororo ya thamani na masoko ya kikanda na kimataifa ili kuongeza imani kwa wawekezaji na kuingiza fedha za kigeni.
(vi) Kuimarisha mazingira wezeshi ya kiudhibiti na yanayotabirika katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi, Maeneo ya Uzalishaji kwa Ajili ya Mauzo ya Nje na Maeneo Yanayosimamiwa na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi na Uwekezaji Tanzania ili kupunguza gharama za kufanya biashara.

Mpango huu unatambua pia umuhimu wa minyororo mingine ya thamani ya kimkakati ambayo haimo moja kwa moja katika programu za kielelezo. Hii ni kutokana na asili ya shughuli zake, mtawanyiko wake wa kijiografia, na namna inavyoendeshwa. Hata hivyo, minyororo hiyo ina mchango mkubwa katika kuzalisha ajira kwa wingi, kupunguza umasikini ngazi ya jamii na kukuza ujasiriamali. Vilevile, ina nafasi muhimu katika kuimarisha ubunifu, kupanua wigo wa shughuli mseto za kiuchumi na kujenga Uchumi ulio himilivu na endelevu. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Mpango umetambua pia minyororo ya thamani yenye sifa hizi ili iwe sehemu ya utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo. Minyororo hiyo ni pamoja na:

(i) Shughuli za uzalishaji wa mazao ya bustani na mbogamboga zenye thamani ya juu, ikiwemo parachichi, viungo, matunda na mbegu za mafuta. Afua muhimu za kufanikisha utekelezaji wake ni pamoja na kuboresha huduma za usafirishaji na uchukuzi, kuimarisha miundombinu ya utunzaji wa mazao yanayoharibika haraka, kuongeza thamani ya bidhaa, kuimarisha viwango vya ubora, na kupanua upatikanaji wa masoko.
(ii) Ukusanyaji na usindikaji wa chakula nchini kwa ajili ya kuhakikisha usalama na uzalishaji wa chakula cha mifugo ili kuongeza tija katika shughuli za ufugaji na samaki. Afua muhimu ni pamoja na kupanua uzalishaji, usambazaji na usindikaji wa mahindi ya njano, alizeti na soya, kurahisisha upatikanaji wa pembejeo, mitaji na masoko.
(iii) Kukuza fursa katika sekta ya uvuvi na ufugaji wa samaki, ikiwa pamoja na kurahisisha taratibu za vibali, kuhamasisha uanzishaji wa machinjio za kibiashara na kuandaa programu maalumu za mafunzo.
(iv) Kuimarisha biashara changa ili kuchochea ubunifu na ujasiriamali. Afua muhimu ni pamoja na kuandaa programu za kuongeza ujuzi, kuimarisha ushirikiano kati ya vyuo vikuu na biashara changa, kuweka mazingira wezeshi ili kugeuza ubunifu kuwa shughuli za kibiashara, kutunga Sheria mahsusi za biashara changa itakayoweka bayana mfumo wa uendeshaji, vivutio, na ulinzi wa hakimiliki.
(v) Kushajihisha uwekezaji katika kilimo na viwanda vya mazao ya misitu kibiashara. Hatua za kipaumbele ni kuimarisha na kupanua vitalu vya miche, kuweka mifumo ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya upanuzi wa mashamba ya miti, kupanda miti, na kusimamia misitu kwa njia endelevu na kukuza ushiriki wa wakulima wadogo kupitia utaratibu wa ubia na wakulima wakubwa.
(vi) Kuimarisha shughuli za wachimbaji wadogo na wa kati wa madini. Afua muhimu ni pamoja na kurahisisha masharti ya upatikanaji wa leseni, kuongeza urasimishaji wa biashara, kuongeza wigo wa upatikanaji wa mitaji na kutoa mafunzo ya usalama kazini na huduma za taarifa za jiolojia. Aidha, ni muhimu kuendeleza miundombinu ya kimkakati ikiwemo barabara, umeme, bandari ili kusaidia shughuli za wachimbaji wakubwa, wa kati na wadogo hususan katika uchimbaji na uchakataji madini.

## 4.4 Programu za Kielelezo

Jedwali Namba 4.2 linaonyesha programu za kielelezo zilizochaguliwa pamoja na minyororo ya kimkakati na makadirio ya gharama za utekelezaji wake. Aidha, katika utekelezaji, programu zote za kielelezo zitafungamanishwa na miradi mtambuka ya kimkakati katika sekta mbalimbali, ikiwemo miradi ya uzalishaji (3500 MW[1]), usafirishaji na usambazaji wa umeme; kuboresha miundombinu ya ujifunzaji na ufundishaji; na Mradi wa Gridi ya Taifa ya Maji[1] ambayo ni muhimu katika kurahisisha utekelezaji. Gharama halisi za kila mradi na minyororo ya thamani inayohusiana na programu za kielelezo zitabainishwa baada ya kukamilika kwa tafiti za kina za upembuzi yakinifu na kuthibitishwa katika hatua za utekelezaji wa miradi husika.

*Jedwali Na. 4.2 : Programu za Kielelezo za FYDP IV*

| **1. Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi** | |
|---|---|
| **Maelezo ya Programu** | Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo na Usafirishaji Fungamanishi itatekelezwa kama bandari ya kina kirefu iliyounganishwa na mji mahiri wa viwanda. Programu hii itafungamanishwa na Eneo Maalum la Kiuchumi na kuendelezwa kuwa kitovu cha mageuzi ya kimkakati katika ukanda wa mashariki ya Tanzania. Aidha, itawezeshwa na mifumo jumuishi ya usafirishaji na uchukuzi wa njia mbalimbali. Lengo ni kuchochea maendeleo ya viwanda vinavyozalisha kwa ajili ya mauzo ya nje, kukuza uchumi wa buluu, na kuimarisha huduma za usafiri, usafirishaji na ugavi kwa masoko ya kikanda na kimataifa. Maeneo muhimu ya programu hii ni pamoja na:<br><br>i. Uendelezaji wa bandari ya Mbegani kwa kufungamanisha na miundombinu ya eneo huru la bandari pamoja na miundombinu ya viwanda katika Eneo Maalum la Kiuchumi;<br>ii. Kuendeleza ukanda za viwanda vya kijani kwa ajili ya ujenzi wa meli, uhandisi wa bahari, pamoja na huduma za usafirishaji na ugavi;<br>iii. Kuboresha mifumo ya nishati jadidifu na viwanda vya kuchakata taka kwa ajili ya kuzalisha nishati;<br>iv. Kujenga miji na wilaya mahiri zenye miundombinu himilivu katika ukanda wa pwani.<br>v. Miji bunifu ya kisasa na maeneo ya makazi yaliyo na miundombinu himilivu katika ukanda wa pwani.<br><br>Mradi huu unaendana na mikakati ya kitaifa ya maendeleo ya viwanda na minyororo ya thamani ya usafirishaji na ugavi, kwa kuimarisha nafasi ya Tanzania kama lango la biashara la kikanda na kupunguza gharama za usafirishaji na ugavi. |
| **Lengo** | Kujenga kituo cha kisasa cha shughuli za bahari na viwanda vitakavyojumuisha bandari, huduma za usafirishaji na ugavi, uzalishaji wa viwandani na huduma za mijini. Utekelezaji wake utakwenda sambamba na kuimarisha miundombinu ya kijani, ubunifu katika uchumi wa buluu na ushindani wa biashara. |

1 Uunganishaji wa vyanzo vikuu vya maji (ziwa Victoria, ziwa Tanganyika na mito mikuu)

| | |
|---|---|
| **Miradi Shikizi** | i. Reli ya kisasa ya SGR inayounganisha Ruvu na Bagamoyo, pamoja na vipande vya 3–8 vya reli ya kati vinavyounganisha Tabora, Mwanza, Kigoma na Msongati, pamoja na vipande vya reli kuelekea Kabanga na Buzwagi;<br>ii. barabara ya Pangani–Bagamoyo, ukanda wa barabara wa Kigamboni–Chanika–Kibaha–Mbweni (km 77.5);<br>iii. uendelezaji, uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege;<br>iv. uendelezaji wa Bandari ya Mbegani;<br>v. ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ya kisasa, ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;<br>vi. viwanda vya dawa, hususan kwa kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa dawa;<br>vii. Kitovu cha biashara ya ugavi na usafirishaji wa njia mbalimbali na biashara ya mtandao;<br>viii. Mradi wa kuendeleza biashara na mfumo fungamanishi wa usafirishaji na uchukuzi nchini;<br>ix. kukuza ujuzi kupitia taasisi ya mafunzo ya ufundi stadi kwa umahiri maalumu; na<br>x. upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam hadi kufikia gati 22. |
| **Minyororo ya Thamani ya Kimkakati** | i. Utalii na huduma za ukarimu: miundombinu ya utalii wa pwani, ikiwemo hoteli, vituo vya mapumziko na huduma za burudani, pamoja na kukuza utalii wa matukio na utalii wa meli za kitalii;<br>ii. Viwanda na uzalishaji: uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje, ikiwemo viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vinavyotengeneza nguo, chakula, vifaa vya kielektroniki, mashine, magari, pamoja na uchakataji wa chuma, kemikali na mbolea;<br>iii. Usafirishaji na ugavi wa bahari: kushughulikia mizigo, uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa, huduma za ugavi, pamoja na huduma za bandari;<br>iv. Biashara na huduma za kifedha: kituo cha biashara ya mtandao; huduma za kifedha na ugavi; biashara ya bidhaa zisizotozwa ushuru na usafirishaji wa bidhaa kwa masoko ya nje; biashara ndogo na za kati pamoja na watoa huduma; maendeleo ya majengo na huduma za msingi; mafunzo ya ujuzi na uundaji wa ajira;<br>v. Utafiti, ubunifu na teknolojia: vituo vya utafiti na ubunifu, pamoja na matumizi ya teknolojia katika uzalishaji wa viwandani na biashara changa;<br>vi. Mawasiliano na mifumo ya kidijitali: miundombinu ya kidijitali itakayorahisisha biashara na uwekezaji, usimamizi wa ugavi na usafirishaji kwa wakati, urahisishaji wa biashara kwa njia za kisasa, na utangazaji wa utalii kwa njia za kidijitali. |
| **Taasisi zinanzohusika katika Utekelezaji** | Tume ya Mipango; Sekta Binafsi; Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji (Taasisis Kiongozi); Wizara ya Fedha; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Nishati; Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania na Maeneo Maalum ya Kiuchumi; Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Shirika la Reli Tanzania; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Shirika la Umeme Tanzania; Wakala wa Barabara Tanzania; Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania; Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania; Mamlaka za Maji; Mamlaka ya Bandari Tanzania; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Shirika la Mawasiliano Tanzania |
| **Makadirio ya Gharama** | Shilingi trilioni 8.5 |

| **2. Kitovu Changamani cha Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga** | |
|---|---|
| **Maelezo ya Programu** | Programu hii inafungamanisha uchimbaji wa chuma na makaa ya mawe na viwanda vya uchakataji kwa ajili ya uzalishaji wa chuma, aloi na bidhaa nyingine za metali. Utekelezaji wake utaimarisha mnyororo wa thamani wa chuma nchini kwa kuunganisha uzalishaji wa malighafi na uchakataji wa bidhaa za chuma kwa ajili ya sekta ya ujenzi, viwanda na shughuli nyingine za uzalishaji. Chuma na malighafi za metali ni nyenzo muhimu katika mchakato wa kuendeleza viwanda. Uzalishaji wa chuma nchini utapunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje na kuchochea ushiriki wa biashara ndogo na za kati katika utengenezaji wa bidhaa za metali, sekta ya magari, na minyororo ya ugavi ya sekta ya ujenzi. |
| **Lengo** | Kujenga kituo changamani cha chuma na makaa ya mawe kinachojitosheleza kwa uzalishaji kwa ajili ya kuongeza thamani ya madini, kuimarisha mseto wa viwanda na kupunguza utegemezi wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje. |
| **Miradi Shikizi** | i. Reli ya Kisasa ya SGR kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay pamoja na maeneo ya Mchuchuma na Liganga (km 1,000);<br>ii. Mradi wa Maganga Matitu kwa ajili ya matumizi ya madini ya chuma yanayopatikana wilayani Ludewa;<br>iii. Mradi wa Kiwira wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe, wenye uwezo wa zaidi ya megawati 200;<br>iv. Barabara za kimkakati za Mawengi–Manda (km 110), Mkiu–Mavanga–Madaba(km 112), Nkomang'ombe–Liganga(km70), Nkomang'ombe–Mchuchuma (7 km) na Igawa–Tunduma pamoja na barabara ya mchepuko ya Uyole (km 266.9);<br>v. Uendelezaji, uboreshaji na upanuzi wa miundombinu ya usafirishaji, hususan viwanja vya ndege na bandari;<br>vi. Miundombinu ya mawasiliano, ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; na<br>vii. Maendeleo ya ujuzi kupitia taasisi za elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa ajili ya ujuzi maalumu; |
| **Minyororo ya Thamani Kimkakati** | i. Madini na uchimbaji: uchimbaji wa chuma na makaa ya mawe, pamoja na uzalishaji wa chuma;<br>ii. Nishati: uzalishaji, usambazaji na usafirishaji wa nishati;<br>iii. Ujenzi na usafirishaji: reli, barabara, huduma za ugavi na uhifadhi wa bidhaa, pamoja na maendeleo ya majengo;<br>iv. Viwanda: viwanda vya chuma na bidhaa za chuma; viwanda vinavyotegemea chuma kama malighafi, ikiwemo mashine, vipuri vya magari, vifaa vya ujenzi na zana za kilimo; pamoja na viwanda vya kemikali na bidhaa zitokanazo na uzalishaji huo, ikiwemo saruji, gesi za viwandani na mbolea;<br>v. Ujuzi, huduma na ubunifu: kuimarisha rasilimali watu, ikiwemo kutoa mafunzo ya ufundi na utaalamu kwa sekta za madini na nishati; kufanya tafiti; na kuchochea maendeleo pamoja na ubunifu wa teknolojia ya chuma na mazingira;<br>vi. Ushirikiano wa kibiashara: huduma na shughuli saidizi katika mnyororo wa ugavi, ikiwemo usafirishaji, upishi, na utengenezaji wa bidhaa za metali. |
| **Taasisi zinanzohusika katika Utekelezaji** | Tume ya Mipango; Sekta Binafsi; Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji; Wizara ya Viwanda na Biashara (Taasisi Kiongozi); Shirika la Taifa la Maendeleo; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Fedha; Wizara ya Nishati; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Shirika la Reli Tanzania; Mamlaka ya Bandari Tanzania; Shirika la Umeme Tanzania; Wakala wa Barabara Tanzania; Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania; Shirika la Mawasiliano Tanzania; Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania; na Mamlaka za Maji. |
| **Makadirio ya Gharama** | Shilingi trilioni 16 |

| **3. Programu ya Kitaifa ya Umwagiliaji na Mageuzi ya Viwanda vya Uchakataji wa Mazao ya Kilimo** | |
|---|---|
| **Maelezo ya Programu** | Programu hii ni hatua ya kimkakati ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji wa chakula katika ukanda wa Afrika. Inalenga kutumia kwa tija mabonde makuu ya mito kukuza kilimo cha umwagiliaji, kukuza kilimo himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi na maendeleo ya viwanda vya kilimo. Programu inajumuisha miradi ya Mabonde ya Rufiji, Mara na Songwe. Lengo ni kupanua eneo la umwagiliaji kufikia zaidi ya hekta 420,000 ambazo zitahudumiwa kwa kutumia maji yanayotoka katika miundombinu ya mabwawa ya kuzalisha umeme na matumizi mengine. Hatua hii itaongeza uzalishaji wa mpunga, mahindi, miwa, mazao ya mafuta na mazao ya bustani kwa mwaka mzima. Pia itachochea uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, ikiwemo kukoboa mpunga na kusaga nafaka, uzalishaji wa mafuta ya kula na vituo vya kufungasha chakula. Kwa kutumia mtiririko wa maji uliodhibitiwa, Mradi wa Umeme wa Rufiji na miradi mingine ya mabonde, programu hii itaongeza usalama wa chakula, ushindani wa mauzo ya mazao katika masoko ya nje na maendeleo ya viwanda vijijini. Aidha, itaimarisha usimamizi wa maji, kukuza ushirikiano wa kikanda, hususani nchi ya Malawi kupitia Bonde la Songwe na kuongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na ujenzi wa uchumi mseto. Kwa ujumla, hatua hizi za kimageuzi zitaiwezesha Tanzanaia kutumia mabonde yenye rutuba kuwa vitovu endelevu vya uzalishaji na uchakataji wa mazao ya kilimo. Hivyo, kuimarisha uwezo wa kujitosheleza kwa chakula na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa chakula kwa ajili ya mauzo nje ifikapo mwaka 2050. |
| **Lengo** | Kuboresha na kupanua miundombinu ya umwagiliaji na uchakataji wa mazao ya kilimo ili kuongeza tija, kuimarisha minyororo ya thamani ya viwanda vya kilimo na kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza ushindani kwa mazao katika mauzo ya nje. |
| **Miradi Shikizi** | i. Kilimo: miradi ya umwagiliaji katika Mabonde ya Rufiji, Songwe na Mara inayolenga kuongeza uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje;<br>ii. Barabara: Rufiji–Kilwa, Kilwa–Morogoro, Igawa–Tunduma pamoja na barabara ya mchepuo wa Uyole (km 266.9), Handeni–Kiberashi–Singida (km 434.33), pamoja na barabara za kuunganisha maeneo ya uzalishaji vijijini.<br>iii. Ugavi na usafirishaji: kuendeleza, kuboresha na kupanua viwanja vya ndege, bandari na bandari kavu, vitovu vya ugavi wa mazao ya kilimo pamoja na miundombinu ya kuhifadhi na kusafirisha mazao katika hali ya ubaridi;<br>iv. Mradi wa Bugwema wa Umwagiliaji Jumuishi wa Kisasa na Kilimo cha Biashara;<br>v. Shamba Kubwa la Lumpungu la Umwagiliaji kwa Kilimo cha Biashara;<br>vi. Mradi wa Bonde la Umwagiliaji la Kamsamba;<br>vii. Mradi wa Kuendeleza Umwagiliaji Membe; na<br>viii. Kitovu cha biashara, ugavi na usafirishaji wa njia mbalimbali pamoja na biashara ya mtandao. |
| **Minyororo ya Thamani Kimkakati** | i. Mazao: mpunga, mahindi, mbegu za mafuta, mazao ya bustani na jamii ya mikunde.<br>ii. Mifugo na Uvuvi: minyororo ya thamani ya maziwa na nyama ya ng'ombe inayounganishwa na uzalishaji wa chakula cha mifugo kutoka maeneo ya umwagiliaji; pamoja na ufugaji wa samaki katika mabwawa ya matumizi mbalimbali.<br>iii. Viwanda vya Kilimo: viwanda vya kukoboa mpunga na kusaga nafaka, uchakataji wa mafuta ya kula, uzalishaji wa sukari na ethanoli, ufungashaji wa chakula, pamoja na uendelezaji wa viwanda vya wanga na nishati jadidifu ya kibaolojia.<br>iv. Sekta Saidizi: usimamizi wa maji, nishati jadidifu, ugavi na usafirishaji, usimamizi wa mashamba kwa kutumia mifumo ya kidijitali na huduma za kifedha.<br>v. Utafiti, maendeleo na Ubunifu: vituo vya Tafiti na Maendeleo na kampuni chipukizi. |

| | |
|---|---|
| **Taasisi zinanzohusika katika Utekelezaji** | Tume ya Mipango; Sekta Binafsi; Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji; Wizara ya Kilimo (Taasisi Kiongozi); Wizara ya Fedha; Mamlaka za Mabonde ya Maji; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji; Wakala wa Barabara Tanzania; Mamlaka ya Bandari Tanzania; Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania; Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi na Uwekezaji Tanzania; na Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. |
| **Makadirio ya Gharama** | Shilingi trilioni 10 |
| **4. Kitovu cha Teknolojia na Uchakataji wa Madini Adimu Dodoma** | |
| **Maelezo ya Programu** | Programu hii inalenga kuifanya Dodoma kuwa kitovu cha kitaifa cha kuongeza thamani ya madini muhimu kama kobalti, lithiamu, helimu na grafaiti kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya viwanda vipya na ajira. Programu itaunganisha uchakataji wa madini, kuongeza ubunifu katika matumizi ya teknolojia na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika uzalishaji. Utekelezaji wake utaimarisha ukuaji wa uchumi, kuzalisha ajira na kujenga msingi imara wa uchumi wa madini wa siku zijazo. Msisitizo mahsusi ni viwanda vya utengenezaji wa betri. |
| **Lengo** | Kuifanya Dodoma kuwa kitovu cha kitaifa cha ubunifu na teknolojia kwa kuunganisha uongezaji thamani wa madini, miundombinu ya uchumi wa kidijitali na mifumo ya utafiti wa viwanda. |
| **Miradi Shikizi** | i. Barabara: barabara ya Nyakahura–Kabanga (km 141), barabara ya Dodoma–Iringa–Mbeya, barabara ya mwendokasi ya Kibaha–Morogoro–Dodoma (km 465), na barabara ya Kidatu–Lupilo–Lumecha/Songea (km 512);<br>ii. Ugavi na usafirishaji: uendelezaji, uboreshaji na upanuzi wa bandari, viwanja vya ndege, na vitovu vya ugavi;<br>iii. Kitovu cha kitaifa cha utafiti na ubunifu katika akili unde na kompyuta za kiwango cha juu;<br>iv. Miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano;<br>v. Mradi wa magadi-soda wa Engaruka;<br>vi. Utafiti na maendeleo: tafiti za teknolojia na uchumi kwa ajili ya kuboresha viwanda vya madini; na<br>vii. Kukuza ujuzi: taasisi mahiri za elimu na mafunzo ya ufundi stadi. |
| **Minyororo ya Thamani Kimkakati** | i. Madini: kobalti, lithiamu, helimu, grafaiti na nikeli;<br>ii. Viwanda na uzalishaji: kuzalisha bidhaa za viwandani kama betrii, aloi, bidhaa za kijani zinazotokana na madini muhimu<br>iii. Nishati na miundombinu: uzalishaji wa nishati jadidifu inayotokana na jua, maji, upepo na jotoardhi, usambazaji wa umeme na mifumo ya gridi, pamoja na usimamizi wa maji safi na usafi wa mazingira;<br>iv. Utafiti, maendeleo na ubunifu: vituo vya utafiti, maendeleo ya ujuzi, teknolojia za uchakataji wa kemikali, matumizi ya mifumo ya kisasa viwandani na biashara changa;<br>v. Biashara, ugavi na huduma za kifedha: uchakataji wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje na urahisishaji wa biashara, mifumo ya ugavi na usafirishaji pamoja na huduma za kifedha na uwekezaji ikiwemo hatifungani za kijani, mitaji bunifu na fedha zinazotokana na biashara ya kaboni kwa ajili ya kuwezesha biashara changa na biashara ndogo na za kati. |
| **Taasisi zinazohusika katika Utekelezaji** | Tume ya Mipango; Sekta Binafsi; Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji; Wizara ya Fedha; Wizara ya Nishati; Wizara ya Madini (Taasisi Kiongozi); Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Ujenzi; Wakala wa Barabara Tanzania; Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania; Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania na Maeneo Maalum ya Kiuchumi; Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Shirika la Mawasiliano Tanzania; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania; Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania; Mamlaka ya Bandari Tanzania; na Shirika la Reli Tanzania. |
| **Makadirio ya Gharama** | Shilingi trilioni 7 |

| **5. Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia ya Kimiminika Lindi** | |
|---|---|
| **Maelezo ya Programu** | Mradi wa kitaifa wa kujenga kiwanda cha kuchakata Gesi Asilia ya Kimiminika katika mkoa wa Lindi. Mradi huu unalenga kutumia kwa tija akiba kubwa ya gesi asilia ya Tanzania ili kuwa kichocheo muhimu cha maendeleo ya viwanda na ukuaji wa mauzo ya nje. Kupitia mradi huu, gesi asilia itachakatwa kufikia tani milioni 10 kwa mwaka kwa ajili ya masoko ya nje na matumizi ya viwandani. Utekelezaji wake utaimarisha usalama wa nishati, kuongeza ajira, mauzo nje ya nchi na kuchochea ukuaji wa uchumi. |
| **Lengo** | Kuanzisha kituo cha kimataifa cha usafirishaji wa gesi asilia iliyoyeyushwa kwa ajili ya mauzo ya njekitakachoharakisha mageuzi ya sekta ya nishati, kuongeza mapato na maendeleo ya mnyororo wa thamani viwandani. |
| **Miradi Shikizi** | i. Uendelezaji wa barabara kuu ya Mtwara–Dar es Salaam;<br>ii. Bomba la kusafirisha gesi;<br>iii. Taasisi mahiri za kuendelea ujuzi kwa ajili ya petroleum na viwanda vya kuchakata gesi. |
| **Minyororo ya Thamani Kimkakati** | i. Nishati: utafutaji wa gesi asilia, usafishaji na ukaushaji wa gesi, usafirishaji kwa njia ya mabomba, matenki ya kuhifadhia, vituo vya kupokea na kusafirisha gesi, vitengo vya kurejesha gesi kutoka hali ya kimiminika, usambazaji, na mauzo ya nje;<br>ii. Mradi wa Kinyerezi III wa kuzalisha umeme wa megawati 1,000 kwa kutumia gesi asilia;<br>iii. Viwanda na uzalishaji: bidhaa za kemikali zitokanazo na mafuta na gesi asilia, uzalishaji wa mbolea, gesi asilia iliyoshindiliwa, na usambazaji wa gesi kwa matumizi ya viwandani;<br>iv. Huduma za baharini, ugavi na ujenzi: miundombinu ya baharini, huduma za ugavi, huduma za ujenzi na uhandisi, pamoja na uboreshaji wa bandari;<br>v. Maendeleo yatokanayo na ujuzi, teknolojia na huduma za kifedha: mafunzo ya rasilimali watu katika uhandisi wa mafuta na gesi, shughuli za baharini, uchomeleaji na udhibiti wa mifumo ya uzalishaji; uhawilishaji wa teknolojia na ubunifu; huduma za kifedha; na biashara za wananchi. |
| **Taasisi zinanzohusika katika Utekelezaji** | Tume ya Mipango; Sekta Binafsi; Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji; Wizara ya Nishati (Taasisi Kiongozi); Wizara ya Viwanda na Biashara; Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania; Mamlaka ya Bandari Tanzania; na Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania na Maeneo Maalum ya Kiuchumi. |
| **Makadirio ya Gharama** | Shilingi trilioni 108 |
| **6. Kitovu cha Kisasa cha Viwanda na Uchumi wa Buluu katika Ukanda wa Maziwa Makuu** | |
| **Maelezo ya Programu** | Programu hii ni ya mageuzi katika Ukanda Pembetatu wa Maziwa Makuu na itajikita katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara na Kagera. Itaunganisha kongane za viwanda, biashara, usafiri na usafirishaji nchi kavu na majini, pamoja na shughuli za uchumi wa buluu katika ukanda wa ziwa Victoria na maeneo ya nchi kavu yanayouzunguka. Hii itaongeza nafasi ya Tanzania katika biashara ya kikanda kwa kuiunganisha na masoko ya Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. |
| **Lengo** | Kuliwezesha eneo la kanda ya ziwa kuwa kitovu cha kikanda katika viwanda, usafiri na usafirishaji na uchumi wa buluu ili kuunganisha masoko ya Eneo Huru la Biashara Afrika, kupanua fursa za kujipatia kipato katika uvuvi, madini na uchakataji wa mazao ya kilimo, na kuhimiza maendeleo ya viwanda vya kijani na matumizi ya teknolojia ya kidijitali. |

| | |
|---|---|
| **Miradi Shikizi** | i. Kuboresha shirika la ndege la Taifa;<br>ii. meli ya Mizigo inayotumia reli Iliyopachikwa;<br>iii. barabara za kikanda zinazounganisha Bukoba, Kyaka, Simiyu, Shinyanga na Mara;<br>iv. barabara za kikanda zinazounganisha Tanzania na Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo<br>v. uendelezaji, uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege na bandari;<br>vi. kiwanda cha kutengeneza pamba tiba na viwanda vya kutengeneza dawa;<br>vii. vituo vya elimu ya ufundi stadi na ubunifu kwa ajili ya uhandisi wa bahari, matumizi ya mifumo ya kisasa ya viwanda, usafirishaji na ugavi pamoja na ujasiriamali. |
| **Minyororo ya Thamani Kimkakati** | i. Uchakataji na usafirishaji wa samaki kwa ajili ya mauzo nje ya nchi;<br>ii. Uchenjuaji wa dhahabu na vito uliofungamanishwa na Kitovu cha Dodoma cha Madini Muhimu na Ubunifu wa Teknolojia kupitia Soko la Madini ya Thamani;<br>iii. mnyororo wa thamani wa kuchakata pamba kuwa nguo na ngozi kuwa bidhaa za ngozi na viatu;<br>iv. uchakataji wa kahawa na chai ili kuongeza thamani ya maziwa;<br>v. Mazao ya umwagiliaji yatakayofungamanisha mazao ya nafaka biashara za kikanda Kenya, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; na<br>vi. na kuimarisha uendeshaji wa Shirika la Ndege Tanzania. |
| **Taasisi zinanzohusika katika Utekelezaji** | Tume ya Mipango; Sekta Binafsi; Wizara ya Viwanda na Biashara (Taasisi Kiongozi); Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji; Wizara ya Fedha; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania na Maeneo Maalum ya Kiuchumi; Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Shirika la Reli Tanzania; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Shirika la Umeme Tanzania; Wakala wa Barabara Tanzania; Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania; Mamlaka ya Bandari Tanzania; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Wizara ya Nishati; Wizara ya Madini; Ofisi ya Makamu wa Rais; na taasisi nyingine. |
| **Makadirio ya Gharama** | Shilingi trilioni 15 |
| **7. Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji Nchini** | |
| **Maelezo ya Programu** | Programu Shirikishi ya Uendelezaji wa Miji Tanzania– 2050 inalenga kuimarisha mfumo wa miji ya ngazi na hadhi mbalimbali kwa kuzingatia mpangilio wa kitaifa wa miji mikubwa, miji ya kikanda na miji ya kati, ili kuwa na miji yenye uwiano kijeografia nchini. Programu hii itaunganisha uwekezaji katika miundombinu, makazi ya gharama nafuu, mageuzi ya kiutawala ili kuboresha utoaji wa huduma na kuimarisha uchumi wa mijini. Kutokana na kasi ya ukuaji wa miji, fursa za kuongeza tija pamoja na changamoto za miundombinu na huduma zinaongezeka. Hivyo, programu hii itasaidia ukuaji wa miji iliyopangwa, kuimarisha mifumo ya mapato ya mamlaka za serikali za mitaa na kuendeleza ujenzi wa kisasa unaoendana na kanuni za uchumi wa kijani, na kuzalisha ajira zinazotokana na ubunifu. |
| **Lengo** | Kujenga miji imara, jumuishi na endelevu kwa kutumia miundombinu na huduma za kisasa, upanuzi wa makazi nafuu, kuzalisha ajira za kijani na kidijitali, na kuimarisha usimamizi wa miji unaozingatia mabadiliko ya tabianchi. |
| **Miradi Shikizi** | i. Usimamizi endelevu wa ardhi ya Mijini;<br>ii. Miundombinu ya msingi;<br>iii. Makazi nafuu na miundombinu ya huduma za kijamii;<br>iv. Usambazaji wa nishati safi,<br>v. Miundombinu ya msingi inayohimili mabadiliko ya tabianchi;<br>vi. Vituo vya kisasa vya huduma za afya;<br>vii. Vituo vya mapumziko na burudani;<br>viii. Mifumo fungamani ya usafiri na usafirishaji na kitovu cha biashara mtandao; |

| | |
|---|---|
| | viii. na miji ya kisasa inayosimamiwa kwa kutumia majukwaa ya kidijitali yanayowezeshwa na akili unde. |
| **Minyororo ya Thamani Kimkakati** | Mnyororo wa thamani wa makazi na ujenzi utaunganishwa na huduma za usafiri na usafirishaji hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya huduma na kuzalisha ajira; na uwekezaji katika nishati utachochea maendeleo ya miundombinu ya kisasa na kukuza uchumi wa kidijitali. |
| **Taasisi zinanzohusika katika Utekelezaji** | Tume ya Mipango; Sekta Binafsi; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Taasisi Kiongozi); Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji; Wizara ya Fedha; Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji Tanzania; Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Shirika la Reli Tanzania; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Shirika la Umeme Tanzania; Wakala wa Barabara Tanzania; Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania; Mamlaka ya Bandari Tanzania; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Nishati; Wizara ya Madini; Ofisi ya Makamu wa Rais; Wizara ya Maliasili na Utalii; na taasisi nyingine. |
| **Makadirio ya Gharama** | Shilingi trilioni 8 |

### 4.5 Mfumo wa Utekelezaji wa Programu za Kielelezo

Utekelezaji wenye mafanikio wa programu za kielelezo unahitaji mfumo imara wa utendaji, ulioratibiwa kwa ufanisi na unaoweka wazi majukumu pamoja na uwajibikaji. Mfumo huu unaunganisha mwelekeo wa sera, utekelezaji wa miradi, na ufuatiliaji wa matokeo ili kuhakikisha programu zinatekelezwa kwa ufanisi na kuleta matokeo yaliyokusudiwa. Uzoefu wa utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya mipango iliyopita unaonesha kuwepo kwa mapungufu kadhaa, yakiwemo mwingiliano wa majukumu kati ya Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, pamoja na Mashirika ya Umma; uratibu usioridhisha; ucheleweshaji wa maamuzi na mapungufu katika uwajibikaji; kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi; udhaifu katika usimamizi wa mikataba; na utekelezaji usio shirikishi uliosababishwa na kutokuwiana kwa ratiba, mpangilio wa vipaumbele na vigezo miongoni wa waliopewa dhamana ya kutekeleza. Kwa kuzingatia uzoefu huo, utaratibu wa utekelezaji wa programu za kielelezo za Mpango IV unalenga kuimarisha usimamizi wianifu wa kisera, uratibu wa utekelezaji kiufundi, na kujengea uwezo taasisi zinazotekeleza miradi. Mfumo huu utaongozwa na kuratibiwa na Tume ya Taifa ya Mipango, ambayo itasimamia mwelekeo wa kimkakati na uratibu wa jumla wa utekelezaji wa programu za kielelezo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kimkakati wa programu hizi, mfumo huu unalenga:

(i) kuhakikisha utekelezaji wa programu za kielelezo kwa wakati na kwa ubora unaotarajiwa;

(ii) kuunganisha uratibu, upangaji wa vipaumbele na ratiba ya utekelezaji wa miradi ya serikali na miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi chini ya mfumo mmoja wa ufuatiliaji wa matokeo;

(iii) kuimarisha maandalizi na utekelezaji wa miradi, kwa miradi kuandaliwa vizuri ili kuvutia uwekezaji na kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha;

(iv) kuweka mifumo ya ufuatiliaji wa maendeleo ya utekelezaji, utoaji wa taarifa, na utatuzi wa changamoto kwa wakati; na

(v) kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji, ujifunzaji endelevu, na uboreshaji wa utekelezaji. Maelezo ya kina kuhusu mfumo huu wa utekelezaji yameainishwa katika Sura ya Sita.

# MUHTASARI – SURA YA NNE

MPANGO IV · SURA YA 4

## Programu za Kielelezo za Taifa

### Asilimia 20 ya miradi inayozalisha zaidi ya 80% ya matokeo

Kugeuza mageuzi mapana ya Sura ya 3 kuwa mkusanyiko maalum wa programu za kielelezo zenye ufanisi wa Pareto — ukiongeza thamani ya kitaifa huku ukipunguza mtawanyo wa rasilimali na ucheleweshaji wa utekelezaji.

| | |
|---|---|
| **7** PROGRAMU ZA KIELELEZO | **8** VIGEZO VYA UTEUZI |
| **TZS 172.5T** GHARAMA YA JUMLA | **3,500 MW** NISHATI MTAMBUKA |

MPANGO IV · Sura ya 4 — *Programu za Kielelezo za Taifa*

MANTIKI YA UTEUZI WA PROGRAMU

## Kanuni ya Ufanisi ya Pareto ya 20:80

Mkusanyiko maalum wa programu fungamanishi zenye uwezo mkubwa wa kichocheo — zilizotathminiwa dhidi ya vigezo nane vilivyopangwa vinavyowiana na Mpango IV na Dira 2050.

**20%**
**Uwekezaji Uliochaguliwa Kimkakati**
Programu 7 za kielelezo pamoja na nguzo mtambuka za nishati na maji.

**80%+**
**Matokeo ya Kijamii na Kiuchumi Yanayotarajiwa**
Ukuaji · ushindani · mageuzi ya kimuundo · tija · ajira.

VIGEZO NANE VYA UTEUZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| I Uwianifu wa Kimkakati | II Matokeo Makubwa ya Kijamii-Kiuchumi | III Uendelevu na Ustahimilivu | IV Utayari wa Utekelezaji |
| V Mfungamano wa Kisekta | VI Kuvutia Mtaji wa Sekta Binafsi | VII Ushindani wa Kimataifa | VIII Usawa wa Kijiografia |

MPANGO IV · Sura ya 4 — *Kanuni ya 20:80 · Vigezo vya Uteuzi*

PROGRAMU SABA ZA KIELELEZO

# Mkusanyiko wa Programu za Kielelezo zenye Ufanisi wa Pareto

Kila programu inaunganisha minyororo ya thamani inayowiana kiasili, ikitengeneza mifumo fungamanishi ya kiuchumi inayozalisha tija, mauzo nje na ajira kwa kiwango kikubwa.

**01 · TZS 8.5T**
**BEMCIT**
Mji wa Ikolojia ya Bahari Bagamoyo · bandari + SEZ + viwanda vya kijani.

**02 · TZS 16T**
**Liganga na Mchuchuma**
Kitovu cha Chuma na Makaa · Ludewa · madini + chuma + nishati ya makaa.

**03 · TZS 10T**
**NAGITA**
Umwagiliaji na Viwanda vya Kilimo · hekta 420,000 za umwagiliaji.

**04 · TZS 7T**
**Madini Adimu Dodoma**
Kitovu cha Teknolojia · mnyororo wa betri · ubunifu wa teknolojia.

**05 · TZS 108T**
**Kiwanda cha LNG Lindi**
Tani milioni 10 za LNG kwa mwaka · MW 1,000 Kinyerezi III.

**06 · TZS 15T**
**GL-SIBEH**
Kitovu cha Kisasa cha Viwanda Maziwa Makuu · biashara ya mipakani ya AfCFTA.

**07 · TZS 8T**
**TUGNe 2050**
Uendelezaji wa Miji · mfumo wa miji wa ngazi · utawala wa kisasa.

**MTAMBUKA**
**Gridi ya Nishati + Maji**
MW 3,500 + Gridi ya Taifa ya Maji (maziwa + mito).

MPANGO IV · Sura ya 4 — *Programu Saba + Nguzo Mtambuka*

MUHTASARI WA GHARAMA NA UTEKELEZAJI

# Gharama — TZS Trilioni 172.5

Mgawanyo wa gharama za programu za kielelezo na mfumo wa mafunzo-kwenda-vitendo unaohakikisha utekelezaji unaoongozwa na Tume ya Mipango, uwajibikaji na uwezo wa kupata fedha.




**⚠ Mafunzo Kutoka Mipango Iliyopita**
Majukumu yaliyogawanyika · uratibu dhaifu · ucheleweshaji · gharama kuzidi · usimamizi hafifu wa mikataba.

**✓ Mfumo wa Mpango IV**
Uratibu unaoongozwa na Tume ya Mipango · ufuatiliaji wa pamoja wa matokeo · ubia fungamanishi · uwezo bora wa kupata fedha · utamaduni wa uwajibikaji.

MPANGO IV · Sura ya 4 — *Muhtasari wa Gharama · Mfumo wa Utekelezaji*









# SURA YA TANO: MAHITAJI NA MFUMO WA KUGHARAMIA UTEKELEZAJI








# SURA YA TANO

# MAHITAJI NA MFUMO WA KUGHARAMIA UTEKELEZAJI

## 5.1 Muhtasari

Sura hii inaainisha kwa kina mfumo wa kutafuta, kugawa na kusimamia rasilimali fedha zitakazowezesha utekelezaji wa Mpango IV. Jumla ya uwekezaji unaohitajika inakadiriwa kufikia Shilingi bilioni 477,746.76 za Tanzania (sawa na Dola za Marekani bilioni 183). Mkakati wa ugharamiaji wa Mpango umejengwa katika uwiano wa uwekezaji wa asilimia 70 kwa sekta binafsi na asilimia 30 kwa sekta ya umma, ukitambua sekta binafsi kama injini kuu ya ukuaji wa uchumi, kuongeza tija, kuendeleza ubunifu na kuzalisha ajira. Sekta binafsi inatarajiwa kuchangia Shilingi bilioni 324,487.46 katika utekelezaji wa Mpango.

Sekta ya umma, inayojumuisha Serikali na Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara, inatarajiwa kuchangia Shilingi bilioni 153,259.30. Mgawanyo huu wa ugharamiaji ni endelevu na umezingatia mwelekeo wa uendeshaji wa uchumi wa soko na ufanisi. Unasisitiza kuhusu kuimarisha zaidi ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuvutia mitaji ya sekta binafsi kwa ajili ya kugharamia mageuzi ya kiuchumi, kuchochea ukuaji jumuishi na kuongeza uzalishaji wa ajira. Kulingana na Sura ya Nne, asilimia 20 ya afua zimeainishwa kama programu za kielelezo, pamoja na minyororo ya thamani inayohusiana nazo. Afua hizo zitagharimu takriban asilimia 40 hadi 50 ya gharama za Mpango, na zinatarajiwa kuzalisha zaidi ya asilimia 80 ya matokeo ya kijamii na kiuchumi ifikapo mwaka 2031. Hivyo, mwelekeo huu unaakisi mpangilio unaozingatia vipaumbele katika mgawanyo wa rasilimali fedha na juhudi za kukuza uwekezaji.

## 5.2 Mahitaji ya Rasilimali Fedha

Ili kuweka msingi wa kufikia azma ya muda mrefu ya kuwa na uchumi wa Dola za Marekani trilioni 1 ifikapo mwaka 2050. Mpango unatoa kipaumbele katika uwekezaji wa haraka, mkubwa na wenye ufanisi. Kufikia lengo hilo kunahitaji kudumisha ukuaji halisi wa pato la Taifa wa takribani asilimia 10 kwa mwaka katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango. Uwezekano wa kufikia kiwango hicho cha ukuaji unategemea kudumisha uwiano wa nyongeza ya mtaji kwa pato la Taifa usiozidi nne. Kwa msingi huo, ukuaji wa asilimia 10 kwa mwaka unamaanisha hitaji la uwekezaji wa takribani asilimia 35 hadi 40 ya pato la Taifa kila mwaka, kwa kutegemea maboresho katika kuongeza ufanisi wa uwekezaji.

Aidha, kiwango hiki cha uwekezaji kinapaswa kuelekezwa katika sekta zenye uwezo mkubwa wa kuleta mageuzi ya haraka ya kiuchumi, kijamii na kimazingira. Sekta hizo, kama zilivyoainishwa katika Dira 2050, ni: usafirishaji na uchukuzi , nishati na uchimbaji madini, viwanda na biashara, kilimo, utalii, ujenzi na umilki, TEHAMA, mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, uchumi wa buluu, michezo na burudani, huduma za kijamii na maendeleo ya rasilimali watu, utawala bora, usimamizi wa umma na utafiti na maendeleo (Jedwali 5.1).

*Jedwali 5.1: Mahitaji ya Fedha kwa kila Sekta ya Kipaumbele*

| Na. | Sekta | Mahitaji (Dola za Marekani Bilioni) | Mgawanyo Kisekta (%) |
|---|---|---|---|
| 1 | Miundombinu ya Uchukuzi na Usafirishaji | 45.8 | 25.0 |
| 2 | Nishati na Uchimbaji wa Madini | 27.5 | 15.0 |
| 3 | Viwanda na Biashara | 22.0 | 12.0 |
| 4 | Kilimo, Mifugo na Uvuvi | 18.3 | 10.0 |
| 5 | Elimu na Maendeleo ya Ujuzi | 14.6 | 8.0 |
| 6 | Afya na Hifadhi za Jamii | 12.8 | 7.0 |
| 7 | Maji, Usafi wa Mazingira na Maendeleo ya Miji | 9.2 | 5.0 |
| 8 | TEHAMA na Uchumi wa Kidijitali | 9.2 | 5.0 |
| 9 | Utalii na Huduma | 7.3 | 4.0 |
| 10 | Uhifadhi wa Mazingira na Ustahamilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi | 5.5 | 3.0 |
| 11 | Utawala Bora, Amani, Utulivu, Usimamizi wa Umma, Utafiti na Maendeleo na Mengineyo | 10.0 | 5.5 |
| | JUMLA | 183 | 100 |

***Chanzo:*** *Mpango Elekezi 2050*

## 5.3 Muundo wa Ugharamiaji

Mfumo wa ugharamiaji wa Mpango unatumia uwiano wa asilimia 70 kwa sekta binafsi na asilimia 30 kwa sekta ya umma, ukionesha dhamira ya Mpango ya kujenga uchumi unaoendeshwa kwa misingi ya soko. Katika mpangilio huu, sekta binafsi inatarajiwa kuwekeza takribani Shilingi trilioni 324.49 kupitia uwekezaji wa ndani wa sekta binafsi, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, nyenzo za ugharamiaji wa kijani na tabianchi, pamoja na masoko ya mitaji ya ndani. Kama ilivyoelezwa katika Sura ya Tatu, Serikali itaanzisha na kuendesha chombo maalum cha kugharamia vihatarishi vya miradi ili kuimarisha miradi inayoweza kupata uwekezaji, hususan ile inayotokana na programu za kielelezo na minyororo ya thamani ya kipaumbele.

Kwa upande wa sekta ya umma, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitachangia Shilingi trilioni 115.04, zinazopatikana kupitia mapato ya ndani na ukopaji endelevu. Mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara yanatarajiwa kuwekeza Shingi trilioni 38.22 kupitia mapato yanayorejeshwa katika uwekezaji, nyongeza ya mtaji, na maboresho ya kiutendaji yatakayoimarisha hali ya fedha na ufanisi wa taasisi hizo, kama inavyoonesha katika Jedwali 5.2. Ili kufanikisha muundo huu wa ugharamiaji, Mpango unalenga kutekeleza yafuatayo: urasimishaji wa biashara ndogo, za kati ili kupanua wigo wa kodi na kufungua fursa zaidi za uwekezaji katika miradi inayokopesheka. Eneo lingine muhimu ni kuimarisha mfumo wa kitaifa wa taarifa na huduma za mikopo ili kudhibiti vihatarishi na kupunguza gharama ya mtaji. Pia, kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa Kituo cha Kimataifa cha Huduma za Fedha hatua itakayovutia uwekezaji wa mitaji ya muda mrefu kutoka nje na kuimarisha sekta ya fedha nchini.

*Jedwali 5.2: Muundo wa Ugharamiaji wa Mpango IV*

| Mchangiaji | TZS (Trilioni) | Mchango % | Chanzo cha Mapato |
|---|---|---|---|
| Sekta Binafsi | 324.49 | 70 | Mitaji ya moja kwa moja kutoka nje, ubia wa sekta ya umma na binafsi, fedha za mazingira na uchumi wa kijani, mitaji ya ndani kwa miundombinu yenye matokeo makubwa na viwanda vinavyotumia nguvu kazi yenye ujuzi maalum. |
| Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa | 115.04 | 22 | Mapato ya kodi na yasiyo ya kodi na mikopo endelevu ya gharama nafuu. |
| Mashirika ya Umma | 38.22 | 8 | Mapato yanayotokana na uwekezaji na mitaji wa hisa |

***Chanzo:*** *Mpango Elekezi 2050*

## 5.4 Vyanzo vya Rasilimali Fedha na Mikakati ya Serikali

### 5.4.1 Vyanzo vya Kawaida vya Mapato

Serikali itaimarisha uwezo wake wa kugharamia Mpango kwa kutumia mchanganyiko wa vyanzo vya kawaida vya mapato, ambapo takriban Shilingi bilioni 115,043.30 zitaelekezwa katika utekelezaji wa Mpango. Ukusanyaji wa mapato ya ndani utaongezwa kwa kiasi kikubwa ili kuongeza mapato ya ndani kutoka msingi wa Shilingi bilioni 40,466.13 mwaka 2025/26 hadi kufikia jumla ya Shilingi bilioni 292,398.14 katika kipindi cha miaka mitano. Hili litafikiwa kwa kuongeza mapato ya ndani kutoka asilimia 14.9 hadi 20 ya pato la Taifa, uwiano wa kodi kwa pato la Taifa kutoka asilimia 13.3 hadi 18, na mapato yasiyo ya kodi kutoka asilimia 2.7 hadi 5.0 ya pato la Taifa.

Ukuaji huu wa mapato utachangiwa na ongezeko la idadi ya walipa kodi kufuatia usajili na urasimishaji wa sekta isiyo rasmi. Aidha, kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA na teknolojia ya kidijitali, kupanua wigo wa mifumo ya kielektroniki ya ulipaji kodi na kuunganisha huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi ili kuongeza mwitikio wa ulipaji kodi bila shuruti na kupunguza upotevu wa mapato. Vilevile, sera na mfumo wa usisimamizi wa kodi vitaboreshwa ili kuwa rafiki na kutabibirika. Kadhalika, mapato yasiyo ya kodi yataongezeka kwa kuimarisha usimamizi na kuongeza ufanisi wa Mashirika ya Umma pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na rasilimali za asilia.

Serikali itaendelea kusimamia mchakato wa ukopaji na usimamizi wa deni la Taifa Katika kipindi cha Mpango, ili kuhakikisha utulivu na uendelevu wa sera ya bajeti na uchumi kwa ujumla. Nakisi ya bajeti itadhibitiwa katika ukomo wa chini ya asilimia tatu ya pato la Taifa, sawa na jumla ya Shilingi bilioni 20,093.75 kwa kipindi cha Mpango. Lengo ni kuhakikisha utulivu wa uchumi na kuepuka kuathiri mitaji ya sekta binafsi. Deni la nje litasimamiwa kwa umakini kwa kuzingatia mkakati wa muda wa kati wa kusimamia deni la taifa  pamoja na taarifa za kila mwaka za tathmini ya uhimilivu wa deni. Jumla ya Shilingi bilioni 25,506.73 inatarajiwa kuwa mkopo wenye masharti nafuu na Shilingi bilioni 14,614.48, mkopo wa kibiashara hususan kwa ajili ya kugharamia miradi ya kielelezo yenye matokeo makubwa, tija na maslahi mapana kwa Taifa. Misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa washirika wa maendeleo itaendelea kuwa na mchango mkubwa, ikikadiriwa kufikia Shilingi bilioni 2,460.08. Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kugharamia miradi ya kijamii na kuimarisha uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

### 5.4.2 Udhibiti wa Matumizi na Mgawanyo wa Kimkakati

Serikali itapitia na kupanga upya matumizi ya fedha za umma pamoja na rasilimali zilizopo, ili kupanua wigo wa kifedha kwa utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo. Hatua hii itapunguza shinikizo kwenye bajeti na kuimarisha uwezo wa Serikali kugharamia miradi ya maendeleo kwa kupunguza utegemezi mkubwa wa mikopo. Miongoni mwa hatua na kimkakati itakayotumika ni pamoja na kufanya mapitio ya matumizi ya umma, kuboresha mifumo na kuweka vipaumbele katika matumizi ya Serikali ili kuhakikisha mgawanyo wenye tija na kuongeza ufanisi katika matumizi ya rasilimali fedha kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango IV. Lengo ni kupunguza upotevu, kudhibiti matumizi yasiyo na tija na kudhibiti matumizi yanayojirudia au mwingiliano wa shughuli zinazofanana. Fedha zitakazookolewa kutokana na maboresho hayo zitaelekezwa kwenye miradi yenye tija kubwa ya kiuchumi na kijamii. Kadhalika, kuhakikisha bajeti inatekelezeka na kudhibiti nakisi ya bajeti ndani ya ukomo uliowekwa kisheria. Aidha, serikali itaweka ukomo wa matumizi kisekta ili kudhibiti matumizi ya kawaida na kuelekeza fedha hizo katika matumizi ya maendeleo. Utekelezaji wa bajeti utazingatia matokeo, huku mfumo wa ufuatiliaji wa matumizi ya Serikali ukiimarishwa ili kupunguza upotevu wa fedha za umma na kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali hizo. Ugharamiaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati na malipo ya huduma zilizotolewa na sekta binafsi, utapewa kipaumbele mahsusi ili kuepuka ucheleweshaji usio wa lazima wa miradi na kudhibiti ongezeko la malimbikizo ya madeni ya wazabuni.

Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mageuzi katika mifumo ya usimamizi wa fedha za umma, utafutaji wa fedha, ugawaji, kuweka mifumo thabiti wa utoaji taarifa na takwimu za matumizi ya rasilimali za umma na kuhakikisha matumizi yanafanyika kwa kuzingatia vipaumbele katika Mpango. Maboresho hayo yanalenga kuhakikisha kuwa kila shilingi inatumika ipasavyo kugharamia vipaumbele vya maendeleo. Ili kuongeza uwazi na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu, Serikali itatumia mfumo wa bajeti unaoakisi mapato yanayotokana na matumizi yanapotokea. Hii itasaidia kuonesha kwa usahihi zaidi hali ya kifedha kwa wakati tofauti na mfumo wa bajeti unaozingatia fedha taslimu pekee.

Jitihada za kupunguza matumizi na kuboresha ufanisi katika mgawanyo wa rasilimali fedha zitahusisha hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwemo kuwezesha Mashirika ya Umma kujitegemea kifedha. Katika muktadha huo, mashirika hayo yatawajibika kugharamia matumizi yao ya kawaida kwa kutumia mapato yanayozalishwa ndani ya taasisi husika. Pia, yatapaswa kujiendesha kwa faida ya asilimia 10 ya uwekezaji uliolengwa ifikapo Juni 2031. Hatua hii itapunguza ruzuku kwa mashirika ya umma kwa angalau asilimia 50 ifikapo mwaka 2028 na kuokoa takribani Shilingi trilioni 1.5 zitakazoelekezwa katika kugharamia miradi ya maendeleo

Katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto sugu ya ajira hususan kwa vijana, Serikali itaanzisha Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji ambao utaunganisha mifuko ya uwekezaji iliyopo. Hatua hiyo itawezesha uzalishaji wa mtaji wa Shilingi bilioni 123.13 ifikapo Juni 2027. Mfuko huu unatarajiwa kuchochea ubunifu, kulea miradi ya vijana inayochipukia na kuipa sifa za kukopesheka katika taasisi za fedha, pamoja na kuvutia mitaji kutoka kwa wawekezaji. Mfuko huu utafanya kazi kwa uratibu wa pamoja na kushirikiana na mfuko wa Serikali za Mitaa/Halmashauri utakaotenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kufadhili miradi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Fedha hizo zinakadiriwa kufikia Shilingi bilioni 157.83 kwa mwaka 2025/26. Ushirikiano na uratibu wa pamoja wa mifuko hii kutasaidia kuongeza ufanisi na kupata matokeo makubwa. Mifuko ya halmashauri itaelekezwa katika kujenga kongani za biashara katika kila halmashauri au manispaa kwa lengo la kuchochea shughuli za kiuchumi za eneo husika. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji utajikita katika kutoa huduma za kifedha kama mikopo ya gharama nafuu, dhamana na mitaji ya kuanzisha biashara, pamoja na kulea

na kukuza miradi ya vijana. Serikali itaharakisha ukuaji wa Maeneo Maalum ya Uchumi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kutenga asilimia 10 ya fedha kutoka katika mifuko maalum iliyopo ikiwemo mfuko wa barabara, umeme vijijini, Maendeleo ya reli, mawasiliano kwa Wote na maji, bila kuathiri shughuli za msingi za mifuko hiyo. Matarajio ni kukusanya zaidi ya Shilingi trilioni 1.3 kutoka katika mifuko hiyo. Chanzo kingine ni fedha zinazoweza kuokolewa kupitia utekelezaji wa kampeni ya kutokomeza ugonjwa wa malaria ifikapo 2028 kupitia uwekezaji katika kinga na uteketezaji wa vimelea katika mazalia ya mbu. Kupitia kampeni hizi, Serikali inakadiriwa kuokoa Shilingi trilioni 4.2 katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya uidhibiti wa malaria.

Ili kuhakikisha nidhamu na uadilifu katika matumizi, Serikali itaanzisha Mfuko wa Taifa wa Akiba na Uwekezaji utakaokuwa na mfumo unaojitegemea ndani ya Wizara ya Fedha. Usimamizi wake utazingatia uwazi, uwajibikaji na kujiendesha kwa tija. Majukumu la msingi ya Mfuko ni kujenga uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya bei za bidhaa zinazozalishwa nchini na misukosuko ya kiuchumi na kijamii. Kadhalika, itaanzisha mfuko wa kuweka akiba ya mapato yatokanayo na rasilimali asilia kama gesi na madini kwa ajili ya vizazi vijavyo; Mfuko wa uwekezaji unaotokana na fursa na bidhaa mbalimbali za kifedha; na Mfuko wa maendeleo kwa ajili ya kufadhili miradi ya kijamii na kiuchumi. Kwa kuanzishwa kwa kinga hii ya kifedha, mfuko huo utasaidia kulinda bajeti ya Taifa dhidi ya misukosuko ya vipindi vya kupanda na kushuka kwa mapato, na kuweka msingi imara wa upangaji wa uchumi wa muda mrefu.  Fedha za mtaji katika Mfuko huu zitatokana na vyanzo mbali mbali ikiwemo sehemu ya mapato kutokana na mauzo ya rasilimali asilia hususan katika sekta ya madini na gawio kutoka katika mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara. Hivyo, Mfuko huu utawekeza katika Mashirika ya Umma na Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji katika maeneo huru ya kiuchumi na hivyo kuipunguzia Serikali shinikizo la kibajeti na kuchochea uwekezaji.

### 5.4.3 Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Fedha

Serikali itatumia vyanzo mbadala na bunifu vya fedha ili kuimarisha vyanzo vya kawaida vya fedha na ziada itakayopatikana katika mgawanyo wa kimkakati wa rasilimiali. Vyanzo hivyo vitajumuisha hatifungani za miundombinu, hatifungani za manispaa, na hatifungani za watanzania waishio ughaibuni. Pia, hatifungani za kijani pamoja na nyenzo nyingine za kifedha zitatumika kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa kuzingatia uwezo wa Tanzania kutekeleza vigezo vya uhifadhi wa mazingira na kufikia shabaha za maendeleo endelevu. Aidha, Serikali itatekeleza Mkakati wa Data Monetisation kwa kutumia kibiashara data zisizo za kibinafsi za Serikali ili kuanzisha chanzo kipya cha mapato, huku ikizingatia usalama wa taarifa.

Aidha, Serikali itaimarisha mfumo wa dhamana ya mikopo ya mauzo ya nje (export credit) ili kutoa dhamana na bima kwa wauzaji wa bidhaa nje ya nchi, kupunguza vihatarishi na kuwezesha taasisi za fedha nchini kutoa kwa urahisi mikopo kwa biashara zinazolenga masoko ya nje.  Hatua hii itawawezesha wafanyabiashara na wazalishaji kuaminiwa na taasisi za fedha na kukopeshwa kwa gharama nafuu. Kadhalika, utaratibu wa ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma utaimarishwa ili kuvutia uwekezaji mkubwa kutoka wa sekta binafsi.

Vyanzo hivi bunifu vitatekelezwa sambamba na matumizi ya mbinu mbadala za kugharamia utekelezaji wa Mpango, ikiwemo mikopo yenye masharti nafuu inayounganishwa na rasilimali asilia, fedha za mazingira ya kijani na biashara ya kaboni. Tanzania inatarajiwa kupata takribani Shilingi trilioni 15 kutoka biashara ya kaboni ifikapo Juni 2031. Vilevile, Serikali itaweka mazingira ya kukuza matumizi yenye tija na rasilimali ambazo hazijatumika ipasavyo, ikiwemo  kupitia mbinu za kuongeza thamani ya mali na ardhi, kama njia mbadala ya kuongeza mapato. Jedwali 5.3 linaonesha makadirio na mchango wa vyanzo bunifu na mbadala vya fedha.

*Jedwali 5.3: Makadirio na Uwiano wa Mchango wa Vyanzo Bunifu na Mbadala vya Fedha*

| **Chanzo** | **Shabaha** | **Makadirio (Sh. Trilioni)** |
|---|---|---|
| Maeneo Maalum ya Kiuchumi | Maeneo Maalum ya Kiuchumi matano (5) (mfano, Bagamoyo, Dodoma) kwa kuzingatia ubia wenye uwiano wa 1:3–1:4 baina ya Serikali na sekta binafsi. | 5.2–6.5 |
| Hatifungani ya Watanzania waishio ughaibuni | Dola za Marekani bilioni 1.0 kwa watanzania waishio nje ifikapo 2030/31 | 2.0-2.5 |
| Ugharamiaji wa masuala ya tabianchi na ujanishaji (Hatifungani za Kijanj) | Utafutaji wa fedha za mazingira kwa kushirikiana na wabia wenye ithibati; Kutekeleza malengo ya mazingira kitaifa dola za Marekani bilioni 4 kwa mwaka | 8–10 |
| Biashara ya Kaboni | Kunufaika na fursa ya biashara ya kaboni inayokadiriwa kufikia dola za Marekani bilioni 3 kwa mwaka ifikapo 2030/31 | 12–15 |
| Vyanzo vya fedha mseto | Mifuko ya maendeleo ya miundombinu ya barabara, nishati, na miradi ya biashara ndogo, ndogo za kati na za kati kupitia vyanzo vya fedha vya masharti nafuu | 2–3 |
| Biashara ya kukodisha/ kubinafsisha rasilimali zisizotumika (Asset Monetisation & Land Value Capture) | Lengo ni kuingiza Shilingi trilioni 2 ifikapo 2030/31 | 1.5-2.0 |
| Mfuko wa Mafao & Akiba | Kutumia ipasavyo mifuko ya mafao ya jamii na soko la mitaji | 3–4 |
| Taasisi za fedha za maendeleo (TADB na TIB) | Kutumia ipasavyo mitaji na ufadhili mchanganyiko | 6–8 |
| Mashirika ya Umma – Hatifungani na hisa | Kuandaa na kuuza hatifungani za kampuni/ miundombinu/kijani na ubia wa kimkakati wa hisaMiradi | 5–6 |
| Miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na inayokopesheka | Miradi 6–8 ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ifikapo 2030 | 4–5 |
| Majukwaa ya kidijitali/mtandao na huduma bunifu za fedha za kidijitali mtandao/kiganjani | Kuongezeka kwa matumizi ya huduma za fedha mtandao, kuongezeka kwa urasimishaji wa biashara ndogo na kati na ushiriki mkubwa wa umma katika kufadhili miradi kwa kuchangia kidogokidogo | 0.5–1.0 |
| Hatifungani ya maendeleo | Kuingizwa sokoni kwa miradi/sekta zenye matokeo makubwa | 0.5–1.0 |
| Jumla ya fedha zitakazokusanywa 42–62 | | |

***Chanzo:*** *Uchambuzi uliofanywa na waandishi*

***Ufafanuzi:*** *Jumla ya rasilimali zinazohitajika kwa utekelezaji wa Mpango IV ni Shilingi trilioni 477.746, kutoka vyanzo vya kawaida, bunifu na mbadala. Vyanzo bunifu na mbadala vinatarajiwa kuchangia kati ya asilimia 9 na 13, sawa na Shilingi trilioni 42–62, ambapo sehemu kubwa itatumika kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi, kuimarisha matumizi ya tija ya rasilimali za umma na kuvutia mitaji ya muda mrefu.*

## 5.5 Vyanzo na Mikakati ya Kuvutia Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Sekta binafsi inatarajiwa kuwekeza jumla ya Shilingi bilioni 324,487.46 katika kipindi cha miaka mitano. Kufikia lengo hili, Mpango unalenga kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje kufikia asilimia 10 ya pato la Taifa ifikapo 2030. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na kuboresha miundombinu na huduma za ugavi ikiwemo kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi yenye huduma za msingi. Serikali itaanzisha Mfuko wa Kuwezesha Maandalizi ya Miradi ili kuandaa miradi yenye ubora, inayotekelezeka kibiashara na yenye manufaa kwa Taifa. Aidha, Serikali itaondoa vizuizi katika soko la mitaji ifikapo Juni 2027 ili kuvutia uwekezaji na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa mitaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Vilevile, ili kukuza mitaji ya ndani na kupanua wigo wa mikopo, hatua za kimkakati zitachukuliwa kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi ya ndani kufikia asilimia 25–30 ya pato la Taifa. Hatua hizo zitahusisha mageuzi katika sekta ya benki ili kupunguza gharama za mikopo, kudhibiti kiwango cha mikopo chechefu kibaki chini ya ukomo wa kisheria wa asilimia 5, kuboresha soko la hisa na mitaji ili kukuza mitaji na ukwasi wa benki nchini.

Sambamba na jitihada hizi za kutekeleza programu ya urasimishaji biashara ndogo na za kati, kwa kulenga usajili angalau wafanyabiashara 250,000 kila mwaka na kuwawezesha kupata huduma za mikopo ya gharama nafuu. Lengo ni kuhakikisha kuwa angalau asilimia 40 ya wafanyabiashara wamesajiliwa rasmi ifikapo Juni 2031. Hatua hii itaambatana na maboresho ya miundombinu ya usimamizi wa mikopo pamoja na mifumo ya taarifa na tathmini ya wakopaji, ili kupanua wigo wa huduma na kufikia angalau asilimia 60 ya watu wazima. Katika kuboresha huduma ya dhamana, Shirika la Taifa la Dhamana litaanzishwa na kuimarishwa ili kutatua changamoto ya wakopaji wengi kushindwa kukidhi masharti la dhamana. Lengo ni kutoa dhamana zenye thamani ya Shilingi bilioni 7 ifikapo Juni 2031. Kadhalika, Taasisi za Fedha za Maendeleo zitaongezewa mitaji kupitia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na ufadhili mseto ili kuzijengea uwezo na ushindani katika soko. Vyanzo vingine muhimu vya kukuza mitaji ya muda mrefu ni hatifungani pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Sambamba na hilo, Serikali itawezesha kuanzishwa kwa huduma za fedha au mikopo katika mnyororo wa uzalishaji ili kuwawezesha wazalishaji kupata huduma za fedha za uhakika wakati wanapofanya makubaliano ya ununuzi na wateja wao. Pia, Jukwaa la Uwekezaji la Watanzania Waishio Ughaibuni litaanzishwa kuwaunganisha wafanyabiashara na wazalishaji hao na wale waliopo nchini.

Hatua hii itaongeza fursa za uwekezaji, kubadilishana uzoefu, kupata mafunzo na kujenga ushirikiano wa kiuchumi wenye manufaa kwa pande zote. Ili kuwafikia vijana, Dirisha la Uwekezaji Mahusus kwa Vijana litaanzishwa ndani ya mfumo wa kibenki ili kuwahudumia kundi la wajasiriamali vijana. Muhimu zaidi, jiji la Dar es Salaam litaendelezwa kimkakati na kupandishwa hadhi kuwa Kituo cha Kimataifa cha Huduma za Kifedha ili kuvutia mitaji ya aina mbalimbali kufikia lengo la angalau dola za Marekani bilioni 1 ifikapo Juni, 2031. Kwa maelezo zaidi, rejea Jedwali 5.4.

*Jedwali 5.4: Mikakati ya Kupata Fedha kutoka Sekta Binafsi*

| Shabaha | Hatua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **Lengo la 1: Kukuza Masoko ya Mitaji kwa ugharamiaji endelevu wa maendeleo na kuvutia uwekezaji wa nje** | | | | | | |
| 1. Kuongeza ushiriki wa wawekezaji wa kigeni katika soko la ndani la mitaji kwa angalau asilimia 50 ya Mtaji wa Soko ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kulifungua soko la mitaji zaidi ya nchi za EAC/SADC ili kuvutia uwekezaji zaidi kutoka nje ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | 1.2. Kuboresha miudombinu ya soko la mitaji kuendana na maendeleo ya teknlojia ya sasa ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | 1.3. Kuanzisha bidhaa bunifu mahususi kwa Diaspora na wawekezaji wengine wa nje kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **Lengo la 2: Kuongeza uwekezaji kwa njia ya ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi** | | | | | | |
| 1. Kuongeza mchango wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi hadi 10% ya pato la Taifa ifikapo Juni 2030 | 1.1 Kuimarisha Kituo cha ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kwa kukijengea uwezo wa kuchakata miradi na ufuatiliaji ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | 1.2 Kuipitia na kuiboresha mifumo ya udhibiti na kisheria ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kufikia Juni 2028 | | | | | |
| | 1.3 Kuanzisha mfumo wa Kupima Utendaji wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (viashiria vya utendaji, ulinganisha na nchi nyingine n.k.) kufikia Juni 2027 | | | | | |
| | 1.4. Kuanzisha mfuko wa dhamana mahususi kwa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kufikia Juni 2027 | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo la 3: Kuchochea Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Mitaji kutoka nje katika Sekta za Kimkakati ifikapo Juni 2030** | | | | | | |
| | 1.1 Kuharakisha utekelezaji wa Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara – Awamu ya Pili (MKUMBI II) ifikapo 2027 | | | | | |
| | 1.2 Kutunga sheria ya kuzuia mabadiliko makubwa ya sera na Sheria ya Fedha katika muda wa kati kufikia Juni 2028 | | | | | |
| | 1.3 Boresha taratibu za kujitoa kwa wawekezaji na mifumo ya ukwasi ifikapo Juni 2028 | | | | | |
| | 1.4 Kuanzisha benki ya kitaifa ya ardhi na kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| **Lango la 4: Kuongeza Ufadhili katika Miradi ya Mazingira na Uwekezaji wa Kijani ifikapo Juni 2031** | | | | | | |
| Kuongeza ufadhili katika miradi ya mazingira kufikia asilimia 8 ya pato la Taifa ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha Soko la Hiari la Kaboni ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | 1.2 Kusaini mikataba na makubaliano ya ushirikiano na masoko ya kaboni ya kimataifa ifikapo Juni 2030 | | | | | |
| | 1.3 Kuanzisha na kutekeleza programu ya nishati safi yenye mnasaba na biashara ya kaboni ifikapo 2027 | | | | | |
| | 1.4 Kuhakikisha Wizara ya Fedha inapata ithibati ya kuwa mwenyeji wa miradi ya Mfuko wa Kijani wa Tabianchi ifikapo Juni 2027. | | | | | |
| 2. Kuingiza sokoni hatifungani za miradi endelevu yenye thamani ya asilimia 1 ya Pato la Taifa ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuingiza sokoni mpango wa ubadilishanaji wa Madeni kwa miradi ya uhifadhi wa mazingira yenye thamani ya asilimia 10 ya deni la nje la taifa ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 2.2 Kuingiza sokoni hatifungani ya ubia (Serikali, Sekta binafsi) ili kufadhili miradi ya kijani ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo la 5: Kuvutia Mifumo/Taratibu Bunifu za Kugharamia Miradi Mikubwa ili Kuchochea Utekelezaji wa Miradi ya Miundombinu na Kimkakati ifikapo Juni 2031.** | | | | | | |
| 1. Kuongeza kiasi cha ufadhili kutoka vyanzo bunifu kulingana na ukomo wa DSA ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuziongezea mitaji Taasisi za Fedha za Maendeleo (TADB, TIB) ili ziweze kutumia fursa za ufadhiri kwa utaratibu wa ushirikiano ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | 1.2 Kuboresha mfumo wa kisheria na udhibiti ili kutoa fursa kwa taasisi za kifedha bobezi zinazojikita katika maeneo maalum (kama vile ufadhili wa miundombinu, benki za Kidijitali n.k) kufikia Juni 2028 | | | | | |
| | 1.3 Kuimarisha mfuko ya dhamana kwa miradi ya kimkakati ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| **Lengo la 6: Kuboresha Mwenendo wa Ukuaji na Ubora wa Mikopo kwa Sekta Binafsi kufikia 2031** | | | | | | |
| 1. Kuongeza mikopo ya sekta binafsi kufikia asilimia 10 ya mikopo yote ya ndani ifikapo Juni 2030. | 1.1 Kuendelea fanya maboresho ya sekta ya fedha ikiwemo kupunguza madeni chechefu hususan katika benki za maendeleo na kuwezesha benki kuingiza sokoni rasilimali zao ili kuongeza ukwasi. | | | | | |
| | 1.2 Kuimarisha mtaji na ukwasi kupitia hatua mbalimbali ikiwemo ulipaji wa malimbikizo ya serikali kwa watoa huduma wake. | | | | | |
| | 1.3 Kuanzisha mchakato wa utoaji zabuni wa upendeleo ili kuongeza ushiriki wa ndani katika miradi ya maendeleo ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.4 Kuongeza ujumuishi katika sekta ya fedha kwa kuboresha mifumo ya utambuzi wa wateja, matumizi ya akili unde na kanzidata za taarifa za wateja ifikapo Juni 2031. | | | | | |

### 5.6 Vyanzo na Mikakati ya Kutumia Rasilimali za Mashirika ya Umma

Mpango IV unayaweka Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara kama nyenzo muhimu za kugharamia maendeleo ya Taifa, yakitarajiwa kuchangia takribani Shilingi trilioni 38.216 katika kipindi cha utekelezaji. Ili kufanikisha lengo hili, Serikali itafanya mageuzi ya kiutendaji katika Ofisi ya Msajiri wa Hazina ili aweze kuelekeza jukumu lake katika usimamizi wa mashirika kibiashara, kuondoa mwingiliano wa majukumu na kuongeza thamani kibiashara.

Aidha, Serikali itaimarisha utawala bora na nidhamu ya kifedha kwa kuyaelekeza mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara kugharamia matumizi yao ya kawaida kupitia mapato ya ndani. Kadhalika, bodi na watendaji wakuu wa mashirika hayo watalazimika kusaini mikataba ya utendaji itakayoweka shabaha mahsusi za kifedha na kiutendaji, kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji, kuongeza ufanisi na kuhakikisha matokeo yanayopimika, ikiwemo kuhakikisha wanatengeneza faida ya angalau asilimia 10 ya mitaji ifikapo Juni 2031. Maboresho haya yanakadiriwa kupunguza ruzuku kwa mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara kwa angalau asimia 50 ifikapo mwaka wa fedha wa 2030/31.

Kufikia lengo lililowekwa, mashirika ya umma yatatumia mbinu mbalimbali za uhamasishaji wa rasilimali fedha, zikiwemo mapato ya ndani na kushiriki ipasavyo katika soko la mitaji. Shabaha ni kuorodhesha katika soko la hisa angalau mashirika matatu hadi matano yenye uwezo wa kujiendesha kibiashara, ili kuuza hisa za angalau Shilingi trilioni 2.0 ifikapo Juni 2031 na kuingiza sokoni hatifungani ya kampuni na miundombinu zenye thamani ya zaidi ya Shilingi trilioni 50.

Katika kuvutia ujuzi, teknolojia  na mitaji zaidi, mashirika ya umma yatapaswa kuingia ubia wa kimkakati wa umiliki wa hisa na ushirika wa kibiashara na wabia kati ya nane na kumi ili kukuza mtaji kwa takriban Shilingi trilioni 1.5 na kunufaika na uhamishaji wa maarifa, ujuzi na teknolojia. Vilevile, kwa upande wa mauzo na ukodishaji na ubinafsishaji wa rasilimali zisizotumika kwa tija, mashirika ya umma yatapaswa kuongeza mitaji kwa takribani Shilingi trilioni 1.5. Aidha, miradi isiyopungua sita hadi nane ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi itaanzishwa. Matarajio ni kuwa kwa kuhamasisha ushirikiano kati ya wawekezaji kutoka ndani na nje watavutia mtaji wa takribani Shilingi trilioni 4.0.

Ili kuwa na nguvu ya pamoja na kuzuia mtawanyiko wa rasilimali, mashirika ya umma yatashirikiana kimkakati. Hii ni pamoja na kuunganisha rasilimali kwa kuzingatia makundi ya kisekta kama vile, usafirishaji na ugavi, huduma, ujenzi wa nyumba ili kunufaika na maendeleo ya uchumi, kupunguza gharama za uwekezaji na utekelezaji wa miradi na kuongea nguvu ya ushindani wa kuweza kushiriki hata katika miradi iliyopo chini ya programu za Kielelezo za Mpango IV. Ushirikiano huu utafanywa kwa kutumia mikataba ya ushirikiano wa uwekezaji ili kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi. Mageuzi yatafanyika katika Ofisi ya Msajiri wa Hazina na kuanzisha Dirisha la  Uwekezaji ambao litafanya kazi kama chombo cha uwekezaji wa pamoja. Kuhakikisha ukaribu na jamii, mashirika ya umma yataunganisha bajeti zao za Uwajibikaji kwa jamii na kuzielekeza katika miradi ya kijamii yenye matokeo yanayopimika ilikuboresha ustawi wa watu. Jedwali 5.5 linawasilisha mikakati ya mashirika ya umma ya utafutaji wa rasilimali fedha.

*Jedwali 5.5: Mikakati ya Kutumia Rasilimali za Mashirika ya Umma*

| Shabaha | Hatua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2026/27 | 2026/27 | 2026/27 | 2026/27 |
| **Lengo 1: Kuongeza Umiliki wa Rasilimali za Viwango vya Juu, zenye Tija na Uwezo wa Kuleta Faida na Matokeo Endelevu Yayoonekana** | | | | | | |
| 1. Mchango wa uwekezaji wa mashirika ya umma kuongezeka kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10 | 1.1. Kupunguza idadi ya mashirika ya umma yanayojiendesha kwa hasara kwa asilimia 50 ifikapo 2029/30 | | | | | |
| | 1.2. Kuongeza kiwango cha matumizi yenye tija ya rasilimali za mashirika ya umma kwa asilimia 10. | | | | | |
| | 1.3. Kuongeza mapato na faida za mashirika ya umma ili kukuza mchango katika mapato ya Serikali yasiyo ya kikodi hadi asilimia 10 ifikapo 2027/28 | | | | | |
| | 1.4. Kuyafanyia mashirika ya umma mageuzi ya kina ili yawe injini ya ukuaji badala ya kujikita katika kutoa huduma. | | | | | |
| **Lengo la 2: Kuimarisha Mbinu ya Mashirika ya Umma ya Utafutaji wa Fedha na Ukuzaji wa Uwekezaji** | | | | | | |
| 2. Kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini na kujenga uwezo endelevu wa kifedha. Mashirika ya umma yawe na vyanzo vya uhakika vya fedha, yaweze kugharamia miradi ya uwekezaji na yasaidie ukuaji wa sekta binafsi. | 1.1. Kuweka mfumo thabiti wa usimamizi na utekelezaji wa majukumu | | | | | |
| | 1.2 Kutumia mfumo madhubuti wa utawala na usimamizi wa mapato na matumizi | | | | | |
| | 1.3. Kutafuta fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwemo: | | | | | |
| | 1.3.1. Masoko ya Mitaji | | | | | |
| | 1.3.2. Ufadhili Mchanganyiko (blended financing) | | | | | |
| | 1.3.3. Hisa na ubia wa kimkakati | | | | | |
| | 1.3.4. Hatifungani | | | | | |
| | 1.3.5. Dhamana | | | | | |
| | 1.3.6. Ubia wa Serikali na sekta binafsi | | | | | |
| | 1.3.7. Kuunganisha mitaji (pooling) | | | | | |
| | 1.3.8. Ukodishaji/ubinafsishaji wa rasilimali zisizotumika kwa tija | | | | | |

## 5.7 Mgawanyo wa Kina wa Rasilimali Fedha Kutoka Vyanzo Vikuu

Jumla ya gharama ya utekelezaji wa Mpango IV inakadiriwa kufikia Shilingi bilioni 477,746.76 zitakazopatikana kutoka vyanzo vitatu vikuu. Mfuko Mkuu wa Serikali utachangia Shilingi bilioni 115,043.30 (asilimia 22), sekta binafsi itachangia Shilingi bilioni 324,487.46 (asilimia 70), na mashirika ya umma yatachangia Shilingi bilioni 38,216.00 (asilimia 8). Muundo huu wa ugharamiaji unalenga kuharakisha mageuzi ya uchumi, kuimarisha uthabiti wa kiuchumi, na kusaidia kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa. Mchanganuo wa kina wa rasilimali fedha umeainishwa katika Jedwali 5.6.

*Jedwali 5.6: Rasilimali Fedha Zinazohitajika Kufadhili Mapango IV: Vyanzo Vikuu*

| Mapato ndani | Msingi 2025/26 | Makadirio ya Mpango IV (Shilingi Bilioni) | | | | | Jumla kwa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya ya kodi | Shilingi Bilioni | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | TZS |
| Mapato ya ndani | 40,466.13 | 45,806.25 | 51,455.18 | 57,658.40 | 64,831.20 | 72,647.11 | 292,398.14 |
| Mapato ya kodi | 32,157.63 | 36,629.32 | 41,253.27 | 46,230.78 | 52,180.90 | 58,626.41 | 234,920.68 |
| Mapato yasiyo ya kodi | 6,628.00 | 7,372.65 | 8,220.61 | 9,191.75 | 10,192.80 | 11,216.96 | 46,194.76 |
| Mapato ya Ndani ya Serikali za Mitaa | 1,680.51 | 1,804.28 | 1,981.30 | 2,235.88 | 2,457.50 | 2,803.74 | 11,282.70 |
| Misaada | 1,069.88 | 623.05 | 526.46 | 496.22 | 469.2 | 345.15 | 2,460.08 |
| Mikopo ya gharama nafuu | 6,047.04 | 6,046.07 | 5,851.65 | 4,863.37 | 4,495.60 | 4,250.03 | 25,506.73 |
| Mikopo ya Nje ya biashara | 2,629.01 | 2,750.37 | 2,842.67 | 2,923.83 | 2,990.10 | 3,107.51 | 14,614.48 |
| Mikopo ya ndani (Iliyosogezwa mbele (rollover) | 3,325.56 | 3,285.39 | 4,094.78 | 2,949.01 | 3,761.80 | 3,607.41 | 17,698.39 |
| Mikopo ya ndani | 2,952.63 | 3,254.42 | 3,677.04 | 4,074.93 | 4,345.00 | 4,742.36 | 20,093.75 |
| Jumla | 56,490.26 | 61,765.55 | 68,447.78 | 72,965.77 | 80,892.90 | 88,699.57 | 372,771.57 |
| Ongezeko la Mwaka la Mapato | | 4,471.69 | 4,623.95 | 4,977.51 | 5,950.12 | 6,445.51 | 26,468.78 |
| Rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya FYDP IV | 80,541.00 | 85,013.92 | 89,284.98 | 95,033.35 | 100,911.63 | 107,502.89 | 477,746.76 |
| Rasilimali kutoka Serikalini kwa ajili ya FYDP IV (Pamoja na Serikali za Mitaa) | 17,493.73 | 19,325.76 | 20,692.75 | 22,635.12 | 24,892.80 | 27,496.87 | 115,043.30 |
| Sekta binafsi (Ndani na Nje) | 58,393.16 | 60,144.96 | 62,250.03 | 64,740.03 | 67,329.63 | 70,022.82 | 324,487.46 |
| Mashirika ya Umma | 4,654.11 | 5,543.20 | 6,342.20 | 7,658.20 | 8,689.20 | 9,983.20 | 38,216.00 |
| Pato la Taifa | 241,412.30 | 266,160.02 | 289,076.75 | 313,178.12 | 345,185.59 | 375,550.64 | 317,830.23 |
| (Bei za Soko) | | | | | | | |
| Uwiano wa Mapato ya kodi kwa Pato la Taifa | 13.30% | 13.80% | 14.30% | 14.80% | 15.10% | 15.60% | 14.70% |
| Uwiano wa mapato yasiyo ya kodi kwa Pato la Taifa | 2.70% | 2.80% | 2.80% | 2.90% | 3.00% | 3.00% | 2.90% |
| Uwiano wa mapato ya Halmashauri kwa Pato la Taifa | 0.70% | 0.70% | 0.70% | 0.70% | 0.70% | 0.70% | 0.70% |
| Mchango wa mapato yote ya ndani katika Pato la Taifa | 16.80% | 17.20% | 17.80% | 18.40% | 18.80% | 19.30% | 18.30% |
| Uwiano wa Nakisi ya bajeti (NDF) kwa Pato la Taifa | 1.20% | 1.20% | 1.30% | 1.30% | 1.30% | 1.30% | 1.30% |
| Asilimia ya bajeti ya Serikali ya kutelekeza Mpango IV kwa Bajeti Kuu ya Serikali | 31.00% | 31.30% | 30.20% | 31.00% | 30.80% | 31.00% | 30.90% |

***Vyanzo:*** *Wizara ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania na Ofisi ya Takwimu ya Taifa*

## 5.8 Ugharamiaji Kisekta

Jumla ya Shilingi trilioni 477.7 zinatarajiwa kukusanywa ifikapo 2030/31 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo katika sekta 12 za kipaumbele (Jedwali 5.7 na 5.8). Sekta hizi, zilizoainishwa katika Mpango Elekezi 2050, zinalenga kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani, na hivyo kuharakisha maendeleo na ustawi wa Taifa. Mgawanyo huu wa rasilimali kisekta unatoa mwongozo katika uandaaji wa mipango ya mwaka, kwa kuhakikisha rasilimali zinaelekezwa kwenye vipaumbele vya maendeleo, kuimarisha uwazi na uwajibikaji, na kuwezesha usimamizi madhubuti wa utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa.

*Jedwali 5.7: Ugharamia wa Mpango IV Kisekta (%) – Msisitizo Ukiwa katika Uwekezaji katika Utaratibu wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi*

| Na. | Sekta | Wadau | Msingi/ Kianzio | Mchango wa Kisekta (%) | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| 1. | Miundombinu ya Usafirishaji na Uchukuzi | Serikali | 21.72 | 22.73 | 23.17 | 23.79 | 24.67 | 25.57 | 24.08 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.82 | 6.47 | 7.04 | 8.12 | 8.63 | 9.29 | 8.00 |
| | | Sekta Binafsi | 72.458 | 70.81 | 69.79 | 68.09 | 66.69 | 65.14 | 67.92 |
| 2. | Nishati na Uchimbaji Madini | Serikali | 21.71 | 22.72 | 23.16 | 23.78 | 24.69 | 25.57 | 24.08 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.84 | 6.479 | 7.053 | 8.089 | 8.601 | 9.304 | 8.004 |
| | | Sekta Binafsi | 72.45 | 70.80 | 69.78 | 68.13 | 66.71 | 65.13 | 67.92 |
| 3. | Viwanda na Biashara | Serikali | 21.69 | 22.73 | 23.19 | 23.80 | 24.69 | 25.58 | 24.09 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.86 | 6.44 | 7.05 | 8.11 | 8.61 | 9.32 | 7.99 |
| | | Sekta Binafsi | 72.46 | 70.83 | 69.76 | 68.09 | 66.69 | 65.10 | 67.92 |
| 4. | Kilimo, Mifugo na Uvuvi | Serikali | 21.73 | 22.74 | 23.19 | 23.79 | 24.68 | 25.58 | 24.08 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.80 | 6.45 | 7.02 | 8.07 | 8.59 | 9.27 | 8.01 |
| | | Sekta Binafsi | 72.47 | 70.81 | 69.79 | 68.13 | 66.73 | 65.15 | 67.92 |
| 5. | Elimu na Kujenga Ujuzi | Serikali | 21.67 | 22.76 | 23.22 | 23.78 | 24.72 | 25.55 | 24.09 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.88 | 6.46 | 6.99 | 8.15 | 8.65 | 9.29 | 8.00 |
| | | Sekta Binafsi | 72.45 | 70.78 | 69.79 | 68.07 | 66.63 | 65.16 | 67.91 |
| 6. | Afya na Kinga ya Jamii | Serikali | 21.73 | 22.78 | 23.13 | 23.80 | 24.68 | 25.56 | 24.08 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.83 | 6.53 | 7.02 | 8.08 | 8.60 | 9.27 | 7.99 |
| | | Sekta Binafsi | 72.44 | 70.69 | 69.86 | 68.11 | 66.71 | 65.17 | 67.93 |
| 7. | Maji, Usafi na Maendeleo ya Miji | Serikali | 21.62 | 22.66 | 23.23 | 23.75 | 24.71 | 25.65 | 24.09 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.90 | 6.54 | 7.08 | 8.13 | 8.63 | 9.23 | 8.00 |
| | | Sekta Binafsi | 72.48 | 70.79 | 69.69 | 68.13 | 66.67 | 65.13 | 67.91 |
| 8. | TEHAMA na Uchumi wa Kidigitali | Serikali | 21.62 | 22.66 | 23.23 | 23.75 | 24.71 | 25.65 | 24.09 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.90 | 6.54 | 7.08 | 8.13 | 8.63 | 9.23 | 8.00 |
| | | Sekta Binafsi | 72.48 | 70.79 | 69.69 | 68.13 | 66.67 | 65.13 | 67.91 |
| 9. | Utalii na Huduma | Serikali | 26.27 | 27.16 | 27.53 | 28.04 | 28.69 | 29.45 | 28.26 |
| | | Mashirika ya Umma | 7.13 | 7.76 | 8.29 | 9.55 | 10.04 | 10.71 | 9.38 |
| | | Sekta Binafsi | 66.61 | 65.08 | 64.18 | 62.40 | 61.26 | 59.84 | 62.37 |
| 10. | Mazingira na Uhimilivu wa Tabianchi | Serikali | 21.81 | 22.66 | 23.05 | 23.78 | 24.67 | 25.62 | 24.08 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.76 | 6.64 | 7.06 | 8.04 | 8.55 | 9.26 | 7.98 |
| | | Sekta Binafsi | 72.43 | 70.70 | 69.89 | 68.18 | 66.78 | 65.12 | 67.94 |

| Na. | Sekta | Wadau | Msingi/ Kianzio | Mchango wa Kisekta (%) | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| 11. | Utawala Bora na Usimamizi wa Umma (yaani, utekelezaji, usimamizi, na uratibu wa sera, mipango, na shughuli za kiserikali ili kuhudumia umma) | Serikali | 21.67 | 22.75 | 23.22 | 23.80 | 24.73 | 25.59 | 24.7 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.87 | 6.44 | 7.13 | 8.06 | 8.66 | 9.32 | 8.01 |
| | | Sekta Binafsi | 72.46 | 70.82 | 69.65 | 68.14 | 66.61 | 65.08 | 67.91 |
| 12 | Utafiti na Maendeleo | Serikali | 22.00 | 22.00 | 22.00 | 22.00 | 22.00 | 22.00 | 22.00 |
| | | Mashirika ya Umma | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 |
| | | Sekta Binafsi | 70.00 | 70.00 | 70.00 | 70.00 | 70.00 | 70.00 | 70.00 |
| 13 | Jumla Ndogo | Serikali | 21.71 | 22.73 | 23.18 | 23.79 | 24.68 | 25.58 | 24.08 |
| | | Mashirika ya Umma | 5.83 | 6.48 | 7.05 | 8.11 | 8.62 | 9.30 | 8.00 |
| | | Sekta Binafsi | 72.46 | 70.79 | 69.76 | 68.11 | 66.70 | 65.12 | 67.92 |
| | **Jumla Kuu** | | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** |

***Chanzo:*** *Imekokotolewa kutoka LTPP 2050 na Wizara ya Fedha*

*Jedwali 5.8: Ugharamia wa Mpango IV Kisekta (Shilingi bilioni) – Msisitizo Ukiwa katika Uwekezaji katika Utaratibu wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi*

| Na | Sekta | Wadau | Msingi/ Kianzio | Mchango wa Kisekta | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| 1 | Miundombinu ya Usafirishaji na Uchukuzi | Serikali | 4.4 | 4.85 | 5.2 | 5.68 | 6.26 | 6.91 | 28.91 |
| | | Mashirika ya Umma | 1.18 | 1.38 | 1.58 | 1.94 | 2.19 | 2.51 | 9.6 |
| | | Sekta Binafsi | 14.68 | 15.11 | 15.66 | 16.26 | 16.92 | 17.6 | 81.55 |
| 2 | Nishati na Uchimbaji Madini | Serkali | 2.64 | 2.91 | 3.12 | 3.41 | 3.76 | 4.15 | 17.36 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.71 | 0.83 | 0.95 | 1.16 | 1.31 | 1.51 | 5.77 |
| | | Sekta Binafsi | 8.81 | 9.07 | 9.4 | 9.77 | 10.16 | 10.57 | 48.96 |
| 3 | Viwanda na Biashara | Serikali | 2.11 | 2.33 | 2.5 | 2.73 | 3.01 | 3.32 | 13.89 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.57 | 0.66 | 0.76 | 0.93 | 1.05 | 1.21 | 4.61 |
| | | Sekta Binafsi | 7.05 | 7.26 | 7.52 | 7.81 | 8.13 | 8.45 | 39.17 |
| 4 | Kilimo, Ufugaji na uvuvi | Serikali | 1.76 | 1.94 | 2.08 | 2.27 | 2.5 | 2.76 | 11.55 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.47 | 0.55 | 0.63 | 0.77 | 0.87 | 1 | 3.84 |
| | | Sekta Binafsi | 5.87 | 6.04 | 6.26 | 6.5 | 6.76 | 7.03 | 32.58 |
| 5 | Elimu na Maendeleo ya Ujuzi | Serikali | 1.4 | 1.55 | 1.66 | 1.81 | 2 | 2.2 | 9.22 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.38 | 0.44 | 0.5 | 0.62 | 0.7 | 0.8 | 3.06 |
| | | Sekta Binafsi | 4.68 | 4.82 | 4.99 | 5.18 | 5.39 | 5.61 | 25.99 |
| 6 | Afya na Uhifadhi wa Jamii | Serikali | 1.23 | 1.36 | 1.45 | 1.59 | 1.75 | 1.93 | 8.08 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.33 | 0.39 | 0.44 | 0.54 | 0.61 | 0.7 | 2.68 |
| | | Sekta Binafsi | 4.1 | 4.22 | 4.38 | 4.55 | 4.73 | 4.92 | 22.79 |

| Na | Sekta | Wadau | Msingi/ Kianzio | Mchango wa Kisekta | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| 7 | Maji, Usafi na Maendeleo ya Miji | Serikali | 0.88 | 0.97 | 1.05 | 1.14 | 1.26 | 1.39 | 5.81 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.24 | 0.28 | 0.32 | 0.39 | 0.44 | 0.5 | 1.93 |
| | | Sekta Binafsi | 2.95 | 3.03 | 3.15 | 3.27 | 3.4 | 3.53 | 16.38 |
| 8 | TEHAMA na Uchumi wa Kidigitali | Serikali | 0.88 | 0.97 | 1.05 | 1.14 | 1.26 | 1.39 | 5.81 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.24 | 0.28 | 0.32 | 0.39 | 0.44 | 0.50 | 1.93 |
| | | Sekta Binafsi | 2.95 | 3.03 | 3.15 | 3.27 | 3.4 | 3.53 | 16.38 |
| 9. | Utalii na Huduma | Serikali | 0.70 | 0.77 | 0.83 | 0.91 | 1.00 | 1.10 | 4.61 |
| 10. | Mazingira na Uhimilivu wa Tabianchi | Serikali | 0.53 | 0.58 | 0.62 | 0.68 | 0.75 | 0.83 | 3.47 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.14 | 0.17 | 0.19 | 0.23 | 0.26 | 0.3 | 1.15 |
| | | Sekta Binafsi | 1.76 | 1.81 | 1.88 | 1.95 | 2.03 | 2.11 | 9.79 |
| 11. | Utawala Bora na Usimamizi wa Umma (yaani, utekelezaji, usimamizi, na uratibu wa sera, mipango, na shughuli za kiserikali ili kuhudumia umma) | Serikali | 0.96 | 1.06 | 1.14 | 1.24 | 1.37 | 1.51 | 6.31 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.26 | 0.30 | 0.35 | 0.42 | 0.48 | 0.55 | 2.10 |
| | | Sekta Binafsi | 3.21 | 3.30 | 3.42 | 3.55 | 3.69 | 3.84 | 17.8 |
| 12 | Utafiti na Maendeleo | Serikali | 0.12 | 0.12 | 0.12 | 0.12 | 0.12 | 0.12 | 0.82 |
| | | Mashirika ya Umma | 0.05 | 0.05 | 0.05 | 0.05 | 0.05 | 0.05 | 0.30 |
| | | Sekta Binafsi | 0.40 | 0.40 | 0.40 | 0.40 | 0.40 | 0.40 | 2.61 |
| Jumla Ndogo | | Serikali | 17.5 | 19.3 | 20.7 | 22.6 | 24.9 | 27.5 | 115.1 |
| | | Mashirika ya Umma | 4.7 | 5.5 | 6.3 | 7.7 | 8.7 | 10 | 38.2 |
| | | Sekta Binafsi | 58.4 | 60.1 | 62.3 | 64.7 | 67.3 | 70 | 324.4 |
| **JUMLA KUU** | | | **80.6** | **84.9** | **89.3** | **95** | **100.9** | **107.5** | **477.7** |

***Chanzo:*** *Imekokotolewa kutoka Mpango elekezi 2050 na Wizara ya Fedha*

## 5.9 Uratibu na Usimamizi wa Mkakati wa Kugharamia Mpango

Utekelezaji wenye mafanikio wa mkakati huu wa kugharamia Mpango unahitaji usimamizi thabiti na uratibu wa karibu miongoni mwa taasisi kuu za kitaifa. Hivyo, Serikali itaanzisha Kamati ya Uratibu wa Ugharamiaji wa Mpango itakayoongozwa na Wizara ya Fedha, ikijumuisha Benki Kuu ya Tanzania, Tume ya Taifa ya Mipango, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na wawakilishi wa sekta binafsi. Kamati hii itasimamia utekelezaji wa mkakati wa kugharamia Mpango, kutatua changamoto za uratibu kati ya taasisi, kuhakikisha ulinganifu wa sera katika nyenzo mbalimbali za ugharamiaji, na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kila robo mwaka kwa Baraza la Mawaziri. Mfumo huu wa uratibu wa kati ni muhimu katika kudumisha mshikamano wa kimkakati, kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kujitokeza, na kuhakikisha taasisi zote zinafanya kazi kwa pamoja kufikia lengo la kukusanya Shilingi trilioni 477.7 zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango IV.

## 5.10 Hatua za Kimkakati na Viashiria Vikuu vya Utafutaji

Utekelezaji wa Mpango utaongozwa na hatua za kimkakati zenye malengo mahsusi ya kuongeza upatikanaji wa rasilimali fedha. Malengo makuu ni pamoja na kuimarisha soko la mitaji ili kuongeza ushiriki wa wawekezaji wa nje kufikia angalau asilimia 50 ifikapo Juni 2031; kuboresha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuongeza mchango wake kufikia asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2030; na kuharakisha uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje kwa kufikia angalau asilimia 10 ya Pato la Taifa. Tanzania itaongeza ukusanyaji wa mapato kupitia ufadhili wa miradi ya mazingira

kufikia asilimia 8 ya pato la Taifa ifikapo 2031; kuimarisha vyanzo bunifu vya fedha kwa kuongeza mtaji katika taasisi za fedha za maendeleo; na kupanua upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa kuongeza ushiriki wake katika mikopo ya ndani. Hatua hizi, kama zilivyoainishwa katika Jedwali 5.9, zinalenga kujenga mfumo thabiti, shindani na wenye ufanisi wa ugharamiaji wa maendeleo, utakaowezesha kufikiwa kwa malengo ya maendeleo ya Taifa.

*Jedwali 5.9: Muhtasari wa Hatua Muhimu za Kimkakati, Matokeo Tarajiwa, na Muda wa Utekelezaji*

| Na | Hatua Mahususi | Matokeo Tarajiwa | Muda wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji | Mifuko ya uwezeshaji nchini kuunganishwa. Hatua hii iwezeshe kupatikana kwa Shilingi bilioni 123.13 zitakazotumika kama dhamana ya mikopo na mitaji kwa biashara changa za makundi maalum ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. | Ifikapo 2027 |
| 2. | Kupunguza ruzuku kwa mashirika ya umma. | Mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara kupewa jukumu la kugharamia matumizi yao ya kawaida ili kupunguza ruzuku kwa zaidi ya 50% na kuiwezesha Serikali kuokoa Shilingi trilioni 1.5. | Ifikapo 2029 |
| 3. | Kutenga asilimia 10 ya mapato kutoka katika mifuko ya Serikali kugharamia uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi | Kiasi cha zaidi ya Shilingi trilioni 1.3 kutengwa katika utekelezaji wa Mpango IV kuharakisha uendelezaji wa angalau SEZ tano (5) | Muda wote wa Mpango |
| 4. | Kutenga asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri kwa ajili ya miradi ya maendeleo. | Fedha zilizotengwa kugharamia mitaji ya biashara changa na kuwezesha uanzishwaji wa kongani/maeneo maalum ya biashara katika kila Halmashauri/Manispaa. | Muda wote wa Mpango |
| 5. | Kufuzu kuwa taifa lililotokomeza ugonjwa wa Malaria. | Kiasi cha Shilingi trilioni 4.2 kuokolewa katika bajeti kuu ya Serikali kupitia mpango wa kutokomeza ugonjwa wa Malaria kwa njia ya kinga. | Ifikapo 2030 |
| **Na** | **Hatua Mahususi** | **Matokeo Tarajiwa** | **Muda wa Utekelezaji** |
| 6. | Kuanzisha Mfumo wa Kutambua, Kuvutia na Kuratibu Fedha Endelevu. | Serikali itaanzisha mfumo wa uainishaji wa shughuli za kijani na endelevu ili kuvutia fedha za kimataifa za miradi ya mazingira na maendeleo endelevu. | Ifikapo 2027 |
| 7. | Kuingiza sokoni Hatifungani ya Serikali mahsus kwa masuala ya uhifadhi wa mazingira. | Hatifungani iliyofungamanishwa na vigezo vya uhifadhi wa mazingira yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1 kuuzwa ili kuhamasisha maendeleo endelevu. | Ifikao 2031 |
| 8. | Serikali kuondoa kabisa vizuizi na sheria zinazokwamisha utiririkaji wa mitaji (pesa na mali) kuingia na kutoka nchini. | Vizuizi dhidi ya uingiaji na utokaji wa mitaji kuondolewa ili kuvutia uwekezaji kutoka nje | Ifikapo 2027 |
| 9. | Kurasimisha biashara ndogo na za kati. | Biashara ndogo na za kati 250,000 ziwe zinasajiriwa kila mwaka na asilimia 40 ya hizo ziwezeshwe kupata huduma rasmi za kifedha. | Kipindi chote cha Mpango |
| 10. | Kuanzisha Shirika la Dhamana ya Mikopo kwa wauzaji bidhaa na huduma nje. | Dhamana ya takribani Shilingi bilioni 7 kutolewa kwa walengwa ili kutatua changamoto ya ufinyu wa dhamana na kupunguza hatari zinazoweza kusababisha hasara kwa wauzaji bidhaa na huduma nje na hivyo kuchochea upatikanaji wa fedha za kigeni. | Ifikapo Juni 2031 |
| 11. | Kuzindua na kuanzisha jukwaa la Diaspora mahususi kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa mitaji. | Wafanyabiashara wadodo na wa kati kuunganishwa kimkakati na Wana-Disapora ili kunufaika na fursa za uwekezaji na mafunzo. | Ifikapo 2028 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Kuorodhesha katika Soko la Hisa Dar es-Salaam mashirika ya umma 3-5. | Hisa zenye thamni ya Shilingi trilioni 2.0 kupatikana kutoka katika soko la mitaji | Ifikapo 2031 |
| 13. | Kuanda na kuuza sokoni hatifungani ya mashirika ya umma na miundombinu. | Shilingi trilioni 5.0 kupatikana kutoka soko la mitaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali | Kipindi chote cha Mpango |
| 14. | Serikali kuanzisha Ubia wa Kimkakati na makampuni 8-10 kutoka sekta binafsi ili kuunganisha rasilimali kwa ajili ya miradi ya kimkakati. | Shiling trilioni 1.5 kupatikana kupitia hisa na ubadilishanaji wa maarifa/teknolojia. | Ifikapo Juni 2031 |
| 15. | Kuanzisha Kituo cha Kimataifa cha Huduma za Kifedha Dar es Salaam | Dola za Marekani bilioni 1 kuvutiwa nchini kutokana na uanzishwa kwa Kituo cha Kimataifa cha Huduma za Kifedha Dar es Salaam | Ifikapo 2031 |
| 16. | Kuanzisha utaratibu wa kuwezesha taasisi za kifedha kugharamia/kufadhili hatua mbalimbali za mnyororo wa uzalishaji na ugavi. | Wazalishaji wa ndani kupatiwa huduma za kifedha/ufadhili pindi mauzo ya bidhaa zao yanapothibitishwa na wanunuzi. | Kipindi chote cha Mpango |
| 17. | Kuimarisha na kutekeleza mageuzi katika sekta ya benki. | Mikopo chechefu kudhibitiwa chini ya ukomo wa kisheria wa asilimia 5 na mchakato wa kubadili madeni kuwa dhamana kuboreshwa ili rasilimali hizo za benki kuuzwa kwa wawekezaji na kuwezesha benki kujiongezea ukwasi. | Kipindi chote cha Mpango |
| 18. | Kuboresha Miundombinu ya Usimamizi wa Mikopo. | Wigo wa Kanzidata ya Taarifa za Wakopaji kuongezeka kufikia kuhifadhi taarifa za angalau asilimia 60 ya walengwa. | Ifikapo 2031 |
| **Na** | **Hatua Mahususi** | **Matokeo Tarajiwa** | **Muda wa Utekelezaji** |
| 19. | Kuingiza sokoni hatifungani ya Diaspora iliyofungamanishwa na fedha wanazorejesha nyumbani/nchini. | Makusanyo/uwekezaji kutoka kwa Watanzania waishio nje ufikie angalau dola za Marekani bilioni 1.0 ifikapo 2030/31. | Ifikapo 2031 |
| 20. | Kutekeleza Mkakati wa Kuziongezea Takwimu Thamani ya Kiuchumi ili kuongeza kipato, kupunguza gharama na kuboresha utendaji. | Kuwa na chanzo kipya cha mapato kupitia biashara ya maarifa kutoka katika uchakataji wa takwimu za Serikali zisizohusiana na watu binafsi. | Ifikapo Juni 2031 |
| 21. | Kuanzisha Soko la Kaboni la Tanzania. | Kuwezesha uratibu, kuongeza uwazi na kuwa na biashara ya kaboni yenye tija itakayoliingizia taifa angalau Shilingi trilioni 15 ifikapo 2031. | Ifikapo Juni 2031 |
| 22. | Kuimarisha Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wauzaji Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi. | Kuongezeka kwa huduma ya dhamana na bima kwa Watanzania wanaouza bidhaa na huduma nje. Hatua hii itahamasisha ukuaji wa mauzo ya nje, kuongeza ajira, kukuza fedha za kigeni na kusaidia biashara kukabiliana na changamoto za ushindani wa kimataifa. | Kipindi chote cha Mpango |
| 23. | Kuunganisha bajeti za mashirika ya umma zinazohusiana na Uwajibikaji kwa Jamii kwa uratibu mzuri na matokeo makubwa. | Fedha kwa ajili ya Uwajibikaji uni kwa Jamii kuongezeka na kuelekezwa kwenye miradi ya kipaumbele yenye matokeo makubwa katika jamii. | Kipindi chote cha Mpango |
| 24. | Kuanzisha Kamati ya Uratibu wa Ugharamiaji wa Mpango inayojumuisha taasisi/wadau mbalimbali. | Kuimarika kwa ufuatilia, utekelezaji, utatuzi wa vikwazo, na kuhakikisha vyombo vyote vya ufadhili vinaendana na sera na mipango husika. | Ifikapo 2027 |
| 25. | Kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji Mahususi kwa Vijana. | Kutoa bidhaa/huduma za kifedha mahususi kwa wajasiriamali wachanga | Ifikapo 2028 |
| 26. | Kukodishaji na kubinafsisha raslimali za mashirika ya umma zisizotumika kwa tija | Kupatikana wa Shillingi trilioni 2 ifikapo 2030/31 kwa kukodisha na kubinafsisha rasilimali zisizotumika kwa tija | Ifikapo 2031 |

# MUHTASARI – SURA YA TANO

MPANGO IV · SURA YA 5

## Ugharamiaji na Utafutaji wa Rasilimali

### Mfumo wa uwekezaji wa uwiano 70:30 wa sekta binafsi na umma

Mfumo wa kutafuta, kugawa na kusimamia rasilimali fedha za Mpango IV — mfumo unaoongozwa na soko unaoiweka sekta binafsi kama injini kuu ya ukuaji wa uchumi.

**TZS 477.7T**
RASILIMALI ZINAZOHITAJIKA

**USD 183B**
WIGO WA MIAKA 5

**70:30**
UWIANO BINAFSI KWA UMMA

**12**
SEKTA ZA KIPAUMBELE

MPANGO IV · Sura ya 5 — *Ugharamiaji na Utafutaji wa Rasilimali*

MUUNDO WA UGHARAMIAJI

## Wachangiaji Watatu — Mgawanyo wa 70:22:8

Mfumo unaoongozwa na soko ambapo sekta binafsi inaongoza, ikiungwa mkono na uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato ya serikali na Mashirika ya Umma yaliyoimarishwa.




TZS TRILIONI 477.7 — JUMLA YA WIGO

**70%**
**TZS 324.49T · Sekta Binafsi**
Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, ubia, nyenzo za kijani na tabianchi pamoja na mitaji ya ndani katika miundombinu na viwanda.

**22%**
**TZS 115.04T · Wizara na Halmashauri**
Ukusanyaji wa mapato ya ndani na ukopaji endelevu — mapato ya kodi na yasiyo ya kodi pamoja na deni la busara.

**8%**
**TZS 38.22T · Mashirika ya Umma**
Injini za kimkakati kupitia mapato yanayorejeshwa, nyongeza ya mtaji na ubia wa hisa.

MPANGO IV · Sura ya 5 — *Wachangiaji Watatu · Mgawanyo 70:22:8*

UGHARAMIAJI MBADALA NA BUNIFU

## Vyanzo Bunifu — TZS 42–62T za Mtaji Kichocheo

Vimebuniwa si kuchukua nafasi ya ushiriki wa sekta binafsi bali kuvutia, kupunguza vihatarishi na kuongeza nguvu ya uwekezaji katika wigo wote wa uchumi.

| Chanzo | Kiasi |
|---|---|
| Soko la Biashara ya Kaboni | TZS 12-15T |
| Fedha za Tabianchi na Kijani | TZS 8-10T |
| Benki za Maendeleo (TADB na TIB) | TZS 6-8T |
| Maeneo Maalum ya Kiuchumi | TZS 5.2-6.5T |
| Hati Fungani na Hisa za Mashirika | TZS 5-6T |
| Miradi ya Ubia Inayokopesheka | TZS 4-5T |
| Mifuko ya Pensheni na Muda Mrefu | TZS 3-4T |
| Ugharamiaji Mseto | TZS 2-3T |
| Hati Fungani za Watanzania Wanaoishi Nje | TZS 2-2.5T |
| Uhuishaji wa Mali | TZS 1.5-2T |
| Kidijitali na Ukusanyaji wa Umati | TZS 0.5-1T |
| Hati Fungani za Matokeo na Athari | TZS 0.5-1T |

**TZS 42–62 Trilioni Jumla · 9–13% ya wigo wote wa rasilimali**

MPANGO IV · Sura ya 5 — *Vyanzo Bunifu vya Ugharamiaji*

MWENENDO NA MGAWANYO WA MIAKA MITANO

## Rasilimali za Mwaka TZS 80.5T → TZS 107.5T

Mwenendo wa mwaka wa jumla ya rasilimali sambamba na mgawanyo wa kisekta — ukiimarisha uaminifu na utabirifu wa fedha za Mpango IV.

### JUMLA YA RASILIMALI ZA MWAKA (TZS TRILIONI)

| Mwaka | TZS Trilioni |
|---|---|
| 2025/26 Msingi | 80.5 |
| 2026/27 | 85.0 |
| 2027/28 | 89.3 |
| 2028/29 | 95.0 |
| 2029/30 | 100.9 |
| 2030/31 | 107.5 |

### SEKTA KUU ZA KIPAUMBELE (TZS TRILIONI)

| Sekta | Kiasi |
|---|---|
| 1 · Uchukuzi na Usafirishaji | TZS 120.1T |
| 2 · Nishati na Madini | TZS 72.1T |
| 3 · Viwanda na Biashara | TZS 57.7T |
| 4 · Kilimo na Uvuvi | TZS 48.0T |
| 5 · Elimu na Ujuzi | TZS 38.3T |
| 6 · Afya na Kinga ya Jamii | TZS 33.6T |
| 7 · Utawala na Utumishi wa Umma | TZS 26.2T |
| 8 · Maji, Usafi na Miji | TZS 24.1T |

MPANGO IV · Sura ya 5 — *Mwenendo wa Miaka Mitano · Mgawanyo wa Kisekta*






# SURA YA SITA: USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA UWAJIBIKAJI





# SURA YA SITA

# USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA UWAJIBIKAJI

## 6.1 Muhtasari

Mipango ya maendeleo ya miaka mitano ya utekelezaji wa Dira 2025 (Mpango wa Maendeleo I, II na III), ilitekelezwa kwa kuzingatia taratibu mahsusi za usimamizi zilizowekwa na Serikali. Utekelezaji ulihusisha wadau mbalimbali ikiwemo Wizara, Idara, Taasisi na Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi, asasi za kiraia na washirika wa maendeleo. Aidha, utekelezaji wake ulifanyika kupitia mipango ya maendeleo ya kila mwaka iliyofungamanishwa na mzunguko wa bajeti ya Taifa ili kuhakikisha uwiano kati ya mipango na sera ya fedha za umma.

Katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 (Mpango III), usimamizi, uratibu na ufuatiliaji ulizidi kuimarika kufuatia kurejeshwa kwa Tume ya Taifa ya Mipango. Tume imepewa jukumu la kuandaa, kusimamia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Vilevile, Serikali ilianzisha vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini katika taasisi zote za umma pamoja na kuweka mikakati ya kuimarisha ufuatiliaji wa matokeo na uwajibikaji.

Hivyo, utekelezaji wa miradi mingi katika kipindi hiki ulipata mafanikio makubwa na uwianifu kati ya mipango na utekelezaji wa bajeti uliongezeka. Licha ya mafanikio haya, changamoto kadhaa zilibainika katika utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kushindwa kuainisha bayana vipaumbele vya mipango na mpangilio wa muda wa utekelezaji wake baina ya taasisi. Hali hii ilisababisha kuwepo kwa miradi mingi mikubwa kutekelezwa kwa wakati mmoja na hivyo gharama zake kuzidi uwezo wa kugharamia na usimamizi wa utekelezaji. Aidha, rasilimali zililazimika kugawiwa kidogo kidogo katika maeneo mengi na hivyo kuchangia miradi kuchelewa au kutokukamilika kikamilifu.

Utegemezi mkubwa wa fedha za umma kugharamia utekelezaji pia ulipunguza matumizi ya mifumo mbadala ya ugharamiaji, kama vile uwekezaji wa moja kwa moja wa sekta binafsi, ubia kati ya sekta za umma na binafsi, pamoja na vyanzo bunifu vya fedha, mintaarafu, hati fungani za kijani na hati fungani za Watanzania waishio ughaibuni. Aidha, mifumo mingi ya Ufuatiliaji na Tathmini ilikosa viashiria bayana na takwimu zinazojitosheleza. Vilevile, kukosekana kwa mfumo thabiti wa kuratibu na kutoa mrejesho kwa wakati kuliathiri utekelezaji na ujifunzaji. Kadhalika, kasi ya ugatuzi wa madaraka na rasilimali kwa mamlaka za serikali za mitaa ilidorora na hivyo kudhoofisha utekelezaji katika ngazi ya jamii. Hamasa kubwa ya ushiriki wa wadau iliyokuwepo wakati wa kuandaa mpango, ilipungua wakati wa utekelezaji. Aidha, mchango na majukumu ya Mashirika ya Umma katika kuchangia utekelezaji wa mipango hayakufafanuliwa kwa uwazi na hivyo kuathiri uratibu na uwajibikaji wa taasisi hizo.

Mafunzo yaliyotokana na uzoefu huu yanaonesha kuwa mafanikio ya Mpango IV yanahitaji: (i) Kuboresha uwezo wa kitaalam na mifumo ya usimamizi wa utekelezaji itakayosimamiwa na Tume ya Taifa ya Mipango; (ii) kukuza uwezo wa kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa miradi na utunzaji wa nyaraka; (iii) kuweka mkakati shirikishi wa kugharamia unaopanua wigo wa vyanzo vya fedha na kutumia mbinu bunifu za ugharamiaji; (iv) kujikita katika misingi ya utendaji inayozingatia matokeo na uwajibikaji; (v) kuimarisha ushiriki wa wadau; (vi) kuharakisha ugatuzi wa madaraka na rasilimali (vii) kuboresha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwa kutumia teknolojia za kidijitali; (viii) kuhakikisha msimamo wa kisiasa ulio thabiti na uwepo wa sera endelevu na

zisizoyumba au kubadilikabadilika. Kwa ujumla, masuala haya yanahitajika ili kujenga msingi imara utakaowezesha Mpango IV kutekelezwa kwa mwelekeo unaozingatia matokeo na uwajibikaji.

### 6.2 Mfumo na Mikakati ya Utekelezaji

Mpango huu unatekelezwa kwa mtazamo jumuishi unaoshirikisha Serikali na jamii kwa ujumla, kwa kufungamanisha vipaumbele vya Taifa na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka, Mwongozo wa Bajeti na Mpango wa Matumizi ya Serikali wa Muda wa Kati. Utekelezaji unaongozwa na mgawanyo wa majukumu ya taasisi ulioainishwa bayana, mikataba ya utendaji yenye viashiria vinayopimika, na ufuatiliaji unaozingatia ushahidi chini ya uratibu wa Tume ya Mipango, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, wizara za kisekta na wadau wengine. Mikakati mikuu ni:

i. **Uratibu Madhubuti**
Tume ya Mipango itaongoza utekelezaji na usimamizi wa Mpango ili kuhakikisha uwiano wa kimkakati wa hatua na vipaumbele miongoni mwa Wizara, Idara na Wakala, Mashirika ya Umma na Taasisi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na sekta binafsi.

ii. **Uwianishaji wa Mipango na Bajeti**
Taasisi zote zitaoanisha mipango, bajeti na viashiria vya utendaji na vipaumbele vya Mpango IV.

iii. **Kuainisha Vipaumbele vya Kimkakati**
Rasilimali zitaelekezwa kwenye sekta za mageuzi na miradi ya kielelezo yenye uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa. Utekelezaji utafanyika kwa awamu ili kuhakikisha mwendelezo na uwezo wa kuhimili mabadiliko.

iv. **Kuwezesha Uwekezaji wa Sekta Binafsi**
Kuimarisha majadiliano ya mara kwa mara kati ya sekta ya umma na binafsi, kurasimisha biashara zilizo katika sekta isiyo rasmi, kupanua ubia kati ya sekta ya umma na binafsi katika utekelezaji wa Mpango IV.

v. **Ushiriki Mpana wa Jamii**
Kukuza ushiriki wa wananchi na umiliki wa Mpango kupitia kampeni za uhamasishaji na mipango ya uchumi ngazi ya jamii.

vi. **Mifumo Madhubuti ya Ukusanyaji wa Taarifa na Ufuatiliaji:**
Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu, kuunganisha vyanzo vya taarifa, na kuboresha upatikanaji wake kupitia majukwaa ya kidijitali ili kuwezesha ufuatiliaji unaoendana na wakati.

vii. **Usanifu na Usimamizi wa Miradi:**
Kutumia mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa miradi ili kuimarisha usanifu wa miradi na ufuatiliaji wake kwa ukamilifu na viwango vya juu.

viii. **Ufuatiliaji na Tathmini**
Kuwianisha mifumo ya kisekta ya ufuatiliaji na tathmini na mfumo wa utekelezaji unaozingatia matokeo.

ix. **Usimamizi Unaotegemea Takwimu na Ushahidi**
Kutumia dashibodi zinazoendeshwa na akili-unde na zana za kidijitali ili kuimarisha uwazi na kutoa fedha kwa kuzingatia matokeo ya utendaji.

### 6.3 Utaratibu wa Kufungamanisha Mipango

Utekelezaji wa Mpango IV unazingatia mfumo fungamanishi wa mipango ya kati kuendana na Mpango Elekezi 2050. Lengo ni kuhakikisha kuwa matarajio ya muda mrefu yanatekelezwa sawia katika malengo ya muda wa kati na matokeo kupimika katika kipindi husika. Kwa utaratibu huu, vipaumbele vya Mpango vitatekelezwa kupitia mipango ya maendeleo ya kila mwaka, ikibainisha shughuli, viashiria na rasilimali zinazohitajika kwa utekelezaji wa malengo ya Mpango kwa mwaka husika kwa kufungamanishwa katika

mpango na bajeti ya Taifa na kisekta. Ili kuinua ufanisi na kuondoa migongano katika utekelezaji, uratibu utaimarishwa kupitia mifumo ya upangaji, vikosikazi na majukwaa ya kidijitali yanayounganisha taasisi husika. Hatua hii itawezesha utekelezaji wa pamoja wa miradi ya kielelezo kwa wakati. Tume ya Mipango itaongoza na kuratibu ufuatiliaji wa kimkakati ili kuhakikisha uwianifu wa sera na mikakati ya utekelezaji na hivyo kuimarisha uongozi wenye uwazi katika mawasiliano, vipaumbele vya utekelezaji, majukumu na maamuzi, sanjari na uwajibikaji kitaasisi. Aidha, sekta binafsi, asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali yatahamasishwa kuoanisha programu za uwekezaji wake na vipaumbele vya kitaifa.

### 6.4 Mpangilio wa Majukumu ya Taasisi na Usimamizi wa Utekelezaji

Mchoro Namba 6.1 unaonesha muundo wa uratibu na utekelezaji kuakisi Dhana ya Mabadiliko kufikia matokeo yanayopimika. Wizara, Idara na Taasisi zinawajibika kufanikisha matokeo ya utekelezaji katika maeneo yao. Vile vile, Serikali za Mamlaka za Mitaa, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zitatekeleza programu katika ngazi ya jamii ili kuhakikisha kunakuwa mafanikio jumuishi na kutoa mrejesho. Uratibu wa kitaifa utaongozwa na Tume ya Mipango, ambayo imepewa jukumu la uangalizi na usimamizi kimkakati. Pia, Tume ya Mipango itahakikisha uwiano wa sera ya uwekezaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wake kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Aidha, ili kuwianisha utekelezaji wa mipango na sera ya fedha za umma, Tume ya Mipango itashirikiana na Wizara ya Fedha kupitia Mfumo wa Matumizi ya Serikali wa Muda wa Kati. Vile vile, Ofisi ya Msajili wa Hazina itaimarisha utendaji wa Mashirika ya Umma kwa kufanyia mabadiliko mifumo ya uendeshaji, mikataba ya utendaji na kutafsiri sera ya ubia katika uwekezaji.

Serikali itaimarisha usimamizi na uwajibikaji kwa kuratibu sekta mbalimbali, kuunda vikosi kazi vya kisekta, na kuendesha majukwaa ya majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi yatakayounganisha Programu za Kielelezo, Wizara, Idara na Taasisi, pamoja na vyombo vya udhibiti na urekebu. Dashibodi za kidijitali na mifumo ya ufuatiliaji inayozingatia matokeo itatoa taarifa mbashara za hatua za utekelezaji kwa wakati, hivyo kuwezesha usimamizi unaoendana na mabadiliko na kuimarisha uwajibikaji kwa wananchi. Aidha, Mahakama, hususan Divisheni ya Biashara, itahakikisha inatatua migogoro kwa wakati na ufanisi. Vyombo vya habari pamoja na vitengo vya mawasiliano na uhusiano wa umma katika Wizara, Idara na Taasisi vitaongeza uwazi na kuboresha mawasiliano na umma. Aidha, wananchi wataendelea kuwa wahusika wakuu katika utekelezaji kwa kushiriki kikamilifu katika ufuatiliaji na kutumia mifumo ya kutoa maoni na mrejesho.

#### 6.4.1 Tume ya Taifa ya Mipango

Tume ya Taifa ya Mipango, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango Na. 1 ya mwaka 2023 (iliyorekebishwa mwaka 2024), ni chombo cha juu kabisa cha taifa katika masuala ya upangaji, uratibu na uangalizi wa kimkakati wa maendeleo. Vile vile, Tume ya Taifa Mipango inawajibika kufuatilia utekelezaji kimkakati, kuhakikisha ulinganifu wa sera na kusimamia ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo. Aidha, kama msimamizi mkuu wa Dira ya muda mrefu ya Tanzania, Tume ya Taifa ya Mipango itahakikisha kuwa mipango yote ya kitaifa, ikiwemo Mpango huu, inawiana, inalenga matokeo, na inaendana kikamilifu na Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050.

Hivyo, Tume ya Mipango itatoa mwongozo elekezi wa upangaji wa mipango na bajeti kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Miongozo hii italenga kuoanisha mipango na vipaumbele vya Mpango, kuboresha matumizi ya rasilimali na kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na uwajibikaji unaozingatia

matokeo. Vilevile, itasaidia kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji. Hatua hizi zitawezesha utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya taifa kuratibiwa kwa uwazi na mwelekeo unaozingatia matokeo. Usimamizi wa utekelezaji wa programu za kielelezo na mnyororo wa thamani umeainishwa katika Sura ya Nne.




*Kielelezo 6.1: Muundo wa Uratibu na Utekelezaji*

### 6.4.2 Washirika wa Kimkakati na Taasisi Saidizi

- **Vituo vya Tafiti na Ushauri Sera:** Tume ya Taifa ya Mipango itashirikiana na Taasisi za Tafiti na Ushauri wa Sera za ndani na za kimataifa katika kufanya tafiti za kisera zinazotegemea ushahidi, kufanya uchambuzi wa kitaalamu na tathmini ya athari za changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa Mpango. Ushirikiano huu utafanyika kupitia hati rasmi za makubaliano na utalenga kuimarisha ubunifu wa sera, kujenga uwezo wa kitaasisi, na kuimarisha maamuzi yanayozingatia ushahidi wa takwimu.
- **Sekta Binafsi na Baraza la Taifa la Biashara:** Sekta binafsi inatarajiwa kugharamia, takriban, asilimia 70 ya uwekezaji wa Mpango IV. Sekta hii ni mhimili muhimu wa utekelezaji kupitia ubia na sekta ya umma, ubunifu na uzalishaji wa ajira.
- **Majukwaa ya majadiliano na Baraza la Taifa la Biashara:** Mabaraza ya biashara

ya mikoa na kikanda yatasaidia kuoanisha vipaumbele vya uwekezaji na malengo ya taifa. Aidha, yatabainisha vikwazo vya kisera na kanuni zinazoathiri utekelezaji. Kadhalika, majukawaa haya yataimarisha mazingira ya biashara kwa kuhakikisha yanayotabirika na ni yenye ushindani halali na hivyo kuharakisha mageuzi katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango.

- ❖ **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Asasi za Kiraia na Mashirika ya Kijamii:** Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Asasi za Kiraia na Mashirika ya Kijamii yana mchango mkubwa katika kuchochea maendeleo. Mashirika haya huchangia kujenga uwezo, kufanya tafiti na mapitio na kusaidia utoaji wa huduma muhimu kama afya na elimu. Aidha, taasisi hizi huleta na kusambaza ujuzi wa vitendo, kusaidia kuhamisha teknolojia, kuendeleza na kuboresha huduma za maji, kutoa mafunzo ya kilimo, pamoja na kuendesha shughuli za utetezi na kutekeleza mipango ya maendeleo ya jamii. Mpango unasisitiza ushirikiano wa karibu na uratibu madhubuti kati ya Serikali na mashirika haya ili kuhamasisha rasilimali, kuongeza ufanisi katika utekelezaji na kuhakikisha matumizi yenye tija.
- ❖ **Wizara, Idara na Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa:** Wizara, Idara na Taasisi zina wajibu wa kutekeleza afua za kisekta kwa kuoanisha mipango na bajeti na vipaumbele vya taifa na kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Tume ya Mipango kupitia mifumo ya kidijitali. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaweka vipaumbele ya taifa katika mikakati yao ya uchumi na kuhakikisha ushiriki wa wananchi katika upangaji na ufuatiliaji.
- ❖ **Wizara inayohusika na Mipango na Uwekezaji:** Ofisi hii ina dhamana ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera. Sera hizi zinaongoza programu na miradi ya maendeleo iliyo chini ya Tume ya Taifa ya Mipango, pamoja na kukuza na kuwezesha uwekezaji wa ndani na nje ya nchi. Vilevile, inawajibika kufuatilia utendaji wa idara zilizo nje ya wizara, mashirika ya umma na taasisi mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Msajili wa Hazina na Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania na Maeneo Maalum ya Kiuchumi. Kadhalika, Wizara itaunda na kutekeleza sera zitakazokuza mazingira ya uwekezaji yenye ushindani na yanayotabirika, kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi, na kuhakikisha ulinganifu wa sera katika sekta mbalimbali. Kupitia hatua hizi, Wizara itachochea na kuharakisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii, na hivyo kuchangia kikamilifu katika kufanikisha malengo ya Mpango.
- ❖ **Wizara inayosimamia Fedha:** Wizara itasimamia utekelezaji wa Mpango IV kwa kuhakikisha vipaumbele vya Mpango vinafungamana na Mfumo wa Matumizi ya Serikali wa Muda wa Kati na bajeti za mwaka. Wizara itatenga na kusimamia rasilimali fedha na kuhakikisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango itahakikisha bajeti za sekta zinaendana na malengo ya Mpango IV. Aidha, Wizara itaimarisha usimamizi wa fedha za umma na kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya fedha kwa ufanisi, uwazi na uendelevu. Hii itawezesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati na vipaumbele vingine vya maendeleo kwa wakati.
- ❖ **Ofisi ya Msajili wa Hazina:** Mageuzi yaliyolengwa katika Mpango IV yatabadili Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa Mamlaka ya Kimkakati ya Uwekezaji wa Umma. Ofisi hii itafuatilia Utendaji wa mashirika ya umma, utawala bora na kuendana na vipaumbele vya taifa.
- ❖ **Ofisi ya Taifa ya Takwimu:** Taasisi hii itaongoza na kuratibu Mfumo wa Taifa wa Takwimu. Itakusanya, kuchakata na kusambaza takwimu sahihi, zenye ubora na zinazopatikana kwa wakati kwa ajili ya kupanga, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango. Ofisi ya Taifa ya Takwimu itatekeleza Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Takwimu kwa awamu ili kuimarisha uwezo wa mifumo ya takwimu kubadilishana taarifa, kuimarisha usimamizi wa takwimu na kuunganisha taarifa katika mifumo ya Serikali.

### 6.4.3 Taasisi za Usimamizi na Uwajibishaji

i. **Bunge:** Iitasimamia uwajibikaji wa Serikali, kuimarisha nidhamu ya fedha na kuhakikisha sera pamoja na bajeti zinaoana na vipaumbele vya Mpango. Hatua hizi zitaimarisha uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa Mpango.
ii. **Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi:** Itafanya ukaguzi wa fedha na utendaji mara kwa mara ili kuhakikisha rasilimali zinatumika kwa ufanisi, kupunguza mianya ya upotevu na kuongeza imani ya wananchi.
iii. **Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Sekretarieti ya Maadili:** Taasisi hizi zitasimamia uadilifu, uwazi na maadili ya utumishi wa umma. Pia zitazuia rushwa na kuhakikisha miradi ya kielelezo inatekelezwa kwa uwazi na uadilifu.
iv. **Mamlaka za Udhibiti:** zitabadilisha mtazamo wa udhibiti kwa kujikita zaidi kwenye kuchochea ubunifu, uwekezaji na ushindani ili kuendana na mageuzi yaliyolengwa katika Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI II).
v. **Mahakama (Kitengo cha Biashara):** zitaharakisha utatuzi wa migogoro ili kuongeza imani ya wawekezaji.
vi. **Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora:** itaongoza juhudi za kuhimiza, kulinda na kudumisha haki za binadamu pamoja na misingi ya utawala bora katika jamii.
vii. **Vyombo vya Habari na Vitengo vya Uhusiano wa Umma:** vitakuwa washirika wakuu wa ufuatiliaji wa utekelezaji na uwajibikaji kwa umma. Vyombo hivi vitakusanya takwimu za utekelezaji, kufuatilia maendeleo na kubainisha vikwazo vinavyokwamisha utekelezaji wa Mpango. Pia vitachangia kupunguza usambazaji wa taarifa zisizo sahihi na kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu hatua na matokeo ya Mpango.
viii. **Asasi za Kiraia na Washirika wa Maendeleo:** watashiriki katika utetezi wa sera, kuchochea utekelezaji jumuishi, kutoa misaada ya kitaalamu na kujenga uwezo wa wadau katika kuzingatia vipaumbele vya taifa.
ix. **Wananchi:** watashiriki kikamilifu katika kupanga, kufuatilia na kutoa mrejesho. Ushiriki huu utahakikisha hatua za utekelezaji wa Mpango IV zinazingatia mahitaji ya jamii ili kupata matokeo jumuishi.

## 6.5 Mfumo wa Usimamizi Kufikia Matokeo

Mpango IV ni hatua muhimu ya kwanza katika kutafsiri maono ya muda mrefu yaliyoainishwa katika Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050 kuwa matokeo yanayopimika. Mtazamo wake unaozingatia matokeo unaunganisha mipango, bajeti na utekelezaji ili kuhakikisha kuwa mageuzi, uwekezaji na afua za kitaasisi zinaleta mabadiliko halisi na yanayoonekana katika ushindani wa viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, utawala bora na ustawi wa jamii.

Kwa kijikita katika mfumo thabiti wa ufuatiliaji, tathmini, uwajibikaji na kujifunza katika kufikia matokeo, Mpango unaweka mfumo wianifu wa kufuatilia utekelezaji, kuimarisha uwajibikaji na kuwezesha marekebisho ya utekelezaji kutokana na mafunzo yanayopatikana kwa wakati. Mfumo unahakikisha kila mageuzi yaliyokusudiwa na miradi inatekelezwa kwa ufanisi, utekelezaji unafuatiliwa kwa uwazi na kutathminiwa kwa kuzingatia mchango wake katika kufikia malengo ya vipaumbele vya kitaifa. Vilevile, unajenga utamaduni wa utendaji kwa kuwianisha matumizi ya rasilimali na matokeo yanayopimika kadri ya hatua mahsusi za mageuzi kusudiwa, na upimaji huu utafanyika kwa msaada wa zana za kidijitali na mifumo ya utoaji taarifa kwa wakati halisi.

Kwa kujikita katika Mfumo wa Ufuatiliaji Matokeo, Tathmini, Uwajibikaji na Kujifunza (NF-MEDeP), Mpango unaanzisha utaratibu mmoja na wianifu wa kufuatilia maendeleo, kuimarisha uwajibikaji, na kuwezesha usimamizi unaoendana na mabadiliko. Mfumo huu unahakikisha kuwa kila mageuzi na mradi unatekelezwa kwa ufanisi, unafuatiliwa kwa uwazi, na unatathminiwa kwa kuzingatia mchango wake katika kufikia vipaumbele

vya kitaifa. Aidha, kwa kutumia zana za kidijitali na mifumo ya utoaji taarifa mbashara, Mfumo unakuza utamaduni wa utendaji kwa kuoanisha rasilimali na matokeo yanayopimika kulingana na hatua mahsusi za utekelezaji wa miradi na mageuzi.

Katika utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji Matokeo, Tathmini, Uwajibikaji na Kujifunza, Tume ya Taifa ya Mipango itakuwa mamlaka kuu ya usimamizi wa mfumo huo, ikiwa na jukumu la kuratibu, kuweka viwango na kusimamia utekelezaji katika Wizara, Idara na Taasisi pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Taarifa za utekelezaji zitapitia Dashibodi Jumuishi ya Kidijitali ya e-Mpango IV, itakayounganisha Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Usimamizi wa Miradi na Kanzidata ya Ufuatiliaji ya Serikali za Mitaa katika jukwaa moja litakalokusanya na kuunganisha taarifa za miradi, bajeti na matokeo ya utekelezaji. Aidha, mifumo ya ufuatiliaji inayoshirikisha jamii itawezesha ukusanyaji wa taarifa katika ngazi za chini na kuziwasilisha katika mfumo mkuu wa kitaifa. Hatua hii itahakikisha ujumuishi na kuimarisha uwajibikaji kuanzia ngazi ya jamii hadi taifa.

Usimamizi wa uwajibikaji utaimarishwa na kukaziwa kupitia Mikataba ya Utendaji iliyounganisha utendaji wa taasisi na ufanisi wa matokeo yaliyopangwa. Mapitio ya utendaji ya mwaka yatafanyika kwa kuongozwa na Tume ya Mipango. Aidha, kutakuwepo na kaguzi na tathmini huru zitakazofanywa na taasisi nje ya muundo wa utekelezaji. Mfumo wa Uhakiki wa Ubora wa Takwimu utaongoza uhakiki, ukaguzi na matumizi ya viwango jumuishi. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa takwimu za kuaminika na zinazowiana katika mifumo yote ya Serikali. Jukwaa la Taifa la Mapitio ya Maendeleo litafanyika kila mwaka ili kutathmini maendeleo, kubadilishana uzoefu, kushirikisha na kuhabarisha wananchi. Wakati huo huo, kadi-alama za utekelezaji zitatolewa kila robo mwaka kwa lengo la kuwataarifu wadau kuhusu mwenendo was utekelezaji wa Mpango katika maeneo yao.

Kujifunza na kufanya marekebisho ya utekelezaji kwa kuzingatia mafunzo yanayopatikana ni msingi muhimu wa Mfumo huu. Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitatumika katika mapitio ya sera na bajeti, ili maamuzi yawe na ushahidi, na marekebisho ya utekelezaji yafanyike kwa wakati kulingana na changamoto zinazojitokeza. Kuunganisha mifumo ya kidijitali, kuendesha maabara za utekelezaji za siku 100 na kuanzisha Kitengo Mahsusi cha Kusimamia Utekelezaji kutaharakisha mageuzi na kushughulikia vikwazo mapema. Kupitia mfumo huu, Mpango IV inaasisi utamaduni wa utendaji unaojenga uwajibikaji, uwazi na tija katika Serikali na jamii kwa ujumla. Kwa kuhakikisha kuwa kila afua inapimwa, inafuatiliwa na kuripotiwa kwa umma, Mfumo wa Ufuatiliaji Matokeo, Tathmini, Uwajibikaji na Kujifunza utaimarisha nidhamu ya utekelezaji na kuiwezesha Tanzania kufanikisha mageuzi endelevu na kuongeza ustahimilivu katika safari ya kuelekea Dira 2050.

### 6.5.1 Usimamizi waKufikia Matokeo

Mpango unaasisi utamaduni wa utendaji unaozingatia matokeo ili kuimarisha uwajibikaji na kuoanisha kazi za taasisi na watumishi na matokeo yanayokusudiwa katika ngazi ya taifa. Hivyo, taasisi na watumishi wa umma wataelekeza juhudi zao katika kutekeleza mipango na majukumu yanayoendana na vipaumbele na matokeo yaliyokusudiwa kitaifa. Kufikia hapa, njia kuu za utekelezaji zitakazotumika ni hizi:

i. **Mifumo ya Kupima Matokeo na Mikataba ya Utendaji:**
Malengo ya FYDP IV yatashushwa kwenye mipango kazi ya sekta, taasisi na kila mtumishi. Kutakuwa na mikataba ya utendaji kati ya Tume ya Mipango na Wizara, Idara na Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kusimamia uwajibikaji unaopimika. Tathmini za watumishi zitaunganishwa na matokeo ya kitaifa. Mfumo wa motisha utatumika kuwafidia na kuwatambua watendaji bora kwa wazi na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watendaji ambao hawatafikia viwango vya ufanisi wa utendaji vilivyowekwa.

ii. **Uwajibikaji na Viongozi kuwa Karibu na Wananchi:**
Ili kuimarisha uwajibikaji na ukaribu wa viongozi kwa wananchi, Mpango utaanzisha Kadi Alama za Uwajibikaji wa Uongozi kwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri na Wakuu wa Taasisi za Umma. Matokeo yatakuwa yanachapishwa kila robo mwaka kupitia Dashibodi ya Kidijitali ya Mpango IV ili kuwezesha ufuatiliaji wa wananchi na kuhakikisha uwazi katika utendaji. Aidha, Vikao vya Hadhara vya Uwajibikaji wa Utendaji vitarasimishwa, ambapo viongozi wa kitaifa na wa mikoa watawasilisha taarifa za maendeleo, kupokea maoni ya wananchi na kubainisha mikakati inayokusudiwa katika kutatua changamoto zinakazojitokeza katika utekelezaji. Utaratibu huu ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba viongozi wanapaswa kuwa karibu na wananchi.

iii. **Ufanisi wa Ufuatiliaji Kidijitali:**
Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Usimamizi wa Miradi na Kanzidata ya Ufuatiliaji ya Serikali za Mitaa vitaunganishwa ili kuunda dashibodi jumuishi ya taifa ya kufuatilia matokeo. Dashibodi hiyo itawezesha ufuatiliaji wa moja kwa moja wa utekelezaji wa miradi, ufanisi wa bajeti, na matokeo ya utekelezaji. Uchambuzi wa takwimu utaofanyika kupitia akili unde, utatumika kutambua mapema mwenendo wa utekelezaji, changamoto pamoja na maeneo yanayohitaji hatua za haraka za maboresho. Aidha, viashiria vya rangi vitatumika kufanya uchambuzi wa haraka wa hali ya utekelezaji na maeneo yanayohitaji uamuzi wa haraka.

iv. **Tathmini Huru:**
Kutakuwa na Tathmini huru itakayofanyika katikati na mwisho mwa kipindi Mpango. Vyuo vikuu, taasisi za utafiti na makampuni huru ya kitaalama na watu binafsi wenye uzoefu watashirikishwa katika kufanya tathmini hiyo. Tathmini itapima maendeleo na kutoa mapendekezo, ikiwa ni pamoja na maboresho ya kisera, miundo-taasisi na bajeti ili kuongeza ufanisi.

v. **Maabara za Utekelezaji na Utatuzi wa Changamoto:**
Mpango utaanzisha Kitengo cha Uratibu wa Utekelezaji chini ya Tume ya Mipango/ Ofisi ya Waziri Mkuu ili kufuatilia utekelezaji, hususan, kwa miradi ya kielelezo. Aidha, kitengo hiki kitasaidiwa na maabara za utekelezaji za kisekta zitakazofanya kazi kwa mizunguko ya siku 100 ili kutatua vikwazo vinazokwamisha utekelezaji.

vi. **Ushiriki wa Wananchi:**
Mpango utaimarisha uwazi na uwajibikaji wa kijamii kupitia majukwaa ya kidijitali ya maoni na mrejesho wa wananchi. Majukwaa haya yatawawezesha wananchi kutoa taarifa kuhusu changamoto katika utoaji wa huduma, vihatarishi vya rushwa, ucheleweshaji wa utekelezaji pamoja na kiwango cha kuridhika na huduma zinazotolewa. Maoni na taarifa hizi zitaunganishwa katika mfumo wa uchambuzi wa wakati halisi kupitia Dashibodi ya Kidijitali ya e-FYDP IV. Aidha, matumizi ya kadi za tathmini za wananchi, mifumo ya wazi ya takwimu (open-data portals), na Jukwaa la Kitaifa la Mapitio ya Maendeleo linalofanyika kila mwaka yataimarisha zaidi ushiriki wa wananchi na umma kwa ujumla katika kusimamia utekelezaji wa Mpango.

vii. **Bajeti Kuendana na Utendaji:**
Ugawaji wa rasilimali utaongozwa na matokeo ya utendaji, ambapo taasisi na watendaji wanaofanya vizuri watapewa kipaumbele katika mgao wa rasilimali. Kwa taasisi na watendaji wasiokidhi malengo yaliyowekwa, hatua za maboresho na ufuatiliaji maalum zitachukuliwa ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji. Hatua hii inalenga kuimarisha utamaduni wa utendaji unaozingatia matokeo katika taasisi za umma.

viii. **Mafunzo kwa Masahihisho ya Utekelezaji:**
Mapitio ya kila mwaka ya mafunzo yanayotokana na utekelezaji wa Mpango pamoja na matokeo ya Mfumo wa Ufuatiliaji Matokeo, Tathmini, Uwajibikaji na Kujifunza yatatumika kuongoza marekebisho ya sera na kuimarisha maboresho endelevu katika Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 6.5.2 Utaratibu wa Kutoa Taarifa

Mpango umeweka utaratibu unganishi wa ukusanyaji na utoaji taarifa, unaojumuisha ngazi zote na unaoendeshwa kwa uwazi, ili kupima utendaji, kusaidia maamuzi na kuimarisha uwajibikaji. Kuendana na hili, njia zitakazotumika ni:

**(a) Utaratibu – Maudhui na Muda wa Taarifa:**

i. Taarifa za Utendaji za Robo Mwaka: Taarifa fupi zitatolewa kila robo mwaka kwa mfumo wa alama za rangi ili kuonesha kwa muhtasari matokeo muhimu, matumizi ya rasilimali, vihatarishi vinavyojitokeza, na hatua zinazochukuliwa katika utekelezaji wa Mpango.

ii. Tathmini ya Kina ya Sekta kwa Nusu Mwaka: Kila baada ya miezi sita, ripoti za uchambuzi wa kina zitatolewa kuhusu sekta ili kubainisha changamoto zinazojitokeza na suluhu zilizopendekezwa kupitia Maabara za Utekelezaji.

iii. Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji: Kila mwaka, Mpango utatoa ripoti ya kina inayolinganisha maendeleo ya taifa na malengo ya Mpango IV pamoja na mwelekeo wa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa 2050. Ripoti hii itawasilishwa Serikalini, Bungeni na kwa wananchi.

iv. Mapitio ya Kipindi cha Kati: Mapitio ya utekelezaji wa Mpango yatafanyika katika mwaka wa tatu. Lengo ni kutathmini maendeleo, kupendekeza maboresho, na kufanya marekebisho ya sera au bajeti.

v. Ripoti ya Utendaji ya Miaka Mitano: Mwishoni mwa mwaka wa tano wa Mpango, Ripoti ya Utendaji ya Miaka Mitano itatolewa ili kutathmini mafanikio na kuonesha ulinganifu wake na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa 2050 pamoja na Dira 2050.

**(b) Watoa Taarifa - Majukumu na Uwajibikaji**

i. Tume ya Taifa ya Mipango: Itaongoza mchakato, kusimamia dashibodi ya kidijitali ya Mpango, kuandaa ripoti, kusimamia mikataba ya utendaji, nakutoa motisha au kuonya na kuelekeza hatua zakurekebisha utendaji.

ii. Wizara/Idara/Wakala na Serikali za Mitaa: Zitatuma takwimu za kila mwezi, kuthibitisha taarifa za sekta, na kutekeleza hatua zilizokubaliwa.

iii. Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wataalam Huru: Watafanya ukaguzi na mapitio huru ya utekelezaji wa Mpango.

iv. Bunge na Umma: Watapitia ripoti kupitia vikao vya kamati ya Bunge na majukwaa ya wazi.

**(c) Njia za Kuwasilisha Taarifa**

i. Dashibodi ya Kidijitali ya Mpango IV: Itaunganisha Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za Mipango na Ufuatiliaji na Kanzidata ya Ufuatiliaji ya Serikali za Mitaa, na hutumia takwimu za moja kwa moja na kutoa alama za utekelezaji kutoka kila eneo kijografia. Alama hizi zinazotengenezwa moja kwa moja kwenye mfumo.

ii. Vitengo vya Utekelezaji na na Maabara za Siku 100: Vitafuatilia utekelezaji na kuondoa vikwazo.

iii. Mikataba ya Utendaji: itachapisha malengo ya kila mwaka ya kwa wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

iv. Tovuti ya Umma: Itachapisha ripoti, takwimu na maoni ya wananchi ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji.

### 6.5.3 Mfumo wa Mapitio ya Mpango

Mpango IV utafanyiwa mapitio mara mbili, yaani katikati ya kipindi na tathmini ya mwisho wa kipindi kwa lengo la kujifunza kwa wakati, kuimarisha uwajibikaji, na kurekebisha utekelezaji wa Mpango.

i. **Mapitio ya Muda wa Kati (2028/29):** Mapitio huru yatafanyika ili kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa Mpango IV kwa kuzingatia vipaumbele vyake vikuu. Mapitio haya yatachambua uimara wa uchumi, maendeleo ya viwanda, uundaji wa

ajira, maendeleo ya miundombinu, na utoaji wa huduma za jamii. Aidha, mapitio yataangalia uratibu wa taasisi na iwapo fedha za utekelezaji zinatosha. Vilevile, yataangalia kama hatua za utekelezaji zinawafikia wanawake, vijana na makundi yaliyoachwa nyuma. Pia, yatachambua uwezo wa Mpango kuhimili mitikisiko, kukabili hatari za mabadiliko ya tabianchi na changamoto za ushiriki kikanda. Matokeo ya mapitio haya yataongoza hatua za kurekebisha utekelezaji na kufanya maboresho ya sera ili kuuweka Mpango katika mwelekeo sahihi wa kufikia malengo yake.

ii. **Tathmini ya Mwisho wa Kipindi (2031):** Tathmini ya mwisho itapima mafanikio ya Mpango IV kwa ujumla. Itazingatia ukuaji wa uchumi, maendeleo ya rasilimali watu, kupunguza umaskini, ushindani wa sekta ya viwanda na ustahamilivu wa mazingira. Aidha, itafanya tathmini mageuzi ya taasisi, usimamizi wa fedha za umma na mageuzi ya kidijitali kwa kulinganisha maendeleo ya Tanzania na nchi za kikanda na kimataifa. Matokeo yake yataongoza maandalizi ya Mpango V (2031/32–2035/36).

### 6.6 Mapitio ya Mwaka na Usimamizi Kuendana na Mabadiliko

Mpango IV unasisitiza matumizi ya mfumo unaowezesha kujifunza na kurekebisha utekelezaji ili kuimarisha utekelezaji unaozingatia ushahidi na unaoweza kukabiliana na changamoto zinazojitokeza. Kupitia mapitio ya kila mwaka, Mpango utatathmini maendeleo ya utekelezaji, kubaini mapungufu, na kuchukua hatua za kurekebisha utekelezaji kwa kuzingatia mafunzo yanayopatikana. Mikakati muhimu katika kutekeleza hili, ni pamoja na:

i. **Mfumo wa Usimamizi wa Maarifa:** Mpango utaanzisha jukwaa la kidijitali la pamoja ili kukusanya, kuchambua na kushirikishana uzoefu mzuri, ubunifu na mafunzo yanayotokana na utekelezaji katika sekta na mikoa. Jukwaa hili litatumia uchambuzi wa takwimu wa kina na teknolojia za kisasa kutambua mapema mwenendo na vihatarishi vinavyojitokeza, na hivyo kuwezesha kufanya marekebisho ya sera kwa wakati kwa kuzingatia ushahidi na taarifa/takwimu.

ii. **Mfumo wa Kujifunza ulioungajishwa na Mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini, Uwajibikaji na Ujifunzaji:** Malengo ya ujifunzaji yataingizwa katika taratibu zote za ufuatiliaji na tathmini. Hii itawezesha mikakati na hatua za utekelezaji kurekebishwa kwa haraka kwa kuzingatia taarifa zinazopatikana moja kwa moja na mabadiliko ya mazingira ya utendaji.

iii. **Ushirikishwaji wa Wadau na Majadiliano ya Sera:** Kuwepo kwa majadiliano ya mara kwa mara na wadau, majukwaa ya kujifunza na mijadala ya sera. Kupitia majukwaa haya kutakuwa na kubadilishana uzoefu na kupata suluhu ya pamoja kati ya watendaji wa serikali, asasi za kiraia, wanazuoni na washirika wa maendeleo. Matokeo ya mapitio ya mwaka yataingizwa moja kwa moja kwenye marekebisho ya Mpango. Hii itahakikisha kuwa dira ya muda mrefu inatekelezwa kwa mnyumbuliko, na vipaumbele pamoja na ugawaji wa rasilimali vitarekebishwa kulingana na mabadiliko ya utekelezaji wa Mpango.

iv. **Mfumo wa Mrejesho na Uwazi:** Serikali itaimarisha njia za kusikiliza na kujibu maoni ya wananchi kwa kuzingatia mawasiliano ya pande mbili. Hii litafanyika kwa kutumia mifumo ya kidijitali yaukusanyaji taarifa, dashibodi zitakazotoa taarifa kwa umma kwa uwazi na mapitio ya pamoja na wadau. Mafunzo yatokanayo na mrejesho yataingia moja kwa moja kwenye maamuzi ya utekelezaji. Wananchi, jamii na wafanyabiashara wataweza kutoa taarifa kwa wakati kuhusu changamoto na maendeleo ya utekelezaji. Taarifa hizo zitatumika kuchukua hatua za haraka na kuboresha utekelezaji.

v. **Usimamizi unaobadilika kulingana na wakati:** Taasisi zitatambua vihatarishi mapema, kuandaa njia mbadala na kurekebisha hatua za utekelezaji kwa haraka kulingana na ushahidi na mabadiliko ya mazingira ya utekelezaji.

vi. **Kujenga Uwezo na Ujifunzaji wa Taasisi:** Mafunzo endelevu na ushauri elekezi yataimarisha ujifunzaji wa taasisi na ubunifu.
vii. **Usimamizi Huru:** Bunge, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na taasisi huru za utafiti zitathibitisha taarifa na kuimarisha uwajibikaji.
viii. **Utunzaji wa Kumbukumbu na Usambazaji wa Maarifa:** Mpango utaweka utaratibu wa kuandika na kuhifadhi kumbukumbu za mafunzo yatokanayo na utekelezaji, ubunifu na matokeo ya Mpango. Taarifa hizi zitasambazwa ili zipatikane kwa urahisi na zitumike kuongoza maamuzi, kuboresha usanifu wa programu na kuimarisha mipango ya maendeleo ya taifa itakayofuata.

## 6.7 Mkakati wa Mawasiliano wa Mpango

Mafanikio ya Mpango IV, kwa kiasi kikubwa, yatategemea kuwepo kwa mkakati thabiti wa mawasiliano uliojumuishi na unaozingatia hali halisi ili kuhakikisha kuwa wananchi na wadau katika ngazi zote wanauelewa na kuupokea Mpango huu. Mpango wenye maudhui bora huleta matokeo pale tu malengo, vipaumbele na matokeo yake yanapowasilishwa kwa uwazi na kwa ufanisi. Hivyo, mawasiliano ni nyenzo ya kimkakati inayochangia kuimarisha uwazi, uwajibikaji, upokeaji wa maoni ya wadau, na kujifunza endelevu katika utekelezaji wa Mpango.

### 6.7.1 Lengo na Uratibu wa Mawashiliano

Lengo la mkakati huu ni kujenga uelewa wa kitaifa, umiliki jumuishi wa Mpango, ushiriki wa wadau na uwajibikaji katika kipindi chote cha utekelezaji. Tume ya Mipango itaratibu na kusimamia mawasiliano, kwa ushirikiano wa karibu na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini pamoja na Wizara na Taasisi husika. Maafisa mawasiliano walioteuliwa katika wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa watasimamia utoaji wa taarifa, uwasilishaji wa ripoti na ukusanyaji wa maoni katika ngazi zao.

### 6.7.2 Kanuni za Mawasiliano

Mawasiliano yataongozwa kwa msingi wa uwazi, ujumuishi, kupokea mrejesho na kubalilisha mbinu kadri mazingira yanavyobadilika. Ujumbe utaandaliwa kwa kuzingatia muktadha wa maeneo na sekta, na utasambazwa kwa njia na teknolojia zinazowafikia walengwa. Ili kuongeza upatikanaji wa taarifa, Mpango utaandaa Zana ya Mawasiliano Rafiki kwa Mwananchi zitakayojumuisha maudhui ya Kiswahili, vielelezo na ujumbe mfupi wa simu. Aidha, Mpango utaanzisha mfumo wa kufuatilia na kujibu upotoshaji wa taarifa ili kutambua mapema taarifa zisizo sahihi na kuzirekebisha kwa wakati na hivyo kulinda imani ya umma katika utekelezaji wa Mpango.

### 6.7.3 Hadhira na Mbinu za Kufikisha Ujumbe

Mawasiliano yatalenga makundi muhimu ya wadau kama ifuatavyo:

i. **Umma** – Kuongeza uelewa na umiliki wa Mpango; uratibu utaongozwa na Wizara yenye dhamana ya Habari kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
ii. **Sekta Binafsi** – Kuwasilisha taarifa za sera na fursa za uwekezaji; uratibu utafanywa na taasisi za uwekezaji na maendeleo ya viwanda na biashara.
iii. **Asasi za Kiraia** – Kuimarisha ujumuishi na uwajibikaji; uratibu utaongozwa na wizara zinazohusika na maendeleo ya jamii na serikali za mitaa.
iv. **Washirika wa Maendeleo**–wataoanisha programu na rasilimali zao na vipaumbele vya Mpango na kushiriki katika uratibu wa utekelezaji. Wizara ya Fedha, kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango, itaratibu ushiriki huo ili kuhakikisha ulinganifu wa vipaumbele na ufanisi katika utekelezaji..
v. **Vijana na wanazuoni** – Kukuza utafiti, ubunifu na majadiliano ya sera; uratibu utafanywa kupitia taasisi za elimu, sayansi na teknolojia.

Mawasiliano yatafikisha ujumbe wa Mpango kwa uwazi na kwa wakati, kupitia vyombo vya habari, majarida, majukwaa ya kidijitali, mikutano ya wananchi na majukwaa ya kitaaluma. Njia hizi kuu zitatumika kujenga uelewa wa pamoja, kuhamasisha ushiriki na kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji.

### 6.7.4 Mawasiliano na Mrejesho wakati wa Dharura

Kitengo cha Mawasiliano ya Dharura chini ya Tume ya Taifa ya Mipango kitasimamia utoaji wa taarifa wakati wa mitikisiko ya kiuchumi, mabadiliko makubwa ya sera au wimbi la upotoshaji wa taarifa dhidi ya utelelezaji wa Mpango. Kitengo hiki kitaundwa na wasemaji waliopatiwa mafunzo pamoja na mifumo ya tahadhari za kidijitali. Aidha, maoni ya wadau yataendelea kukusanywa kupitia tafiti, mashauriano ya umma na majukwaa ya wadau ili kuboresha sera na kufikia malengo ya utekelezaji.

### 6.7.5 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mawasiliano

Mpango utapima ubora na ufanisi wa mawasiliano kwa kutumia ukaguzi wa kila mwaka wa mawasiliano, takwimu za majukwaa ya kidijitali, tafiti za maoni ya umma na mpangilio wa maoni ya wadau. Uratibu utafanywa na Kitengo cha Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji cha Tume ya Taifa ya Mipango. Mafunzo yatakayotokana na zoezi hili yatawezesha kufanya maboresho ili kuhakikisha taarifa sahihi zinawafikia walengwa.



## MUHTASARI - SURA YA SITA

MPANGO IV · SURA YA 6

# Usimamizi wa Utekelezaji, Ufuatiliaji na Uwajibikaji

### Mtazamo jumuishi wa Serikali nzima na jamii nzima

Mipango fungamanishi, usimamizi unaozingatia matokeo, ufuatiliaji unaotokana na ushahidi na uwajibikaji unaomweka mwananchi kitovuni — chini ya uratibu wa Tume ya Taifa ya Mipango.

**9**
MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

**17**
TAASISI WASHIRIKA

**e-FYDP IV**
DASHIBODI YA MATOKEO

**Siku 100**
MIZUNGUKO YA MAABARA

MPANGO IV · Sura ya 6 — *Usimamizi wa Utekelezaji, Ufuatiliaji na Uwajibikaji*

KUJENGA JUU YA UZOEFU

## Kutoka Mafunzo hadi Vipaumbele vya Kimkakati

Utekelezaji wa mipango iliyopita ulipata mafanikio makubwa, lakini changamoto kadhaa zilikwamisha utendaji. Vipaumbele vinane sasa vinaegemeza utekelezaji madhubuti zaidi wa Mpango IV.

**⚠ Changamoto Chini ya Mipango Iliyopita**

- Uainishaji na mpangilio dhaifu wa vipaumbele
- Utegemezi mkubwa wa fedha za umma
- Viashiria visivyo bayana vya ufuatiliaji na mrejesho dhaifu
- Kasi ndogo ya ugatuzi kwa halmashauri
- Majukumu ya Mashirika ya Umma yasiyo bayana

**✓ Vipaumbele vya Kimkakati vya Mpango IV**

① Uratibu na usimamizi wa Tume ya Mipango
② Mkakati mseto wa ugharamiaji
③ Usimamizi unaozingatia matokeo na ujifunzaji
④ Ugatuzi wa kasi
⑤ Mifumo ya kisasa ya kidijitali ya ufuatiliaji

MIKAKATI TISA YA UTEKELEZAJI

| | | |
|---|---|---|
| i. Uratibu Madhubuti wa Tume ya Mipango | ii. Uwianishaji wa Mipango na Bajeti | iii. Kuainisha Vipaumbele vya Kimkakati |
| iv. Kuwezesha Sekta Binafsi | v. Ushiriki wa Jamii | vi. Mifumo ya Takwimu na Ufuatiliaji |
| vii. Usimamizi wa Miradi | viii. Mfumo Madhubuti | ix. Usimamizi Unaowezeshwa na Akili Unde |

MPANGO IV · Sura ya 6 — *Mafunzo · Mikakati Tisa*

MFUMO UNAOZINGATIA MATOKEO

## Usimamizi Kufikia Matokeo + Dashibodi ya e-FYDP IV

Mfumo madhubuti wa kufuatilia maendeleo, kuimarisha uwajibikaji na kuwezesha usimamizi unaobadilika — ukiegemea mtiririko wa takwimu kutoka ngazi ya jamii hadi Baraza la Mawaziri.

### Vyanzo vya Takwimu

Mfumo wa Kitaifa wa Miradi
+
**LGMD** · Ufuatiliaji wa Serikali za Mitaa
+
**Ufuatiliaji wa Jamii** · Takwimu za ngazi ya jamii

### e-Delivery

DASHIBODI

Jukwaa moja fungamanishi · takwimu za muda halisi zenye eneo · kadi za matokeo otomatiki

### Matokeo ya Uwajibikaji

**Mikataba ya Matokeo**
**Mapitio ya Mwaka** · ya Tume ya Mipango
**Ukaguzi Huru**
**Jukwaa la Mapitio ya Kitaifa**

MISINGI MINNE

- **Utamaduni wa Utendaji** Matokeo yameunganishwa na hatua
- **Utoaji Taarifa wa Muda Halisi** Kadi za matokeo za robomwaka
- **Usimamizi Unaobadilika** Maabara za Siku 100
- **Ujifunzaji na Kubadilika** Matokeo yanaongoza mapitio



MUHTASARI · KUTEKELEZA MPANGO IV

## Kutoka Mpango hadi Utendaji

Nidhamu ya utekelezaji ni daraja kati ya dira tarajiwa ya Mpango IV na utekelezaji wake unaopimika — ukiegemea uongozi ulioratibiwa, mifumo fungamanishi na uwajibikaji unaomweka mwananchi kitovuni.

1. **Panga** ADP · MTEF · uratibu wa kisekta.
2. **Tekeleza** Wizara · Halmashauri · Mashirika ya Umma · washirika chini ya Tume.
3. **Fuatilia** e-FYDP IV · takwimu za muda halisi zenye eneo.
4. **Pitia** Mapitio ya kati 2028/29 · ya mwisho 2031.
5. **Jifunze** Maabara za siku 100 · usimamizi unaobadilika.

- **ULIORATIBIWA** Tume ya Mipango mamlaka kuu
- **KIDIJITALI** Muda halisi, eneo
- **UWAJIBIKAJI** Mikataba ya utendaji
- **MWANANCHI KITOVUNI** Majukwaa ya mapitio ya mwaka

FUATILIA

DHIBITI

# SURA YA SABA: TATHMINI YA VIHATARISHI NA MBINU ZA KUVIKABILI

TATHMINI

TAMBUA

# SURA YA SABA:

# TATHMINI YA VIHATARISHI NA MBINU ZA KUVIKABILI

## 7.1 Muhtasari

Mpango IV unatekelezwa katika mazingira yanayobadilika kwa kasi kutokana na mageuzi ya kiuchumi maendeleo ya teknolojia ndani ya nchi, kikanda, na mabadiliko na mivutano ya siasa kikanda na kidunia. Ingawa Mpango huu umejengwa juu ya msingi imara wa uthabiti wa vigezo vingi vya uchumi jumla na maendeleo ya taasisi yaliyopatikana kupitia mipango iliyotangulia, mafanikio ya mpango huu yatategemea uratibu madhubuti wa utekelezaji, nidhamu katika usimamizi wa fedha za umma, uthabiti wa sera, na uwepo wa mifumo imara ya utawala.

Sura hii inatoa tathmini ya uwezekano wa vihatarishi katika maeneo mbalimbali ambavyo vinaweza kukwamisha utekelezaji wa Mpango kwa ufanisi. Aidha, inaainisha mikakati ya kudhibiti hatari hizo ili kujenga ustahimilivu, kuongeza uwezo wa taasisi kujifunza kwa haraka namna ya kukabiliana na mabadiliko yanayotokea. Hivyo, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, mkazo wa kipekee umewekwa katika kuimarisha usimamizi wa utekelezaji kuhakikisha kuwa nchi inaendelea kubaki katika mwelekeo thabiti ili kufikia matarajio na malengo ya Dira 2050.

## 7.2 Maeneo yaVihatarishi na Mikakati ya Kuvikabili

Mpango IV utatekelezwa katika mazingira ya kisera na uchumi yanayotoa fursa mpya pamoja na vihatarishi vya aina mbalimbali. Vihatarishi hivi vinajitokeza katika nyanja za taasisi, usimamizi wa fedha za umma, siasa, mazingira na teknolojia, na vinaweza kuathiri kasi na ufanisi wa utekelezaji wa Mpango endapo havitasimamiwa ipasavyo. Kwa hiyo, Mpango umeweka mfumo wa kubaini na kushughulikia vihatarishi hivi mapema ili kuhakikisha utekelezaji unaendelea kwa uthabiti na ufanisi. Hivyo, mfumo umetengenezwa kubaini na kuchukua hatua za kuvithibiti mapema. Mfumo utategemea uchambuzi unaotokana na ushahidi, uratibu na ufuatiliaji endelevu wa kitaasisi utakaofanyika kupitia Dashibodi za kidijitali zitakazoandaliwa mahsusi kwa ajili ya Mpango IV. Mfumo huu unawezesha kutoa tahadhari na hatua za marekebisho ili kuchukuliwa kwa wakati. Jedwali Na. 7.1 linaonesha muhtasari wa maeneo makuu ya vihatarishi na hatua za kukabiliana navyo ili kuongoza utekelezaji wa Mpango katika kipindi cha 2026/27–2030/31.

*Jedwali 7.1: Maeneo na Hatua za Udhibiti wa Vihatarishi (2026/27–2030/31)*

| ***Eneo*** | ***Ufafanuzi wa Kihatarishi*** | ***Mikakati (2026/27–2030/31)*** |
|---|---|---|
| *1. Uwezo mdogo wa utekelezaji na uratibu* | *Upangaji usioratibiwa, kuchelewa kuanza kwa miradi, uratibu dhaifu wa Wizara, Idara na Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na taasisi au mashirika ya umma. Hali hii inaweza kukwamisha utekelezaji wa programu za kimkakati na mageuzi yaliyokusudiwa.* | *Kuanzisha Kitengo cha Utekelezaji cha ngazi ya juu chini ya Tume ya Taifa ya Mipango kwa ajili ya kuratibu programu kielelezo; kuunda vikosi kazi vya pamoja vya wizara kwa miradi mtambuka; kufanya ufuatiliaji kwa wakati kwa kutumia dashibodi ya kidijitali ya Mpango IV; kuandaa mikataba ya kupima utendaji; na kuimarisha uwajibikaji wa taasisi kwa kutumia Mfumo wa Wazi wa Tathmini ya Utendaji Kazi na mikataba ya kupima matokeo.* |
| *2. Hatari katika fedha za umma na ugharamiaji* | *Uchache wa vyanzo mseto vya ugharamiaji kunaweza chelewesha miradi ya kielelezo na ya kijamii.* | *Kupanua vyanzo vya mapato kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, hati fungani za Watanzania waishio ughaibuni, hati fungani za kijani, fedha za kugharamia miradi ya mabadiliko ya tabianchi, pamoja na masoko ya mitaji; kuimarisha uhamasishaji wa mapato ya ndani na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma; na kuweka Mfumo wa Taifa wa Tathmini na Uwekaji Vipaumbele vya Miradi ili kuoanisha miradi na rasilimali zilizopo.* |
| *3. Hatari za kisiasa na kiutawala* | *Kukosekana kwa mwendelezo wa sera, kuongezeka kwa mpasuko wa kisiasa na kukosekana kwa uadilifu ndani ya taasisi vinaweza kudhoofisha imani ya wananchi, kupunguza kasi ya mageuzi na kuchelewesha utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango.* | *Kuweka usimamizi wa pamoja wa Mpango IV kwa kushirikisha vyama vyote vya siasa; kuimarisha uwajibikaji wa taasisi kupitia ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; kufanya mapitio ya uadilifu wa watendaji; kuwasilisha taarifa za utendaji kwa uwazi; na kuendeleza mageuzi ya utawala bora kupitia Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma.* |

| Eneo | Ufafanuzi wa Kihatarishi | Mikakati (2026/27–2030/31) |
|---|---|---|
| 4. Mitikisiko ya uchumi wa nchi na kimataifa | Mitikisiko ya uchumi wa nchi na uchumi wa dunia, ikiwemo mfumuko wa bei, kuyumba kwa thamani ya shilingi, kudorora kwa uchumi wa dunia na mabadiliko makubwa ya bei za bidhaa, inaweza kupunguza mapato, kuongeza gharama za mikopo, kuvuruga minyororo ya usambazaji na kudhoofisha uwekezaji. Athari hizi zinaweza kupunguza wigo wa upatikanaji wa kifedha wa Serikali, kuchelewesha utekelezaji wa programu za kielelezo, kuongeza gharama za utekelezaji na kuchelewesha kufikiwa kwa malengo ya Mpango IV. | Kuimarisha uwezo wa bajeti na akiba ya fedha za kigeni; kupanua mauzo ya nje kwa kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, madini na bidhaa za viwandani; na kuimarisha ufuatiliaji wa uchumi kwa kutumia takwimu na ruwaza za uchambuzi. |
| 5. Mazingira ya biashara | Kuchelewa kutekeleza mageuzi ya uwekezaji, kodi na mifumo ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kunaweza kudhoofisha ushiriki wa sekta binafsi. | Kuharakisha mageuzi ya biashara na kodi kupitia mpango wa kuboresha mazingira ya biashara; kuimarisha mfumo wa kituo kimoja cha huduma za uwekezaji wa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA); na kuhakikisha sera zinatabirika kupitia mazungumzo ya kila robo mwaka kati ya Serikali na sekta binafsi. |
| 6. Utekelezaji wa miradi ya miundombinu | Ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya nishati, usafirishaji na viwanda unaweza kudhoofisha kasi ya mageuzi ya kiuchumi ya Mpango IV. | Kuweka vipaumbele na kutekeleza programu za kielelezo kwa awamu; kuimarisha usimamizi wa mikataba; kufanya upembuzi yakinifu wa miradi; na kuanzisha "Maabara za Utekelezaji za Siku 100" ili kuharakisha utekelezaji wa miradi. |

| ***Eneo*** | ***Ufafanuzi wa Kihatarishi*** | ***Mikakati (2026/27–2030/31)*** |
|---|---|---|
| *7. Mazingira na mabadiliko ya tabianchi* | *Kuongezeka kwa ukame, mafuriko na uharibifu wa mazingira kunaathiri kilimo na miundombinu ya usafirishaji, na hivyo kuathiri kipato cha wananchi. Hatari hizi zinaweza kupunguza uzalishaji, kuzuia upatikanaji wa masoko, kufinya bajeti, na kuongeza matumizi ya dharura pamoja na gharama za urejeshaji wa miundombinu baada ya maafa.* | *Kujenga ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; kuhakikisha uhifadhi wa mazingira katika miradi mikubwa; na kupanua programu za nishati mbadala na uchumi wa mzunguko.* |
| *8. Rasilimali watu na ujuzi* | *Tofauti kati ya mahitaji ya soko na elimu pamoja na ujuzi unaotolewa hupunguza kasi ya maendeleo ya viwanda na ubunifu.* | *Kuhakikisha mitaala na mafunzo inaendana na sekta za kipaumbele za Mpango IV; kupanua elimu ya ufundi stadi na mafunzo ya ujuzi kazini; kuimarisha masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati, pamoja na ujuzi wa kidijitali; na kuimarisha ikolojia ya mifumo ya uvumbuzi.* |
| *9. Mshikamano wa kijamii na mabadiliko ya fikra* | *Kupinga mageuzi, kutojali na kutokuaminiana miongoni mwa makundi ya kijamii kunaweza kudhoofisha umoja wa kitaifa na juhudi za maridhiano.* | *Kutekeleza hatua za kitaifa za kujenga mtazamo chanya na utaratibu wa maridhiano; kuendeleza elimu ya uraia; kuongeza ushiriki wa vijana na majukwaa ya mazungumzo jumuishi; na kuhakikisha rasilimali na huduma za ulinzi wa jamii zinawafikia watu kwa usawa.* |
| *10. Mabadiliko ya kidijitali na hatari za usalama wa mtandao* | *Kuenea kwa mifumo ya kidijitali huongeza hatari ya mashambulizi ya mtandao, uvujaji wa taarifa, kutokuwiana kwa mifumo ya kielektroniki na uelewa mdogo wa matumizi ya teknolojia za kidijitali. Hali hii inaweza kudhoofisha jitihada za serikali mtandao na utekelezaji wa ajenda ya uchumi wa kidijitali.* | *Kuweka Mfumo wa Kitaifa wa Usalama wa Mtandao, Udhibiti na Utawala wa Taarifa; kuimarisha Timu ya Taifa ya Kukabiliana na Dharura za Kompyuta pamoja na usimamizi wa mfumo wa ulinzi wa taarifa; kuendeleza programu za kitaifa za elimu ya kidijitali na matumizi yake; pamoja na kuunganisha na kulinda mifumo ya serikali kupitia usanifu shirikishi na salama wa kidijitali wa Mpango IV.* |

| Eneo | Ufafanuzi wa Kihatarishi | Mikakati (2026/27–2030/31) |
|---|---|---|
| 11. Hatari za kijiografia na kikanda | Kukosekana kwa utulivu katika ukanda, kuvurugika kwa njia za biashara na mabadiliko katika jumuiya ya kimataifa kunaweza kuathiri uwekezaji, usafirishaji na uhakika wa upatikanaji wa rasilimali. | Kuimarisha diplomasia ya kikanda na ushirikiano wa kiusalama kupitia mifumo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Umoja wa Afrika; kusetusha miundombinu ya usafirishaji ikiwemo bandari, kanda za usafiri na mabomba; kuanzisha mifumo ya tahadhari ya mapema dhidi ya mitikisiko katika minyororo ya ugavi na nishati; na kuimarisha mawasiliano ya kimkakati pamoja na uratibu wa sera katika miradi ya kikanda. |
| 12. Hatari za usimamizi wa biashara ya kaboni | Mikataba isiyo na usawa, mifumo dhaifu ya mgawanyo wa manufaa kwa jamii, udhibiti usiotosheleza wa haki za biashara ya kaboni, na changamoto za utawala katika makubaliano vinaweza kupunguza mapato yanayotarajiwa kwa Taifa, kudhoofisha imani ya jamii na kuhatarisha uhifadhi pamoja na ustahimilivu wa mazingira. | Kuweka mfumo imara wa kitaifa wa utawala wa soko la kaboni; kuimarisha uwezo wa kisheria na kitaalamu katika majadiliano, usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba; kuhakikisha kuwepo kwa mifumo ya wazi na inayozingatia haki katika mgawanyo wa manufaa kwa Taifa; na kuanzisha kanzidata kuu ya miradi yote ya kaboni kwa ajili ya usimamizi, ufuatiliaji na uwajibikaji. |
| 13. Hatari za uchumi usio rasmi na msongamano mijini | Kasi ya ukuaji wa miji na kuongezeka kwa shughuli zisizo rasmi husababisha msongamano, migogoro ya matumizi ya ardhi, uharibifu wa mazingira na upotevu wa mapato. Zisipozuiwa, changamoto hizi zinaweza kudhoofisha utekelezaji wa programu kinzani kama Programu Shirikishi ya Uendelezaji Miji Tanzania 2050, kupunguza ubora wa huduma na kushusha ushindani pamoja na ustahimilivu wa kimazingira wa miji. | Kuanzisha maeneo rasmi ya biashara kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo; kuimarisha mipango miji na usimamizi wa matumizi ya ardhi; kujumuisha usimamizi wa sekta isiyo rasmi katika mipango miji na Programu Shirikishi ya Uendelezaji Miji Tanzania 2050; na kuimarisha uratibu kati ya TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, vyama vya wafanyabiashara, na vyombo vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha matumizi yenye utaratibu na haki ya maeneo ya umma. |

| ***Eneo*** | ***Ufafanuzi wa Kihatarishi*** | ***Mikakati (2026/27–2030/31)*** |
|---|---|---|
| *14. Hatari za ukosefu wa ajira kwa vijana, kutoridhika na kuyumba kwa utulivu wa jamii* | *Uwezo mdogo wa uchumi kuzalisha ajira na kasi ndogo ya kuwaingiza wahitimu katika mfumo rasmi wa ajira huongeza hatari ya vijana kukata tamaa, kupunguza imani kwa taasisi za serikali, na kuchochea uhalifu au misukosuko ya kijamii, hasa katika maeneo ya mijini ambako fursa za ajira kwa vijana hazijadhihirika.* | *Kupanua vituo vya ujuzi na ubunifu kwa vijana; kuimarisha mifumo ya uwekezaji inayowawezesha vijana; kuhamasisha ajira zinazowapa kipaumbele vijana wa maeneo husika; kuongeza mafunzo ya ufundi na uanagenzi yanayoendana na mahitaji ya soko, hususan katika stadi za kidijitali, uchumi wa kijani na viwandani; na kuimarisha majukwaa ya mazungumzo na ushiriki wa vijana ili hoja na changamoto zao zipatiwe ufumbuzi kwa njia yenye kujenga.* |

Utekelezaji wa Mpango huu unahitaji usimamizi unaoweza kubaini vihatarishi vya kibajeti, kimazingira, kijamii, kitaasisi na kimasoko vinavyoweza kukwamisha mafanikio ili kuchukua hatua mapema. Vihatarishi hivi vina uhusiano na kama havipatiwi ufumbuzi vinaweza kusababisha changamoto kubwa za utekelezaji wa bajeti na kuchelewesha miradi, kuathiri imani ya wawekezaji binafsi, na kupunguza matokeo ya kimaendeleo. Kwa hiyo, utekelezaji wake unahitaji kuondokana na utendaji wa mazoea wa kusubiri kupata ufumbuzi baada ya madhara kutokea na badala yake kuwa na utaratibu wa kubaini vihatarishi kabla. Kuimarisha utekelezaji wa bajeti, afua za ustahilimivu wa mabadiliko ya tabia nchi na uendeshaji wa biashara ya kaboni, shughuli zisizo rasmi, ukosefu wa ajira kwa vijana, kuimarisha uwezo wa kitaasisi, na kuchochea kasi ya kusetusha muundo wa uchumi ni masuala muhimu katika kuhakikisha ukuaji thabiti na endelevu wa uchumi.

Kwa ujumla usimamizi thabiti wa vihatarishi unategemea uratibu imara maamuzi yanayozingatia ushahidi wa chambuzi makini za kitakwimu na ujifunzaji endelevu kutokana na mrejesho wa taarifa za utekelezaji, ili kuruhusu masahihisho ya kasoro kwa wakati. Uzingatiaji, ustahimilivu, uendelevu, usawa na ubunifu wa utendaji katika mifumo yote ya uongozi na usimamizi utasaidia kuimarisha utekelezaji wa Mpango na kuepuka vihatarishi kuwezesha kufikia matokeo ya kiuchumi na kijamii kuendana na malengo Dira ya 2050.



# MUHTASARI – SURA YA SABA

MPANGO IV · SURA YA 7

## Tathmini ya Vihatarishi na Mbinu za Kuvikabili

### Kutoka kukabili majanga kwa mwitikio hadi utawala wa utabiri

Mtazamo madhubuti na fungamanishi wa usimamizi wa vihatarishi kwa Mpango IV — ukiegemea uchambuzi unaotokana na ushahidi, uratibu kati ya taasisi na ufuatiliaji endelevu kupitia Dashibodi ya e-FYDP IV.

**14** MAENEO MAKUU YA VIHATARISHI

**5** NYANJA ZA VIHATARISHI

**e-FYDP IV** DASHIBODI YA VIHATARISHI

**Siku 100** MIZUNGUKO YA MAABARA

MPANGO IV · Sura ya 7 — *Tathmini ya Vihatarishi na Mbinu za Kuvikabili*

MFUMO WA VIHATARISHI

## Nyanja Tano za Vihatarishi · Misingi Tano

Vihatarishi vinajumuisha nyanja tano za kimkakati, kila moja ikiwa na uwezo wa kuathiri utekelezaji wa Mpango — vikikabiliwa na misingi mitano ya kudumu ya utekelezaji thabiti.

| NYANJA 01 | NYANJA 02 | NYANJA 03 | NYANJA 04 | NYANJA 05 |
|---|---|---|---|---|
| **Kitaasisi** | **Kifedha** | **Kisiasa** | **Kimazingira** | **Kiteknolojia** |
| Uratibu, uadilifu wa utawala katika Wizara, Halmashauri na Mashirika ya Umma. | Ugharamiaji, ukusanyaji wa mapato, uhimilivu wa deni. | Mwendelezo wa sera, kasi ya mageuzi, imani ya wananchi. | Mabadiliko ya tabianchi, msongo wa ikolojia, hatari za majanga. | Usalama wa mtandao, mageuzi ya kidijitali, uadilifu wa takwimu. |

MISINGI MITANO YA MWITIKIO WA KIMKAKATI WA MPANGO IV

| Uratibu | Nidhamu ya Kifedha | Uthabiti wa Sera | Utawala Imara | Uwezo wa Kubadilika |
|---|---|---|---|---|
| Tume ya Mipango mamlaka kuu | Deni endelevu | Mageuzi tabirifu | Mifumo yenye uwazi | Ujifunzaji endelevu |

MPANGO IV · Sura ya 7 — *Mfumo wa Vihatarishi · Nyanja 5 · Misingi 5*

MAENEO MAKUU YA VIHATARISHI

## Maeneo Kumi na Manne ya Vihatarishi na Udhibiti

Vihatarishi vya msingi (1–4) vinaunda wigo wa fedha · vya utekelezaji (5–8) vinaamua kasi na ubora · mtambuka (9–11) vinatokana na nguvu za kijamii na nje · vinavyoibukia (12–14) viko mstari wa mbele.

**01 Kitaasisi**
Kitengo cha Utekelezaji, OPRAS

**02 Kifedha**
Ubia, hati fungani za ughaibuni na kijani

**03 Kisiasa**
Ukaguzi wa CAG, uwazi

**04 Uchumi Jumla**
Akiba ya fedha za kigeni, useto

**05 Kiudhibiti**
Kituo kimoja cha TISEZA, mageuzi

**06 Miundombinu**
Utekelezaji wa awamu, maabara za siku 100

**07 Kimazingira**
Kukabiliana, nishati mbadala

**08 Rasilimali Watu**
Ufundi stadi, STEM, fikra

**09 Mshikamano wa Jamii**
Elimu ya uraia, mazungumzo

**10 Kidijitali na Mtandao**
TZ-CERT, mfumo wa usalama

**11 Kijiografia**
Diplomasia ya EAC/SADC

**12 Soko la Kaboni**
Mfumo wa kitaifa, kanzidata

**13 Sekta Isiyo Rasmi Mijini**
TUGNe, biashara rasmi

**14 Vijana na Utulivu**
Ujuzi, Madirisha ya Uwekezaji

**E-FYDP IV**
**Dashibodi ya Vihatarishi**
Ufuatiliaji wa muda halisi

**SIKU 100**
**Maabara za Utekelezaji**
Mwitikio wa vichocheo

MPANGO IV · Sura ya 7 — *Maeneo Kumi na Manne ya Vihatarishi*

MUHTASARI

## Kutoka Mwitikio hadi Sera ya Utabiri

Vihatarishi vinahusiana na, visipodhibitiwa, vinaweza kuongezeka — vikiathiri wigo wa fedha, kuchelewesha miradi, kudhoofisha imani ya sekta binafsi na kupunguza matokeo ya maendeleo.

**1**
**Bainisha**
Uchambuzi endelevu unaotokana na ushahidi, uchunguzi wa upeo na kanzidata za vihatarishi katika ngazi za kisekta, kimkoa na kielelezo — zinazolisha Dashibodi ya e-FYDP IV.

**2**
**Dhibiti**
Itifaki za vichocheo zinazoanzishwa kupitia mipango ya dharura inayoratibiwa na Tume ya Mipango, akiba ya fedha, mifumo ya tahadhari ya mapema na Maabara za Siku 100.

**3**
**Badilika na Jifunze**
Mrejesho endelevu, tathmini ya kati na urekebishaji wa sera vinahakikisha Mpango unabaki tabirifu na vinalisha usanifu wa Mpango V.

**NIDHAMU YA KIFEDHA**
Akiba na deni endelevu

**TABIANCHI na KABONI**
Utawala imara

**USETO**
Uchumi na njia za biashara

MPANGO IV · Sura ya 7 — *Bainisha · Dhibiti · Badilika na Jifunze*







# VIAMBATISHO







## KIAMBATISHO I: UCHAMBUZI WA KINA WA MBINU NA AFUA KUFIKIA USTAWI

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **3.2 Mwenendo wa Uchumi Jumla** | | | | | | |
| **3.2.1: Uthabiti na Utabirifu wa Mwenendo wa Uchumi Jumla** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuwepo kwa Mazingira Thabiti ya Usimamizi wa Uchumi ili Kuinua Imani ya Wawekezaji na Utabirifu wa Mwenendo wa Uchumi** | | | | | | |
| 1. Ukuaji wa Pato la Taifa wa angalau asilimia 7, ifikapo mwaka 2030. | 1.1 Kutumia vivutio zinavyozingatia ufanisiwa mauzo ya nje, ikiwa ni pamoja na marejesho ya ushuru katika bei ya umeme kwa makampuni ya viwanda yenye uthibitisho wa ongezeko la mauzo ya nje kwa mwaka. | | | | | |
| | 1.2 Kuboresha miundombinu ya masoko (biashara, malipo, maghala) ifikapo Juni 2027. | | | | | |
| 2. Mfumuko wa bei uliodumishwa ndani ya wigo uliopangwa wa kati ya asilimia 3 – 5 kwa mwaka | 2.1 Kuimarishwa kwa mfumo wa sera ya fedha, kwa kuimarisha utaratibu wa kuweka shabaha za mfumuko wa bei kila mwaka. | | | | | |
| | 2.2 Kuimarishwa kwa upatikanaji wa chakula na uthabiti wa bei, kwa kuongeza uzalishaji wa ndani, kuboresha mnyororo wa thamani wa kilimo, na kuanzisha utaratibu wa vocha za kidijitali za pembejeo kwa wakulima wadogo kila mwaka. | | | | | |
| | 2.3 Kuanzishwa mfumo wa kidijitali wa kitaifa wa ufuatiliaji wa bei za bidhaa muhimu kwa wakati na kongeza uwazi wa soko kila mwaka. | | | | | |
| | 2.4 Kudumisha utaratibu wa utunzaji wa akiba ya chakula na petroli toshelevu ya mahitaji kitaifa kwa angalau miezi sita, ili kupunguza athari za kuyumba kwa bei za nje, kila mwaka . | | | | | |
| | 2.5 Kuimarishwa kwa uwianifu wa sera za fedha na bajeti ili kuhakikisha uwiano na utulivu wa kiuchumi kila mwaka. | | | | | |
| **3.2.2 Kuimarisha Ustahimilivu wa Kifedha** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kusimikwa kwa mfumo endelevu wa kifedha kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, kupunguza vihatarishi vya deni la Taifa sanjari na kuhakikisha uendelevu wa matumizi thabiti, uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa uendelezaji wa miundombinu na upatikanaji wa huduma za jamii, na kudumisha nidhamu ya matumizi** | | | | | | |
| 1. Makusanyo ya mapato ya ndani kuongezeka kutoka asilimia 14.9 hadi 20 ya | 1.1 Kuimarishwa ukusanyaji wa kodi kidijitali kupitia mifumo ya kiotomatiki, utoaji wa ankara ya kielektroniki na matumizi ya mifumo ya kikodi ya kisasa kwa zaidi ya | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| Pato la Taifa. | asilimia 80 ya walipa kodi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Makusanyo ya kodi kuongezeka hadi 18% ya Pato la Taifa, ifikapo mwaka 2031. | 2.1 Kuimarishwa taratibu kuwezesha urasimishaji wa shughuli za sekta isiyo rasmi, kwa kurahisisha michakato ya kukidhi masharti ya sheria za kodi na vivutio kufikia 2031. | | | | | |
| | 2.2 Kutekeleza maboresho ya mfumo wa kodi jumuishi unaozingatia uwezo na utaratibu wa misamaha ya kodi ili kuongeza usawa na ufanisi wa makusanyo, ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3 Kuimarishwa na kuingiwa kwa makubaliano ya kimataifa na washirika wa biashara itakayowezesha mabadilishano ya taarifa za kodi, ili kuzuia vitendo haramu vya kifedha na ukwepaji wa kodi kwenye mifumo ya biashara za kidijitali, kila mwaka. | | | | | |
| 3. Makusanyo ya maduhuli/yasiyo ya kodi kuongezeka kufikia asilimia 5 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2030. | 3.1 Kufanya mapitio na marekebisho ya kina ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kusasishwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kufanyia mapitio ya kina mifumo ya kisheria na taratibu na kuchagiza mabadiliko ya mifumo kuwa ya kidijitali na otomatiki ili kuongeza ufanisi ifikapo mwaka 2028. | | | | | |
| | ii. Kuharakishwa upangaji wa matumizi ya ardhi, upimaji, na urasimishaji kwa kutumia teknolojia za kisasa, kama vile, picha za satelaiti na ndege zisizo na rubani, ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 4. Deni la Serikali kudhibitiwa kubaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 50 – 55 wa vigezo vya DSA ifikapo Juni 2031. | 4.1 Kuimarishwa kwa mikakati ya usimamizi wa deni la serikali kwa kipindi chote, kwa kujielekeza kukopa katika vyanzo vya masharti nafuu na kupunguza mikopo aghali ya kibiashara muda wote kufikia 2031. | | | | | |
| | 4.2 Kufuatilia kwa karibu faida kwenye uwekezaji uliofanyika kwa fedha za mkopo, kuhakikisha faida inayopatikana na matokeo yake ni makubwa, kwamba matumizi ya mikopo yanakuwa mazuri, kila mwaka | | | | | |
| 5. Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti inadhibitiwa chini ya | 5.1 Kutekelezwa kwa mfumo wa bajeti ya matokeo kiutendaji na mapitio kila mwaka | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| asilimia 3 ya Pato la Taifa kila mwaka. | ya uhalali wa matumizi katika wizara zote za Serikali kufikia 2031. | | | | | |
| | 5.2 Kuimarisha mifumo ya matumizi ya fedha za umma muda wote ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kufikia 2031. | | | | | |
| | 5.3 Kuimarisha mipango na usimamizi wa mifuko ya kitaifa ya dharura na maafa, ili kushughulikia kikamilifu matumizi ya mifuko hiyo yanayozidi kuongezeka kila mwaka. | | | | | |
| 6. Bajeti ya maendeleo kudhibitiwa ndani ya wigo wa kati ya asilimia 31 - 35 ya matumizi yote ya Serikali kila mwaka | 6.1 Kuimarishwa kwa ufanisi wa manunuzi na utoaji huduma za umma, kwa kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali na kuweka ukomo bayana wa matumizi, kila mwaka | | | | | |
| | 6.2 Kuongeza matumzi ya mifumo ya kidijitali ili kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma na matumizi ya fedha, kufikia 2031. | | | | | |
| **3.2.3 Ustahimilivu na Usetushaji wa Sekta ya Nje** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kupunguza hatari za kiuchumi kwa kusetusha bidhaa za kuuza nje, kupunguza utegemezi uagizaji wa mahitaji kutoka nje na kuimarisha mizania ya malipo, na kuimarisha utabilifu wa biashara na ustahimilivu wa kiuchumi.** | | | | | | |
| 1. Mchango wa mauzo ya bidhaa za viwandani nje kuongezeka kutoka asilimia 12 hadi 30 ya jumla ya mauzo yote ya bidhaa nje ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kutekeleza sera za viwanda zinazohamasisha kuongeza thamani katika kilimo, madini na uzalishaji viwandani, ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuanzishwa kwa mfumo rasmi wa motisha kwa wauzaji wa bidhaa za viwandani nje (kama vile kupunguza kodi na upatikanaji wa mikopo nafuu) ili kusaidia ongezeko la bidhaa za viwandani na zilizosindikwa zinazouzwa nje, ifikapo mwaka 2027. | | | | | |
| | ii. Kuwezesha ongezeko la uzalishaji viwandani na usindikaji wa mazao ghafi ya kilimo, madini na maliasili zingine za uzalishaji viwandani ili kupunguza mauzo ghafi nje ya bidhaa ghafi, ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | iii. Kuongeza uwekezaji katika miundombinu wezeshi kibiashara, ikiwa ni pamoja na kusasisha miundombinu na huduma za bandari, ujenzi wa vituo mahsusi vya usafirishaji na uchukuzi, na kuongeza ufanisi wa huduma za forodha, ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Kiwango cha utegemezi uagizaji wa mahitaji kutoka nje kupungua kwa asilimia 15 kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuongeza uzalishaji wa malighafi na mahitaji mengine muhimu, sanjari na kupanua uwezo wa ndani wa uzalishaji viwandani wa bidhaa muhimu, kama vile, dawa za tiba ya binadamu, pembejeo na vifaa vya kilimo na nguo na mavazi ndani ya nchi, kupitia mkakati mahsusi wa ujenzi wa uchumi wa viwanda na ongezeko la uwekezaji katika | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ujenzi wa uwezo wa utafiti na maendeleo ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 3. Kuhakikisha nakisi ya urari wa malipo haizidi asilimia 6 ya Pato la Taifa, kufikia 2030 | 3.1 Kuimarisha ujenzi wa akiba ya fedha za kigeni usiopungua uwezo wa uagizaji wa mahitaji kutoka nje wa aghalabu miezi minne na nusu kila mwaka. | | | | | |
| | 3.2 Kuhamasisha ongezeko la mauzo ya huduma nje, ikiwa ni pamoja na utalii na huduma za kifedha kwa usetushaji wa vyanzo vya mapato ya fedha za kigeni kila mwaka. | | | | | |
| | 3.3 Kuimarisha ushirikiano wa biashara kikanda kuweza kupunguza utegemezi wa nchi zilizoendelea kwa masoko ya mauzo, sanjari na kujenga uhimilivu wa misukosuko ya kiuchumi ya nje, kila mwaka. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **3.3 Mabadiliko Muhimu katika Sekta Mageuzi** | | | | | | |
| **3.3.1 Sekta ya Kilimo** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kilimo -mazao cha kibiashara na stahimilivu kinachochochea ukuaji wa uchumi na msingi wa maisha ya wakazi wa vijijini kwa mazingira imara ya uchumi, na ukuzaji wa imani ya wawekezaji na mazingira tabirifu kibiashara.** | | | | | | |
| **1.1.1 Kilimo-Mazao cha Kibiashara** | | | | | | |
| 1. Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 7 bora, Kusini mwa Jangwa la Sahara zenye kilimo - mazao chenye uwezo wa ushindani, ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuimarisha mmalaka za uthibiti na urekebu kuweza kuimarisha faida na ushindani katika uendeshaji wa kilimo- mazao kibiashara, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuwajengea uwezo wadhibiti, ili kusimamia viwango vya kimataifa na kupunguza kukataliwa kwa bidhaa nje, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuwianisha viwango vya kitaifa na vya kiitifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika vya mazao, kufikia mwaka 2026. | | | | | |
| | iii. Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji kidijitali vyanzo vya mazao makuu ya biashara ya nje , kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | 1.2 Kufanya mapitio, kurekebisha na kutunga sheria mpya, ili kufuta urasimu na kurahisisha ufanyaji biashara kufikia Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | i. Kufanya tathmini ya kina ya sheria za biashara za kilimo na uwekezaji, kufikia Juni 2028. | | | | | |
| | ii. Kuwianisha sheria za kitaifa na za Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika , Shirika la Biashara Duniani na mifumo ya kilimo bora kinachozingatia hali ya hewa kufikia mwaka 2028. | | | | | |
| | 1.3 Kuongeza fursa za upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu, riba nafuu na masharti nafuu kwa wakulima wa kibiashara na wadogo kutoka vyanzo vya ndani na nje kila mwaka. | | | | | |
| | i. Kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ili kupunguza hatari za uwekezaji wa muda mrefu (kila mwaka). | | | | | |
| | ii. Kuhamasisha ushirikiano na taasisi za fedha za ndani katika mifumo ya fedha mseto ili kuongeza mikopo kwa wafanyabiashara na wakulima wa kati na wadogo, kila mwaka. | | | | | |
| | iii. Kuanzisha Mfuko wa Kitaifa wa Dhamana ya Mikopo (kwa wakulima vijana na wanawake). | | | | | |
| | 1.4 Kupanua ufikiaji wa ruzuku za serikali na zana za kupunguza vihatarishi ili kuimarisha usalama wa kifedha na msaada kwa wakulima, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kutekeleza programu za ruzuku zinazolenga pembejeo muhimu za kilimo, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa taarifa za soko, ili kutoa bei za wakati halisi mwelekeo wa mahitaji, na taarifa zingine za soko, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | iii. Kuanzisha zana za kupunguza vihatarishi katika uwekaji wa mitambo ya kilimo , ikijumuisha motisha za kodi kwa ununuzi wa zana na vituo vya kukodisha zana za kilimo, kufikia 2028. | | | | | |
| | iv. Kuongeza zana za kupunguza vihatarishi vya kifedha katika sekta ya kilimo, ikijumuisha bidhaa ya bima ya kilimo mipango ya dhamana ya mikopo na kuimarisha mifumo ya ufadhili wa ushirika kufikia mwaka 2029. | | | | | |
| | v. Kuhamasisha kilimo cha vitalu kwa kuandaa wakulima katika vikundi vilivyoboreshwa, ili kuongeza tija, kupunguza gharama za pembejeo, na kurahisisha upatikanaji wa masoko, kila mwaka. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 1.5 Kuanzisha mfumo wa kilimo cha mkataba kuwawezesha wakulima mmoja mmoja, kwa kuwapa masoko ya uhakika, upatikanaji wa pembejeo bora, msaada wa kitaalamu na bei thabiti, kwa kuwa na mapatano ya moja kwa moja na wanunuzi, kila mwaka. | | | | | |
| | i. Kutengeneza mfumo sanifu wa kilimo cha mikataba, ili kuwalinda wote, mkulima na mnunuzi, kila mwaka. | | | | | |
| | 1.6 Kuimarisha mnyororo wa thamani wa nguo, kwa kuzalisha pamba, kuichambua, kutengeneza nyuzi, kufuma vitambaa, kuvitia rangi, na kutengeneza bidhaa ya nguo iliyokamilika, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha kituo cha kisasa cha uzalishaji wa nguo kinachotumia nishati bora, kwa kuboresha viwanda muhimu vya kuchambua pamba, kuendeleza kongani mbili au zaidi za viwanda vya nguo vilivyounganishwa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Tanzania kuwa kitovu kikuu cha usafirishaji wa nguo kwa kuongeza motisha maalum za uwekezaji, na kuzindua kampeni ya kimataifa ya "Made in Tanzania" kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | iii. Kuendeleza nguvukazi watu stadi katika sekta ya nguo kwa kuanzisha programu za mafunzo katika usanifu na utengenezaji wa nguo, na kuwawezesha vijana na wanawake 5,000 kufanya kazi viwandani kufikia mwaka 2029. | | | | | |
| | 1.7 Kufufua viwanda vya kilimo vilivyobinafsishwa na kushindwa kuzalisha , hususan viwanda vya nguo vya zamani (kama Urafiki, Mwatex, n.k.) ili kuongeza thamani, kufikia Juni 2030 . | | | | | |
| | i. Kutengeneza mkakati wa kitaifa wa kufufua viwanda vya nguo, kuweka kipaumbele katika kusasisha viwanda muhimu, kufikia Juni 2027 | | | | | |
| | ii. Kuhamasisha uwekezaji binafsi kwa ajili ya ufufuaji wa uchumi kupitia kifurushi maalum cha motisha na ushirikiano wa kimkakati kufikia Juni 2028. | | | | | |
| | iii. Kuhakikisha ushindani kwa kuelekeza matumizi ya pamba ya ndani na kuanzisha vituo vya teknolojia na mafunzo ya ujuzi kufikia Juni 2029. | | | | | |
| 2. Angalau asilimia 45 ya wakulima wapate pembejeo za kilimo bora za kilimo kufikia Juni 2030 | 2.1 Kuimarisha mifumo ya upandaji wa mbegu bora zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi na viunganishi vya utafiti na ugani kufikia 2029. | | | | | |
| | 2.2 Kuimarisha udhibiti wa ubora wa pembejeo na mifumo ya uthibiti, ili kuepuka bidhaa bandia kufikia 2029. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| 3. Ardhi ya kilimo inayoendelezwa kikamilifu kwa kutumia mbinu bora za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kuongezeka hadi kufikia asilimia 40 kufikia Juni 2031 | 3.1 Kuasili mbinu za kilimo zinazohimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa maeneo yote ya kilimo kufikia 2029. | | | | | |
| | 3.2 Kutekeleza kilimo cha teknolojia sahihi ya umwagiliaji kwa matone na majukwaa jumuishi kufikia 2029. | | | | | |
| 4. Uwiano wa maafisa ugani na wataalamu wa kilimo kuboreshwa kutoka 1:20,000 ya sasa hadi 1:10,000 ifikapo Juni 2031 | 4.1 Kuimarisha upatikanaji endelevu wa huduma za ugani kwa mifumo ya teknolojia ya kidijitali kufikia Juni 203. | | | | | |
| | 4.2 Kujenga mfumo thabiti wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za ugani, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 2:** | **Sekta ndogo za mifugo na uvuvi imara na zenye tija kibiashara zinazoendesha ukuaji wa uchumi na maisha ya vijijini** | | | | | |
| **1.1.2. Mifugo na Uvuvi** | | | | | | |
| 1. Angalau asilimia 50 ya mazao ya mifugo kufanyiwa ongezeko la thamani la kiwango cha pili kufikia mwaka 2031 | 1.1 Kuimarisha uwezo wa kitaifa wa uzalishaji na jenetiki katika mifugo na ukulima wa ukuzaji viumbe maji kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2 Kuendeleza kanda maalum za viwanda vya mifugo na uvuvi pamoja na miundombinu ya kusindika kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 2. Uzalishaji wa ndani wa pembejeo za mifugo na uvuvi pamoja na vyakula vya wanyama kuongezeka kwa angalau asilimia 50 kufikia mwaka 2031 | 2.1 Kuongeza uzalishaji wa pembejeo muhimu na aina ya mifugo iliyoboreshwa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 3. Kufikia angalau asilimia 50 ya usambazaji wa soko la kikanda na kimataifa kwa samaki na mazao ya ufugaji wa viumbe maji kufikia mwaka 2031. | 3.1 Kujenga na kusasisha bandari za uvuvi, maeneo ya kutua samaki, na vifaa vya kuhifadhia baridi kando ya pwani ya Bahari ya Hindi, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 3.2 Kuanzisha mifumo ya viwanda vya samaki na ufugaji wa viumbe maji iliyoidhinishwa na tayari kwa mauzo ya nje, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 3:** | **Uzalishaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo ulioboreshwa unaohusisha kuunganisha kilimo cha msingi na usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao, kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna, na kuinua kipato cha wakulima wadogo** | | | | | |
| **1.1.3 Mnyororo wa thamani wa chakula na usio wa chakula** | | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| 1. Kuanzisha Kanda za Ukuaji wa Kilimo (katika kanda mbili zitakazoanzishwa kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha maeneo yaliyounganishwa kwa ajili ya minyororo ya thamani wa chakula, vinywaji/bidhaa zisizo za chakula, na mifugo , kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2 Kuanzisha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika usindikaji wa mazao ya kilimo na mnyororo wa thamani uliounganishwa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 4: Kuimarisha ugharamiaji bunifu katika kilimo, kukuza uendelevu wa kifedha na kuharakisha maendeleo ya kilimo kwa kuboresha upatikanaji wa mikopo nafuu, kuhimiza uwekezaji, na minyororo ya thamani inayostahimili mabadiliko** | | | | | | |
| **1.1.4. Ugharamiaji Bunifu wa Kilimo** | | | | | | |
| 1. Idadi ya wajasiriamali wa kilimo wanaopata huduma rasmi za kifedha kuongezeka kutoka asilimia 15 hadi asilimia 30 kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuunda vyombo na mifumo ya kifedha bunifu (masoko ya mitaji, benki za maendeleo, na fedha mchanganyiko kwa uwekezaji wa muda mrefu katika kilimo, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2 Kutekeleza mifumo ya kupunguza vihatarishi ili kuvutia uwekezaji binafsi katika maeneo yasiyofikiwa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 2. Angalau asilimia 5ya bajeti ya serikali kuelekezwa kwenye maendeleo ya kilimo, kila mwaka | 2.1 Kuweka utaratibu rasmi wa bajeti ya kimkakati ya kilimo na kuunganisha kilimo katika mipango ya maendeleo ya kiuchumi ya ndani kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 5: Kuhakikisha usambazaji endelevu wa mazao na huduma za misitu kwa kudumisha eneo la kutosha la misitu chini ya usimamizi bora, na kuboreshwa kwa afya ya mfumo wa ikolojia, kuimarisha maisha ya vijijini, na usambazaji wa uhakika wa malighafi kwa viwanda vya misitu** | | | | | | |
| **1.1.5 Misitu ya Biashara** | | | | | | |
| 1. Kupanua eneo la kibiashara kwa mashamba ya miti na vitalu vya jamii kufikia angalau hekta milioni 1.5 kufikia Juni 2031 | 1.1 Kupanua na kuimarisha mashamba ya miti ya kibiashara na vitalu vya miti vya jamii, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2 Kuunganisha mbinu za usimamizi wa misitu zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi kufikia June 2031. | | | | | |
| | 1.3 Kuanzisha ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya upanuzi wa misitu, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 6: Kuhamasisha ukuzaji wa viwanda na biashara endelevu ya misitu ili kuongeza thamani ya mazao ya misitu, kusetusha bidhaa, kuongeza mapato ya nje, na kuzalisha bidhaa ndani mbadala wa zinazoagizwa toka nje** | | | | | | |
| 2. Kuongeza mchango wa sekta ya misitu katika Pato la Taifa kufikia angalau asilimia 3- 4 na kuongeza mauzo ya | 2.1 Kuendeleza viwanda vya misitu kupitia kuongeza thamani, kusetusha , na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika usindikaji, kufikia Juni 2031 . | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| nje ya mazao ya misitu kufikia dola za Marekani milioni 150-200 kufikia Juni 2031 | 2.2 Kuhamasisha ugharamiaji wa mabadiliko ya tabia nchi na uwekezaji unaolinda mazingira ili kusaidia viwanda endelevu, kila mwaka. | | | | | |
| | 2.3 Kuimarisha sera wezeshi kwa viwanda vinavyotegemea misitu, ikijumuisha kuzingatia taratibu, uratibu, na ushirikishwaji, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **1.1.6 Ufugaji Nyuki** | | | | | | |
| **Lengo 1:** | **Kusasisha na kuendesha kibiashara sekta ya ufugaji nyuki kwa maisha endelevu, uzalishaji viwandani unaolinda mazingira, na ushindani wa mauzo ya nje kupitia uendelezaji wa ujuzi, matumizi ya teknolojia, na ujumuishaji wa soko** | | | | | |
| 1. Kuongeza uzalishaji wa asali na mazao ya nyuki nchini kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuimarisha mifumo ya udhibiti, mazingira halisi, na viwango vya uzalishaji ili kutoa mazingira bora ya uzalishaji na uuzaji wa mazao ya nyuki kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | 1.2 Kusasisha mbinu za kuboresha ufugaji nyuki na kuwezesha mabadiliko kutoka mizinga ya asili kwenda kwenye vifaa vya kisasa vilivyosanifiwa kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3 Kutekeleza mpango mkubwa wa kitaifa wa kupanda na kuhifadhi mimea rafiki kwa nyuki, ili kuingunisha na mabadiliko tabia nchi kitaifa, na juhudi za upandaji miti, kufikia 2029. | | | | | |
| | 1.4 Kuandaa na kusambaza mtaala wa kisasa wa ufugaji nyuki, kwa kukizingatia maeneo mbalimbali ya hali ya hewa na kuunganishwa na huduma za ugani za kilimo nchini kufikia 2028. | | | | | |
| 2. Kuongeza uwekezaji unaoongozwa na sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa na kuanzisha angalau biashara 5 kubwa za ufugaji nyuki zinazolenga masoko ya nje, kufikia Juni 2031. | 2.1 Kutengeneza chapa bora ya kitaifa yenye mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji (na kusaidia wazalishaji kupata vyeti vya kimataifa kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2 Kuwezesha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na mipango ya wazalishaji wa nje katika ufugaji nyuki inayounganisha kampuni kubwa za kibiashara na wafugaji wadogo, ili kuhakikisha usambazaji thabiti wa malighafi bora, na kuhakikishia upatikanaji wa masoko ya uhakika na msaada wa kitaalamu kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3 Kujenga na kuendeleza mradi wa mipango ya biashara iliyoidhinishwa, inayoweza kuwekezwa kwa ufugaji nyuki mkubwa, viwanda vya kusindika, na uzalishaji bidhaa, ili | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.4 Kuanzisha na kusimamia viwango vya kitaifa vya ubora kwa mazao yote ya nyuki, ili kuhakikisha usalama, kuongeza upatikanaji wa masoko ya kimataifa, na kujenga imani kwa walaji, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **3.3.2 Sekta ya Viwanda na Uzalishaji** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuibadilisha Tanzania kuwa kituo kikuu cha utengenezaji bidhaa katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa kufikia kiwango cha wastani cha ukuaji wa viwanda cha asilimia 9 kwa mwaka, na mchango endelevu wa sekta hiyo wa asilimia 15 katika Pato la Taifa** | | | | | | |
| 1. Tanzania kuwa kati ya nchi 50 bora, kulingana na taarifa za Benki ya Dunia juu ya fahirisi ya urahisi wa kufanya biashara kufikia Juni 2031 | 1.1 Kutengeneza sera ya taifa ya viwanda na mkakati wa viwanda 2050, inayohamasisha usetushaji na uongezaji thamani kwenye uzalishaji viwandani, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kutengeneza kanuni ya kisheria na kitaasisi itakayowezesha utekelezaji wa dhati wa sera mpya ya viwanda kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kutekeleza sera mpya ya viwanda itakayojikita katika kipaumbele cha kuimarisha mnyororo wa thaman kama mwelekeo wa taifa katika kukuza maendeleo ya viwanda kufikia mwaka 2029. | | | | | |
| | 1.2 Kutengeneza sera lengwa ya bajeti na maboresho ya kanuni za kisheria ili kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja toka nje na uingizaji wa teknolojia na maendeleo ya viwanda vya ndani, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuanzisha mfumo shindani wa kifedha unaotoa motisha maalum kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni unaolenga uhawilishaji wa teknolojia na maendeleo ya viwanda vya ndani kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mfumo wa kisheria uliorahisishwa, ikijumuisha kituo jumuishi cha uwekezaji (ili kurahisisha uwekezaji, kupunguza muda na gharama za kuanzisha, na uendeshaji biashara za viwanda, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3 Kuandaa mkakati wenye mfumo wa kukuza uwekezaji binafsi katika viwanda vya kuongeza thamani madini (viwanda vya uchakataji wa madini), uhamasishaji uwekezaji binafsi katika viwanda vinavyotumia madini, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuandaa mwongozo wa uwekezaji katika uzalishaji viwandani wa bidhaa za madini, ikijumuisha motisha za kisera, matumizi ya rasilimali za ndani, na fursa za utafiti na maendeleo ili kuonyesha ahadi ya thamani kwa wawekezaji, kufikia mwaka 2028. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ii. Kuzindua kampeni ya kimataifa ya uwekezaji iliyolengwa, kwa kuzingatia mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa taarifa za viwanda kufikia mwaka 2027, kwa kutumia fursa za maonyesho ya biashara yaliyoboreshwa na ya kimataifa ili kuvutia wawekezaji mahiri katika maeneo yaliyobainishwa ya mnyororo wa thamani wa madini, kufikia Juni 2031.<br>iii. Kuanzisha dawati la kuwezesha uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa za madini, ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | | | | | | |
| | 1.4 Kuweka kipaumbele cha kununua bidhaa zilizozalishwa za ndani kwa manunuzi ya serikali na kuhakikisha kuwa wazalishaji wa ndani wanapata mahitaji thabiti kwa bidhaa zao muda wote, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kutekeleza sera ya kuweka kima cha chini matumizi ya rasilimali za ndani (local content) katika ununuzi wa umma, kwa kutatenga angalau asilimia 30 ya matumizi ya bidhaa zinazostahiki kwa wazalishaji wananchi waliothibitishwa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mpango wa kuwaendeleza wasambazaji kuwathibitisha na kuinua MSMEs kufikia viwango vya manunuzi serikalini, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 2. Mauzo nje kwa bidhaa ambazo zimezalishwa SEZ na EPZ kupanuka na kufikia 22 % ya jumla yote ya mauzo nje ya sekta, ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuanzisha maeneo ya ubunifu na teknolojia ili kuvutia uwekezaji wa utafiti na maendeleo, na utengenezaji wa bidhaa katika maeneo ya mauzo ya nje, hususan kwa viwanda vinavyotumia teknolojia ya hali ya juu, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuanzisha mfumo maalum wa kanuni za kisheria kwa maeneo maalum ya ubunifu na teknolojia utakaotoa taratibu zilizorahisishwa na motisha zilizolengwa, kufikia Juni 2028. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha maeneo maalum ya ubunifu na teknolojia ikilenga sekta zenye fursa kubwa zaidi, kufikia Juni 2030. | | | | | |
| | iii. Kuboresha na kupanua Kanda Maalum za Kiuchumi (SEZ) na Kanda za Uzalishaji mauzo Nje (EPZ) zilizopo kwa kuweka miundombinu ya kisasa, kuweka kipaumbele katika kuendeleza kando ya reli ya kisasa (SGR), kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2 Kuanzisha uzalishaji viwandani kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu katika Kanda Maalum za Uchumi (SEZ) na Maeneo Maalumu ya Uwekekezaji (EPZ) kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kanda Maalum za Uchumi (SEZs) Maeneo Maalumu ya Uwekekezaji (EPZs) kuwekewa | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | miundombinu ya msingi ya kidijitali (kama vile intaneti yenye kasi ya juu na mifumo ya IoT(na kusaidia kupitishwa kwa teknolojia ya Viwanda 4.0 kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kujenga mazingira mazuri ya kuanzishwa viwanda vya madawa ya binadamu vyenye ithibati, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | iii. kuanzisha motisha maalum kwa uzalishaji viwandani kwa kutumia mbinu za kisasa na kuanzisha vituo vya mafunzo ya ujuzi ndani ya kanda maalum za uchumi (SEZs) ili kuchapusha uwekezaji wa sekta binafsi, kufikiaJuni 2031. | | | | | |
| | 2.3 Kuanzisha asilimia 50 ya Maeneo Maalumu ya Uwekekezaji/ Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZs) zenye vivutio maalum na masharti, kwa ajili ya uzalishaji wa viwanda vinavyotumia teknolojia ya juu na viwanda vya utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na madini, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuanzisha teknolojia maalum ya hali ya juu (na kuimarisha mfumo wa vivutio vya kuongeza thamani madini katika Kanda Maalum za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZs), kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuteua na kuboresha asilimia 50 ya Kanda zote Maalum za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZs) kama Kanda za Viwanda vya Hali ya Juu kufikia Juni 2031, na kuziwezesha kwa mahitaji muhimu ya miundombinu ya kidijitali na nguvukazi watu yenye ujuzi, ili kuendesha viwanda vinavyotumia teknolojia ya hali ya juu, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.4 Kuhamasisha utengenezaji bidhaa zenye ufanisi wa nishati na rafiki wa mazingira, kulingana na viwango vya kimataifa na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kila mwaka. | | | | | |
| | i. Kutekeleza mfumo wa ukaguzi wa lazima wa nishati na mazingira kwa viwanda vyote vya uzalishaji na kuanza ukaguzi wa kufuata viwango kwa taasisi za ithibati, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuvutia Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni wa Kijani (Green FDI) kwa kutoa vivutio maalum kwa kampuni za kigeni zinazohamisha teknolojia ya hali ya juu ya viwanda safi na kuokoa nishati kwenda kwa viwanda vya ndani kila mwaka. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | iii. Kuanzisha Mpango wa Motisha kwa uzalishaji unaojali mazingira unaotoa msamaha wa kodi kwa kampuni zinazopata vyeti vya kimataifa vya mazingira, kama vile ISO 14001, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.5 Kuhakikisha wazalishaji wa ndani wanakidhi viwango vya ubora vya kimataifa ili kushindana katika masoko ya kimataifa, hasa kwa bidhaa za thamani ya juu, kila mwaka. | | | | | |
| | i. Kuanzisha mtandao wa kitaifa wa vituo vya ukaguzi na uthibitisho vya kimataifa ifikapo mwaka 2028, ili kuwezesha wazalishaji wa ndani kuthibitisha bidhaa zenye thamani kubwa kufikia viwango vya kimataifa ndani ya nchi, kila mwaka. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha na kuvutia hisa za uzalishaji wa bidhaa za thamani ya juu (elektroniki, dawa, mitambo na vipuri vya magari), kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 3. Kuongezeka kielezo (index) cha mauzo nje ya bidhaa mseto kutoka 0.4 hadi 0.52, ifikapo Juni 2031 | 3.1. Kuanzisha na kuongeza wigo wa uzalishaji wa ndani wa chuma, magari, makaa ya mawe na uzalishaji wa bidhaa za kielektroniki hadi kufikia angalau asilimia 40 na asilimia 1 katika mnyororo wa mauzo ya nje wa kikanda na kimataifa, mtawalia,kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuendeleza maeneo maalumu ya kongani za viwanda kwa ajili ya chuma, magari na vifaa vya elektroniki, kuweka wazalishaji viwandani pamoja na vituo vya mafunzo ya ujuzi na vitovu vya mnyororo wa ugavi, kufikia mwaka 2029. | | | | | |
| | ii. Kuandaa vivutio vya kimkakati katika maeneo ya uzalishaji, ikijumuisha punguzo maalum la kodi, ruzuku ya viwango vya umeme, na vipaumbele kwenye kugharamia miradi itakayozingatia matumizi ya rasilimali za ndani na malengo ya mauzo ya nje, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 3.2 Kutengeneza na kuuza nje bidhaa za viwandani za teknolojia ya juu katika masoko ya kimataifa (Ulaya,Asia, Amerika), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha mtandao wa kitaifa wa vituo maalumu vya ubunifu vinavyolenga akili unde na uzalishaji wa viwango vya juu, ifikapo mwaka 2028, unaofikia viwango vya kimataifa ili kuwa injini ya ukuzaji wa bidhaa za teknolojia ya juu, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha kituo au mpango maalum wa kuwezesha utafiti ifikapo mwaka 2029, pamoja na kutoa ruzuku kwa tafiti na maendeleo na unafuu wa biashara, na motisha maalum kwa wawekezaji, kufikia Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | iii. Kuandaa Mpango wa Kimataifa wa uuzaji wa teknolojia ya juu nje, ifikapo mwaka 2030, ili kusajili bidhaa za teknolojia ya juu kwa viwango vya kimataifa na kuzindua kampeni maalum za kupenya kwenye masoko ya Ulaya, Asia na Amerika kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 2: Kuimarisha matumizi ya rasilimali za ndani na kukuza uchumi jumuishi unaolenga biashara ndogondogo ndogo na za kati (MSMEs)** | | | | | | |
| 4.Kuongeza thamani katika uzalishaji kwa MSMEs kutoka asilimia 12 hadi 22, kufikia Juni 2031 | 4. Kufanya mapitio na kuanzisha mifumo ya udhibiti kwa ajili ya kurasimisha MSMEs, kuongeza upatikanaji wa fedha, kujenga uwezo na upatikanaji wa masoko ya kikanda na kimataifa, maeneo ya biashara yaliyorasimishwa, na miundombinu wezeshi ya kutosha, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 4.2 Kuandaa mpango wa kusaidia biashara ndogondogo na za kati (SMEs) za uzalishaji viwandani kupitia ruzuku/mikopo, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuanzisha kituo maalum cha kuwezesha biashara ndogondogo na za kati (MSMEs) za uzalishaji, kutoa ruzuku na mikopo nafuu kwa ajili ya kuboresha teknolojia na kupanua biashara kufikia 2028. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mpango maalumu wa dhamana ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, ili kuwezesha benki za kibiashara kutoa mikopo kwa ajili ya kuinua teknolojia na kupanua biashara, kufikia mwaka 2028. | | | | | |
| | iii. Kujumuisha huduma maalum za kusaidia biashara, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha na msaada wa kitaalam ndani ya maeneo yote maalum ya viwanda vidogo na vya Kati (MSME parks) yanayofanya kazi, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 4.3 Kuwezesha ushirikishwaji wa viwanda vidogovidogo vya ndani katika mnyororo wa ugavi wa viwanda kwa kusaidia viwango vya ubora, kujenga uwezo na upatikanaji wa masoko, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha mpango wa kitaifa wa udhibiti wa ubora wa viwanda vidogovidogo (MSMEs) ili kusaidia kufikia viwango vya kimataifa vya uzalishaji, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuzindua mpango wa kitaifa wa kuunganisha minyororo ya ugavi, utakasaidia kuoainisha biashara na makubaliano ya kandarasi kati ya biashara ndogondogo na za kati zilizothibitishwa na wazalishaji wakubwa, kufikia Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | iii. Kuandaa mtaala wa mafunzo ya utayari wa kushiriki katika mnyororo wa usambazaji na kuupeleka kwa viwanda vidogo, kwa ajili ya taratibu za manunuzi, usafiri na usafirishaji, na kuongeza uzalishaji, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **3.3.3 Sekta ya Ujenzi** | | | | | | |
| **Lengo 1:** | **Kuanzishwa kwa sekta ya ujenzi endelevu, jumuishi, shindani kikanda, inayoongozwa na wakandarasi wa ndani, inayochochea ukuaji wa uchumi, kuendeleza viwanda, kuboresha viwango vya maisha, na kuhimiza maendeleo ya teknolojia na ubunifu** | | | | | |
| 1. Kuongezeka kwa thamani ya hisa za wakandarasi wa ndani wanaoshiriki katika miradi mikubwa ya ujenzi hadi asilimia 50, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuandaa mwongozo wa ugharamiaji kwa wakandarasi utakaoimarisha upatikanaji wa fedha kwa kampuni za ndani na kuimarisha ushiriki wao katika miradi mikubwa, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | 1.2 Kutekeleza mwongozo wa uwezeshaji wakandarasi wa ndani, utakaoelekeza malipo kufanyika ndani ya siku 30, kutoa kipaumbele kwa rasilimali za ndani katika manunuzi, na utekelezaji wa vifungu vya ubia vyenye viashiria (KPIs) vya uhawilishaji teknolojia kwa miradi yote ya umma, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | 1.3 Kuboresha mfumo wa kupanga, kusimamia, kufuatilia na kutathmini ushiriki wa wananchi katika manunuzi ya umma, kufikia Juni 2028 | | | | | |
| | 1.4 Kutekeleza motisha ya kuhamasisha matumizi ya vifaa vya kisasa vya ujenzi na teknolojia, kila mwaka. | | | | | |
| | 1.5 Kuzindua programu ya utayari wa kimataifa, ili kuzitunukia kampuni za ndani vyeti vya viwango vya kimataifa (kama ISO), kuongeza uaminifu na ushindani kwa miradi ya kikanda, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 2. Angalau asilimia 50 ya miradi mikubwa ya ujenzi kutekelezwa kupitia fedha zilizopatikana toka vyanzo mbadala, ikiwa ni pamoja na Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuimarisha na kutafsiri miongozo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa kuwezesha kuandaliwa kwa miradi inayotekelezeka na inayoweza kupata ufadhili, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | 2.2 Kutoa motisha za kifedha na zisizo za kifedha kwa wawekezaji binafsi, kila mwaka . | | | | | |
| | 2.3 Kuimarisha ujuzi wa watumishi wa umma katika kusimamia mikataba ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kila mwaka. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 2.4 Kuhamasisha matumizi ya zana za soko la mitaji (kama hisa na dhamana ) ili kufadhili miradi mikubwa ya ujenzi, kila mwaka. | | | | | |
| | 2.5 Kuimarisha utekelezaji wa mifumo iliyopo ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuandaa orodha ya miradi inayoweza kupata ufadhili, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | 2.6. Kuimarisha na kuendesha utendaji wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika Wizara, Idara, Wakala (MDAs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ili kuvutia wawekezaji, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| 3. Angalau asilimia 50 ya kampuni za ujenzi za ndani zitatumia teknolojia za kisasa na mbinu endelevu katika miradi mikubwa ya ujenzi, kufikia Juni 2031 | 3.1 Kuimarisha matumizi ya tafiti na teknolojia mpya katika sekta ya ujenzi, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuhamasisha ushirikiano kati ya makampuni ya ndani na ya kimataifa katika miradi mikubwa ya ujenzi, kila mwaka, | | | | | |
| | ii. Kufadhili vituo vya ubunifu kwa ajili ya Utafiti na Maendeleo ya malighafi za ndani, kila mwaka. | | | | | |
| | iii. Kuimarisha uhawilishaji na usambazaji wa teknolojia za kisasa na utumiaji wa matokeo ya utafiti katika sekta ya ujenzi, kila mwaka. | | | | | |
| | iv. Kuanzisha mfumo endelevu wa ufadhili wa utafiti, ubunifu, na uboreshaji wa mifumo ya ujenzi, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | v. Kuimarisha TanT, kufikia Juni 2027. | | | | | |
| 4. 80% ya kazi za kitaalamu na zenye ujuzi zinazopatikana katika sekta ya ujenzi kufanywa na wakandarasi wa ndani, ifikapo Juni 2031 | 4.1 Kuimarisha matumizi ya tafiti na teknolojia mpya katika sekta ya ujenzi kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuanzisha chuo cha kisasa cha mafunzo ya ujenzi ifikapo 2028 ili kuweka viwango na kutoa mafunzo katika nyenzo za kidijitali (utakaozingatia ujenzi rafiki wa mazingira, na usimamizi wa miradi ya kimataifa . | | | | | |
| | ii. Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Mafunzo kwa Vitendo katika sekta ya ujenzi utakaowataka washiriki wa miradi mikubwa kushirikiana na taasisi za mafunzo ya ufundi, ili kuwezesha mafundi kupata ithibati ya ujuzi wa ujenzi wa kisasa, kila mwaka. | | | | | |
| | iii. Kuboresha programu za mafunzo kulingana na mahitaji ya sekta ya ujenzi, kila mwaka. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | iv. Kuimarisha vyanzo vya upatikanaji wa fedha kusaidia mafunzo katika sekta ya ujenzi, kila mwaka. | | | | | |
| | v. Kuimarisha programu maalum za mafunzo ya ufundi, kwa mafundi wananchi wa ujenzi, kila mwaka. | | | | | |
| 5. kujumuisha asilimia 30 ya miradi ya ujenzi katika miundo yenye ufanisi wa matumizi ya nishati na mbinu za ujenzi rafiki kwa mazingira na ujenzi stahimilivu, kufikia Juni 2031 | 5.1 Kuhamasisha ujenzi wa kijani na stahimilivu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kutekeleza Kanuni za Majengo ya Kijani (na Sera ya Manunuzi ya Umma ya Kijani kwa miradi yote mipya ya serikali, kufikia Juni 2029. | | | | | |
| | ii. Kuunda kanuni stahimilivu za miundombinu za kiufundi, viwango, na miongozo kufikia Juni 2027. | | | | | |
| | iii. Kuzindua kifurushi cha motisha ya teknolojia zinazotunza mazingira kinachotoa punguzo la kodi na ruzuku kwa miradi inayotumia nishati mbadala, ujenzi wa awali na ubunifu wa vifaa vya ndani, kufikia Juni 2028. | | | | | |
| | iv. Kuanzisha na kuthibitisha wataalamu wa ujenzi katika usanifu, usimamizi na uthibitishaji wa majengo rafiki wa mazingira kupitia programu ya kitaifa ya kuongeza kasi ya ujuzi, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | v. Kutekeleza programu za mafunzo ya kujenga uwezo wa wadau wa ujenzi kuhusu ujenzi wa kijani na kanuni za miundombinu stahimilivu, kila mwaka. | | | | | |
| | vi. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi unaotunza mazingira na ustahimilivu kila mwaka. | | | | | |
| **3.3.4 Sekta ya Madini na Uchimbaji Mawe** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuendeleza sekta shindani na jumuishi ya madini inayotegemea viwanda na inayotumia kwa ufanisi rasilimali za madini huku ikidumisha na kuimarisha minyororo ya thamani ya ndani** | | | | | | |
| 1. Asilimia 25 ya wataalamu wa wa sekta ya madini kupewa mafunzo ya umahiri, unaoendana na uongezaji thamani wa madini na uchumi wa viwanda, kufikia Juni 2031. | 1.1 Kuhakikisha upatikanaji wa nguvu kazi yenye ujuzi ili kusaidia uongezaji thamani wa madini na uzalishaji viwandani kufikia mwaka 2028. | | | | | |
| | 1.2 Kupanua na kuboresha taasisi za mafunzo ya kiufundi (mfano, Moshi) ili kukuza nguvu kazi ya uchimbaji wa madini na uongezaji thamani, kufikia mwaka 2029. | | | | | |
| | 1.3 Kuanzisha vyuo vya mafunzo ya madini na ufundi vilivyofungamanishwa, kwa lengo la kujenga mfumo endelevu wa kuzalisha | | | | | |

| Shabaha | Afua | | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | | wataalamu wenye ujuzi na utayari wa kufanya kazi katika sekta ya madini, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4 | Kuboresha kanuni za maudhui ya ndani katika sekta ya madini kwa kuanzisha mfumo wa dhamana ya madini kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 2. Kuongeza kiwango cha ufanisi wa usimamizi wa sekta ya madini kutoka kiwango cha sasa hadi angalau asilimia 65, kufikia Juni 2031 | 2.1 | Kuandaa na kutekeleza Mfumo Jumuishi wa Serikali-Mtandao (E-Government) katika sekta ya madini, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2 | Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa vyombo muhimu vya udhibiti (Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia, nk) ili kuimarisha utawala, ukaguzi, uzingatiaji wa sheria, na usimamizi wa sera , kufikia mwaka 2028. | | | | | |
| | 2.3 | Kuunganisha usimamizi wa sekta ya madini na viwango vya kimataifa, ikiwa ni pamoja na Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Uchimbaji (EITI), kupitia utoaji wa taarifa za lazima za kila robo mwaka, kufikia 2029. | | | | | |
| | 2.4 | Kuanzisha utaratibu wa pamoja wa uratibu kati ya Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), na vyombo vya udhibiti wa madini, ili kurahisisha utoaji wa maamuzi, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.5 | Kuanzisha mfumo thabiti wa kitaifa wa uwekezaji katika sekta ya madini ili kurahisisha usaidizi wa wawekezaji, kupunguza ucheleweshaji kutokana na urasimu, na mfumo wa utatuzi wa malalamiko kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.6 | Kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Ubora kwa ajili ya uchumi wa madini, uchimbaji wa kidijitali, ukadiriaji wa akiba, mbinu za kijiolojia na utii wa viwango vya mazingira, kijamii, na utawala bora kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.7 | Kuweka Mikataba ya Maendeleo ya Jamii (CDAs) katika mfumo wa taasisisi na kusimamia kikamilifu uzingatiaji wa athari za kijamii na kimazingira kupitia mfumo thabiti wa kitaifa , kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 3. Kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini kutoka asilimia 19 hadi asilimia 40, kufikia Juni 2031 | 3.1 | Kuimarisha mifumo ya kisheria na udhibiti ili kuhakikisha ushiriki sawa wa wanawake katika mnyororo mzima wa thamani wa madini, kufikia 2028. | | | | | |
| | 3.2 | Kuanzisha programu na viwango vya kitaifa vya kuongeza uwezo wa kiufundi, usimamizi, na ujasiriamali kwa wanawake, kufikia Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 3.3 Kuanzisha mifumo maalum ya gharamiaji na motisha, ikijumuisha upatikanaji wa mitaji, teknolojia, na vifaa, ili kuendeleza biashara za madini zinazoongozwa na wanawake, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 4. Kudumisha ushiriki wa vijana katika uchimbaji madini kwa angalau asilimia 10ya jumla ya nguvu kazi katika sekta ya madini, kufikia Juni 2031 | 4.1 Kuanzisha programu na motisha za kitaifa zinazohamasisha ubunifu wa kiteknolojia kwa vijana na masuala ya kidijitali katika sekta ya madini, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 4.2 Kuandaa mfumo wa kitaifa wa kukuza umahiri kwa ajili ya kuboresha taaluma endelevu ya vijana wanaofanya kazi katika sekta ya madini, unaoendana na mabadiliko ya kidijitali ya sekta, na teknolojia mpya, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 4.3 Kuanzisha mifumo ya udhibiti na ununuzi inayoweka masharti au kutoa motisha kwa zabuni ndogo (subcontracts) kwa biashara zinazomilikiwa na vijana katika nyanja mbalimbali za mnyororo wa thamani wa madini, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 2: Kuongezeka kwa uanzishaji wa miradi mipya ya uchimbaji wa madini na kufunguliwa kwa miradi ya utafiti na uchimbaji wa madini iliyokwama, kuweka mazingira wezeshi na urahisishaji wa taratibu kwa wawekezaji wa ndani na wa nje (FDI) katika utafiti na maendeleo ya madini** | | | | | | |
| 1. Kuongezeka kwa huduma za ramani za kijiolojia, kijiofizikia na kijiokemia zinaofanywa na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na kufikia asilimia 100%, kufikia mwaka 2030 | 1.1 Kufanya mapitio ya kina na uwiano wa mifumo ya kisheria na udhibiti wa madini, viwanda, fedha, na kodi ni hatua muhimu ya kuongeza kasi ya utafiti, kukuza maendeleo ya madini, na kusaidia viwanda vya madini, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | 1.2 Kuimarisha uwezo wa kitaalamu na mifumo ya kusimamia uendeshaji wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania , ili kuinua utoaji wa huduma na ufanisi wa kitaasisi, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3 Kuipatia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) teknolojia za kisasa za uchoraji ramani za kijiolojia, kijiokifizikia na kijiokemia pamoja na maabara ya uchambuzi, ili kuwezesha upatikanaji kamili wa taarifa za kitaifa, kufikia mwaka 2028. | | | | | |
| 2. Kulibadilisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kuwa kampuni ya umma ya kibiashara inayokidhi | 2.1 Kuifanya STAMICO kuwa kampuni ya kimkakati ya kitaifa, ya uchimbaji madini ambayo serikali ina umiliki mkubwa wa hisa ifikapo mwaka 2028, ili kuweka msingi wa mageuzi ya utawala bora wa kampuni. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| viwango vya kimataifa vya utawala bora na uendeshaji wa mashirika, ikiwa na angalau cheti cha ubora cha ISO 9001 na taarifa za fedha zilizokaguliwa kila mwaka, kufikia Juni 2031 | 2.2. Kuiwezesha kifedha (mtaji) na kutoa mafunzo kwa watendaji na wafanyakazi, katika nyanja za ujuzi wa kiufundi, kifedha na kiutendaji, sambamba na kuboresha miundombinu na mifumo, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3 Kuiwezesha STAMICO kupata haki za uchimbaji wa madini na kuongeza shughuli za utafiti na uchimbaji kutoka migodi 3 hadi 7 na kuwa na ukuaji unaopimika na uzingatiaji wa viwango vya kimataifa, kufikia Juni 2031 . | | | | | |
| 3. Kulibadilisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kuwa kampuni ya umma ya kibiashara inayokidhi viwango vya kimataifa vya utawala bora na uendeshaji wa mashirika, ikiwa na angalau cheti cha ubora cha ISO 9001 na taarifa za fedha zilizokaguliwa kila mwaka, kufikia Juni 2031 | 3.1 Kuanzisha mfumo wa kimuundo wa kurahisisha uwekezaji kwa ajili ya kuvutia na kurasimisha ubia kati ya Serikali na wawekezaji binafsi katika miradi yenye tija ya uchimbaji wa madini, kufikia mwaka 2028. | | | | | |
| | 3.2 Kuandaa mipango ya pamoja ya maendeleo ya miundombinu (barabara, umeme, maji, na vituo vya usafirishaji) kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi ili kufungua fursa za madini na kuongeza tija ya sekta, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 3.3 Kuanzisha vivutio vya kisheria, kiudhibiti na kifedha ili kuongeza mvuto wa ubia na uwekezaji wa muda mrefu katika sekta ya madini, kufikia 2027. | | | | | |
| 4. Kuidhinisha, kupata uwekezaji, na kuanza utekelezaji wa angalau miradi 5 ya kimkakati ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini, kufikia Juni 2031. | 4.1 Kutoa kipaumbele na kuharakisha utoaji wa leseni na vibali vya udhibiti kwa miradi ya madini ya kimkakati na maeneo muhimu, ili kuvutia wawekezaji wa kimkakati, kufikia mwaka 2028. | | | | | |
| | 4.2 Kuanzisha ubia wa kimkakati kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya miradi mikubwa, kama Liganga–Mchuchuma (chuma/chuma cha pua), viwanda vya uchenjejuaji nikeli, cobalt na shaba, pamoja na mitambo ya usindikaji wa madini adimu (Rare-Earth Minerals – REE), ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha, uhawilishaji wa teknolojia, na utayari wa uendeshaji, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 4.3 Kuendeleza miundombinu jumuishi na maeneo ya viwanda (nishati, usafiri, maji, na vifaa/logistics) ili kusaidia utekelezaji wa miradi ya madini na uchenjuaji wa madini, kufikia Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **Lengo 3: Kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa kigeni (FDI) katika usindikaji, uchenjuaji, usafishaji, na utengenezaji wa madini ya viwandani na madini muhimu, kwa lengo la kuchochea maendeleo ya viwanda na ukuaji wa uchumi** | | | | | | |
| 1. kuongezeka kwa mchango wa madini ya viwandani na madini muhimu (critical base metals) kupitia uongezaji thamani na uzalishaji wa viwandani hadi angalau asilimia 3 kufikia Juni 2031 . | 1.1 Kuanzishwa kwa viwanda vya kauri, mbolea, vioo, saruji, kemikali, dawa, na betri vinavyotumia madini ya viwandani na madini mkakati kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2 Kuanzisha Kituo cha Teknolojia ya Madini Muhimu (Critical Minerals Technology Hub), kwa ajili ya kuuendeleza viwanda vya ndani vya betri za lithiamu-iron na teknolojia nyingine rafiki kwa mazingira (mradi wa kimkakati), kufikia June 2031. | | | | | |
| | 1.3 Kuwekeza katika uanzishaji wa mitambo ya kuyeyusha na kusafisha metali za msingi (kama vile shaba, zinki, bati, alumini, risasi, nikeli n.k.), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **Lengo 4: Kuongezeka kwa uzalishaji na mauzo nje ya dhahabu na vito, na hivyo kuinua nafasi ya Tanzania katika soko ya kimataifa la madini** | | | | | | |
| 1. Kuongeza uzalishaji na uuzaji nje wa dhahabu na vito kwa angalau asilimia 30 ifikapo Juni 2031, ikichangiwa na ushirikishwaji wa migodi mikubwa na ya wachimbaji wadogo kurasimisha sekta, na kupatikana kwa fedha na teknolojia, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuandaa na kutekeleza mfumo wa kitaifa wa urasimishaji wa wachimbaji wadogo na wa kati (ASM), utakaowawezesha kuwaunganisha katika minyororo rasmi ya ugavi, uzingatiaji wa sheria, na masoko ya kuuza nje, ifikapo mwaka 2027. | | | | | |
| | 1.2 Kuanzisha ubia wa kimkakati kati ya Serikali na sekta binafsi (PPPs) pamoja na ubia wa pamoja (joint ventures) ili kuvutia uwekezaji katika utafiti na uchimbaji mkubwa wa dhahabu na vito, ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kuanzisha jukwaa la kitaifa la ugharamiaji na na teknolojia kwa wachimbaji wadogo (ASM) na wachimbaji wakubwa, likijumuisha mikopo yenye riba nafuu, ukodishaji wa vifaa, na msaada wa kitaalamu ili kuboresha ufanisi wa uzalishaji na ubora wa bidhaa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4 Kuimarisha mifumo ya takwimu za kijiolojia na kijiospatia ili kuongoza utafutaji wenye tija na kuwezesha uchimbaji endelevu wa dhahabu na vito kufikia , Juni 2031. | | | | | |
| 2. Kuongeza uzalishaji na mauzo ya nje ya dhahabu na | 2.1 Kuongeza uwezo wa uchimbaji mkubwa wa dhahabu kwa kutoa leseni kimkakati | | | | | |

| Shabaha | Afua | | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| vito kwa angalau asilimia 30 kupitia ushirikishwaji | | kwa migodi mipya na kuboresha utendaji wa migodi iliyopo ili kufikia angalau migodi 7 inayofanya kazi kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2 | Kuimarisha hifadhi ya dhahabu ya taifa na usimamizi wa mikuo ya dhahabu kwa kuongeza akiba ya dhahabu ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutoka tani 3.7 hadi tani 20, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3 | Kuanzisha uongezaji thamani wa dhahabu nchini kupitia usafishaji uthibitisho wa ubora na uwekaji chapa ili kuongeza mapato ya kigeni na ushindani wa kimataifa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.4 | Kuwezesha ubia wa kimkakati wa sekta ya umma na sekta binafsi ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje katika uchimbaji, uchakataji, na miundombinu ya madini ya kusafirisha nje, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 5: Kuifanya Tanzania kuwa Kitovu cha Vito Afrika** | | | | | | | |
| 1. Kuwa na sekta ya vito yenye ushindani na inayodhibitiwa vizuri, ikiwa na angalau asilimia 40 ya biashara iliyorasimishwa, na miundombinu ya kuongeza thamani kuanzishwa, kufikia Juni 2031 | 1.1 | Kuandaa mfumo wezeshi wa kiudhibiti na kifedha kwa ajili ya utafiti, uchimbaji, uongezaji thamani, na biashara ya vito unaovutia wawekezaji wa ndani na wa kigeni, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | 1.2 | Kuimarisha programu za ukuzaji uwezo ili kujenga ujuzi, maarifa, na rasilimali kwa watu binafsi na taasisi katika sekta ndogo ya vito, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3 | Kuanzisha miundombinu ya kimkakati ya uongezaji thamani wa vito, ikiwemo ukataji, ung'arishaji, utengenezaji wa mapambo ya vito, na vituo vya viwanda vya kukata na kusafisha vito, ikijumuisha kituo kikuu jijini Dodoma, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4 | Kuanzisha Eneo Maalum la Kiuchumi kwa ajili ya biashara na maonesho ya kimataifa ya vito jijini Dodoma kama mradi wa mfano kufikia , Juni 2031. | | | | | |
| 2. Vituo vikuu vya biashara ya vito vilivyothibitishwa nchini Tanzania vinavyolenga kuunganishwa rasmi na masoko ya kimataifa kuanzishwa, ifikapo Juni 2031 | 2.1 | Kujenga muunganiko na soko la kimataifa kupitia ubia na mashirika ya vito vya kimataifa, taasisi za biashara, na vituo vya elimu, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2 | Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa utengenezaji wa chapa ya vito vya thamani, kwa lengo la | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | kuvitambulisha vito vya Tanzania (ikiwemo tanzanite) katika masoko ya kimataifa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3 Kuzitumia fursa za ushiriki katika maonesho ya kimataifa ya vito vya thamani na maonesho ya vito vya mapambo ili kuongeza utambulisho, kuvutia wanunuzi, na kuimarisha fursa za mauzo ya nje, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **3.3.5 Sekta ya Mafuta na Gesi** | | | | | | |
| **Lengo 1 :Kuongeza utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi, ili kufungua kikamilifu fursa za rasilimali za nishati za taifa kwa ajili ya kuendeleza nishati endelevu na kukuza uchumi** | | | | | | |
| 1. Kutekeleza mpango wa motisha mahsusi kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika utafiti wa mafuta na gesi, unaolenga kufikia angalau asilimia 50 ya mabonde ya mashapo ya Tanzania, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni zinazohusiana, ili kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji katika utafiti wa mafuta na gesi asilia, ifikapo June 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha mfumo wa kifedha na udhibiti wa utafutaji wa mafuta na gesi ifikapo 2027, kwa kutoa masharti yaliyo wazi, imara na vivutio maalum ili kuvutia mitaji hatarishi | | | | | |
| | iii. Kuzindua mkakati maalum wa uhamasishaji wa utafiti wa mafuta na gesi asilia na kituo cha wazi cha taarifa kwa ajili ya kuonesha fursa za kijiolojia za Tanzania, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | iv. Kuanzisha kituo kimoja cha huduma kwa wawekezaji wa mafuta na gesi asilia kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa leseni, vibali, na idhini za udhibiti, na kupunguza muda wa uidhinishaji maombi, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| 2. Kulifanya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuwa Kampuni ya Kibiashara inayokidhi viwango vya kimataifa, kufikia Juni 2031 | 2.1 kubadilisha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuwa kampuni ya umma ya viwango vya kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuongeza mara mbili wigo wake wa utafiti kwa kupewa vitalu vya ziada vilivyo na leseni, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuimarisha uwezo wa kibiashara wa Shirika la Tanzania (TPDC) kwa kupata mtaji, kuunda timu ya usimamizi wa shirika ya kiwango cha kimataifa, na kuboresha mifumo yake ya kiufundi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **Lengo 2: Kuongeza uzalishaji na matumizi ya ndani ya gesi asilia nchini, ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati kwa ajili ya viwanda vya ndani na ukuaji wa uchumi,** kufikia **Juni 2031** | | | | | | |
| | 1.1 Kuhamasisha ongezeko la uzalishaji wa gesi nchini, kufikia Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| 1. Kuongezeka kwa Uzalishaji wa gesi asili nchi kavu kutoka MMSCFD 320 (milioni za futi za ujazo sanifu kwa siku) hadi MMSCFD 1000, kufikia Juni 2031 | i. Kuongeza kasi ya majadiliano ya mkataba wa uwekezaji kwa mradi wa LPG wa Mtwara, kufikia mwaka 2027. | | | | | |
| | ii. Kuimarisha mnyororo wa thamani wa gesi asilia ya ndani kwa kuanzisha ushirikiano wa kimataifa wa uhamishaji wa ujuzi na kuboresha mtandao wa usambazaji wa gesi wa nchi kavu ili kupunguza upotevu wa usafirishaji kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuongeza uzalishaji wa gesi nchi kavu kwa kuanzisha kisima kipya cha gesi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 2. Matumizi ya gesi asilia nchini kuongezeka toka 290 MMSCFD hadi 800 MMSCFD, ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuendeleza matumizi ya gesi asilia nchini, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Anzisha vivutio vya matumizi ya gesi (kwa kutoa vivutio vya kifedha na visivyo vya kifedha kwa viwanda na kaya vinavyohamia kwenye matumizi ya gesi kufikia 2028 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mpango wa kitaifa wa "Gesi kwa Viwanda" nchini, ambao utayataka maeneo makubwa ya viwanda kutumia gesi asilia, na hivyo kutengeneza uhitaji wa gesi hiyo, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Ubora wa Gesi ili kujenga uwezo wa kiufundi wa ndani, kusaidia Utafiti na Maendeleo katika matumizi ya gesi, na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi maalum kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 3: Tanzania kuwa kituo kinachoongoza cha uzalishaji na usafirishaji wa gesi barani Afrika, kwa kuongeza ushawishi katika masoko ya kikanda na kimataifa, na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa** | | | | | | |
| 1. Kuongeza usambazaji wa gesi katika Kituo cha Biashara ya Gesi cha Kikanda kutoka milioni 290 za futi za ujazo kwa siku, hadi milioni 3,500 za futi za ujazo kwa siku, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuanza mchakato wa kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa wauzaji wakuu wa gesi barani Afrika | | | | | |
| | i. Kuhakikisha upatikanaji wa mikataba ya muda mrefu ya mauzo ya gesi na nchi muhimu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kufikia Juni 2028. | | | | | |
| | ii. Kujenga kituo cha biashara ya gesi cha kikanda, chenye mabomba ya kuvuka mipaka na miundombinu ya kuhifadhia gesi, kwa ajili ya kusambaza gesi katika masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | iii. Kujenga ushirikiano wa kimkakati katika sekta ya nishati na kuoanisha sera za biashara ya nishati za kuvuka mipaka na nchi | | | | | |

| Shabaha | | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | | wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika , ili kuwezesha biashara ya gesi katika ukanda huu, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| 2. Uzalishaji wa gesi baharini utakaowezesha biashara ya mauzo ya LNG kufikia tani milioni 15 kwa mwaka kufikia Juni 2031 | 2.1 | Kukuza uzalishaji na mauzo nje ya gesi asilia ya kimiminika , kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. | Kujenga mfumo thabiti wa udhibiti na kifedha utakaohakikisha mazingira rafiki kwa uwekezaji katika mradi wa LNG na uthabiti wa mikataba ya mauzo ya gesi kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. | Kuanzisha mradi wa kusindika gesi asilia ya kimiminika kwa ajili ya mauzo nje ya nchi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **3.3.6. Sekta ya Utalii.** | | | | | | | |
| **Lengo 1:** | | **Kuimarisha shughuli, bidhaa, mbinu na uzoefu wa utalii ili kukuza uendelevu, ujumuishi na uimara, sambamba na kupanua fursa za ushiriki kwa jamii za wenyeji na kuhakikisha ukuaji wa muda mrefu wa sekta** | | | | | |
| 1. Kuboresha nafasi ya Tanzania katika Usafiri na fahirisi ya maendeleo ya utalii kutoka nafasi ya 81 hadi 60 kati ya nchi 119 duniani, kufikia Juni 2031 | 1.1 | Kusaidia maendeleo ya bidhaa na masoko mapya ya utalii, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. | Kuandaa na kuzindua bidhaa mpya za utalii zilizo tayari kuingia sokoni kwa kuzingatia tathmini ya kina ya vivutio vya utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. | Kuandaa mkakati wa kitaifa wa kusetusha utalii unaolenga kuvutia watalii wenye matumizi ya juu kutoka masoko mapya, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | iii. | Kuzindua kampeni za masoko ya kimataifa zilizolengwa kwa bidhaa mpya za utalii katika masoko mapya ya kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.2 | Kuhamasisha uwepo na upatikanaji na fedha za gharama nafuu kwa ajili ya utalii, kila mwaka | | | | | |
| | i. | Kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Utalii | | | | | |
| | ii. | Kuanzisha mpango wa dhamana ya mikopo ya utalii ili kupunguza hatari kwa benki za biashara na kuwezesha upanuzi wa mikopo kwa sekta binafsi, kila mwaka | | | | | |
| | 1.3 | Kuimarisha uwezo wa maendeleo ya miundombinu ya utalii, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. | Kuwezesha Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi kuu za serikali kuwa na mifumo ya kisasa ya usimamizi wa miradi na fedha, ili kupanga, kununua, kufadhili, kutekeleza na kusimamia miradi mikubwa ya | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | miundombinu ya utalii kwa ufanisi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.4 Kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za utalii, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa kitaifa wa uthibitishaji wa utalii endelevu, unaowataka waendeshaji wote wa shughuli za utalii katika maeneo yaliyohifadhiwa kufuata viwango vya kimazingira na kitamaduni, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuweka sharti la utekelezaji wa mikataba ya mgao wa mapato kwa jamii katika miradi yote mipya ya utalii, ili kuhakikisha jamii za wenyeji zinapata sehemu ya moja kwa moja ya mapato ya utalii, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.5 Kuimarisha uwezo wa uratibu wa shughuli za utalii, kufikia ,Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kuendesha mfumo wa kitaasisi na sera kwa sekta ya utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuharakisha utekelezaji wa mifumo shirikishi ya kidijitali na majukwaa ya uratibu wa wadau, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | iii. Kuimarisha uunganishaji na uhamasishaji wa pamoja wa maeneo yaliyohifadhiwa katika kanda za utalii za mashariki na kusini, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | iv. Kuoanisha na kuunganisha hifadhi za taifa za kanda ya ziwa katika mizunguko ya utalii ya kikanda (Uganda na Rwanda), kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 1.6 Kufanya uwindaji wa kitalii kuwa wa ushindani, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha utawala na uwezo wa kiutendaji wa sekta ndogo ya uwindaji wa kitalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha mifumo ya udhibiti na sera ili kuhakikisha uwindaji wa kitalii unakuwa endelevu na shindani, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | iii. Kukuza masoko mseto na kuboresha ongezeko la thamani katika mnyororo wa uwindaji wa kitalii, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | iv. Kuanzisha na kuimarisha maeneo ya usimamizi wa wanyamapori katika vijiji vinavyozunguka hifadhi, ili kuongeza jitihada za kupambana na ujangili na kushirikisha jamii katika uhifadhi, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 1.7 Kuanzisha taasisi ya Urithi wa Asili na Maeneo ya Kale chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kufikia mwaka 2030 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | i. Kufanya ukaguzi wa urithi wa asili na maeneo ya kale yote yaliyopo nchini, kufikia Juni 2028 | | | | | |
| | ii. Kuhamisha shughuli zote za urithi wa asili na maeneo ya kale kutoka taasisi zingine za Wizara ya Maliasili na Utalii kwenda kwenye taasisi ya Urithi wa Asili na Maeneo ya Kale Tanzania (TNHAS) kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 1.8 Kujenga imani zaidi kwa watalii na wageni wanaotembelea Tanzania, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kutekeleza ratiba ya uhakika ya kupitia kodi, ada na tozo zinazohusiana na utalii kila baada ya miaka mitatu , kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuweka utaratibu wa lazima wa uanachama kwa wawekezaji wa utalii katika vyama vinavyotambulika vya sekta ya utalii, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.9 Kutumia fursa za mikataba ya ushirikiano wa nchi na nchi, wa kikanda, na wa kimataifa kwa ajili ya kukuza na kuendeleza utalii wa ukanda wa pwani na baharini, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kukuza na kuendeleza bidhaa za utalii rafiki wa mazingira katika fukwe katika maeneo ya pwani yenye kipaumbele, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha Taasisi ya Hifadhi za Pwani na Maeneo ya Baharini Tanzania chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| 2. Kuendeleza maeneo manne (4) maalum kiuchumi ya utalii na kuanza kazi, kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuongeza idadi ya Halmashauri za Serikali za Mitaa (LGAs) zinazoandaa ya na kutenga maeneo maalum kwa ajili utalii ya uwekezaji katika sekta utalii kutoka 13 hadi 26, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | i. Kuhalalisha na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya halmashauri zote ili kuzuia mabadiliko ya matumizi ya ardhi yasiyopangwa ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuagiza kutengwa, kutathmini, na kuhifadhi rasmi maeneo ya ardhi yanayofaa kwa uwekezaji wa utalii, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 2.2 Kujenga mifumo ya kifedha, kisheria na udhibiti ili kuvutia uwekezaji na kukuza biashara katika sekta ya utalii, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kufanya mapitio na mageuzi ya mifumo iliyopo ya kifedha, kisheria na udhibiti | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | inayosimamia uwekezaji katika sekta ya utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha na kusimamia kisheria marekebisho ya kodi, kanuni na taratibu, na mfumo wa udhibiti na urekebu unaosimamia uwekezaji katika sekta ya utalii kufikia mwaka 2029. | | | | | |
| | 2.3 Kuanzisha Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Utalii kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kujenga na kuendesha vituo vya meli za kitalii katika bandari zilizopo (Dar es Salaam, Tanga, Mtwara) na maeneo mapya (Kilwa, Bagamoyo, Mafia), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuanza na kuendesha huduma ya meli za kitalii katika Ziwa Victoria itakayounganisha Speke Bay, Mwanza, Musoma, Geita, Serengeti, Burigi–Chato, Kisumu na Entebbe, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kujenga na kuendesha vituo vya mikutano vya kimataifa katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | iv. Kuendeleza Kisiwa cha Mafia kuwa kituo maalum cha kutia nanga meli za kitalii kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 2.4. Kuandaa sera na mifumo shindani ya kuhimiza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) katika maendeleo ya utalii, kwa kuzingatia miundombinu, ubora wa huduma, na utalii endelevu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha na kuoanisha mifumo ya kisera, kisheria na ya udhibiti inayosimamia ubia kati ya sekta ya umma na sektabinafsi (PPP) katika sekta ya utalii, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya utawala na usimamizi wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuhakikisha maendeleo ya kimkakati ya miundombinu na ubora wa huduma, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | iii. Kuoanisha sera na mifumo ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na malengo ya utalii endelevu na jumuishi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kuongezea kwa Ushiriki wa wananchi katika sekta ya talii hadi kufikia asilimia 10 kufikia Juni 2031 | 3.1 Kurahisisha kanuni na taratibu za kiutawala ili kuwezesha wajasiriamali wa ndani kuingia kwenye soko la utalii, kufikia mwaka 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | i. Kurahisisha taratibu za utoaji wa leseni na vibali kupitia uanzishaji wa jukwaa la kidijitali lenye huduma zote, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kupitia, kurahisisha, na kuoanisha kanuni za utalii ili kuwaondolea urasimu wajasiriamali wa ndani, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | iii. Kuweka utaratibu rasmi wa kusaidia wajasiriamali wa utalii wa ndani, ikijumuisha ushauri wa kisheria, kifedha, na kiufundi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 3.2 Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa biashara na ujasiriamali ili kuwawezesha wananchi, wakiwemo wanawake na watu wenye mahitaji maalum, kuanzisha na kuendeleza biashara zinazohusiana na utalii, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuanzisha mifumo jumuishi ya mafunzo na usaidizi wa ujasiriamali kwa biashara ndogondogo na za kati (SMEs) katika sekta ya utalii, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha mifumo ya kisheria na udhibiti ili kuwezesha upatikanaji wa fedha na rasilimali kwa wajasiriamali wa ndani wa sekta ya utalii, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 3.3 Kuanzisha mfuko wa utalii ili kuwaezesha kampuni chipukizi na biashara ndogondogo na za kati kwa wajasiriamali wa ndani, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kuweka utaratibu wa kutoa msaada wa kifedha na kiufundi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati (MSMEs) katika sekta ya utalii kupitia mfuko wa utalii (TBF), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 3.4 Kuanzisha majukwaa ya wafanyabiashara wa ndani kushirikiana waendesha utalii wakubwa na masoko ya kikanda na kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha majukwaa ya kawaida na ya kidijitali, ili kurahisisha mitandao, ushirikiano, na upatikanaji wa soko kwa biashara za utalii za ndani, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha rasmi mifumo ya kujenga uwezo na kusaidia upatikanaji wa masoko kwa biashara za utalii za ndani, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | iii. Kutayarisha orodha ya miradi iliyodhibitiwa, yenye masharti ya ushiriki wa watanzania katika hisa na umiliki wa biashara za utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | iv. Kusimamia kampuni za utalii zinazomilikiwa na wageni nchini kuoanisha | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | usajili na uendeshaji wa sera zinazohimiza ushiriki wa wananchi, kufikia 2028 | | | | | |
| 4. Kuhifadhiwa na kuunganishwa kwa zaidi ya asilimia 12 ya maeneo ya vivutio vya utalii, kufikia Juni 2031 | 4.1 Kuongeza ufikiaji wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa usafiri wa anga, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuboresha na kusimamia njia za kurukia ndege za viwanja vyote 39 vya ndege vilivyopo, ambavyo vinavyohudumia maeneo yaliyohifadhiwa, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | ii. Kujenga viwanja vya ndege vipya na kuimarisha viwanja vya ndege vya kanda ambavyo viko karibu na maeneo muhimu yaliyohifadhiwa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kupitia na kurahisisha kodi, ada na tozo zinazohusiana na usafiri wa anga, ili kuimarisha muunganisho wa biashara ya utalii, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | 4.2. Kuongeza huduma ya malazi yenye nyota moja hadi tano, kutoka 315 hadi 508, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuyatambua na kuyapa kipaumbele maeneo yenye upungufu wa malazi na kuanzisha mfumo wa uwezeshaji wa ardhi na miundombinu, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha na kuainisha viwango vya malazi, mifumo ya uainishaji, na miundo ya motisha, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | 4.3 Kuhakikisha ufunguaji upya wa kudumu na ulinzi wa shoroba zote za wanyamapori nchini kote, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kuainisha mfumo wa kisheria wa urejeshaji na ulinzi wa shoroba za wanyamapori, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha sera, miundombinu, na mifumo ya ufuatiliaji ili kusaidia shoroba za wanyamapori, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | iii. Kurasimisha mifumo ya ushirikishwaji wa jamii na utatuzi wa migogoro ili kusaidia ulinzi wa shoroba za wanyamapori, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 4.4 Kuongeza vituo vya malazi ya gharama nafuu katika hifadhi za taifa kwa ajili ya watalii wa ndani kutoka 10 hadi 22, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kurasimisha mpango wa taifa wa upanuzi na uboreshaji wa vituo vya malazi ya gharama nafuu kwa watalii wa ndani, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha sera wezeshi na mbinu za motisha ili kuvutia uwekezaji na usaidizi wa uendeshaji wa malazi ya bei nafuu katika kila eneo lenye shughuli nyingi za utalii (protected area), kufikia Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 4.5 Kuanzisha mfumo wa kimtandao wa uhifadhi wa nafasi kwa watalii kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kutumia usanifu, viwango na mfumo jumuishi ya kidijitali, kwa ajili ya kurahisha matumizi ya mfumo wa kitaifa wa maombi ya uhifadhi wa nafasi za utalii, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kuweka utaratibu rasmi wa kujenga uwezo na kutoa elimu kwa wafanyabiashara ya utalii, ili wapitishe na kutumia mfumo wa kuhifadhi nafasi mtandaoni kufikia mwaka 2031 | | | | | |
| | 4.6 Kuandaa fursa za kuvutia uwekezaji kwa wawekezaji wa kimataifa zinazolenga hoteli za kifahari, vivutio vya utalii na miundombinu ya utalii inayolenga masoko ya kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kupitia na kuimarisha sera za kutenga, kuandaa, na kugawa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa kigeni katika miundombinu ya utalii wa daraja la juu, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuandaa na kuimarisha mfumo wa kurahisisha uwekezaji na vivutio ili kuvutia mitaji mikubwa ya kigeni, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | iii. Kuendeleza na kuimarisha mifumo ya kukuza masoko na miundombinu, ili kuongeza imani ya wawekezaji wa kimataifa kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 4.7 Kutoa motisha za kila mwaka kwa biashara za utalii ili kuchochea utekelezaji wa mbinu endelevu, ikiwa ni pamoja na upunguzaji wa taka, matumizi bora ya nishati, na uhifadhi wa mazingira, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kutumia mfumo wa motisha za kifedha na utambuzi kwa ajili ya mbinu endelevu za utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha mifumo ya kujenga uwezo na mikakati ya masoko ya kimataifa ili kukuza maeneo mahiri ya utalii kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 5. Angalau asilimia 40 ya biashara za utalii kuendeshwa kidijitali, kufikia Juni 2031 | 5.1 Kuendeleza vituo vitano vya utalii wa kidijitali vilivyowezeshwa na teknolojia ya Intaneti ya Vitu, Akili Unde (na uchambuzi wa takwimu nyingi mchanganyiko (Big Data) ili kuboresha safari za wageni, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kutumia mifumo ya miundombinu ya utalii wa kisasa iliyounganisha teknolojia ya Intaneti ya Vitu (Akili Unde (AI), na uchambuzi wa Big Data, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha mifumo ya kujenga uwezo na mikakati ya masoko ya kimataifa ili kukuza maeneo mahiri ya utalii kufikia Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 5.2 Kuzindua majukwaa ya mafunzo ya mtandaoni kwa wataalamu wa utalii ili kuimarisha ujuzi katika ukarimu, huduma kwa wateja, na uelewa wa kidijitali, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kutumia usanifu, viwango, na mfumo wa maudhui kwa ajili ya majukwaa ya mafunzo ya utalii kwa njia ya mtandao, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya mafunzo ya mtandaoni (online training platforms), ikijumuisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini (M&E), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 5.3 Kuanzisha kituo cha taifa cha takwimu za utalii (National Tourism Data Hub) kwa ajili ya kukusanya, kuchambua, na kusambaza takwimu za wakati halisi (real-time) kuhusu mienendo ya watalii, mapendeleo yao, na mchango wa kiuchumi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kurasimisha usanifu, utawala, na mfumo wa uendeshaji wa kituo cha taifa cha takwimu za utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya kujengea uwezo na mifumo ya kusaidia mapokeo, ili kuhakikisha uendelevu katika kujifunza na ushiriki wa sekta nzima, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | iii. Kusanifisha na kurasimisha matumizi ya mfumo wa malipo uliounganishwa kwenye taasisi zote za Wizara ya Maliasili na Utalii, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | 5.4 Kupevusha (kampuni changa za utalii zinazozingatia suluhisho bunifu za kidijitali, kama vile ziara za uhalisia , programu endelevu za usafiri na uzoefu wa kitamaduni, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya ubunifu na mifumo ya ugharamiaji kwa uanzishaji wa biashara changa za utalii kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kuweka utaratibu rasmi wa kujenga uwezo na kupata masoko ili kuunganisha wajasiriamali wachanga na masoko ya utalii ya ndani, kikanda, na kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 6. Kufikia kiwango cha matumizi ya mfumo jumuishi wa utalii wa kisasa nchini kwa asilimia 33, unaoendeshwa na majukwaa ya kidijitali, miundombinu na uboreshaji wa matumizi ya | 6.1. Kuzindua uzoefu wa uhalisia pepe kwenye tovuti za kitamaduni na urithi, ili kuvutia watalii wanaopenda teknolojia za kisasa na kutoa uzoefu wa kipekee kwa watalii, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kutumia teknolojia fungamani na viwango vya maudhui kwa uzoefu wa uonaji wa uhalisia (VR), kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kurasimisha ujengaji wa uwezo na mifumo ya masoko ya kimataifa, ili | | | | | |

| Shabaha | | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| rasilimali kwa kutumia teknolojia za kidijitali kufikia Juni 2031 | | kupelekea uzoefu wa kipekee, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 6.2 | Kuanzisha mfumo thabiti wa ubunifu kwa ajili ya matumizi ya teknolojia bunifu katika sekta ya utalii kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | i. | Kuendeleza miundombinu ya ubunifu pamoja na mifumo inayosaidia utawala, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. | Kurasimisha programu za kujenga uwezo na mifumo ya sera inayosaidia matumizi ya teknolojia, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 6.3 | Kuimarisha nguvukazi watu kwa ujuzi unaohitajika kwa teknolojia za kisasa, kila mwaka | | | | | |
| | i. | Kurasimisha programu za mafunzo endelevu na uboreshaji wa ujuzi katika mifumo ya kitaifa ya ujuzi wa utalii, kila mwaka | | | | | |
| | ii. | Kuendeleza na kurasimisha ushirikiano na mifumo ya ithibati kupitia ushirikiano kati ya sekta, vyuo vya elimu na serikali kila mwaka | | | | | |
| | 6.4 | Kuutengeneza mazingira yanayotabirika na yanayofaa kwa utalii, ubunifu wa kiteknolojia na maendeleo ya rasilimali watu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. | Kuimarisha mifumo ya sera, miundombinu, na ufadhili ili kusaidia ubunifu katika utalii, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | ii. | Kuweka utaratibu thabiti wa maendeleo ya rasilimali watu na njia za kubadilishana maarifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 7. Kuifanya Tanzania kuwa kituo kikuu cha utalii wa matukio utamaduni, na ikolojia kufikia Juni 2031 | 7.1 | Kuendeleza uzoefu wa kina wa utalii wa kitamaduni (mfano: Maeneo ya Urithi wa Dunia ya UNESCO, ziara za jamii za asili, sherehe za kitamaduni), unaovutia wasafiri wa kimataifa wanaopenda historia na utamaduni, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. | Kuanzisha mifumo ya masoko ya kidijitali na mitandao ya kijamii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. | Kuweka mifumo ya kitaasisi ya ushiriki na ushirikiano wa kimkakati katika maonyesho ya kimataifa ya utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 7.3 | Kuandaa zana za ukusanyaji na uchakataji wa takwimu pamoja na kufuatialia utendaji wa sekta ya utalii, demografia ya watalii na masoko yanayoibukia ili kuoainisha huduma za utalii wa Tanzania na mahitaji ya kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. | Kuanzisha na kurasimisha jukwaa la kituo shirikishi cha uangalizi wa takwimu za utalii, kufikia mwaka 2028 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ii. Kupitisha na kusanifisha uchambuzi wa kina wa takwimu na teknolojia zinazoibuka ndani ya kitovu cha takwimu, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | iii. Kurasimisha kukuza uwezo wa takwimu kwa wadau, utafiti wa masoko, na mifumo ya kupima ufanisi, kufikia mwaka 2031 | | | | | |
| | 7.4 Kuanzisha vituo vya mafunzo ya ufundi stadi kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kutoa programu maalum za mafunzo zinazoendana na viwango vya kimataifa vya utalii na mienendo inayoibuka, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa mitaala na kurasimisha mifumo ya kukuza uwezo, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuendeleza miundombinu ya kisasa na kuingiza viwango vya kiteknolojia katika vituo vya mafunzo, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | iii. Kurasimisha uhusiano wa viwanda na mifumo ya ajira, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 7.5 Kuhamasisha mikakati ya kukuza bidhaa za utalii za Tanzania, kuvutia watalii wa kimataifa wanaotumia kiasi kikubwa cha fedha, na kuingia katika masoko mapya ya kimataifa yanayokua kwa kasi katika sekta ya utalii duniani, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kurasimisha mifumo ya kitaasisi ya ukuzaji, uendelezaji, na kusetusha bidhaa za utalii, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha miundombinu ya kiwango cha juu na upatikanaji wa masoko kupitia mifumo ya uwekezaji wa kimkakati, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuandaa na kurasimisha utambulisho wa chapa ya Tanzania duniani, kampeni za masoko, na mifumo ya ushirikiano wa kimkakati, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 7.6 Kuendeleza ushirikiano na mashirika ya ndege ya kimataifa na waendeshaji wa safari za utalii ili kuanzisha njia mpya za usafiri, pamoja na kuitangaza Tanzania katika maonesho ya kimataifa ya utalii na majukwaa ya kidijitali, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuandaa na kurasimisha mifumo ya uunganishaji wa safari za anga na ufunguaji wa njia mpya za ndege, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuwa na ushirikiano rasmi na wa kimkakati na waendeshaji wa safari za utalii wa kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuimarisha mifumo ya masoko ya kidijitali na ushiriki katika majukwaa ya kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 7.7 Kuendeleza miundombinu ya utalii, ikijumuisha malazi ya kisasa, vituo vya mikutano, mapumziko rafiki kwa mazingira, na mitandao ya usafiri (mfano: viwanja vya ndege, barabara na reli) ambayo inasaidia mnyororo wa thamani wa utalii, kila mwaka | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | i. Kutekeleza mifumo ya utalii wa hali ya juu na miundombinu ya mikutano (MICE), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kurasimisha taratibu za uhifadhi wa mazingira na mifumo ya uendelezaji wa miundombinu ya usafirishaji wa kisasa kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 7.8 Kuanzisha Mamlaka ya Taifa ya Utalii na Ukarimu kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kutunga na kusimamia sheria ya muundo wa kitaasisi na utawala, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha, kurasimisha na kutumia sera, kanuni na mfumo wa viwango, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 8. Kuongezeka kwa idadi ya watalii wa kimataifa katika sehemu za kifahari kuongezeka kwa asilimia 8 kufikia Juni 2031 | 8.1 Kurahisisha michakato ya viza na kuanzisha viza za baada ya kuwasili au viza ya kidijitali kwa masoko makuu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha sera ya viza na mifumo ya kuwezesha michakato ya viza iliyorahisishwa, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. k u t a yarisha na kurasimisha mifumo ya viza ya kidijititali (e-viza) salama na mifumo iliyounganishwa, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 8.2 kuanzisha mifumo ya malipo isiyohitaji pesa taslimu na majukwaa ya kidijitali, ili kuwapunguzia adha wasafiri, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. kuanzisha na kurasimisha mfumo wa malipo usio wa pesa taslimu, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. kuanzisha na kusanifisha jukwaa la kitaifa la kitalii lililofungamanishwa kidijitali, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | iii. Kuimarisha mifumo ya usalama wa mtandao ili kulinda malipo na taarifa binafsi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 8.3 Kuanzisha programu za mafunzo kwa wataalamu wa utalii ili kuboresha ubora wa huduma za ukarimu uongozaji watalii na huduma kwa wateja wa kiwango cha juu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa mitaala inayolingana na viwango vya kimataifa, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya kisasa ya utoaji mafunzo na kujenga uwezo, kufikia 2029 | | | | | |
| | iii. Kuanzisha miongozo ya ushirikiano kati ya sekta ya utalii na uendelezaji kitaaluma, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 8.4 Kujenga hoteli, sehemu za mapumziko na kutoa huduma za utalii zenye hadhi ya juu katika maeneo tengefu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa viwango vya miundombinu na vituo vya huduma za utalii, kufikia mwaka 2029 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ii. Kuandaa miongozo ya kuboresha na kusimamia uzoefu wa wageni, kufikia mwaka 2028. | | | | | |
| | 8.5 Kukuza utalii endelevu ili kuvutia watalii wa kipato cha juu na wanaojali mazingira, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuandaa na kuanzisha viwango vya kijani (pamoja na mifumo ya ithibati, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kurasimisha mifumo ya kukuza miundombinu na uendeshaji endelevu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuanzisha miongozo ya ushirikishwaji wa jamii, kila mwaka | | | | | |
| | iv. Kuanzisha miongozo ya kimataifa ya masoko na uhamasishaji wa utalii endelevu, kila mwaka | | | | | |
| **3.3.7 Sekta ya Fedha** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuimarisha utawala bora, ufanisi wa uendeshaji na uthabiti wa kifedha ili kuhakikisha ushindani na uimara wa sekta ya benki za biashara** | | | | | | |
| 1. Kuongeza kiwango cha uwiano wa utoshelevu wa mtaji (CAR) kufikia zaidi ya asilimia 16.5, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vihatarishi kwenye mahitaji ya mitaji, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.2 Kuwezesha kuunganishwa na kununuliwa kwa benki dhaifu ili kuimarisha mitaji, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.3 Kuanzisha na kuendesha uwekezaji wa muda mrefu wa sekta ya umma na sekta binafsi katika benki za biashara, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 2. Kuongeza uwiano wa amana kwa Pato la Taifa kufikia angalau asilimia 40, kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuimarisha mfumo wa fedha wa kidijitali unaoongozwa na matumizi ya takwimu, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 2.2 Kuanzisha mifumo ya kitaifa ya kuweka akiba inayotumia motisha zinazohusishwa na amana, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 2.3 Kupanua kiwango cha ujumuishaji wa huduma za kifedha kupitia mawakala wa benki na upanuzi wa huduma za kidijitali nchi nzima, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kudhibiti mikopo chechefu kubaki chini ya asilimia 5, kufikia Juni 2031 | 3.1 Kuanzisha mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa vihatarishi vya mikopo unaotumia akili unde na uchambuzi wa takwimu kufikia Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 3.2 Kuweka sharti la matumizi ya mifumo madhubuti ya urejeshaji na ufuatiliaji makini wa mikopo, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | 3.3 Kujumuisha sera za ukopeshaji zinazozingatia mazingira, jamii na utawala bora katika kanuni za kibenki, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| 4. Kupanua kiwango cha mikopo kwa sekta binafsi kufikia asilimia 25 ya Pato la Taifa, kufikia mwaka 2030 | 4.1 Kuimarisha sera za ugawaji mtaji kulingana na vihatarishi kwa ajili ya kuhamasisha mikopo kwenye sekta zenye tija kubwa, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 4.2 Kuimarisha mifumo ya dhamana ya serikali kwenye mikopo ili kupunguza vihatarishi vya utoaji mikopo kwa biashara ndogondogo ndogo na za kati na sekta za kimkakati, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 4.3 Kuanzisha jukwaa la kidijitali la kupima uwezo wa mkopaji kwa kutumia teknolojia ya fedha (fintech) na takwimu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 5. Kuongezeka kwa kiasi cha watu wazima wanaopata na kutumia huduma rasmi za kifedha kufikia asilimia 90, ifikapo Juni 2031 | 5.1 Kuanzisha programu za elimu ya fedha za kidijitali kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 5.2 Kutoa motisha kwa benki za biashara kuanzisha akaunti na pochi za kidijitali zenye gharama nafuu kwa wananchi wa vijijini na makundi yaliyotengwa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 5.3 Kuunganisha majukwaa ya pesa za simu na benki ili kutoa huduma jumuishi, kufikia Juni 203. | | | | | |
| **Lengo 2:** | **Kuimarisha mtaji wa Taasisi za Kifedha za Maendeleo (DFIs), na kuwezesha uwekezaji wa sekta binafsi, mifuko ya hifadhi ya jamii na makampuni ya bima ili kuwa na ukuaji na uendelevu, kufikia mwaka 2030.** | | | | | |
| 1. Kuongeza mtaji wa DFIs kufikia angalau asilimia 1.25 ya Pato la Taifa, kufikia Juni 2031. | 1.1 Kuanzisha mpango wa hatua kwa hatua wa serikali kuongeza mtaji wa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 1.2 Kusetusha vyanzo vya fedha kupitia hati fungani za ndani na ushirikiano na mifuko ya pensheni, na taasisi nyingine za uwekezaji | | | | | |
| | 1.3 Kutumia mbinu za ugharamiaji mseto na kupata fedha, kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na washirika wengine wa kimataifa, ifikapo Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| 2. Kufikia uwiano wa chini wa mtaji wa umma na binafsi wa 1:1.14 katika Uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni DFIs, kufikia Juni 2031 | 2.1 | Kuimarisha mifumo ya udhibiti ili kuruhusu ushiriki wa usawa wa ndani na nje ya nchi kwa wawekezaji binafsi wa ndani na nje, ikijumuisha ubinafsishaji kwa sehemu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 2.2 | Kuwezesha ushiriki wa IFC, Benki ya Maendeleo ya Afrika , Benki ya Uwekezaji ya Ulaya , na taasisi kama hizo, ili kuchochea mitaji binafsi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 2.3 | Kuongeza uwekezaji wa sekta ya kibinafsi, ikijumuisha makampuni, biashara za ndogondogo na za kati na wawekezaji wa taasisi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **Lengo 3: Kuboresha mwongozo wa maendeleo ya Taasisi za Fedha za Maendeleo kwa kuimarisha usimamizi wa vihatarishi na kuboresha michakato ya tathmini ya mikopo na kuhakikisha ufanisi katika ufuatiliaji na urejeshaji wake** | | | | | | | |
| 1. Kudhibiti mikopo chechefu ya uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni kuwa chini ya asilimia 5, kufikia Juni 2031 | 1.1 | Kuimarisha udhibiti na mifumo ya usimamizi wa vihatarishi, kupitia nyenzo za teknolojia ya Akili unde, viwango vya usimamizi wa sekta binafsi, kusetusa mikopo, na zana zinazoendana na hisa, kila mwaka | | | | | |
| | 1.2 | Kuongeza ugharamiaji wa miundombinu, uzalishaji viwandani, na kilimo, kila mwaka. | | | | | |
| | 1.3 | Kupanua wigo wa ufadhili kwa biashara ndogondogo na za kati (SMEs) na kampuni chipukizi kwa kutumia mitaji ya hisa, uhitaji wa ubia and mikopo ya kidijitali, mara mbili kwa mwaka | | | | | |
| | 1.4 | Kuanzisha dirisha la ufadhaili kwa teknolojia ya masuala ya fedha na makampuni yanayoendeshwa kiteknolojia, mara mbili kwa mwaka | | | | | |
| | 1.5 | Kutumia mfumo wa *block chain* kufadhili mnyororo wa thamani wa kilimo na ufadhili endelevu wa modeli za kijani, kila mwaka | | | | | |
| **Lengo 4**: Sekta ndogo ya bima iliyoimarishwa inayoongozwa na sekta binafsi ambayo huchochea ukuaji endelevu wa uchumi kwa kuongeza uwepo wa bima, kuimarisha uthabiti wa soko na kutoa na kusetusha bidhaa zinazoingizwa sokoni | | | | | | | |
| 1. Kuongeza matumizi ya bima (jumla ya malipo kwa Pato la Taifa) hadi asilimia 2.6, kufikia Juni 2031 | 1.1 | Kuimarishwa kwa mifumo ya udhibiti, kukuza bima ndogo, na kuendesha programu za uhamasishaji nchi nzima kufikia Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 1.2 Kukuza ubunifu kupitia bima ya kidijitali, kilimo mahsusi na bidhaa za afya, na kuboresha ujuzi kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3 Kuongeza ushiriki wa soko la bima ya kikanda na kimataifa kupitia viwango vya kimataifa vya uandishi, uhakikisho wa bima na madai, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **Lengo 5: Kuhamasisha usetushaji wa mitaji na kuongeza uzingatiaji wa kanuni, ikiambatana na viwango vya Nchi zenye Mapato ya Kati ya Juu (UMIC) ili kuchochea ukuaji wa uchumi na uhimilivu** | | | | | | |
| 2. Kufikia asilimia 33 ya ufadhili wa mtaji mseto na ujumuishaji kamili wa huduma ndogo za kifedha vijijini, kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuimarisha mifumo ya usetushaji na kuanzisha biashara ndogondogo na za kati na mbinu za kifedha zinazofaa vijijini, ikijumuisha dhamana ya mikopo midogo midogo na miamala ya kidijitali ifikapo kufikia 2031 | | | | | |
| | 2.2 Kuwezesha uhimilivu na ujumuishwaji wa sekta ndogo ya fedha na ushirikishwaji wa sekta ya mikopo midogo midogo kupitia uwekaji rekodi za biashara zisizo rasmi kidijitali, kandarasi mahiri, na ufadhili unaozingatia mazingira, jamii na utawala ESG, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| 3. Asilimia 25 ya huduma za kifedha kupatikana kupitia mfumo wa kidijitali, kufikia Juni 2031 | 3.1 Kutekeleza huduma za benki ndogo za kidijitali na huduma za simu/kidijitali katika maeneo ya vijijini ambayo hayana huduma ya kutosha, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 3.2 Kuandaa majukwaa ya ukopeshaji yanayoendeshwa na akili unde pamoja na sera zinazosaidia teknolojia ya kifedha (fintech), ifikapo June 2031. | | | | | |
| | 3.3 Kuunganisha mifumo ya kidijitali ya mikopo midogo midogo na suluhu za fedha zisizodhibitiwa na mamlaka kuu (DeFi) | | | | | |
| 4. Kubadilika kuelekea mfumo unaoendeshwa kikamilifu na sekta ya mikopo midogo midogo kwa Biashara Ndogo na za Kati (SME), ukiwa na ujumuishi wa maeneo ya vijijini kwa asilimia 20–25, kufikia Juni 2031 | 4.1 Kuimarisha mifumo ya udhibiti ili kuongeza ujumuishaji wa kifedha wa kwa biashara ndogo na za kati na vijijini, na kukuza uwekezaji wa vijijini, i kufikia, Juni 2031 | | | | | |
| | 4.2 Kuendesha programu za kitaifa za elimu ya kifedha kwa taasisi za fedha za kati MFIs na na biashara ndogo na za kati SMEs, ifikapo June 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **Lengo 6: Kuongeza mikopo na kuboresha udhibiti wa kanuni ili kuhakikisha unaendana na viwango vya UMIC ili kuchochea maendeleo endelevu na ustahimilivu wa kifedha** | | | | | | |
| 1. Kupunguza kutengwa kwenye huduma za kifedha hadi chini ya asilimia 10, ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa makundi yaliyokosa fursa, ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijijini, kupitia ushirikiano kati ya mabenki, taasisi za mikopo midogo midogo (MFIs), na kampuni za teknolojia ya kifedha (fintechs) kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.2 Kuwezesha ujuzi wa masuala ya kifedha nchini kote ili kuongeza ufahamu wa manufaa ya akaunti, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.3 Kusasisha huduma za sekta ya kifedha chini ya NFIF, ikijumuisha majukwaa kimtandao na kidijitali kupitia mabenki, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 2. Kuinua ukopaji rasmi, kufikia asilimia 31.2, kufikia Juni 2031 | 2.1 Kufanya mageuzi ya mifumo ya mikopo, ili kuwezesha biashara ndogo na za kati, makampuni ya biashara ya vijijini, na sekta isiyo rasmi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 2.2 Kubadilisha utoaji wa mikopo kupitia mifumo ya kidijitali inayoendeshwa na akili unde na teknolojia ya kifedha (Fintech), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kuongeza umiliki wa akaunti za benki hadi asilimia 33 na ushiriki wa kuweka akiba hadi asilimia 35 kufikia Juni 2031 | 3.1 Kupanua miundombinu ya huduma za kifedha kidijitali ikiunganishwa na ubunifu wa kampuni za teknolojia ya kifedha Fintech kutaifanya Tanzania kuibuka kinara wa kikanda wa Fintech, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 3.2 Kutekeleza programu ya kitaifa ya ujuzi na utaalamu wa masuala ya fedha ili kuongeza imani na ushiriki wa watumiaji, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| **Lengo 7: Kuboresha mazingira ya biashara kwa ajili ya ukuaji wa mtaji wa biashara Tanzania na mfumowa uwekezaji binafsi kwa kuongeza upatikanaji wa fedha kwa kampuni chipukizi na Makampuni makubwa** | | | | | | |
| 1. Kuongezeka kwa uwekezaji wa mtaji wa ubia (na uwekezaji binafsi wa hatua za awali kutoka dola za Marekani milioni 52 hadi zaidi ya dola za Marekani milioni 242 kwa mwaka, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha Mtandao wa Kitaifa wa wawekezaji wa binafsi wa wa hatua za awali na kurekebisha kanuni za uwekezaji binafsi na uwekezaji wa mtaji kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 1.2 Kuanzisha mfuko wa kitaifa kwa ajili ya kampuni chipukizi ili kuwezesha mitaji ya awali, ruzuku ya utafiti na maendeleo kutoka serikalini, na kuimarisha Soko la | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | Hisa la Dar es Salaam (DSE) kwa IPOs na M&A kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.3 Kwa kutumia ushirikiano wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika , kutavutia uwekezaji wa kikanda, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **Lengo 8: Kuongezeka kwa mitaji ya ubia na mikataba ya wawekezaji binafsi itakayowezesha ustawi wa mfumo wa kampuni chipukizi na ukuaji wa biashara unaoongozwa na ubunifu** | | | | | | |
| 1. Kuongeza mikataba ya mitaji ya ubia na wawekezaji binafsi kutoka 10 hadi 30 kwa mwaka kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuanzishwa kwa Programu ya Kitaifa ya Usaidizi wa Hakimiliki (National IP Support Programme) ili kulinda bunifu za kampuni chipukizi kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 1.2 Kuendeleza Hifadhi za Teknolojia (na Vituo vya Ubunifu ili kuchochea mabadiliko ya kidijitali na ujasiriamali, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| **Lengo 9: Kukuza ujasiriamali jumuishi na endelevu, utakaowezesha ushiriki katika ukuaji wa kiuchumi na kuleta athari chanya katika mazingira** | | | | | | |
| 1. Kuboresha nafasi ya Tanzania katika Fahirisi ya Ubunifu Duniani kufikia nafasi ya 90, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha kongani za kiteknolojia na vituo vya ubunifu na mfuko wa uwekezaji wa kibiashara uliokusudiwa wa kutumia akili unde teknolojia ya kibiologia na teknolojia za kimazingira, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | 1.2 Kuanzisha masoko ya hisa ya upili ya kikanda, kurahisisha IPO tano (5) za kuanzisha biashara chipukizi na kuwezesha mifuko ya pensheni kuwekeza kwenye kampuni changa kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | 1.3 Kutekeleza mpango wa "kuhakikisha maendeleo ya baadaye" ili kuiwezesha Tanzania kupiga hatua kubwa za kimaendeleo, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **3.3.8. Sekta ya Michezo na Ubunifu** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuimarishwa kwa ushindani wa ndani, kikanda na kimataifa wa tasnia ya michezo na ubunifu,kukuza ukuaji, na fursa za uwekezaji** | | | | | | |
| 1. Ukuaji halisi wa sekta kutopungua asilimia 20 kwa mwaka, kufikia Juni 2031. | 1.1 Kujenga na kuboresha miundombinu ya michezo (viwanja, vituo vya mafunzo na kumbi za michezo) kote nchini, kwa kuanzisha angalau vituo 5 vya ubora wa kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha taasisi za kukuza vipaji za kikanda, na kudahili vijana 100,000 katika programu za michezo, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuzindua programu za kila mwaka za ufadhili wa masomo ili kusaidia vijana wenye vipaji wasiopungua 100 kwenda | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | shule za michezo na sekta za ubunifu ng'ambo, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | iii. Kuanzisha sera na vifurushi vya motisha kurahisisha upatikanaji wa ardhi ili kuvutia uwekezaji binafsi katika miundombinu ya michezo na sekta za ubunifu (sanaa/filamu), kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | iv. Kujenga mfumo endelevu wa biashara ya michezo unaokuza utalii wa michezo katika ngazi zote, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 2. Kuvutia watalii zaidi 100,000 wa michezo kila mwaka kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuanzisha mfumo/utaratibu wa biashara ya michezo ili kukuza utalii wa michezo, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha mfumo/utaratibu wa biashara ya michezo ili kukuza utalii wa michezo, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| 3. Wasanii wa Tanzania kutambulika kimataifa katika angalau nyanja moja kuu ya ubunifu, kufikia Juni 2031 | 3.1 Kujenga mfumo endelevu wa utengenezaji wa filamu, usambazaji na kurekodi muziki, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha majukwaa ya kanda (zonal platforms) ili wasanii wa Tanzania waweze kuonyesha kazi zao kitaifa na kimataifa, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| 4. Angalau asilimia 10 ya maudhui iweze kupatikana duniani kote, kupitia majukwaa ya kidijitali, kufikia Juni 2031 | i. Kwa kutumia fursa ya ushirikiano na majukwaa ya kidijitali ya kimataifa, kupanua wigo wa wabunifu wa Tanzania, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuandaa mikakati ya kuongeza mauzo nje ya sanaa, muziki, filamu, na mitindo ya Tanzania, ikilenga masoko ya kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuanzisha vituo vya kulelea na vichapuzi vya ubunifu kwa wajasiriamali wabunifu, kwa kutoa ufadhili, ushauri na fursa za mitandao, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 5. Mashirika yote ya wabunifu na michezo ya Tanzania yawezeshe wasanii kupokea mirabaha kwa kazi zao kila mwaka, kufikia Juni 2031 | 5.1 Kuimarisha mifumo ya Hakimiliki na Hatimiliki kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | i. Anzisha mfumo bora wa usajili wa hakimiliki na IP ili kulinda wasanii wa ndani dhidi ya matumizi yasiyoidhinishwa na uharamia, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mfumo madhubuti wa kuwasaidia wabunifu na mashirika ya michezo Tanzania kuwa na uwezo wa kusajili na kulinda haki zao za miliki (IP), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuanzisha huduma maalum za kisheria na kifedha kwa usimamizi wa Haki miliki (IP), ikijumuisha motisha za kifedha | | | | | |

| **Shabaha** | **Afua** | | **Mpango wa Maendeleo wa Mwaka** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** |
| | | (kama kupunguza kodi) na zisizo za kifedha ili kulinda haki miliki IP na kibiashara, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iv. | Kuhakikisha ulinzi wa hakimiliki kwa wabunifu wa kidijitali na watengeneza maudhui kwenye majukwa ya kieletroniki, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | v. | Kuhakikisha sheria za hakimiliki (IP) na kanuni za hakimiliki katika michezo zinatekelezwa kikamilifu, zikijumuisha haki za matangazo uuzaji wa bidhaa na maudhui ya kidijitali, kufikia Juni2031 | | | | | |
| **3.3.9 Maendeleo ya Makazi na Biashara ya Ardhi na Majengo** | | | | | | | |
| **Lengo 1:** **Kuboresha mazingira ya ushindani, uwazi na rafiki, kwa wawekezaji wa ndani na nje katika sekta ndogo ya majengo na ardhi (real Estate), ili kuchochea ukuaji wake na kuongeza mchango wake katika uchumi** | | | | | | | |
| 1. Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya majengo katika pato la taifa kutoka asilimia 4 hadi 5 kufikia Juni 2031 | 1.1 | Kuimarisha mifumo ya udhibiti inayohusiana na maendeleo ya ardhi na miji, ili kuchochea maendeleo ya soko la majengo na ardhi, ifikapo mwaka 2028. | | | | | |
| | 1.2 | Kuanzisha mfumo wa motisha kwa waendelezaji wa majengo na ardhi wanaowekeza katika miradi mikubwa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 2. Kuendeleza jumla ya nyumba milioni 2 ili kukidhi ongezeko la idadi ya watu mijini, kufikia Juni 2031 | 2.1 | Kuanzisha na kuhamasisha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuongeza ugavi wa nyumba nafuu chini ya Mpango wa Nyumba Nafuu Tanzania (TAHP), kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. | Kuanzisha mfumo wa motisha kwa nyumba zinazojengwa za utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. | Kuanzisha vituo mseto vya mijini vinavyounganisha makazi, biashara, na burudani, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 2.2 | Kuendeleza teknolojia za ujenziendelevu na za gharama nafuu, ili kuharakisha ujenzi na kupunguza gharama, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. | Kuwezesha uhawilishaji wa wa teknolojia na uendelezaji wa ujuzi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. | Kutoa motisha kwa wazalishaji wa ndani wa vifaa vya ujenzi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kuongeza Uwiano wa dhamana kwa Pato la Taifa kutoka asilimia 0.5 hadi 2, kufikia Juni 2031 | 3.1 | Kuanzisha na kuendesha dirisha/taasisi za fedha za nyumba kama TMRC/TIB zenye angalau Shilingi bilioni 100 za kitanzania, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 3.2 | Kufanya marekebisho ya udhibiti ili | | | | | |

| Shabaha | | Afua | | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | | | kupunguza viwango vya riba ya mikopo ya nyumba kutoka wastani wa asilimia 15 hadi asilimia 12, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | | 3.3 | Kuanzisha na kuwezesha upatikanaji wa ardhi zenye huduma kwa waendelezaji binafsi na umma maeneo ya miji na pembezoni mwa miji, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | | 3.4 | Kuanzisha na kuhuisha benki za ardhi (land banks) kwa ajili ya kuendeleza miradi ya majengo na ardhi (real estate), kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | | 3.5 | Kuendeleza miundombinu na huduma za kijamii kwa ardhi iliyopimwa kwa ajili ya miradi, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| 4. | Uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs), Miji ya Kisasa Kongani za biashara za kimataifa na vitovu vya usafirishaji, kufikia jumla ya dola za Marekani bilioni 3, kufikia Juni 2031 | 4.1 | Kuanzisha miji ya kisasa mitatu (3) yenye mpango wa kujiendesha kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya usimamizi wa miji kwa ufanisi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | | i. | Kusanifu miji ya kisasa ifikapo mwaka 2028 | | | | | |
| | | ii. | Miundombinu ya kiteknolojia inayohitajika kwa ajili ya miji ya kisasa kukamilishwa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 5. | Kuongezeka kwa thamani ya jumla ya mali zinazosimamiwa na REIT na TAHF kufikia dola za Marekani bilioni 1.5, kufikia Juni 2031. | 5.1 | Kuongeza wigo wa Masoko ya mitaji kwa kuorodheshwa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja katika Majengo (REITs) na Mpango wa Nyumba Nafuu Tanzania (TAHP) kwenye soko la hisa la Dar es salaam kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | | 5.2 | Kufadhiliwa kwa nyumba za gharama nafuu kupitia mipango mahsusi na mipango bora ya usimamizi kupitia REITs na TAHP, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | | 5.3 | Kuanzishwa kwa maendeleo yanayozingatia Usafiri wa Umma kwa kujumuisha upangaji wa matumizi mchanganyiko ya ardhi na mifumo bora ya usafiri wa umma, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | | 5.4 | Kuandaa mpango wa usimamizi wa ToD, zana, na mbinu za ufadhili, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | | 5.5 | Kuanzisha miundombinu ya kidijitali ili kuwezesha ulinzi kwa rehani za kielektroniki uhamishaji wa mali kidijitali, na mifumo ya mipango miji | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | inayoongozwa na teknolojia ya akili unde, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| 6. Jumla ya asilima 50ya miamala ya majengo na ardhi kufanyika kidijitali, kufikia mwaka 2030 | 6.1 Kuanzisha mfumo rafiki wa usajili wa mali kwa watu wasio raia, kupitia mageuzi ya sheria za udhibiti, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 6.2 Kutekeleza mikakati ya usimamizi wa majengo na ardhi inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, ikijumuisha kanuni za ujenzi na viwango, ili kuimarisha uendelevu katika ujenzi, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuanzisha viwango vya usanifu na vifaa vya ujenzi vinavyostahimili mabadiliko ya tabianchi , kufikia Juni 2027 | | | | | |
| | iii. Kupitishwa kwa kanuni za ujenzi unaostahimili mabadiliko ya tabianchi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **Lengo 2: Uboreshaji wa nyumba na makazi ya watu unaolenga kuinua hali ya maisha na kuleta maendeleo shirikishi ya mijini** | | | | | | |
| 1. Kuongezeka kwa idadi ya watu wanaoishi katika makazi yaliyopangwa kutoka asilimia 30 hadi 50, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kutekeleza mageuzi ya msingi ya kisheria na mageuzi ya kisera za haki za ardhi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kutekeleza mageuzi ya kina ya kisheria, ili kuhakikisha haki za ardhi zilizo wazi, za uwazi, na zinazotekelezeka kwa raia wote, ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana, na makundi ya wanyonge, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | ii. Kuoanisha mifumo ya kisheria, kimila, na kidini, ya umiliki wa ardhi, ili kuhakikisha ulinzi na utambuzi sawa wa haki za ardhi kufikia Juni 2029 | | | | | |
| | iii. Kuimarisha utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa haki na ufanisi, kila mwaka | | | | | |
| | 1.2. Kusasisha mifumo ya usimamizi wa ardhi na michakato yake, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuzindua Mfumo Jumuishi wa Taarifa za Ardhi wa Taifa, ambao unajumuisha taarifa za ramani, na mipango miji kufikia Juni 2029 | | | | | |
| | ii. Kurahisisha na kuhamishia madaraka ya utoaji hati za ardhi ngazi za chini ili kupunguza muda, gharama na urasimu, na hivyo kufanya urasimishaji wa ardhi kupatikana kwa urahisi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kutumia sekta binafsi katika upimaji, usimamizi wa takwimu na matumizi ya | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | teknolojia katika kuchapusha utoaji wa huduma, kila mwaka | | | | | |
| **3.3.11. Mabadiliko katika Sekta ya Biashara** | | | | | | |
| **Lengo 1:** Kuimarishwa kwa sekta ya biashara yenye ushindani wa kimataifa, iliyosetushwa, inayotumia teknolojia ya kidijitali, inayowezesha mauzo nje, kukuza ukuaji jumuishi kwa viwanda vidogo na vya kati na kuimarisha ushirikiano na masoko muhimu ya kikanda na kimataifa | | | | | | |
| 1. Kuongezeka kwa bidhaa zilizoongezwa thamani katika mauzo ya nje kwa asilimia 10, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha vituo vya usindikaji wa mazao (agro-processing hubs) katika kanda maalum za mauzo ya nje, kupanua mifumo ya umwagiliaji, na kusambaza pembejeo bora kwa wakulima kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 1.2 Kuanzisha vivutio maalum vya kifedha na visivyo vya kifedha na kuboresha upatikanaji wa mikopo ya riba nafuu kwa biashara ndogondogo na za kati zinazoongeza thamani ya mazao kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.3 Kuendesha mafunzo ya kitaifa ya utunzaji wa mazao baada ya kuvuna, na usaidizi kwa vyama vya ushirika katika uwekaji chapa na vifungashio, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.4 Kuzindua mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa kidijitali, majaribio ya *blockchain* kwa mauzo ya nje ya thamani ya juu, na kuongeza majukwaa ya ithibati ya blockchain/IoT kwa ufikiaji mpana wa soko, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 2. Kupunguzwa kwa Kielezo cha Ujumuishaji wa Mauzo ya Nje kwa asilimia 10, kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuzindua jukwaa la usetushaji wa biashara linaloendeshwa na akili unde na kufanya utafiti wa masoko ya mazao yanayouzwa nje, ili kubainisha fursa mpya, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 2.2 Kurasimisha misheni za biashara nje ya nchi kufanyika ana kwa ana na kwa mtandao, ili kuwezesha majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi (bilateral trade), na kutoa motisha kwa bidhaa kupata ithibati na hivyo kurekebishwa kulingana na soko, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kuboreshwa kwa kielezo cha ugumu wa Mauzo ya Nje kufikia 0.04, ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuunganisha akili unde na teknolojia ya roboti katika uzalishaji viwandani na kuanzisha kongani maalum za viwanda kwa ajili nya bioteknolojia, nanoteknolojia na sekta zingine za teknolojia ya juu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 3.2 Kuzindua vituo vya utafiti na maendeleo vya kimtandao, ili kuhamasisha mikataba ya uhawilishaji wa teknolojia na washirika | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | wa kimataifa, na kuwezesha uhusiano na wauzaji bidhaa kwa viwanda vya hali ya juu, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 3.3 Kuongeza wigo wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ili kujielekeza kwenye uzalishaji wa kisasa viwandani na teknolojia ya roboti, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 4. Kuboreshwa kwa kielezo cha ugumu wa Mauzo ya Nje, kufikia 0.04, ifikapo Juni 2031 | 4.1 Kutekeleza mfumo wa forodha unaotegemea teknolojia ya blockchain na kuanzisha malango ya biashara ya kidijitali inayovuka mipaka, ili kupunguza misuguano, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 4.2 Kuoanisha viwango vya kitaifa vya biashara na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na kuandaa sera mahsusi za kurahisisha biashara mipakani, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 4.3 Kuboresha mitandao ya usafiri na usafirishaji kwenda maeneo ya mipakani na kuanzisha kanda za masoko ya mipakani, ili kuchochea biashara ya ndani, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 5. Kuimarishwa kwa Kielezo cha Utendaji wa usafirishaji (LPI) kwa asilimia 10 ili kufikia nafasi ya 50 bora duniani kufikia Juni 2031 | 5.1 Kusasisha miundombinu ya bandari na kuimarisha barabara pamoja na reli muhimu zinazounganisha bandari hizo na bohari za ndani kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | 5.2 Kutekeleza mifumo ya usimamizi wa bandari inayoendeshwa na akili unde na mifumo ya kidijitali, kujenga maghala ya kisasa na kutumia mifumo ya satelite kufuatilia shehena za mizigo, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 5.3 Kuunganisha na kurahisisha michakato yote ya forodha katika maeneo makuu ya biashara ya kuingia na kutoka, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 5.4 Kuanzisha vituo maalum vya mafunzo ya ugavi na usafirishaji, ili kujenga kikosi cha wafanyakazi wenye ujuzi katika mnyororo wa ugavi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 6. Kuongezeka kwa biashara ya kidijitali kuongezeka na kufikia asilimia 50 ya biashara yote, kufikia Juni 2031 | 6.1 Kuanzisha na kuzindua majukwaa ya biashara ya kielektroniki yanayoendeshwa na akili unde kwa soko la Afrika na kuanzisha mfumo wa malipo ya kidijitali wa *blockchain* kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 6.2 Kutekeleza suluhu za usafirishaji za IoT (kwa uwasilishaji wa maili ya mwisho na uanzishwaji wa vituo vya kikanda vya | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | biashara mtandao , ili kuboresha ufanisi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 6.3 Kuoanisha kanuni za kitaifa za biashara-mtandao kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **3.3.12 Sekta Imara ya Biashara** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuongezeka kwa uwekezaji wa sekta binafsi kunakoibua ubunifu, ushindani, na ushirikishwaji; kukidhi mahitaji ya ndani; na kuunganisha Tanzania katika minyororo ya thamani ya kimataifa ili kusaidia ukuaji wa uchumi endelevu** | | | | | | |
| 1. Kuongezeka kwa uwekezaji binafsi hadi kufikia angalau asilimia 5 ya pato la taifa, kufikia mwaka | 1.1 Kuweka mfumo thabiti wa utoaji wa motisha na usaidizi unaolengwa kwa wawekezaji wa kimkakati, uanzishaji wa teknolojia ya juu na biashara za kidijitali ili kukuza ubunifu, ujasiriamali na miundo ya biashara inayotegemea teknolojia, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Uhakiki wa kina wa kanuni za biashara ili kuboresha urahisi wa kufanya biashara kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | ii. Kupitia mifumo ya udhibiti ya Mashirika ya Umma ili kuhakikisha uwazi na uwekezaji wenye faida, kufikia mwaka 2029 | | | | | |
| | iii. Kuanzisha mwongozo mahsusi unaozingatia vigezo vya kutoa motisha iliyopangwa kwa uwekezaji wa kimkakati na makampuni chipukizi ya teknolojia ya juu, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | iv. Kurahisisha michakato yote ya uwekezaji na kuimarisha uwezo wa mashirika ya kukuza uwekezaji kutatua migogoro, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | v. Kuwezesha ukuaji wa viwanda unaotegemea kongani na uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | vi. Kuongeza wigo wa huduma za kifedha na kuboresha miundombinu inayosaidia ukuaji wa biashara, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 2. Kuongezeka kwa ushiriki katika mnyororo wa thamani wa kidunia hadi angalau asilimia 25 ya pato la taifa, kufikia mwaka 2030 | 2.1 Kutekeleza mabadiliko ya kimkakati ya kubadilisha uzalishaji wa ndani kuwa viwanda Shindani, vinavyolenga mauzo ya nje, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kutekeleza programu ya kitaifa ya kuunganisha viwanda vidogo na vya kati vya ndani na kampuni kubwa za kimataifa ili kuongeza ushiriki kwenye mnyororo wa thamani, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | ii. Kutumia nafasi ya Kijiografia ya Kimkakati ili kuunganishwa kwa ufanisi zaidi na masoko ya kikanda na kimataifa, kila mwaka | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | iii. Kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa kuwezesha biashara kuinufaisha Tanzania kutokana na eneo lake la kijiografia kwa kuunganishwa vyema na masoko ya kikanda na kimataifa, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | iv. Kutoa kipaumbele kwa maendeleo ya sekta za kimkakati (k.m., usindikaji wa mazao ya kilimo, uzalishaji mdogo viwandani) kwa ajili ya mabadiliko ya kimuundo na mwelekeo wa kuuza nje, kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| 3. Kudumisha kiwango cha chini cha mgao wa Gini na tofauti za kijiografia katika viwango vya sasa kufikia mwaka 2030 | 3.1 Kuimarisha sera za kifedha za usambazaji upya ikijumuisha kodi shirikishi na programu za ulinzi wa jamii zinazolengwa, kila mwaka | | | | | |
| | 3.2 Kuweka kipaumbele kwenye viwanda vinavyotumia nguvu kazi kubwa na usindikaji wa mazao ya kilimo katika maeneo ya vijijini na nusu-miji ili kutengeneza ajira kwa wingi, kila mwaka | | | | | |
| | 3.3 Kuwekeza katika usafirishaji, nishati, na miundombinu ya kidijitali katika mikoa yote ili kupunguza tofauti kati ya miji na vijiji, kila mwaka | | | | | |
| | 3.4 Kuhakikisha ubia na ushiriki wa lazima wa hisa za ndani katika miradi mikubwa ya uwekezaji wa kigeni uwekezaji wa moja kwa moja wa nje (FDI), kila mwaka | | | | | |

**3.3.13 Kuweka Mikakati ya Ushirikiano baina ya Nchi Mbili, Kikanda na Kimataifa katika Ulimwengu wa Mabadiliko**

**Lengo 1: Kuimarishwa kwa uwezo wa nchi kukuza maslahi ya kiuchumi na kuinua ushawishi wa Tanzania duniani, kuchangia maendeleo endelevu na ushirikiano imara wa kimataifa**

| Shabaha | Afua | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Kutekeleza kikamilifu diplomasia ya uchumi, ili kuongeza ukuaji wa uwekezaji kwa asilimia 40, kufikia mwaka 2030 | 1.1 Kubainisha na kuchapisha vipaumbele vya msingi vya kimkakati na maslahi ya Tanzania katika mawanda ya dunia, kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 1.2 Kuimarisha uwezo wa kitaifa wa majadiliano na kuanzisha mfumo wa habari wa wakati halisi (real-time) kati ya misheni za kidiplomasia na taasisi za ndani kufikia mwaka 2028 | | | | | |
| | 1.3 Kuboresha mfumo wa ajira na miundo ya misheni za kidiplomasia, ili ilenge kwenye matokeo ya kiuchumi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.4 Kuimarisha Kituo cha Mahusiano ya Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, kwa ajili ya kuwajengea uwezo kizazi | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | kijacho cha wanadiplomasia ya kiuchumi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.5 Kuzindua na kutekeleza mkakati wa utambulisho wa kimataifa ili kuboresha taswira ya Tanzania kama kituo cha uwekezaji, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.6 Kupanua upatikanaji wa huduma za kibalozi katika miji ya kiuchumi muhimu na kuimarisha ushirikishwaji wa diaspora ili kuvutia uwekezaji na ujuzi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.7 Kuimarisha ulinzi wa haki miliki (na ushindani kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 1.8 Kuhakikisha ujumuishaji wa masuala ya jinsia na fursa za vijana katika maeneo yote ya ushirikiano wa kimataifa, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| **3.3.14 Mienendo ya Kimataifa (Global Dynamics)** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu imara cha nguvu za kiuchumi, kikanda na kimataifa,ifikapo Juni 2031, kupitia biashara ya kimkakati, uwekezaji na ushirikiano wa kidiplomasia, kuongeza ustahimilivu, ushindani na ustawi endelevu** | | | | | | |
| 1. Tanzania kujumuishwa kikamilifu katika Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, , Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika , kwa kufikia angalau asilimia 70 ya utekelezaji wa itifaki za biashara za kikanda kufikia mwaka 2030 | 1.1 Kukamilisha mahitaji yote ya kuhaulisha sera ya biashara ya kikanda, kuhakikisha mtiririko huru wa bidhaa, huduma na mitaji, na kufikia utekelezaji wa 100% wa itifaki za biashara za kikanda ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuhuisha sera za kitaifa za biashara na forodha kulingana na matakwa ya Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kufikia mwaka 2030 | | | | | |
| | ii. Kukamilisha mikataba yote iliyosalia ya biashara ya pande mbili na ya pande nyingi, inayohusiana na jumuiya za kikanda, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuimarisha uwezo wa taasisi zinazohusika na uratibu masuala ya biashara kitaifa, kila mwaka | | | | | |
| | iv. Kuzindua mfumo jumuishi wa biashara ya kidijitali unaoendeshwa na akili unde , kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | v. Kutekeleza mfumo jumuishi wa forodha unaoendeshwa na teknolojia ya akili katika mipaka yote, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | vi. Kuanzisha dirisha moja la mfumo unaotegemea teknolojia ya kidijitali ya | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | blockchain, ili kurahisisha uwezeshaji wa michakato ya biashara, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 2. Kuimarisha diplomasia ya Tanzania kwa kuingia makubaliano ya ushirikiano wa kimataifa na wadau watatu 3 muhimu, kuongeza matumizi ya Kiswahili katika mashirika 4 ya kimataifa, na kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kazi katika angalau taasisi moja ya kimataifa iliyoendelea, ifikapo mwaka 2030 | 2.1 Kuimarisha ushawishi wa kidiplomasia wa Tanzania katika kupata ushirikiano wa kimataifa na kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kazi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuongeza mtandao wa balozi za Tanzania hadi kufikia nchi 60, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kukuza diplomasia ya kitamaduni na ubadilishanaji wa elimu na nchi 25 na vyuo vikuu 35–40, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kutekeleza huduma ya kutafsiri lugha ya kiswahili katika wakati halisi kupitia teknolojia ya akili unde katika mikutano na nyaraka nyaraka za Umoja wa Afrika, na Umoja wa Mataifa , kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iv. Kuzindua jukwaa la diplomasia ya kidijitali linaloendeshwa na akili unde ili kuongeza ushirikiano wa kimataifa na uchambuzi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | v. Kuanzisha Baraza Maalumu la Biashara ya Kimataifa ili kuendeleza malengo ya diplomasia ya kiuchumi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kuifanya Tanzania kuwa lango kuu la biashara barani Afrika, kwa kufikia TEU milioni 20 (za makontena kwa mwaka, kufikia Juni 2031 | 3.1 Kuitangaza Tanzania ili kuwa lango kuu la biashara, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kukamilisha usasishaji wa bandari za Dar es Salaam, Tanga, na Mtwara na kuzifanya kuwa za kisasa, na kuikamilisha ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuzindua mfumo wa bandari bora unaoendeshwa na akili unde ili kuwezesha bandari kuwa na uwezo wa kufikia malengo ya TEU milioni 20, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kujenga reli na barabara maalum zinazounganisha bandari kuu na vituo vya mizigo vya bara kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iv. Kuanzisha njia ya reli ya mwendokasi ya mizigo, ili kupunguza muda wa safari, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | v. Kutekeleza mfumo unaoendeshwa na AI-wa uboreshaji wa usafirishaji na usambazaji katika bandari zote kuu na njia za usafiri kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | vi. Kujenga mtandao wa kitaifa wa mnyororo wa ugavi, kwa kutumia fursa yateknolojia | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ya IoT, blockchain, na akili unde, ili kuona mwanzo na mwisho wa shehena na kwa ufanisi, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| 4. Kuanzishwa kwa mashirikiano ya uwekezaji kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuvutia uwekezaji kutoka nje (FDI's) katika sekta muhimu, kufikia Juni 2031 | 4.1 Kujadiliana na kuanzisha ushirikiano wa uwekezaji wa nchi na nchi, kikanda na wa kimataifa ili kuvutia Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka nje (FDIs) katika sekta muhimu za kimkakati, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa ushirikiano wa uwekezaji wa pande mbili, kikanda na kimataifa, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | ii. Kuanzisha vitengo vya kukuza ushirikiano wa uwekezaji (Investment Partnership Promotion Units - IPPUs) ndani ya TISEZA na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ili kuratibu na kufuatilia misheni za uwekezaji, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | iii. Kujadiliana na kufikia makubaliano mapya ya pande mbili, kikanda na kimataifa kwa ajili ya uwekezaji wa Moja kwa Moja (FDI) katika sekta za kimkakati, kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | iv. Kuandaa na kuhifadhi orodha ya miradi ya kibiashara inayoweza kukopesheka na yenye matokeo makubwa, kwa ajili ya kuhamaisha uwekezaji kwenye miradi iliyolengwa, kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **3.3.14 Urasimishaji wa Uchumi na Usimamizi Wake** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuifanyia mabadiliko sekta isiyo rasmi kuwa injini ya ukuaji, kuchochea ushiriki wa sekta rasmi, na ukuaji wa uchumi** | | | | | | |
| 1. Mchango wa sekta rasmi katika Pato la Taifa kuongezeka kutoka asilimia 55 hadi 63, kufikia Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha kitengo maalumu ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) cha kukuza na kuendeleza Biashara Ndogo Ndogo na za Kati (MSMEs), kufikia Juni 2027 | | | | | |
| | 1.2 Kuzindua jukwaa la kidijitali, eneo moja la uandikishaji na jukwaa la uzingatiaji wa kodi, kufikia Juni 2028 | | | | | |
| | 1.3 Kuanzisha programu maalumu ya kusaidia kurasimisha biashara zisizo rasmi, kufikia Juni 2029 | | | | | |
| | 1.4 Kuandaa na kutekeleza motisha kwa sekta mahususi kwa lengo la kuwezesha urasimishaji, kufikia Juni 2028 | | | | | |
| | 1.5 Kuingiza biashara zisizo rasmi zilizosajiliwa kwenye minyororo ya ugavi ya sekta rasmi ya serikali na binafsi kupitia programu ya | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | maendeleo ya wasambazaji, kufikia Juni 2030 | | | | | |
| 2. Kupunguza ajira katika sekta isiyo rasmi kutoka asilimia 29 hadi 22, kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuandaliwa kwa programu ya kitaifa kwa ajili ya kuongeza ujuzi na mafunzo ya ufundi, programu hii ni mahususi kwa ajili ya kusaidia wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kupata ujuzi wa kuwawezesha kupata ajira katika sekta rasmi zenye ujuzi wa juu, kufikia mwaka 2027 | | | | | |
| | 2.2 Kutekeleza mpango wa motisha za ajira rasmi kwa biashara zinazoajiri na kuwabakiza wafanyakazi wanaohama kutoka sekta isiyo rasmi, kwa kutoa ruzuku za muda wa mishahara au mikopo ya kodi, kufikia 2030 | | | | | |
| | 2.3 Kuimarisha ukaguzi wa kazi na mifumo ya utekelezaji, ili kuhakikisha viwango vya haki vya kazi, ulinzi wa wafanyakazi, na michango ya usalama wa kijamii, na kufanya ajira rasmi kuwa ya kuvutia zaidi, kila mwaka | | | | | |
| | 2.4 Kuwezesha kuanzishwa kwa ushirika na vyama vya biashara ili kuwezesha wajasiriamali wadogo wa sekta isiyo rasmi kuunganisha rasilimali, kupata masoko makubwa, na kurasimishwa kwa pamoja, kila mwaka | | | | | |

| **Shabaha** | **Afua** | **Mpango wa Maendeleo wa Mwaka** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** |
| **3.4. Kujenga Uwezo wa Binadamu na Maendeleo ya Jamii** | | | | | | |
| **3.4.1. Jamii iliyoelimika, yenye ujuzi na inayojifunza** | | | | | | |
| **Lengo 1:** Kuwa na jamii iliyoelimika, yenye ujuzi na inayojifunza kwa kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu bora, jumuishi na mafunzo endelevu ya ujuzi. | | | | | | |
| 1. Kuongeza uwiano wa wasichana na wavulana wanaopata malezi na makuzi bora ututoni kwa asilimia 20 na udahili elimu bora ya awali kutoka asilimia 88.8 hadi 96.7 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuongeza upatikanaji na ubora wa miundombinu ya vituo vya malezi na maendeleo ya mtoto na elimu ya awali ili kuwajengea msingi bora na kuwaandaa tayari kwa elimu ya msingi | | | | | |
| | i. Malezi na elimu ya awali kwa watoto kuwa ya lazima na mfumo wa uandikishaji kuimarishwa kupitia utambuzi katika ngazi ya jamii kitaifa. | | | | | |
| | ii. Kuhakikisha angalau asilimia 20 ya watoto wenye umri wa miaka 3–4 wanapata huduma za malezi na makuzi katika vituo bora vya maendeleo ya awali ya mtoto. | | | | | |
| | 1.2 Kuhakikisha upatikanaji wa walimu wenye sifa na ujuzi, miundombinu rafiki na rasilimali za kujifunzia kwa watoto zinazozingatia umri pamoja na huduma za WASH, ifikapo 2031 | | | | | |
| | i. Kuhakikisha upatikanaji wa walezi na walimu wenye sifa na ujuzi na usawa katika ugawaji wa rasilimali za kufundishia na kujifunzia zinazozingatia umri stahiki katika shule zote za awali, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuandaa programu maalumu za mafunzo kwa walezi na walimu wote wa vituo vya malezi, makuzi na madarasa ya awali, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuimarisha ujuzi wa walimu kupitia mafunzo endelevu kazini ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.3. Kujumuisha huduma za maendeleo ya mtoto katika sekta za elimu, afya na lishe ili kuhakikisha maendeleo jumuishi ya awali kwa mtoto, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha uratibu wa kisekta kuanzia ngazi ya taifa hadi jamii ili kuwa na | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | utekelezaji shirikishi wa programu za malezi, elimu, afya na lishe . | | | | | |
| | ii. Kuboresha na kusimamia utekelezaji wa viwango vya ubora wa huduma za maendeleo ya awali ya mtoto kwa kutumia miongozo inayokidhi matarajio ya jamii, taifa na kimataifa, ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| 2. Kuongeza uwiano wa wanafunzi wanaopata elimu bora kwa usawa katika shule za msingi kutoka asilimia 98.2 hadi 100 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kupunguza uwiano kati ya wanafunzi na mwalimu na kuimarisha ubora wa walimu katika shule za msingi | | | | | |
| | i. Kuboresha upatikanaji wa walimu, hususan wa masomo ya STEM na lugha ya Kiingereza, pamoja na kuhakikisha ufanisi wa matumizi ya walimu waliopo . | | | | | |
| | ii. Kuimarisha ubora wa walimu kupitia utekelezaji wa programu endelevu za maendeleo ya taaluma (CPD) zinazozingatia mbinu bunifu za ufundishaji na teknolojia za kisasa | | | | | |
| | 2.2 Kuinua ubora wa ufundishaji na mazingira ya kujifunzia katika shule za msingi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha na kuwezesha vituo vya mafunzo kwa lengo la kuendeleza kada ya ualimu. | | | | | |
| | ii. Kuimarisha upatikanaji wa elimu bora na usawa kwa shule za msingi kupunguza utoro, kukatisha masomo, kuinua uhitimu, ufanisi wa matokeo ya kujifunza, na kiwango cha wanafunzi wanaovuka kuingia ngazi ya elimu ya sekondari | | | | | |
| | iii. Kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za kufundishia na kujifunzia ili kufikia uwiano wa kitaifa wa mwalimu kwa wanafunzi wa 1:40, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.3 Kuimarisha ujumuishi na ushiriki wa jamii katika maendeleo ya elimu ya msingi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha mifumo ya utambuzi na tathmini ya mahitaji maalum ya wanafunzi | | | | | |
| | ii. Kuimarisha uwezo wa walimu wa shule za msingi za elimu maalum na jumuishi. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | iii. Kuimarisha ushiriki wa jamii katika kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo ya shule. | | | | | |
| | iv. Kuimarisha stadi msingi za kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na matokeo ya ujifunzaji, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.4. Kuanzisha mfumo maalum wa walimu wa shule za msingi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata elimu bora kwa usawa katika shule za sekondari kutoka asilimia 75.3 kufikia asilimia 100 sanjari na kuongeza upatikanaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kutoka asilimia 4 hadi 30 ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuajiri na kudumisha walimu wenye sifa na ujuzi maalum, hususan wa masomo ya STEM na lugha kila mwaka | | | | | |
| | 3.2 Kuimarisha mfumo wa idhibati na utoaji wa leseni, kwa kuuhusisha na ujuzi wa ufundishaji wa masomo mahsusi, umahiri na ufanisi **ifikapo Juni 2031.** | | | | | |
| | 3.3 Kusasisha mazingira kufundishia ujifunzaji katika shule za sekondari, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule za sekondari ili kuendana na mahitaji ya kisasa, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha na kuwezesha vituo vya mafunzo ya walimu kwa kuvipatia vifaa na teknolojia inayohitajika kwa maendeleo ya kitaaluma, kila mwaka | | | | | |
| | 3.4 Kupanua na kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET), ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuboresha na kuongeza miundombinu ya mafunzo ya amali katika shule za sekondari , kila mmwaka | | | | | |
| | ii. Kuimarisha ushirikiano wa shule na shughuli za viwanda ili kuimarisha upatikanaji wa mafunzo kwa vitendo, uanagenzi na programu za kukuza ujuzi, kila mwaka | | | | | |
| | iii. Kuweka maabara na maeneo maalumu ya kulea ubunifu (maker spaces) yenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya shughuli za STEM na TVET. | | | | | |
| | 3.5 Kuimarisha Elimu Bora na Jumuishi ya Sekondari, ifikapo Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | i. Kuimarisha mifumo wa kubaini na kutathmini mahitaji maalum ya kila mwanafunzi wa sekondari kila mwaka. | | | | | |
| | ii. Kuboresha umahiri wa walimu wa sekondari wa elimu maalumu na elimu jumuishi, kila mwaka | | | | | |
| 4. Kuongeza kiwango cha wanafunzi wa wanaoendelea na elimu ya sekondari ya juu hadi angalau kufikia asilimia 30 ifikapo Juni 2031 . | 4.1 Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Juu pamoja na kuboresha miundombinu, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kujenga na kuboresha vyuo vikuu, vyuo vya ufundi na vituo huria vya kujifunzia katika mikoa yote, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuongeza upatikanaji wa elimu ya juu kupitia programu za kujifunzia kwa masafa, mtandaoni na mifumo huria ya elimu, kila mwaka | | | | | |
| | 4.2 Kuwianisha mitaala ya elimu ya juu na mahitaji ya sekta ya viwanda, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kutekeleza utaratibu shirikishi wa mapitio ya mitaala kujibu mahitaji ya sekta ya viwanda na mabadiliko ya teknolojia kwa kukushauriana ya wadau\, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu na sekta ya viwanda kwa ajili ya kuimarisha upatikanji wa mafunzo kwa vitendo na ajira kwa wahitimu, kila mwaka | | | | | |
| | iii. Kukuza vituo vya ubunifu na viatamizi vinavyoungwa mkono na wadau wa sekta ya viwanda, kila mwaka | | | | | |
| | 4.3 Kutumia diplomasia ya uchumi kuimarisha fursa na ubora wa elimu ya juu, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kukuza ushirikiano wa kimataifa katika elimu kupitia programu za udhamini, ubadilishanaji wa wanafunzi na utafiti wa pamoja, kila mwaka | | | | | |
| 5. Kufikia angalau asilimia 50 ya nguvu kazi yenye ujuzi wa kidijitali ifikapo Juni 2031 | 5.1 Kuweka mfumo endelevu wa ujifunzaji wa kidijitali na elimu kwa masafa, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha mifumo ya ujifunzaji mitandaoni ili kupanua fursa ya elimu kwa watu wazima na mafunzo ya ujuzi, kila mwaka | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ii. Kukuza ubunifu katika utengenezaji wa maudhui ya kidijitali, programu za simu na mifumo ya ujifunzaji, kila mwaka | | | | | |
| | 5.2 Kuimarisha mazingira ya utafiti na uvumbuzi wa teknolojia, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuweka mifumo ya udhibiti inayowezesha matumizi salama ya teknolojia mpya kwa kuzingatia maadili na faragha, ifikapo m waka 2028 . | | | | | |
| | ii. Kuongeza uwekezaji katika utafiti wa teknolojia zinazoibukia kama akili mneemba (AI), bioteknolojia na sayansi ya mazingira, kikla mwaka | | | | | |
| | 5.3 Kukuza fursa za ujifunzaji endelevu na ubunifu, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kupanua vituo vya ujifunzaji kwa watu wazima vinavyozingatia stadi za msingi, ujuzi wa kidijitali na mbinu sdadi za maisha, kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kujenga mfumo thabiti wa ubunifu nchini kwa ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu, viwanda, na serikali, ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **3.4.2 Nguvukazi watu Yenye Uwezo na Ari** | | | | | | |
| **Lengo 1: Kuwa na nguvu kazi yenye uwezo na ari ya kazi, ili kuongeza tija na ubunifu** | | | | | | |
| 1. kuongezeka kwa nguvukazi watu yenye ujuzi, ufundi na utaalamu unaohusiana na ubunifu wa viwandani kufikia angalau asilimia 35 ya jumla ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuwianisha maendeleo ya ujuzi nchini na viwango vya kimataifa | | | | | |
| | i. Kupitia na kuhuisha mitaala ya TVET kuendana na viwango vya kimataifa na mabadiliko ya mahitaji ya soko la ajira, ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | ii. Kuwianisha na viwango vya kimataifa vya ujuzi katika sera za elimu, mafunzo na ajira, kila mwaka | | | | | |
| | 1.2 Kuongeza usawa katika upatikanaji wa huduma za TVET, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kupanua vituo vya TVET hususan katika maeneo ya vijijini na maeneo yenye upungufu wa huduma . | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ii. Kuendeleza na kutekeleza mitaala, miundombinu, na mbinu za kufundishia zinazozingatia jinsia na ushirikishwaji ifikapo Juni 2028 | | | | | |
| | 1.3 Kuimarisha mfumo wa ujifunzaji na utambuzi endelevu wa ujuzi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa utambuzi wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi, ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| | ii. Kuimarisha mfumo wa ujifunzaji kwa watu wazima kupitia programu za kila mwaka zinazokuza njia wazi za kazi na utambuzi wa ujuzi. | | | | | |
| 2. Kiwango cha nguvukazi watu yenye ujuzi wa kidijitali kufikia angalau asilimia 50 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuboresha miundombinu ya TVET na kuwa ya kisasa pamoja na muundo wa ufadhili, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kukuza ushirikiano wa uwekezaji wa ubia wa maendeleo ya TVET kati ya sekta za umma na binafsi (PPP), kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kuvipatia vituo vya mafunzo zana za kisasa, maabara, na mazingira ya kujifunzia ya kidijitali, kila mwaka | | | | | |
| | 2.2 Kukuza ujuzi wa msingi kwa maendeleo ya uchumi wa kidijitali, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya kijamii vya ubunifu wa kidijitali vijijini na mijini kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | ii. Kujumuisha umahiri wa kidijitali katika programu zote za mafunzo na elimu endelevu, ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| 3. Kuongeza kiwango cha nguvukazi watu yenye ujuzi, hususan katika teknolojia, uhandisi na uchambuzi wa taarifa ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuimarisha programu za mafunzo kwa vitendo na mafunzo kazini, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuimarisha programu za mafunzo kwa vitendo kwa kushirikiana na waajiri katika sekta za ubunifu na viwanda, kilka mwaka | | | | | |
| | ii. Kuhalalisha mfumo wa utambuzi wa uzoefu, mafunzo kwa vitendo na programu za uanagenzi katika utoaji wa vyeti na sifa za kitaifa, ifikapo Juni 2029 | | | | | |

**3.4.3 Kusimamia na Kuitumia Fursa ya Kidemografia**

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **Lengo la 2:** Kuhakikisha Tanzania inanufaika na fursa ya kidemografia kupitia maendeleo ya rasilimali watu, ajira zenye staha, ujasiriamali, maendeleo ya biashara, na uwezeshaji kiuchumi ili kuwa na ukuaji wa uchumi jumuishi na kuboresha maisha. | | | | | | |
| 1. Kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana wa umri wa kati ya miaka 15–34 kutoka asilimia 21.5 hadi 19.3 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuwianisha elimu na ujuzi unaotolewa na mahitaji ya soko la ajira, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kushirikisha sekta binafsi katika kubaini ujuzi unaohitajika katika sekta za uzalishaji na utoaji wa huduma kwa mitaala ya mafunzo, kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kujumuisha ujuzi, teknolojia zinazoibukia na stadi za maisha katika mitaala ya elimu, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kukuza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuingiza teknolojia mpya na ujuzi mahsusi wa kisekta katika programu za kukuza ujuzi, kila mwaka | | | | | |
| | 1.2 Kuimarisha usawa wa jinsia katika elimu na ajira, ifikapo ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kujenga na kuzipatia vifaa shule za wasichana husus an zilizo katika maeneo ya pembezoni sanjari na kuhamasisha ushiriki wa wasichana katika masomo ya STEM na ufundi, kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kuwezesha huduma za malezi ya watoto na kuhamasisha mazingira rafiki katika familia na maeneo ya kazi, ikiwa ni pamoja na kuogeza utekelezaji wa sera za usawa kwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi na shughuli kubwa za uchumi, kikla mwaka | | | | | |
| | 1.3 Kukuza ujasiriamali na ubunifu kwa Vijana, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya ubunifu na viatamizi kwa vijana, kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kutoa huduma jumuishi za maendeleo ya biashara ikiwemo fedha na masoko, kila mwaka | | | | | |
| | 1.4 Kukuza fursa za uchumi wa kidijitali na na ajira za mtandaoni, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha mifumo ya kuunganisha vijana na ajira za kidijitali, kila mwaka | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ii. Kuwajengea vijana ujuzi wa kujitangaza na kusimamia kazi za kujiajiri, kila mwaka | | | | | |
| | 1.5 Kuimarisha kasi ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuweka mfumo wa vivutio unaozingatia ufanisi wa utendaji na taratibu zitakazochochea kasi ya urasimishaji wa biashara na kupunguza mzigo kwa wafanyabiashara kufikia 2028 | | | | | |
| | 1.6 Kuwajumuisha Diaspora katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo, kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuweka vivutio kwa wataalamu wa Kitanzania walioko nje kurejea au kuchangia katika sekta za afya, elimu na teknolojia, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kukuza ushirikiano wa kitaaluma na utafiti kati ya diaspora na taasisi za utafiti za ndani, kila mwaka | | | | | |
| 2. Kiwango cha utegemezi kutoka asilimia 87.4 hadi 79.4 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuongeza upatikanaji wa huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuongeza upatikanaji wa huduma rafiki za afya ya uzazi, mafunzo ya stadi za maisha na elimu kwa vijana, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kujumuisha elimu ya afya ya uzazi katika mitaala ya elimu, kila mwaka | | | | | |
| 3. Angalau asilimia 20 ya wazee wa zaidi ya miaka 60 kufikiwa kikamilifu na mpango wa hifadhi ya jamii ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na uchumi jumuishi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuongeza mafao ya uzeeni na programu zisizohitaji michango, hususan kwa wazee wenye kipato cha chini katika sekta isiyo rasmi kila mwaka. | | | | | |
| | ii. Kuwezesha ujasiriamali kwa wazee kupitia mikopo na mafunzo, kila mwaka | | | | | |
| | 3.2 Kuimarisha mifumo ya malezi ya wazee ya kijamii, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kupeleka maafisa ustawi wa jamii katika ngazi ya wilaya na kata kwa ajili ya kuwasaidia wazee na walezi, kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kutambua na kuongeza mbinu za jadi/kijamii zilizobora za kuhudumia wazee sanjari na kutoa mafunzo ya utunzaji wa | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | wazee kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kila mwaka | | | | | |
| | 3.3 Kuimarisha huduma za dharura kwa wazee, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha mifumo ya kutoa tahadhari mapema kwa kuzingatia mahitaji na mawasiliano ya wazee na kuhusisha viongozi wa jamii na maafisa ustawi kusambaza taarifa wakati wa dharura, kila mwaka | | | | | |
| **3.4.4 Soko la Ajira na Mazingira ya Kazi** | | | | | | |
| **Lengo la 3:** Kusasisha mfumo wa soko la ajira la Tanzania ili kuongeza nafasi za ajira zenye staha na kujenga nguvukazi watu iliyo tayari na ari kwa mustakabali wa baadae. | | | | | | |
| 1. Angalau ajira milioni 8 zenye staha kupatikana kupitia uwekezaji na ubunifu ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuimarisha mazingira ya biashara ilikuruhusu ukuaji wa biashara ndogo, za kati (SMEs) na ubunifu (startups), ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha vituo vya kitaifa vya ubunifu vinavyotoa malezi ya biashara, ufadhili na miundombinu ya kazi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kukuza uwekezaji katika utafiti na maendeleo (R&D), ubadilishanaji wa teknolojia na ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya upatikanaji wa masoko, kila mwaka | | | | | |
| | iii. Kuvutia uwekezaji mkubwa unaozalisha ajira, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | iv. Kutekeleza kampeni mahsusi za kuvutia uwekezaji kutoka makampuni makubwa ya ndani na kimataifa. | | | | | |
| | v. Kuendeleza maeneo maalum ya kiuchumi na viwanda yaliyo vibali na miundombinu iliyotayari kuwezesha shughuli za viwanda kuanza uzalishaji moja kwa moja na kutoa ajira kutokana na biashara mpya zitakazoanzishwa, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | vi. Kuimarisha ukuaji na urasimishaji wa biashara, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | vii. Kutoa huduma za kifedha na kiufundi kwa SMEs zenye uwezo wa kukua, kila mwaka | | | | | |
| | viii. Kutekeleza vivutio kuwezesha urasimishaji wa biashara, ifikapo Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| 2. Ajira katika sekta za umma na shughuli za viwanda zenye thamani kuongezeka kwa angalau asilimia 10 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuanzisha na kufungamanisha utoaji wa mafunzo ya ujuzi na mahitaji ya viwanda vya kisekta, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuanzisha programu za ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi zinazolenga kukuza upatikanaji wa mafunzo kwa vitendo ya teknolojia mpya, nishati safi na viwanda vya thamani, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha vituo vya mafunzo vyenye teknolojia za kisasa, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.2 Kukuza uwekezaji katika shughuli za viwanda, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kutoa vivutio maalum vya kifedha na visivyo vya kifedha ili kuvutia na kudumisha uendelevu wa uwekezaji katika sekta zenye thamani ya juu kama vile: teknolojia, viwanda vya dawa, na viwanda thamani ya juu, kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kukuza ushirikiano kati ya makampuni ya kimataifa, *startups* za ndani na SMEs ili kuwaunganisha katika minyororo ya thamani ya kimataifa na kutengeneza ajira zinazohitaji ujuzi wa juu, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| **3.4.5 Jamii jumuishi na iliyolindwa** | | | | | | |
| **Lengo la 1:** Kuongeza wigo wa jamii jumuishi iliyolindwa kwa kuongeza shughuli za hifadhi ya jamii ili kupunguza vihatarishi na kuhakikisha usawa wa fursa kwa makundi yote. | | | | | | |
| 1. Kuhakikisha angalau asilimia 40 ya watu walio katika mazingira hatarishi wanafikiwa na kulindwa ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kutekeleza sheria zinazolinda usawa na kupinga ubaguzi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuimarisha uwezo wa taasisi za udhibiti, urekebu, wakaguzi wa kazi, na mahakama kusimamia sheria zinazokataza ubaguzi kijinsia, umri, ulemavu au kabila, kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kujumuisha mbinu sahihi kimataifa katika mfumo wa kitaifa, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.2 Kuhakikisha upatikanaji sawa wa ardhi kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kutekeleza sera za mageuzi ya usimamizi wa ardhi kuwezesha umiliki sawa kwa wanawake na watu wenye ulemavu, kila mwaka | | | | | |

| **Shabaha** | **Afua** | **Mpango wa Maendeleo wa Mwaka** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** |
| | ii. Kukuza programu za umilikishaji ardhi na kuimarisha vituo vya pamoja vya utoaji huduma kwenye maeneo yasiyofikika na yasiyo na huduma ili kuwainua wanachi kiuchumi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.3 Kujumuisha sekta isiyo rasmi katika mifumo ya hifadhi ya jamii, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kutekeleza mifumo ya usajili wa kidijitali iliyorahisishwa kwa uandikishaji wa wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi kila mwaka. | | | | | |
| | ii. Kuhuisha mifumo ya kitaifa ya hifadhi ya jamii ili kufikia wafanyakazi wote wa sekta isiyo rasmi, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.4. Kuboresha na kuimarisha programu za hifadhi ya jamii, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kupitia na kuboresha Programu za TASAF na PSSN ili ziweze kutumia daftari la kidijitali kuhifadhi kumbukumbu za walengwa, kuboresha ufuatiliaji, na kupunguza utegemezi wa wafadhili ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kujumuisha vipengele vya ujuzi na kipato katika programu za hifadhi ya jamii ili kuwawezesha walengwa kujitoa katika umaskini, kila mwaka | | | | | |
| | iii. Kujenga uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa katika kusimamia utoaji wa hifadhi ya jamii kwa ufanisi, ifikapo mwaka 2028 | | | | | |
| | iv. Kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji wa hifadhi ya jamii, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.5. Kujumuisha mafunzo ya afya ya akili katika elimu na huduma za jamii, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kujumuisha elimu ya afya ya akili katika mitaala yote ya elimu, ifikapo mwaka 2028 | | | | | |
| | ii. Kuongeza moduli za afya ya akili katika mafunzo ya walimu na programu za maendeleo ya kitaaluma, kila mwaka | | | | | |
| | iii. Kuimarisha mazingira ya shule na jamii yanayokuza ustawi,kupunguza unyanyapaa na kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya ya akili | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **3.4.6. Kuboresha huduma ya afya kwa wote** | | | | | | |
| **Lengo la 1:** Kuboresha afya ya wananchi, ili kuongeza tija, na kupunguza tofauti katika upatikanaji wa huduma za afya. | | | | | | |
| 1. Vifo vya watoto wachanga kupungua kutoka 43 hadi 27 kwa vizazi hai 1,000 ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuimarisha Huduma za Afya ya mama na mtoto mchanga, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuajiri, kutoa mafunzo na kupeleka wakunga wenye ujuzi katika vituo vyote vya afya ili kufikia asilimia 90 ya upatikanaji ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kuweka vifaa muhimu vya uchunguzi na dawa katika vituo vya ANC na PNC, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kuondoa gharama za moja kwa moja za huduma za ANC na PNC kwa wanawake wanaoishi katika maeneo yasiyofikika kirahisi, ya kipoto cha chini na wanaoishi katika mazingira hatarishi, ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| | iv. Kuimarisha kliniki zinazotembea za huduma za ANC/PNC kufikia jamii za wafugaji zinazoishi katika maeneo yasiyofikika, kila mwaka | | | | | |
| | 1.2. Kutekeleza Programu za Lishe kitaifa kwa akina mama na watoto, kikla mwaka | | | | | |
| | i. Kuongeza upatikanaji wa vyakula vilivyoongezewa virutubisho kwa watoto wenye umri wa miezi 6–24, kila m waka | | | | | |
| | ii. Kuhakikisha utoaji wa kirutubisho cha vitamini A na dawa za minyoo kwa watoto chini ya miaka 5, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kusambaza virutubisho kwa watoto wadogo, kila mwaka | | | | | |
| | iv. Kuimarisha kliniki zinazotembea za ANC/PNC ili kufikia jamii za mbali na wafugaji wanaohama, kila mwaka. | | | | | |
| | 1.3. Kuimarisha mfumo wa mafunzo ya taratibu za utoaji lishe kwa watoto wadogo na wachanga, Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kuwaandaa na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili waweze kutoa mafunzo ya taratibu za | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | unyonyeshaji katika ngazi ya jamii, kila mwaka | | | | | |
| | ii. Kutekeleza utoaji elimu ya unyonyeshaji kwa wanaume ili kuongeza ushiriki wao. | | | | | |
| | 1.4. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya ya mama na mtoto ngazi ya jamii, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | i. Kutoa mafunzo kwa angalau asilimia 50 ya wahudumu wa afya katika huduma za mama na mtoto ngazi ya jamii, yakilenga elimu ya afya ya akili na saikolojia, ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.4. Kujumuisha elimu ya masuala ya tabianchi katika ngazi zote za mitaala ya kitaifa na kuandaa Viwango vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET) - ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| 2. Kupunguza uzalishaji wa gesi joto (GHG) kwa asilimia 30–35 na kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika umeme wa taifa kufikia asilimia 75 ifikapo Juni 2031. | 2.1. Kuongeza nishati safi ya kupikia kwa angalau asilimia 50 ya kaya na kutekeleza programu za matumizi ubora wa nishati ili kupunguza matumizi ya nishati kwa asilimia 10 katika sekta muhimu ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 2.2. Kuongeza nishati mbadala kwa kuongeza uwezo wa kuzalisha MW 500-700 za uwezo mpya na kusambaza umeme kwa 30% ya kaya zisizo kwenye gridi ya taifa kupitia mifumo ya jua ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kuanziasha hudumaza usafiri waumma ulio rafiki kwa mazingirakwa kuanzisha mabasi 200 ya umeme na miundombinu/vituo vya kuongezea umeme katika miji mikubwa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.4. Anzisha soko la kaboni lenye mfumo wa kupanga bei na wa kuwezesha mauziano ya viwango vya uchafuzi (Emissions Trading System (ETS)) ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kukabiliana na hasara na uharibifu (Loss and Damage) ifikapo Juni 2031 | 3.1. Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa hasara na uharibifu kwa ajili ya kuratibu maandalizi, urejeshwaji na fedha za kukabiliana na athari za tabianchi zisizoweza kuepukika ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.2. Kuimarisha na kupanua mifumo ya uhamishaji wa vihatarishi na bima (bima huru, ya mazao) ili kutoa huduma ya kitaifa kwa jamii zilizo hatarini ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.3. Kuanzisha na kuongeza wigo wa mifumo ya uokozi and fidia katika ngazi ya jamii kwa mikoa angalau mitano | | | | | |

| **Shabaha** | **Afua** | **Mpango wa Maendeleo wa Mwaka** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** |
| | inayokabiliwa zaidi na changamote za hali ya hewa kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 3.4. Kuhamasisha na kuanzisha mfuko maalum wa hasara na uharibifu kwa kutumia vyanzo bunifu kama vile bima za tabianchi, angalau kufikia dola za Marekani milioni 100 kwa mwaka ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo la 2**: **Kuchochea teknolojia na ubunifu katika kilimo, mifugo, uvuvi na misitu ili kujenga minyororo ya thamani yenye ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha ukuaji endelevu wa uchumi ifikapo 2050** | | | | | | |
| 1. Asilimia 30 ya wazalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kutumia teknolojia rafiki kwa mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kutumia mifumo ya kisasa ya umwagiliaji inayoendeshwa kwa njia ya mtandao na mfumo wa ufuatiliaji wa udongo ili kuboresha matumizi ya maji katika kilimo ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2. Kuongeza majukwaa ya ushauri kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ili kutoa taarifa za hali ya hewa na soko kwa wakati halisi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kutumia mifumo ya kisasa ya kidijitali ya ufuatiliaji wa mifugo ili kuimarisha usimamizi na masoko ya mifugo ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Asilimia 20 ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo kutumia nishati jadidifu na kutekeleza mbinu stahimilivu za mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2031. | 2.1. Kuwekeza katika majokofu na vyombo vingine vya uhifadhi vinayotumia umeme wa jua ili kuimarisha utunzaji na kulinda thamani ya bidhaa za uvuvi, ufugaji na mbogamboga ifikapo 2031. | | | | | |
| | 2.2. Kuwezesha kongani za viwanda vya kilimo zinazoendeshwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi zenye mifumo ya kidijitali kwa ajili ya ufanisi wa matumizi ya rasilimali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kuanzisha mifumo ya udhibiti wa ubora inayoendeshwa na Akili Unde katika usindikaji wa chakula na uvuvi ili kuimarisha thamani na usalama wa bidhaa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 3. Kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno kwa asilimia 15, na asilimia 40 ya biashara ya mazao ya kilimo kupitia matumizi ya | 3.1. Kukuza na kuimarisha biashara kwa njia ya mtandao na huduma za fedha kiganjani/kwa njia ya simu za mkononi hususan miongoni mwa biashara ndogo na za kati pamoja vyama vya ushirika ili | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| teknolojia mbalimbali ikiwemo ya kidijitali ifikapo Juni 2031 | kuwaongezea ushindani na wigo wa soko ifikapo 2031. | | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | 3.2. Kuwekeza katika majokofu na maghala yanayostahimili hali ya hewa katika maeneo yenye uhaba wa chakula ili kupata akiba ya chakula ifikapo Juni 2031. | | | ✓ | ✓ | ✓ |
| | 3.3. Kuanzisha majukwaa jumuishi ya takwimu yanayounganisha uzalishaji, usafirishaji na mahitaji ya watumiaji ili kuboresha ufanisi wa minyororo ya ugavi ifikapo Juni 2031. | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Mfumo wa Utoaji Tahadhari Mapema na Uwezo wa Taasisi | | | | | | |
| Lengo la 1: Kuanzisha mfumo jumuishi wa sekta mbalimbali wa utoaji wa tahadhari ya mapema utakaoimarisha uhimilivu wa taifa kupitia taarifa za wakati, za kuaminika na zinazoweza kuchukuliwa hatua katika sekta za mazingira, uchumi, afya na kijamii ifikapo 2050. | | | | | | |
| 1. Kuongeza uwekezaji na ugharamiaji wa Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema (EWS) kwa angalau asilimia 0.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka, ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuanzisha mifumo ya Ubia baina ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya kufadhili miundombinu ya tahadhari ya mapema ifikapo Juni 2030. | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | |
| | 1.2. Kuanzisha programu ya kuwezesha ubunifu wa mifumo ya tahadhari ya mapema mahususi kwa ajiri ya sekta binafsi na jamii ifikapo 2028. | | ✓ | | | |
| | 1.3. Kutenga angalau asilimia 30 ya bajeti ya uboreshaji wa teknolojia ya maafa/majanga katika akili-unde (AI), takwimu na teknolojia nyingine za kisasa ifikapo Juni 2031. | | | ✓ | ✓ | ✓ |
| 2. Kutumia teknolojia ya kidijitali kutoa taarifa za tahadhari ya mapema katika kanda zote zenye hatari kubwa ifikapo Juni 2031. | 2.1. Kuanzisha mifumo ya tahadhari za moja kwa moja (automated) katika maeneo 2–3 yenye hatari kubwa yanayokumbwa mara kwa mara na changamoto za tabianchi kufikia Juni 2027. | ✓ | | | | |
| | 2.2. Kujumuisha mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa taarifa na takwimu kama satelaiti, droni, IoT katika mfumo wa Taifa wa Tahadhari ya Mapema ili kuweza kutambua kwa wakati vihatarishi mbalimbalii ifikapo Juni 2031. | | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | 2.3. Kuhakikisha mfumo wa usambazaji taarifa unawafikiwa watu wote, kwa wakati unaofaa, kwa lugha mbalimbali na katika maeneo yote yenye hatari kubwa ifikapo Juni 2031. | | | ✓ | ✓ | ✓ |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| 3. Kuongeza idadi ya watu wanaofikiwa na Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema (EWS) kutoka asilimia 2 (2023) hadi angalau asilimia 30 ifikapo Juni 2031, kwa kuongeza mifumo jumuishi ya kijamii kwa angalau miji 10. | 3.1. Kuanzisha kampeni za kitaifa za uhamasishaji katika sekta mbalimbali kuhusu Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema na kuanzisha mazoezi ya majaribio kila mwaka katika sekta mbalimbali ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 3.2. Kubuni kwa pamoja itifaki za tahadhari mahususi kwa sekta na wadau na kuziwasilisha katika miundo inayoweza kufikiwa kirahisi (mfano kwa kutumia Kiswahili) ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 3.3. Kuongeza mifumo ya utoaji tahadhari mapema iliyounganishwa na jamii ili kuhakikisha utendakazi katika ofanya kazi, iliyounganishwa na jamii kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **3.5.6. Kuimarisha Ushiriki katika Biashara ya Kaboni** | | | | | | |
| **Lengo la 1: Kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kinara wa kikanda katika biashara ya kaboni, kuchochea mapato endelevu, ajira zinazotokanazo na uchumi wa kijani na uhimilivu wa tabianchi.** | | | | | | |
| 1. Kuanzisha sera ya taifa ya biashara ya kaboni na mfumo wa urekebu ifikapo Juni 2028. | 1.1. Kufanya mapitio na kuhuisha miongozo na kanuni za biashara ya kaboni za kitaifa ili kuendana na mwenendo na viwango vya masoko ya kimataifa ifikapo 2028. | | | | | |
| | 1.2. Kuanzisha mfumo wa ndani wa kupanga bei kaboni kwa sekta za kipaumbele ifikapo 2028. | | | | | |
| | 1.3. Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa Kituo cha Taifa cha Kaboni ili kiweze kuratibu na kusimamia mfumo wa biashara ya kaboni kwa ufasaha ifikapo 2029. | | | | | |
| 2. Kuanza kufanya kazi kikamilifu kwa mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa Upimaji, Utoaji Taarifa na Uthibitishaji (MRV) na usajili wa biashara ya kaboni ifikapo Juni 2030. | 2.1. Kuandaa na kuendesha mfumo imara wa kitaifa wa kidijitali wa upimaji, utoaji taarifa na uthibitishaji na jukwaa la usajili wa biashara ya kaboni ifikapo 2030. | | | | | |
| | 2.2. Kuwekeza katika teknolojia za kisasa, zenye uwazi na zinazotoa taarifa kwa wakati mfano setilaiti ili kuboresha ujumuishaji wa mfumo imara wa kitaifa wa kidijitali wa upimaji, utoaji taarifa na uthibitishaji ifikapo 2030. | | | | | |
| | 2.3. Kuanzisha vivutio na mifumo ya kifedha (mfano: punguzo la kodi, hati fungani za kijani) ili kuvutia wawekezaji wa ndani na jamii kushiriki katika miradi ya biashara ya kaboni ifikapo 2029. | | | | | |
| | 2.4. Kuwezesha uundaji wa vyama vya ushirika na mashirika ya kijamii ili | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | kushiriki kwa pamoja katika miradi ya biashara ya kaboni na na kusimamia manufaa yake ifikapo 2029. | | | | | |
| 3. Angalau miradi ya biashara ya kaboni ya kiwango cha juu 15- 20 iwe imethibishwa na kuanza kufanya kazi ifikapo Juni 2031. | 3.1. Kufanya tathmini ya kitaifa ya awali ili kutambua miradi iliyopo na kutenga maeneo ya misitu yenye sifa ya kutumika katika biashara ya kaboni ifikapo 2029. | | | | | |
| | 3.2. Kuiwezesha na kuithibitisha miradi ya biashara ya kaboni katika sekta za kipaumblele (katika misitu, bahari, nishati jadidifu, usimamizi wa taka na kilimo endellevu) ili kufikia lengo la kuwa na miradi 15-20 inayofanya kazi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.3. Kuimarisha ustawi wa biashara za kaboni zilizosajiriwa ndani ya nchi na kikanda ili kujenga msingi wa kulifikia soko la kimataifa ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| 4. Angalau asilimia 15 ya miradi ya kaboni iwe imeshirikisha/jumui sha jamii ifikapo Juni 2031 | 4.1. Kutekeleza programu za kujenga uwezo na ushiriki katika biashara ya kaboni katika ngazi ya jamii, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, wawekezeji katika biashara ya kaboni ifikapo 2029. | | | | | |
| | 4.2. Kuanzisha na kufanya majaribio ya vituo vya biashara ya kaboni katika ngazi ya serikali za mitaa katika Halmashauri 2-5 ili kuwezesha miradi inayoongozwa na jamii ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 4.3. Kutoa motisha (ikiwemo za kikodi, hatifungani za kijani mapumziko ya kodi, dhamana ya kijani, fedha zinazozunguka) ili kuvutia wawekezaji wa ndani na jumuiya kushiriki katika miradi ya biashara ya kaboni ifikapo 2030. | | | | | |
| | 4.4. Kusaidia uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya kijamii kushiriki katika miradi ya biashara ya kaboni ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **3.5.7. Kuimarisha Manufaa ya Uchumi wa Buluu** | | | | | | |
| **Lengo la 1: Kutumia rasilimali za bahari na maji baridi kwa njia endelevu ili kuchochea ukuaji jumuishi wa uchumi, kuzalisha ajira, kulinda mazingira na kuboresha maisha, pamoja na kuchochea ubunifu na kuimarisha usimamizi.** | | | | | | |
| 1.1. Kuongezeka kwa mchango wa uvuvi na ufugaji samaki katika Pato la Taifa kufikia asilimia 3.5 ifikapo 2030. | 1.1. Kuanzisha maeneo makubwa ya ufugaji samaki yenye vituo vya kuzalisha vifaranga, viwanda vya chakula cha samaki pamoja na miundombinu ya | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | uchakataji ili kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani ya samaki ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2. Kuwekeza katika mtandao wa usafirishaji na uhifadhi wa bidhaa zinazoharibika na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa kidijitali ili kupunguza upotevu baada ya mavuno na kulinda ubora wa kukidhi viwango katika masoko ya kimataifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kutoa mikopo nafuu na ruzuku kwa wavuvi na wafanyabiashara wadogo na wa kati ili kuwawezesha kutumia vifaa vya kisasa, mbinu endelevu na kuwekeza katika uongezaji thamani ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.4. Kusimamia na kutekeleza viwango vya uvunaji vinavyozingatia tafiti za kisayansi na kulinda maeneo muhimu ya kuzaliana samaki ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa sekta kila mwaka. | | | | | |
| | 1.5. Kuwekeza katika viwanda vikubwa vya uzalishaji wa chakula cha samaki ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.6. Kuanzisha maeneo makubwa ya ufugaji samaki yenye vituo vya kuzalisha vifaranga, viwanda vya chakula cha samaki pamoja na miundombinu ya uchakataji ili kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani ya Samaki ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.7. Kuongeza miundombinu ya usafirishaji na kuhifadhia bidhaa za uvuvi zinazoharibika ifikapo Juni 2028. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **3.6. Vichocheo vya Kusukuma Maendeleo** | | | | | | |
| **3.6.1 Nishati Itakayowezesha Ukuaji wa Uchumi wa Viwanda** | | | | | | |
| **Lengo 1: Sekta ya nishati inaongozwa kisasa, kwa uwazi na ufanisi, sanjari na kuwa na wataalamu wenye ujuzi kuweza kutoa huduma za kuaminika, bunifu na endelevu** | | | | | | |
| 1. Nguvukazi watu yenye wataalamu wa nishati angalau 10,000 kitaifa walio na ithibati kufikia Juni 2031. | 1.1. Kuandaa Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Ujuzi katika Sekta ya Nishati ifikapo Juni 2027. | | | | | |
| | 1.2. Kutekeleza Mkakati wa Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Ujuzi katika Sekta ya Nishati ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Kuhakikisha kuwepo kwa uwazi, ufanisi na uwajibikaji katika uendeshaji wa sekta ya nishati nchini kufikia Juni 2031 | 2.1. Kuimarisha mifumo ya udhibiti na urekebu katika usimamizi madhubuti na ufanisi wa sekta ya nishati ifikapo 2028. | | | | | |
| | 2.2. Kuandaa kanuni wazi na zenye nguvu ya kisheria katika usimamizi wa Mashirika na makampuni ya umma katika uendeshaji wa sekta ya nishati sanjari kuwea masharti kwa kutoa taarifa za fedha na utekelezaji ifikapo 2028. | | | | | |
| **Lengo 2: Tanzania iwe imefanyia marekebisho sekta yake ya nishati kuwa ya ushindani, uwazi na uendelevu wa kifedha, ikiwa ni pamoja na kubadilishwa kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwa kampuni ya kibiashara na shughuli zake kutenganishwa katika vitengo vitatu vya uzalishaji, usafirishaji na usambaji wa umeme zinavyofanya kazi kwa kujitegemea na kuendeshwa kwa taratibu zinazo zingatia utendaji utakaowezesha ushindani na ushiriki wazi wa sekta binafsi na utoaji wa huduma za uhakika.** | | | | | | |
| 3. Shirika la Umeme Tanzania kuwa imebadilishwa kuwa kampuni tatu za kibiashara zinazojitegemea za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa umeme ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kufanyika kwa maboresho ya muundo wa taasisi na kifedha kupitia mkaguzi huru, kuboresha mpango kazi na kuhuisha kanuni za uendeshaji kuendana na matakwa ya sheria Ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.2 Kutenganisha mundo ya uhasibu na usimamizi katika shughuli za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.3 Kutunga sheria na nyenzo za udhibiti ili kuifungua sekta kuruhusu ushiriki wa sekta binafsi katika taasisi za Uzalishaji na Usambazaji, na kuligawa Shirika la Umeme Tanzania ili kuanzisha mashirika ya umma yanayojitegemea katika Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 3.4 Kuanzishwa kwa mfumo wa bei za umeme zinazoakisi gharama halisi (cost-reflective tariffs) na uwazi ili kupunguza | | | | | |

| **Shabaha** | **Afua** | **Mpango wa Maendeleo wa Mwaka** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** |
| | ruzuku na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi | | | | | |
| | 3.5 Kuanzishwa kwa mikataba ya udhibiti na usimamizi wa utendaji (performance-based regulation and management contracts) ili kuboresha ufanisi, kupunguza hasara, na kuimarisha utoaji wa huduma. | | | | | |
| 4. Kuanzisha mfumo huru, unaogharamiwa kkikamilifu na kufanyakazi kwa mamlaka kamili katika kuratibu usambazaji na kuruhusu wasambazaji wengine na kukuza ufanisi wa soko la ratibu umeme ifikapo Juni 2031 | 4.1 Kuandaliwa kwa mwongozo wa udhibiti na urekebu, na uendeshaji wa soko huru la umeme kwa kushirikiana na EWURA na wadau wa sekta wa nishati wa sekta binafsi na umma ifikapo 2028. | | | | | |
| | 4.2 Kuitambua na kuiwezesha EWURA, kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Mipango, kuwa inaandaa na kuratibu utekelezaji Mpango wa Taifa wa nishati ya umeme ifikapo mwaka 2027. | | | | | |
| | 4.3 Kukusanya fedha, misaada ya kitaalam na ujenzi wa uwezo wa kitaasisi unaohitajika kuanzisha msimamizi wa soko huru la nishati ya umeme pamoja na utayari wa uendeshaji wake kila mwaka. | | | | | |
| | 4.4 Kuwezesha muundo wa Soko Huru la Umeme wenye mamlaka kamili ya upangaji, usawa na, kanuni wazi za upatikanaji, na uratibu wa soko la ushindani kati ya wazalishaji wa umma na binafsi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo la 3: Tanzania kuwa na miundombinu ya nishati thabiti, unganishi na iliyo tayari kwa uwekezaji ambayo inawezesha upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme kwa matumizi ya ndani, biashara ya umeme na nchi jirani, na iliyojengwa kwa ubia endelevu kati ya sekta za umma na binafsi pamoja na inakua na sekta ya nishati yenye** utumia **mitaji itokanayo na mipango ya hifadhi za mazingira.** | | | | | | |
| 5. Angalau njia moja ya msongo wa kV 400 ijengwe sanjari na kuimarishwa kwa mtandao mkuu wa usafirishaji wa umeme ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini na uendeshaji wa biashara ya umeme kikanda ifikapo Juni 2031 | 5.1 Kujengwa kwa kiunganishi kimoja (1) mpakani cha msongo wa 400kV inayounganisha Tanzania na nchi za Zambia, Uganda na Kenya ili kuimarisha ubadilishanaji thabiti wa umeme kikanda ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.2 Kutumia mifumo ya SCADA na teknolojia za kisasa katika gridi na angalau asilimia 90 ya vituo vya udhibiti kikanda ifikapo 2031. | | | | | |
| | 5.3 kusasisha gridi ya taifa ya usafirishaji wa umeme katika vishoroba zilizopewa vya kipaumbele kwa kiwango cha 400kV | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | kuhakikisha utayari wa kupokea na kusafirisha umeme wenye uwezo mkubwa kwa matumizi ya kwa biashara kikanda ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.4 Kuwianisha kanuni na taratibu za uendeshaji wa gridi umeme nchini na zile za umeme wa pamoja kwa nchi za ukanda wa Kusini na Mashariki Mashariki (SAPP na EAPP) mtawalia, angalau kwa asilimia 70 kufikia Juni, 2031. | | | | | |
| 6 Angalau kiasi cha Dola za Marekani bilioni 7 ziwe zimekusanywa kutoka vyanzo vya mikopo ya masharti nafuu na hatifungani za mazingira kwa ajili ya kufadhili uzalishaji na usafirishaji wa nishati safi ya umeme nchini ifikapo Juni 2031 | Kuanzisha na kutumika Mfumo wa ufadhili wa nishati safi ya kupikia - kufikia Juni, 2031. | | | | | |
| | i. Kuanzishwa kwa mwongozo wa mfumo wa ufadhili wa nishati safi ya kupikia ifikapo Juni, 2028. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha ushirikiano na Benki za Maendeleo za Kimataifa na mifuko yaufadhili ya mabadiliko ya tabianchia ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | iii. Kuandaa mfumo wa kitaifa wa upangaji wa miradi ya kipaumbele inayozingatia mabadiliko ya tabia nchi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 4: Kuongeza a uwezo wa uzalishaji umeme nchini Tanzania kufikia MW 8,000 ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadae, kuimarisha ujenzi wa sekta ya viwanda na kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa wote ifikapo 2031** | | | | | | |
| 7. Wastani wa matumizi ya nishati ya umeme kwa mtu kuongezeka kufikia 600 kWh ifikapo Juni 2031 | 7.1. Kuharakisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya uzalishaji wa nishati safi ya umeme (wa maji, jua, upepo, jotoardhi, gesi na nyuklia) ifikapo Juni 3029. | | | | | |
| | 7.2 Kuandaa mpango kabambe jumuishi wa upanuzi wa uzalishaji wa umeme ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 7.3. Kutumia ruzuku kwa uunganishaji wa umeme katika kaya na teknolojia za nje ya gridi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 8. Uwezo wa uzalishaji wa nishati safi nchini kuongezeka kufikia MW 8,000 ifikapo Juni 2031 | 8.1 Kuzindua kwa awamu mitambo mikubwa ya uzalishaji wa umeme wa maji, jua, upepo na jotoardhi kwa awamu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 8.2 Kuandaliwa na kuanza ujenzi wa mtambowa uzalishaji wa umeme wa nyuklia wa uwezo wa MW 1,000 kwa majaribio e ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 8.3. Kuandaa na kutekeleza mifumo ya vivutio na minada ya ushindani kwa | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | wazalishaji binafsi wa umeme (IPPs) ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 5: Kuongeza kiwango cha nishati jadidifu katika mseto wa nishati ya umeme angalau kufikia asilimia 50, kuweza kupunguza uzalishaji wa hewaukaa na kuimarisha ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.** | | | | | | |
| 9. Uwezo wa kuzalisha MW 1,700 umeme wa jotoardhi, MW 500 za umeme wa upepo, na MW 715 za umeme jua ifikapo Juni 2031. | 9.1 Kuharakisha utoaji wa leseni za nishati jadidifu (RE) na taratibu za vibali vya mazingira kwa kurahisisha hatua za udhibiti, kuweka muda maalumu wa utekelezaji na kuimarisha uratibu wa kitaasisi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kufanyika kwa mapitio na kufungamanisha mifumo ya udhibiti ya nishati jadidifu ifikapo Juni 2027. | | | | | |
| 10. Angalau asilimia arobaini ya uzalishaji wa umeme itokane na vyanzo vya nishati jadidifu ifikapo Juni 2031 | **10.1** Kuanzisha Kituo jumuishi cha pamoja cha Kutoa vibali vya Nishati Jadidifu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | **10.2** Kuboresha miundombinu ya gridi (mifumo ya usimamizi na udhibiti wa gridi, teknolojia za kuongeza uthabiti wa mfumo wa umeme,mifumo ya uhifadhi wa betri, na miunganiko) ili kusaidia ujumuishaji wa asilimia 80 ya nishati jadidifu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 11. Gridi ya Taifa iwe imefanyiwa matengenezo kuongezea uwezo wa kuweza kuchukua asilimia 80 ya nishati ya umeme mbadala inayotazamiwa kuzalishwa karibuni, ifikapo Juni 2031 | 11.1 Kuanzisha kanda za uzalishaji wa nishati jadidifu na vituo vya ubunifu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 11.2 Kuanzisha mnada wa ushindani wa nishati jadidifu na mifumo ya ufadhili ya hati fungani za kijani/ nishati safi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 11.3 Kuwezesha usambazaji wa MW 300 kutoka katika gridi ndogo za jamii za ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 11.4 Kuweka rasmi wa kupanga ustahimilivu na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na utyari wa hifadhi ya nishati ya jua ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 6: Mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini Tanzania kuboreshwa ili kupunguza kiwango cha upotevu wa umeme kwa sababu za kiufundi na kibiashara kuwa angalau chini ya asilimia 5 pamoja na kuhakikisha uthabiti wa gridi** | | | | | | |
| 12 Kupunguza upotevu wa umeme katika mfumo wa Taifa kutoka asilimia 14.2 hadi asilimia 12.4 ifikapo Juni 2031 | 12.1 Kubadilishwa kwa angalau asilimia 70 ya transfoma zilizochakaa na kuboreshwa kwa kilomita 1,000 za njia kongwe za usambazaji wa umeme mijini kupunguza mzigo na hasara za kiufundi ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 12.2 Kubadilisha transfoma zilizochakaa na kuboresha njia za umeme mijini ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 13 Kujenga vituo vidogo 100 vya kupooza umeme vijijini na mifumo ya gridi ya teknolojia za kisasa katika mikoa mikubwa ifikapo Juni 2031. | 13.1 Kuwekeza katika gridi za umeme vijijini na miundombinu ya usambazaji bora ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 13.2 Kuanzisha usimamizi na ratiba ya ukarabati wa gridi ya taifa kwa kutumia teknolojia ya kidijitali kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 13.3 Kutumia mita za teknolojia za kisasa kwa asilimia 100 kwa wateja wa kibiashara na wa kati ifikapo 2031. | | | | | |
| | 13.4 Kutumia nyaya za umeme za chini ya ardhi katika maeneo yenye msongamano mkubwa mijini ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 13.5 Kuongeza wigo wa ushiriki wa sekta binafsi katika usafirishaji na usambazaji wa umeme kupitia Makampuni Huru kwenye kanda za viwanda ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo Na. 7: Kaya nchini kupata umeme wa uhakika na gharama nafuu kwa asilimia 100** | | | | | | |
| 1. Kuongeza wastani wa uunganishwaji wa umeme kwa kaya nchini kutoka asilimia 49 hadi asilimia 55.2 kitaifa na uunganishaji wa umeme vijijini kutoka asilimia 36 hadi asilimia 42.8 ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kutekeleza kampeni ya kitaifa ya uunganishaji wa umeme kwa kaya mpya milioni 4 ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2. Kufanya mapitio,kurahisisha taratibu na kupunguza gharama za uunganishaji wa umeme za uunganishaji kwa asilimia 50 kwa kaya za kipato cha chini ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 1.3. Kuanzisha utaratibu wa kutoa vivutio vinavyozingatia ufanisi wa utendaji kwa wawekezaji binafsi wanaotoa huduma katika maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| 1. Uhakika wa upatikanaji wa umeme kwa ngazi ya kaya uimarike kufikia angalau 80% ifikapo Juni 2031. | 2.1. Kujenga vituo vidogo 100 vya kupooza umeme kwa maeneo ya vijijini pamoja na kuboresha transfoma za maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2. Kutumia gridi za na mifumo ya ufuatiliaji ya kisasa kwa angalau asilimia 80 katika ya maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kuanzisha mikataba ya matengenezo kwa kigezo cha ufanisi wa utendaji kwa watoaji wa huduma za umeme katika maeneo ya vijijini ifikapo Juni 2028. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **Lengo 8: Kuimarisha uhakika na uthabiti wa upatikanaji wa umeme nchini kwa kuwa na vyanzo mchanganyiko, vikijumuisha matumizi ya kimkakati ya mashapo yamakaa ya mawe na nishati jadidifu sanjari na matumizi ya teknolojia zenye uchafuzi mdogo wa hewa** | | | | | | |
| 1. Angalau mitambo yenye uwezo wa kuzalisha MW 1,000 za umeme wa makaa ya mawe yenye kuzingatia vigezo vya kimazingira ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kutambuliwa na kutengwa kwa maeneo yenye makaa ya mawe na kuharakisha utoaji wa leseni kwa ajili ya mitambo ya uzalishaji wa umeme wa makaa ya mawe wa MW 3,000 ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2. Kuhamasisha ubia kati ya sekta za umma na binafsi na kuweka mfumo wa dhamana kwa uwekezaji katika matumizi ya teknolojia safi za makaa ya mawe, ikijumuisha mifumo ya kupunguza salfa katika gesi na teknolojia za kunasa hewa ukaa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kuanzishwa kwa mwongozo wa Mfumo Endelevu wa Uzalishaji Umeme unaotokana na Makaa ya Mawe utakaosimamia uibuaji wa miradi na ufuatiliaji wa mazingira ifikapo Juni 2027. | | | | | |
| 2. Kuwa na utaratibu wa kudumu wa ziada ya umeme wa kiwango cha asilimia 20 ifikapo Juni 2031 | 2.1. Kuongeza uunganishaji wa umeme wa gridi kufikia MW 1,500 kupitia gesi, umeme wa maji na mifumo ya nishati jadidifu kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2. Kuanzishwa kwa Sera ya Kimkakati ya Nishati ya Akiba yenye sharti la kuwa na akiba isiyopungua ziada asilimia 20 ya umeme ifikapo 2027. | | | | | |
| | 2.3. Kutekelezwa kwa mfumo wa maoteo wa wakati halisi wa mahitaji na upatikanaji wa nishati ili kuimarisha usimamizi wa akiba ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| **3.6.2. Usafirishaji na biashara ya uchukuzi fungamanishi kufikia masoko ya kimataifa** | | | | | | |
| **Lengo 1: Ufanisi na ufungamanishi wa miundombinu ya usafirishaji na biashara ya uchukuzi kuimarishwa kwa kuboresha usafirishaji wa watu, bidhaa na rasilimali mijini na mikoani ili kuchochea ukuaji endelevu, , maendeleo ya uchumi viwanda, na kuboresha upatikanaji wa masoko ya kimataifa** | | | | | | |
| **Miundombinu ya Barabara** | | | | | | |
| 1. Kuwa na mfumo jumuishi, endelevu na barabara zenye teknolojia ya kisasa nchini ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuanza usanifu wa barabara zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi na kwa zana za kidijitali (akili unde na mifumo ya taarifa za kijiografia) kwa ajili ya kupanga ukarabati wa barabara, taa za barabarani zinazoendeshwa kwa nishati ya jua, na mifumo ya kisasa ya kuongoza vyombo vya usafiri barabarani ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 1.2. Kutumia mifumo ya teknolojia mahiri ya barabara, ikiwemo mitambo ya kufuatilia mwenendo wa usalama wa barabarani wa wakati, utozaji wa malipo ya matumizi ya njia za kidijitali, mizani ya kidijitali, na udhibiti wa uzito ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kutengeneza ramani kidijitali za barabara za vijijini ambazo hazijaanishwa na kuzingiza katika ramani ya dunia na zana huria ili kusaidia upangaji, matengenezo na kukabiliana na matukio ya dharura ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4. Kuwekeza katika miundombinu ya mijini ili kupunguza msongamano wa magari katika miji mikuu ikiwemo Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya na Mwanza na kurahisisha usafiri na uchukuzi mijini ifikapo Juni, 2031 | | | | | |
| 2. Kuongeza kiwango cha barabara za lami kutoka asilimia 8.6 hadi 10.58 ifikapo Juni 2031. | 2.1. Kujenga, kukarabati na kufanyia matengenezo barabara za mikoa na vijijini zinazoiunganisha kanda za kilimo, madini na viwanda na masoko kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2. Kupanua mtandao wa barabara za kisasa na mifumo ya Usafiri wa Mabasi yaendayo Haraka (BRT) katika miji mikuu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kuendeleza barabara zinazoiunganisha Tanzania na nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki Na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ili kukuza biashara ya kikanda ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.4. Kujenga barabara mpya za mwendokasi zinazounganisha miji mikubwa na vituo vya kiuchumi, zikiwa viwango vya juu vya usanifu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.5. Kusanifu na kujenga madaraja ya kisasa kuwezesha kuvuka mito mikubwa, kuimarisha uthabiti wa barabara na kuwa utambulisho wa kikanda ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.6. Kupanga na kujenga kwa majaribio ya barabara za magari ya umeme zikiwana vituo vya kuchajishia magari ya mizigo | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | na abiria katika njia zenye misongamano mikubwa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 3. Kufikia asilimia 35 ya kiwango cha matengenezo ya barabara ifikapo Juni 2031 | 3.1. Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa miundombinu na rasilimali za barabara, ikijumuisha mifumo ya utunzaji wa taarifa kwa teknolojia za GIS na za taarifa utekelezaji mwaka za miundombinu kuweza kujua maendeleo na athari zake ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.2. Kuongeza bajeti ya matengenezo ya barabara na kubuni vyanzo vipya vya kugharamia ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.3. Kutenga ardhi kwa ajili ya njia na kujenga mabomba chini ya ardhi kwa upitishaji wa maji, umeme, intaneti na maji- taka mijini kuweza kupunguza uchimbaji na uharibifu wa miundombinu mara kwa mara ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Usafiri wa Anga** | | | | | | |
| 4. Farihisi ya Muunganiko wa Usafiri wa Anga kuongezekakutoka asilimia 0.35 mwaka 2025 hadi asilimia 0.85 ifikapo Juni 2031 | 4.1. Kuongeza uwezo wa majengo ya abiria, maegesho ya ndege, njia za kuruka na kutua ndege, na miundombinu ya usafirishaji wa katika viwanja vikuu vya kimataifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 4.2. Kukarabati na kupanua uwezo wa viwanja vidogo vya ndege katika mikoa ya Mbeya, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mtwara, Musoma, na Shinyanga ifikapo June 2031.<br>4.3. Kuanzisha majengo mahsusi kwa usafirishaji wa mizigi katika viwanja vya ndege vya Mbeya, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mtwara, Musoma na Shinyanga. | | | | | |
| | 4.4. Kuweka mifumo ya rada za ufuatiliaji wa mwenendo wa ndege na kusambaza satelaiti katika anga la Tanzania ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 4.5. Kuwianisha taratibu za utoaji wa leseni, usalama wa anga na wa nchi jirani kuwezesha usafiri wa kikanda kufanyika bila vikwazo na kuwa na anga huru ifikapo 2031. | | | | | |
| | 4.6. Kujenga kituo cha kitaifa cha mafunzo ya usafiri wa anga kwa ushirikiano na wadau wa kimataifa ili kuzalisha marubani, wahandisi, waongozaji ndege, wahudumu na huduma za droni. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 4.7. Kutumia mifumo ya Kieletroniki ya kuhakiki taarifa kwa kutumia alama za vidole katika milango ya kusafiriia, viza na uthibitisho wa kiafya ili kuboresha usalama, kasi na ufanisi wa huduma za abiria ifikapo 2031. | | | | | |
| | 4.8. Kutumia mifumo ya Kieletroniki ya kuhakiki taarifa kwa kutumia alama za vidole katika milango ya kusafiriia, viza na uthibitisho wa kiafya ili kuboresha usalama, kasi na ufanisi wa huduma za abiria 203 ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Usafiri wa reli** | | | | | | |
| 5. Kuongeza eneo lenye mtandao wa reli kutoka kilomita 4.97 kwa eneo mraba la kilomita 1,000 kufikiai kilomita 7.98 ifikapo Juni 2031. | 5.1. Kukamilisha ujenzi wa reli za mizigo na abiria kwa kiwango cha reli ya kimataifa kuunganisha Dar es Salaam–Dodoma–Mwanza, Isaka–Kigali, Tabora–Kigoma.–DRC, Tabora–Mpanda–Kalemie na Mtwara–Mbambabay–Mchuchuma–Liganga (shoroba ya kusini) ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.2. Kukarabati reli ya upana wa mita ikiwemo maunganisho, hasa ya Dar–Tanga–Arusha ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.3. Kujenga njia mahsusi za reli kutoka njia kuu kufikia maeneo ya migodi (mf. Liganga, Mchuchuma) na maeneo ya viwanda (mf. Bagamoyo, Kisarawe, Mlandizi) ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.4. Kuwianisha huduma za reli na meli katika maziwa makuu (Victoria, Tanganyika, Nyasa) kati ya bandari na njia za reli ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.5. Kujenga au kuboresha maghala na vituo vya mizigo katika vituo vikubwa vya reli, kama Tabora, Mwanza na Kigoma ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.6. Kuboresha miundombinu chakavu (reli, nguzo, mawe) kutoka Dar es Salaam hadi New Kapiri Mposhi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.7. Kufanyia maboresho sheria na taratibu za uwekezaji Shirika la Reli ya Tanzania na Zambia kuruhusu ushiriki wa waendeshaji binafsi, wakodishaji na wabia wa usafirishaji na biashara ya uchukuzi ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 5.8. Kuanzisha au kupanua bandari kavu katika shoroba wa usafirishaji na uchukuzi katika miji ya Mbeya, Tunduma na Mpika (Zambia) ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 6. Msongamano wa abiria katika miji mikubwa kupungua kwa asilimia 40 ifikapo Juni 2031. | 6.1. Kukamilisha, kwa awamu, ujenzi wa reli za abiria za umeme mijini zinazounganisha vitongoji vikuu na maeneo ya kibiashara. | | | | | |
| | 6.2. Kujenga miundombinu unganishi ya usafiri mijini, ikiunganisha ainambalimbali za usafiri vituo vya reli, mabasi ya mwendokasi, mabasi ya mikoani na vituo vya mizigo ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 6.3. Kuanza utekelezaji wa mfumo wa kidijitali wa tiketi na mnyororo wa usafiri unaounganisha reli, BRT, mabasi ya jiji na huduma za usafirishaji wa mizigo ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 6.4. Kuwekeza kwenye mabehewa ya umeme na miundombinu ya bora ya nishati kukuza uendeshaji wa reli za zilizo rafiki kwa mazingira na zenye utoaji mdogo wa hewa chafu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 6.5. Kuanzisha mfumo fungamanishi wa reli ya abiria Jijini Dar es Salaam kama mradi wa kielelezo ili kupunguza msongamano kwa angalau asilimia 40 na kuboresha muunganiko wa usafiri kupitia vituo vya usafiri wa aina mbalimbali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 6.6. Kujenga mifumo ya kisasa ya reli ya abiria katika Mikoa ya Arusha, Mwanza na Dodoma, ikijumuishwa na mitandao ya usafiri wa ndani na miundo mbinu inayolenga usafiri wa umma ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 6.7. Imarisha mafunzo ya kitaifa ya reli na usafirishaji, yakiwemo mafunzo ya ufundi stadi na uthibitishaji wa lazima kwa wahandisi wa reli, waendeshaji wa mabehewa na mitambo ya reli, wahudumu wa treni, na mameneja wa usimamizi wa usafirishaji ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 6.8. Kushirikiana na waendelezaji wa reli za mijini wa kimataifa kutoka kampuni za kimataifa za (CRRC, Alstom, Siemens Mobility) kwa uhaulishaji wa teknolojia na utekelezaji kufikia Juni 2031. | | | | | |
| **Usafiri wa Maji** | | | | | | |
| 7. Kuongeza ujazi wa miundombinu ya usafiri wa maji kutoka km 3.2 kwa kila kilomita za mraba 1,000 kufikia ujazi wa kilomita 4.36 kwa kila kilomita za mraba 1,000 ifikapo Juni 2031 | 7.1. Kujenga Bandari ya Kina Kirefu ya Bagamoyo kama lango la kimataifa la kimkaakti ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 7.2. Kukarabati na kuboresha bandari za maziwa makubwa (Mwanza, Bukoba, Musoma, Kigoma, Kasanga, Itungi, Liuli, Mbamba Bay) ikiwa na vifaa vya kisasa vya mizigo, abiria na vifaa vya kuhifadhi baridi kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 7.3. Kujenga maeneo maalum ya kiuchumi (SEZs) na viwanda vinavyotumia bandari katika Mwanza, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Kilwa na Bagamoyo. Kuchochea ubiasharishaji unaoongozwa na mauzo ya nje ifikapo 2031. | | | | | |
| | 7.4. Kutumia mifumo ya kidijitali katika shughuli zote za bandari—tiketi, mizigo, forodha na ufuatiliaji wa meli ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 7.5. Kuhuisha na kuratibu kanuni za uongozaji ili kuhakikisha uwiano wa utoaji wa leseni za vyombo vya usafirishaji, utozaji wa tozo na taratibu za ukaguzi kwa mujibu wa viwango vya EAC, SADC na COMESA ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 7.6. Kuendeleza vituo vya usafirishaji vyenye mifumo mchanganyiko vya bandari kavu zilizounganishwa na bandari kuu na maziwa, ili kuboresha muda wa mzunguko wa mizigo na kuimarisha minyororo ya thamani ya kikanda.ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 7.7. Kusimika mifumo ya ufuatiliaji wa hali ya hewa kwa wakati halisi, rada na mifumo ya usalama inayotegemea satelaiti katika maziwa na maeneo ya ukanda wa pwani ifikapo 2031. | | | | | |
| | 7.8. Kujenga vituo bora vya mafunzo ya usafiri wa majini na usafirishaji vyenye uthibitisho wa lazima kwa marubani wa | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | meli, wahandisi, mafundi mitambo na wafanyakazi wa gati ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Mabomba ya Mafuta** | | | | | | |
| 8. Kuongeza mtandao wa mabomba kutoka km 1,500 hadi angalau km 2,200 ifikapo Juni 2031. | 8.1. Kukamilisha ujenzi na kuanza uendeshaji wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Uganda hadi Bandari ya Tanga, ili kuiweka Tanzania kama njia kuu ya usafirishaji wa mafuta ghafi Afrika Mashariki na kuchochea shughuli za kiuchumi katika ukanda wa mradi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 8.2. Kuboresha na kuongeza mtandao wa bomba la gesi asilia uliopo kutoka Mtwara na Songo Songo hadi vituo muhimu vya mijini (k.m. Dodoma, Mwanza, Arusha, Mbeya) na maeneo ya viwanda na Maeneo ya Maalum ya uwekezaji (SEZ) ili kuwezesha upatikanaji wa gesi kwa gharama nafuu kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, viwanda na usafiri ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 8.3. Kujenga mabomba ya bidhaa mbalimbali kutoka bandari za pwani (Dar es Salaam, Tanga, Mtwara) hadi kwenye bohari za nchi kavu (Dodoma, Mwanza, Kigoma) ili kupunguza utegemezi wa meli za barabarani, kuboresha usalama na kupunguza gharama za usafiri ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 8.4. Kujenga mifumo ya kuweka gesi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Morogoro kwa ajili ya gesi ya kupikia majumbani, taasisi za umma na mabasi ya mijini na viwanda vidogo ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 8.5. Kusimika mabomba ya gesi katika SEZ na IDZ zilizopangwa (k.m. Bagamoyo, Mtwara, Kibaha) ili kuboresha urahisi wa kufanya biashara na kuvutia wawekezaji wa viwanda ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 8.6. Kuanzisha maabara ya kisasa kwa ajili ya kupima vifaa vya bomba, vali na mita za kupimia maji jijini Dar es Salaam au Dodoma ili kuhakikisha udhibiti wa ubora, viwango vya usalama na kusaidia wazalishaji wa ndani ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Sayansi, Teknolojia na Ubunifu** | | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| 1. Tanzania kuwa kinara wa kikanda katika sayansi,teknolojia na ubunifu ifikapo 2031 | 1. Kutoa ufadhili endelevu kwa Utafiti na Maendeleo, ubunifu na biashara ya teknolojia kila mwaka | | | | | |
| | i. Kuanzisha mwongozo endelevu wa kitaifa wa ugharamiaji wa muda mrefu wa utafiti na maendeleo, ubunifu na biashara ya teknolojia ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | ii. Kulinda na kuendeleza ubunifu wa ndani kupitia mfumo imara wa haki miliki (IP) ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | iii. Kujumuisha masuala ya Sayansi, Teknolojia, Hisabati na Uhandisi na umahiri wa kidijitali katika ngazi zote za elimu na kuboresha elimu ya ufundi stadi (TVET) ujifunzaji wa muda mrefu, ili kujenga nguvu kazi iliyo tayari kwa ubunifu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | iv. Kuwezesha nguvu kazi ujuzi wa juu wa Kidijitali kwaa ajili ya kusaidia ubunifu katika sekta zote kila mwaka | | | | | |
| | v. Kuboresha upatikanaji wa takwimu za utafiti na ushirikiano wa kitaasisi kila mwaka | | | | | |
| | vi. Kusaidia Utafiti na Maendeleo katika nishati jadidifu, bioteknolojia, kilimo na uendelezaji taka kila mwaka. | | | | | |
| | vii. Kukuza mifumo ya ikolojia ya ubunifu kwa vijana katika ngazi zote ilikuongeza wigo wa ushirikishwaji na kujenga uwezo wa ubunifu kuanzia ngazi ya chini kwenda juu kila mwaka. | | | | | |
| 2. Angalau asilimia 10 ya Pato la Taifa kuchangiwa na sayansi, teknolojia na ubunifu ifikapo 2031. | 2.1. Tumia mitandao ya maarifa ya kimataifa kwa ajili ya ugharamiaji, uhawilishaji wa teknolojia, na ushirikiano wa utafiti wa kimataifa kila mwaka. | | | | | |
| | 2.2. Kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya intaneti ya kasi ya juu yenye gharama nafuu ili kusaidia ubunifu wa kidijitali na uchumi wa kidijitali kufikia ifikapo 2031 | | | | | |
| | 2.3. Kusimamia upitishaji na upanuzi wa AI, blockchain, IoT na bioteknolojia katika sekta za kipaumbele (kilimo, afya, nishati, viwanda) ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.4. Kuongeza wigo wa maeneo ya utafiti katika tafiti kama vile tafiti za kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi, | | | | | |

| **Shabaha** | **Afua** | **Mpango wa Maendeleo wa Mwaka** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** |
| | nishati mbadala, bioteknolojia na teknolojia za afya ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.5. Kuendeleza vituo maalumu vya utafiti, ubunifu na ujasiriamali vinavyolenga sekta za kiuchumi zenye athari kubwa kufikia Juni 2031 | | | | | |
| | 2.6. Kukuza iteknolojia za ndani ya nchi ili kuimarisha ushindani wa Tanzania na nafasi yake ya kuuza nje katika masoko ya kiteknolojia ya kikanda na kimataifa kufikia ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.7. Kutumia teknolojia zinazoibuka (AI, otomatiki, roboti, IoT) kuendesha ubiasharishaji, tija na uzalishaji na ongezeko la thamani kila mwaka. | | | | | |
| | 2.8. Kujenga miji ya kisasa na maeneo ya ubunifu (smart cities) wa kiteknolojia kwa ajili ya kufanya majaribio, kupanua wigo na kubiasharisha biashara ya teknolojia kwa kizazi kijacho ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.9. Tumia takwimu, Akili unde na ujifunzaji wa mashine kuongeza tija na kuanzisha fursa mpya za kiuchumi katika sekta za kimkakati kila mwaka | | | | | |
| | 2.10. Kusaidia ubunifu wa teknolojia ya kijani na uendelevu ili kuifanya Tanzania kuwa kinara kikanda katika nishati safi, usimamizi wa taka na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwa mwaka.<br><br>2.11. Kuanzisha teknolojia ya mnyororo wa thamani wa ugavi inayowezesha kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa ndani katika sekta kama vile kilimo, viwanda na nishati kila mwaka. | | | | | |
| **3.6.4. Mfumo wa utafiti na maendeleo** | | | | | | |
| Lengo la 1: Kuanzishwa kwa Mfumo endelevu wa utafiti na maendeleo unaoendeshwa kidijitali, unaoendesha ushindani wa kimataifa na kuleta maboresho yanayoweza kupimika katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika sekta muhimu ifikapo 2050 | | | | | | |
| 1. Vijana milioni 1 kuwa na ujuzi wa Akili Unde na ujuzi wa juu wa kidijitali ifikapo 2031 | 1.1. Kuandaa na Mkakati Wa kiTaifa Wa Ujuzi Wa Akili Unde (AI) ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 1.2. Kuanzisha mpango maalum wa kukuza ujuzi wa baadaye (Tanzania Future Skills Accelerator (TFSA) ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 1.3. Kujumuisha masomo ya coding, roboti na umahiri wa kidijitali katika mfumo wa elimu ya msingi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4. Kuziwezesha shule na vituo vya ufundi na ufundi stadi – TVET kupata maabara za Akili Unde. | | | | | |
| | 1.5. Kuingia ubia na makampuni ya kimataifa ya Akili Unde kwa ajili ya kutoa mafunzo yenye ithibati na vyeti. | | | | | |
| 2. Kuongeza uwekezaji katika utafiti na maendeleo (R&D) kutoka asilimia 0.56 hadi angalau asilimia 0.8 ya Pato la Taifa ifikapo 2031 | 2.1. Kuandaa na Mkakati wa Kitaifa wa Ujuzi Wa utafiti na maendeleo chini ya COSTECH ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | 2.2. Kutunga Sheria ya ugharamiaji wa utafiti na ubunifu (Research and Innovation Finance Act) ili kuhakikisha kuwa na bajeti endelevu za Utafiti na Maendeleo ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| | 2.3. Kuanzisha Mfuko wa Uhawilishaji Teknolojia kwa Makampuni yanayoibukia (startups) na vyuo vikuu ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| | 2.4. Kuweka vivutio vya kodi (tax incentives) kwa shughuli za Utafiti na Maendeleo ili kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.5. Kuwezesha angalau asilimia 50 ya SMEs kutumia teknolojia za viwanda 4.0 ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.6. Kuanzisha kanda nne za teknolojia (tech parks) katika miji ya Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.7. Kuanzisha maabara za kitaifa za Akili Unde (AI) na Kituo cha Super computing ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.8. Kuandaa Mwongozo wa kitaifa wa Akili Unde na miundombinu ya supercomputing | | | | | |
| | 2.9. Kuandaa Mkakati wa kitaifa wenye dhamana ya serikali wa ugharamiaji wa tafiti kwa sekta za kipaumbele ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| 3. Kuongeza idadi ya vituo vya ubunifu kutoka 5 vya sasa kufikia angalau 10 ifikapo Juni 2031. | 3.1. Kuimarisha Sera ya Taifa ya Ubunifu (National Innovation Policy) ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | 3.2. Kuanzisha Kituo cha Ubunifu wa Akili Unde na Mnemba jijini Uchambuzi Mpana | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | wa Takwimu Dar es Salaam ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| | 3.3. Kujenga angalau vituo vitatu vya sayansi na teknolojia katika kanda ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 3.4. Kuweka mfumo rasmi wa maabara za maarifa asilia (Indigenous Knowledge Labs) ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 3.5. Kujumuisha program za kukuza na kulea ubunifu katika vyuo vikuu vyote nchini ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 3.6. Kuanzisha vituo atamizi vya utafiti na maendeleo katika vituo vyote vya ubunifu zote ili kusaidia startups za utafiti. | | | | | |
| 4. Asilimia 100 ya tafiti muhimu zinazohusiana na malengo ya kimkakati zinatumika ifikapo Juni 2031. | 4.1. Kuandaa na kuzindua hazina ya kitaifa ya utafiti ya uwazi na inayofikika kufikia Juni 2028 | | | | | |
| | 4.2. Kuanzisha jukwaa la pamoja la sera na utafiti kati ya wizara ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| 5. Kuanzisha Mwongozo wa Kitaifa wa Agenda ya Utafiti na kuhakikisha mipango ya taasisi zote inalingana ifikapo Juni 2031. | 5.1. Kufufua Mwongozo wa kitaifa wa Uratibu wa tafiti pamoja na kanzidata ya kitaifa ya watafiti ifikapo Juni 2027 | | | | | |
| | 5.2. Kuhakikisha wizara zote zinaoanisha mipango yao ya utafiti ya agenda ya utafiti ya kitaifa ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| | 5.3. Kutumia mifumo ya Akili unde ya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa agenda ya utafiti ya kitaifa ifikapo Juni 2028 | | | | | |
| | 5.4. Kuanzisha Baraza la Taifa la Utafiti ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| | 5.5. Kuunganisha taasisi zote za utafiti kwenye jukwaa la kidijitali la agenda ya utafiti ya kitaifa ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 5.6. Kuandaa mkakati wa ugharamiaji wa agenda ya utafiti ya kitaifa ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 5.7. Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa utabiri wa hali ya hewa unaotumia Akili Unde ifikapo Juni 2028 | | | | | |
| | 5.8. Kuibadilisha TARI kuwa Taasisi Mahiri ya Utafiti wa Kilimo ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 5.9. Oanisha teknolojia za kidijitali na zinazoibuka katika Sera ya Taifa ya Kilimo kufikia Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| 6. Ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika utafiti kuongezeka kwa asilimia 50 ifikapo 2031. | 6.1. Kuandaa mwongozo wa ushirikiano wa kimataifa wa utafiti (International Research Cooperation Framework) ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 6.2. Kutengeneza mfumo wa ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma katika utafiti wa kimataifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 7. Kuanzisha kwa hazina ya wazi ya kitaifa ya takwimu (National Open Data Repository - NODAR) na Mwongozo wa Maadili ya takwimu ifikapo 2031 | 7.1. Kuanzisha Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa takwimu Data (National Data Governance Board). | | | | | |
| | 7.2. Kuanzisha kwa hazina ya wazi ya kitaifa ya takwimu (National Open Data Repository - NODAR) ifikapo Juni 2029 | | | | | |
| | 7.3. Kutekeleza mwongozo wa maadili ya Akili Unde na usalama wa taarifa (AI Ethics and Data Protection Framework) ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| **3.6.5. Kuwekeza katika Mfumo Ikolojia Unaotegemea Takwimu** | | | | | | |
| **Lengo 3: Kuanzishwa kwa mfumo imara wa ikolojia unaotegemea takwimu, wenye mifumo bora na jumuishi ya takwimu, ili kuimarisha utoaji wa maamuzi sahihi, ubunifu wa kidijitali na maendeleo jumuishi ya kijamii na kiuchumi ifikapo 2050.** | | | | | | |
| 1. Asilimia 100 ya miongozo ya takwimu za ufuatiliaji na tathmini ya Dira 2050 na Mpango Elekezi 2050 ziwe zimewianishwa ifikapo Juni 2031. | 1.1. Kuandaa na kupitisha mpango kazi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Takwimu inayooanisha matokeo ya takwimu na malengo ya Dira 2050, ikijumuisha muda wa utekelezaji na mwongozo wa ufuatiliaji, ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2. Kufanya mapitio ya sheria ya Takwimu ili kuingiza mahitaji mapya ya takwimu pamoja na maboresho ya muundo wa usimamizi wa takwimu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kushirikiana na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali (MDAs) na sekta binafsi zinafungamanisha Dira 2050, kuonanisha viashiria vinavyoendana na Dira 2050 katika mifumo yao ya utoaji taarifa kwa kuzijengea uwezo na kuzipa msaada wa kitaalamu ifikapo 2031. | | | | | |
| | 1.4. Kuhakikisha ulinganifu na muunganiko wa mifumo yote mikuu ya takwimu ndani ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili kuwezesha upatikanaji wa takwimu kwa wakati halisi, uchambuzi na katika kufanya maamuzi ya kisera ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 1.5. Kujumuisha makundi muhimu ya takwimu kama vile picha za setelaiti, takwimu za simu za mkononi, taarifa za mitandao ya kijamii, taarifa za tovuti, taarifa za sensa na big data katika mifumo ya takwimu ya taifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.6. Kuboresha na kuimarisha mifumo ya wazi ya takwimu na dashibodi za umma zinazoonyesha angalau sekta kuu mbili za maendeleo ili kuongeza uwazi na matumizi ya takwimu katika maamuzi ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 1.7. Kuweka mfumo wa kuchapisha takwimu za wakati halisi za viashiria muhimu vya kiuchumi na kijamii kwa kila robo mwaka ili kuwa na majibu ya kisera na kwa wakati ifikapo 2031. | | | | | |
| 2. Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi za Takwimu Kitaifa ziwe zimeongezeka kufikia angalau asilimia 0.4 ya Pato la Taifa (GDP) ifikapo 2031 | 2.1. Kuanzisha mifumo mitatu ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya kuwekeza kwenye teknolojia za kisasa za ukusanyaji wa takwimu na mifumo ya uchambuzi wa takwimu (ugharamiaji bunifu + teknolojia) ifikapo 2027. | | | | | |
| | 2.2. Kuweka katika muundo wa kidijitali na kuunganisha mifumo ya usimamizi ya takwimu katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha ulinganifu na utoaji taarifa kwa wakati ifikapo 2028. | | | | | |
| | 2.3. Kuongeza wigo wa aina za takwimu za kiofisi na kuanzisha aina mpya za takwimu za kipaumbele kwa kutumia zana za kidijitali na mbinu bora zilizoboreshwa ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 2.4. Kuhakikisha takribani asilimia 70 ya watakwimu na wanasayansi wa takwimu wanakamilisha mafunzo yaliyoidhinishwa katika matumizi ya takwimu kubwa akili unde na , AI na teknolojia zinazoibukia ifikapo 2029. | | | | | |
| 3. Mfumo wa Taifa wa Takwimu ubadilishwe kuwa wa kidijitali kwa | 3.1. Kuanzisha miundombinu jumuishi ya kitaifa ya takwimu (uhifadhi wa takwimu kwenye cloud, dashibodi za wakati halisi) ifikapo Juni 2028. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| angalau asilimia 80 ifikapo Juni 2031 | 3.2. Kuhamisha kwa asilimia 100 ya ukusanyaji mkubwa wa takwimu kwenda kwenye majukwaa ya kidijitali (CAPI, programu za simu) ambayo ni hatua hatua muhimu ya mabadiliko ya kidijitali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.3. Kuanzisha programu za utafiti wa Akili unde na sayansi ya takwimu katika vyuo vikuu nchini ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.4. Kuandaa na kuzindua Mtaala wa Kitaifa wa Mafunzo ya Takwimu unaolenga sayansi ya takwimu, big data, Akili unde na utumiaji wa mifumo inayojiendesha na kujisimamia ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 3.5. Kuweka utaratibu wa matumizi ya Akili unde na maamuzi yanayotokana na uchambuzi wa takwimu Serikalini, ikiwa ni pamoja na kuanzisha vitengo maalumu vya uchambuzi wa takwimu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 4. Muda wa kuchakata data kupunguzwa kwa asilimia 50 ifikapo Juni 2031 | 4.1. Kuongeza wigo wa ukusanyaji takwimu kwa simu na teknolojia za utambuzi wa mbali kufikia aslimia 100 kwa maeneo lengwa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 4.2. Kuanzisha vitengo vya Akili unde na uhandisi wa takwimu katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara mbalimbali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 4.3. Kuweka majukwaa ya uoanishaji na na uchakataji wa takwimu inayoendeshwa na Akili unde ifikapo 2031. | | | | | |
| | 4.4. Kuanzisha dashibodi za takwimu za wakati halisi katika wizara za kisekta ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 4.5. Kutekeleza machine learning algorithim katika vitengo muhimu vya takwimu serikalini ili kuharakisha uhakiki, uchambuzi wa takwimu, na maoteo mbalimbali ya takwimu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 4.6. Kuanzisha kituo cha Taifa cha Utafiti wa Akili unde kwa ajili ya Takwimu na matumizi ya blockchain katika usalama wa takwimu ifikapo Juni 2031.. | | | | | |
| 5. Kuanzishwa kwa mfumo wa kiintelijensia wa kidijitali wa taarifa za idadi ya watu na makazi | 5.1. Kuanzishwa kwa mfumo jumuishi wa kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya kiraia unaounganisha taaarifa za vizazi, vifo, ndoa, uhamiaji na kitambulisho cha | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kwa wakati halisi ifikapo Juni 2031 | taifa katika wizara na Taasisi zote, kuwezesha uwepo wa kumbukumbu za, sahihi kidemografia ifikapo 2031. | | | | | |
| | 5.2. Kutungwa na kutekelezwa kwa weka mifumo ya kisheria na usimamizi wa takwimu kwa ajili ya mifumo ya kidijitali ya idadi ya watu ili kuhakikisha faragha ya takwimu, usalama, ulinganifu wa mifumo na uwajibikaji wa taasisi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.3. Kufanya Sensa za Watu na Makazi kwa kutumia njia za kidijitali kwa kutumia tablet, GPS na dashibodi za wakati halisi ifikapo 2031. | | | | | |
| | 5.4. Kuweka mfumo wa ufuatiliaji wa wakati halisi wa maendeleo ya sensa, ubora wa takwimu na uendeshaji wa kazi katika mikoa yote, kwa kutumia dashibodi za moja kwa moja zinazoweza kufikiwa na timu za uratibu za ngazi ya kitaifa na kikanda ifikapo 2031. | | | | | |
| | 5.5. Kuanzishwa kwa Rejesta Jumuishi ya Watu na Makazi kwa kuunganisha CRVS, NIDA na mifumo ya kiutawala kwa ajili ya kuendelea kuhuisha takwimu za kidemographia ifikapo 2031. | | | | | |
| | 5.6. Kuanzishwa kwa jukwaa la kitaifa la ujumuishaji wa takwimu za watu kwa wakati halisi likiunganisha CRVS, sensa za kidijitali, mifumo ya kijiografia (GIS) na kanzidata ya takwimu za kiutawala, kusaidia kupata taarifa za kidemografia za wakati halisi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.7. Kuanza kwa utekelezaji wa mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa taarifa za kidemografia kwa wakati halisi unaojengwa kupitia majukwaa yanayojiendesha yenyewe na ulinganifu wa mifumo kutoka sekta muhimu kama afya, elimu na uhamiaji ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.8. Kutumia zana za kijiografia na Akili unde kufuatilia mienendo ya idadi ya watu kwa kutumia picha za satelaiti, takwimu na chunguzi kwa jili ya kuwa na taarifa za wakati husika ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 5.9. Kuanzishwa kwa dashibodi salama na jumuishi ya taarifa za idadi ya watu inayopatikana kwa watumiaji waliothibitishwa wa taarifa za kidemografia kwa wakati halisi kwa ajili ya upangaji, ufuatiliaji na kukabiliana na dharura ifikapo 2031. | | | | | |
| **3.6.6. Mageuzi ya Kidijitali** | | | | | | |
| Lengo 1: Jamii jumuishi iliyounganishwa na yenye ujuzi wa kidijgtali, inayowezeshwa na miundombinu salama itakayosaidia ubunifu, utoaji huduma na mageuzi ya kijamii na kiuchumi katika mikoa yote nchini. | | | | | | |
| 1. Kufikia angalau asilimia 80 ya uunganishwaji wa kidijitali nchini ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuandaa na kuendesha vituo vya maarifa ya kidijitali katika kila mkoa ili kuongeza uwezo wa kidijitali, ujuzi na ubunifu kwa vijana, wanawake na makundi maalumu. | | | | | |
| | 1.2. Kutekeleza mkakati wa uratibu wa uwekaji wa miundombinu ya TEHAMA kwa Serikali na Sekta Binafsi ili kuongeza ufanisi katika miundombinu ya fiber optic na kuharakisha uunganishwaji wa broadband nchi nzima. | | | | | |
| | 1.3. Kuanzisha jukwaa salama na jumuishi la kubadilishana takwimu na taarifa kati ya sekta ya umma na binafsi. | | | | | |
| | 1.4. Kutoa msaada wa kifedha na kitaalamu kwa biashara ndogo ndogo, na za kati (MSMEs) ili kuziwezesha kutumia teknolojia za kidijitali, majukwaa ya kidijitali na biashara mtandaoni (e-commerce) kwa lengo la kuongeza tija na kukuza ujumuishaji wa kiuchumi. | | | | | |
| | 1.5. Kusimamia na kuamuru uanzishaji na utekelezaji wa huduma za kidijitali zinazoweza kufikiwa na kutumika na watu wenye ulemavu ili kuhakikisha usawa wa upatikanaji wa huduma hizi kwa makundi yote ya kijamii ifikapo. | | | | | |
| | 1.6. Kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kidijitali vya bei nafuu, vilivyotengenezwa ndani au kuingizwa kutoka nje kwa makundi yote ya jamii. | | | | | |
| **Lengo 2: Kuimarisha miundombinu ya kitaifa ya usalama wa mtandao na mifumo ya usimamizi, huku tukitumia kimkakati teknolojia zinazoibuka, ili kulinda mageuzi ya kidijitali ya Tanzania na kuiweka nchi katika nafasi ya ushindani wa kimataifa** | | | | | | |
| 1. Kuasili matumizi ya teknolojia zinazoibukia | 1.1. Kuanzisha vituo maalumu vya utafiti na maendeleo na mafunzo ya akili unde katika AI, robotics, IoT, blockchain na | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2031 | teknolojia zingine zinazoibukia ili kujenga uwezo wa kitaalamu wa nchi ifikapo 2031 | | | | | |
| | 1.2. Kuendeleza uwezo wa ndani katika teknolojia za setelaiti, uchunguzi wa anga na matumizi ya takwimu kwa kushirikiana na taasisi za anga za kimataifa ili kuunga mkono vipaumbele vya maendeleo ya taifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kukuza matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, vituo vya takwimu vinavyotumia nishati kidogo na mifumo ya kompyuta inayotumia matumizi kidogo ya nishati katika sekta za umma na binafsi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Mashambulizi ya kimtandao kupunguzwa kwa asilimia 80 ifikapo Juni 2031 | 2.1. Kuanzisha na kuendesha Kituo cha Kitaifa cha Uendeshaji wa Usalama (SOC) kilicho na vifaa kamili kwa ajili ya kufuatilia, kugundua, na kukabiliana na vitisho na mashambulizi ya mtandao kwa wakati halisi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2. Kuanzisha Timu ya Kitaifa ya Kukabiliana na Matukio ya Usalama wa kimtandao (CSIRT) na Baraza la Usimamizi wa Usalama wa Mtandao ili kuratibu jitihada za usalama wa mtandao kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kusimamia vihatarishi vya usalama wa kimtandao ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kuendesha mazoezi ya kitaifa ya usalama wa mtandao mara kwa mara ili kupima uwezo wa kukabiliana na matukio, kuongeza utayari, na kuimarisha ustahimilivu wa miundombinu muhimu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.4. Kuhakikisha takwimu zote za serikali na sekta muhimu zinahifadhiwa ndani ya mamlaka ya nchi, chini ya mifumo salama cloud, ili kuimarisha wa takwimu, faragha na usalama wa taarifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 3: Mfumo thabiti, jumuishi na wenye rasilimali za kutosha wa ubunifu na teknolojia zinazoibukia unaochochea ujasiriamali, utafiti na maendeleo (R&D) na utatuzi wa kiteknolojia** | | | | | | |
| 1. Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 10 bora Afrika katika fahirisi ya ubunifu ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuanzisha mfumo maalum wa ufadhili ili kutoa ruzuku, mtaji wa mwanzo, na msaada wa uwekezaji kwa ubunifu wa kidijitali wenye matokeo makubwa na na | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | miradi ya utafiti kote Tanzania ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2. Kuanzisha jukwaa la kukuza uuzaji, upatikanaji wa masoko, na uwekezaji katika suluhisho za kidijitali zilizotengenezwa ndani ya nchi kwaaajili ya ukuaji wa uchumi na ujasiriamali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kurasimisha ushirikiano kati ya vyuo vya elimu, vituo vya utafiti, na sekta binafsi ili kuharakisha utafiti na maendeleo yanayotekelezeka (R&D), kukuza ujuzi, na uhawilishaji wa teknolojia ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4. Kuanzisha mtandao ulioratibiwa wa vituo atamizi (incubators) na vichocheo vya ukuaji (accelerators) ili kulea kampuni changa (startups), kuongeza wigo wa biashara za kidijitali zenye uwezekano mkubwa wa kukua, na na kurahisisha upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 4: Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa usimamizi wa mageuzi ya kidijitali nchini katika sekta zote.** | | | | | | |
| 1. Angalau asilimia 80 ya mifumo ya kidijitali ya sekta kuwa imefungamanishwa ifikapo Juni 2031 | 2.1. Kuanzisha taasisi kwa ajili ya kujenga uwezo wa uongozi, uwezo wa kitaalamu na usimamizi wa mageuzi ya kidijitali katika sekta zote, ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi na usimamizi madhubuti ifikapo Juni 2031 | | | | | |
| | 2.2. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa viwango vya ubora, usalama, usiri na ubora kwa mifumo yote ya kidijitali ya umma na binafsi, ili kuwezesha utoaji wa huduma jumuishi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kujumuisha na kuboresha mifumo ya udhibiti ili kuwezesha modeli za biashara ya kidijitali, ulinzi wa taarifa, usalama mtandao na ubunifu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.4. Kuanzisha jukwaa jumuishi la kidijitali la serikali kwa ajili ya kuunganisha mifumo yote ya kisekta, kuwezesha utoaji huduma bila vikwazo na kufuatilia maendeleo ya mabadiliko ya kidijitali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **3.6.7. Miundombinu na Huduma za TEHAMA** | | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **Lengo 1. Miundombinu dhabiti na jumuishi ya TEHAMA inayohakikisha muunganiko wa kidijitali nchini, kuimarisha ujuzi wa kidijitali kwa makundi yote ya watu na kuwezesha matumizi yenye maadili ya teknolojia zinazoibukia ili kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.** | | | | | | |
| 1. Matumizi ya intanenti yenye kasi kuongezeka kufikia angalau asilimia 80 ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano na wasimamizi ili kuhakikisha upatikanaji wa mtandao wa 5G katika miji yote, ili kuwezesha upatikanaji wa huduma ya intaneti ya kasi na ya kuaminika kwa ajili ya biashara, elimu na huduma za serikali. | | | | | |
| | 1.2. Kusambaza huduma ya itanenti (Wi-Fi ) ya bure au ya gharama nafuu katika maeneo ya kimkakati yaliyochaguliwa katika taasisi za umma, maeneo ya wazi na vituo vya umma ili kuongeza upatikanaji wa huduma za intaneti kwa wananchi, wakiwemo walio katika maeneo ya pembezoni kila mwaka. | | | | | |
| | 1.3. Kutekeleza mifumo ya udhibiti inayochochea uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo yasiyyo pata huduma za kutosha ili kuhakikisha upatikanaji wa usawa wa huduma za kidijitali katika maeneo ya vijijini na maeneo ya pemebzoni kila mwaka. | | | | | |
| | 1.4. Kuandaa miradi maalumu ya miundombinu kwa kutumia fiber, wireless na teknolojia za setelaiti ili kuunganisha jamii za vijijini na maeneo ambayo ni hayafikiki kwa urahisi. | | | | | |
| | 1.5. Kushirikiana na waendeshaji wa setelaiti kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za kidijitali nchini, hususani katika maeneo yenye changamoto ya miundombinu ya ardhini ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kidijitali. | | | | | |
| 2. Uelewa wa matumizi ya kidijitali kuongezeka kutoka asilimia 30 hadi angalau asilimia 60 ifikapo Juni 2031 | 2.1. Kuanzisha Taasisi ya Kitaifa ya Mafunzo ya Kidijitali (DTI) ifikapo Juni 2028 | | | | | |
| | 2.2. Kutoa mafunzo kwa walimu 30,000 juu ya teknolojia zinazoibukia ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kuandaa mifumo ya elimu ya kisasa inayoendeshwa na Akili Unde ikijumuisha majukwaa ya elimu mtandao yanayotumia Akili Unde ifikapo Juni 2031 | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 2.4. Kujumuisha Akili Unde na usalama mitandaoni katika mitaala ya elimu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.5. Kujumuisha ujuzia wa kidijitali katika mtaala wa elimu wa Taifa katika ngazi zote, kuhakikisha angalau asilimia 60 ya wanafunzi wanapata ujuzi wa msingi wa kidijitali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.6. Kutekeleza programu za kitaifa za mafunzo ya ujuzi wa kidijitali katika jamii zinazolenga makundi yasiyopata huduma za kutosha ili kuwafikia angalau watu milioni 20 ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.7. Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa uthibitishaji wa ujuzi wa kidijitali na kuhakikisha angalau asilimia 50 ya nguvu kazi inapata cheti/uthibitisho wa kiwango cha awali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 3. Mifumo ya Usalama Mtandao na Ulinzi wa Takwimu kutekelezwa kwa asilimia 100 kila mwaka | 3.1. Kuimarisha mfumo wa kisheria wa Taifa wa Usalama Mtandao na Ulinzi wa Taarifa ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 3.2. Kuhakikisha uimara wa mifumo ya usalama mtandao kwa kufanya tathmini za mara kwa mara za usalama mtandao, majaribio na ukaguzi kila mwaka. | | | | | |
| | 3.3. Kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Uendeshaji wa Usalama Mtandao ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 3.4. Kutoa mafunzo ya usalama mtandao kwa wataalamu wote wa TEHAMA katika sekta muhimu kila mwaka. | | | | | |
| 4. Kupanda kwa kiwango cha kuasili akili unde (AI Adoption Index) kutoka kiwango cha chini hadi cha kati ifikapo Juni 2031 | 4.1. Kuendeleza sera kamili pamoja na mfumo wa kisheria na kanuni za udhibiti wa Akili Unde ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 4.2. Kufanya mapitio ya kila mwaka juu ya utekelezaji wa mfumo wa udhibiti wa Akili Unde ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **3.6.8. Huduma za Mawasiliano na Usafirishaji Kiposta** | | | | | | |
| **Lengo 1. Kuboresha upatikanaji wa huduma za mawasiliano zenye kuaminika, nafuu na za kasi ya juu, mijini na vijijini, ili kuwezesha ushiriki jumuishi wa kidijitali, ukuaji wa uchumi na maisha bora kwa wote ifikapo 2050** | | | | | | |
| 1. Upatikanaji wa huduma za posta kwa wote, muunganisho wa kidijitali na huduma salama za biashara mtandaoni (e- | 1.1. Kukuza na kuwezesha matumizi ya intaneti inayotumia setelaiti katika maeneo ambayo miundombinu ya ardhini haiwezekani ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2. Kuboresha upatikanaji wa huduma za posta za kisasa na huduma za kusafirisha | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| commerce) umefikiwa ifikapo Juni 2031. | vifurushi (courier) zinazojumuishwa na mifumo ya fedha kidijitali katika maeneo ya pembezoni ili kuhakikisha upatikanaji nchi nzima ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kuandaa na kutekeleza mfumo jumuishi (harmonized framework) wa huduma za posta na usafirishaji vifurushi ndani nan je ya nchi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4. Kuboresha mfumo wa kitaifa wa anwani za makazi, unaounganishwa na majukwaa ya Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS), ili kusaidia utoaji bora na wenye ufanisi wa huduma za usafirishaji na huduma za usambazaji wa barua na mizigo midogo nchini kote ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.5. Tanzania kuongoza na kuwa kitovu cha Biashara Mtandao (e-Commerce) Afrika Mashariki na ukanda wa Kusini mwa Afrika kwa kutumia huduma za usafirishaji, majukwaa ya kidijitali, na urahisishaji wa huduma za usafirishaji ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Fahirisi ya ushindani wa huduma za kidijitali kuongezeka hadi asilimia angalau 50 ifikapo Juni 2031 | 2.1. Kufanya tathmini za mara kwa mara za utoaji wa huduma za kidijitali na miundombinu, na kutumia ubunifu na mbinu bora ili kuhakikisha ubora na ushindani ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2. Kuhuisha na kutekeleza mifumo ya kisheria kwa ajili ya kulinda watumiaji wa huduma za kidijitali ili kuhakikisha usalama, uwazi na uwajibikaji katika biashara mtandaoni (e-commerce) na usafirishaji wa vifurushi ifikapo 2031. | | | | | |
| 3. Kuimarishwa kwa usalama wa mtandao na kuongezeka kwa imani kwa raia, kutekelezwa kwa mifumo ya kitaifa ya usalama wa mtandao kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2031. | 3.1. Kutoa elimu kwa wananchi, waafanya biashara na taasisi za umma kuhusu matumizi salama ya teknolojia za kidijitali, cyber hygiene na vihatarishi vipya vya kimtandao ili kujenga uaminifu katika huduma za kidijitali . | | | | | |
| | 3.2. Kuwezesha shughuli za kitafiti zinazolenga katika uibuaji wa teknolojia mpya, zana na uvumbuzi wa kukabiliana na vihatarishi vya kidijitali, ili kuimarisha ustahimilivu katika mitandao ya mawasiliano. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 3.3. Kuhamasisha ushirikiano kati ya taasisi za kiserikali, kampuni za teknolojia, na wataalamu wa usalama mtandao ili kuendeleza ubunifu, kushirikishana mbinu bora, na kuimarisha uwezo wa taifa wa kujilinda kimtandao. | | | | | |
| **3.6.9 Mazingira ya Biashara na Uwekezaji** | | | | | | |
| **Lengo 1. Kuimarisha uhamasishaji wa uwekezaji kupitia uanzishwaji wa mazingira ya ushindani, uwazi, ufanisi na mfumo wa taasisi, wenye hadhi ya nchi ya nchi ya uchumi wa kipato cha kati cha juu kufikia mwaka 2050.** | | | | | | |
| 1. Kutoa huduma za serikali kwa njia ya kidijitali kwa angalau asilimia 50 kufikia Juni 2031. | 1.1. Kuandaa mwongozo wa sera ya Serikali Mtandao ifikapo Juni 2027. | | | | | |
| | 1.2. Kutekeleza Mfumo wa Kitaifa wa utambulisho cha Kidijitali (Digital ID) ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 1.3. Kuunda mfumo wa ufuatiliaji wa kodi unaoutumia akili mnembe (AI) ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 1.4. Kuimarisha miundombinu ya kidijitali na uwezo wa taasisi za serikali ili kufanikisha upatikanaji wa huduma mtandao kwa asilimia 60 ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Kufungamanisha huduma wezeshi za biashara zitakazowezesha takribani asilimia 50 ya miamala ya biashara kufanyika kidijitali na kuwezesha upatikanaji wa huduma kidijitali kwa wajasiriamali wadogo na kampuni zinazoibukia kufikia Juni 2031. | 2.1. Kuendeleza miongozo ya udhibiti wa biashara ya kidijitali ifikapo Juni 2028 | | | | | |
| | 2.2. Kuboresha upatikanaji na uwezo wa kidijitali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na biashara chipukizi kupitia zana, mafunzo na majukwaa maalumu ili kuwawezesha kushiriki katika biashara za mtandaoni (online trade) ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kuhamasisha matumizi ya mifumo salama ya malipo na miamala ya kidijitali katika mifumo ya biashara ili kuhakikisha angalau asilimia 60 ya biashara za wajasiriamali wadogo na wakati zinafanyika kidijitali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 3. Kuongeza mchango wa uwekezaji kutoka nje katika Pato la Taifa kufikia takribani asilimia 10 kila mwaka ifikapo Juni 2031. | 3.1. Kukamilisha maboresho ya sera ya uwekezaji ifikapo Juni 2027. | | | | | |
| | 3.2. Kuanzisha vituo vya uwekezaji katika mikoa yote nchini ifikapo 2031. | | | | | |
| | 3.3. Kuimarisha udhamini wa uwekezaji (Investment Ombudsman) ifikapo Juni 2029. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | 3.4. Kuimarisha jukwaa la kidijitali la usajili wa uwekezaji ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 3.5. Kuhamasisha utoaji wa vivutio za uwekezaji katika teknolojia ya hali ya juu ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 3.6. Kuandaa miongozo ya uwekezaji kwa sekta za teknolojia ya hali ya juu ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| 4. Kuwezesha uwekezaji wa angalau asilimia 5 ya teknolojia mpya za hali ya juu ifikapo Juni 2031. | 4.1. Kuanzisha angalau kanda maalumu tatu za akili unde na kanda za ubunifu wa kidijitali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 5. Kuwezesha angalau asilimia 15 ya nguvu kazi kuwa na ujuzi wa kisasa na wa kitaalamu ifikapo Juni 2031. | 5.1. Kuandaa programu ya kitaifa ya kujenga ujuzi katika uwekezaji ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 5.2. Kuongeza wigo wa ushirikiano katika mafunzo ya ufundi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 6. Kuongeza miradi ya maendeleo ya miundombinu kupitia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kufikia takribani asilimia 20 ifikapo Juni 2031 | 6.1. Kuwezesha angalau miradi mitano ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwam mwaka ili kuimarisha maendeleo ya miundombinu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 7. Kuwezesha uwekezaji katika teknolojia wenye thamani ya takribani Dola za Marekani Bilioni 2 kufikia Juni 2031. | 7.1. Kupanua motisha kwa viwanda vya kisasa kila mwaka ili kufanikisha jumla ya uwekezaji wa teknolojia wa Dola za Marekani bilioni 2 (USD 2bilioni) ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo 2: Kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuiweka Tanzania katika nafasi ya tatu bora miongoni mwa nchi zenye uchumi rafiki wa biashara barani Afrika, kwa lengo la kuongeza kasi ya uwekezaji na kuharakisha urasimishaji wa biashara katika sekta zote ifikapo mwaka 2050**. | | | | | | |
| 1. Tanzania kushika nafasi ya tatu kati ya vituo vinavyovutia zaidi kwa biashara na uwekezaji barani Afrika kufikia Juni 2031. | 1.1. Kutenganisha malengo ya ukusanyaji mapato na majukumu ya udhibiti ili kuhakikisha tozo zinagharamia utoaji huduma ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2. Kuratibu na kusanifu upya vyombo vya udhibiti ili kuharakisha ukuaji wa biashara na uwekezaji ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.3. Kuzingatia na kuunganisha kanuni zinazofanana na kuondoa urudufu ili kupunguza gharama za miamala ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4. Kufanya tathmini ya athari za udhibiti (Regulatory Impact Assessments – RIAs) kwa kanuni zote na sheria ndogo za | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA by-laws) zinazoweza kuathiri biashara kufikia Juni 2031. | | | | | |
| | 1.5. Kuongeza imani kwa wawekezaji kupitia sera za kukabiliana na vihatarishi dhamana za mapato, na utatuzi wa migogoro kwa haraka ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Kurasimisha biashara kwa asilimia 80 na kuweka mfumo wa kidijitali wa taratibu za biashara ifikapo Juni 2031. | 2.1. Kuanzisha wakala maalum wa kukuza uwekezaji na kampuni changa bunifu kufikia 2031. | | | | | |
| | 2.2. Kuwezesha ushiriki wa kampuni zinazoibukia na wafanyabiashara wadogo wadogo wasio rasmi katika ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.3. Kukuza fursa za soko la Tanzania ndani ya soko huru la AfCFTA na Jumuiya ya Afrika Mashariki ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mipango ya Maendeleo ya Mwaka Mmoja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| **3.7. Misingi ya Uendelevu wa Taifa** | | | | | | |
| **3.7.1. Kuimarisha Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu** | | | | | | |
| **Lengo la 1: Kuimarisha uwazi, uwajibikaji, maadili, na tunu za kidemokrasia, pamoja na amani na utulivu ili kuwezesha ushiriki wenye ufanisi na usawa wa wanajamii wote katika maendeleo ya taifa** | | | | | | |
| 1. Kuimarika kwa vitendo vya utoaji maoni na uwajibikaji hadi kufikia - 0.45 ifikapo Juni 2031 | i. Kufanya mapitio ya kina ya mifumo iliyopo ya kikatiba na kisheria ifikapo Juni 2027. | | | | | |
| | ii. Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa mageuzi ya kisheria na kiutawala baada ya utekelezaji wake ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.1. Kufanya Mageuzi ya Kitaasisi ili Kuhakikisha Utawala Bora wa Rasilimali za Taifa na Usimamizi Endelevu wa Mipango ya Kijamii na Kiuchumi ya Muda Mrefu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kufanya mageuzi katika mifumo ya sasa ya kitaasisi ili kuhakikisha kuwa mihimili yote ya dola inawajibika kwa usimamizi wa pamoja na huru katika matumizi ya rasilimali za taifa na katika maamuzi | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mipango ya Maendeleo ya Mwaka Mmoja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | yanayogusa maslahi ya taifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa ushirikishwaji wa kijamii na kitaasisi katika usimamizi wa rasilimali za taifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | iii. Kuimarisha au kuanzisha chombo huru kitakachohakikisha kuwa manufaa yatokanayo na kupungua kwa gharama na kuongezeka kwa tija vinavyotokana na matumizi ya rasilimali za taifa yanagawanywa kwa usawa kwa umma ili kupunguza pengo la kijamii ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | iv. Kufanya mapitio na maboresho ya muundo wa taasisi muhimu za umma, hususan mashirika ya umma na taasisi za udhibiti, ili kuondoa urudufu wa majukumu, vitendo vya kutafuta faida binafsi, na ukosaji wa ufanisi ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 1.2 Kuandaa Mikakati ya Kuoanisha Sheria za Kimila na Sheria za Kiserikali katika Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Haki za Binadamu ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kufanya ukaguzi wa kitaifa wa sheria za kimila ili kubaini maeneo yenye migongano, mwingiliano, au kinzani na sheria za kiserikali ifikapo mwaka 2030. | | | | | |
| | ii. Kuandaa na kutekeleza mikakati ya jinsia na haki za binadamu ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 1.3 Kukuza ushiriki jumuishi katika uchaguzi kwa kujumuisha masuala ya jinsia, vijana na watu wenye ulemavu katika sera na taratibu za uchaguzi ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | i. Kuoainisha na kuratibu sera za kitaasisi ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | ii. Kuendeleza miundombinu, zana na majukwaa yatakayowezesha ushiriki wa watu wenye mahitaji maalum katika michakato ya uchaguzi ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 1.4 Kuandaa na kutekeleza programu ya kitaifa ya muda mrefu ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria, hususan kwa wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na jamii zenye kipato cha chini, kwa kushirikiana na asasi za kiraia na sekta binafsi ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mipango ya Maendeleo ya Mwaka Mmoja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | i. Kufanya mapitio na kuandaa programu ya kitaifa ya muda mrefu ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria yenye uwazi na ushirikishwaji mpana ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | ii. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa elimu ya uraia, utetezi pamoja na ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| 2. Fahirisi ya Mtazamo wa Rushwa (CPI) imeimarika kutoka 41/100 (2024) hadi 55/100 ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuweka mfumo wa kidijitali katika huduma za mahakama na utawala ili kuimarisha uwazi ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 2.2 Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mifumo ya mikataba ya wazi na ununuzi wa kielektroniki ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 2.3 Kuimarisha majukwaa ya maoni ya wananchi na mifumo ya kushughulikia malalamiko kila mwaka. | | | | | |
| 3. Farihisi ya utulivu wa kisiasa, amani na usalama kimeimarika kufikia +0.10 ifikapo Juni 2031. | 13.1 Kuboresha mifumo ya ulinzi na usalama kwa kutumia teknolojia za kisasa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 13.2 Kuanzisha mfumo wa polisi jamii na kuandaa programu ya pamoja ya ushirikishwaji, ushiriki na uhusishwaji wa wananchi ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 13.3 Kufanya mapitio ya mitaala ya mafunzo ya polisi ili kuleta mabadiliko ya mtazamo kuelekea utoaji bora wa huduma kwa wananchi ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 13.4 Kufanya mapitio ya Jeshi la Magereza la Tanzania na vyombo vingine vinavyohusika kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Haki Jinai ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| **Lengo 2:** | **Kuimarisha utumishi wa umma unaoendana na mahitaji ya wananchi, unaowajibika na unaozingatia maadili kwa ajili ya utawala bora na utoaji huduma wenye ufanisi** | | | | | |
| 1.1 Kufanya maboresho na kurahisisha muundo wa Wizara na Wakala za Serikali kwa kuzipanga katika idadi ndogo zenye majukumu mapana ili kuongeza ufanisi na wepesi wa utekelezaji ifikapo Juni 2030 | | | | | | |
| 1. Ufanisi wa Serikali kiboreshwe kufikia -0.30 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kufanya mapitio ya kina ya majukumu na muundo wa taasisi za Wizara, Idara na Wakala pamoja na mifumo yake ifikapo Juni 2030 | | | | | |
| | i. Kufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi ili kuboresha upangaji wa rasilimali watu kwa kuzingatia muundo mpya wa wizara na taasisi pamoja na mahitaji ya mabadiliko ya kidijitali katika utoaji wa huduma ifikapo Juni 2028. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mipango ya Maendeleo ya Mwaka Mmoja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | ii. Kuanzisha jukwaa litakalowawezesha mawaziri na viongozi wakuu wa serikali kujibu madai na malalamiko ya wananchi ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | iii. Kutekeleza maboresho ya muundo wa wizara, idara na wakala kwa awamu ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 1.2 Kuanzisha Mfumo Jumuishi wa Kidijitali wa Uchumi ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | i. Kubuni na kuendeleza usanifu wa jukwaa kuu la mfumo Jumuishi wa Kidijitali wa Uchumi ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | ii. Kuweka katika mfumo wa kidijitali na kuunganisha kazidanta na majukwaa muhimu ya taarifa za kiuchumi katika taasisi zote za serikali ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | iii. Kubuni na kuendeleza miundombinu na mifumo ya ulinzi wa taarifa na usalama wa mtandao ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 1.3 Kuimarisha uwezo wa kitaaluma, kiufundi na kiuongozi katika sekta ya umma ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuandaa na kutekeleza programu jumuishi ya mafunzo na mwongozo wa kujenga uwezo ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | ii. Kuandaa na kutekeleza mfumo jumuishi wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.4 Kuimarisha uundaji wa modeli za kiuchumi na maoteo ya mapato ya Serikali ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kufanya mapitio ya modeli iliyopo kwa kuzingatia mahitaji ya maendeleo ya baadaye na mbinu bora za kimataifa ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | ii. Kuandaa na kutekeleza programu ya mapitio na uboreshaji wa mara kwa mara wa modeli kadri takwimu mpya, mbinu na mahitaji mapya yanavyojitokeza ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | iii. Kuandaa programu ya kitaifa ya maadili na utamaduni wa kazi katika utumishi wa umma, ikijumuisha mafunzo ya mara kwa mara ya maadili na ushauri wa uongozi katika taasisi zote za serikali ifikapo Juni 2030.` | | | | | |
| 2. Kufikia angalau asilimia 80 ya taasisi za umma zenye kuonesha utamaduni wa kazi | 2.1 Kuweka utaratibu wa tathmini ya utendaji wa watumishi kwa mfumo wa nyuzi 360 pamoja na mifumo ya maoni ya papo kwa papo katika taasisi zote za umma ifikapo Juni 2030. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mipango ya Maendeleo ya Mwaka Mmoja 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| wenye utendaji wa juu, maadili na uwajibikaji nchini ifikapo Juni 2031 | i. Kuandaa sera na miongozo ya tathmini ya utendaji ya nyuzi 360 pamoja na mfumo wa maoni ya wakati halisi ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | ii. Kufanya mapitio, kuanzisha na kuunganisha majukwaa ya kidijitali ya kusimamia tathmini ya utendaji na maoni ya wakati halisi ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| 3. Kiwango cha kuridhika na huduma za umma kuongezeka kutoka asilimia 45 (2024) hadi asilimia 70 ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuanzisha mikataba ya utendaji kazi kwa viongozi wakuu wa umma ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 3.2 Kuanzisha programu endelevu za maendeleo ya kitaaluma na mafunzo ya maadili kila mwaka. | | | | | |
| | 3.3 Kuongeza ugatuzi wa kifedha ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo la 3: Kuimarisha uadilifu na kuaminika kwa taasisi zinazosimamia mahusiano ya wananchi** | | | | | | |
| 1. Utawala wa Sheria kiboreshwa kufikia -0.20 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kukuza ushirikiano na wadau wa kikanda na kimataifa kwa ajili ya kubadilishana maarifa kuhusu kuimarisha mifumo ya kisheria ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kukuza ushirikiano na wadau wa kikanda na kimataifa kwa ajili ya kubadilishana maarifa kuhusu kuimarisha mifumo ya kisheria ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuandaa na kutekeleza programu na majukwaa ya kubadilishana maarifa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 2. Imani ya wananchi kwa taasisi za umma kiongezeka kutoka asilimia 52 (2024) hadi asilimia 75 ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuimarisha taasisi za usimamizi na ukaguzi (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, na Kamati za Bunge) ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 2.2 Kutekeleza mifumo ya uwazi katika ajira na upandishaji vyeo kila mwaka. | | | | | |
| | a. Kukuza majadiliano ya kitaifa kuhusu mageuzi ya utawala ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **3.7.2. Kujenga Utawala Imara na Wenye Ufanisi katika Serikali za Mitaa** | | | | | | |
| **Lengo la 1: Kufikia Utawala Imara na Wenye Ufanisi katika Serikali za Mitaa** | | | | | | |
| 1. Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikia uhuru wa | 1.1. Kuimarisha Sera ya Kitaifa ya Ugatuzi wa Madaraka na Mfumo wa Kisheria ifikapo Juni 2030. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mipango ya Maendeleo ya Mwaka Mmoja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| kiutendaji kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2031 | 1.2. Kuanzisha majukwaa ya kidijitali ya utoaji huduma katika ngazi za mitaa pamoja na mifumo ya kupokea maoni ya wananchi ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 1.3. Kubuni na kuendeleza majukwaa ya kidijitali ya utoaji huduma na mifumo ya maoni ya wananchi ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | 1.4. Kusambaza na kuanza kutekeleza majukwaa na mifumo ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 1.5. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 1.6. Kuimarisha mfumo wa uhamishaji wa rasilimali za fedha kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.7. Kuboresha na kupanua vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.8. Kuimarisha usimamizi wa fedha, uwajibikaji na uwazi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.9. Kukuza Maendeleo ya Uchumi wa Serikali za Mitaa kama chanzo muhimu cha mapato ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| 1 Miundo ya kiutawala ya Serikali za Mitaa na mifumo ya usimamizi wa Serikali Kuu kuboreshwa kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kufanya mapitio ya muundo wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuwezesha utekelezaji bora wa sera, msaada wa kitaalamu na ufuatiliaji wa utendaji, kwa lengo la kuimarisha utawala wa ugatuzi na uhuru wa Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 2.2 Kuoanisha na kuratibu mifumo ya kisheria na kitaasisi inayohusiana na ugatuzi wa madaraka ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 2.3 Kubuni, kuendeleza na kutumia zana na majukwaa ya kidijitali kwa ajili ya uratibu, uwazi, uwajibikaji na ufanisi wa utekelezaji ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 2.4 Kuboresha majukumu na kazi za viongozi wa ngazi za mikoa na serikali za mitaa ili kuongeza ushirikiano na kukamilishana katika utoaji wa huduma bora na zenye uwajibikaji ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 2.5 Kurekebisha miundo ya kiutawala kwa kuzingatia uwiano wa idadi ya watumishi na majukumu yao ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| 3. Ushiriki wa wananchi na uwajibikaji wa mitaa husika katika asilimia 80 ya Mamlaka | 3.1 Kuweka msingi wa kisheria wa mipango shirikishi na bajeti shirikishi katika ngazi ya kata na vijiji kupitia marekebisho ya sera na utekelezaji wake ifikapo Juni 2031. | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mipango ya Maendeleo ya Mwaka Mmoja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| za Serikali za Mitaa (LGAs) umefikiwa ifikapo Juni 2030. | i. Kufanya mapitio ya kina ya miundo iliyopo, mifumo ya kisheria na taratibu za utekelezaji ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | ii. Kubuni, kuendeleza na kuanza kutekeleza mifumo na taratibu jumuishi za ushiriki wa wananchi na utekelezaji wake ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 3.2 Kusambaza matumizi ya zana za tathmini ya jamii na ukaguzi wa kijamii angalau asilimia 60 ya Serikali za Mitaa ifikapo 2028 na kufikia utekelezaji wa kitaifa ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | i. Kubuni na kuendeleza zana za tathmini ya jamii ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | ii. Kusambaza kwa awamu matumizi ya zana za tathimini ya jamii katika Serikali za Mitaa zote ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 3.3. Kuanzisha majukwaa ya kidijitali ya maoni ya wananchi (kupitia ujumbe mfupi wa simu, tovuti na programu za simu) kwa ajili ya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma katika Serikali za Mitaa zote ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | i. Kusambaza na kuanza kupitia majukwaa ya kidijitali ya maoni ya wananchi katika Serikali za Mitaa zote ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | ii. Kusambaza na kuanza kuyatumia katika Serikali za Mitaa zote ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | iii. Kutoa mafunzo na kuziwezesha taasisi za utawala wa mitaa, madiwani, kamati za maendeleo za kata, serikali za vijiji na asasi za kiraia ili kuimarisha ushiriki wa wananchi na mifumo ya maoni ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 3.4 Kuimarisha uwezo wa madiwani pamoja na kamati za maendeleo za kata na vijiji kama majukwaa ya ushirikiano katika utoaji wa huduma na ubunifu wa maendeleo ya ngazi ya jamii ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | i. Kuandaa na kuanzisha programu na majukwaa ya usimamizi wa mabadiliko na ubunifu katika ngazi ya jamii ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | ii. Kutekeleza kikamilifu programu na majukwaa ya ubunifu katika halmashauri zote, kata na vijiji ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **Lengo la 2: Kuboresha mifumo ya kifedha na kiutawala iliyogatuliwa** | | | | | | |
| 1. Sehemu ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa iongezeke kutoka asilimia 12 (2024) hadi asilimia 25 ifikapo Juni 2031 | i. Kutoa mamlaka mapana zaidi kwa Serikali za Mitaa kuanzisha na kusimamia kodi za ndani ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | ii. Kuanzisha mfumo wa uhamishaji wa | | | | | |

| Shabaha | Afua | Mipango ya Maendeleo ya Mwaka Mmoja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 |
| | rasilimali kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa unaozingatia utendaji ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | iii. Kuimarisha uratibu kati ya Tume ya Taifa ya Mipango, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Serikali za Mitaa kila mwaka. | | | | | |
| **Lengo la 3: Kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika Serikali za Mitaa** | | | | | | |
| 1. Kiwango cha kuridhika kwa wananchi na utendaji wa Serikali za Mitaa kiongezeka kutoka asilimia 40 (2024) hadi asilimia 65 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kusambaza na kutekeleza majukwaa ya bajeti shirikishi na mipango shirikishi ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| | 1.2 Kuweka mifumo ya kidijitali katika taarifa za fedha na mifumo ya utoaji huduma ya Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 1.3 Kuanzisha kamati huru za ukaguzi wa hesabu katika Serikali za Mitaa ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| **Lengo la 4: Kuimarisha uthabiti wa kitaasisi na kifedha wa Serikali za Mitaa** | | | | | | |
| 1. Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinazokidhi viwango vya utoaji huduma kuongezeka kutoka asilimia 45 (2024) hadi asilimia 75 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kujenga uwezo wa watumishi wa Serikali za Mitaa katika usimamizi wa miradi na mipango kila mwaka. | | | | | |
| | 1.2 Kukuza ushirikiano kati ya Serikali za Mitaa, sekta binafsi na asasi za kiraia ifikapo Juni 2031. | | | | | |
| **3.7.3 Kuimarisha usimamizi wa mifumo ya kidijitali na takwimu** | | | | | | |
| **Lengo la 1: Kuanzisha mfumo salama wa utawala wa kidijitali ifikapo mwaka 2050.** | | | | | | |
| 1. Asilimia 50 ya huduma za serikali kuwa zimewekwa katika mfumo wa kidijitali ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuimarisha sera, mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuhakikisha utawala bora wa kidijitali serikalini ifikapo Juni 2029 . | | | | | |
| | i. Kufanya mapitio na kuoanishwa kwa sera na sheria zinazohusiana na utawala wa kidijitali ifikapo Juni 2028. | | | | | |
| | ii. Kufanya mapitio na kuandaa viwango pamoja na miongozo ya kuoanisha mifumo ya kidijitali na usimamizi wa takwimu ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | iii. Kuimarisha miundo ya taasisi, mamlaka na ujuzi wa taasisi iliyopo inayosimamia utawala wa kidijitali ifikapo Juni 2029. | | | | | |
| | 1.2 Kuboresha, kuendeleza na kulinda miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ifikapo Juni 2030. | | | | | |
| | 1.3 Kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za serikali ifikapo Juni 2028. | | | | | |

